

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

Juzuu ya Pili

Al-Imran mpaka An-Nisa

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

IBN HAZM MEDIA CENTER
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم
للإمام ابن كثير

TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.

Chapa ya Kwanza 2021.

Msimamizi Mkuu wa Mradi:
Yassir Salim Awadh Masoud

Kimetafsiriwa na:
Kamati ya Wataalamu

Kimehaririwa na:
Wanazuoni wa Kiislamu

Usanifu Kurasa:
Ally Said Abdallah
Ibn Hazm Media Center
P.O. Box 22197,
Dar es Salaam
Tanzania.

Kimechapwa:
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

Haki Zote Zimehifadhiwa.

Yaliyomo:

Tafsiri ya Suratu Al-Imran	1
Ubainifu wa Aya zenye Utatanishi " <i>Mutashaabihaat</i> ".....	7
Allah تعالی Pekee Ndiye Ajuaye Tafsiri ya Kweli ya <i>Mutashaabihaat</i>	10
Siku ya Kiyama, Mali na Watoto Haitosaidia.	16
Mayahudi Wakhofishwa kwa Kushindwa na Wanatakiwa Kujifunza.....	19
Maelezo Kuhusu Maisha ya Duniani.....	23
Malipo ya Wachamungu ni Bora kuliko Starehe.....	26
Dua na Sifa Bainifu za Wachamungu " <i>Al-Muttaqin</i> ".....	28
Ushuhuda wa Kumpwekesha Allah تعالی, " <i>Tawhid</i> ".....	31
Hakika Dini ya Kweli Mbele ya Allah تعالی ni Uislamu.....	32
Uislamu ni Dini ya Watu wote na Mtume ﷺ alitumwa kwa Wote.....	34
Mayahudi Kushutumiwa kwa kufuru yao.....	36
Makosa ya Watu wa Kitabu	39
Muongozo Unaopelekea Kwenye Kushukuru.....	40
Kuharamishwa Kuwafanya Makafiri Marafiki.....	43
Allah تعالی Anajua Yanayofichwa na Mioyo.....	46
Mapenzi ya Allah تعالی ni kwa Kumfuata Mtume ﷺ.....	48
Wateule Miongoni mwa Walimwengu.....	50
Kisa cha Kuzaliwa kwa Maryam.....	51
Makuzi ya Maryam; Heshima Yake kwa Allah تعالی.....	54
Dua ya Zakariyyah عليه السلام na Kubashiriwa Kwake Kuzaliwa Yahya عليه السلام.....	57
Utukufu wa Maryam Juu ya Wanawake wa Zama Zake.....	61
Maryam Anapokea Bishara ya Kuzaliwa Isa عليه السلام.....	65
Isa عليه السلام Alizungumza Katika Rika la Utoto.....	66
Isa عليه السلام Aliumbwa Bila Baba.....	67
Sifa Bainifu za Issa عليه السلام na Miujiza Aliyoifanya	69
Wafuasi Wanamuunga Mkono Isa عليه السلام.....	74
Mayahudi Walipanga Njama za Kumuuza Isa عليه السلام.....	75
Maana ya <i>Mutawaffyka</i>	77
Kupotoshwa kwa Dini ya Issa عليه السلام	78
Kuwatisha Makafiri kwa Mateso Hapa Duniani na Akhera.....	80
Kufanana Katika Kuumbwa kwa Adam عليه السلام na Isa عليه السلام.....	83
Mwito kwa ajili ya Kulaaniana	84
Masuala ya Kumpwekesha Allah تعالی " <i>Tawhid</i> " Yanajulikana kwa wote.....	89
Kubishana kwa Mayahudi na Wakristo Juu ya Dini ya Ibrahim عليه السلام.....	92

Husuda na Njama za Mayahudi Dhidi ya Waislamu.....	96
Maelezo kuhusu Tabia ya Uaminifu kwa Mayahudi.....	99
Waliovunja Ahadi ya Allah تعالى Hawana Hisa Siku ya Kiyama.....	101
Mayahudi Wabadilisha Maneno ya Allah تعالى kwa Kupindisha Ndimi.....	105
Hakuna Mtume Aliyewalingania Watu Kumuabudu yeye.....	107
Ahadi iliyochukuliwa kwa Mitume ya Kumuamini Mtume Wetu ﷺ	110
Dini ya Kweli Mbele ya Allah تعالى ni Uislamu.....	113
Allah تعالى Hawaongozi Watu waliokufuru Baada ya Kuamini.....	117
Toba ya Kafiri wakati wa Kufa Haikubaliwi wala Fidia Yake.....	119
Wema 'Birr' ni Mtu Kutoa Mali Yake Iliyo Bora.....	122
Maswali ya Mayahudi Waliyomuuliza Mtume Wetu ﷺ	124
Ka'bah ni Nyumba ya Kwanza Iliyowekwa kwa Ajili ya Ibada.....	129
Sababu ya Makkah Kuitwa <i>Bakkah</i> , na Majina Mengine.....	130
Makamu Ibrahim عليه السلام	131
Eneo Takatifu la <i>Al-Haram</i> ya Makkah ni Mahali pa Salama.....	132
Ufafanuzi Kuhusu Wajibu wa Kuhiji.....	135
Mwenye Kukanusha Nguzo ya Hajj ni Kafiri.....	137
Kukaripiwa Watu wa Kitabu kwa Kukufuru na Kuzuia Watu.....	138
Waislamu Wametahadharishwa Kuwatii Watu wa Kitabu.....	139
Ni Nini Maana ya Haki ya Kumcha Allah تعالى	142
Amri ya Kushikamana na Kamba ya Allah تعالى na Umuhimu wa Umoja.....	143
Amri ya Kuwaita Watu " <i>Da'wah</i> " kwa Allah تعالى	147
Makatazo Juu ya Mfarakano.....	148
Matunda ya Mshikamano na Madhara ya Mfarakano Siku ya Kiyama.....	149
Ubora wa Ummah wa Muhammad ﷺ kwa zama zote.....	153
Hadithi zingine zinazoonesha ubora wa ummah huu.....	155
Bishara Njema kwa Waislamu ya Kupata Ushindi na Nusra.....	158
Ubora wa Waliosilimu katika <i>Ahlul Kitab</i>	162
Ubainifu wa Hatima ya Sadaqa za Makafiri.....	164
Kukatazwa Kuwafanya Makafiri Kuwa Marafiki Vipenzi.....	166
Maelezo Juu ya Vita vya Uhud.....	171
Sababu ya Kutokea Vita vya Uhud.....	171
Msaada wa Allah تعالى kwa Kuwatuma Malaika.....	176
Kuharamishwa kwa Riba Moja kwa Moja.....	187
Kuhimiza Kufanya Mema Ambapo Malipo Yake ni Pepo.....	188
Hekima ya Kushindwa kwa Waislamu Katika Vita vya Uhud.....	197
Maelezo Juu ya Uvumi wa Kufa kwa Mtume ﷺ katika Vita vya Uhud.....	202

Katazo la Kuwatii Makafiri.....	210
Matatizo yaliyowapata baadhi ya Waislamu katika vita vya Uhud.....	215
Ansar na Muhajirin Walivyomhami Mtume ﷺ Siku ya Uhud.....	216
Amani ya Usingizi Ilivyowashukia Waumini Wakati wa Vita.....	220
Waumini waliokimbia vita vya Uhud na Namna Walivyosamehewa.....	223
Makatazo Juu ya kujifananisha na Makafiri.....	225
Miongoni mwa Sifa za Mtume wetu Muhammad ﷺ.....	229
Amri ya kufanya Shura na kufungamana Nayo.....	230
Utegemezi wa Allah ﷻ ni Baada ya Ushauri.....	232
Hiana na Hadaa Katika Vita si Katika Sifa za Mtume ﷺ.....	233
Kutumwa kwa Nabii Wetu Muhammad ﷺ ni Neema Kubwa.....	238
Sababu ya Majanga Yaliyowasibu Siku ya Uhud na Hekima Yake.....	242
Fadhila za Mashahidi.....	247
Maelezo ya Vita vya Hamra Al-Asad na Fadhila za Walioshiriki	251
Kumfariji Mtume ﷺ.....	258
Shutuma Dhidi ya Ubakhili na Onyo Kali Dhidi Yake.....	261
Onyo la Allah ﷻ kwa Washirikina.....	265
Kila nafsi itaonja Kifo.....	268
Kufaulu kutakuwa ni kwa nani siku hiyo?.....	268
Muumini Anajaribiwa na Anasikia Kutoka kwa Adui.....	270
Shutuma kwa watu wa Kitabu juu ya kuvunja Ahadi.....	274
Shutuma kwa Watu wa Kitabu juu ya Udanganyifu.....	274
Dalili za Tawhid kwa Watu Wenye Akili.....	277
Allah ﷻ Hujibu Dua za Watu Wenye Akili.....	283
Tahadhari Dhidi ya Kughurika Tabia za Wapenda Dunia.....	287
Mustakbali wa Baadhi ya watu wa Kitabu na Malipo Yao.....	290
Amri ya kuvumilia na Kudumu katika Ibada.....	294
Tafsiri ya <i>Suratu An-Nisaj'</i>.....	301
Amri ya Kuwa na Taqwa, Inakumbushwa Kuumbwa na Kuwatendea Wema.....	303
Ulinzi wa Mali za Mayatima.....	306
Kuharamishwa Kuoa Mayatima kwa Kuwapa Mahari Duni.....	307
Kuishia Kuoa Wake Wanne.....	309
Kutosheka Kuoa Mke mmoja.....	310
Kutoa Mahari ni Wajibu.....	311
Kuzuia Mali ya Mtu Mbadhirifu.....	312
Amri ya Kuwapa Matumizi Wasio na Busara kwa Uadilifu.....	313
Kuwakabidhi Mayatima Mali yao Wanapofika Baleghe.....	314

Waangalizi Masikini Wanaruhusiwa Kutumia kwa Hekima.....	316
Amri ya Kurithisha na Kuwapa Kidogo	319
Kuangalia Usawa Katika Mirathi (Wasia).....	320
Onyo Kali Dhidi ya Wale Wanaotumia Mali za Mayatima	321
Kuamrisha Mirathi na Kuhimizwa Kujifunza Elimu Yake.....	323
Sababu za Kushushwa Ayah 4:11.....	323
Hadithi Nyingine Iliyopokelewa Kutoka kwa Jabir رضي الله عنه	324
Watoto Hurithishwa kwa Kuzingatia.....	325
Fungu la Mabinti Wanapokuwa Peke Yao.....	326
Mafungu ya Wazazi katika Mirathi.....	327
Kutanguliza Deni, Kisha Wasia, Kabla ya Urithi.....	327
Mirathi ya Wanandoa.....	330
Maana ya <i>Kalalah</i>	330
Hukumu kuhusu Watoto wa Mama ambao Hakuwazaa na Marehemu.....	331
Indhari Dhidi ya Kuchupa Mipaka ya Mirathi.....	332
Amri ya Kumzuilia Mzinifu Mwanamke Nyumbani Kwake.....	335
Kukubaliwa kwa Toba ya Mja.....	339
Maana ya 'Kurithi Wanawake kwa Nguvu'.....	343
Wanawake Wasidhuriwe.....	344
Amri ya Kukaa na Wanawake kwa Wema.....	345
Kuharamishwa Jambo la Kutaka Kurudishiwa Mahari.....	346
Kuharamishwa Kumuoia Mke wa Baba.....	349
Kubainisha Wanawake Maharim.....	351
Haramu Kuwaoa Mama Wakwe na Binti zao.....	353
Mtoto wa Kambo ni Haramu Kuolewa.....	354
Maana ya "Kuingilia".....	355
Kuharamishwa Kuwaoa Wake wa Watoto Halisi.....	355
Utatanishi na Majibu Yake.....	356
Kuharamishwa Kuoa Dada Wawili kwa Wakati Mmoja	357
Kuharamishwa <i>Muhsawat</i> Watakapokuwa Chini ya Milki.....	359
Kuharamishwa Wanawake Wasiokuwa Hao Waliotajwa	360
Maelezo Juu ya Ndoa ya <i>Mut'ah</i> na Uharamu wake.....	361
Kujuzu Jambo la Kuoa Mjakazi kama Mtu Hawezi Kuoa.....	363
Adhabu ya Mjakazi Mzinifu ni Nusu ya Mwanamke Huru.....	365
Kuharamishwa Mali iliyochumwa kwa Haramu.....	369
Uchaguzi wa Kununua au Kuuza Kabla ya Kuachana.....	371
Makatazo na Maonyo Dhidi ya Kuua Nafsi.....	372

Madhambi Madogo Yatasamehewa Iwapo Mtu Atajizuia.....	374
Ufafanuzi wa Madhambi Saba Yaangamizayo.....	375
Hadithi Nyingine Inadhukuru Ushahidi wa Uongo	375
Hadithi Nyingine Inayotaja Kuua Mtoto	376
Hadithi Nyingine ya Abdullah bin Amir رضي الله عنه.....	377
Kukatazwa Kutamani Ambavyo Allah تعالى Amewafadhili Wengine.....	378
Sifa za Mwanamke Muadilifu.....	383
Kushughulikia Ujeuri wa Mke.....	385
Mwanamke Mtiifu kwa Mume Hapaswi Kubughudhiwa.....	387
Kuteuliwa Wasuluhishi Wawili Inapokhofiwa Mfarakano.....	387
Amri ya Kumcha Allah تعالى Pekee na Kuwatii Wazazi.....	389
Haki za Jirani.....	390
Amri ya Kuwatendea Wema Watumwa na Watumishi.....	393
Karipio kwa Tabia ya Ubahili.....	398
Allah تعالى Hamdhulumu Mja Wake Hata kwa Uzito wa Chembe ya Vumbi.....	401
Je, Washirikina Watapunguziwa Adhabu?.....	403
Malipo Makubwa Maana Yake Nini?.....	404
Mtume wetu Atakuwa Shahidi Dhini ya au kwa Ajili ya Umma.....	405
Kuharamisha Kusogelea Sala Mtu Anapokuwa Amelewa.....	408
Maelezo ya <i>Tayamamu</i>	413
Sababu za Kuruhusiwa <i>Tayammum</i>	417
Kuwarudi Mayahudi kwa Kuchagua Upotofu.....	420
Kuwalingania Watu wa Kitabu Kuamini na Kuwaonya.....	423
Ka'ba Al-Ahbar Alisilimu Baada ya Kusikia Aya 4:47.....	424
Kuwakemea na Kuwalaani Mayahudi kwa Kujitangazia Utakasifu.....	429
Makafiri Hawana Ubora Juu ya Waumini.....	431
Laana ya Allah تعالى kwa Mayahudi kwa Kuwasaidia Washirikina.....	432
Ubakhili wa Husda ya Mayahudi.....	433
Adhabu ya Wale Wasioamini Vitabu na Mitume ya Allah تعالى.....	435
Mafikio ya Waja Wema ni Peponi na Neema Zake.....	436
Amri ya Kurejesha Amana kwa Yeyote Anayestahiki.....	437
Amri ya kuwa Muadilifu Katika Hukumu.....	438
Ulazima wa Kuwatii Viongozi Katika Yasiyomuasi Allah تعالى.....	440
Ulazima wa Kurejesha Hukumu katika Qur'an na Sunna.....	443
Kutoyarejesha Masuala ya Dini Kwenye Qur'an na Sunnan.....	446
Karipio la Wanafiki.....	447
Ulazima wa Kumtii Mtume ﷺ.....	449

Mtu Hatokuwa Muumini Mpaka Ayarejeshe Masuala Yake.....	450
Watu Wengi Hukataa Wanayoamrisha.....	454
Yeyote Atakayemtii Allah تعالى na Mjumbe wake ﷺ	455
Umuhimu wa Kuchukua Tahadhari Dhidi ya Adui.....	460
Kukataa Kujiunga na <i>Jihad</i> ni Dalili ya Unafiki.....	460
Uhamasishaji Kushiriki katika <i>Jihad</i>	462
Kuhimiza Jihad Ili Kuwatetea Wanyonge.....	464
Kulaumiwa Waliopenda Kucheleweshwa <i>Amri ya Jihad</i>	466
Kifo Hakikwepeki.....	467
Wanafiki Walihisi Ndege Mbaya (Nuksi).....	469
Kumtii Mtume ﷺ ni Kumtii Allah تعالى	472
Ujinga wa Wanafiki.....	473
Qur'an ni ya Kweli.....	475
Kukataza Kuarifu Habari Zisizo za Hakika na Zisizochunguzwa.....	477
Allah تعالى Anamuamuru Mjumbe Wake Afanye <i>Jihad</i>	480
Kuwashawishi Waumini Kupigana.....	481
Kuombea kwa Ajili ya Njia ya Heri au Shari	483
Kuitikia Salam, kwa Salam Bora Zaidi.....	485
Kuwakaripia Masahaba kwa Kutokuafikiana juu ya Wanafiki.....	488
Wenye Kupigana na Wasiopigana.....	490
Hukumu Kuhusu Kumuuu muumini kimakosa.....	495
Onyo Juu ya Mauaji ya Makusudi.....	499
Je, Toba ya Wanaoua kwa Makusudi Inapokelewa?.....	501
Maamkizi ya Salama ni Dalili ya Uislamu.....	503
<i>Mujahid</i> na Wasiojiunga na Jihadi Hawalingani.....	509
Kukatazwa Kuishi Pamoja na Makafiri.....	513
<i>Salat ya Al-Qasr</i> , Kufupisha Swala.....	518
Maelezo ya Sala ya Hofu.....	523
Amri ya Dhikri ya Kutosha Baada ya Sala ya Hofu.....	526
Kuhimizwa kukimbizwa Adui licha ya Majeraha	527
Umuhimu wa Kuegemea katika Hukumu Alizoshusha Allah تعالى	530
Kuhimiza Kuomba Msamaha wa Allah تعالى	533
Najwa Adilifu, Mazungumzo ya Semi.....	537
Adhabu kwa Kumpinga Mtume na Kufuata Njia Tofauti.....	538
Shirki Haitosomehewa.....	541
Malipo kwa Waja Wema.....	545
Ufanisi Unafikiwa kwa Kufanya Amali Njema.....	548

Ibrahim <i>Khalil</i> عليه السلام wa Allah تعالى	552
Hukumu Kuhusu Mayatima wa Kike	555
Hukumu Inayohusu Kujitenga kwa Mume	559
Maana ya "Suluhu ni Bora".....	560
Usia na Umuhimu wa Kumcha Allah تعالى.....	564
Kuamrisha Haki na Kuwa Shahidi wa Allah تعالى	567
Kujitenga ni Njia ya Kuzuia na Kuficha Ushahidi	570
Utaratibu wa Kuwa na Imani Baada ya Kuwa Muumini.....	570
Sifa Bainifu za Wanafiki na Hatima yao.....	572
Wanafiki Wanasubiri Kuona Yatayowapata Waislamu.....	576
Wanafiki Wanajaribu Kumdanganya Allah تعالى	579
Kuharamishwa kwa <i>Wilayah</i> na Makafiri.....	584
Wanafiki na Marafiki wa Makafiri Wako katika Moto wa Chini.....	585
Rukxa ya Kutangaza Uovu kwa Aliyedhulumiwa.....	588
Kuamini baadhi ya Mitume na Kuwakana Wengine ni Ukafiri Halisi.....	591
Ukorofi wa Mayahudi	594
Makosa Makubwa ya Mayahudi.....	598
Maneno Machafu Waliyoyatamka Mayahudi	599
Wakristo Watamuamini Issa عليه السلام Kabla Hawajafariki Dunia.....	603
Hadithi Kuhusu Kushuka kwa Issa عليه السلام	603
Wasifu wa Issa عليه السلام	614
Mayahudi Waliharamishiwa baadhi ya Vyakula.....	618
Wahyi Ulikuwa Kwa Mtume Muhammad ﷺ.....	622
Mitume Ishirini na Watano Wametajwa Ndani ya Qur'an.....	622
Utukufu wa Mussa عليه السلام.....	623
Sababu za Kupelekwa Mtume niKusimamisha Hoja.....	624
Kukatazwa kwa Watu wa Kitabu Kufanya <i>Ghuluu</i> Katika Dini.....	631
Maana ya Kauli ya Allah تعالى	633
Madhehebu ya Kikristo.....	636
Mitume na Malaika Hawajifaharishi Katika Kumuabudu Allah تعالى.....	638
Maelezo ya Wahyi Uliotoka kwa Allah تعالى.....	640
Aya ya Mwisho Kuteremshwa, Hukumu ya <i>Al-Kalala</i>	641

Tafsiri ya Suratul Imran Sura ya 3 Iliteremshwa Madinah

Suratu Al-Imran iliteremshwa Madinah, kama ilivyo shuhudiwa na ukweli kuwa Aya themanini na tatu za mwanzo ndani yake zimeteremshwa kuhusu ujumbe wa Najran uliowasili Madinah, mwaka wa Tisa wa Hijrah (632 CE).

Tutafafanua suala hili wakati wa kuelezea Aya inayo - husu *Mubahalah* (3:61) ndani ya sura hii, Allah تعالیٰ Akipenda.

Pia, tumezitaja fadhila za *Suratu Al-Imran* pamoja na fadhila za *Suratu Al-Baqarah*, mwanzoni mwa Tafsiri ya *Suratu Al-Baqarah*.



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ آلِ عِمْرَانَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾

الْم ﴿٢﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ﴿٣﴾ نَزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَأَنْزَلَ التَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ ﴿٤﴾ مِنْ قَبْلُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَأَنْزَلَ الْفُرْقَانَ ۗ إِنَّ الْفُرْقَانَ ۗ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ ذُو انتِقَامٍ ﴿٥﴾ إِنَّ اللَّهَ لَا يَخْفَى عَلَيْهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ ﴿٦﴾ هُوَ الَّذِي يُصَوِّرُكُمْ فِي الْأَرْحَامِ كَيْفَ يَشَاءُ ۗ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٧﴾ هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخَرُ مُتَشَبِهَاتٌ ۗ فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَبَهَ مِنْهُ ابْتِغَاءَ الْفِتْنَةِ وَابْتِغَاءَ تَأْوِيلِهِ ۗ وَمَا يَعْلَمُ تَأْوِيلَهُ إِلَّا اللَّهُ ۗ وَالرَّاسِخُونَ فِي الْعِلْمِ يَقُولُونَ ءَأَمَّنَّا بِمِثْلِ كُلِّ مِمَّنْ عِنْدَ رَبِّنَا ۗ وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٨﴾ رَبَّنَا لَا تُرِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ رَحْمَةً ۗ إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ ﴿٩﴾ رَبَّنَا إِنَّكَ جَامِعُ النَّاسِ لِيَوْمٍ لَا رَيْبَ فِيهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُخْلِفُ الْمِعَادَ ﴿١٠﴾

الْم ﴿٢﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ﴿٣﴾ نَزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَأَنْزَلَ التَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ ﴿٤﴾ مِنْ قَبْلُ هُدًى لِّلنَّاسِ وَأَنْزَلَ الْفُرْقَانَ ۗ إِنَّ الْفُرْقَانَ ۗ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ ذُو انتِقَامٍ ﴿٥﴾

1. Alif Laam Miim.

2. Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye - Mwenye Uhai wa Milele, na Mwendeshaji wa mambo yote.

3. Amekuteremshia Kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyo kuwa kabla yake. Na Aliteremsha Taurati na Injili

4. Kabla yake, zive uwongofu kwa watu. Na Akateremsha Furqani (chenye kupambanua baina ya haki na batili). Hakika waliozikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu watakuwa

na adhabu kali. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Kulipa.

Tuliitaja Hadithi katika Tafsiri ya *Ayat Al-Kursi* (2:255) inayosema kuwa Jina Kuu la Allah تعالى limo ndani ya Aya hizi mbili.

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ﴿٢٥٥﴾

“Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye - Mwenye Uhai wa Milele, na Mwendeshaji wa mambo yote.” (2:255)

الْم ﴿٢٥٦﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ﴿٢٥٧﴾

“Alif Laam Miim. Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye - Mwenye Uhai wa Milele, na Mwendeshaji wa mambo yote.” (3:1-2)

Pia yamepita mazungumzo kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

الْم ﴿٢٥٦﴾

“Alif, Lam, Mim.”

Mwanzoni mwa *Surah Al-Baqarah*, na maana ya،

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَيُّ الْقَيُّومُ ﴿٢٥٥﴾

“Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye - Mwenye Uhai wa Milele, na Mwendeshaji wa mambo yote.” (3:2)

Tumeshaeleza katika Tafsiri ya *Ayat Al-Kursi* kiasi kwamba hakuna haja ya kurudia. Halikadhalika, maana ya Kauli Yake،

نَزَّلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ

“Amekuteremshia Kitabu kwa haki.” (3:3)

Maana yake: Alikuteremshia Qur’an, Ewe Muhammad, kwa ukweli. Maana: Hapana, shaka wala wasiwasi kuwa iliteremshwa kutoka kwa Allah تعالى. Kwa hakika, Allah تعالى Aliteremsha Qur’an kwa Ujuzi Wake, na malaika wanathibitisha ukweli huu, Allah تعالى Anatosha kuwa Shahidi. Kauli ya Allah،

مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ

“Kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake”. (3:3)

Maana yake: Kutoka katika vitabu vitakatifu vilivyoshushwa kabla, na kupelekwa kwa waja na Mitume wa Allah تعالى. Vitabu hivyo vinathibitisha uhakika wa Qur'an, na Qur'an pia inathibitisha ukweli uliomo ndani ya Vitabu hivyo, pamoja na habari na bishara njema za utume wa Muhammad ﷺ na kuteremshwa kwa Qur'an Takatifu. Allah تعالى Anasema,

وَأَنْزَلَ التَّوْرَةَ

“Na Aliteremsha Taurati.”

Maana yake: Kwa Nabii Musa bin Imran عليه السلام.

وَالْإِنْجِيلَ

“Na Injili.” Kwa Issa bin Mariam عليه السلام.

مِنْ قَبْلُ

“Kabla yake.” Maana yake: Kabla ya Qur'an hii.

هُدًى لِّلنَّاسِ

“Ziwe uwongofu kwa watu.” Maana yake: Katika zama zao.

وَأَنْزَلَ الْفُرْقَانَ

“Na Akateremsha Furqani (chenye kupambanua baina ya haki na batili).”

Ambayo ni kipambanuzi kati ya upotofu, batili na kukengeuka kwa upande mmoja, na mwongozo, ukweli na uchaji kwa upande mwingine. Hii ni kwa sababu ya alama, na ushahidi ulio wazi na uthibitisho dhahiri uliomo, na kwa sababu ya maelezo, uchanganuzi n.k. kutoka kwa Allah تعالى.

Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ اللَّهِ

“Hakika waliozikanusha Ishara za Mwenyezi Mungu.”

لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌ

“watakuwa na adhabu kali.” Maana yake: Siku ya Kiama.

وَاللَّهُ عَزِيزٌ ذُو انتِقَامٍ ﴿١﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye kulipa.”

Maana yake: Mwenye Ufalme Mkuu.

انتِقَامٍ ﴿٢﴾

“Na Mwenye Kulipa.”

Maana yake: Kwa yule anayekadhibisha Ishara Zake na akawapinga Mitume Mitukufu na Manabii Watukufu.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَخْفَىٰ عَلَيْهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ ﴿٣﴾ هُوَ الَّذِي يُصَوِّرُكُمْ فِي الْأَرْحَامِ كَيْفَ يَشَاءُ ۗ لَّا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٤﴾

5. Hakika Mwenyezi Mungu Hakifichiki chochote Kwake, duniani wala mbinguni.

6. Yeye Ndiye Anayekutengezeni Sura ndani ya matumbo ya mama zenu kwa namna Apendayo. Hapana muabudiwa ila Yeye, Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.

Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye Ana Elimu Timilifu kuhusu mbingu na ardhi na kuwa hapana kinachojificha katika Uoni Wake.

هُوَ الَّذِي يُصَوِّرُكُمْ فِي الْأَرْحَامِ كَيْفَ يَشَاءُ

“Yeye Ndiye Anayekutengezeni Sura ndani ya matumbo ya mama zenu kwa namna Apendayo.”

Maana yake: Anakuumbeni katika fuko la uzazi Apendavyo, ima mwanaume au mwanamke, mzuri au mbaya, mwema au muovu.

لَّا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٥﴾

“Hapana muabudiwa ila Yeye, Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.”

Maana yake: Yeye ni Muumba, Pekee Mwenye Haki ya Kuabudiwa, bila mshirika, na Yeye Ana Nguvu Madhubuti, Mwenye Hekima na Uamuzi. Aya hii

inahusu ukweli kuwa Isa عليه السلام, mwana wa Mariam, ni kiumbe aliyeumbwa, kama Allah تعالى Alivyoumba viumbe wengine. Allah تعالى Alimuuumba Isa عليه السلام ndani ya tumbo la mama yake na Akamsawiri (Akampa sura) kama Alivyopenda. Kwa hiyo, vipi Isa عليه السلام atakuwa Mungu, kama Manasara wanavyodai, Laana za Allah تعالى ziwashukie. Isa عليه السلام aliumbwa ndani ya tumbo, na maumbile yake yalibadilika hatua kwa hatua, kama Allah تعالى Alivyosema,

تَخْلُقُكُمْ فِي بُطُونِ أُمَّهَاتِكُمْ خَلْقًا مِّنْ بَعْدِ خَلْقٍ فِي ظُلُمَاتٍ ثَلَاثٍ

“Anakuumbeni katika matumbo ya mama zenu, umbo baada ya umbo, katika viza vitatu.” (39:9)

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخْرُ مُتَشَابِهَاتٌ فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَبَهَ مِنْهُ ابْتِغَاءَ الْفِتْنَةِ وَابْتِغَاءَ تَأْوِيلِهِ وَمَا يَعْلَمُ تَأْوِيلَهُ إِلَّا اللَّهُ وَالرَّاسِخُونَ فِي الْعِلْمِ يَقُولُونَ ءَأَمَّنَّا بِهِ كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ رَبِّنَا وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٦﴾ رَبَّنَا لَا تُرِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ ﴿٧﴾ رَبَّنَا إِنَّكَ جَامِعُ النَّاسِ لِيَوْمٍ لَا رَيْبَ فِيهِ إِنَّ اللَّهَ لَا يُخْلِفُ الْمِيعَادَ ﴿٨﴾

7. Yeye Ndiye Aliyekuteremshia Kitabu hichi. Ndani yake zimo Aya muhkam, zenye maana wazi. Hizo ndizo msingi wa Kitabu hichi. Na ziko nyengine Mutashabiha (zinazotatanisha). Ama wale ambao nyoyoni mwao umo upotovu wanafuata zile zenye kutatanisha kwa kutafuta fitna, na kutafuta maana ya hakika yake; yenye kuwafiki matamano ya nafsi zao, na wala hapana ajuaye maana ya hakika yake ila Mwenyezi Mungu. Na wale wenye msingi madhubuti katika ilimu husema: Sisi tumeziamini, zote zimetoka kwa Mola wetu Mlezi. Lakini hawakumbuki hayo isipokuwa wenye akili.

8. (Na hao husema): Mola wetu Mlezi! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kwishatuongoa, na Utupe Rehema itokayo Kwako. Hakika Wewe Ndiye Mpaji.

9. Mola wetu Mlezi! Wewe Ndiye Mkusanyaji wa watu kwa Siku isiyo na shaka ndani yake. Hakika Mwenyezi Mungu Havunji miadi yake.

Ubainifu wa Aya zenye Utatanishi “Mutashaabihaat” na Zilizo wazi Maelezo Yake “Muhkamaat”

Allah ﷻ Ameeleza kuwa ndani ya Qur’an, kuna Aya ambazo maelezo yake yapo wazi “Muhkamaat” nazo ndizo *Ummul-Kitaab* (msingi wa Kitabu). Maana: Ziko dhahiri, wazi na zinajulisha, haziingiliani na Aya nyinginezo. Pia zipo Aya ndani ya Qur’an ambazo zina utatanishi “Mutashaabihaat” ambazo hazijulikani uwazi kwa wengi au baadhi ya watu. Hivyo basi, yule atakayefanya Aya yenye maelezo yenye utatanishi, kama Aya yenye maelezo ya wazi kwake ni sawa na Aya yenye maelezo ya utatanishi. Atakuwa ameongoka. Na mwenye kwenda kinyume amehasirika. Hii ndiyo sababu Allah ﷻ Amesema,

هٰنْ اُمُّ الْكِتٰبِ

“Hizo ndizo msingi wa Kitabu hichi”.

Maana yake: Ndiyo asili ya Qur’an, na lazima zirejewe kwa ufafanuzi ikiwa kuna mushkeli mahali.

وَاٰخِرُ مَثَلِهِنَّ

“Na ziko nyengine Mutashabiha (zinazotatanisha)”.

Kwa kuwa zina maana nyingi; kuna zinazowiana na Aya zenye maelezo ya wazi “Muhkamaat” na kuna nyingine zenye maana nyingine za kisarufi, japo maana hizi zinaweza kuwa na mushkeli. Aya zenye maelezo ya wazi *Muhkamaat* ni Aya ambazo zinaelezea sharia zilizofutwa, vilivyohalalishwa, vilivyo-haramishwa, sharia, mipaka, wajibu na amri zinazotakiwa kuaminiwa na kutekelezwa. Na Aya zenye utatanishi maelezo yake “Mutashabihaat” ni pamoja na zilizofutwa, iliyotangulia kuja na kuchelewa, mafumbo, viapo, na kile kinachoaminiwa, lakini hakitekelezwi. Muhammad bin Is-haq bin Yasar رحمه الله تعالى alitolea maelezo Aya hii,

مِنْهُ ءَايٰتٌ مُّحْكَمٰتٌ

“Ndani yake zimo Aya muhkam.”

Ndani yake kuna ushahidi wa Mola, kinga kwa waja na ukanushaji wa wakinzani na upotofu. Haziwezi kubadilishwa au kugeuzwa kutokana na yale yaliyokusudiwa. Pia alisema kuhusu Aya zenye maelezo tatanishi “*Mutashaabihaat*” kuwa kweli zinaweza kubadilishwa au kugeuzwa. Na Allah تعالى Anawatahini waja wake kupitia Aya hizo, kama Alivyowajaribu kwa vitu vilivyohalalishwa na vilivyoharamishwa. Hivyo Aya hizi hazitakiwi kuchezewa, kuleta maana potofu wala zisigeuzwe dhidi ya ukweli. Kwa hiyo Allah تعالى Amesema,

فَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ زَيْغٌ

“Ama wale ambao nyoyoni mwao umo upotovu.”

Maana yake: Wale waliopotoshwa na kutoka kwenye ukweli na kuuendea upotofu,

فَيَتَّبِعُونَ مَا تَشَبَهَ مِنْهُ

“wanafuata zile zenye kutatanisha.”

Maana yake: Wanafanya marejeo kwenye Aya zenye maelezo tatanishi “*Mutashaabiha*.” Kwa sababu wanaweza kubadilisha maana zake ili zikubaliane na malengo yao maovu. Labda tu kwa sababu lafudhi ya Aya zenye maelezo tatanishi “*Mutashaabiha*” imebeba yale wanayoya elekea au wanayoyataka kubadilisha. Ama kwa Aya zenye maelezo ya wazi “*Muhkamaat*” hawapati chochote, kwa sababu haziwezi kubadilishwa ziko wazi, na hivyo zina ushahidi usiopingika dhidi ya watu waliopotoka. Ndiyo sababu Allah تعالى Amesema,

أَبْتِغَاءَ الْفِتْنَةِ

“Kwa kutafuta fitna.”

Maana yake: Ili wawapotoshe wafuasi wao kwa kudai kuthibitisha uzushi na bidaa zao kwa kutegemea Qur’an, lakini, huu ni ushahidi dhidi yao, na haziwaungi mkono. Ni kama vile Wakristo, wangedai kuwa Qur’an imetamka kwamba Isa عليه السلام ni *Ruhullah* na Neno lake, ambalo Alilipeleka kwa Mariam, wakati huo huo wakaiacha Kauli ya Allah تعالى,

إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ

“Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa Tuliye mneemesha.” (43:59)

Na Kauli Yake Allah تعالى،

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ ۖ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾

“Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam; Alimuumba kwa udongo kisha Akamuambia: Kuwa! Basi akawa”. (3:59)

Wakati zipo Aya zenye maelezo ya wazi “Muhkamaat” zinazoeleza kuwa yeye (Isa عليه السلام) ni kiumbe mmoja wapo miongoni mwa viumbe wa Allah تعالى na kuwa ni mja na Mtume ﷺ, miongoni mwa wajumbe wa Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى،

وَاتَّبِعَاءَ تَأْوِيلِهِ

“Na kutafuta maana yake.” (3:7)

Maana yake: Kuigeuza ili ilingane na vile wanavyotaka wao. Imam Ahmad amenukuu kuwa Aisha رضي الله عنها alisema, Mtume ﷺ alisoma،

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ هُنَّ أُمُّ الْكِتَابِ وَأُخَرُ مُتَشَابِهَاتٌ ۚ

“Yeye Ndiye Aliyekuteremshia Kitabu hichi. Ndani yake zimo Aya muhkam, zenye maana wazi. Hizo ndizo msingi wa Kitabu hichi. Na ziko nyengine Mutashabiha (zinazotatanisha).”

Hadi Kauli Yake Allah تعالى،

أُولُوا الْأَلْبَابِ ﴿٦٠﴾

“Wenye akili.”

Mtume ﷺ akasema،

﴿فَإِذَا رَأَيْتُمُ الَّذِينَ يُجَادِلُونَ فِيهِ، فَهُمْ الَّذِينَ عَنَى اللَّهُ، فَاحْذَرُوهُمْ﴾

“Mtakapowaona ambao wanajadiliana ndani yake, basi hao ni ambao Allah Amewakusudia, hivyo tahadharini nao.”¹

¹ Ahmad 6:48.

Bukhari alinukuu Hadithi sawa na hiyo katika Tafsiri ya Ayah (3:7), kama alivyofanya Muslim katika Kitabu cha *Qadar* (Uweza wa Allah تعالى) katika Sahihi yake, na Abu Dawud katika sehemu ya Sunan yake, kutoka kwa Aisha رضي الله عنها alisema, "Mtume ﷺ aliisoma Aya hii,

هُوَ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَيْكَ الْكِتَابَ مِنْهُ آيَاتٌ مُحْكَمَاتٌ

"Yeye Ndiye Aliyekuteremshia Kitabu hichi. Ndani yake zimo Aya muhkam, zenye maana wazi"

Hadi Kauli Yake Allah تعالى,

وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٧٠﴾

"Lakini hawakumbuki hayo isipokuwa wenye akili."

Aisha رضي الله عنها amesema: Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا رَأَيْتَ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ مَا تَشَابَهَ مِنْهُ؛ فَأُولَئِكَ الَّذِينَ سَمَى اللَّهُ، فَاحْذَرُوهُمْ»

"Utakapowaona ambao wanafuata yanayotatanisha, basi hao ni ambao Allah Amewataja, Basi jihadharini nao".¹

Hadithi hii pia imepokewa na Imamu Bukhari.

Allah تعالى Pekee Ndiye Ajuaye Tafsiri ya Kweli ya Mutashaabihaat

Allah تعالى Amesema,

وَمَا يَعْلَمُ تَأْوِيلَهُ إِلَّا اللَّهُ

"Na wala hapana ajuaye maana yake ila Mwenyezi Mungu."

Wanazuoni wasomaji wa Qur'an wana rai zenye kutofautiana kuhusu kutua baada ya kusoma Aya hiyo. Imesemwa kwamba kisimamo kipo kwenye jina Tukufu la Allah تعالى, ni kama ilivyotangulia kutajwa kwamba Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, kuna *Tafsir* za aina nne. *Tafsir* ambayo hakuna udhuru wa

¹ Fat'hul Al-Bari 8:57, Muslim 4:2053, Abu Dawud 5:6.

kutokujua, *Tafsir* wanavyoijua Waarabu kilugha, *Tafsir* wanayojua wanazuoni, na *Tafsir* ambayo Anaijua Allah تعالى Peke Yake¹. Kauli hii imesimuliwa kutoka kwa Aisha, Urwah, Abu Ash-Shatha na Abu Nahik na wengineo رضي الله عنهم. Baadhi wanasimama baada ya kusoma,

وَالرَّاسِخُونَ فِي الْعِلْمِ

“Na wale wenye msingi madhubuti katika ilimu.”

Wenye mtazamo huu wafuasi wao ni wengi miongoni mwa wafasiri na wanazuoni wa Misingi na kanuni za kisharia *“Usuul”*. Na wamesema: ‘Qur’an haiwezi kulingania watu kile wasichokielewa’. Ibn Abu Najih alisema kutoka kwa Mujahid alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mimi ni miongoni mwa wenye msingi madhubuti katika *Ta’awil* (ufafanuzi)”². Mtume ﷺ aliomba Dua kwa manufaa ya Ibn Abbas رضي الله عنهما,

«اللَّهُمَّ تَقْنِنِي فِي الدِّينِ وَعَلِّمْنِي التَّأْوِيلَ»

“Ewe Alah! Mfundishe ilimu katika Dini na mfundishe Ta’awil (ufafanuzi)”³

Ta’awil ina maana mbili ndani ya Qur’an, uhakika wa jambo, na jambo litakavyokuwa. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema,

وَقَالَ يَتَابِتْ هَذَا تَأْوِيلُ رُءْيَايَ مِنْ قَبْلُ

“Na akasema: Ewe baba yangu! Hii ndiyo tafsiri ya ile ndoto yangu ya zamani.” (12:100)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

هَلْ يَنْظُرُونَ إِلَّا تَأْوِيلَهُ ۗ يَوْمَ يَأْتِي تَأْوِيلَهُ

“Je, lipo wanalolingoja isipokuwa matokeo yake? Siku yatapofika matokeo yake.” (7:53)

¹ At-Tabari 1:57.

² At-Tabari 6:203.

³ Fat’hul Al-Bari 1:205; Ahmad (2399) 4:225.

Maana yake: Uhakika wa yale waliyoelezwa kuhusu Siku ya kurejea. Ikiwa hii ndio maana iliyokusudiwa katika Ayah hapo juu, basi kutua kisimamo ni baada ya kusoma Jina la Allah تعالی, kwa sababu Allah تعالی Pekee ndiye Ajuaye ukweli wa mambo na jinsi yatakavyokuwa. Katika hali hii Kauli Yake Allah تعالی .

وَالرَّسُخُونَ فِي الْعِلْمِ

“Na wale wenye msingi madhubuti katika ilimu.”

Inakuwa katika Sarufi ya lugha ya kiarabu “*Mubtadah*” Maana husomwa kwa kuanzia hapo. Na Kauli Yake Allah تعالی ,

يَقُولُونَ ءَأَمِنَّا بِهِ

“Husema: Sisi tumeziamini.”

Inakuwa katika sarufi ya lugha ya kiarabu “*khabari*” Maana yake: Inayotoa maelezo ya “*Mubtada*” kilichoanzwa. Na ama Iwapo neno *Ta’awil* lina maana ya pili, nayo ni ubainifu na ufafanuzi. Kama Alivyosema Allah تعالی ,

نَبِّئْنَا بِتَأْوِيلِهِ

“Tuambie tafsiri yake.” (12:36)

Maana yake: Tafsiri na maelezo yake. Iwapo itakusudiwa maana hii, basi kutua kisimamo ni baada ya kusoma,

وَالرَّسُخُونَ فِي الْعِلْمِ

“Na wale wenye msingi madhubuti katika ilimu.”

Ni kwa sababu, wanakijua na wanakielewa walichohutubiwa kwacho katika maelezo hayo, japokuwa hawana ilimu ya uhakika wa kiini cha mambo. Kwa hiyo, maneno ya Allah تعالی ,

يَقُولُونَ ءَأَمِنَّا بِهِ

“Husema: Sisi tumeziamini.” Katika sarufi ya kiarabu inabeba kanuni ya “Hali” Yaani, hali yakuwa hiyo ni hali inayotokana nao. Linaruhusiwa jambo hili, nalo ni katika kuunganisha kitu pasina kuchukua hukumu ya maelezo ya kile chenye kuunganishwa juu yake kama Neno Lake Allah تعالی ,

وَجَاءَ رَبُّكَ وَالْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا ﴿٢٢﴾

“Na Atakuja Mola wako Mlezi na Malaika safu safu.” (89:22)

Maana yake: Malaika watakuja hali ya kupangana safu. Kauli ya Allah تعالى Kueleza habari zao,

يَقُولُونَ ءَأَمْنًا بِهٖ

“Husema: Sisi tumeziamini.”

Maana yake: Wanaamini Aya zenye Maelezo ya utatanishi *“Mutashaabih.”*

كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ رَبِّنَا

“Zote zimetoka kwa Mola wetu Mlezi.”

Maana yake: Zote zenye maelezo ya wazi *“muhkam”* na zenye maelezo ya utatanishi *“Mutashaabih”* ni za ukweli na ni sahihi, na kila mojawapo inathibisha ukweli wa nyingine. Hii ni kwa sababu zote zinatoka kwa Allah تعالى na hapana kitokacho kwa Allah تعالى chenye migongano au hitilafu. Kwa uthibitisho wa Kauli Yake Allah تعالى,

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ أَلْقُرْآنَ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا كَثِيرًا ﴿٨٢﴾

“Hebu hawazingatii Qur’ani hii? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangelikuta ndani yake khitilafu nyingi”. (4:82)

Kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Amesema katika Aya:

وَمَا يَذَّكَّرُ إِلَّا أُولُو الْأَلْبَابِ ﴿٧٧﴾

“Lakini hawakumbuki hayo isipokuwa wenye akili.”

Maana yake: Wenye akili timamu na ufahamu mzuri, uelewa, kutafakari na kuzingatia maana katika njia iliyo sahihi. Zaidi, Ibn Al-Mundhir alinukuu katika *Tafsir* kuwa Nafii bin Yazid alisema, “wale wenye msingi madhubuti katika ilimu ni wale wenye staha kwa ajili ya Allah تعالى, wakitaka ridhaa ya Allah تعالى kwa unyenyekevu, na hawawakwezi mno walio juu yao wala hawawadharau walio chini yao”.

Kisha Allah تعالى Amesema kuhusu wao kuwa waliomba Dua kwa Mola wao.

رَبَّنَا لَا تُزِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا

(Na hao husema): “Mola wetu Mlezi! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kwisha tuongoa.”

Maana yake: “Usizipotoe nyoyo zetu kutoka kwenye uwongozi baada ya kuturuhusu kuupata. Usitufanye kama wale wenye uovu ndani ya nyoyo zao, wale wanaofuata Aya zenye maelezo tatanishi “Mutashaabih” ndani ya Qur’an. Bali, tubakize imara katika Njia Yako iliyonyooka na Dini sahihi”.

وَهَبْ لَنَا

“Na Utupe.” Maana yake: Kutoka kwako,

مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً

“Rehema itakayo Kwako.”

Ambayo kwayo Umeifanya mioyo yetu madhubuti, na Unaupa nguvu umoja wetu, na kuongeza Imani zetu na yakini,

إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ

“Hakika Wewe Ndiye Mpaji.”

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى walinukuu kuwa Ummu Salamah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alikuwa akiomba,

«يَا مُقَلَّبَ الْقُلُوبِ بَيِّنْ قَلْبِي عَلَى دِينِكَ»

“Ewe Mwenye Kubadili nyoyo, ithibitisha nyoyo yangu kwenye Dini Yako.” Kisha akasoma,

رَبَّنَا لَا تُزِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَّدُنكَ رَحْمَةً إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ

“(Na hao husema): Mola wetu Mlezi! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kwisha tuongoa, na Utupe Rehema itakayo Kwako. Hakika Wewe Ndiye Mpaji.¹

¹ Ibn Abu Hatim 2:84, At-Tabari 6:213.

Na Kauli Yake Allah تعالى,

رَبَّنَا إِنَّكَ جَامِعُ النَّاسِ لِيَوْمٍ لَا رَيْبَ فِيهِ

“Mola wetu Mlezi! Wewe Ndiye Mkusanyaji wa watu kwa Siku isiyo na shaka ndani yake.”

Maana yake: Wanasema katika maombi yao: “Mola wetu! Utakusanya viumbe Vyako katika siku ya marejeo yao, na Utawapambanulia, na Utatoa uamuzi katika yale waliyobishania. Baada ya hapo, Utawalipa au Kuwaadhibu kila mmoja kwa mujibu wa amali alizozifanya wakati wa uhai wake, ima za kheri au za shari”.

* * *

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَنْ تُغْنِيَ عَنْهُمْ
 أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ
 مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۗ وَأُولَئِكَ هُمْ
 كَذَّابُونَ ﴿١٠﴾
 فِرْعَوْنَ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ
 كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ
 بِذُنُوبِهِمْ ۗ وَاللَّهُ شَدِيدُ
 الْعِقَابِ ﴿١١﴾ قُلْ لِلَّذِينَ
 كَفَرُوا سَعْتَةٌ ۖ وَتُحْشَرُونَ
 إِلَىٰ جَهَنَّمَ ۖ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٢﴾
 قَدْ كَانَ لَكُمْ آيَةٌ فِي فِتْنَةِ
 آلِفِرْعَوْنَ ۖ فَهَيَّا لَهُمْ فِي
 سَبِيلِ اللَّهِ وَأُخْرَىٰ كَافِرَةٌ
 يَرَوْنَهَا ۚ لَيْسَ لَكَ مِنَ اللَّهِ
 لَاحِزٌ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً
 لِّأُولِي الْأَبْصَارِ ﴿١٣﴾ زُيِّنَ
 لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ
 النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ وَالْقَنَاطِيرِ
 الْمُمْقَنْطَرَةِ مِنَ الذَّهَبِ وَالْفِضَّةِ
 وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ وَالْأَنْعَامِ
 وَالْأَنْعَامِ وَالْأَنْعَامِ ۗ ذَٰلِكَ
 مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَاللَّهُ
 عِنْدَهُ حُسْنُ الْمَقَابِلِ ﴿١٤﴾ * قُلْ
 أُوتِيتُكُمْ بِخَيْرٍ مِّنْ ذَٰلِكُمْ
 ۗ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا عِندَ رَبِّهِمْ
 جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا
 الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَأَزْوَاجٌ
 مُّطَهَّرَةٌ وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ
 ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿١٥﴾

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَنْ تُغْنِيَ عَنْهُمْ
 أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۗ
 وَأُولَئِكَ هُمْ كَذَّابُونَ ﴿١٠﴾
 فِرْعَوْنَ وَالَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ
 كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَأَخَذَهُمُ اللَّهُ
 بِذُنُوبِهِمْ ۗ وَاللَّهُ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١١﴾

10. Kwa hakika wale walio-kufuru hazitowafaa kitu chochote kwa Mwenyezi Mungu malizao, wala watoto wao; nao hao ndio kuni za Motoni.

11. Kama yaliyo wapata watu wa Firauni na waliokuwa kabla yao. Walikanusha Aya Zetu, basi Mwenyezi Mungu Aliwaangamia kwa madhambi yao; na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa Kuadhibu.

Siku ya Kiyama, Mali na Watoto Haitowasaidia.

Allah تعالى Anasema kuwa makafiri watakuwa kuni za Motoni,

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ ۖ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿١٥﴾

“Siku ambayo hautawafaa madhaalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata makaazi mabaya kabisa”. (40:52)

Zaidi ya hayo, walichoruzukiwa katika maisha ya dunia iwe mali au watoto havitawasidia kwa Allah تعالى, au kuwaokoa na adhabu na mateso yake makali. Pia Allah تعالى Anasema,

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ
أَنْفُسُهُمْ وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٥٥﴾

“Yasikuajabishe mali yao wala wana wao. Hakika Mwenyezi Mungu Anataka Kuwaadhibu kwayo hapa duniani, na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri”. (9:55) Na Allah تعالى Amesema:

لَا يَغُرُّكَ تَقَلُّبُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي الْبِلَادِ ﴿١٩٦﴾ مَتَّعٌ قَلِيلٌ ثُمَّ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ﴿١٩٧﴾

“Kabisa kusikudanganye kubakia kutangatanga kwa waliokufuru katika nchi. Hiyo ni starehe ndogo. Kisha makaazi yao yatakuwa Jahannamu. Na ni mahali pabaya mno pa kupumzikia.” (3:196-197)

Kama Allah تعالى Alivyosema katika Aya hii,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Kwa hakika wale waliokufuru.” Maana yake: Waliokanusha Aya za Allah تعالى, waliwakanusha Mitume Wake, wakaenda kinyume na Vitabu Vyake na hawakunufaika na Ufunuo Wake kwa Mitume Wake,

لَنْ تُغْنِيَ عَنْهُمْ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا وَأُولَئِكَ هُمْ وَقُودُ النَّارِ ﴿٩٨﴾

“Hazitowafaa kitu kwa Mwenyezi Mungu mali zao, wala watoto wao; nao hao ndio kuni za Motoni”.

Maana yake: Kuni zake za Kuwachomea na Kuwaunguza.

Kama vile Kauli Yake Allah تعالى,

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ

“Hakika nyinyi na hao mnaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni kuni za Jahannamu”. (21:98)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

كَذَّابٌ ءَالِ فِرْعَوْنَ

“Kama yaliyowapata watu wa Firaun”.

Adh-Dhahhak alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa Ayah hii ina maana, "Kama ilivyokuwa tabia ya watu wa Firauni."¹ Tafsir hii ni sawa na ya Ikrimah, Mujahid, Abu Malik, Adh-Dhahhak, na wengine. Miongoni mwao wanasema kuwa Ayah hii ina maana, "Kama mwenendo wa watu wa Firauni; na kama matendo ya watu wa Firauni; na kama mfano wa watu wa Firauni."² Matamko haya yanakaribiana. *Da'ab* ina maana ya matendo, shughuli, jambo na desturi, kwa mfano, kama isemwavyo, "Hii ni *Da'ab* (desturi) yangu na yako." Ayah inaamaanisha kuwa makafiri hawatunufaika na mali wala watoto. Bali wataangamia na wataadhibiwa. Ni kama yaliyowafika watu wa Firauni na kaumu zilizawatangulia, miongoni mwa wale waliokataa Mitume pamoja na Ishara na ushahidi wa Allah تعالى waliotumwa nao.

وَاللَّهُ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿١٠﴾

"Na Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu". Maana yake: Adhabu Yake ni kali na mateso Yake yanaumiza. Hapana atakayeepa Mkono wa Allah تعالى, wala atakayeepa Ufahamu Wake. Allah تعالى Hufanya Alitakalo na Anashinda juu ya kila kitu, na kila kitu kimedhalilishwa Kwake na hapana mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye.

قُلْ لِلَّذِينَ كَفَرُوا سَعْتَابُونَ وَتَحْشُرُونَ إِلَىٰ جَهَنَّمَ ۖ وَيَسَّسَ الْأَمْهَادُ ﴿١٠﴾ قَدْ
كَانَ لَكُمْ آيَةٌ فِي فِئَتَيْنِ الَّذِينَ اتَّقَوْا ۖ فَمَا تَقْبَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَأُخْرَىٰ كَافِرَةٌ يَرَوْنَهُمْ
مِثْلِهِمْ رَأَىٰ الْعَيْنِ ۖ وَاللَّهُ يُؤَيِّدُ بِنَصَرِهِ مَن يَشَاءُ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَعِبْرَةً لِّأُولِي
الْأَبْصَارِ ﴿١١﴾

12. Waambie walio kufuru: Karibuni mtashindwa na mtakusanywa, mtiwe kwenye Jahannam; nako huko ni makazi mabaya kabisa.

13. Hakika ilikuwa ni maonyo na mazingatio kwenu katika yale majeshi mawili yalipopambana. Jeshi moja likipigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na jingine kafiri likiwaona zaidi kuliko wao mara mbili, kwa kuona kwa macho. Na Mwenyezi Mungu Humdhihirishia Nguvu Zake Amtakaye kwa Nusura Yake. Hakika katika hayo yapo mazingatio kwa watu wenye utambuzi.

¹ At-Tabari 6:224. Adh-Dhahaak hakukutana na Ibn Abbas: Sanadi yake ni dhaifu.

² Ibn Abu Hatim 2:92.

Mayahudi Wakhofishwa kwa Kushindwa na Wanatakiwa Kujifunza Kutokana na Vita vya Badr:

Allah تعالی Alimuamuru Mtume Muhammad ﷺ kuwatangazia makafiri,

سَتُغْلَبُونَ

“Karibuni mtashindwa.” Katika maisha haya ya dunia.

وَتُحْشَرُونَ

“Na mtakusanywa.” katika siku ya Kiama.

إِلَىٰ جَهَنَّمَ ۚ وَيَبْسُ أَلْمِهَادُ

“Mtiwe kwenye Jahannam; nako huko ni makazi mabaya kabisa”

Muhammad bin Is-haq bin Yasar رحمه الله تعالی alinukuu kuwa Asim bin Umar bin Qatadah alisema kuwa, “Mtume ﷺ alipopata ushindi katika vita vya Badr na akarejea Madinah, aliwakusanya Mayahudi katika soko la Bani Qainuqa. Na akasema; *“Enyi Mayahudi ingieni katika Uislamu! Kabla hayajawakuta yale yaliyowakuta Maquraishi”*

Mayahudi wakasema, ‘Ewe Muhammad, usijidanganye kwa kuwa umewapiga Maqurayshi waliochanganyikiwa, ambao hawajui kupigana vita. Tunaapa kwa Mwenyezi Mungu! Lau utapigana na sisi, ndio utatujua hasa sisi ni akina nani, inaelekea bado hujakutana na watu mithili yetu.’ Hivyo Allah تعالی Akateremsha kwa maneno yao haya:

قُلْ لِلَّذِينَ كَفَرُوا

“Waambie waliokufuru.” Hadi Kauli Yake Allah تعالی,

لِأُولِي الْأَبْصَارِ

“Kwa watu wenye utambuzi.”¹

Na Kauli Yake Allah تعالی,

قَدْ كَانَ لَكُمْ آيَةٌ

“Hakika ilikuwa ni Ishara kwenu.”

¹ At-Tabari 6:234.

Maana yake: Enyi Mayahudi, mliosema mliyoyasema! Mna ishara, yaani ni ushahidi, kuwa Allah تعالى Ataifanya Dini Yake ishinde. Atampa ushindi Mjumbe, Atalidhihirisha Neno Lake na Dini Yake kuwa Juu.

فِي فُتَيْينَ

“Katika yale majeshi mawili.” Maana yake: Kambi mbili.

الَّتَقْنَا

“Yalipopambana.” Katika badri.

فَعَةً تُقْتَلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ

“Jeshi moja likipigana katika njia ya Mwenyezi Mungu.”

Hao ni Waislamu,

وَأُخْرَى كَافِرَةٌ

“Na jingine kafiri.”

Maana yake: Washirikina wa Kiquraishi katika Badr. Kauli ya Allah تعالى,

يَرَوْنَهُمْ مِّثْلَهُمْ رَأَى الْعَيْنِ

“Ikiwaona zaidi kuliko wao mara mbili kwa kuona kwa macho.”

Maana yake: Washirikina walidhani ya kuwa Waislamu walikuwa mara mbili zaidi yao. Kwani Allah تعالى Aliufanya uoni wao huo kuwa ni sababu ya ushindi wa Waislamu dhidi yao.

Kadhalika, yameelezwa maelezo mengine tofauti na hayo. Kuwa maana ya Kauli ya Allah تعالى,

يَرَوْنَهُمْ مِّثْلَهُمْ رَأَى الْعَيْنِ

“Ikiwaona zaidi kuliko wao mara mbili kwa kuona kwa macho.”

Maana yake: Waislamu waliwaona washirikina mara mbili zaidi yao, yaani makafiri wakiwa wengi kuliko wao. Hata hivyo Allah تعالى Aliwapa ushindi dhidi ya makafiri. Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema, “Tulipoangalia majeshi ya makafiri, tuliyaona kuwa mara mbili kuliko tulivyokuwa. Tulipowaangalia tena tulidhani hawakutuzidi hata kwa mtu mmoja.” Hivyo Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذْ يُرِيكُمُوهُمْ إِذِ التَّقِيْتُمْ فِي آعْيُنِكُمْ قَلِيْلًا وَيُقَلِّلُكُمْ فِي آعْيُنِهِمْ

“Na mlipokutana Akakuonesheni machoni mwenu kuwa wao ni wachache, na Akakufanyeni nyinyi ni wachache machoni mwao.” (8:44)¹

Abuu Is-hak amesema kutoka kwa Abuu Ubaida, kutoka kwa Abdillah bin Mas’ud رضي الله عنه amesema: ‘Hakika walipunguzwa idadi yao machoni mwetu, hadi nikasema kumuambia mtu mmoja aliyekuwa karibu nami: Utadhani idadi yao ni kama watu sabiini?’ Akasema: ‘Ninavyooneshwa mimi ni kama watu mia moja.’ Akasema: ‘Hivyo, tukamteka mtu mmoja miongoni mwao, tukasema, idadi yenu mlikuwa watu wangapi?’ Akasema: ‘Elfu moja.’¹

Wakati pande mbili zilipokabiliana, Waislamu walidhani kuwa makafiri walikuwa wengi, mara mbili zaidi yao.

Hivyo walimuamini Allah تعالى ili wamtegemee na kuomba msaada wake. Makafiri walidhani waumini walikuwa mara mbili zaidi yao, hivyo waliogopa, wakapatwa na kihoro, na wakakata tamaa. Pande mbili ziliposimama katika safu na kukabiliana katika vita. Allah تعالى Aliifanya kila kambi kuiona nyingine chache ili washajiike kupigana,

لَيَقْضِيَ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا

“ili Mwenyezi Mungu Atimize jambo lililokuwa lazima litendeke,” (8:42)

Maana yake: Ili ukweli na uongo uweze kupambanuliwa, na hivyo neno la ukweli linaushinda upotofu na uasi, ili waumini washinde na makafiri wadhaliishwe. Katika Kauli sawa na hiyo, Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ

“Na Mwenyezi Mungu Alikwisha kunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge.” (3:123)

Katika Aya hii Allah تعالى hapa Amesema,

¹ At-Tabari 6:234.

² At-Tabari 6:236.

وَاللَّهُ يُؤَيِّدُ بِنَصَرِهِ مَن يَشَاءُ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَعِبْرَةً لِّأُولِي الْأَبْصَارِ ﴿١٣﴾

“Na Mwenyezi Mungu Humuunga mkono Amtakaye kwa Nusura Yake. Hakika katika haya mna mazingatio kwa watu wenye utambuzi”. (3:13)

Maana yake: Huu ni mfano kwa wale wenye akili na mazingatio. Lazima watafakari juu ya Hikima ya Allah تعالى, Maamuzi na Amri, kuwa huwa Anawapa ushindi waja Wake waumini hapa duniani na siku (ya kiama) mashahidi watasimama kuthibitisha.

زُيِّنَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ وَالْقَنَاطِيرِ الْمُقَنْطَرَةِ مِنَ الذَّهَبِ
وَالْأَفْضَةِ وَالْخَيْلِ الْمُسَوَّمَةِ وَالْأَنْعَامِ وَالْحَرْثِ ۗ ذَلِكَ مَتَّعَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ۗ وَاللَّهُ عِنْدَهُ
حُسْنُ الْمَقَابِلِ ﴿١٤﴾ * قُلْ أُوْتِيتُكُمْ بِخَيْرٍ مِّنْ ذَٰلِكُمْ ۗ لِلَّذِينَ اتَّقَوْا عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنَّاتٌ
تَجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا وَأَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌ
بِالْعِبَادِ ﴿١٥﴾

14. Watu wamepambiwa namna za matamano ya kuwafitinisha katika kuwapenda wanawake, na wana, na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi wenye uzuri wa asili, na mifugo, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema.

15. Sema: Nikuambieni yaliyo bora kuliko hayo? Kwa wachamngu ziko Bustani kwa Mola wao zipitazo mito kati yake. Watadumu humo, na wale waliotakaswa, na wanazo radhi za Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja wake,

Maelezo Kuhusu Maisha ya Duniani:

Allah تعالى Anataja vitu vya Kuwapendezesha watu Alivyowapambia katika maisha haya ya duniani kama vile wanawake na watoto, na Alianza na wanawake, kwa sababu mtihani wao una ushawishi mno, kama ilivyothibiti kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا تَزَكَّتْ بَعْلِي فِتْنَةً أَضَرَ عَلَى الرَّجَالِ مِنَ النِّسَاءِ»

"Sikuacha baada yangu mtihani wenye madhara zaidi kwa wanaume kuliko wanawake."¹

Ama ikiwa makusudio ya kuwaendea wanawake ni kujihifadhi na machafu na kupata watoto, hilo ndilo litakikanalo na lina manufaa. Ni kama zilivyopokewa Hadithi nyingi zinazohimiza ndoa na kuongeza watoto,

«وَأِنَّ خَيْرَ هَذِهِ الْأُمَّةِ مَنْ كَانَ أَكْثَرَهَا نِسَاءً»

"Na kwa hakika mbora wa umati huu ni ambaye ni mwingi wao wa wanawake."²

Na maneno yake mengine, Mtume ﷺ

«الدُّنْيَا مَتَاعٌ، وَخَيْرُ مَتَاعِهَا الْمَرْأَةُ الصَّالِحَةُ»

"Dunia ni starehe na kheri ya starehe yake ni mwanamke mwema."

Mume anapomtazama humpa faraja, na akiwa yupo mbali naye, mwanamke hujichunga yeye mwenyewe na mali yake.³

Mtume ﷺ alisema kwenye Hadithi nyingine,

«حُبِّبَ إِلَيَّ النِّسَاءُ وَالطَّيِّبُ، وَجُعِلَتْ قُرَّةُ عَيْنِي فِي الصَّلَاةِ»

"Kumependezeshwa kwangu wanawake na manukato, na pozo la jicho langu likafanywa katika Sala."⁴

¹ Fat'hul Al-Bari 9:41.

² Fat'hul Al-Bari 9:15.

³ Muslim 1:512.

⁴ An-Nasai Al-Kubra 5:280.

Aisha رضي الله عنها alisema, “Hapana kilichompendeza zaidi Mtume ﷺ kuliko wakeze isipokuwa farasi.” Na katika mapokezi mengine kutoka kwa Anas رضي الله عنه, “kuliko farasi isipokuwa wakeze”.¹

Hamu ya kuwa na watoto wakati mwingine ni kwa lengo la majivuno na majisifu. Jambo hili nalo linaingia hapa. Wakati mwingine huwa ni kwa ajili ya kuongeza ukoo na kuuzidisha Ummah wa Muhammad ﷺ miongoni mwa wanaomuabudu Allah تعالى Pekee bila mshirika, hili ni jambo jema na lenye kusifiwa.

Kama ilivyothibiti katika Hadithi,

اتَّزَوْجُوا الْوُدُودَ الْوُلُودَ، فَإِنِّي مُكَاتِرٌ بِكُمْ الْأَمَمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Oeni wenye upendo wenye kuzaa, kwani mimi nitajifakharisha nanyi kwa umati zingine siku ya kiama.”²

Tamaa ya mali halikadhalika, mara nyingine huwa ni kwa ajili ya ufahari na majivuno, kuwafanyia kiburi wanyonge na kuwakandamiza masikini. Tabia hii imeharamishwa. Wakati mwingine, huwa ni kwa ajili ya kuwakimu ndugu, kuimarisha udugu na namna mbalimbali za wema na utii, mwenendo huu unasifiwa na kushajiishwa katika Sharia.

Wanazuoni wa *Tafsir* wana rai zinazotofautiana kuhusu kima cha *Qintar*, zote zinaonesha kuwa *Qintar* ni mali nyingi, kama Adh-Dhahak na wanazuoni wengine walivyosema.³ (Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kwamba *Qintaar* moja ni sawa na *Uwqiyah* elfu kumi na mbili, na kila *Uwqiyah* ni bora kuliko baina ya mbingu na ardhi. Hii ilinukuliwa na Ibn Jarir رحمه الله تعالى⁴).

Kupenda kuwa na farasi ni namna tatu. Kuna wakati watu huwafuga farasi ili watumike katika njia ya Allah تعالى, na wanapowahitaji huwatumia katika vita. Wamiliki hawa hupata malipo mema. Mara nyingine huwafuga kwa ajili ya ufahari na kufanya uadui kwa Waislamu, wamiliki wa farasi wa aina hii watabeba mzigo (wa madhambi). Na wakati mwingine ni kwa ajili ya kukidhi

¹ An-Nasai Al-Kubra 6:217, 7:61.

² Abu Dawud, An-Nasai, Ibn Hibbaan 6:134.

³ At-Tabari 6:250.

⁴ At-Tabari 6:252.

haja zao na kukusanya watoto (wa farasi) na hawasahau haki za Allah تعالی zinazostahiki juu ya farasi wao. Wamiliki wake watapata stara, kama ilivyothibitishwa na Hadithi ambayo tutaitaja, Allah تعالی Akipenda, tutakapoeleza Kauli ya Allah تعالی,

وَأَعِدُّوا لَهُمْ مَا اسْتَطَعْتُمْ مِنْ قُوَّةٍ وَمِنْ رِبَاطِ الْخَيْلِ

“Basi waandalieni nguvu kama muwezavyo, na kwa farasi walio fungwa tayari-tayari”. (8:60)

Ama kuhusu “Musawwamah” Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa ni farasi wenye kwenda malishoni na wazuri. Maelezo haya ni sawa na ya Mujahid, Ikrimah, Said bin Jubayr, Abdur-Rahman bin Abdullah bin Abza, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas na Abu Sinan na wengineo.¹ Mak-hul alisema “Musawwamah” ni farasi mwenye madoa meupe usoni, na farasi² mwenye miguu meupe.³ Pia imesemwa kuwa si hao wa namna hiyo.

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَيْسَ مِنْ فَرَسٍ عَرَبِيٍّ إِلَّا يُؤَدُّ لَهُ مَعَ كُلِّ فَجْرٍ يَدْعُو بِدَعْوَتَيْهِ يَقُولُ: اللَّهُمَّ إِنَّكَ خَوَّلْتَنِي مِنْ بَنِي آدَمَ، فَأَجْعَلْنِي مِنْ أَحَبِّ مَالِهِ وَأَهْلِهِ إِلَيْهِ - أَوْ أَحَبِّ أَهْلِهِ وَمَالِهِ إِلَيْهِ»⁴

“Hakuna farasi yoyote wa kiarabu isipokuwa ameruhusiwa pamoja na kila Alfajiri kuomba dua mbili, anasema: Ewe Mola, hakika Wewe Umenifanya mtumishi wa binadamu, basi nifanye ni katika mali yake pendwa zaidi, na watu wake kwake, au mpendwa zaidi wa watu wake kwake na mali yake.”

Kauli ya Allah تعالی,

وَالْأَنْعَامِ

“Na mifugo.” Maana yake: Ngamia, Ng'ombe na Kondoo.

¹ Ibn Abu Hatim 2:123-125.

² Ibn Abu Hatim 2:127.

³ Ahmad 5:170.

وَالْحَرْثِ

“Na mashamba.”

Ina maana: Ardhi inayotumika kwa ajili ya kulima na kupanda mimea. Kisha Allah تعالى Amesema,

ذَلِكَ مَتْنُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

“Hayo ni starehe ya maisha ya duniani.”

Maana yake: Hizi ndio starehe za maisha ya dunia na furaha ya muda mfupi tu,

وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْبُ الْمَقَابِلِ

“Na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema.”

Maana yake: Mwisho mzuri na malipo.

Malipo ya Wachamungu ni Bora Kuliko Starehe zote za Dunia:

Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema,

* قُلْ أَوْفَيْتُكُمْ بِحَيْرٍ مِّنْ ذَلِكُمْ

“Sema: Nikuambieni yaliyo bora kuliko hayo?”

Aya hii ina maana, “Sema, Ewe Muhammad, kuwaambia watu, “Je, nikuambieni juu ya lile lililo bora kuliko waliyopambiwa watu katika maisha haya ya duniani miongoni mwa starehe zake na neema zake ambazo kwa hakika zitatoweka?” Kisha Akawaeleza yaliyo bora Aliposema,

لِّلَّذِينَ أَتَقَوْا عِنْدَ رَبِّهِمْ جَنَّاتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Kwa wachamngu ziko Bustani kwa Mola wao zipitazo mito kati yake.”

Maana yake: Mito inayotiririka katika pande zote kwa kupitisha vinywaji anuwai: asali, maziwa, mvinyo, maji na vingine, kiasi hapana jicho lililoyaona, hapana sikio lililoyasikia, wala haijapata kuingia katika fikira za mwanadamu.

خَلْدَيْنَ فِيهَا

“Watadumu humo.”

Maana yake: Watakaa humo milele, huku wakiwa hawana tamaa ya kutaka mambo hayo kubadilika.

وَأَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ

“Na wake waliotakaswa.”

Maana yake: Kutokana na Uchafu, Taka, Hedhi, Nifasi, na mambo mengine yanayowaathiri wanawake wa duniani.

وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ

“Na wanazo Radhi za Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Radhi za Allah تعالى Zitawashukia na Hatowakasirikia baada ya hapo. Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema katika Surah *Bara'ah*,

وَرِضْوَانٌ مِّنَ اللَّهِ أَكْبَرُ

“Na Radhi za Mwenyezi Mungu ndio kubwa kuliko yote.” (9:72)

Maana yake: Kuliko furaha ya milele Aliyowajaalia. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja wake.”

Na Anawapa riziki kama wanavyostahili.

* * *

الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا إِنَّنَا ءَامِنَا فَاعْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَقِنَا
 عَذَابَ النَّارِ ﴿١٦﴾ الصَّابِرِينَ وَالصَّادِقِينَ وَالْقَنِيتِينَ
 وَالْمُنْفِقِينَ وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ ﴿١٧﴾ شَهِدَ
 اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُو الْعِلْمِ قَائِمًا
 بِالْقِسْطِ ۗ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٨﴾ إِنَّ
 الَّذِينَ عِنْدَ اللَّهِ الْأَسْلَمَةُ وَمَا اخْتَلَفَ الَّذِينَ أُوتُوا
 الْكِتَابَ إِلَّا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ ۗ وَمَنْ
 يَكْفُرْ بِآيَاتِ اللَّهِ فَإِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿١٩﴾ فَإِنْ
 حَاجُّوكَ فَقُلْ أَسْلَمْتُ وَجْهِيَ لِلَّهِ وَمَنِ اتَّبَعَنِ ۗ وَقُلْ لِلَّذِينَ
 أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْأُمِّيِّينَ ءَأَسْلَمْتُمْ ۗ فَإِنْ أَسْلَمُوا فَقَدِ
 اهْتَدَوْا ۗ وَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌ
 بِالْعِبَادِ ﴿٢٠﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ
 وَيَقْتُلُونَ النَّبِيَّاتِ بَغْيٍ حَقٍّ وَيَقْتُلُونَ الَّذِينَ
 يَأْمُرُونَ بِالْقِسْطِ مِنَ النَّاسِ فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ
 ﴿٢١﴾ أُولَٰئِكَ الَّذِينَ حَبِطَتِ أَعْمَالُهُمْ فِي الدُّنْيَا
 وَالْآخِرَةِ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿٢٢﴾

الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا إِنَّنَا ءَامِنَا
 فَاعْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ
 ﴿١٦﴾ الصَّابِرِينَ وَالصَّادِقِينَ
 وَالْقَنِيتِينَ
 وَالْمُنْفِقِينَ
 وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ ﴿١٧﴾

16. Ambao husema: Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumeamini, basi tufutie madhambi yetu, na tuepushe na adhabu ya Moto,

17. Wanaosubiri, wanao sema kweli, na watiifu, na wanao toa sadaka, na wanaoomba maghufira kabla ya alfajiri.

Dua na Sifa Bainifu za Wachamungu "Al-Muttaqin"

Allah تعالی Ameerleza sifa bainifu za "Muttaqin" Waja Wake wachamungu, ambao Amewaahidi malipo makubwa,

الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا إِنَّنَا ءَامِنَا

"Ambao husema: Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumeamini." Maana yake: tumekuamini Wewe, Kitabu Chako na Mjumbe Wako,

فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا

“Basi tufutie madhambi yetu.”

Kwa sababu ya Imani yetu Kwako na kwa yale uliyotuamrisha. Kwa hiyo tusamehe dhambi zetu na udhaifu wetu kwa Fadhila na Rehema Zako,

وَفَنَّا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٦﴾

“Na tuepushe na adhabu ya Moto.”

Kisha Allah تعالى Amesema,

الصَّابِرِينَ

“Wanaosubiri.”

Wakati wanafanya amali kwa utiifu na kuacha mambo ya haramu,

وَالصَّادِقِينَ

“Wanaosema kweli.”

Kuhusu kutangaza imani zao kwa kutenda amali zenye taklifu.

وَالْقَانِتِينَ

“Na watiifu.” Neno *Qunut* lililotumika hapa lina maana ya utiifu na unyenyekevu,

وَالْمُنْفِقِينَ

“Na wanaotoa sadaka.” Maana yake: Kutokana na mali zao kwa ajili ya yote waliyoamrisha yanayohusu masuala ya utiifu, kuwatendea wema ndugu na marafiki, kuwasaidia masikini na kuwafaraji.

وَالْمُسْتَغْفِرِينَ بِالْأَسْحَارِ ﴿١٧﴾

“Na wanaoomba maghufira kabla ya Alfajiri.”

Inajulisha fadhila za kuomba maghufira kwa Allah تعالى, sehemu ya mwisho ya usiku. Ilisimuliwa kuwa Ya'qub alipowaambia wanawe,

سَوْفَ أَسْتَغْفِرُ لَكُمْ رَبِّي

“Nitakuja kukuombeeni msamaha kwa Mola wangu Mlezi.” (12:98)

Alisubiri mpaka wakati wa kabla ya Al-fajiri ndipo akaomba Dua. Zaidi ya hayo, Sahihi mbili, *Musnad* na *Sunan* kupitia Masahaba wengi zimerikodi kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يُنزِلُ اللَّهُ تَبَارَكَ وَتَعَالَى فِي كُلِّ لَيْلَةٍ إِلَى سَمَاءِ الدُّنْيَا حِينَ يَنْقُضُ نُلُكُ اللَّيْلِ الْآخِرُ، فَيَقُولُ: هَلْ مِنْ سَائِلٍ فَأُعْطِيَهُ؟ هَلْ مِنْ دَاعٍ فَأَسْتَجِيبَ لَهُ؟ هَلْ مِنْ مُسْتَغْفِرٍ فَأُغْفِرَ لَهُ؟»

*“Allah تعالى Anashuka katika kila usiku kwenye mbingu ya dunia kunapobakia theluthi ya mwisho ya usiku, Anasema: Je kuna muombaji Nimpe?, je kuna mwenye kuomba dua Nimjibu?, je kuna mwenye kuomba maghufira Nimsamehe?”*¹

Sahihi mbili zimeandika kuwa Mama Aisha رضي الله عنها amesema: “Mtume ﷺ alikuwa akisali witri mwanzo wa usiku, katikati na mwisho wake, (katika maisha yake), alisali tu katika wakati wa mwisho wa usiku.”²

Abdullaahi bin Umar رضي الله عنه alikuwa akiswali usiku, na alikuwa akiuliza: “Ewe Naafi, huu tayari ni wakati wa mwisho wa usiku?”, na kama akisema: Ndio, basi Ibn Umar رضي الله عنهما ataanza kumuomba Allah تعالى na kumuomba msamaha wake mpaka Alfajiri. Hadithi hii imepokewa na Ibn Abi Hatim ³. رحمه الله تعالى

شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَالْمَلَائِكَةُ وَأُولُوا الْعِلْمِ قَائِمًا بِالْقِسْطِ ۚ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْعَزِيزُ
الْحَكِيمُ ﴿١٧٠﴾ إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ ۗ وَمَا اخْتَلَفَ الَّذِينَ أوتُوا الْكِتَابَ إِلَّا
مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ ۗ وَمَنْ يَكْفُرْ بِبَايَعَاتِ اللَّهِ فَإِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ
﴿١٧١﴾ فَإِنْ حَاجُّوكَ فَقُلْ أَسْلَمْتُ وَجْهِيَ لِلَّهِ وَمَنِ اتَّبَعَنِ ۗ وَقُلْ لِلَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ
وَالْأُمِّيِّينَ ءَأَسْلَمْتُمْ ۚ فَإِنْ أَسْلَمْتُمْ فَقَدْ أَهْتَدُوا ۗ وَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاغُ ۗ وَاللَّهُ
بَصِيرٌ بِالْعِبَادِ ﴿١٧٢﴾

¹ Fat’hul Al-Bari 11:133, Muslim 1:521, Abu Dawud 2:77, Tuhfatul Al-Ahwadhi 9:471, An-Nasai katika Al-Kubra 6:123, Ibn Majah 1:435, Ahmad 2:487.

² Fat’hul Al-Bari 2:564, Muslim 1:512.

³ Ibn Abu Hatim 2:145.

18. Mwenyezi Mungu, na Malaika, na wenye ilimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana mola ila Yeye, Ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana mola ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye Hikima.

19. Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu. Na waliopewa Kitabu hawakukhitalifiana ila baada ya kuwajia ujuzi, kwa sababu ya uhasidi uliokuwa baina yao. Na anaepinga Qur'an maneno ya mwingi wa Rehema basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.

20. Na pindi wakikuhoji, basi sema: Mimi nimeusalimisha uso wangu kumuelekea Mwenyezi Mungu, na kadhaalika walionifuata. Na waambie waliopewa Kitabu na wasiojua kusoma: Je! Mmesilimu? Wakisilimu basi wameongoka. Na wakikengeuka basi juu yako ni kufikisha ujumbe tu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja wake.

Ushuhuda wa Kumpwekesha Allah تعالى, "Tawhid"

Allah تعالى Mwenyewe Ameshuhudia, na inatosha Kwake Yeye kuwa Shahidi, Yeye ni Mkweli wa mashahidi wote na Muadilifu wao, na Msema kweli kushinda viumbe wote.

أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

"hakika hapana mola ila Yeye." Maana yake: Viumbe wote wanatakiwa kumfanya Yeye Mmoja tu katika Uungu. Na kwamba viumbe wote wanamuhitajia Yeye. Na Yeye ni Mkwasi Hahitajii chochote kutoka kwao. Kama Allah تعالى Alivyosema:

لَكِنَ اللَّهُ يَشْهَدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ

"Lakini Mwenyezi Mungu Anayashuhudia Aliyokuteremshia wewe." (4:166)

Kisha Allah تعالى Akakutanisha Ushuhuda Wake pamoja na Ushuhuda wa Malaika Wake na watu wenye elimu. Hivyo, Akasema,

شَهِدَ اللَّهُ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَأَمَلَائِكَتُهُ وَأُولُوا الْعِلْمِ

"Mwenyezi Mungu, na Malaika, na wenye ilimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana mola ila Yeye."

Na huu ni uhusishwaji wenye taadhima kwa wanazuoni katika nafasi hii.

قَائِمًا بِالْقِسْطِ

“Mwenye kusimamisha uadilifu.”

Maana yake: Yeye katika hali zote Yupo hivyo.

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

“Hapana mola ila Yeye.”

Ni msisitizo wa maelezo yaliyopita.

الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.”

Mwenye Nguvu ambaye hakuna wa kuzishinda, Mwenye Hekima katika Kauli Zake, Vitendo Vyake, Sharia Zake na Kadari Yake.

Hakika Dini ya Kweli Mbele ya Allah تعالى ni Uislamu

Na Kauli Yake Allah تعالى,

إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ

“Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu.”

Haya ni maelezo kutoka kwa Allah تعالى ya kwamba hakuna Dini yoyote kutoka kwa yeyote Anayoikubali isipokuwa Uislamu, nayo ndio waliofuata Mitume wote Aliowatuma katika kila zama, hadi Mtume wa mwisho Muhammad ﷺ ambaye yeye ndiye aliyehitimishiwa Uislamu.

Hivyo basi, mtu yeyote atakayekuja kutana na Allah تعالى baada ya kupewa Utume Muhammad ﷺ akiwa na Dini iliyo tofauti na sharia Yake, hatokubaliwa mtu huyo. Kama Aliyetukuka Alivyosema:

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ

“Na anayetafuta dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake.”

(3:85)

Na Amesema katika aya hii kwa Kuelezea kuwa Dini inayokubalika Kwake ni Uislamu pekee.

إِنَّ الدِّينَ عِنْدَ اللَّهِ الْإِسْلَامُ

“Bila ya shaka Dini mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu.”

Kisha Allah تعالى Akahabarisha kwamba wale ambao wamepewa kitabu huko nyuma.

Hakika si vingine walitofautiana baada ya hoja kusimama juu yao kwa Kupelekewa Mitume na Kuteremshiwa vitabu juu yao. Allah تعالى Akasema,

جَاءَهُمُ الْعِلْمُ بَغْيًا بَيْنَهُمْ

“Baada ya kuwajia ujuzi, kwa sababu ya uhasidi uliokuwa baina yao.”

Maana yake: Walifanya uovu baadhi yao juu ya baadhi nyingine. Hivyo wakatofautiana katika haki. Kwa sababu ya husda yao, chuki yao na kuelekea mashonde.

Hivyo baadhi yao wakawachukia wengine kwa kuipinga elimu hiyo, kwa maneno na vitendo ijapokuwa ni ya kweli.

Kisha Allah تعالى Amesema;

وَمَنْ يَكْفُرْ بِآيَاتِ اللَّهِ

“Na anayezikataa Ishara za Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Yeyote anayekataa yaliyoteremshwa na Allah تعالى ndani ya Kitabu Chake,

فَإِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ

“Basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa kuhisabu.”

Allah تعالى Atamuadhibu kwa sababu ya hilo, Atamhesabu kwa kukanusha kwake, na Atampa adhabu kwa kukikhalifu Kitabu Chake. Kisha Allah تعالى Amesema,

فَإِنَّ حَاجُوكَ

“Na pindi wakikuhoji.” Maana yake: Sema, “Ibada zangu ni kwa ajili ya Allah تعالى Pekee bila washirika, washindani, watoto au mke.”

فَقُلْ أَسْلَمْتُ وَجْهِيَ لِلَّهِ

“Basi sema: Mimi nimeusalimisha uso wangu kumuelekea Mwenyezi Mungu.”

وَمَنْ اتَّبَعِنِ

“Na kadhalika walionifuata.” Maana yake: Waliofuata Dini yangu na wakafuata maneno yangu. Ni kama Allah تعالى Alivyosema,

قُلْ هَذِهِ سَبِيلِي أَدْعُوا إِلَى اللَّهِ عَلَىٰ بَصِيرَةٍ أَنَا وَمَنِ اتَّبَعَنِي

“Sema: Hii ndiyo Njia yangu - ninalingania kwa Mwenyezi Mungu kwa kujua - mimi na wanaonifuata.” (12:108)

Uislamu ni Dini ya Watu wote na Mtume ﷺ Alitumwa kwa Wote:

Kisha Allah تعالى Amezungumzia katika Kumuamrisha mja wake na Mtume, Muhammad ﷺ, kuwalingania watu waliopewa Vitabu viwili na washirikina wasiojua kusoma na kuandika katika Dini yake, njia, Sharia na yote yale Allah تعالى Aliyomtuma nayo. Allah تعالى Amesema,

وَقُلْ لِلَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ وَالْأُمِّيِّينَ ءَأَسْلَمْتُمْ ؕ فَإِنْ أَسْلَمُوا فَقَدِ اهْتَدَوْا ؕ وَإِنْ تَوَلَّوْا

فَأِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلَاغُ

“Na waambie waliopewa Kitabu na wasio na kisomo: Je! Mmesilimu? Wakisilimu basi wameongoka. Na wakikengeuka basi juu yako ni kufikisha ujumbe tu.”

Maana yake: Hesabu yao ni kwa Allah تعالى na kurejea kwao na makazi ya mwisho ni Kwake. Ni Yeye Ndiye Ambaye Anamuelekeza Amtakaye na Humruhusu kwenda kombo Yule Amtakaye, na Ana Hikima isiyo na dosari na Ushahidi usiopingika kwa yote haya. Ndio sababu Allah تعالى Amesema,

وَاللَّهُ بِصِرِّ الْعِبَادِ عَلِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwaona waja wake.”

Kwani Ana yakini kwa yule anayestahiki kuongozwa na yule asiyestahiki hilo la kuongozwa, kwani,

لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ ﴿٢٣﴾

“Yeye hahojiwi kwa Ayatendayo, na wao ndio wanahojiwa kwa wayatendayo”. (21:23)

Na yote hayo hufanyika kwa sababu ya Hikima na Huruma Yake. Ayah hii na nyingine kama hii ni miongoni mwa ushahidi ulio wazi kabisa kuwa Ujumbe wa Muhammad ﷺ ni kwa viumbe wote, kama ilivyoelezwa katika Dini yake, kwa mujibu wa maandiko mbalimbali ya Kitabu na Sunnah. Kwa mfano, Allah تعالی Amesema,

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا

“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote.” (7:158)

Na Allah تعالی Amesema,

تَبَارَكَ الَّذِي نَزَّلَ الْفُرْقَانَ عَلَى عَبْدِهِ لِيَكُونَ لِلْعَالَمِينَ نَذِيرًا ﴿٢٥﴾

“Ametukuka Aliyeteremsha Furqani kwa mja wake, ili awe mwonyaji kwa walimwengu wote.” (25:1)

Sahihi Mbili na vitabu vingine vya Hadithi vimenukuu kuwa Mtume ﷺ alipeleka barua za kuwalingania kwa Allah تعالی, wafalme kadhaa wakati wa utawala wake, pia kwa jamii tofauti, Waarabu na wasiokuwa Waarabu, watu wa Kitabu na wasiojua kusoma, kama Allah تعالی Alivyowaamrisha.¹ Abdur-Razzaq alinukuu kuwa Ma'mar kutoka kwa Hammam alisema kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ alisema,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَا يَسْمَعُ بِي أَحَدٌ مِنْ هَذِهِ الْأُمَّةِ: يَهُودِيٌّ وَلَا نَصْرَانِيٌّ، وَمَاتَ وَلَمْ يُؤْمِنْ بِالَّذِي أُرْسِلْتُ بِهِ، إِلَّا كَانَ مِنْ أَهْلِ النَّارِ»

“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake, hasikii yeyote kutoka kwangu katika umma huu, Myahudi wala Mnaswara, na akafa na hakuniamini kwa nilichotumwa nacho, isipokuwa atakuwa katika watu wa motoni”.²

¹ Fat'hul Al-Bari 1:42, Muslim 4:1993.

² Muslim 1:134.

Mtume ﷺ alisema,

«بُعِثْتُ إِلَى الْأَخْمَرِ وَالْأَسْوَدِ»

“Nimetumwa kwa wekundu na weusi.” Na akasema:

«كَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً، وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً»

“Kila Mtume alikuwa akitumwa kwa watu wake mahususi, na nimetumwa kwa watu wote.”¹

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ النَّبِيَّاتِ بِغَيْرِ حَقٍّ وَيَقْتُلُونَ الَّذِينَ
يَأْمُرُونَ بِالْقِسْطِ مِنَ النَّاسِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٢١﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ حَبِطَتْ
أَعْمَلُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿٢٢﴾

21. Hakika wale wanaozikanusha Aya za Mwenyezi Mungu, na wakawaua Manabii pasipo haki, na wakawaua watu waamrishao Haki wabashirie adhabu kali.

22. Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika duniani na Akhera. Nao hawatapata wa kuwanusuru.

Mayahudi Kushutumiwa kwa kufuru yao na Kuaa Mitume na Watu Wema

Ayah hii inawashutumu Watu wa Kitabu kwa kuchupa mipaka na kutenda yaliyoharamishwa kwa kukanusha yaliyopita na yale ya siku ya karibuni, waliyofikishiwa na Mitume; kuwafanyia kwao kiburi na ukaidi; kuukataa ukweli na kutoufuata.

Licha ya hayo waliua Mitume ﷺ walipowafikishia yale waliyoamrishwa na Allah تعالى, bila sababu wala kufanya makosa ya jinai, bali ni kwa kuwalingania wao katika wito wa haki.

وَيَقْتُلُونَ الَّذِينَ يَأْمُرُونَ بِالْقِسْطِ

“Na wakawaua watu waamrishao Haki.”

¹ Al-Bukhari 335.

Na huo ndio ufedhuli wa hali ya juu. Kwa hakika Mtume ﷺ amesema,

«الْكِبْرُ بَطْرُ الْحَقِّ وَغَمَطُ النَّاسِ»

“Kiburi ni kukandamiza ukweli na kudharau watu.”²

Hii ndio sababu, walipokataa ukweli na wakafanya kiburi kwa viumbe, Allah تعالی Aliwaadhibu na Kuwadhalilisha katika maisha ya dunia, na watapata adhabu yenye kudhalilisha siku ya kiyama. Allah تعالی Amesema,

فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿١٦﴾

“Wabashirie adhabu kali.”

Maana yake: Inayoumiza na kuhilikisha,

أُولَئِكَ الَّذِينَ حَبِطَتِ أَعْمَلُهُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿١٦﴾

“Hao ndio ambao vitendo vyao vimeharibika duniani na Akhera. Nao hawatapata wa kuwanusuru.”

* * *

¹ Muslim 1:93.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ يُدْعَوْنَ
 إِلَى كِتَابِ اللَّهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ يَتَوَلَّى فَرِيقٌ مِّنْهُمْ
 وَهُمْ مُّعْرِضُونَ ﴿٢٣﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لَن نَّمَسِّنَا
 النَّارَ إِلَّا أَيَّامًا مَّعْدُودَاتٍ ۗ وَغَرَّهُمْ فِي دِينِهِمْ مَا
 كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢٤﴾ فَكَيْفَ إِذَا جُمِعْتَهُمْ لِيَوْمٍ
 لَا رَيْبَ فِيهِ وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا
 يُظْلَمُونَ ﴿٢٥﴾ أَللَّهُمَّ مَلَكَ الْمَلَائِكَةِ تَوْتِي الْمَلَائِكَةِ
 مَن نَشَاءُ وَتَنزِعُ الْمَلَائِكَةَ مِمَّن نَشَاءُ وَتُعْزِزُ
 مَن تَشَاءُ وَتُذِلُّ مَن تَشَاءُ ۗ بِيَدِكَ الْخَيْرُ ۗ
 إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٦﴾ تُولِجُ اللَّيْلَ فِي
 النَّهَارِ وَتُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ ۗ وَتُخْرِجُ
 مِنَ الْأَمْنِ مَن تَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢٧﴾ لَا يَتَّخِذِ
 الْمُؤْمِنُونَ الْكُفْرِينَ أَوْلِيَاءَ مِن دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ۗ
 وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ اللَّهِ فِي شَيْءٍ
 إِلَّا أَن تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقَنَّةً ۗ وَيُحَذِّرُكُمُ اللَّهُ نَفْسَهُ ۗ
 وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٢٨﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا مِّنَ
 الْكِتَابِ يُدْعَوْنَ إِلَى كِتَابِ اللَّهِ
 لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ يَتَوَلَّى فَرِيقٌ مِّنْهُمْ
 وَهُمْ مُّعْرِضُونَ ﴿٢٣﴾ ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ
 قَالُوا لَن نَّمَسِّنَا النَّارَ إِلَّا أَيَّامًا
 مَّعْدُودَاتٍ ۗ وَغَرَّهُمْ فِي دِينِهِمْ مَا
 كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢٤﴾ فَكَيْفَ إِذَا
 جُمِعْتَهُمْ لِيَوْمٍ لَا رَيْبَ فِيهِ وَوُفِّيَتْ
 كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا
 يُظْلَمُونَ ﴿٢٥﴾

23. Huwaoni wale walio
 pewa sehemu ya Kitabu?
 Wanaitwa kukiendea
 Kitabu cha Mwenyezi
 Mungu ili kiwahukumu
 baina yao; kisha baadhi yao
 wanageuka wanakikataa.

24. Hayo ni kwa sababu
 walisema: Hautatugusa

Moto isipokuwa kwa siku chache tu. Na yakawadanganya katika dini yao yale ambayo wenyewe walikuwa wakiyazua.

25. Basi itakuwaje Tutakapowakusanya Siku ambayo haina shaka kuja kwake? Na kila nafsi italipwa kama ilivyo chuma, bila ya kudhulumiwa.

Makosa ya Watu wa Kitabu Juu ya Kutohukumu kwa Kutumia Kitabu cha Allah تعالى:

Allah تعالى Anawakosoa Mayahudi na Wakristo wanaoshikamana na wanavyodai kuwa ni vitabu vyao, Taurati na Injili. Na wanapoitwa kwa ajili ya kuvirejea Vitabu hivyo kwa ajili ya kumtii Allah تعالى katika Aliyowaamuru ambamo Aliwaamuru wamfuate Muhammad ﷺ, hukataa na kuvipa mgongo. Na huu ndio ukomo wa madhambi yao uliosababishwa na khitilafu zao na ukaidi. Kisha Allah تعالى Akasema,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لَنْ نَمَسَّنَا إِلَّا آيَاتًا مَّعْدُودَاتٍ ^ط

“Hayo ni kwa sababu walisema: Hautatugusa Moto isipo kuwa kwa siku chache tu”.

Ikiwa na maana kuwa kilichowafanya wathubutu kupinga ukweli ni madai yao potofu kuwa Allah تعالى Atawaadhibu kwa Kuwatia motoni kwa siku saba tu, ambapo siku moja ni sawa na miaka elfu moja ya hapa duniani. Somo hili tulilijadili katika Tafsir ya *Suratu Al-Baqarah*. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَعَرَّهْمُ فِي دِينِهِمْ مَا كَانُوا يَفْتَرُونَ ﴿٢٤﴾

“Na yakawadanganya katika dini yao yale ambayo wenyewe walikuwa wakiyazua”.

Maana yake: Kudumu kwao katika imani yao potofu ni kwa kuwa walijidanganya wenyewe, huku wakiamini kuwa moto utawagusa siku chache tu kutokana na makosa yao. Hata hivyo, ni wao wenyewe ndio waliojizushia dhana hiyo, na Allah تعالى Hakuwapa mamlaka yanayounga mkono madai haya. Allah تعالى Alisema huku Akiwatisha na Kuwapa ahadi,

فَكَيْفَ إِذَا جَمَعْنَاهُمْ لِيَوْمٍ لَا رَيْبَ فِيهِ

“Basi itakuwaje Tutakapowakusanya Siku ambayo haina shaka kuja kwake.”

Ina maana: “Hali yao itakuwaje baada ya kuwa wamesema uongo kuhusu Alla تعالى, wakawakataa Mitume Yake na wakawaua Mitume Wake na Wanazuoni wao waliokuwa wakiamrisha mema na kukataza maovu.” Allah تعالى Atawauliza kuhusu yote haya na Atawaadhibu kwa waliyoyafanya. Ndio sababu Allah تعالى Amesema,

فَكَيْفَ إِذَا جَمَعْتَهُمْ لِيَوْمٍ لَا رَيْبَ فِيهِ

“Basi itakuwaje Tutakapowakusanya Siku ambayo haina shaka kuja kwake.” (3:25)

Maana yake: Hapana shaka kuwa siku hiyo itakuja.

وَوُفِّيَتْ كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٢٦﴾

“Na kila nafsi italipwa kama ilivyochuma, bila ya kudhulumiwa.” (3:25)

قُلِ اللَّهُمَّ مَلِكُ أَلْمَلِكِ تُؤْتِي أَلْمَلِكَ مَن دَشَاءَ وَتَنزِعُ أَلْمَلِكَ مِمَّن دَشَاءَ وَتُعْزِزُ مَن دَشَاءَ وَتُذِلُّ مَن دَشَاءَ بِيَدِكَ أَلْخَيْرُ إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٧﴾ تُولِجُ أَلَّيْلَ فِي أَلنَّهَارِ وَتُؤَلِّجُ أَلنَّهَارَ فِي أَلَّيْلِ وَتُخْرِجُ أَلْحَيَّ مِّنَ أَلْمَيِّتِ وَتُخْرِجُ أَلْمَيِّتَ مِّنَ أَلْحَيِّ وَتَرْزُقُ مَن دَشَاءَ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢٨﴾

26. Sema: Ewe Mwenyezi Mungu Uliyemiliki Ufalme wote! Wewe Humpa ufalme Umtakaye, na Humuondolea ufalme Umtakaye, na Humtukuza Umtakaye, na Humdhalilisha Umtakaye. Kheri yote iko Mikononi Mwako. Hakika Wewe ni Muweza wa kila kitu.

27. Wewe Huingiza usiku katika mchana, na Huuingiza mchana katika usiku. Na Humtoa hai kutokana na maiti, na Humtoa maiti kutokana na aliye hai. Na Unamruzuku Umtakaye bila ya hisabu.

Muongozo Unaopelekea kwenye Kushukuru:

Allah تعالى Amesema,

قُلِ

“Sema.” Ewe Muhammad ﷺ kwa kumtukuza Mola wako, kumshukuru Yeye, Kumtegemea Yeye pamoja na kutaka Hifadhi Kwake”

أَللَّهُمَّ مَلِكُ أَلْمَلِكِ

“Ewe Mwenyezi Mungu Uliyemiliki ufalme wote!”Maana yake: Ufalme wote ni Wako,

تُؤْتِي الْمُلْكَ مَنْ تَشَاءُ وَتَنْزِعُ الْمُلْكَ مِمَّنْ تَشَاءُ وَتُعِزُّ مَنْ تَشَاءُ وَتُذِلُّ مَنْ تَشَاءُ

“Wewe Humpa ufalme Umtakaye, na Humuondolea ufalme Umtakaye, na Humtukuza Umtakaye, na Humuangusha Umtakaye.”

Maana yake: Wewe ni Mtoaji, Wewe ni Mchukuaji, na Utashi Wako ndio Unaokuwa, na lolote Usilolitaka halitokei. Katika Ayah hii kuna maonyo na mwongozo wa namna ya kumshukuru Allah تعالى kwa neema Alizompa Mtume wake ﷺ na Ummah Wake. Ni kwa sababu Allah تعالى Aliuhamisha Utume kutoka kwa Wana wa Israel kwenda kwa Mwarabu, Mquraishi, mtu wa Makkah, asiyejua kuandika wala kusoma kilichoandikwa - “Ummiy”, Mtume wa mwisho kabisa, naye ni Mtume ﷺ kwa binadamu wote na Majini. Allah تعالى Alimjaalia Mtume ﷺ kuwa na sifa bora kuliko Mitume waliokuja kabla yake. Pia Allah تعالى Alimjaalia sifa za ziada ambazo hapana Mtume wala Nabii kabla yake aliyeruzukiwa - kuwa na elimu ya Allah تعالى na Sharia Yake; elimu zaidi juu ya mambo ya kale na yajayo; ummah wake kuenea toka mashariki mwa dunia mpaka magharibi yake na Dini na Sharia yake kuzishinda dini na sharia nyingine. Rehema na Amani za Allah تعالى ziwe juu ya Mtume ﷺ mpaka Siku ya Hukumu, muda wa kuwa mchana na usiku vinabadilishana. Hii ndio sababu Allah تعالى Amesema,

قُلِ اللَّهُمَّ مَلِكُ الْمُلْكِ

“Sema: Ewe Mwenyezi Mungu Uliyemiliki Ufalme wote!”Maana yake: Wewe Ndiye Unayeamua Unalolitaka kuhusu viumbe Wako na Unafanya Ulitakalo. Allah تعالى Anawakanusha wale waliodhani kuwa wangeamua kwa niaba ya Allah تعالى katika jambo lake, pale Aliposema:

وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ هَذَا الْقُرْآنُ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنَ الْقَرْيَتَيْنِ عَظِيمٍ

“Na walisema: Kwa nini Qur’ani hii haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii?.” (43:31)

Allah تعالى Aliwakanusha kwa Kusema,

أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ

“Kwani wao ndio wanaogawa Rehema za Mola wako Mlezi?.” (43:32)

Maana yake: “Tunaamua kwa ajili ya viumbe yale Tuyatakayo, bila uasi au vikwazo kutoka kwa yeyote. Sisi Tuna hekima na hoja zilizo wazi kamilifu katika hayo, na Tunampa Utume yule Tumtakaye.” Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ تَجْعَلُ رِسَالَتَهُ

“Mwenyezi Mungu Ndiye Mjuzi kuliko wote kujua wapi Anaweka ujumbe Wake”. (6:124)

Na Allah Amesema,

أَنْظِرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ

“Angalia vipi Tulivyowafadhili baadhi yao kuliko wengine.” (17:21)

Allah Amesema,

تُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَتُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ

“Wewe Huuingiza usiku katika mchana, na Huuingiza mchana katika usiku.”

Maana yake: Unachukua kutoka urefu wa kimojawapo katika hivyo na kuongeza katika kilicho kifupi ili vililingane, na Kuchukua urefu wa mmoja wao na Kuuongeza kwa mwingine ili visilingane, kisha vinakuwa sawasawa. Hili hutokea katika misimu yote ya mwaka: masika, kipupwe, kiangazi na kusi. Kauli ya Allah,

وَتُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَتُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ

“Na Humtoa hai kutokana na maiti, na Humtoa maiti kutokana na aliye hai.”

Maana yake: Anazitoa mbegu kutokana na mmea; mmea kutokana na mbegu, mtende kutokana na mbegu na mbegu ya mtende kutokana na mtende. Waumini kutokana na makafiri na makafiri kutokana na waumini. Kuku kutokana na yai na yai kutokana na kuku, vivyo hivyo katika mengine.

وَتَرْزُقُ مَنْ نَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٧٧﴾

“Na Unamruzuku Umtakaye bila ya hisabu”. Ina maana: Unampa yeyote Umtakaye utajiri usio na kifani wakati Unawanyima wengine, kutokana na Hikima, Utashi na Uadilifu Wako.

لَا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ

اللَّهِ فِي شَيْءٍ إِلَّا أَنْ تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقْنَةً وَيُحَذِّرْكُمْ اللَّهُ نَفْسَهُ ۗ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٧٨﴾

28. Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu."

Kuharamishwa Kuwafanya Makafiri Marafiki

Allah تعالی Amewaharamisha waja wake waumini kuwafanya rafiki makafiri, au kuwafanya vipenzi vya kuwapa siri badala ya waumini. Allah تعالی Ameonya kuhusu mwenendo huo Aliposema,

وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ اللَّهِ فِي شَيْءٍ

"Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu."

Maana yake: Yeyote afanyaye lililokatanzwa na Allah تعالی, basi Allah تعالی Atamtelekeza. Vivyo hivyo Allah تعالی Amesema,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا عَدُوِّي وَعَدُوَّكُمْ ءَوْلِيَاءَ تَلْفُوتَ إِلَيْهِمْ بِالْمَوَدَّةِ

"Enyi mlioamini! Msiwafanye adui zangu na adui zenu kuwa marafiki mkiwapa mapenzi." Mpaka

وَمَنْ يَفْعَلْهُ مِنْكُمْ فَقَدْ ضَلَّ سَوَاءَ السَّبِيلِ ﴿٦٠﴾

"Na mwenye kufanya hayo kati yenu basi ameipotea njia ya sawa." (60:1), Allah تعالی Amesema,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْكٰفِرِينَ ءَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ؕ أَتُرِيدُونَ أَنْ تَجْعَلُوا لِلّٰهِ

عَلَيْكُمْ سُلْطٰنًا مُّبِينًا ﴿١٤٤﴾

"Enyi mlioamini! Msiwafanye makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je, mnataka Mwenyezi Mungu Awe na hoja iliyo wazi juu yenu?" (4:144) Na Kauli Yake Allah تعالی,

* يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْيَهُودَ وَالنَّصٰرَى ءَوْلِيَاءَ ۗ بَعْضُهُمْ ءَوْلِيَاءُ بَعْضٍ ۗ وَمَنْ

يَتَوَلَّهُمْ فَاِنَّهُمْ مِنْهُمْ

“Enyi mlioamini! Msiwafanye Mayahudi na Wakristo kuwa ni marafiki. Wao ni marafiki wao kwa wao. Na miongoni mwenu mwenye kufanya urafiki nao, basi huyo ni katika wao.” (5:51)

Allah تعالى Alisema haya baada ya kutaja urafiki wa waumini kwa waumini miongoni mwa Muhajirina, Ansar na Mabedui,

وَالَّذِينَ كَفَرُوا بَعْضُهُمْ أَوْلِيَاءُ بَعْضٍ إِلَّا تَفْعَلُوهُ تَكُنْ فِتْنَةٌ فِي الْأَرْضِ وَفَسَادٌ كَبِيرٌ ﴿٥١﴾

“Na wale waliokufuru ni marafiki wenyewe kwa wenyewe. Msipo fanya hivi itakuwako fitna katika nchi na fisadi kubwa.” (8:73)

Baada ya hapo Allah تعالى Akasema,

إِلَّا أَنْ تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقَنَّةً

“Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao.” (3:28)

Maana yake: Isipokuwa wale waumini katika baadhi ya maneno au baadhi ya nyakati wanachelea usalama wao kutokana na makafiri. Katika hali hii, waumini hao hudhihirisha urafiki na makafiri kwa nje lakini haupo katika nyoyo zao. Kwa mfano, Bukhari alinukuu kuwa Abu Ad-Darda رضي الله عنه alisema, “Tunaonesha nyuso za tabasamu kwa baadhi ya watu, japokuwa mioyo yetu inawalaani.”¹ Bukhari amesema kuwa Al-Hasan alisema, “Tuqyah² imeruhusiwa mpaka siku ya Kiyama.” Allah تعالى Amesema,

وَيُحَذِرُكُمْ اللَّهُ نَفْسَهُ

“Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye...” (3:28), Maana yake: Anakutahadharisheni kutokana na Ghadhabu Yake na Adhabu kali Aliyowaandalia waliowasaidia adui Zake, na wale wenye uadui na marafiki Zake,

وَالِي اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٢٨﴾

“Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu”.

Ina maana kuwa marejeo ni Kwake na Atamlipa au Kumwadhibu kila mtu kwa mujibu wa amali zake.

¹ Fat’h Al-Bari 10:544.

² Kutokudhihirisha kilichomo moyoni.

قُلْ إِنْ تُخْشَوْنَ مَا فِي صُدُورِكُمْ أَوْ تُبْدُوهُ يَعْلَمَهُ اللَّهُ
 وَيَعْلَمُ مَا فِي السَّمَانِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَاللَّهُ عَلَى كُلِّ
 شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٩﴾ يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ
 خَيْرٍ مُّحْضَرًا وَمَا عَمِلَتْ مِنْ سُوءٍ تَوَدُّ لَوْ أَنَّ بَيْنَهَا
 وَبَيْنَهُ أَمَدًا بَعِيدًا وَيُحَذِّرُكُمُ اللَّهُ نَفْسَهُ وَاللَّهُ رَءُوفٌ
 بِالْعِبَادِ ﴿٣٠﴾ قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ
 وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣١﴾ قُلْ أَطِيعُوا
 اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْكٰفِرِينَ ﴿٣٢﴾
 * إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرٰهِيْمَ وَآلَ عِمْرٰنَ
 عَلَى الْعٰلَمِينَ ﴿٣٣﴾ ذُرِّيَّةً بَعْضُهَا مِنْ بَعْضٍ وَاللَّهُ سَمِيعٌ
 عَلِيمٌ ﴿٣٤﴾ إِذْ قَالَتْ أَمْرًاتُ عِمْرٰنَ رَبِّ إِنِّي نَدَرْتُ لَكَ
 مَا فِي بَطْنِي مُحَرَّرًا فَتَقَبَّلْ مِنِّي إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ
 ﴿٣٥﴾ فَلَمَّا وَضَعَتْهَا قَالَتْ رَبِّ إِنِّي وَضَعْتُهَا أُنْثَىٰ وَاللَّهُ أَعْلَمُ
 بِمَا وَضَعْتَ وَلَيْسَ الذَّكَرُ كَالْأُنْثَىٰ وَإِنِّي سَمَّيْتُهَا مَرْيَمَ وَإِنِّي
 أُعِيذُهَا بِكَ وَذُرِّيَّتَهَا مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيمِ ﴿٣٦﴾
 فَتَقَبَّلَهَا رَبُّهَا بِقَبُولٍ حَسَنٍ وَأَنْبَتَهَا نَبَاتًا حَسَنًا وَكَفَّلَهَا
 زَكَرِيَّا كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا زَكَرِيَّا الْمِحْرَابَ وَجَدَ عِنْدَهَا
 رِزْقًا قَالَ يَمْرِئُمُ إِنِّي لَكِ هٰذَا قَالَتْ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ

إِنَّ اللَّهَ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٧﴾

قُلْ إِنْ تُخْشَوْنَ مَا فِي صُدُورِكُمْ أَوْ
 تُبْدُوهُ يَعْلَمَهُ اللَّهُ وَيَعْلَمُ مَا فِي
 السَّمَانِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَاللَّهُ عَلَى
 كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٩﴾ يَوْمَ تَجِدُ
 كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ
 مُّحْضَرًا وَمَا عَمِلَتْ مِنْ سُوءٍ تَوَدُّ لَوْ
 أَنَّ بَيْنَهَا وَبَيْنَهُ أَمَدًا بَعِيدًا
 وَيُحَذِّرُكُمُ اللَّهُ نَفْسَهُ وَاللَّهُ رَءُوفٌ
 بِالْعِبَادِ ﴿٣٠﴾

29. Sema: Mkificha yaliyomo
 vifuani mwenu aumkiyafichua
 Mwenyezi Mungu Anayajua;
 na Anayajua yaliyomo
 mbinguni na yaliyomo duniani.
 Na Mwenyezi Mungu ni
 Muweza wa kila kitu.

30. Siku ambayo kila nafsi
 itakuta mema iliyoyafanya
 yamehudhurishwa, na pia
 ubaya ilioufanya. Itapenda
 nafsi lau kungekuwako
 masafa marefu baina ya
 ubaya huo na yeye. Na
 Mwenyezi Mungu Anaku-
 hadharisheni Naye. Na
 Mwenyezi Mungu ni Mpole
 kwa waja Wake.

Allah تعالی Anajua Yanayofichwa na Mioyo na Siku ya Kiyama Atazihudhurisha Amali Zote za Mja:

Allah تعالی Anawaeleza waja Wake kuwa Anajua siri, dhamira na mambo ya dhahiri, na hapana linalowahusu linalompita Allah تعالی. Bali, Elimu Yake inawaenea wote katika hali, zama, vitambo na nyakati zote. Elimu Yake inayaenea yote yaliyo mbinguni na ardhini, na hapana kilicho chembe ndogo, au kilicho kidogo kuliko hicho duniani, baharini na milimani kinachoepa Uoni Wake.

وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢٩﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kila kitu.”

Na Uweza Wake Unakienea kila kitu. Ayah hii inawazindua waja wa Allah تعالی ili wapate kumuogopa Yeye kiasi cha kutofanya Aliyoyakataza au Anayoyachukia, kwani, bila shaka, Anayajua mambo yao yote na Ana Uweza wa Kuwaadhibu sawia. Na Huwapa baadhi yao nafasi ya kupumua, kisha Huwaadhibu Adhabu Yake, Yeye Mwenye Nguvu, Mwenye Uwezo.

Hii ndiyo sababu Allah تعالی Alisema baada ya hapo,

يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ مُّحَضَّرًا

“Siku ambayo kila nafsi itakuta mema iliyoyafanya yamehudhurishwa.”

Maana yake: Siku ya Kiyama, Allah تعالی Atahudhurisha amali njema na mbovu mbele ya waja, kama Alivyosema,

يُنَبِّئُوا الْإِنْسَانَ يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ﴿٧٥﴾

“Siku hiyo ataambiwa aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha”.
(75:13)

Mja atakapoona mema yake, yatamfurahisha na kumfariji. Na akiona maovu yake, atahuzunika na kukasirika na kusunoneka. Kisha atatamani kukataa maovu yake na kuwa masafa marefu yanayomtenganisha nayo. Pia atamuambia shetani ambaye alifuatana naye wakati wa uhai wake, na ambaye akihimiza kufanya maovu.

Kauli ya Allah تعالى:

يَلَيْتَ بَيْنِي وَبَيْنَكَ بَعْدَ الْمَشْرِقَيْنِ فَيَتَسَّ الْقَرَيْنُ ﴿٣٨﴾

“Laiti ungelikuwako baina yangu na wewe kama umbali baina ya mashariki na magharibi. Rafiki mwovu mno wewe!”. (43:38)

Kisha Allah تعالى Akasema katika hali ya Kutilia mkazo, Kutisha na Kuonya,

وَيُحَذِّرُكُمْ اللَّهُ نَفْسَهُ

“Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye.”

Maana yake: Anawatieni khofu dhidi ya Adhabu Yake. Kisha Allah تعالى Amesema, huku Akiwapa Waja Wake matumaini, ili wasikate tamaa kupata Rehema na Huruma Zake,

وَاللَّهُ رءُوفٌ بِالْعِبَادِ ﴿٣٩﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja Wake.”

Hassan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Allah تعالى ni Mwema sana kiasi Anakuhadharisheni naye.” Wengine wamesema,¹ “Anawahurumia viumbe Wake na Anawapendelea wabaki katika njia Yake iliyonyooka na Akawachagulia Dini sahihi, na wamfuate Mjumbe Wake Mtukufu.”

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ

﴿٤٠﴾ قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ ط فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْكٰفِرِينَ ﴿٤١﴾

31. Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu Atakupendeni na Atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kufuta madhambi na Mwenye Kurehemu.

32. Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakigeuka basi Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri.

¹ At-Tabari 6:202.

Mapenzi ya Allah ﷻ ni kwa Kumfuata Mtume ﷻ:

Aya hii tukufu inamhukumu kila anayedai kumpenda Allah ﷻ, ilhali hamfuati Muhammad ﷻ. Mtu wa aina hiyo si mkweli katika madai yake mpaka afuate Sharia ya Muhammad ﷻ na Dini yake katika kauli, matendo na hali zake zote. Imenukuliwa katika Sahih kuwa Mtume ﷻ alisema,

«مَنْ عَمِلَ عَمَلًا لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا فَهُوَ رَدٌّ»

“Mwenye kufanya amali isio juu ya jambo letu basi itarudishwa”.¹

Ndiyo sababu Allah ﷻ Akasema hapa,

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ

“Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuatani mimi, Mwenyezi Mungu Atakupendeni.” (3:31)

Maana yake: Mtakachochuma ni zaidi kuliko kutafuta mapenzi Yake, kwani Allah ﷻ Atakupendeni na hilo ni kubwa zaidi. Hasan Al-Basri na chungu ya wanazuoni miongoni mwa *Salaf* wamesema, “Baadhi ya watu wanadai kuwa wanampenda Allah ﷻ. Hivyo Allah ﷻ Aliwajaribu na Aya hii,

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ

“Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuatani mimi, Mwenyezi Mungu Atakupendeni.”²

Kisha Akasema,

وَيَغْفِرَ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٣١﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kufuta madhambi na Mwenye Kurehemu.”

Ina maana, kwa kumfuata Mtume ﷻ, mtachuma yote haya kwa baraka za ujumbe wake. Baada ya hapo Allah ﷻ Anamuamuru kila mtu,

¹ *Fat’h Al-Bari* 5:355.

² *Ibn Abuu Hatim* 2:205.

قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَإِنْ تَوَلَّوْا

“Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakigeuka.”

Maana yake: kwa kuzikhalifu amri za Mtume ﷺ,

فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْكٰفِرِينَ ﴿٣١﴾

“Basi Mwenyezi Mungu Hawapendi makafiri”.

Hivyo, kuthibitisha kuwa kukengeuka njia ya mjumbe inasababisha kuelekea kwenye kufuru. Kwa hakika Allah Hampendi Mwenye sifa kama hiyo, na hata akidai ndani ya nafsi yake anampenda Allah تعالى na kujikurubisha Kwake. Ni mpaka amfuata Nabii asiyejua kusoma wala kuandika kikasomwa, “Ummiy”, Mtume wa mwisho ﷺ kutoka kwa Allah تعالى kwenda kwa viumbe wawili: binadamu na majini. Huyu ni Mtume ﷺ ambaye, endapo Mitume waliopita na Mitume *Ulul Azm* kuwa hai wakati wa enzi zake, wasingekuwa na khiyari ila kumfuata, kumtii, na kushikamana na Sharia yake. Tutaja ukweli huu tutakapoelezea Aya hii,

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ

“Na pale Mwenyezi Mungu Alipochukua ahadi kwa Manabii.”

(3:181)

Allah تعالى Akipenda.

﴿ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿٣١﴾ ذُرِّيَّةً

بَعْضُهَا مِنْ بَعْضٍ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٣٢﴾

33. Hakika Mwenyezi Mungu Alimteua Adam na Nuhu na ukoo wa Ibrahim na ukoo wa Imran juu ya walimwengu wote.

34. Ni uzao wao kwa wao; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kujua.

Wateule Miongoni mwa Walimwengu:

Allah تعالى Anaelezea kuwa Amezifadhilisha familia hizi juu ya walimwengu. Allah تعالى Alimteua Adam عليه السلام, Akamuumba kwa Mikono Yake na Akampulizia roho. Akawaamrisha Malaika wamsujudie Adam عليه السلام, Akamfundisha majina ya kila kitu na Akamruhusu aishi peponi, baadaye Alimteremsha chini kutoka peponi kwa Hikima Yake. Allah تعالى Alimchagua Nuh عليه السلام na Akamfanya Nabii wa kwanza kwa watu wa duniani, wakati watu wakiabudu masanamu na wakavishirikisha vingine na Allah تعالى katika ibada zao bila wao kuwa na hoja ya kufanya hivyo. Akalipiza kisasi kwa vitendo walivyomfanyia Nuh عليه السلام, kwani aliwalingania watu wake usiku na mchana, hadharani na kwa siri, kwa muda mrefu. Hata hivyo kuwalingania katika Dini kuliwafanya wamuepoke zaidi, na hapo ndipo Nuh عليه السلام alipoomba dua dhidi yao. Hivyo Allah تعالى Akawagharikisha, na hapana miongoni mwao aliyeokolewa isipokuwa wale waliofuata dini aliyoteremshiwa Nuh عليه السلام. Pia Allah تعالى Aliichagua nyumba ya Ibrahim عليه السلام, pamoja na Mtukufu wa viumbe na Mtume wa mwisho, Muhammad ﷺ. Pia Allah تعالى Aliichagua nyumba ya Imran, baba wa Maryam bint Imran, mama yake Nabii Isa عليه السلام. Hivyo Isa ni kutokana na kizazi cha Ibrahim عليه السلام, kama tutakavyotaja katika *Tafsir ya Surat Al-An'am*, Allah تعالى Akipenda, na tunamuamini Yeye.

إِذْ قَالَتِ امْرَأَتُ عِمْرَانَ رَبِّ إِنِّي نَذَرْتُ لَكَ مَا فِي بَطْنِي مُحَرَّرًا فَتَقَبَّلْ مِنِّي إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿١٢٥﴾ فَلَمَّا وَضَعَتْهَا قَالَتْ رَبِّ إِنِّي وَضَعْتُهَا أُنْثَىٰ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا وَضَعْتَ وَلَيْسَ الذَّكَرُ كَالْأُنْثَىٰ ۗ وَإِنِّي سَمَّيْتُهَا مَرْيَمَ وَإِنِّي أُعِيذُهَا بِكَ وَذَرَيْتَهَا مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿١٢٦﴾

35. Aliposema mke wa Imran: Mola wangu Mlezi! Mimi nimeweka nadhiri kwa ajili ya dhati yako kilichomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Hakika Wewe Ndiye Mwenye Kusikia na Mwenye Kujua.

36. Basi alipomzaa alisema: Mola wangu Mlezi! Nimemzaa mwanamke - na Mwenyezi Mungu Anajua sana aliyemzaa - Na mwanamume si sawa na mwanamke. Na mimi nimemuita Maryamu. Nami namkinga Kwako, yeye na uzao wake, Uwalinde na Shetani aliye laaniwa.

Kisa cha Kuzaliwa kwa Maryam:

Mke wa Imran aliyetajwa hapa ni mama yake Maryam, na jina lake ni Hannah bint Faqud. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alitaja kuwa Hannah hakupata watoto na siku moja alimuona ndege akimlisha kindi lake. Akatamani kama angekuwa na watoto na akamuomba Allah تعالى Amjaalie watoto. Allah تعالى Alijibu Dua yake, na alipolala na mumewe alipata ujauzito. Alikula yamini ya kumfanya mwanaye adumu katika ibada na kuhudhuria *Bayt Al-Maqdis* (Msikiti uliopo Jerusalem), alipotanabahi kuwa ana mimba alisema,

رَبِّ إِنِّي نَدَرْتُ لَكَ مَا فِي بَطْنِي مُحَرَّرًا فَتَقَبَّلْ مِنِّي إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٤٦﴾

“Mola wangu Mlezi! Nimekuwekea nadhiri kilichomo tumboni mwangu kuwa wakfu; basi nikubalie. Hakika Wewe Ndiye Mwenye Kusikia na Mwenye Kujua”.

Maana yake: Usikiaye maombi yangu na Ujuaye nia yangu. Wakati huo hakujua kama angezaa mtoto wa kiume au wa kike.

فَلَمَّا وَضَعَتْهَا قَالَتْ رَبِّ إِنِّي وَضَعْتُهَا أُنْثَىٰ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا وَضَعْتَ

“Basi alipomzaa alisema: Mola wangu Mlezi! Nimemzaa mwanamke - na Mwenyezi Mungu Anajua sana aliyemzaa”.

وَلَيْسَ الذَّكَرُ كَالْأُنْثَىٰ

“Na mwanamume si sawa na mwanamke.”

Maana yake: Kuwa na nguvu na kwa kujizatiti kumuabudu Allah تعالى na kuuhudumia Msikiti wa Aqsa - *“Al-Masjidul-Aqswaa.”* (Jerusalem).

وَإِنِّي سَمَّيْتُهَا مَرْيَمَ

“Na mimi nimemuita Maryamu.”

Hivyo, inathibitisha ukweli kuwa inaruhusiwa kumpa jina mtoto siku aliyozaliwa, kama ilivyo wazi katika Aya, ambayo pia ni sehemu ya sharia ya waliotutangulia. Zaidi ya hayo, Sunna ya Mtume ﷺ imetaja kuwa Mtume ﷺ alisema,

«وُلِدَ لِي اللَّيْلَةَ وَوَلَدٌ، سَمَّيْتُهُ بِاسْمِ أَبِي إِبْرَاهِيمَ»

“Usiku wa leo amezaliwa mtoto wangu, nimemuita kwa jina la baba yangu Ibrahiim.”¹

Bukhari na Muslim wameipokea hadithi hii.

Pia walinukuu kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alimleta ndugu yake mchanga kwa Mtume ﷺ ambaye alimtafunia kipande cha tende na akakitia kinywani mwa mtoto na akampa jina.² Watoto wengine walipewa majina katika siku waliyozaliwa.

Qatadah alisimulia kuwa Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema kuwa Samurah bin Jundab رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«كُلُّ غُلَامٍ رَجِيْنٌ بِعَقِيْقَتِهِ، يُذْبِحُ عَنْهُ يَوْمَ سَابِعِهِ، وَيُسَمَّى وَيُخَلَقُ رَأْسُهُ»

“Kila mtoto ni rehani kwa Akika yake, anachinjwiwa siku yake ya saba, na anapewa jina na ananyolewa”.

Hadithi hii ameipokea Ahmad na watu wa *Sunan*³, na ilipewa daraja la sahihi na At-Tirmidh. Inapasa tutaje kuwa katika mapokezi mengine ya Hadithi hii kuna maneno, *“Na damu inatolewa kwa niaba yake.”* Ambayo ni maarufu na iliyohifadhiwa zaidi kuliko mapokezi yaliyotangulia, na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Kauli ya Allah تعالى kuwa mamake Maryam alisema,

«وَأِنِّي أُعِيذُهَا بِكَ وَوَدَّعْتَهَا مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿١٠١﴾»

“Nami namkinga Kwako, yeye na uzao wake, Uwalinde na Shetani aliyelaaniwa”.

Maana yake: Nimeomba kimbilio kwa Allah تعالى kutokana na uovu wa shetani. Pia nimemuomba hilo mwanaye, yaani, Isa عليه السلام. Allah تعالى Aliipokea dua

¹ Fa'thul Al-Bari 3:306, Muslim 4:1807.

² Fat'hul Al-Bari 9:501.

³ Ahmad 5:7, Abu Dawud 3:259, Tuhfatul Al-Ahwadhi 5:115, An-Nasai 7:166, Ibn Majah 2:105.

yake. Kama alivyonukuu Abdur-Razzaq kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kuwa alisema, kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا مِنْ مَوْلُودٍ يُوَلَّدُ إِلَّا مَسَّهُ الشَّيْطَانُ جِئِن يُولَدُ، فَيَسْتَهْلِكُ صَارِحًا مِنْ مَسِّهِ إِيَّاهُ، إِلَّا مَرْيَمَ وَابْنَهَا»

“Hakuna mtoto anayezaliwa isipokuwa shetani anamgusa wakati anapozaliwa, kwa hiyo analia kwa kelele kutokana na kumgusa kwake yeye - isipokuwa Maryamu na mtoto wake (hawakuguswa)”.

Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, someni mkitaka:

وَأِنِّي أُعِيدُهَا بِكَ وَذُرِّيَّتَهَا مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ ﴿٣٧﴾

“Nami namkinga Kwako, yeye na uzao wake, Uwalinde na Shetani aliyelaaniwa”.¹

Sahihi Mbili ziliinukuu Hadithi hii.²

فَتَقَبَّلَهَا رَبُّهَا بِقَبُولٍ حَسَنٍ وَأَنْبَتَهَا نَبَاتًا حَسَنًا وَكَفَّلَهَا زَكَرِيَّا كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا زَكَرِيَّا الْمِحْرَابَ وَجَدَ عِنْدَهَا رِزْقًا قَالَ يَنْمَرُمُ أَيُّ لَكَ هَذَا هَذَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٧﴾

37. “Tena Mola wake Mlezi Akampokea kwa mapokeo mema na Akamkuza makuzo mema, na Akamfanya Zakariya awe mlezi wake. Kila mara Zakariya alipoingia chumbani kwake alimkuta na vyakula. Basi alimuuliza: Ewe Maryamu! Unavipata wapi hivi? Naye akamjibu: Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu Humruzuku Amtakaye bila ya hisabu”.

¹ Abdur-Razzaq 1:119.

² Fat’hul Al-Bari 8:60, Muslim 4:1838.

Makuzi ya Maryam; Heshima Yake kwa Allah تعالى:

Allah تعالى Anaeleza kuwa Alikubali nadhiri ya mama yake Maryam,

وَأُنَبِّتَهَا نَبَاتًا حَسَنًا

“Akamkuza makuzo mema.”

Maana yake: Aliifanya tabia yake kuwa nzuri, mwenendo wake wa kupendeza na Akamsahalishia kupendwa na watu. Alimfanya afuatane na watu wema hivyo alijifunza uadilifu, elimu na Dini.

وَكَفَّلَهَا زَكَرِيَّا

“Na Akamfanya Zakariya awe mlezi wake.”

Maana yake: Allah تعالى Alimfanya Zakaria عليه السلام awe mlezi wake. Allah تعالى Alimfanya Zakaria عليه السلام kuwa mlezi wa Maryam kwa manufaa yake, ili ajifunze kutokana na elimu yake na tabia yake ya uadilifu.

Na ni kwa sababu alikuwa mume wa mama yake mkubwa, kama alivyoarifu Ibn Is-haq رحمه الله تعالى, Ibn Jarir رحمه الله تعالى na wengineo.

Na wapo waliosema alikuwa shemeji yake, kama ilivyotajwa ndani ya Sahihi,

«فَإِذَا يَبْتَغِي وَيُعِيسِي، وَهُمَا ابْنَا الْخَالَةِ»

“Nikamuona Yahya na Isa na hao ni watoto wa khalati mama mdogo.”¹

Tunataja hapa kwa ujumla kuwa aliyoyasema Is-haq رحمه الله تعالى yanakubalika, na katika hali hii, Maryam alikuwa chini ya uangalizi wa mama yake mkubwa.

Sahih Mbili zilinukuu kuwa Mtume ﷺ aliamua Umaarah bint Hamzah, alelewe na dada wa mama yake, mke wa Jaafar bin Abu Talib رضي الله عنها, akisema,

«الْخَالَةُ بِمَنْزِلَةِ الْأُمِّ»

“Khalati - Mama mdogo au mkubwa - ni katika daraja la mama.”²

¹Fat'h Al-Bari 6:539.

²Fat'h Al-Bari 7:571.

Kisha Allah تعالى Anaelezea heshima ya Maryam na utukufu wa mahali alipo-kuwa akifanya ibada zake. Akasema:

كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا زَكَرِيَّا الْمِحْرَابَ وَجَدَ عِنْدَهَا رِزْقًا ط

“Kila mara Zakariya alipoingia chumbani kwake alimkuta na vyakula.”

Mujahidi, Ikrimah, Said bin Jubayr, Abu Ash-Shatha, Ibrahim An-Nakhai, Adh-Dhahak, Qatadah, Ar-Rabi bin Anas, Atiyyah Al-Awfi na As-Suddi walisema, “Yaani aliyakuta kwake matunda ya msimu wa kiangazi wakati wa majira ya kusi, na kinyume chake.”¹

Zakariyya عليه السلام alipo-yaona haya, alisema,

قَالَ يَمْرُؤُا أَنَّى لَكَ هَذَا ط

“Basi alimuuliza: Ewe Maryamu! Unavipata wapi hivi?”

قَالَتْ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ ط إِنَّ اللَّهَ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٢٠٦﴾

“Naye alimjibu: Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu Humruzuku Amtakaye bila ya hisabu”.

* * *

¹ Ibn Abu Hatim 2:227-229.

هُنَالِكَ دَعَا زَكَرِيَّا رَبَّهُ ۖ قَالَ رَبِّ هَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ
 ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً ۗ إِنَّكَ سَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٣٨﴾ فَنَادَتْهُ الْمَلْأِكَةُ
 وَهُوَ قَائِمٌ يُصَلِّي فِي الْمِحْرَابِ أَنَّ اللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِيحْيَى
 مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ مِنَ اللَّهِ وَسَيِّدًا وَحَصُورًا وَنَبِيًّا مِنَ
 الصَّالِحِينَ ﴿٣٩﴾ قَالَ رَبِّ أَنَّى يَكُونُ لِي غُلَامٌ وَقَدْ بَلَغَنِي
 الْكِبَرُ وَامْرَأَتِي عَاقِرٌ ۗ قَالَ كَذَلِكَ اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ
 ﴿٤٠﴾ قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِي آيَةً ۗ قَالَ ءآيَتُكَ إِلَّا تُكَلِّمَ
 النَّاسَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ إِلَّا زَمْرًا ۗ وَأَذْكُرُ رَبِّكَ كَثِيرًا وَسَبِّحَ
 بِالْعَشِيِّ وَالْإِبْكَرِ ﴿٤١﴾ وَإِذْ قَالَتِ الْمَلْأِكَةُ يَمْرُؤُكُمْ إِنَّ
 اللَّهَ اصْطَفَاكِ وَطَهَّرَكِ وَأَصْطَفَاكِ عَلَى نِسَاءِ الْعَالَمِينَ
 ﴿٤٢﴾ يَمْرُؤُكُمْ أَفْتَى لِرَبِّكِ وَأَسْجُدِي وَأَرْكَبِي مَعَ
 الرَّاكِعِينَ ﴿٤٣﴾ ذَلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ ۗ
 وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يَقُولُونَ أَقْلَمَهُمْ أَيُّهُمْ يَكْفُلُ مَرْيَمَ
 وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يَخْتَصِمُونَ ﴿٤٤﴾

هُنَالِكَ دَعَا زَكَرِيَّا رَبَّهُ ۖ قَالَ رَبِّ هَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ
 ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً ۗ إِنَّكَ سَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٣٨﴾ فَنَادَتْهُ
 الْمَلْأِكَةُ وَهُوَ قَائِمٌ يُصَلِّي فِي
 الْمِحْرَابِ أَنَّ اللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِيحْيَى
 مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ مِنَ اللَّهِ وَسَيِّدًا
 وَحَصُورًا وَنَبِيًّا مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٣٩﴾
 قَالَ رَبِّ أَنَّى يَكُونُ لِي غُلَامٌ وَقَدْ
 بَلَغَنِي الْكِبَرُ وَامْرَأَتِي عَاقِرٌ ۗ قَالَ
 كَذَلِكَ اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ﴿٤٠﴾
 قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِي آيَةً ۗ قَالَ ءآيَتُكَ
 إِلَّا تُكَلِّمَ النَّاسَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ إِلَّا
 زَمْرًا ۗ وَأَذْكُرُ رَبِّكَ كَثِيرًا وَسَبِّحَ
 بِالْعَشِيِّ وَالْإِبْكَرِ ﴿٤١﴾

38. Pale pale Zakariya akamuomba Mola wake Mlezi, akasema: Mola wangu Mlezi! Nipe kutoka Kwako kizazi chema. Wewe Ndiye Unayesikia maombi.

39. Alipokuwa kasimama chumbani akisali, Malaika akamnadia: Hakika Mwenyezi Mungu Anakubashiria Yahya, atayekuwa mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu, na ni bwana na mt'awa na Nabii kwa watu wema.

40. Akasema Zakariya: Mola wangu Mlezi! Vipi nitapata mwana na hali ukongwe umenifikia, na mke wangu ni tasa? Akasema: Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu Hufanya Apendavyo.

41. Akasema: Mola wangu Mlezi! Niwekee alama. Akasema: Alama yako ni kuwa hutasema na watu kwa siku tatu, isipokuwa kwa kuashiria tu. Na mdhukuru Mola Mlezi wako kwa wingi na mtakase jioni na asubuhi.

Dua ya Zakariyyah عليه السلام, na Kubashiriwa Kwake Kuzaliwa Yahya عليه السلام:

Zakariyyah عليه السلام alipoona Allah تعالى Anampa riziki Maryam kwa kumpa matunda ya wakati wa baridi wakati wa joto na matunda ya wakati wa joto wakati wa baridi, alipata hamu ya kupata mtoto wake mwenyewe, wakati huo Zakariyyah عليه السلام alikuwa Mzee, mifupa yake ikiwa imedhoofika na kichwa chake kikiwa kinang'aa mvi. Mkewe alikuwa ajuza aliyekoma kuzaa. Bado alimuomba Allah تعالى kwa siri,

رَبِّ هَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ

“Mola wangu Mlezi! Nipe kutoka Kwako.”

Maana yake: Kutoka katika Rehema Zako,

ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً

“Uzao mwema.” Maana yake: Mtoto muadilifu.

إِنَّكَ سَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٣٨﴾

“Wewe Ndiye Unayesikia maombi.”

Allah تعالى Akasema,

فَنَادَتْهُ الْمَلَائِكَةُ وَهُوَ قَائِمٌ يُصَلِّي فِي الْمِحْرَابِ

“Alipokuwa kasimama chumbani akisali, Malaika akamnadia.”

Maana yake: Malaika walisema naye moja kwa moja, alipojitenga, akisimama kwenye Sala mahali pa ibada. Kisha Allah تعالى Anaeleza habari njema ambazo Malaika walimpa Zakariyyah عليه السلام,

أَنَّ اللَّهَ يُبْشِّرُكَ بِبَحْيٍ

“Hakika Mwenyezi Mungu Anakubashiria Yahya.”

Mtoto katika kizazi chako, jina lake ni Yahya. Qatadah na wanazuoni wengine walisema, aliitwa Yahya (Maana anaishi) kwa sababu Allah تعالى Alimuhuisha kwa kumjaza Imani.¹ Kisha Allah تعالى Amesema,

مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ مِّنَ اللَّهِ

“Atayekuwa mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu.”

Al-Awfi alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, na pia Hasan, Qatadah, Ikrimah, Mujahid, Abu Ash-Shatha, As-Suddi, Ar-Rabi bin Anas, Adh-Dhahak, na wengine wengi wameizungumzia Aya hii,

مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ مِّنَ اللَّهِ

“Ataye kuwa mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Isa bin Maryam عليه السلام.² Abu Al-Aliyah, Ar-Rabi bin Anas, Qatadah na Said bin Jubayr na wengineo walisema kuwa Kauli ya Allah تعالى,

وَسَيِّدًا

“Na ni bwana”.

Maana yake: Mtu mwenye busara.¹ Ibn Abbas, Ath-Thawri na Adh-Dhahak رضي الله عنهم walisema kuwa *Sayyidan* ina maana, “Muadilifu, mwenye busara na mchamungu.”² Said bin Al-Musayyib alisema kuwa ‘*Sayyid* ni mwanazuoni na *Faqih*.’ Atiyyah alisema kuwa ‘*Sayyid* ni mtu mwenye tabia ya uadilifu na uchamungu.’ Ikrimah alisema kuwa inamuhusu mtu ambaye anazishinda hasira zake, ambapo Ibn Zayd alisema kuwa inamhusu mtu muadilifu. Mujahid alisema kuwa *Sayyidan* ina maana ‘aliyetukuzwa na Allah تعالى.’ Kauli ya Allah تعالى,

¹ Ibn Abu Hatim 2:235.

² Ibn Abu Hatim 2:235-237.

وَحَصُورًا

“Na mtawa”.

Haina maana ya kujizuia kuwa na mahusiano ya kimwili na wanawake, lakini ana kinga dhidi ya maovu na mambo machafu. Hilo halimzuii kuwaoa wanawake wa halali na kuwaingilia kisheria na kuzaa nao. Kwani Zakariyyah عليه السلام alisema katika dua yake kumuomba Yahya عليه السلام,

هَبِّ لِي مِنْ لَدُنْكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً

“Nipe kutoka kwako uzao mwema.”

Maana yake: Nijaalie mtoto ambaye atakuwa na watoto, na Allah تعالى Anajua zaidi. Kauli ya Allah تعالى,

وَنَبِيًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٣٨﴾

“Na Nabii kwa watu wema.”

Hii ni bishara ya pili kuhusu Yahya عليه السلام kupewa Utume baada ya habari njema ya kwanza kuwa atazaliwa. Habari hizi zilikuwa nzuri zaidi kuliko habari ya kuzaliwa Yahya عليه السلام. Ni kama Kauli sawa na hiyo, Allah تعالى Alimuambia mama yake Musa عليه السلام,

إِنَّا رَأَدُّوهُ إِلَيْكَ وَجَاعِلُوهُ مِنَ الْمُرْسَلِينَ ﴿٧﴾

“Hakika Sisi Tutamrudisha kwako na Tutamfanya miongoni mwa Mitume.” (28:7)

Zakariyyah عليه السلام aliposikia habari njema, akaanza kujihoji vipi atakuwa na watoto katika umri wake. Alianza kushangaa ikiwa atapata mtoto ilhali amefikia umri wa uzeeni.

قَالَ رَبِّ أَنَّى يَكُونُ لِي غُلَامٌ وَقَدْ بَلَغَنِيَ الْكِبَرُ وَامْرَأَتِي عَاقِرٌ قَالَ

“Akasema Zakariya: Mola wangu Mlezi! Vipini nitapata mwana na hali ukongwe umenifikia, na mke wangu ni tasa? Akasema...”

¹ Ibn Abu Hatim 2:238.

² At-Tabari 6:375, 376.

Maana yake: Malaika alisema,

قَالَ كَذَلِكَ اللَّهُ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ﴿٤٤﴾

“Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu Hufanya Apendavyo.”

Maana yake: Hili ni suala la Allah تعالى. Yeye ni Mwenye Nguvu hapana kinachoepa Nguvu Zake, wala hapana kinachokiuka Uwezo Wake.

قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِي آيَةً ۖ قَالَ آيَاتُكَ الْأُولَىٰ تُكَلِّمُ النَّاسَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ إِلَّا رَمَزًا

“Akasema: Mola wangu Mlezi! Niwekee alama. Akasema: Alama yako ni kuwa hutasema na watu kwa siku tatu, isipo kuwa kwa kuashiria tu.”

Maana yake: Nipe ishara itakayonitambulisha kuhusu kupatikana kwa mtoto. Maana yake: Hutasema ila kwa ishara japokuwa wewe si bubu. Katika Ayah nyingine, Allah تعالى Amesema,

قَالَ آيَاتُكَ الْأُولَىٰ تُكَلِّمُ النَّاسَ ثَلَاثَ لَيَالٍ سَوِيًّا ﴿٤٥﴾

“Alama yako ni kuwa hutasema na watu kwa masiku matatu.” (19:10)

Kisha Allah تعالى Alimuamuru Zakariyyah عليه السلام azidishe kumuomba Dua, na amshukuru na kumtukuza kila mara akiwa katika hali ile. Allah تعالى Akasema,

وَأَذْكُرُ رَبِّكَ كَثِيرًا وَسَبِّحَ بِالْعَمِيِّ وَالْإِبْكَرِ ﴿٤٦﴾

“Na mdhukuru Mola Mlezi wako kwa wingi na Mtakase jioni na asubuhi”.

Tutafafanua zaidi mada hii mwanzo wa Surah Maryam (sura ya 19). Allah تعالى Akipenda.

وَإِذْ قَالَتِ الْمَلَائِكَةُ يَا مَرْيَمُ إِنَّ اللَّهَ اصْطَفَاكِ وَطَهَّرَكِ وَأَصْطَفَاكِ عَلَىٰ نِسَاءِ

الْعَالَمِينَ ﴿١٩﴾ يَا مَرْيَمُ اقْنُتِي لِرَبِّكِ وَأَسْجُدِي وَأَرْكَبِي مَعَ الرَّاكِعِينَ ﴿٢٠﴾ ذَلِكَ مِنْ

أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ ۖ وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يَقُولُ أَفْلَمَهْمُ أَيُّهُمْ يَكْفُلُ مَرْيَمَ وَمَا

كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يَخْتَصِمُونَ ﴿٢١﴾

42. Na angalia pale Malaika waliposema: Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu Amekuchague, na Akakutakasa, na Akakutukuza kuliko wanawake wote.

43. Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola Mlezi wako na usujudu na uiname pamoja na wainamao.

44. Hizi ni khabari za ghaibu Tunazokufunulia; nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa kalamu zao ndani ya maji nani wao atamlea Maryamu, na hukuwa nao walipokuwa wakishindana.

Utukufu wa Maryam Juu ya Wanawake wa Zama Zake:

Allah تعالی Ameeleza kuwa Malaika walizungumza na Maryam kwa Amri Yake na Akamueleza ya kuwa Alimchagua ili aweze kumtumikia Yeye, kwa sababu ya kukithirisha ibada Kwake, kuipa mgongo dunia, utukufu na kutwaharika kwake dhidi ya machafu na wasiwasi. Pia Allah تعالی Alimchagua kwa utukufu wake kwa wanawake wa ulimwengu. Hisham bin Urwah ameeleza kwamba Ali bin Abi Talib رضي الله عنه alisema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

أَخَيْرُ نِسَائِهَا مَرْيَمُ بِنْتُ عِمْرَانَ، وَخَيْرُ نِسَائِهَا خَدِيجَةُ بِنْتُ خُوَيْلِدٍ

"Mbora wa wanawake wa ulimwengu ni Mariamu binti Imraan, na mbora wa wanawake wa ulimwengu ni Khadijah binti Khuwaylid".¹

Ibn Jariri رحمه الله تعالی amemnuuu Abu Musa Al-Ash'ari رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

كَمَلَّ مِنَ الرِّجَالِ كَثِيرًا، وَلَمْ يَكْمَلْ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَرْيَمُ بِنْتُ عِمْرَانَ وَآسِيَةُ امْرَأَةِ فِرْعَوْنَ

"Wamekamilika wanaume wengi, na hawakukamilika katika wanawake, isipokuwa Mariamu binti Imraan na Asia mke wa Firauni".²

Hadithi hii imepokewa na Vitabu sita isipokuwa Abu Daud.³ Bukhari aliiandika kama ifuatavyo,

¹ Tuhfaat Al-Ahwadhi 10:388.

² At-Tabari 6:397.

³ Fat'h Al-Bari 6:543, Muslim 4:1886, Tuhfaat Al-Ahwadhi 5:563.

Nimezitaja isnadi tofauti za mapokezi na matamko ya Hadithi hii katika kisa cha Isa mwana wa Maryam katika kitabu *Al-Bidayah wan- Nihayah*, shukrani zote Anastahiki Allah تعالی.

Allah تعالی Anaeleza kuwa Malaika walimuamuru Maryam aongeze vitendo vya ibada, unyenyekevu, kujisalimisha, kusujudu na kadhalika, ili apate kile alichandikiwa na Allah تعالی, kama mtihani kwake. Bado mtihani huu ulimpatia daraja la juu hapa duniani na Akhera, kwani Allah تعالی Alionesha Nguvu Zake kwa Kumuumba mtoto asiye na baba.

Allah تعالی Amesema,

بِسْمِ رَبِّكَ أَقْبَتِي وَاسْجُدِي وَأَرْكَبِي مَعَ الرَّاكِبِينَ ﴿٤٣﴾

“Ewe Maryamu! Mnyenyekee Mola Mlezi wako na usujudu na uiname pamoja na wainamao”. (3:43)

Ama kwa *Qunut* (katika Aya) ina maana kujisalimisha kwa unyenyekevu. Kama Allah تعالی Alivyosema katika Aya nyingine,

بَل لَّهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ كُلُّ لَّهُ قَانُونَ ﴿١١٦﴾

“Bali vyote viliomo mbinguni na duniani ni Vyake. Vyote vinamtii Yeye.” (2:116)

Baada ya hapo Allah تعالی Alimuambia Mjumbe Wake ﷺ baada ya kutaja kisa cha Maryam,

ذَٰلِكَ مِنْ أَنْبَاءِ الْغَيْبِ نُوحِيهِ إِلَيْكَ

“Hizi ni khabari za ghaibu Tunazokufunulia”.

Maana yake: Tunakusimulia wewe (Ewe Muhammad ﷺ),

وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ يُلقُونَ أَقْلَمَهُمْ أَيُّهُمْ يَكْفُلُ مَرْيَمَ وَمَا كُنْتَ لَدَيْهِمْ إِذْ

يَخْتَصِمُونَ ﴿١٢٨﴾

“Nawe hukuwa nao walipokuwa wakitupa kalamu zao nani wao atamlea Maryamu, na hukuwa nao walipokuwa wakishindana.”

Maana yake: “Hukuwa pamoja nao wakati huo, Ewe Muhammad ﷺ, hivyo huwezi kuwasimulia watu yaliyotokea kama uliyeshuhudia kwa macho yako. Bali Allah تعالی Amekufungulia ukweli huo ukawa kama ulikuwepo, walipiga kura kumchagua mwangalizi wa Maryam, alitarajia malipo kwa amali hii njema.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ikrimah alisema, “Mama yake Maryam aliondoka na Maryam huku amemfunika nguo ya mtoto mchanga, na akampeleka kwa makuhani waliotokana na kizazi cha Harun عليه السلام, kaka yake Musa عليه السلام. Na wao katika zama hizo walikuwa ndio waangalizi wa msikiti wa *Bayt Al-Maqdis*, kama ilivyo kwa waangalizi wa Al-Ka`aba. Mama yake Maryam akawaambia, “Mchukueni mtoto huyu ambaye niliweka nadhiri (kuwa atahudumia Msikiti), Nimemuachia huru. Kwa kuwa ni binti yangu, na sitoingia Msikitini kwa sababu niko kwenye hedhi, na sitorejea naye nyumbani!” Wakasema, “Huyu ni binti wa Imamu wetu (kwa kuwa Imran alikuwa akiongoza Swalah) anayesimamia wanyama wetu wa dhabihu.” Zakariyyah عليه السلام akasema, “Nipeni miye kwani dada wa mama yake ni mke wangu wakamuambia, “Nyoyo zetu haziwezi kuridhia umchukue, kwani huyu ni binti wa Imamu wetu.” Hivyo wakapiga kura kwa kalamu walizokuwa wakiandikia Taurati, na kura ikamuangukia Zakariyyah عليه السلام na akamchukua Maryam kumlea.”¹ Ikrimah,² As-Suddi, Qatadah, Ar-Rabi bin Anas na wengine¹ walisema, makuhani walikwenda mto Jordan kupiga kura kwa kutupa mtoni kalamu zao, maji yalizisomba zote isipokuwa ya Zakariyyah عليه السلام. Ambaye alikuwa bwana wao, kiongozi wao, mwanazuoni wao, Imamu na Mtume wao, Rehema na Amani za Allah تعالی zimshukie yeye na Mitume wengine.



¹ At-Tabari 6:351.

² Ibn Abu Hatim 2:266.

³ Ibn Abu Hatim 2:267, 268.

إِذْ قَالَتِ الْمَلٰٓئِكَةُ يَمْرُؤُا۟ إِنَّ اللّٰهَ يُبَشِّرُكَ بِكَلِمَةٍ مِّنْهُ اسْمُهُ
 الْمَسِيحُ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ وَجِيهًا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمِنَ
 الْمُقَرَّبِينَ ﴿٤٥﴾ وَيُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا وَمِنَ
 الصّٰلِحِيْنَ ﴿٤٦﴾ قَالَتْ رَبِّ اَنۢى يُكُوْنُ لِيْ وَلَدٌ وَلَمْ
 يَمَسِّنِي۟ بَشَرًا۟ قَالَ كَذٰلِكَ اَللّٰهُ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُۗ اِذَا قَضٰى
 اَمْرًا۟ فَاِنۡمَآ يَقُوْلُ لَهُ كُنْ فَيَكُوْنُ ﴿٤٧﴾ وَيُعَلِّمُهُ الْكِتٰبَ
 وَالْحِكْمَةَ وَالتَّوْرَةَ وَالانۢجِيْلَ ﴿٤٨﴾ وَرَسُوْلًا۟ اِلَىٰ بَنِي
 إِسْرٰٓءِيْلَ اَنۢى قَدْ جَعَلْتُكُمْ بَيٰٓةٍ مِّنۡ رَّبِّكُمْۗ اَنۢى اَخْلُقُ
 لَكُمْ مِّنۡ مَّرۡبٍ الطَّيۡنِ كَهَيۡةِ الطَّيْرِ فَاَنفُخُ فِيْهِ فَيَكُوْنُ طَيْرًا
 يٰۤاِذۡنِ اللّٰهِؕ وَاُبۡرِءُ الْاَكۡمَةِ وَالْاَبۡرَصِؕ وَاُحِي الۡمَوْتٰى
 يٰۤاِذۡنِ اللّٰهِؕ وَاُنۡبِئُكُمْ بِمَا تَاْكُلُوْنَ وَمَا تَدۡخُرُوْنَ فِي۟ بُيُوْتِكُمْؕ
 اِنَّ فِي۟ ذٰلِكَ لَآيَةً لِّكُمۡ اِنۡ كُنۡتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ﴿٤٩﴾ وَمُصَدِّقًا
 لِّمَا بَيَّنَّ يَدٰى رَبِّ التَّوْرَةِ وَاِلۡجَلٍّ لِّكُمۡ بَعْضَ
 الَّذِى حُرِّمَ عَلَيۡكُمْؕ وَجَعَلْتُكُمْ بَيٰٓةٍ مِّنۡ رَّبِّكُمْۗ فَاتَّقُوا
 اللّٰهَ وَاَطِيعُوْنَ ﴿٥٠﴾ اِنَّ اللّٰهَ رَءِى۟ وَرَبُّكُمْۗ فَاَعۡبُدُوْهُ هٰذَا
 صِرَاطٌ مُّسْتَقِيْمٌ ﴿٥١﴾

إِذْ قَالَتِ الْمَلٰٓئِكَةُ يَمْرُؤُا۟ إِنَّ اللّٰهَ
 يُبَشِّرُكَ بِكَلِمَةٍ مِّنْهُ اسْمُهُ الْمَسِيحُ
 عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ وَجِيهًا فِي الدُّنْيَا
 وَالْآخِرَةِ وَمِنَ الْمُقَرَّبِينَ ﴿٤٥﴾
 وَيُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا
 وَمِنَ الصّٰلِحِيْنَ ﴿٤٦﴾ قَالَتْ رَبِّ
 اَنۢى يُكُوْنُ لِيْ وَلَدٌ وَلَمْ يَمَسِّنِي۟ بَشَرًا۟
 قَالَ كَذٰلِكَ اَللّٰهُ يَخْلُقُ مَا يَشَآءُؕ
 اِذَا قَضٰى اَمْرًا۟ فَاِنۡمَآ يَقُوْلُ لَهُ كُنْ
 فَيَكُوْنُ ﴿٤٧﴾

**45. Na pale Malaika wali-
 posema: Ewe Maryamu!
 Hakika Mwenyezi Mungu
 Anakubashiria (mwana) kwa
 neno litokalo Kwake. Jina
 lake ni Masihi Isa mwana wa
 Maryamu, mwenye hishima
 katika dunia na Akhera, na
 miongoni mwa waliowekwa
 karibu (kwa Mwenyezi
 Mungu).**

**46. Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utu uzima wake,
 na atakuwa katika watu wema.**

**47. Maryamu akasema: Mola wangu Mlezi! Vipi nitampata mwana na hali
 hajanigusa mwanaadamu? Mwenyezi Mungu Akasema: Ndivyo vivyo hivyo,
 Mwenyezi Mungu Huumba Apendacho. Anapo hukumu jambo, Huliambia:
 Kuwa! Likawa.**

Maryam Anapokea Bishara ya Kuzaliwa Isa عليه السلام

Ayah hii ina bishara aliyoletewa Maryam na Malaika, ya kuzaa mtoto wa kiume mwenye uwezo ambaye baadaye atafanya mambo makubwa.

Allah تعالى Amesema,

إِذْ قَالَتِ الْمَلَأِيكَةُ يَمْرَمُ إِنَّ اللَّهَ يُبَشِّرُكِ بِكَلِمَةٍ مِّنْهُ

“Na pale Malaika waliposema: Ewe Maryamu! Hakika Mwenyezi Mungu Anakubashiria (mwana) kwa neno litokalo Kwake” (4:45)

Mtoto atazaliwa kwa Neno kutoka kwa Allah تعالى, maana kwa Kusema, ‘kuwa’, na akawa. Hii ndio maana ya Kauli ya Allah تعالى (kumhusu Yahya عليه السلام)

مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ مِّنَ اللَّهِ

“Atayekuwa mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Mwenyezi Mungu”.

Kama walivyodhukuru Jamhuri ya wanazuoni

أَسْمُهُ الْمَسِيحُ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ

“Jina lake ni Masihi Isa mwana wa Maryamu.”

Ni kuwa atajulikana kwa jina hili hapa duniani, hususan na waumini. Isa عليه السلام aliitwa “Al-Masih” (Masihi) kwa sababu alipowagusa (Mas`h) waliokuwa na ugonjwa, walipona kwa Uweza wa Allah تعالى. Kauli ya Allah تعالى,

عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ

“Isa mwana wa Maryamu.”

Nasabu yake Isa عليه السلام inafuata kwa mama yake, kwa sababu hakuwa na baba.

وَجِيهًا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمِنَ الْمُقَرَّبِينَ

“Mwenye hishima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa waliowekwa karibu (kwa Mwenyezi Mungu)”.

Maana yake: Atakuwa kiongozi aliyetukuzwa na Allah تعالى katika maisha ya dunia, kwa sababu ya sharia atakayofunuliwa na Allah, kuteremshiwa Kitabu pamoja na neema nyingine Atakazomruzuku Allah تعالى. Isa عليه السلام atatukuzwa

siku ya Kiyama na atawaombea watu kwa Allah تعالى, kwa Idhini Yake, kama ilivyo kwa ndugu zake Mitume watano wa Allah تعالى waliopata taabu na misukosuko mikubwa “Ulul Azm”, Rehema na Amani ziwafikie wote.

Isa عليه السلام Alizungumza katika Rika la Utoto

وَيُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا

“Naye atazungumza na watu katika utoto wake na katika utu uzima wake”.

Maana yake: Atawalingania watu wake kumuabudu Allah تعالى Pekee bila mshirika akiwa bado kwenye susu, huu utakuwa ni muujiza kutoka kwa Allah تعالى na atakapokuwa mtu mzima, atapata wahyi kutoka kwa Allah تعالى.

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى amesema, Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema Mtume ﷺ amesema:

«مَا تَكَلَّمَ مَوْلُودٌ فِي صَعْرِهِ إِلَّا عَيْسَىٰ وَصَاحِبُ جُرَيْجٍ»

“Hajazungumza mtoto katika udogo wake, isipokuwa Isa na swahiba wa Jurajj.”¹

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَمْ يَتَكَلَّمْ فِي الْمَهْدِ إِلَّا ثَلَاثَةٌ: عَيْسَىٰ، وَصَبِيٌّ كَانَ فِي زَمَنِ جُرَيْجٍ، وَصَبِيٌّ آخَرٌ»

“Hawakuongea katika utoto isipokuwa watatu, ‘Isa, na kichanga kilichokuwepo wakati wa Jurajj, na mtoto mwingine”.²

وَمِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٤٦﴾

“...na atakuwa katika watu wema.”

Katika kauli na matendo yake, kwani atakuwa na ilimu safi na amali adilifu.

¹ Ibn Abu Hatim 2:272-273 Isnadi yake ina Mushkeli.

² Ibn Abu Hatim 2:272-22, Bukhari, 3436, Muslim, 2550.

Isa عليه السلام **Aliumbwa Bila Baba:**

Maryam aliposikia khabari njema za Allah تعالى Alizoletewa na Malaika, alisema:

رَبِّ أَنْيْ يَكُونُ لِي وَلَدٌ وَلَمْ يَمَسَّسْنِي بَشَرٌ

“Mola Wangu Mlezi! Vipi nitampata mwana na hali hajanigusa mwanaadamu?”

Maryam alisema, “Nitakuwaje na mtoto nami sijaolewa, wala sitarajii kuolewa wala miye si mwanamke mchafu, Allah تعالى apishie mbali?”

Malaika akampatia jibu la swali hili kutoka kwa Allah تعالى,

كَذَلِكَ اللَّهُ يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ

“Mwenyezi Mungu Akasema: Ndivyo vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu Huumba Apendacho”. (3:47)

Maana yake: Hivi ndivyo Alivyo Allah تعالى na Uwezo na Nguvu na Halimshindi jambo. Allah تعالى Ametumia neno, “*Yakhluq*”, ‘Huumba’, na Hakutumia neno ‘*Yaf’alu*’, ‘Hufanya’,” kama katika kisa cha Zakariyyah عليه السلام (3:40), ili kuondoa dhana potofu kumhusu Isa عليه السلام.

Allah تعالى Amesitizia ukweli huu Aliposema,

إِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٤٧﴾

“Anapo hukumu jambo, Huliambia: Kuwa! Likawa”.

Maana yake: Alitakalo Allah تعالى, huwa mara moja bila kukawia.

Katika Aya nyingine Allah تعالى Amesema,

وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَّمَجْ بِأَبْصَرٍ ﴿٥٠﴾

“Na Amri Yetu haikuwa ila ni moja tu, kama kupepesa jicho.” (54:50)

Maana yake: “Kwa hakika, Tunaamuru mara moja bila kusita, na haraka kwa wakati ule ule, hufanyika kwa wepesi zaidi kuliko kufumba jicho.”

وَيُعَلِّمُهُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَالْتَّوْرَةَ وَالْإِنْجِيلَ ﴿٤٥﴾ وَرَسُولًا إِلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَنِّي قَدْ
 جِئْتُكُمْ بِبَيِّنَاتٍ مِّن رَّبِّكُمْ ۖ أَنِّي أَخْلُقُ لَكُمْ مِنَ الطِّينِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ فَأَنْفُخُ فِيهِ فَيَكُونُ
 طَيْرًا بِإِذْنِ اللَّهِ ۖ وَأُبْرِئُ الْأَكْمَةَ وَالْأَبْرَصَ وَأُحْيِي الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِ اللَّهِ ۖ وَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا
 تَأْكُلُونَ وَمَا تَدَّخِرُونَ فِي بُيُوتِكُمْ ۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لِّكُمْ إِن كُنتُمْ مُّؤْمِنِينَ ﴿٤٦﴾
 وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيَّ مِنَ التَّوْرَةِ وَلَا حِلَّ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي حُرِّمَ عَلَيْكُمْ ۗ
 وَجِئْتُكُمْ بِبَيِّنَاتٍ مِّن رَّبِّكُمْ فَأَتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ۖ ﴿٤٧﴾ إِنَّ اللَّهَ نَزَّاهٌ وَأَعْبُدُوهُ
 هٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٤٨﴾

48. Na atamfunza kuandika na Hikima na Taurati na Injili.

49. Na ni Mtume kwa Wana wa Israili kuwaambia: Mimi nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu, ya kwamba nakuundieni kwa udongo kama sura ya ndege. Kisha nampuliza anakuwa ndege kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa na wakoma, na ninawafufua maiti kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu, na ninakuambieni mnachokila na mnachoweka akiba katika nyumba zenu. Hakika katika haya ipo Ishara kwenu ikiwi nyinyi ni wenye kuamini.

50. Na ninasadikisha yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati, na ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mlioharimishiwa, na nimekujieni na Ishara kutokana na Mola Mlezi wenu. Kwa hivyo mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini mimi.

51. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi na ni Mola wenu Mlezi. Basi muabudni Yeye. Hii ndiyo Njia Iliyo nyooka.

Sifa Bainifu za Isa عليه السلام na Miujiza Aliyoifanya

Allah تعالى Anaeleza kuhusu kutimia kwa biashara Alizomletea Maryam kumhusu Isa عليه السلام: Kwamba Allah تعالى Angemfundisha,

وَيُعَلِّمُهُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ

“Na Atamfunza kuandika na hikima”.

Inaelekea kuwa ‘Kitabu’ kilichotajwa hapa inakusudiwa kuandika. Tulieleza maana ya neno *Al-Hikmah* katika Tafsir ya *Surat Al-Baqarah*.

وَالْقُرْآنَ وَالْإِنجِيلَ

“Na Taurati na Injili.”

Taurati ni Kitabu ambacho Allah تعالى Alimteremshia Musa عليه السلام, mtoto wa Imran, ambapo Injili ni kile Kitabu Allah تعالى Alichomteremshia Isa عليه السلام, mwana wa Maryam, Kauli ya Allah تعالى,

وَرَسُولًا إِلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ

“Na ni Mtume kwa Wana wa Israili”.

Maana yake: Allah تعالى Atampeleka Isa عليه السلام kuwa Mtume kwa Wana wa Israil akiwaambia,

أَنِّي قَدْ جَعَلْتُكُمْ بَنِيَّ مِن رَّبِّكُمْ أَنِّي أَخْلَقْتُ لَكُمْ مِنَ الطِّينِ كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ فَأَنْفُخُ فِيهِ

فَيَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِ اللَّهِ

“Mimi nimekujieni na Ishara kutoka kwa Mola Mlezi wenu, ya kwamba nakuundieni kwa udongo kama sura ya ndege. Kisha nampuliza anakuwa ndege kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu”.

Hii ni miujiza iliyofanywa na Isa عليه السلام; alikuwa akifanya umbile la ndege kwa kutumia udongo mfinyanzi na akipulizia ndani yake, na akawa ndege kwa Idhini ya Allah تعالى.

Allah تعالى Alifanya miujiza kwa ajili ya Isa عليه السلام ili kuthibitisha ya kuwa Yeye Ndiye Alimtuma.

وَأُتِرْتُمْ الْأَكْمَةَ

“Na ninawaponesha vipofu wa tangu kuzaliwa.”

Maana yake: Mtu aliyezaliwa kipofu. Na maana hii inaongeza nguvu zaidi muujiza huu na kuipa uzito zaidi.

وَالْأَبْرَصَ

“Na wakoma.”

Ambao ni ugonjwa unaofahamika.

وَأُحْيِ الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِ اللَّهِ

“Na ninawafufua maiti kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu.”

Wanazuoni wengi wamesema kuwa Allah تعالى Alimpeleka kila Mtume na miujiza laiki ya zama zake. Kwa mfano, zama za Musa عليه السلام, uchawi ulikithiri na wachawi walikuwa na daraja ya juu. Hivyo Allah تعالى Alimpeleka Musa عليه السلام na miujiza ambayo iliyaduwa macho na kumshangaza kila mchawi. Wachawi walipotanabahi kuwa miujiza ya Musa عليه السلام ilitoka kwa Allah تعالى, Muweza na Mkuu kabisa, walisilimu na wakawa waumini wachamungu. Ama kuhusu Isa عليه السلام, alipelekwa katika zama za watabibu na wenye Elimu ya viumbe hai, akawajia wao na Ishara ambazo havezi kuzionesha mtu yeyote, isipokuwa yule aliyeandaliwa na Yule Aliyeziweka kanuni. Inawezekanaje tabibu kukipa uhai kisicho na uhai, au kuponya upofu, mbalanga na kuwafufua walio makaburini? Muhammad ﷺ naye alitumwa katika zama za watu wambuji na malenga. Aliwaletea Kitabu kutoka kwa Allah تعالى; endapo binadaamu na majini wakijaribu kuiga Sura kumi au hata moja, watahindwa kabisa kazi hiyo, hata kama watasaidiana kwa pamoja kulifanya hilo. Hili ni kwa sababu Qur'an ni maneno ya Allah تعالى na kamwe hayafanani na ya viumbe. Kauli Yake,

وَأُنَبِّئُكُمْ بِمَا تَأْكُلُونَ وَمَا تَدْخُرُونَ فِي بُيُوتِكُمْ

“Na ninakuambieni mnachokila na mnachoweka akiba katika nyumba zenu.”

Maana yake: Nakuambieni kuhusu kile alichokula mmoja wenu na alichokihifadhi nyumbani kwa matumizi ya kesho.

إِنَّ فِي ذَلِكَ

“Hakika katika haya.”

Maana yake: Katika miujiza yote hii.

لَايَةً لَّكُمْ

“Ipo ishara kwenu.”

Maana yake: Zinazosadikisha ukweli wa lile nililotumwa nalo kwenu.

إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿٤٥﴾

“ikiwi nyinyi ni wenye kuamini.”

وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ التَّوْرَةِ

“Na ninasadikisha yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati.”

Maana yake: Kuthibitisha yaliomo katika Taurati.

وَلَا جُلَّ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي حُرِّمَ عَلَيْكُمْ

“Na ili nikuhalalishieni baadhi ya yale mlioharimishiwa.”

Sehemu hii ya Aya inaonesha kuwa Isa عليه السلام alifuta baadhi ya sharia za Taurati na akawafahamisha Mayahudi ukweli kuhusu baadhi ya mambo waliyokhasimiana kwa makosa. Ni kama Alivyosema katika Aya nyingine,

قَدْ جِئْتُكُمْ بِالْحِكْمَةِ وَلِأُبَيِّنَ لَكُمْ بَعْضَ الَّذِي تَخْتَلِفُونَ فِيهِ

‘Nimekujieni na hikima, na ili nikuelezeni baadhi ya yale mliyo khitalifiana’.

Baadaye Isa عليه السلام alisema,

وَجِئْتُكُمْ بِبَيِّنَاتٍ مِّن رَّبِّكُمْ

“Na nimekujieni na Ishara kutokana na Mola Mlezi wenu”. Maana yake: “kwa hoja zenye uthibitisho na ushahidi juu ya ukweli wangu katika yale ninayowalingania.”

فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا ۖ إِنَّ اللَّهَ رَبُّكُمْ فَاعْبُدُوهُ

“Kwa hivyo mcheni Mwenyezi Mungu na nitiini mimi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu Mlezi na ni Mola wenu Mlezi. Basi muabuni Yeye.”

Ina maana kwamba: Mimi na nyie tuko sawa katika utumwa, kunyenyekea na kujisalimisha Kwake.

هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ۖ

“Hii ndiyo Njia Iliyo nyooka”

* * *

* فَلَمَّا أَحَسَّ عِيسَىٰ مِنْهُمُ الْكُفْرَ قَالَ مَنْ أَنْصَارِي إِلَىٰ
 اللَّهِ ۗ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ ءَامَنَّا بِاللَّهِ
 وَأَشْهَدُ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٥٢﴾ رَبَّنَا ءَامَنَّا بِمَا أَنْزَلْتَ
 وَاتَّبَعْنَا الرَّسُولَ فَاكْتُتِبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ ﴿٥٣﴾
 وَمَكَرُوا وَمَكَرَ اللَّهُ ۗ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٥٤﴾ إِذْ قَالَ
 اللَّهُ يَٰعِيسَىٰ ابْنِ مَرْيَمَ كُنْ فِي سَكِّينَا وَمَنْ يَتَّبِعْكَ
 مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا يَجْعَلُ اللَّهُ لَهُ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٥٥﴾ وَالَّذِينَ
 كَفَرُوا مِنْ أَهْلِ الْبَيْتِ وَالَّذِينَ تَحْتَ الْمَوْتِ حَتَّىٰ تَخْرُجَ
 مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِمْ يَوْمَ يُبْعَثُونَ ۗ أُولَٰئِكَ يَتْلُونَ آيَاتِ
 اللَّهِ وَمَنْ يَتْلِهَا فَلَهُ كُفْرًا وَسُكُوتًا ۗ وَالَّذِينَ
 كَفَرُوا لَهُمْ لُعَابٌ أَسْفَلَ سَافِلِينَ ﴿٥٦﴾ ذَٰلِكَ
 نَتْلُوهُ عَلَيْكَ مِنَ الْآيَاتِ وَالذِّكْرِ الْحَكِيمِ ﴿٥٧﴾

* فَلَمَّا أَحَسَّ عِيسَىٰ مِنْهُمُ الْكُفْرَ
 قَالَ مَنْ أَنْصَارِي إِلَىٰ اللَّهِ ۗ قَالَ
 الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ ءَامَنَّا
 بِاللَّهِ وَأَشْهَدُ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٥٢﴾
 رَبَّنَا ءَامَنَّا بِمَا أَنْزَلْتَ وَاتَّبَعْنَا
 الرَّسُولَ فَاكْتُتِبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ
 ﴿٥٣﴾ وَمَكَرُوا وَمَكَرَ اللَّهُ ۗ وَاللَّهُ
 خَيْرُ الْمَكْرِينَ ﴿٥٤﴾

52. Isa alipohisi kuwa kati
 yao pana ukafiri alisema:
 Nani wasaidizi wangu kwa
 Mwenyezi Mungu? Wana-
 funzi wake wakasema: Sisi
 ni wasaidizi wa Mwenyezi
 Mungu. Tumemuamini
 Mwenyezi Mungu, na
 shuhudia kwamba sisi
 hakika ni Waislamu.

53. Mola wetu Mlezi! Tumeyaamini Uliyoyateremsha, na tumemfuata
 Mtume, basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia.

54. Na Makafiri walipanga mipango na Mwenyezi Mungu Akapanga mipango,
 na Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa wenye kupanga.

Wafuasi Wanamuunga Mkono Isa عليه السلام:

Allah تعالى Amesema,

﴿ فَلَمَّا أَحْسَنَ عِيسَى ﴾

“Isa alipohisi (kuwa kati yao pana ukafiri) alisema.” Maana yake: Isa عليه السلام alipohisi kuwa wamebobeza katika ukafiri na kuendelea na upotofu aliwaambia,

﴿ مَنْ أَنْصَارِي إِلَى اللَّهِ ﴾

“Nani wasaidizi wangu kwa Mwenyezi Mungu?”. Mujahid alisema, ‘Maana yake, nani atanifuata kwa Allah?’¹ Hata hivyo inaelekea kuwa Isa عليه السلام alikuwa anauliza, ‘Nani atanisaidia kufikisha Ujumbe wa Allah?’.

Ni kama Mtume ﷺ alipokuwa akisema wakati wa misimu ya Hajj, kabla ya Hijrah,

﴿ مَنْ رَجُلٌ يُؤَيِّنِي حَتَّى أَبْلُغَ كَلَامَ رَبِّي؟ ، فَإِنَّ قُرَيْشًا قَدْ مَنَعُونِي أَنْ أَبْلُغَ كَلَامَ رَبِّي ﴾

“Ni nani atayenisaidia nifikishe Maneno ya Mola wangu, kwa hakika Makureshi wananizuia kufikisha Maneno ya Mola wangu”²

Mpaka alipowapata Ansar.³ Ansar wakamsaidia Mtume ﷺ na wakampa hifadhi. Baadaye aliamia kwao, walimliwaza Mtume ﷺ na wakamkinga dhidi ya maadui zake wote. Haya ni sawa na yaliyomtokea Isa عليه السلام, kwani baadhi ya Wana wa Israil walimuamini, wakampa msaada na kumuunga mkono na wakafuata nuru aliyokuja nayo. Kwa sababu hiyo Allah تعالى Alisema kuwahusu;

﴿ قَالِ الْخَوَارِثُوتُ نَحْنُ أَنْصَارُ اللَّهِ ءَامِنَّا بِاللَّهِ وَأَشْهَدُ بِأَنَا مُسْلِمُونَ ﴾ ﴿ ٥٧ ﴾ رَبَّنَا

﴿ ءَامِنَّا بِمَا أُنزِلَتْ وَاتَّبَعْنَا الرَّسُولَ فَاكْتُبْنَا مَعَ الشَّاهِدِينَ ﴾ ﴿ ٥٨ ﴾

“Wanafunzi wake wakasema: Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu. Tumemuamini Mwenyezi Mungu, na shuhudia kwamba sisi hakika ni Waislamu. Mola wetu Mlezi! Tumeyaamini Uliyoyateremsha, na tumemfuata Mtume, basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia. ”

¹ Ibn Abu Hatim 3:290.

² Ahmad 3:322.

Hawari kwa kiarabu - maana yake wasaidizi, na iliyo sahihi ni kwamba Al-Hawari ni msaidizi. Ni kama ilivyonyukuliwa katika Sahih Mbili kuwa wakati Mtume ﷺ alipowahamasisha watu kupigana wakati wa vita vya Al-Ahzab, Az-Zubayr رضي الله عنه alijitokeza, kisha Mtume ﷺ akawahamasisha wapiganaji kwa mara ya pili, Az-Zubayr رضي الله عنه akajitokeza tena. Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ لِكُلِّ نَبِيٍّ حَوَارِيًّا، وَحَوَارِيِّي الزُّبَيْرُ»

*"Kila Mtume ana hawari, (mfuasi) na hawari wangu ni Az-Zubayr."*¹

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akizungumzia aya hii:

فَأَكْتَبْنَا مَعَ الشَّهِيدِ

"...basi tuandike pamoja na wanaoshuhudia."

"Alisema: Miongoni mwa Ummah wa Muhammad ﷺ."² Hadithi hii ina isnadi nzuri ya upokezi.

Mayahudi Walipanga Njama za Kumuuu Isa عليه السلام:

Baada ya hapo, Allah تعالى Ameerleza kuwa Wana wa Israil walijaribu kumuua Isa عليه السلام kwa kufanya hila za kumchafulia jina na kumsulubu. Walimlalamikia kwa mfalme wa wakati huo ambaye alikuwa kafiri. Wakasema, "Huyu hapa mtu anayewapotosha watu, anawashawishi kutomtii mfalme, anafanya baba afarakane na mwanaye." Walimzushia uongo mwingine, ambao walikuwa nao shingoni mwao, ikiwa ni pamoja na kumkashifu kuwa alikuwa mwanaharamu. Mfalme akakasirika sana na hivyo akawatuma askari wamkamate, wamtese na wamsulubu, mpaka awe mfano kwa wengine kwa adhabu. Walipozingira nyumba yake na wakadhani kuwa watamkamata, Allah تعالى Alimuokoa kutoka kwao, Akamnyanyua kutoka nyumbani kwake na Kumpeleka mbinguni. Allah تعالى Akamshabihisha kwa mtu mwingine aliyekuwemo nyumbani kwake. Walipoingia, wakachukulia kwamba mtu yule ni Isa عليه السلام ilhali kulikuwa na kiza. Wakamkamata mtu huyo, wakamtesa na kumsulubu. Aidha waliweka miba juu ya kichwa chake. Hata hivyo Allah تعالى Aliwababaishia watu hao, kwani Alimuokoa na Akamnyanyua Mtume Wake ﷺ

¹ Fat'hul Al-Bari 6:63, Muslim 4:1870.

² Ibn Abu Hatim 2:294. Isnadi yake ni nzuri.

kutoka kwao, akiwaacha wakiwa wamepotea katika kiza cha kuchupa mipaka, wakidhani kuwa walifanikiwa kufikia lengo lao. Allah تعالى Aliifanya mioyo yao kuwa migumu, na kukengeuka kutoka kwenye ukweli, na akawadhalilisha, na watadumu katika hali hiyo mpaka Siku ya kufufuliwa.

Kwa sababu hii Allah تعالى Alisema,

﴿مَكَرُوا وَمَكَرَ اللَّهُ وَاللَّهُ خَيْرٌ الْمَاكِرِينَ﴾

“Na Makafiri walipanga mipango na Mwenyezi Mungu Akapanga mipango, na Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa wenye kupanga”.

إِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَىٰ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا وَجَاعِلُ الَّذِينَ اتَّبَعُوكَ فَوْقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۗ ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٥﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَأَعَذِبُهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿٥٦﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُوَفِّيهِمْ أُجُورَهُمْ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿٥٧﴾ ذَلِكَ نَتْلُوهُ عَلَيْكَ مِنَ الْآيَاتِ وَالذِّكْرِ

الْحَكِيمِ ﴿٥٨﴾

55. Pale Mwenyezi Mungu Alipo sema: Ewe Isa! Mimi Nitakutimizia muda wako wa kuishi (hawatakuua hao maadui), na Nitakunyanyua Kwangu, na Nitakutakasa na wale waliokufuru, na Nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa Kwangu, Nikuhukumuni katika yale mliyokuwa mkikhitalifiana.

56. Ama wale waliokufuru, Nitawaadhibu adhabu kali katika dunia na Akhera, wala hawatapata wa kuwanusuru.

57. Na ama wale walioamini na wakatenda mema basi Mwenyezi Mungu Atawalipa ujira wao kamili. Na Mwenyezi Mungu hawapendi madhalimu.

58. Haya Tunayokusomea ni katika Aya na Ukumbusho wenye hikima.

Maana ya Mutawaffiyka:

Kauli ya Allah تعالى،

إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ

“Mimi (mutawaffiyka) Nitakutimizia muda wako wa kuishi (hawatakuua hao maadui) na Nitakunyanyua Kwangu...”

Maana ya neno ‘Mutawaffiyka’ - kufisha - Katika Aya hii ni kulala.

Ni kama Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine،

وَهُوَ الَّذِي يَتَوَفَّاكُم بِاللَّيْلِ

“Naye Ndiye Anayekufisheni (Anayekutieni usingizi) usiku.” (6:60)

Na Allah تعالى Amesema،

اللَّهُ يَتَوَفَّى الْأَنفُسَ حِينَ مَوْتِهَا وَالَّتِي لَمْ تَمُتْ فِي مَنَامِهَا

“Mwenyezi Mungu Huzipokea roho zinapokufa. Na zile zisiokufa wakati wa kulala kwake...” (39:42)

Mtume ﷺ alikuwa akisoma maneno yafuatayo kila alipoamka،

«الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَخْبَانَا بَعْدَ مَا أَمَاتَنَا، وَإِلَيْهِ النُّشُورُ»

“Sifa njema ni za Allah Ambaye Ametuhisha baada ya kutufisha na Kwake ndiko kwenye kukusanywa”.¹ Kauli Yake Allah تعالى،

وَيَكْفُرِهِمْ وَقَوْلِهِمْ عَلَىٰ مَرْيَمَ بِهَتْنًا عَظِيمًا ﴿١٢٧﴾ وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا آلَاسِيحَ عِيسَى ابْنِ

مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَٰكِن سُبُّهُ هُمُ

“Na pia kwa kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa, Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuua Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuua wala hawakumsulubu, bali walifananishiwa tu...”

Mpaka Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا ﴿١٢٧﴾ بَل رَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٢٨﴾ وَإِن مِّنْ أَهْلِ

الْكِتَابِ إِلَّا لَيُؤْمِنَنَّ بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِ ۗ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِدًا ﴿١٢٩﴾

¹ Fat’hul Al-Bari 11:134.

“Wala hawakumuua kwa yakini, Bali Mwenyezi Mungu Alimnyanyua kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima. Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika watamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.” (4:156-159)

Anayekusudiwa katika maneno, (...***Kabla ya kufa kwake...***) Ni Isa عليه السلام. Yaani watu wa Kitabu watamuamini Isa عليه السلام, kabla ya Isa عليه السلام kufa. Hili litajiri wakati Isa عليه السلام atakaporejea tena duniani kabla ya siku ya kiyama, kama tutakavyoeleza. Wakati huo, watu wote wa Kitabu watamuamini Isa عليه السلام, kwani atafuta ushuru na hatairidhia dini nyingine isipokuwa Uislam tu. Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Hasan akiizungumzia Kauli hii ya Allah تعالى،

إِنِّي مُتَوَقِّفُكَ

“Mimi Nitakutimizia muda wako wa kuishi (hawatakuua hao maadui).” “Ni kwa njia ya kifo cha usingizi, kwani Allah تعالى Alimnyanyua Isa عليه السلام akiwa usingizini.”¹

Kupotoshwa kwa Dini ya Isa عليه السلام

Allah تعالى Amesema;

وَمُطَهَّرُكَ مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا

“...Na Nitakutakasa na wale waliokufuru...” Kwa Kukupandisha mbinguni,

وَجَاعِلٌ لِّلَّذِينَ اتَّبَعُوكَ فَوْقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ

“Na Nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru, mpaka Siku ya Kiyama.” (3:55)

Hivi ndivyo ilivyojiri. Allah تعالى Alipomnyanyua Isa عليه السلام kwenda Mbinguni, wafuasi wake waligawanyika makundi makundi baada yake. Baadhi yao waliamini kuwa Allah تعالى Alimtuma Isa عليه السلام kuwa mtumwa wa Allah, Mjumbe Wake, na mtoto wa mjakazi Wake.

Hata hivyo, baadhi yao walivuka mipaka kumhusu yeye, wakamuitakidi kuwa alikuwa mwana wa Allah. Baadhi walisema kuwa Isa عليه السلام alikuwa Allah Mwenyewe, wakati wengine walisema alikuwa mmoja kati ya Watatu. Allah

¹ Ibn Abu Hatim 2:296.

Amezitaja imani potofu hizi ndani ya Qur'an, na Akakanusha dai la kila kundi. Wakaendelea katika hali hiyo kiasi cha miaka mia tatu, wakati mfalme wa Kiyunani aliyetitwa, Konstantino, alipoingia katika Ukristo kwa lengo la kuuangamiza Ukristo. Konstantino alikuwa ni mwanafalsafa na mjinga. Konstantino aliibadili dini ya Isa عليه السلام kwa kuongeza na kupunguza au kufuta baadhi ya kanuni. Alianzisha ibada za Kikristo na kinachoitwa Amana Kuu, ambayo ni khiyana dhalili. Na akahalalisha ulaji wa nyama ya Nguruwe katika zama zake, akakibadili kibla alichofundisha Nabii Isa عليه السلام na kuwageuzia watu upande wa mashariki. Akajenga makanisa kwa ajili ya Isa عليه السلام, na wakaongeza siku kumi za kufunga kwa ajili ya kulipia dhambi alizofanya, kama walivyodai. Hivyo dini ya Isa عليه السلام ikawa dini ya Konstantino, ambaye alijenga makanisa zaidi ya elfu kumi na mbili, mahekalu na nyumba za watawa kwa Wakristo na miji iliyokuwa na Jina lake, Konstantinopo (Istanbul). Wakati wote huo, wakristo walikuwa wamewazidi na kuwatawala Mayahudi. Allah تعالى Aliwasaidia dhidi ya Mayahudi kwa sababu walikuwa karibu na ukweli kuliko Mayahudi, japokuwa makundi yote yalikuwa bado makafiri, Laana za Allah تعالى Ziwashukie.

Allah تعالى Alipomtuma Muhammad ﷺ, kwa wale waliomuamini Allah تعالى, Malaika Wake, Vitabu na Mitume katika hali iliyo nzuri. Hivyo walikuwa ndio wafuasi wa kweli wa kila Mtume aliyekuja duniani. Walimuamini Mtume ﷺ asiyejua kusoma wala kuandika kikasomwa "ummij", Mtume wa mwisho Mtukufu au Mkuu wa wana wa Adamu wote, ambaye aliwalingania kuusadiki ukweli wote. Kwa sababu hii wakawa wanamtukuza kila Mtume aliyetoka katika Taifa hilo, hasa wale wanaodai kufuata njia ya Mitume wao na dini, ilhali wamebadili na kuipotoshwa Dini. Zaidi ya hayo, Allah تعالى Alizifuta sharia zote zilizoteremshwa kwa Mitume baada ya kuja sharia aliyompelekea Mtume Muhammad ﷺ, ambayo ni pamoja na Dini ya kweli ambayo haitobadilika au kupotoshwa mpaka siku ya Kiyama.

Dini aliyopewa Mtume Muhammad ﷺ na Mwenyezi Mungu siku zote itakuwa imara na yenye kuzishinda dini nyinginezo. Kwa sababu Allah تعالى Aliwapa ushindi Waislam kutoka Mashariki na Magharibi ya dunia na himaya zote. Zaidi ya hayo, nchi zote zilisalimu amri kwao; walimuangamiza Kisra (mfalme wa Persia) na Kaizari (Czar), na kuziteka hazina zao na kuzitumia kwa ajili ya Allah تعالى. Yote haya yalijiri mara baada ya Mtume ﷺ kuwaambia kuwa yatatokea, kutokana na Kauli ya Allah تعالى,

وَعَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا
 اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ
 خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۗ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۗ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ
 الْفَاسِقُونَ ﴿٥٨﴾

“Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa waliokuwa kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia Dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu.” (24:55)

Kwa hiyo, Waislamu walipokuwa wao ndio waumini wa kweli wa Isa عليه السلام. Baadaye waliitwaa Sham kutoka kwa Wakristo na kuwasababisha kuhamia Roma, ngome ya jiji la Konstantinopo. Uislamu na Waislamu wataendelea kuwa juu yao mpaka siku ya Kiyama. Kwa hakika, Mkweli mno (Muhammad ﷺ) alipokea habari za kweli, alifikisha ujumbe kwa Waislamu kuwa wataiteka Konstantinopo na kuchukua mali yake. Na kwamba waumini watapigana hapo Roma mapigano ambayo watu hawajawahi kuyaona, wala hawataona mengine yanayoyazidi hayo. Na kuhusu Maudhui hii, nimeelezea katika mlango wa peke yake.

Kuwatisha Makafiri kwa Mateso Hapa Duniani na Akhera

Na kwa kuzingatia hilo, Allah تعالى Amesema,

وَجَاعِلُ الَّذِينَ اتَّبَعُوكَ فَوْقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ ۗ ثُمَّ إِلَىٰ مَرْجِعِكُمْ
 فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٩﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَأَعَدَّ لَهُمْ عَذَابًا
 شَدِيدًا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمَا لَهُم مِّن نَّاصِرِينَ ﴿٦٠﴾

“Na Nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa Kwangu, Nikuhukumuni katika yale mliyokuwa mkikhitalifiana. Ama wale waliokufuru. Nitawaadhibu adhabu kali katika dunia na Akhera, wala hawatapata wa kuwanusuru”.

Haya ndiyo Aliyoyafanya Allah تعالى kwa Mayahudi ambao walimkanusha Isa عليه السلام; na Wakristo ambao walivuka mipaka ya kumsifu. Allah تعالى Aliwaadhibu hapa duniani, kwa kuuawa, kutekwa, kupotea kwa mali zao na kuondolewa tawala zao. Adhabu watakazopata Akhera ni kali zaidi na nzito.

﴿٣٤﴾ وَمَا لَهُمْ مِنَ اللَّهِ مِنْ وَاقٍ

**“Na wala hawatakuwa na wa kuwalinda na Mwenyezi Mungu”
(13:34)**

وَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُوَفِّيهِمْ أُجُورَهُمْ

“Na ama wale walioamini na wakatenda mema basi Mwenyezi Mungu Atawalipa ujira wao kamili”. (3:57)

Hapa duniani, kwa ushindi na kutawala, na Akhera, kwa Pepo zilizo za juu,

﴿٣٥﴾ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ

“Na Mwenyezi Mungu Hawapendi madhaalimu”. (3:57)

Allah تعالى Amesema,

ذَٰلِكَ نَتْلُوهُ عَلَيْكَ مِنَ الْآيَاتِ وَالذِّكْرِ الْحَكِيمِ ﴿٣٦﴾

“Haya Tunayokusomea ni katika Aya na Ukumbusho wenye hikima”. (3:58)

Maana yake: “Tulichokusimulia wewe, Ewe Muhammad ﷺ, kuhusiana na Isa, عليه السلام kuzaliwa kwake na maisha yake, ni kile Allah تعالى Alichokufikishia na Akakufunulia, Alikiteremsha kwako kutoka *Al-Lawh Al-Mahfudh* (Ubao uliohifadhiwa). Hivyo hapana shaka juu yake.” Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema katika Surah ya Maryam,

ذَٰلِكَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ ؑ قَوْلَ الْحَقِّ الَّذِي فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٣٧﴾ مَا كَانَ لِلَّهِ أَنْ يَتَّخِذَ مِنْ

وَالِدٍ سُبْحٰنَهُ ؕ إِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٣٨﴾

“Huyo ndiye Isa mwana wa Maryamu. Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka. Haiwi kwa Mwenyezi Mungu kuwa na mwana, Subhanahu, Yeye Ametakasika! Anapolihukumia jambo basi Huliambia tu: Kuwa! Likawa”. (19:34-35) Na hapa Allah تعالى Amesema,

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ ۗ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ
 ثُمَّ قَالَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُن مِّنَ
 الْمُمْتَرِينَ ﴿٦٠﴾ فَمَنْ حَاجَّكَ فِيهِ مِن بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ
 الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَهُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَهُمْ
 وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَهُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَل لَّعْنَتَ اللَّهِ عَلَى
 الْكٰذِبِينَ ﴿٦١﴾ إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْفَقْصُ الْحَقُّ وَمَا
 مِن إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٢﴾ فَإِن
 تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِالْمُفْسِدِينَ ﴿٦٣﴾ قُلْ يَتَّهَلَّ الْكِتٰبِ
 تَعَالَوْا إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا
 نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّن دُونِ
 اللَّهِ ۗ فَإِن تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾
 يَتَّهَلَّ الْكِتٰبِ لِمَ تُحَاجُّوْنَ فِي إِبْرٰهِيْمَ وَمَا أُنزِلَتْ
 التَّوْرَةُ وَالْإِنْجِيلُ إِلَّا مِنْ بَعْدِهِمْ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٥﴾
 هَٰئِنتُمْ هَٰؤُلَاءِ حٰجَجْتُمْ فِيمَا لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ فَلِمَ
 تُحَاجُّوْنَ فِيمَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ ۗ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا
 تَعْلَمُونَ ﴿٦٦﴾ مَا كَانَ إِبْرٰهِيْمُ يَهُودِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلٰكِنْ
 كَانَتْ حٰنِيْفًا مُّسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٦٧﴾ إِنَّ
 أَوْلَىٰ النَّاسِ بِإِبْرٰهِيْمَ لَلَّذِينَ آتَّبَعُوهُ وَهَدَاَ النَّبِيُّ وَالَّذِينَ
 ءَامَنُوا ۗ وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٨﴾

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ
 آدَمَ ۗ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ
 كُن فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا
 تَكُن مِّنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٦٠﴾ فَمَنْ
 حَاجَّكَ فِيهِ مِن بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ
 الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ أَبْنَاءَنَا
 وَأَبْنَاءَهُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَهُمْ
 وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَهُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ
 فَنَجْعَل لَّعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكٰذِبِينَ ﴿٦١﴾
 إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْفَقْصُ الْحَقُّ وَمَا
 مِن إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ
 الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٢﴾ فَإِن
 تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِالْمُفْسِدِينَ ﴿٦٣﴾

**59. Hakika mfano wa Isa
 kwa Mwenyezi Mungu ni
 kama mfano wa Adam;
 Alimuumba kwa udongo
 kisha Akamwambia: Kuwa!
 Basi akawa.**

**60. Hii ni kweli itokayo kwa
 Mola wako Mlezi. Basi
 usiwe miongoni mwa
 wanaofanya shaka.**

61. Watakaokuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooi tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe, kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.

62. Hakika haya ndiyo maelezo ya kweli. Na hakuna mola ila Mwenyezi Mungu tu, na hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.

63. Na kama wakigeuka basi Mwenyezi Mungu Anawajua wahaaribifu.

Kufanana katika Kuumbwa kwa Adam عليه السلام na Isa عليه السلام:

Allah تعالى Amesema, **إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ**

“Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu.” Kuhusiana na Uweza wa Allah تعالى, kwa kuwa Alimuumba bila ya kuwa na baba,

كَمَثَلِ آدَمَ

“Ni kama mfano wa Adam.” Alimuumba bila baba na mama. Bali,

خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾

“Alimuumba kwa udongo kisha Akamuambia: Kuwa! Basi akawa”.

Kwa hiyo, Yule Aliyemuumba Adam عليه السلام bila ya baba wala mama, Ana Uweza wa Kumuumba Isa عليه السلام vile vile, bila ya baba. Iwapo madai yaliyofanywa kuwa Isa عليه السلام ni mwana wa Mungu kwa sababu aliumbwa bila baba yangepitishwa, basi yangemstahikia zaidi Adam عليه السلام. Hata hivyo, kwa kuwa madai kumhusu Adam عليه السلام ni batili hivyo kufanya madai sawa na hayo kumhusu Isa عليه السلام ni batili zaidi na ni uovu mkubwa.

Zaidi ya hayo, kwa kutaja ukweli huu, Allah تعالى Anatilia mkazo, Uwezo Wake, kwa Kumuumba Adam عليه السلام bila mwanaume au mwanamke, Alimuumba Hawa kutokana na mwanaume bila mwanamke, na Isa عليه السلام kutokana na mwanamke bila mwanaume, ikilinganishwa na Alivyowaumba viumbe wengine kutokana na mwanamume na mwanamke. Ndiyo sababu Allah تعالى Amesema ndani ya Surah ya Maryam;

وَلِتَجْعَلَهُ آيَةً لِلنَّاسِ

“Na ili Tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu”. (19:21) Allah تعالى Anasema katika Aya hii,

الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُنْ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٦٠﴾

“Hii ni kweli itokayo kwa Mola Wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka.” (3:60)

Maana yake: Hii ndiyo Kauli sahihi juu ya Isa عليه السلام, ambayo hakuna kingine kisichokuwa hiki ni ukweli, bali ni upotevu.

Mwito kwa Ajili ya Kuliania “Mubalah” Kuhusu Ukweli wa Isa عليه السلام:

Baada ya hapo Allah تعالى Alimuamuru Mtume ﷺ kuwalingania wale waliokengeuka ukweli, kuhusu Isa عليه السلام na kukhitari Muballah (laana) baada ya kudhihiri ubainifu.

فَمَنْ حَاجَّكَ فِيهِ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَكُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَكُمْ وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَكُمْ

“Watakao kuhoji katika haya baada ya kukufikilia ilimu hii waambie: Njooi tuwaite watoto wetu na watoto wenu, na wake zetu na wake zenu, na sisi wenyewe na nyinyi wenyewe.”

Maana yake: Tunawaleta hapa wote wakati wa “Mubalah” kuapizana na kuliania.

ثُمَّ نَبِّهَانِ

“Kisha tuombe kwa unyenyekevu”. Kuomba dua,

فَنَجْعَل لَّعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكٰذِبِينَ ﴿٦١﴾

“Tutake laana ya Mwenyezi Mungu iwashukie waongo.”

Maana yake: Ama sisi au nyinyi. Sababu ya kuteremshwa kuapizana huku “Mubalah” kuanzia mwanzo wa Surah hii mpaka hapa, ni kuhusu ujumbe kutoka kwa Wakristo wa Najran (Yemen) waliokuja Madinah kubishana kuhusu Isa عليه السلام, wakawa wanatoa madai yao mbalimbali kama umwana wa mungu na uungu wa Isa عليه السلام. Allah تعالى Aliteremsha Aya za mwanzo wa Surah hii mpaka hapa, kukanusha madai yao.

Ni kama vile bin Is-haq alivyosema katika kitabu chake Mashuhuri cha Sira na wanazuoni wengine.

Ujumbe wa Wakristo kutoka Najran ulikuja kwa Mtume ﷺ katika ujumbe huo kulikuwa na wapanda farasi sitini, pamoja na machifu wao kumi na wanne waliokuwa waamuzi wa mambo yao. Watu hawo walikuwa Al-`Aqib ambaye alikuwa akiitwa pia Abdul-Masih, As-Sayyid, pia akiitwa Al-Ayham, Abu Harithah bin `Alqamah ambaye alikuwa ndugu wa Bakr bin Wail, Uways bin Al-Harith, Zayd, Qays, Yazid, Nabih, Khuwaylid, Amr, Khalid, Abdullah na Yuhannas. Watatu kati yao walikuwa viongozi wa ujumbe huo. Hawa walikuwa: Al-`Aqib, aliyekuwa mkuu wao na walikuwa wanamtaka ushauri na kutoa maamuzi. Mwingine alikuwa As-Sayyid ambaye alikuwa msomi wao, msafiri mwenzao na mmojawapo katika jamii yao. Abu Haritha bin `Alqamah, aliyekuwa askofu na kiongozi wao, pia alikuwa mwalimu wao. Asili yake, alikuwa mwarabu aliyetokana na ukoo wa Banu Bakr bin Wail, lakini alibatizwa na kuwa Mkristo. Warumi na wafalme wao walimpa heshima na wakamjengea makanisa (au wakajenga kwa heshima yake). Pia walimsaidia kifedha na wakampa watumishi, kwa sababu walijua msimamo wake katika dini yao.”¹ Abu Harithah alikuwa akiujua wasifu bainifu wa Mtume ﷺ kutokana na alivyojifunza kutoka katika vitabu vitakatifu vilivyotangulia. Hata hivyo, upumbavu wake ukamfanya kubakia katika Ukristo, kwa sababu alipewa heshima na alikuwa na nafasi ya juu kwa Wakristo.

Ibn Is-haq رحمه الله تعالى alisema, Muhammad bin Jaffar bin Az-Zubayr aliniambia, “Ujumbe wa Najran ulikuja kwa Mtume ﷺ Madinah, waliingia Msikitini huku wamevaa nguo na vilemba baada ya Mtume ﷺ kumaliza kuswali Sala ya Alasiri. Walifuatana na msafara wa ngamia ulioongozwa na Bani Al-Harith bin Ka`b. Masahaba wa Mtume ﷺ waliowaona walisema: Hatujawahi kuona msafara kama ule. Muda wa sala yao, msafara ule, ulikuwa umeshawadia. Wakasimama kusali katika Msikiti wa Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akasema, “*Waacheni*”. Wakasali wakiwa wameelekeza nyuso zao upande wa mashariki. Kisha Abu Haritha bin Alqamah na Al-`Aqib Abdul Masih au As-Sayyid Al-Ayham walizungumza na Mtume ﷺ, nao walikuwa Wakristo kama Mfalme wa Roma. Hata hivyo hawakukubaliana kuhusu Isa عليه السلام.

¹ Ibn Hisham 2:222.

Baadhi yao walisema, 'Ni Mungu' ambapo wengine walisema 'Ni mwana wa Mungu' na wengine walisema, 'Ni mmoja katika Utatu'. Allah تعالی Ametakasika na sifa walizomba kutakasika kukubwa.

Kwa hakika, hizi ndizo imani za Wakristo. Wanaodai kuwa Isa عليه السلام ni Mungu, kwa kuwa aliwafufua wafu, aliwaponya vipofu, wenye mbalanga, wenye maradhi, na kueleza habari zilizojificha, na kuunda kutokana na udongo umbile la ndege na akapulizia uhai, na wakawa ndege hai. Hata hivyo miujiza yote hiyo ilitokea kwa uweza wa Allah تعالی, ili Isa عليه السلام awe ishara kwa watu kutoka kwa Allah تعالی.

Pia, wanadai kuwa Isa عليه السلام ni mwana wa Mungu kwa kuwa hakuwa na baba na alizungumza akiwa ndani ya susu, muujiza ambao haukupatapo kutokea kwa yeyote miongoni mwa Wana wa Adamu kabla yake.

Wanadai pia kuwa Isa عليه السلام ni mmoja katika Utatu, kwa sababu Allah تعالی Amesema, 'Tulifanya', 'Tuliamrisha', 'Tuliumba', na 'Tuliamua'. Wanasema, "Iwapo Allah تعالی alikuwa mmoja, angesema, 'Nilifanya', 'Niliamrisha', 'Niliumba', na 'Niliamua'. Kwa sababu hii wanadai kuwa yupo Isa عليه السلام na Maryam. Allah تعالی yuko mbali na yale wanayomhusisha Nayo, na Qur'an ilikanusha madai yote hayo batili ya Wakristo."

Ibn Is-haq رحمه الله تعالی aliendelea, 'Maneno ya Allah تعالی yalipomfikia Mtume ﷺ na upambanuzi wa maamuzi baina yake na wao, na Amri ya Allah تعالی Aliyomuamuru, Mtume ﷺ aliwaita kwenye kuapizana "*Mubahalal*." Walisema, 'Ewe Abu Al-Qasim! Tupe muda tutafakari suala hili na tutarejea na uamuzi wa tunalotaka kufanya. 'Walimuacha Mtume ﷺ na kwenda kushauriana na Al-'Aqib ambaye walirejea kwake kwa ushauri. Wakamuambia, 'Ewe Abdul-Masih! Nini ushauri wako?' Akawajibu, '*Wallahi*, Enyi ndugu zangu Wakristo! Mnajua kuwa Muhammad ﷺ ni Nabii na Mjumbe na kuwa amewaletea neno la mwisho kuhusu jamaa yenu (Isa عليه السلام). Pia mnajua kuwa hapana Mtume aliyeapizana "*Mubahalal*" na watu wowote, na baada ya hapo wakaweza kusalimika wazee miongoni mwao na wadogo katika wao. Bila shaka, mkifanya, ndio utakuwa mwisho wenu. Iwapo mmeamua kubaki katika dini yenu na imani yenu kumhusu jamaa yenu (Isa عليه السلام), basi muageni (Muhammad) na mrejee katika miji yenu." Walirejea kwa Mtume ﷺ na kumuambia, "Ewe Abu Al-Qasim! Tumeamua kutoapizana "*Mubahalal*" nawe

¹ Ibn Hisham 2:233.

² Fat'hul Al-Bari 7:695.

³ Fat'hul Al-Bari 7:696.

baki na dini yako, nasi tubaki na dini yetu.¹ "Hata hivyo tupatie mtu katika Maswahaba wako unayemuamini awe hakimu wetu katika migogoro ya kifedha, kwani nyinyi mnakubalika kwetu."

Bukhari alinukuu kutoka kwa Hudhayfah رضي الله عنه alisema, Al-'Aqib na As-Sayyid, viongozi wawili kutoka Najran, walikuwa kwa Mtume ﷺ wakitaka kuapizana (dhidi ya yeyote aliye dhalimu miongoni mwao), na mmoja wao alimuambia mwenzie, 'Wallahi! Tusifanye, iwapo ni Mtume wa kweli na tukila kiapo kwa Allah تعالى kwa laana, sisi na vizazi vyetu hatutofanikiwa baadaye.' Hivyo wakasema, 'Tutakupa ulichotaka na tupe mtu mwaminifu tuondoke naye, mtu mwaminifu tu.' Mtume ﷺ alisema,

«لَأَبْعَثَنَّ مَعَكُمْ رَجُلًا أَمِينًا حَقَّ أَمِينٍ» فاستشرف لها أصحاب رسول الله ﷺ، فقال: «قُمْ يَا أَبَا عُيَيْدَةَ بْنِ الْجَرَّاحِ» فلما قام، قال رسول الله ﷺ: «هَذَا أَمِينٌ هَذِهِ الْأُمَّةُ»

"Nitamtuma pamoja nanyi mtu mwaminifu mwenye ukweli wa uaminifu, kila mmoja miongoni mwa Masahaba wa Mtume wa Allah ikawa anatamani awe yeye. Mtume wa Allah ﷺ akasema: "Simama ewe Aba Ubaydah bin Al-Jarraah." Aliposimama, Mtume ﷺ akasema: "Huyu ndio mwaminifu wa umma huu".¹

Bukhari alinukuu kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema katika wasaa mwingine,

«لِكُلِّ أُمَّةٍ أَمِينٌ، وَأَمِينُ هَذِهِ الْأُمَّةِ أَبُو عُيَيْدَةَ بْنُ الْجَرَّاحِ»

"Kila umma una mwaminifu wake, na mwaminifu wa umma huu ni Abu 'Ubaydah bin Al-Jarraah."²

Imam Ahmad alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Abu Jahl, Mungu Amlaani, alisema, "Iwapo nitamuona Muhammad ﷺ akisali pambizoni mwa Ka'bah, nitamkanyaga katika shingo yake." Baadae Mtume ﷺ alisema,

«لَوْ فَعَلَ لَأَخَذْتُهُ الْمَلَأَيْتُكَ عَيْنًا، وَلَوْ أَنَّ الْيَهُودَ تَمَنَّا الْمَوْتَ لَمَاتُوا، وَرَأَوْا مَقَاعِدَهُمْ مِنَ النَّارِ، وَلَوْ خَرَجَ الَّذِينَ يَبَاهِلُونَ رَسُولَ اللَّهِ ﷺ لَرَجَعُوا لَا يَجِدُونَ مَالًا وَلَا أَهْلًا».

¹Fat'hul Al-Bari 7:695.

²Fat'hul Al-Bari 7:696.

*“Kama angefanya malaika wangemchukua hadharani, na lau mayahudi wangetamani mauti wangekufa, na wangeona makalio yao motoni, na lau wangetoka wale kwa ajili ya kuapizana na Mtume ﷺ wangerejea bila ya mali wala familia”.*¹

Bukhari, At-Tirmidhi na An-Nasai² nao pia waliinukuu Hadithi hii, ambayo Tirmidhi aliipa daraja la *Hasan sahih*. Kisha Allah تعالى Amesema,

إِنَّ هَذَا لَهُوَ الْفَصُّ الْحَقُّ

“Hakika haya ndiyo maelezo ya kweli.” Maana yake: Tuli yokusimulia, Ewe Muhammad ﷺ, juu ya Isa عليه السلام ni ukweli ulio wazi usiopingika,

وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿٦٠﴾ فَإِنْ تَوَلَّوْا

“Na hakuna mola ila Mwenyezi Mungu tu, na hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima, na kama wakigeuka...”

Maana yake: Wakauacha ukweli huu kuyafuata yaliyo tofauti nayo.

فَإِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِالْمُفْسِدِينَ ﴿٦١﴾

“Basi Mwenyezi Mungu Anawajua waharibifu.” Maana yake: Mwenye kuiacha haki, akaiendea batili basi huyo ndiye mharibifu, na Allah تعالى Anawajua sana na Atawaadhibu vibaya juu ya hilo. Kwa hakika, Allah تعالى Ana Uwezo wa Kudhibiti kila kitu, Hashindwi na jambo, Utakasifu ni Wake, Shukrani na Sifa zote zinamstahikia Yeye, na tunajilinda dhidi ya Kisasi Chake.

قُلْ يَتَاهَلِ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ

شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ ؕ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا

مُسْلِمُونَ ﴿٦٢﴾

“Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooi kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi

¹ Ahmad 1:248.

² Fat’hul Al-Bari 8:595, Tuhfaat Al-Ahwadhi 9:77, An-Nasai katika Al-Kubra 6:518

Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa waola walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu".
(3:64)

Masuala ya Kumpwekesha Allah تعالی "Tawhid" Yanajulikana kwa Wote.

Ayah hii inawajumuisha Watu wa Kitabu, Mayahudi na Wakristo, na wale wanaofuata mwenendo wao.

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَى كَلِمَةٍ

"Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njoooni kwenye neno".

'Neno' - Katika Kiarabu - ina maana ya sentensi kamili, kama ilivyo katika Ayah hii. Allah تعالی Amelieleza neno hili kuwa ni moja,

سَوَاءٌ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمُ

"Lililo sawa baina yetu na nyinyi". Maana yake: Lililo la uadilifu ambalo lina usawa kwa pande zote. Kisha Allah تعالی Akalielezea neno hili,

أَلَا نَعْبُدُ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكُ بِهِ شَيْئًا

"Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote".

Hatuabudu sanamu wala, msalaba, wala *Taghut* (miungu), wala moto wala kitu chengine. Bali, tunamuabudu Allah تعالی Pekee, bila mshirika, na huu ni ujumbe wa Mitume wote wa Allah تعالی. Allah تعالی Amesema,

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٦٥﴾

"Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mola isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu."
(21:25) Na Allah تعالی Amesema,

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطُّغُوتَ

"Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani." (16:36)

Baadaye Allah تعالی Alisema,

وَلَا يَتَّخِذْ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا

“Wala baadhi yetu tusiwafanye wengine kuwa waola walezi badala ya Mwenyezi Mungu”. (3:64)

Ibn Jurayj alisema, “Maana yake ni kwamba kusiwe na utiifu baina yetu katika kumuasi Allah تعالى.”

فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَا مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾

“Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu”.

Wakiachana na ulingano huu wa haki, basi wajue kuwa nyie mtabaki katika Uislamu kama Allah تعالى Alivyokuamrisheni.

Na katika barua ambayo Mtume ﷺ alimpelekea Heraclius inasema, “Kwa Jina la Allah تعالى, Mwenye Kurehemu, Mwingi wa Rehema. Kutoka kwa Muhammad ﷺ, kwenda kwa Heraclius, kiongozi wa Warumi Amani iwe juu yao wale wanaofuata, Muongozo sahihi. Silimu na utapata amani, silimu na Allah تعالى Atakulipa maradufu. Hata hivyo, ukiupa mgongo Uislamu, utabeba Mzigo wa wanyonge.” Na,

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكَ إِلَّا نَعْبُدُ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكُ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِّنْ دُونِ اللَّهِ ۚ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَا

مُسْلِمُونَ ﴿٦٤﴾

“Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njoooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa waola walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu.” (3:64)

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى na wanazuoni wengine walisema kuwa mwanzo wa Surat Al-Imran mpaka zaidi ya Aya themanini baadaye; zilishushwa kuhusiana na ujumbe wa Najran. Az-Zuhri رحمه الله تعالى alieleza kuwa watu wa Najran walikuwa wa mwanzo kulipa Jizyah (Kodi iliyokuwa ikilipwa katika Dola ya Kiislam). Hata hivyo hapana kutofautiana kuwa Aya iliyoweka sheria ya

kodi "Jizyah" (9:29) iliteremshwa baada ya ufunguzi wa Mji wa Makka "Fat-h Makkah" (na kwa hiyo, baada ya ujumbe wa Najran kuja Madinah). Hivyo itakuwaje Ayah (3:64) itakuwepo kwenye barua ya Mtume ﷺ aliyomuandikia Heraclius kabla ya ushindi wa Makkah, na namna gani kupatanisha kati ya kauli ya Muhammad bin Is-haq na Az-Zuhri? Jibu ni kuwa ujumbe wa Najran ulikuja kabla ya Hudaybiyyah (Kabla ya ushindi wa Makkah), na walicholipa badala ya kuapizana "Mubahahlah" haikuwa kodi "Jizyah" bali ilikuwa ni katika kufanya suluhu na kutengeneza Mikataba ya amani. Aya inayohusu kodi "Jizyah" iliteremshwa baadaye na hukumu yake inaunga mkono yaliyojiri kwa watu wa Najran. Kwa kuunga mkono rai hii, tutaja katika tukio jengine, hukumu ya kugawa ngawira ya *khumsi* yaani moja ya tano (kwa ajili ya Mtume ﷺ) na nne ya tano (kwa ajili ya wapiganaji), iliyokubaliwa na Abdullah bin Jahsh wakati wa uvamizi aliouongoza kabla ya Badr. Ayah baadaye inathibitisha jinsi Abdullah alivyogawa ngawira, kwa hiyo inayumkinika kuwa Mtume ﷺ alipoamuru jambo hili, liorodheshwe katika barua aliyomuandikia Heraclius kabla ya kushushwa kwa Aya. Baadaye, Qur`an iliteremka kuafiki kauli ya Mtume ﷺ, neno kwa neno. Kama ambavyo Qur`an iliteremka ikikubaliana na kauli ya Umar رضي الله عنه kuhusu mateka wa kikafiri katika Badr, *Hijab* (vazi la stara kwa mwanamke wa Kiislam), na kujizuia kuwasalia wanafiki, na kuhusiana na Kauli Yake:

وَأَتَّخِذُوا مِنْ مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى

"Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia."
(2:125)

عَسَىٰ رَبُّهُ إِنْ طَلَّقَكُنَّ أَنْ يُبَدِّلَهُ أَزْوَاجًا خَيْرًا مِنْكَ

"Asaa Mola wake Mlezi, akikupeni talaka, Akampa wake wengine badala yenu nyinyi, walio bora kuliko nyinyi." (66:5)

يَتَأَهَّلَ الْكَتَبِ لِمَ تُحَاجُّوْنَ فِي إِبْرَاهِيمَ وَمَا أُنزِلَتِ التَّوْرَةُ وَالْإِنْجِيلُ إِلَّا مِنْ بَعْدِهِمْ
 أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٦﴾ هَتَأْتُمْ هَتَوْلَاءَ حَجَجْتُمْ فِيمَا لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ فَلِمَ تُحَاجُّوْنَ
 فِيمَا لَيْسَ لَكُمْ بِهِ عِلْمٌ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾ مَا كَانَ إِبْرَاهِيمَ يَهُودِيًّا وَلَا
 نَصْرَانِيًّا وَلَكِنْ كَانَ حَنِيفًا مُسْلِمًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٦٨﴾ إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ
 بِإِبْرَاهِيمَ لِلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ وَهَذَا النَّبِيُّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاللَّهُ وَلِيُّ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٩﴾

65. Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahim, na hali Taurati na Injili hazikuteremshwa ila baada yake? Basi hamzingatii?

66. Angalieni! Nyinyi mlibishana katika yale mliyoyajua. Mbona sasa mnabishana katika yale msiyoyajua? Na Mwenyezi Mungu Ndiye Ajuaye, na nyinyi hamjui.

67. Ibrahim hakuwa Yahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu Muislamu, wala hakuwa katika washirikina.

68. Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahim ni wale waliomfuata yeye na Nabii huyu na walioamini. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa Waumini.

Kubishana kwa Mayahudi na Wakristo Juu ya Dini ya Ibrahim عليه السلام:

Allah تعالى Anawakanushia Mayahudi na Wakristo katika mabishano yao juu ya Ibrahim Al-Khalil عليه السلام na madai ya kila kundi kuwa alikuwa mmoja wao. Muhammad bin Is-haq bin Yasar رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, 'Wakristo wa Najran na viongozi wa Dini wa Kiyahudi walijikusanya mbele ya Mtume ﷺ na wakabishana mbele yake.' Makuhani wakasema, 'Kwa hakika Ibrahim alikuwa Myahudi,' Wakristo wakasema, "kwa hakika, Ibrahim alikuwa Mkristo.' Hivyo Allah تعالى Akateremsha,

يَتَأْهَلُ الْكُتُبَ لِمَ تُحَاجُّونَ فِي إِبْرَاهِيمَ

"Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahim."

Maana yake: 'Inakuaje nyie, Mayahudi, mnadai kuwa Ibrahim alikuwa Yahudi, japokuwa aliishi kabla ya Allah تعالى kuteremsha Taurati kwa Musa عليه السلام? Imekuwaje nyie, Wakristo, kudai kuwa Ibrahim عليه السلام alikuwa Mkristo, ilhali Ukristo ulikuja baada yake?'¹

أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٥٩﴾

"Basi hamzingatii?". Kisha Allah تعالى Akasema,

¹ At-Tabari 6:490.

هَتَأْتُمْ هَتُولَاءِ حَسَبِجْتُمْ فِيمَا لَكُمْ بِمِ عِلْمٍ فَلِمَ تُحَاجُّوْنَ فِيمَا لَيْسَ لَكُمْ بِمِ عِلْمٍ

“Angalieni! Nyinyi mlibishana katika yale mliyoyajua. Mbona sasa mnabishana katika yale msiyo yajua?”

Aya hii inawakosoa wale wanaobishana bila ilimu, kama walivyofanya Mayahudi na Wakristo kuhusu Ibrahim عليه السلام. Kama wangebishana juu ya dini zao, ambazo walikuwa na ilimu nazo, na kuhusu sharia walizotakiwa kuzifuata mpaka Muhammad ﷺ alipotumwa, ingekuwa wana ilimu nalo, hivyo Allah تعالى Aliwakosoa kwa tabia yao hiyo. Allah تعالى Aliwaamuru warejee kwa Yule Anayejua vinavyoonekana na visivyonekana na Yule Anayejua ukweli wa vitu vyote kwa yale wasiyo na ilimu nayo. Kwa sababu hii Allah تعالى Alisema,

وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٧﴾

“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Ajuaye, na nyinyi hamjui.”

Allah تعالى Amesema,

مَا كَانَ إِبْرَاهِيمُ يَهُودِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلَكِنْ كَانَ حَنِيفًا مُّسْلِمًا

“Ibrahim hakuwa Yahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu Muislamu.”

Hakuwa mshirikina na aliishi katika Imani.

وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٦٨﴾

“Wala hakuwa katika washirikina.” Aya hii ni sawa na Aya katika Surat Al-Baqarah,

وَقَالُوا كُونُوا هُودًا أَوْ نَصْرَى يَهْتَدُوا

“Na wakasema: Kuweni Mayahudi au Wakristo ndio mtaongoka.”

(2:135) Baadaye Allah تعالى Amesema,

إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِإِبْرَاهِيمَ لَلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ وَهَذَا النَّبِيُّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَاللَّهُ وَبِيُّ

الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٩﴾

“Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahim ni wale waliomfuata yeye na Nabii huyu na walioamini. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa Waumini”.

Ayah hii ina maana, “Watu wenye haki ya kuwa wafuasi wa Ibrahim عليه السلام ni wale waliofuata dini yake na Mtume huyu, Muhammad ﷺ na Maswahaba wake katika *Muhajirin*, *Ansarna* wale waliofuata uongozi wao.” Said bin Mansur alinukuu kutoka kwa Ibn Mas’ud رضي الله عنهما akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ لِكُلِّ نَبِيٍّ وُلَاةً مِّنَ النَّبِيِّينَ، وَإِنَّ وُلِيَّيَ مِنْهُمْ أَبِي وَخَلِيلُ رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ»

“Kila Mtume ana Wali (mfuasi na rafiki wa karibu), miongoni mwa Mitume, mtu wangu wa karibu katika wao, ni baba yangu Ibrahim, Khalili wa Mola wangu, Mtukufu Aliyetukuka.”

Kisha akasoma:

إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِإِبْرَاهِيمَ لَلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ

“Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahim ni wale waliomfuata”. (3:68)

Kauli Yake Allah تعالى،

وَاللَّهُ وِلِيُّ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٨﴾

“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa Waumini.”

Maana yake: Allah تعالى Ndiye Mlinzi wa wale wote wanaoamini Mitume Wake.

* * *

وَدَّتْ طَآئِفَةٌ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ يُضِلُّوكُمْ وَمَا يُضِلُّونَ
 إِلَّا أَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٦٩﴾ يَتَّاهَلُ الْكِتَابِ لِمَ
 تَكْفُرُونَ بِقَايَتِ اللَّهِ وَأَنْتُمْ تَشْهَدُونَ ﴿٧٠﴾ يَتَّاهَلُ
 الْكِتَابِ لِمَ تَلْبِسُونَ الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُونَ الْحَقَّ
 وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٧١﴾ وَقَالَتْ طَآئِفَةٌ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ
 ءَامِنُوا بِالَّذِي أُنزِلَ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَجَهَ النَّهَارِ
 وَكُفِّرُوا ءَاخِرَهُ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٧٢﴾ وَلَا تُؤْمِنُوا إِلَّا لِمَنْ
 تَبِعَ دِينَكُمْ قُلْ إِنْ أَلْهَدَى اللَّهُ هُدَىٰ اللَّهِ أَنْ يُؤْتَىٰ أَحَدٌ مِّثْلَ
 مَا أُوتِيْتُمْ أَوْ يُحَاجُّوكُمْ عِنْدَ رَبِّكُمْ قُلْ إِنْ أَلْفَضَلْ بِيَدِ اللَّهِ
 يُؤْتِيهِ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ وَسِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٧٣﴾ يَخْتَصُّ بِرَحْمَتِهِ
 مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٧٤﴾ * وَمِنْ أَهْلِ
 الْكِتَابِ مَن إِنْ تَأْمَنَهُ بِنَقَارٍ يُؤَدِّهِ إِلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَن إِنْ
 تَأْمَنَهُ بَدِينَارٍ لَا يُؤَدِّهِ إِلَيْكَ إِلَّا مَا دُمْتَ عَلَيْهِ قَائِمًا ۗ
 ذَلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لَيْسَ عَلَيْنَا فِي الْأُمِّيْنَ سَبِيلٌ
 وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٧٥﴾ بَلَىٰ
 مَن أَوْفَىٰ بَعْدِهِ ۗ وَأَتَّقِ فَإِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٧٦﴾ إِنْ
 الَّذِينَ يَشْرُونَ بَعْدَ اللَّهِ وَأَيْمَنِتُمْ ثَمَنًا قَلِيلًا أُوتِيتُمْ لَآ
 خَلْقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ
 يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٧﴾

وَدَّتْ طَآئِفَةٌ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ
 يُضِلُّوكُمْ وَمَا يُضِلُّونَ إِلَّا
 أَنْفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٦٩﴾
 يَتَّاهَلُ الْكِتَابِ لِمَ تَكْفُرُونَ
 بِقَايَتِ اللَّهِ وَأَنْتُمْ تَشْهَدُونَ ﴿٧٠﴾
 يَتَّاهَلُ الْكِتَابِ لِمَ تَلْبِسُونَ الْحَقَّ
 بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُونَ الْحَقَّ وَأَنْتُمْ
 تَعْلَمُونَ ﴿٧١﴾ وَقَالَتْ طَآئِفَةٌ مِّنْ
 أَهْلِ الْكِتَابِ ءَامِنُوا بِالَّذِي أُنزِلَ
 عَلَى الَّذِينَ ءَامِنُوا وَجَهَ النَّهَارِ
 وَكُفِّرُوا ءَاخِرَهُ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٧٢﴾
 وَلَا تُؤْمِنُوا إِلَّا لِمَنْ تَبِعَ دِينَكُمْ قُلْ
 إِنْ أَلْهَدَى اللَّهُ هُدَىٰ اللَّهِ أَنْ يُؤْتَىٰ أَحَدٌ
 مِّثْلَ مَا أُوتِيْتُمْ أَوْ يُحَاجُّوكُمْ عِنْدَ
 رَبِّكُمْ قُلْ إِنْ أَلْفَضَلْ بِيَدِ اللَّهِ يُؤْتِيهِ
 مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ وَسِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٧٣﴾
 يَخْتَصُّ بِرَحْمَتِهِ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو
 الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٧٤﴾

69. Kipo kikundi katika Watu
wa Kitabu wanaopenda

kukupotezeni; lakini hawapotezi ila nafsi zao, nao wenyewe hawatambui.

70. Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu ilhali nyinyi mnashuhudia?

71. Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnachanganya haki na batili, na kweli mnaificha na hali mnajua?

72. Na kikundi katika Watu wa Kitabu walisema: Yaaminini yale waliyoteremshiwa wenye kuamini mwanzo wa mchana, na yakataeni mwisho wake; huenda wakarejea.

73. Wala msimuamini ila anayefuata dini yenu. Sema: Hakika uwongofu ni uwongofu wa Mwenyezi Mungu, kuwa apewe mtu mfano wa mliopewa nyinyi au wakuhojini mbele ya Mola wenu Mlezi. Sema: Hakika Fadhila zimo Mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Humpa Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mjuzi.

74. Yeye Humchagua Kumpa Rehema Zake Amtakaye; na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Fadhila Kubwa.

Husuda na Njama za Mayahudi Dhidi ya Waislamu

Allah تعالی Ameeleza kuwa Mayahudi huwahasudu waumini na kutamani kama wangepotoshwa, Allah تعالی Ameeleza kuwa tabia yao hii ya kutaka Waislamu wafikwe na balaa itawarejea wao, huku hawatambui kwamba Allah تعالی Anawavutia muda. Kisha Allah تعالی Akasema Kupinga vitendo vyao hivyo,

يَتَأْهَلُ الْكِتَابِ لِمَ تَكْفُرُونَ بِفَايْتِ اللَّهِ وَأَنْتُمْ تَشْهَدُونَ ﴿٧٠﴾

“Enyi Watu wa Kitabu! Mbona mnazikataa Ishara za Mwenyezi Mungu ilhali nyinyi mnashuhudia?”

Maana yake: Mnajua na mnauthibitisha ukweli wake.

يَتَأْهَلُ الْكِتَابِ لِمَ تَلْبِسُونَ الْحَقَّ بِالْبَاطِلِ وَتَكْتُمُونَ الْحَقَّ وَأَنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٧١﴾

“Enyi Watu wa Kitabu! Mbona kweli mnaivisha uwongo, na kweli mnaificha na hali mnajua?”

Kwa kuficha yaliyokuwemo ndani ya Vitabu vyenu juu ya sifa bainifu za Muhammad ﷺ wakati mnajua myafanyayo.

وَقَالَتْ طَّائِفَةٌ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ ءَامِنُوا بِالَّذِي أُنزِلَ عَلَى الَّذِينَ ءَامَنُوا وَجَهُ النَّهَارِ
وَأَكْفُرُوا ءَاخِرَهُ

“Na kikundi katika Watu wa Kitabu walisema: Yaaminini yale waliyoteremshiwa wenye kuamini mwanzo wa mchana, na yakataeni mwisho wake”.

Huu ni mpango ovu uliofanywa na Watu wa Kitabu ili kuwahadaa watu dhaifu katika Dini. Waliambia kuwa watajifanya waumini mwanzoni mwa siku, kwa kuhudhuria Sala ya *Subhi* pamoja na Waislamu. Hata hivyo mwisho wa siku, wangerejea kwenye dini yao ya kale ili watu wajinga waseme, “Wamerejea kwenye dini yao ya kale kwa sababu wamegundua udhaifu katika Dini ya Uislamu.” Kwa sababu hii walisema,

لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ

“Huenda wakarejea.”

Ibn Abu Najih رحمه الله تعالى alisema kuwa Mujahid aliitolea maelezo Ayah hii, ambayo inawahusu Mayahudi. “Wakihudhuria Sala ya Alfajiri pamoja na Mtume ﷺ na mwisho hawakuamini ila walifanya kazi ya kuwapotosha watu. Kwa njia hii, watu wangedhani kuwa wamegundua udhaifu katika dini ambayo waliifuata kwa muda mfupi.”² Na Kauli Yake,

وَلَا تُؤْمِنُوا إِلَّا لِمَنْ تَبِعَ دِينَكُمْ

“Wala msimuamini ila anayefuata Dini yenu”.

Maana yake: Msimuamini yeyote kuwadhihirishia siri zenu na yale mliyonayo isipokuwa kwa wale wanaofuata dini yetu, wala msiwadhihirishie Waislamu yale mnayoyajua, kisha wakayaamini na wakatumia kama ushahidi wa kukuhojini. Allah تعالى Amesema,

¹ At-Tabari 6:508.

² At-Tabari 2:508.

قُلْ إِنَّ الْهُدَىٰ هُدَىٰ اللَّهِ

“Sema: Hakika uwongofu ni uwongofu wa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Yeye Ndiye Anaiongoza mioyo ya waumini kufikia imani kamili kupitia Aya bainifu, ushahidi ulio wazi na hoja zisizopingika Alizomteremshia mja Wake na Mjumbe wake Muhammad ﷺ. Haya yatajiri, Enyi Mayahudi! Hata kama mkificha sifa bainifu za Muhammad ﷺ, Mtume asiyejua kusoma wala kuandika kinachosomwa “Ummiy” ambaye mnasoma khabari zake kwenye Vitabu vyenu hapa mlivyovipokea kutoka kwa Mitume wa mwanzo.

Kauli ya Allah تعالى،

أَنْ يُؤْتِيَ أَحَدًا مِّثْلَ مَا أُوتِيْتُمْ أَوْ يُحَاجُّوْكُمْ عِنْدَ رَبِّكُمْ

“Kuwa apewe mtu mfano wa mliopewa nyinyi au wakuhojini mbele ya Mola wenu Mlezi”.

Wanasema, “Msidhihirishie Waislamu ilimu mliyo nayo, ili wasije wakajifunza wakawa sawa nanyi. Watakuwa bora kuliko nyie kwa sababu wataamini au wataitumia dhidi yenu kama ushahidi mbele ya Mola wenu, na hivyo kujenga ushahidi wa Allah dhidi yenu hapa duniani na kesho Kiyama.”

Allah تعالى Amesema،

قُلْ إِنَّ الْفَضْلَ بِيَدِ اللَّهِ يُؤْتِيهِ مَنْ يَشَاءُ

“Sema: Hakika Fadhila zimo Mikononi mwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Mambo yote yako chini ya Udhhibiti Wake, na Anatoa na Kuchukua. Kwa hakika, Allah تعالى Anatoa Imani, Ilimu na Ufahamu mzuri kwa yeyote Amtakaye. Pia Humpotosha yeyote Amtakaye kwa Kumpofusha uoni, akili, Kuutia lakiri moyo wake, usikivu wake na Kuyafumba macho yake. Allah تعالى Ana Hikima iliyotimia na ushahidi usio na shaka.

وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٧٦﴾ يَخْتَصُّ بِرَحْمَتِهِ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٧٧﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Wasaa na Mjuzi, Yeye Humchagua Kumpa Rehema Zake Amtakaye; na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Fadhila kubwa.” (3:73-74)

Maana yake: Amewajaalia, Enyi waumini fadhila zisizo na hesabu, katika hayo Amempa heshima Mtume wenu Muhammad ﷺ juu ya Mitume wengine wote, na kwa kukuongozeni katika Shariah bora kuliko zote.

﴿ وَمِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ مَنْ إِنْ تَأْمَنَهُ بِقِنطَارٍ يُؤَدِّمَهُ إِلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَنْ إِنْ تَأْمَنَهُ بِدِينَارٍ لَا يُؤَدِّمَهُ إِلَيْكَ إِلَّا مَا دُمَّتْ عَلَيْهِ قَائِمًا ۗ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لَيْسَ عَلَيْنَا فِي الْأُمِّيَنَ سَبِيلٌ ۗ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٧٥﴾ بَلَىٰ مَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ وَاتَّقَىٰ فَإِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٧٦﴾﴾

75. Na miongoni mwa Watu wa Kitabu yupo ambaye ukimpa amana ya mrundo wa Mali atakurudishia, na miongoni mwao yupo ambaye ukimpa amana ya dinari moja hakurudishii isipokuwa ukimsimamia kumdai. Haya ni kwa kuwa wakisema: Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasiojua kusoma. Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua.

76. Sivyoy hivyo, bali anayetimiza ahadi yake na akamchamungu basi Mwenyezi Mungu Huwapenda wachamungu.

Maelezo kuhusu Tabia ya Uaminifu kwa Mayahudi

Allah تعالى Anaeleza kuwa wapo waovu miongoni mwa Mayahudi. Pia Anawaonya Waumini dhidi ya kudanganywa nao, kwani miongoni mwao,

﴿ مَنْ إِنْ تَأْمَنَهُ بِقِنطَارٍ ۗ﴾

“Yupo ambaye ukimpa amana ya mrundo wa mali”. Maana yake: Mitita ya mali, Mali nyingi sana,

﴿ يُؤَدِّمَهُ إِلَيْكَ ۗ﴾

“Atakurudishia.” Inamaanisha na kilicho chini ya *Qintar*, kwa njia iliyo bora atakurudishia.

﴿ وَمِنْهُمْ مَنْ إِنْ تَأْمَنَهُ بِدِينَارٍ لَا يُؤَدِّمَهُ إِلَيْكَ إِلَّا مَا دُمَّتْ عَلَيْهِ قَائِمًا ۗ﴾

“Na miongoni mwao yupo ambaye ukimpa amana ya dinari moja hakurudishii isipokuwa ukimsimamia kumdai.”

Maana yake: Kwa kuitaka, kushurutisha na kusisitiza kupewa mali yako ya halali. Iwapo hivi ndivyo atakavyofanya na Dinar, basi vipi ikiwa ni zaidi ya Dinar? Tulitaja maana ya *Qintar*, mwanzoni mwa Surah hii, ambapo thamani ya Dinar inafahamika. Kauli ya Allah تعالى،

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ قَالُوا لَيْسَ عَلَيْنَا فِي الْأُمِّيَّتِ سَبِيلٌ

“Haya ni kwa kuwa wakisema: Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasiojua kusoma”.

Maana yake: Kilichowafanya wakanushe ukweli nikile walichokisema, “Hapana ubaya katika dini yetu endapo tutakula mali ya ummah usiojua kuandika wala kusoma kilichoandikwa *“ummiy”* nao ni Waarabu, kwani Allah تعالى Ameturuhusu.” Allah تعالى Akajibu،

وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٦٩﴾

“Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua.”

Maana yake: Hakika wameyabuni maneno haya, na wakageukia upotofu. Kwani Allah تعالى Aliwaharamishia kula mali isipokuwa kwa haki. Na wao ni watu wazushi.

Abdur-Razzaq alinukuu kutoka kwa Sa’sa’ah bin Yazid alisema kuwa mtu alimuuliza Ibn Abbas رضي الله عنهما، “Wakati wa vita, tulikamata mali ya *Ahl Adh-Dhimmah*,¹ kama vile kuku na kondoo.” Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema، “Mnasemaje?” Akajibu، “Kwetu hatuna ubaya wowote.” Akasema، “Hivi ndivyo walivyosema Watu wa Kitabu،

قَالُوا لَيْسَ عَلَيْنَا فِي الْأُمِّيَّتِ سَبِيلٌ

“Hatuna lawama kwa ajili ya hawa wasiojua kusoma”.

Kwa hakika, wakilipa kodi *“Jizyah”* hamruhusiwi kuchukua mali yao, isipokuwa wakiitoa kwa ridhaa yao.”² Kisha Allah تعالى Amesema،

¹ Wayahudi na Wakristo wanaoishi katika himaya za Waislamu.

² Tafsir ‘Abdur-Razzaq 1:12. Isnadi yake ina dosari.

بَلَىٰ مَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِ وَاتَّقَىٰ

“Sivyo hivyo, bali anaye timiza ahadi yake na akamchamungu”.

Anayetimiza ahadi yake na akamcha Mwenyezi Mungu miongoni mwao, Enyi Watu wa Kitabu, kuhusiana na ahadi mliyoichukua kwa Allah تعالى kuwa mtamuamini Muhammad ﷺ atakapotumwa, kama Mitume wote na Mataifa walivyochukua ahadi kwa Allah تعالى. Yeyote anayejipusha na yaliyo haramishwa na Allah تعالى, anamtii na anashikamana na *shariah* Aliyompeleka nayo Mjumbe Wake wa Mwisho na bwana wa viumbe wote.

فَإِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَّقِينَ ﴿٧٧﴾

“Basi Mwenyezi Mungu Huwapenda wachamungu”.

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا أُولَٰئِكَ لَا خَلْقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ وَلَا

يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمْ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٧٧﴾

“Hakika wanaouza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao kwa thamani ndogo, hao hawatakuwa na sehemu ya kheri yoyote katika Akhera, wala Mwenyezi Mungu Hatasema nao wala hatawatazama Siku ya Kiyama, wala hatawatazama, nao watapata adhabu chungu.” (3:77)

Waliovunja Ahadi ya Allah تعالى Hawana Hisa Siku ya Kiyama

Allah تعالى Ameeleza kuwa wale walioacha kutekeleza yale waliyomuahidi Allah تعالى kwa kumfuata Muhammad ﷺ, kutangaza wasifu wake (kama ulivyo ndani ya Vitabu vyao) kwa watu na kuthibitisha ukweli wake. Na kula viapo vya uongo, viovu na vya madhambi kwa kufadhilisha thamani chache na duni, hayo ni utajiri na starehe za maisha yenye kutoweka.

أُولَٰئِكَ لَا خَلْقَ لَهُمْ فِي الْآخِرَةِ

“Hao hawatakuwa na sehemu ya kheri yoyote katika Akhera.”

وَلَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Wala Mwenyezi Mungu hatasema nao wala hatawatazama Siku ya Kiyama”.

Kwa Huruma Yake, Aya hii inaonesha kuwa Allah تعالى Hatozungumza nao kwa Huruma wala Kuwaangalia kwa Rehema,

وَلَا يُزَكِّيهِمْ

“Wala Hatawatakasa.”

Kutokana na dhambi na uchafu. Bali, Ataamrisha watupwe Motoni,

وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Nao watapata adhabu chungu.”

Kuna Hadithi nyingi juu ya mada ya Aya hii tutataja, baadhi ya Hadithi hizo:-

Hadithi ya Kwanza:

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa Abu Dharr رحمه الله تعالى alisema, “Mtume ﷺ alisema:

«ثَلَاثَةٌ لَا يَكَلِّمُهُمُ اللَّهُ. وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَلَا يُزَكِّيهِمْ، وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ»
 قلت: يا رسول الله، من هم؟ خابوا وخسروا قال: وأعادته رسول الله ﷺ ثلاث
 مرات، قال: «المُسْبِلُ، وَالْمُنْتَفِقُ سَلْعَتَهُ بِالْخَلْفِ الْكَاذِبِ، وَالْمَتَّانُ»

“Kuna watu watatu ambao Allah Hatozungumza nao, wala Hatowaangalia Siku ya Kiyama wala Kuwatakasa, na watapata adhabu iumizayo.” Nikamuuliza, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Ni nani’ hao watakaoharibikiwa na kula khasara?’ Akanijibu, akiirejea kauli hii mara tatu, “Musbil (mtu ambaye nguo yake inavuka fundo za miguu), yule anayeapa kwa uwongo ili auze bidhaa zake na anayetoa Sadaka kisha akawasimbulia watu.”¹

Ilikusanywa pia na Muslim, na wakusanyaji wa Sunan.²

Hadithi ya Pili:

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa ‘Adi bin ‘Amirah Al-Kindi رضي الله عنه alisema, “Mtu mmoja mkorofi wa huko Kindah aliyetitwa kwa jina la Imru’ Al-Qays bin ‘Abis, waligombana na mtu kutoka Hadhramaut mbele ya Mtume ﷺ kuhusu

¹ Ahmad 5:148.

² Muslim 1:102, Abu Dawud 4:346, Tuhfaat Al-Ahwadhi 4:401, An-Nasai 7:245.

kipande cha ardhi. Mtume ﷺ alimtaka Mhadhramaut awasilishe ushahidi wake lakini hakuwa nao. Mtume ﷺ alimtaka Imru' Al-Qays ale kiapo cha uaminifu, lakini Mhadhramaut alisema: 'Ewe Mjumbe wa Allah! Na iwapo unamtaka ale kiapo, kwa jina la Mola wa Ka'abah (Allah تعالى), ardhi yangu imepotea." Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ حَلَفَ عَلَى يَمِينٍ كَأَذِيَّتِهِ لِيُقْتَطَعَ بِهَا مَالٌ أَحَدٍ، لَقِيَ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ وَهُوَ عَلَيْهِ غَضَبَانُ»

"Mwenye kuapa kwa kiapo cha uongo ili kwacho apate kuchukua mali ya mtu, atakutana na Allah Akiwa Amemkasirikia".

Raja, mmoja wa wasimulizi wa Hadithi, alisema kuwa Mtume ﷺ baada ya hapo alisoma:

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا

"Hakika wanaouza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao thamani ndogo."

Imru' Al-Qays akasema "Itakuwaje endapo mmojawapo ataacha, atapata nini, Ewe Mjumbe wa Allah?" Mtume ﷺ alijibu, "Pepo." Imru' Al-Qays alisema, "Kuwa shahidi ya kuwa mimi nimeacha, ardhi yote ni yake."¹ Pia An-Nasai alinukuu Hadithi hii.²

Hadithi ya tatu:

Imam Ahmad bin Abdullah رحمه الله تعالى alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ حَلَفَ عَلَى يَمِينٍ هُوَ فِيهَا فَاجِرٌ، لِيُقْتَطَعَ بِهَا مَالٌ أَمْرِي مُسْلِمٍ، لَقِيَ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ وَهُوَ عَلَيْهِ غَضَبَانُ»

"Mwenye kuapa kwa kiapo cha uongo ili kwacho achukue mali ya Muislamu, atakutana na Allah akiwa amemkasirikia".

Al-Ash'ath alisema, "Wallahi! Aya hii iliteremshwa kwa ajili yangu. Nikimiliki Ardhi shirika na Myahudi ambaye alinipoka haki yangu, na nikamlalamikia Mtume ﷺ Mtume ﷺ aliniuliza,

¹ Ahmad 4:191.

² An-Nasai katika Al-Kubra 3:486.

“Je, una ushahidi?”. Nilimjibu, “Hapana”. Akamuambia Myahudi: “Kula kiapo”. Nikasema. “Ewe Mjumbe wa Allah! Atakula kiapo cha uongo sasa hivi, na nitapoteza mali yangu.” Allah تعالی Aliteremsha Aya hii,

إِنَّ الَّذِينَ يَشْتَرُونَ بِعَهْدِ اللَّهِ وَأَيْمَانِهِمْ ثَمَنًا قَلِيلًا

“Hakika wanaouza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao kwa thamani ndogo.”¹

Sahih Mbili zimenukuu Hadithi Hii.²

Hadithi ya Nne:

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa sahaba wa Mtume ﷺ, Abu Hurayrah عنه رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«ثَلَاثَةٌ لَا يُكَلِّمُهُمُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَلَا يَنْظُرُ إِلَيْهِمْ، وَلَا يُرَكِّبُهُمْ، وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ: رَجُلٌ مَنَعَ ابْنَ السَّبِيلِ فَضْلَ مَاءٍ عِنْدَهُ، وَرَجُلٌ حَلَفَ عَلَى سِلْعَةٍ بَعْدَ الْعَصْرِ - يَعْنِي كَاذِبًا - وَرَجُلٌ بَايَعَ إِمَامًا، فَإِنْ أَعْطَاهُ رَفَى لَهُ، وَإِنْ لَمْ يُعْطِهِ لَمْ يَفِ لَهُ»

“Watu watatu Allah Hatawasemesha siku ya kiama, wala hatawaangalia, wala hatawatakasa, na wana adhabu kali, mtu amemnyima mpita njia ziada ya maji aliyokuwa nayo, mtu ameapa kwa bidhaa baada ya alasiri, - yaani kwa uongo - na mtu aliyechukua ahadi kwa imamu, ikiwa atampa anatekeleza, na asipompa hamtekelezei”³

Abu Dawud na At-Tirmidhi,⁴ nao walinukuu Hadithi hii na At-Tirmidhi aliipa daraja la *Hasan Sahih*.

* * *

¹ Ahmad 1:379.

² Fat’hul Al-Bari 5:336, Muslim 1:122.

³ Ahmad 2:480.

⁴ Abu Dawud 3:749, Tuhfaat Al-Ahwadhi 5:218.

وَإِنَّ مِنْهُمْ لَفَرِيقًا يَلُودْنَ بِالسِّتْرِ مِنَ الْكِتَابِ لِتَحْسَبُوهُ مِنَ
 الْكِتَابِ وَمَا هُوَ مِنْ الْكِتَابِ وَيَقُولُونَ هُوَ مِنْ عِنْدِ
 اللَّهِ وَمَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُمْ
 يَعْلَمُونَ ﴿٧٨﴾ مَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُؤْتِيَهُ اللَّهُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَ
 وَالنَّبِيَّةَ ثُمَّ يَقُولَ لِلنَّاسِ كُونُوا عِبَادًا لِي مِنْ دُونِ اللَّهِ
 وَلَكِنْ كُونُوا رَبَّيْنَ بِمَا كُنْتُمْ تُعْلَمُونَ الْكِتَابَ وَبِمَا
 كُنْتُمْ تَدْرُسُونَ ﴿٧٩﴾ وَلَا يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَتَّخِذُوا اللَّاتِحَةَ
 وَالنَّبِيَّةَ أَرْبَابًا أَيُّكُمْ بِالْكَفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨٠﴾
 وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ لَمَا آتَيْتُكُمْ مِنْ كِتَابٍ
 وَحِكْمَةٍ ثُمَّ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ
 بِهِ وَلَتَنْصُرُنَّهُ قَالَ أَأَقْرَرْتُمْ وَأَخَذْتُمْ عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ إِصْرِي
 قَالُوا أَقْرَرْنَا قَالَ فَاشْهَدُوا وَأَنَا مَعَكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٨١﴾
 فَمَنْ تَوَلَّىٰ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٨٢﴾

وَإِنَّ مِنْهُمْ لَفَرِيقًا يَلُودْنَ السِّتْرَ مِنَ الْكِتَابِ لِتَحْسَبُوهُ مِنَ
 الْكِتَابِ وَمَا هُوَ مِنَ الْكِتَابِ وَيَقُولُونَ هُوَ مِنْ عِنْدِ
 اللَّهِ وَمَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُمْ
 يَعْلَمُونَ ﴿٧٨﴾ مَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُؤْتِيَهُ اللَّهُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَ
 وَالنَّبِيَّةَ ثُمَّ يَقُولَ لِلنَّاسِ كُونُوا عِبَادًا لِي مِنْ دُونِ اللَّهِ
 وَلَكِنْ كُونُوا رَبَّيْنَ بِمَا كُنْتُمْ تُعْلَمُونَ الْكِتَابَ وَبِمَا
 كُنْتُمْ تَدْرُسُونَ ﴿٧٩﴾ وَلَا يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَتَّخِذُوا اللَّاتِحَةَ
 وَالنَّبِيَّةَ أَرْبَابًا أَيُّكُمْ بِالْكَفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨٠﴾
 وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ لَمَا آتَيْتُكُمْ مِنْ كِتَابٍ
 وَحِكْمَةٍ ثُمَّ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ
 بِهِ وَلَتَنْصُرُنَّهُ قَالَ أَأَقْرَرْتُمْ وَأَخَذْتُمْ عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ إِصْرِي
 قَالُوا أَقْرَرْنَا قَالَ فَاشْهَدُوا وَأَنَا مَعَكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٨١﴾
 فَمَنْ تَوَلَّىٰ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٨٢﴾

78. "Na wapo baadhi yao wanaopindua ndimi zao katika kusoma Kitabu ili mdhanie kuwa hayo yanatoka Kitabuni, na wala hayatoki Kitabuni. Na husema: Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu. Na wala hayatoki kwa Mwenyezi Mungu. Na wanamsingizia Mwenyezi Mungu uwongo na wao wanajua".

Mayahudi Wabadilisha Maneno ya Allah تعالیٰ kwa Kupindisha Ndimi

Allah تعالیٰ Amesema kuwa baadhi ya Mayahudi, Allah تعالیٰ Awashushie laana, wanapotosha maneno ya Allah تعالیٰ, wanayabadilisha kutoka sehemu zake, na kubadilisha maana iliyokusudiwa. Wanafanya hayo ili wawaghilibu watu wasiojua kwa kuyafanya maneno yao yanatoka ndani ya Kitabu cha Allah تعالیٰ. Uongo wao wanauhusisha na Allah تعالیٰ, japokuwa wanajua kuwa wamesema uongo na wamezua uongo. Kwa hiyo, Allah تعالیٰ Amesema,

﴿٧٨﴾ وَيَقُولُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿٧٨﴾

"Na wanamsingizia Mwenyezi Mungu uwongo na wao wanajua".

Mujahid, Ash-Shabi, Al-Hasan, Qatadah na Ar-Rabi' bin Anas walisema kuwa,

يَلُونُ أَلَيْسَتْهُمْ بِأَلِكْتَابِ

“Wanaopindua ndimi zao katika kusoma Kitabu”.

Maana yake: “Wanayabadilisha (Maneno ya Allah تعالى).”¹

Bukhari alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya hii ina maana walibadilisha na wakaongeza japokuwa hapana kiumbe wa Allah تعالى Awezaye kuondoa Maneno ya Allah تعالى kutoka kwenye Vitabu Vyake, wanabadili na kupotosha maana zake za ukweli. Wahb bin Munabbih alisema, “Taurati na Injili zimebaki kama Allah تعالى Alivyoziteremsha, na hakuna herufi iliyoondolewa.”

Pamoja na hayo, watu waliwapotosha wenzi wao kwa kuongeza na kutoa tafsiri potofu, wakivitegemea vitabu walivyoviandika wenyewe. Kisha,

وَيَقُولُونَ هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَمَا هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ

“Na husema: Haya yametoka kwa Mwenyezi Mungu. Na wala hayatoki kwa Mwenyezi Mungu”.

Ama kuhusiana na Vitabu vya Allah تعالى bado vimehifadhiwa na haviwezi kubadilishwa. ‘Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kauli hii. Hata hivyo, iwapo Wahb alikuwa na maana ya vitabu ambavyo kwa sasa viko mikononi mwa Watu wa Kitabu, basi tunatakiwa kusema kuwa hapana shaka kuwa vimebadilishwa, kupotoshwa, vimeongezwa na kufutwa baadhi ya mambo. Kwa mfano, vitabu hivyo kwa lugha ya Kiarabu (hata katika lugha zingine) vina makosa makubwa mno, vimeongezwa na kufutwa mambo mengi na vina ufafanuzi mwingi usio sahihi.

Bali wale waliotafsiri vitabu hivyo wengi wao au aghlabu yao ufahamu wao si sahihi. Iwapo Wahb alikusudia Vitabu vya Allah تعالى ambavyo viko Kwake, basi kwa hakika Vitabu hivyo vimehifadhiwa na havikubadilishwa.

¹Ibn Abu Hatim 2:361.

مَا كَانَ لِبَشَرٍ أَنْ يُؤْتِيَهُ اللَّهُ الْكِتَابَ وَالْحُكْمَ وَالنُّبُوَّةَ ثُمَّ يَقُولَ لِلنَّاسِ كُونُوا عِبَادًا لِي مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَكِنْ كُونُوا رَبَّيْنَ بِمَا كُنْتُمْ تُعَلِّمُونَ الْكِتَابَ وَبِمَا كُنْتُمْ تَدْرُسُونَ ﴿٧٩﴾ وَلَا يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَتَّخِذُوا الْمَلَائِكَةَ وَالنَّبِيِّينَ أَرْبَابًا أَيَأْمُرُكُمْ بِالْكُفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨٠﴾

79. Haiwezi kuwa mtu aliyepewa na Mwenyezi Mungu Kitabu na Hikima na Unabii kisha awaambie watu: Kuweni wa kuniabudu mimi badala ya Mwenyezi Mungu. Bali atawaambia: Kuweni wenye kumuabudu Mola Mlezi wa viumbe vyote, kwa kuwa nyinyi mnafundisha Kitabu na kwa kuwa mnakisoma.

80. Wala hatakukuamrisheni kuwafanya Malaika na Manabii kuwa ni miungu. Je, Atakuamrisheni ukafiri baada ya kuwa nyinyi Waislamu?.

Hakuna Mtume Aliyewalingania Watu Kumuabudu yeye au Kumuabudu Asiyekuwa Allah تعالی:

Aya hii (3:79) ina maana, haiwi kwa mtu ambaye Allah تعالی Amempa Kitabu, ilimu ya Sharia na Utume kuwatangazia watu, "Niabuduni mimi badala ya Allah تعالی." Ikiwa na maana, pamoja na Allah تعالی. Kama hii sio haki ya Mtume au Mjumbe, basi kwa hakika, si haki ya mtu yeyote mwingine kutoa madai hayo. Ukosoaji huu unawahusu makuhani wajinga, makasisi na walimu wapotoshaji, tofauti na Manabii na wafuasi wao miongoni mwa wanazuoni walio waadilifu, kwani wanaamrisha yale waliyoamrishwa na Allah تعالی, na kama walivyofikishiwa na Mitume wao watukufu. Pia huyakataza yale yale waliyokatazwa na Allah تعالی, kwa ndimi za Mitume Wake watukufu. Mitume, amani na neema za Allah تعالی ziwe juu yao wote, wao ni mabalozi kati ya Allah تعالی na viumbe Wake, walibalighisha ujumbe wa Allah تعالی, walitoa ushauri na uadilifu kwa viumbe na walifikisha ukweli kwao. Kauli ya Allah تعالی,

﴿٧٩﴾ وَلَا يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَتَّخِذُوا الْمَلَائِكَةَ وَالنَّبِيِّينَ أَرْبَابًا أَيَأْمُرُكُمْ بِالْكُفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨٠﴾

"Bali atawaambia: Kuweni wenye kumuabudu Mola Mlezi wa viumbe vyote, kwa kuwa nyinyi mnafundisha Kitabu na kwa kuwa mnakisoma". (3:79)

Maana yake: Mtume ﷺ anawataka watu wawe *Rabbaniyyun* (wenye kuabudu). Ibn Abbas, Abu Razin na wengine wengi walisema kuwa *Rabbaniyyun* ina maana, “Wenye hikima, wanazuoni, na wastahamilivu.”¹ Adh-Dhahhak aliitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى،

بِمَا كُنْتُمْ تُعَلِّمُونَ الْكِتَابَ وَبِمَا كُنْتُمْ تَدْرُسُونَ ﴿٧٨﴾

“Kwa kuwa nyinyi mnafundisha Kitabu na kwa kuwa mnakisoma”.

(3:79)

“Yeyote anayejifunza Qur`an anastahiki kuwa *Faqih* (mwanazuoni).”

وَبِمَا كُنْتُمْ تَدْرُسُونَ ﴿٧٩﴾

“Na kwa kuwa mnakisoma.”

Wakihifadhi maneno yake. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَلَا يَأْمُرُكُمْ أَنْ تَتَّخِذُوا الْمَلَائِكَةَ وَالنَّبِيِّنَ أَوْلِيَاءَ

“Wala hatakuamrisheni kuwafanya Malaika na Manabii kuwa ni miungu”.

Mtume ﷺ hawaamrishi kumuabudu minghairi ya Allah تعالى، awe Mtume aliyetumwa au Malaika،

أَيُّكُمْ بِالْكَفْرِ بَعْدَ إِذْ أَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨٠﴾

“Je, Atakuamrisheni ukafiri baada ya kuwa nyinyi Waislamu?”.

Maana yake: Hatafanya hivyo, kwani yeyote atakayelingania kumuabudu minghairi ya Allah تعالى، atakuwa amelingania katika kufuru. Mitume huamrisha kushikamana na imani ambayo ni kumuabudu Allah تعالى Pekee bila ya mshiriki. Allah تعالى Amesema،

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنْهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٨١﴾

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mola isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu”.

(21:25)

¹ Ibn Hatim 2:365.

Na Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

“Na kwa hakika kwa kila umma Tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Mwenyezi Mungu, na muepukeni Shetani.” (16:36)

وَسَأَلْنَا مَنْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رُسُلِنَا أَجَعَلْنَا مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ إِلَهًا يُعْبَدُونَ ﴿٤٣﴾

“Na waulize Mitume wetu Tuliowatuma kabla yako: Je! Tulifanya miola mingine iabudiwe badala ya Rahmani?”. (43:45)

Allah تعالى Alieleza kuhusu Malaika,

﴿٢١﴾ وَمَنْ يَقُلْ مِنْهُمْ إِنِّي إِلَهٌ مِنْ دُونِهِ فَذَلِكَ نَجْزِيهِ جَهَنَّمَ كَذَلِكَ نَجْزِي الظَّالِمِينَ ﴿٢٢﴾

“Na yeyote kati yao atakayesema: Mimi ni mungu, badala Yake, basi huyo Tutamlipa malipo yake Jahannamu. Hivyo ndivyo Tuwalipavyo wenye kudhulumu”. (21:29)

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ لَمَا آتَيْنَاكُمْ مِنْ كِتَابٍ وَحِكْمَةٍ ثُمَّ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَكُمْ لَتَتُؤْمِنُنَّ بِهِ وَلَتَنْصُرُنَّهُ ۚ قَالَ أَأَقْرَضْتُمْ وَأَخَذْتُمْ عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ إِصْرِي ۗ

قَالُوا أَأَقْرَضْنَا ۚ قَالَ فَآشْهَدُوا وَأَنَا مَعَكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٢٣﴾ فَمَنْ تَوَلَّىٰ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٢٤﴾

81. Na pale Mwenyezi Mungu alipochukua ahadi kwa Manabii: Nikishakupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo Langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia.

82. Watakaogeuka baada ya haya basi hao ndio wapotovu.

Ahadi iliyochukuliwa kwa Mitume ya Kumuamini Mtume Wetu, Muhammad ﷺ:

Allh تعالى Anaeleza kuwa Alichukua ahadi kutoka kwa kila Mtume Aliyemtuma kuanzia Adam عليه السلام mpaka Isa عليه السلام, na Allah تعالى Anapompa Mtume Kitabu na Hikmah, hivyo kupata daraja za juu anazostahiki, kisha akaja Mtume baada yake, basi amuamini na amuunge mkono. Japokuwa Allah تعالى Amewapa Mitume ilimu na utume, ukweli huu usiwafanye wao kuepuka kumfuata na kumuunga mkono Mtume ajaye baada yao. Kwa sababu hii Allah تعالى, Aliye juu kabisa, Mtukufu Zaidi, Alisema,

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ النَّبِيِّينَ لَمَا آتَيْتُكُمْ مِنْ كِتَابٍ وَحِكْمَةٍ

“Na pale Mwenyezi Mungu Alipochukua ahadi kwa Manabii: Nikishakupeni Kitabu na hikima”.

Maana yake: Ikiwa Nitakupeni Kitabu na Hikmah,

ثُمَّ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مُصَدِّقٌ لِمَا مَعَكُمْ لَتُؤْمِنُنَّ بِهِ وَلَتَنْصُرُنَّهُ قَالَ أَأَقْرَرْتُمْ وَأَخَذْتُمْ عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ إِصْرِي

“Kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyonyo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika Agizo Langu juu ya hayo? ”.

Ibn Abbas, Mujahid, Ar-Rabi, Qatadah na As-Suddi رضي الله عنهم walisema,

إِصْرِي

“...Agizo Langu...”

Maana yake: ‘Ahadi Yangu.’¹

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema, “Maana ya *Isri* ni ‘Ahadi Yangu, nzito mlioichukua,’ Maana:² ‘kiaga Changu ni chenye nguvu na cha uhakika.’”

¹ Ibn Abi Hatim 2:373, 374.

² Ibn Abi Hatim 2:273.

قَالُوا أَقْرَبْنَا قَالَ فَأَشْهَدُوا وَأَنَا مَعَكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٧٨﴾ فَمَنْ تَوَلَّى بَعْدَ ذَلِكَ

“Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia, Watakaogeuka baada ya haya”.

Maana yake: atakayekwenda kinyume na kutekeleza ahadi hii na makubaliano haya:

فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿٧٩﴾

“Basi hao ndio wapotovu”.

Ali bin Abu Talib رضي الله عنه na binamu yake Abdullah bin Abbas رضي الله عنهما walisema, “Allah تعالى Hakumtuma Mtume bila kuchukua ahadi kwake kuwa kama Muhammad ﷺ atatumwa katika uhai wake, angemuamini na kumuunga mkono.”¹ Na alimuamuru kila Mtume kuchukua ahadi kutoka kwa watu wake kuwa iwapo Muhammad atatumwa katika zama zao, watamuamini na kumuunga mkono. Tawus, Al-Hassan Al-Basri na Qatadah walisema, “Allah تعالى Alichukua ahadi kutoka kwa Mitume kuwa wataaminiana.” Na kauli hii haipingani na yale waliyoyasema Ali na Ibn Abbas رضي الله عنهما.

Kwa hiyo, Muhammad ﷺ ni Mtume wa mwisho mpaka siku ya kiyama. Yeye ni Imamu mkuu, ambaye endapo angeliishi katika kipindi chochote angelistahiki kutiiwa, zaidi ya Mitume wengine wote. Hii ndio sababu Muhammad ﷺ aliwaswalisha Mitume wote usiku wa Isra walipokusanyika Bayt Al-Maqdis - Ardhi Takatifu (Jerusalem).

Atawaombea watu siku ya Kiyama, Mwenyezi Mungu Mola Mlezi Atakapowahukumu waja wake. Katika Al-Maqaam Al-Mahmuud (kituo kilichosifiwa) (Rejea 17:79) kuwa Muhammad ﷺ pekee ndiye anayestahiki, jukumu ambalo Mitume na Manabii watukufu zaidi (Ulul`azm) hawatalibeba jukumu hilo. Hata hivyo, Muhammd ﷺ atachukua jukumu la kuwaombea, rehemana amani za Allah تعالى zimshukie.

* * *

¹ At-Tabari 6:555.

أَفْغَيْرَ دِينِ اللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ
 وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾ قُلْ
 ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ عَلَيْنَا وَمَا أُنزِلَ عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ
 وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ وَعِيسَىٰ
 وَالنَّبِيُّونَ مِنْ رَبِّهِمْ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْهُمْ وَنَحْنُ لَهُ
 مُسْلِمُونَ ﴿٨٤﴾ وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ
 وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٨٥﴾ كَيْفَ يَهْدِي اللَّهُ قَوْمًا
 كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَانِهِمْ وَشَهِدُوا أَنَّ الرُّسُولَ حَقٌّ وَجَاءَهُمْ
 الْبَيِّنَاتُ ۗ وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٨٦﴾ أُولَٰئِكَ
 جَزَاؤُهُمْ أَنَّ عَلَيْهِمْ لَعْنَةَ اللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ
 ﴿٨٧﴾ خَالِدِينَ فِيهَا لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ
 يُنظَرُونَ ﴿٨٨﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ
 اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٨٩﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَانِهِمْ ثُمَّ
 أَزْدَادُوا كُفْرًا لَنْ نُقْبَلَ تَوْبَتَهُمْ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الضَّالُّونَ ﴿٩٠﴾
 إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارٌ فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِمْ
 مِلَّةٌ مِنَ الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَوْ اقْتَدَىٰ بِهِ ۗ أُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ
 أَلِيمٌ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ ﴿٩١﴾

أَفْغَيْرَ دِينِ اللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُ أَسْلَمَ
 مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا
 وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾
 قُلْ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ عَلَيْنَا وَمَا
 أُنزِلَ عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ
 وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَمَا
 أُوتِيَ مُوسَىٰ وَعِيسَىٰ وَالنَّبِيُّونَ مِنْ
 رَبِّهِمْ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْهُمْ وَنَحْنُ
 لَهُمْ مُسْلِمُونَ ﴿٨٤﴾ وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ
 الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي
 الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿٨٥﴾

83. Je, wanataka dini isiyo kuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumtii Yeye kikipenda kisipende, na kwake Yeye watarejeshwa?

84. Sema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu, na tuliyo teremshiwa sisi, na aliyo teremshiwa Ibrahim, na

Ismail, na Is-haak na Yaakub na wajukuu zao, na aliyopewa Musa na Isa na Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi. Hatubagui baina yao hata mmoja, na sisi ni wenye kusilimu Kwake.

**85. Na anayetafuta dini isiyokuwa Uislamu haitakubaliwa kwake.
Naye Akhera atakuwa katika wenye kupata hasara.**

Dini ya Kweli Mbele ya Allah تعالی ni Uislamu na Haitakubaliwa Dini Nyingine;
Allah تعالی Amewakanusha wale wanaokhitari dini nyingine isiyokuwa Dini ambayo imekuja na Vitabu Vyake na Mitume, Dini ambayo ni ya kumuabudu Allah تعالی Pekee bila ya Kumshirikisha. Ambaye,

وَلَهُدَّ أَشْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Kwake kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu”. (8:83)

Neno ‘Kikipenda Kisipende’. Ni sawa na Kauli ya Allah تعالی katika Aya nyingine,

وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا

“Na viliomo mbinguni na katika ardhi vinamsujudia Mwenyezi Mungu tu vikitaka visitake”. (13:15)

Kauli Yake Allah تعالی,

أُولَئِكَ يَرَوْنَ إِلَىٰ مَا خَلَقَ اللَّهُ مِنْ شَيْءٍ يَتَفَتَّحُونَ ظُلُمَاتٍ عَنِ الْيَمِينِ وَالشَّمَائِلِ سُجَّدًا لِلَّهِ وَهُمْ

دَاخِرُونَ ﴿١٥﴾ وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ مِنْ دَابَّةٍ وَالْمَلَائِكَةِ وَهُمْ لَا

يَسْتَكْبِرُونَ ﴿١٦﴾ خَافُونَ رَبَّهُمْ مِنْ فَوْقِهِمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ﴿١٧﴾

“Je! Hawavioni vitu Alivyoviumba Mwenyezi Mungu - vivuli vyao vinachomoza kushotoni na kuliani, kumsujudia Mwenyezi Mungu na vikinyenyekea?, Na vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi, tangu wanyama mpaka Malaika, vinamsujudia Mwenyezi Mungu, na wala havitakabari. Vinamkhofu Mola wao Mlezi aliye juu yao, na vinafanya vinavyo amrishwa.” (16:48-50)

Kwa hiyo, muumini mtiifu anajisalimisha kwa Allah تعالی kwa moyo na mwili wake ambapo makafiri wanajilazimisha kujisalimisha Kwake kwa mwili tu, kwa kuwa yuko chini ya Nguvu za Allah تعالی, na Udhhibiti usiozuilika, na Utawala wenye nguvu ambao hauwezi kudhibitiwa au kuasiwa. Waki' alisimulia kutoka kwa Mujahid alisema maana ya Aya,

وَلَهُ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا

“Na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumtii Yeye kikipenda kisipende”. Ni sawa na Aya,

وَلَيْنَ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

“Na ukiwauliza: Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi. Bila ya shaka watasema: Mwenyezi Mungu.” (39:38)

Pia Ibn Abbas رضي الله عنهما alizungumzia kuhusu Aya,

وَلَهُ أَسْلَمَ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا

“Na hali kila kilichomo mbinguni na katika ardhi kimesilimu kwa kumtii Yeye kikipenda kisipende.” (3:83)

Kwamba ni, “Alipochukua ahadi kutoka kwao.”¹

وَالْيَهُ يُرْجَعُونَ

“Na Kwake Yeye watarejeshwa?”. Watarejeshwa Siku ya Kiyama, ambapo Atawalipa au Kuwaadhibu kila mmoja kwa mujibu wa amali zake. Kisha Allah تعالى Alisema:

قُلْ ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ عَلَيْنَا

“Sema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu, na tuliyoteremshiwa sisi”.

Maana yake: Qur’an,

وَمَا أُنزِلَ عَلَيْنَا مِنْ آيَاتٍ مِنْ رَبِّنَا إِلَّا نَسْتَعِيبُ الْوَعْدَ الَّذِي نُسَبِّحُ بِحَمْدِ رَبِّنَا وَنُؤْمِنُ بِهِ وَنَعْلَمُ أَنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ عَلِيمٌ

“Na aliyoteremshiwa Ibrahim, na Ismail, na Is-haak na Yaakub”.

Maana yake: Vitabu na Wahyi,

وَأَلْسِنَاتٍ

“Na wajukuu zao.” Asbat ni koo na matumbo kumi na mawili yaliyotokana na Watoto kumi na wawili wa Israil ambaye ni Ya’qub عليه السلام.

وَمَا أُوتِيَ مُوسَىٰ وَعِيسَىٰ

“Na aliyopewa Musa na Isa.” Maana yake: Taurati na Injili.

¹ At-Tabari 6:565.

وَالنَّبِيِّينَ مِنْ رَبِّهِمْ

“Na Manabii wengine kutoka kwa Mola wao Mlezi.”

Na hii inawaenea Mitume wote wa Allah تعالى.

لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْهُمْ

“Hatubagui baina yao hata mmoja.”

Maana yake: Bali tunawaamini wote.

وَنَحْنُ لَهُ مُسْلِمُونَ ﴿٨٤﴾

“Na sisi ni wenye kusilimu.” Waumini wa Umma huu humuamini kila Nabii aliyetumwa, kila Kitabu kilichoteremshwa, hawakanushi chochote katika hivyo. Bali huamini kila kilichoteremshwa kutoka kwa Allah تعالى, na kila Mtume aliyemtuma. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ

“Na anayefuata dini isiyokuwa Uislamu haitokubaliwa kwake.”

Maana yake: Yeyote atakayefuata mfumo wa maisha tofauti na Aliouwekea sharia abadan hatokubaliwa kwake.

وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

“Na Akhera atakuwa mwenye kupata hasara.”

Kama Mtume ﷺ alivyosema katika Hadithi iliyo sahihi.

«مَنْ عَمِلَ عَمَلًا لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا، فَهُوَ رَدٌّ»

“Mwenye kufanya amali isio juu yake jambo letu, basi hiyo itarudishwa.”¹

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Hasan alisema: ‘Abu Hurayrah رضي الله عنه alitueleza wakati tukiwa Madinah wakati huo, kuwa Mtume ﷺ alisema:

“Siku ya kiama amali zitakuja, Sala itakuja, itasema: ‘Ewe Mola wangu Mlezi! Mimi ndiye Sala.’ Hivyo Atasema: ‘Hakika wewe upo

¹ Fat’hul Al-Bari 5:355.

katika kheri." Kisha Saumu nayo itakuja na kusema: 'Ewe Mola wangu Mlezi! Mimi ndio Saumu.' Allah تعالى Atasema: 'Hakika upo katika kheri.' Kisha amali nazo zitakuja, na kila moja itasema kwa Allah تعالى, na Allah تعالى Atasema kuziambia, 'Mpo katika kheri." Kisha Uislamu utakuja kusema, 'Ewe Mola wangu Mlezi! Wewe Ndiye "Assalam" Mwenye Amani, na mimi ni "Uislamu". Hivyo Allah تعالى Atasema, 'Hakika wewe upo katika kheri. Kupitia wewe leo hii Nitachukua na Kutoa." Hadithi hii ameipokea Imamu Ahmad peke yake.¹

Allah تعالى Amesema katika Kitabu Chake,

وَمَنْ يَبْتَغِ غَيْرَ الْإِسْلَامِ دِينًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَسِرِينَ

"Na anayefuata dini isiyokuwa Uislamu haitokubaliwa kwake, Na Akhera atakuwa mwenye kupata hasara." Kauli ya Allah تعالى,

كَيْفَ يَهْدِي اللَّهُ قَوْمًا كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَانِهِمْ وَشَاهَدُوا أَنَّ الرَّسُولَ حَقٌّ وَجَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ

وَأَنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ ﴿٨٦﴾ أُولَئِكَ جَزَاءُهُمْ أَنْ عَلَيْهِمْ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ

وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ ﴿٨٧﴾ خَالِدِينَ فِيهَا لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ الْعَذَابُ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٨٨﴾ إِلَّا

الَّذِينَ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٨٩﴾

86. Mwenyezi Mungu Atawaongozaje watu waliokufuru baada ya kuamini kwao, na wakashuhudia ya kuwa Mtume huyu ni wa haki, na zikawafikia hoja zilizo wazi? Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu madhaalimu.

87. Hao malipo yao ni kuwa ipo juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote.

88. Humo watadumu. Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa nafasi.

89. Isipokuwa wale waliotubu baada ya hayo na wakatengenea; kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.

¹ Ahmad 2:362. Isnadi yake ni dhaifu. "Taqrib At-Tahdhib" 2:177.

Allah تعالی Hawaongozi Watu waliokufuru Baada ya Kuamini, Isipokuwa Wakitubia

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alipokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Alikuwapo mtu mmoja katika Ansar ambaye alisilimu, halafu akaritadi na akajiunga na Washirikina. Baadaye alijuta na aliwatuma watu, 'Muulizenu Mtume ﷺ iwapo ninaruhusiwa kutubia?' Ikateremshwa Aya,

كَيْفَ يَهْدِي اللَّهُ قَوْمًا كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَانِهِمْ

"Mwenyezi Mungu Atawaongoaje watu waliokufuru baada ya kuamini kwao". Mpaka,

فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ

"Kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu".

Watu wake wakampelekea khabari na akarejea kwenye Uislamu."¹

Masimulizi haya ndivyo pia yalivyoelezwa na An-Nasai, Al-Hakim na Ibn Hibban.² Hakim alisema, "Isnadi yake ni Sahih na hawakuiandika."

Kauli ya Allah تعالی,

كَيْفَ يَهْدِي اللَّهُ قَوْمًا كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَانِهِمْ وَشَهِدُوا أَنَّ الرَّسُولَ حَقٌّ وَجَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ

"Mwenyezi Mungu Atawaongoaje watu waliokufuru baada ya kuamini kwao, na wakashuhudia ya kuwa Mtume huyu ni wa haki, na zikawafikia hoja zilizo wazi?".

Maana yake: Uthibitisho na ushahidi uliwekwa, ukithibitisha ukweli wa lile alilopelekwa nalo Mtume ﷺ. Ukweli ulielezwa kwao, lakini wakarejea kwenye kiza na ushirikina. Kwa hiyo, watu watapataje uongofu baada ya wao kujitosa kwenye upofu?, Kwa sababu hii Allah تعالی Amesema,

وَاللَّهُ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الظَّالِمِينَ

"Mwenyezi Mungu Hawaongoi watu madhaalimu".

Kisha Akasema,

¹ At-Tabari 6:572.

² An-Nasai katika Al-Kubra 6:311, Al-Hakim 4:366, Ibn Hibban 6:323.

﴿٨٧﴾ **أُولَئِكَ جَزَاؤُهُمْ أَنْ عَلَيْهِمْ لَعْنَةُ اللَّهِ وَالْمَلَتِيكَةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ**

“Hao malipo yao ni kuwa ipo juu yao laana ya Mwenyezi Mungu na ya Malaika na ya watu wote”.

Allah تعالى Anawalaani na viumbe Vyake pia vinawalaani,

خَالِدِينَ فِيهَا

“Humo watadumu.” Katika laana,

﴿٨٨﴾ **لَا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ الْعَذَابَ وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ**

“Hawatapunguziwa adhabu wala hawatapewa nafasi.”

Kwani, adhabu haitapunguzwa hata kwa saa moja. Baada ya hapo, Allah تعالى Amesema,

﴿٨٩﴾ **إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ وَأَصْلَحُوا فَإِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَحِيمٌ**

“Isipokuwa wale waliotubu baada ya hayo na wakatengenea; kwani Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu”.

Ayah hii inaonesha kuwa Allah تعالى ni Mwema, Mwenye Kubariki, Mwenye Huruma, Mwenye Rehema na Anawapendelea viumbe Wake wanapoomba toba Kwake, kwani Huwasamehe katika hali hii,

﴿٩٠﴾ **إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَانِهِمْ ثُمَّ أَزْدَادُوا كُفْرًا لَنْ تُقْبَلَ تَوْبَتُهُمْ وَأُولَئِكَ هُمُ الضَّالُّونَ**

﴿٩١﴾ **إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِمْ مِلَّةٌ مِنَ الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَوْ**

﴿٩٢﴾ **أَفْتَدَى بِمِثْلِ أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ**

90. Hakika wale waliokufuru baada ya kuamini kwao, kisha wakazidi kukufuru, toba yao haitakubaliwa, na hao ndio walio potea.

91. Hakika wale waliokufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangeliitoa. Hao watapata adhabu chungu, wala hawatakuwa na wa kuwanusuru.

Toba ya Kafiri wakati wa Kufa Haikubaliwi wala Fidia Yake Haitakubaliwa Siku ya Kiyama

Allah تعالى Anawakhofisha na kuwaonya wanaorejea kwenye ukafiri baada ya kuwa wameamini na baadaye wakakufuru mpaka wakafa. Anaelezea kuwa katika hali hii, hapana toba itakayokubaliwa wakati wa kifo chao. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ حَتَّىٰ إِذَا حَضَرَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ

“Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yakamfikia mmoja wao mauti”. (4:18)

Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema hapa,

لَنْ تُقْبَلَ تَوْبَتُهُمْ وَأُولَٰئِكَ هُمُ الضَّالُّونَ ﴿١٨﴾

“Toba yao haitakubaliwa, na hao ndio waliopotea”.

Kwa kuwa wameacha njia ya kweli kwa ajili ya kufuata njia ya uovu.

Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bazzar رحمه الله تعالى alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema: ‘kuna watu walisilimu kisha wakarejea kwenye ukafiri kisha wakawa Waislamu tena, kisha wakaacha Uislam. Waliwatuma watu wao kuulizia hukumu ya khabari hizi na wao wakamuuliza Mtume ﷺ. Kwa ajili hiyo Aya hii iliteremka,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بَعْدَ إِيمَانِهِمْ ثُمَّ أَزْدَادُوا كُفْرًا لَنْ تُقْبَلَ تَوْبَتُهُمْ

“Hakika wale walio kufuru baada ya kuamini kwao, kisha wakazidi kukufuru, toba yao haitakubaliwa.”¹

Baadaye Allah تعالى Alisema,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِمْ مِلَّةٌ مِنَ الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَوْ

أَفْتَدَىٰ بِهَا

“Hakika wale waliokufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangeliitoa”.

¹ Ad-Dur Al-Manthur 2:258 Isnadi yake ni nzuri.

Wale wanaokufa katika ukafiri abadani, hazitakubaliwa amali zao njema, hata kama watatoa ardhi iliyojaa dhahabu ambayo itachukuliwa, kama kitendo cha utiifu. Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu Abdullah bin Jud'an, ambaye alikuwa akiwakirimu wageni, akiwasaidia wenye madeni na akiwapa chakula masikini; Je, yote yatamnufaishaje?, Mtume ﷺ alisema,

«لَا، إِنَّهُ لَمْ يَقُلْ يَوْمًا مِنَ الدَّهْرِ: رَبِّ اغْفِرْ لِي خَطِيئَتِي يَوْمَ الدِّينِ»

*"La, kwani yeye hajasema hata siku moja katika dahari: Ewe Mola wangu nisamehe makosa yangu siku ya kiama."*¹

Vivyo hivyo, kama makafiri wangetoa ardhi iliyojaa dhahabu kama fidia haingekubaliwa kutoa kwao huko. Allah تعالى Amesema,

وَلَا يُقْبَلُ مِنْهَا عَدْلٌ وَلَا تَنْفَعُهَا شَفْعَةٌ

"Wala hakitakubaliwa kwake kikomboleo, wala maombezi hayatamfaa." (2:123) Na Amesema:

لَا يَبِيعُ فِيهِ وَلَا خِلَالٌ ﴿٣١﴾

"Isiyo kuwa na biashara wala urafiki". (14:31) Na Amesema tena,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ أَنَّ لَهُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مِثْلَ مَعْدِنِ مَعْدِنِ لِيَفْتَدُوا بِهِ مِنْ

عَذَابِ يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَا تُقْبَلُ مِنْهُمْ وَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٣٦﴾

"Hakika waliokufuru lau wangukuwa na yote yaliyomo duniani, na mengine kama hayo, ili watoe fidia ya kuepukana na adhabu ya Siku ya Kiyama, yasingelipokelewa kwao; na watapata adhabu chungu." (5:36).

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema hapa,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَمَاتُوا وَهُمْ كُفَّارًا فَلَنْ يُقْبَلَ مِنْ أَحَدِهِمْ مِلَّةُ الْأَرْضِ ذَهَبًا وَلَا

أَفْتَدَى بِهِ

"Hakika wale waliokufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wanguiitoa." (3:91)

¹Muslim 1:196.

Muradi wa Aya hii ni kuwa makafiri hawataweza kuepa adhabu ya Allah تعالى, hata kama watajifidia kwa kutoa dhahabu iliyojaa ardhi, zenye uzito wa milima yake yote, vilima, mchanga, udongo, mabonde, misitu, ardhi kavu na bahari.

Imam Ahmad رضي الله عنه alinukuu kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يُؤْتَى بِالرَّجُلِ مِنْ أَهْلِ الْجَنَّةِ فَيَقُولُ لَهُ: يَا ابْنَ آدَمَ، كَيْفَ وَجَدْتَ مَنْزِلَكَ؟ فَيَقُولُ: أَيْ رَبِّ خَيْرٍ مَنْزِلٍ، فَيَقُولُ: سَلْ وَتَمَنَّ، فَيَقُولُ: مَا أَسْأَلُ وَلَا أَتَمَنَّى إِلَّا أَنْ تَرُدَّنِي إِلَى الدُّنْيَا فَأَقْتَلَ فِي سَبِيلِكَ عَشْرَ مِرَارٍ، لِمَا بَرَى مِنْ فَضْلِ الشَّهَادَةِ، وَيُؤْتَى بِالرَّجُلِ مِنْ أَهْلِ النَّارِ فَيَقُولُ لَهُ: يَا ابْنَ آدَمَ، كَيْفَ وَجَدْتَ مَنْزِلَكَ؟ فَيَقُولُ: يَا رَبِّ شَرٌّ مَنْزِلٍ، فَيَقُولُ لَهُ: تَفْتِدِي مِنِّي بِطِلَاعِ الْأَرْضِ ذَهَبًا؟ فَيَقُولُ: أَيْ رَبِّ نَعَمْ، فَيَقُولُ: كَذَبْتَ، فَذُ سَأَلْتُكَ أَقَلَّ مِنْ ذَلِكَ وَأَبْسَرَ فَلَمْ تَفْعَلْ، فَيَرُدُّ إِلَى النَّارِ»

“Mtu miongoni mwa watu wa Peponi ataletwa mbele ya Allah تعالى na ataulizwa, “Ewe mwana wa Adam! Umeyakutaje makazi yako?” Atasema, “Ewe Mola wangu, ni makazi bora kabisa.” Allah تعالى Atamuambia, “Omba unachotamani.” Mtu yule atasema, “Miye siombi wala sitamani isipokuwa nirejeshe duniani ili nipate kuuawa mara kumi katika njia Yako hiyo, kwa sababu ya fadhila ya kufa shahidi.” Na mtu miongoni mwa watu wa Motoni ataletwa mbele ya Allah تعالى Atamuambia, “Ewe mwana wa Adam! Umeyakutaje makazi yako?” Atasema, “Ni makazi mabaya kabisa, Ewe Mola.” Allah تعالى Atamuuliza, ‘Je utajitolea fidia Kwangu kwa kuijaza ardhi yote kwa dhahabu?’ Atajibu, “Ndiyo, Ewe Mola.” Allah تعالى Atamuambia, “Umesema urongo. Nilikutaka ufanye dogo na jepesi kuliko hayo, hukufanya.” Kisha atarejeshwa Motoni.”¹

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

﴿أُولَئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ وَمَا لَهُمْ مِنْ نَاصِرِينَ﴾

“Hao watapata adhabu chungu, wala hawatakuwa na wa kuwanusuru”.

Kwani hatokuwepo atakayewaokoa kutokana na Adhabu ya Allah تعالى au kuwaokoa kutokana na Adhabu Yake iumizayo sana.

¹ Ahmad 3:207.

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ ۚ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٩٢﴾ * كُلُّ الطَّعَامِ كَانَ حَلَالًا لِيَبْنَى إِسْرَائِيلَ إِلَّا مَا حَرَّمَ إِسْرَائِيلُ عَلَى نَفْسِهِ مِنْ قَبْلِ أَنْ تُنَزَّلَ التَّوْرَةُ ۗ قُلْ فَأْتُوا بِالتَّوْرَةِ فَاتْلُوهَا إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٩٣﴾ فَمَنْ أَفْتَرَى عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٩٤﴾ قُلْ صَدَقَ اللَّهُ ۗ فَاتَّبِعُوا مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٩٥﴾ إِنْ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِلْعَالَمِينَ ﴿٩٦﴾ فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ مَقَامُ إِبْرَاهِيمَ ۗ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ ءَامِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا ۗ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٩٧﴾ قُلْ يَتَاهَلُ الْكِتَابِ لِمَ تَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَاللَّهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَا تَعْمَلُونَ ﴿٩٨﴾ قُلْ يَتَاهَلُ الْكِتَابِ لِمَ تَصُدُّونَ عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ مَنْ ءَامَنَ تَبَغُّوهَا عِوَجًا وَأَنْتُمْ شُهَدَاءُ ۗ وَمَا اللَّهُ بِغَفِيلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٩٩﴾ يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذْ تُطِيعُوا فَرِيقًا مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ يَرُدُّوكُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ كُفْرِينَ ﴿١٠٠﴾

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ ۚ وَمَا تُنْفِقُوا مِنْ شَيْءٍ فَإِنَّ اللَّهَ بِهِ عَلِيمٌ ﴿٩٢﴾

92. "Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda. Na kitu chochote mnachokitao basi hakika Mwenyezi Mungu Anakijua."

Wema 'Birr' ni Mtu Kutoa Mali Yake Iliyo Bora:

Katika Tafsir yake, Waki' aliandika kuwa Amri bin Maymun alisema kuwa,

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ

"Kabisa hamtafikia wema".

Maana yake: Ni kuipata Pepo.¹

Imam Ahmad alisimulia kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa, "Abu Talha alikuwa na mali nyingi kuliko yeyote miongoni mwa Ansar

waliokuwepo Madinah, na alikuwa akiipenda sana kuliko mali nyingine miongoni mwa mali zake, bustani ya Bairuha, ambayo ilikuwa mbele ya Msikiti wa Mtume ﷺ. Kuna wakati Mtume ﷺ alikuwa akienda kwenye bustani ile na kunywa maji yake safi." Anas رضي الله عنه ameongeza, Aya hii iliposhuka,

¹ At - Tabari 6:587. Isnadi yake ina dosari.

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ

“Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda”.

Abu Talha alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Allah تعالى Anasema,

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ

“Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda”.

Hapana shaka bustani ya Bairuha ni mali niipendayo kuliko mali zangu zote, hivyo nataka kuitoa sadaka katika Njia ya Allah تعالى, na nataraji malipo yake na fidia kutoka kwa Allah تعالى. Ewe Mjumbe wa Allah! Itumie pale ambapo Allah تعالى amekuelekeza panafaa.” Kwa hilo, Mtume ﷺ alisema

«بَيْعَ نَيْحٍ، ذَاكَ مَالٌ رَابِعٌ، ذَاكَ مَالٌ رَابِعٌ، وَقَدْ سَمِعْتُ، وَأَنَا أَرَى أَنْ تَجْعَلَهَا فِي الْأَقْرَبِينَ»

“Umefanya vizuri! Umefanya vizuri! Ni mali yenye faida, ni mali yenye faida. Nimesikia uliyoyasema, na mimi naona itakuwa vema uwape ndugu na jamaa zako.”

Abu Talha alisema, ‘Nitafanya hivyo, Ewe Mjumbe wa Allah.’ Abu Talha aliigawa bustani miongoni mwa jamaa zake na binamu zake.”¹

Hadithi hii ilinukuliwa katika Sahih Mbili.² Pia walinukuu kuwa Umar رضي الله عنه alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Sijawahi kumiliki mali bora zaidi kuliko hisa yangu niliyoipata Khaybar. Kwa hiyo, unaniamuru niifanyie nini mali hiyo?” Mtume ﷺ alimjibu,

«حَبْسِ الْأَضَلِّ وَسَبْلِ الثَّمَرَةِ»

“Baki na rasilimali na matunda yake yatoe katika njia ya Allah.”³

¹ Ahmad 3:141.

² Fat’hul Al-Bari 8:71, na Muslim 2:663.

³ Muslim 3:1256 na An-Nasai 6:232.

* كُلُّ الطَّعَامِ كَانَ حِلالًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ إِلَّا مَا حَرَّمَ إِسْرَائِيلُ عَلَى نَفْسِهِ مِنْ قَبْلِ أَنْ
 تُنزَلَ التَّوْرَةُ ۗ قُلْ فَأْتُوا بِالتَّوْرَةِ فَاتْلُوهَا إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿٩٣﴾ فَمَنْ أَفْتَرَى عَلَى اللَّهِ
 الْكَذِبَ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٩٤﴾ قُلْ صَدَقَ اللَّهُ ۗ فَاتَّبِعُوا مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ
 حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٩٥﴾

93. Kila chakula kilikuwa halali kwa Wana wa Israili isipokuwa alichojizulia Israili mwenyewe kabla haijateremshwa Taurati. Sema: Leteni Taurati muisome ikiwa nyinyi ni wasema kweli.

94. Na wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu baada ya hayo, basi hao ndio madhalimu.

95. Sema: Mwenyezi Mungu Amesema kweli. Basi fuateni mila ya Ibrahim mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.

Maswali ya Mayahudi Waliyomuuliza Mtume Wetu ﷺ:

Imam Ahmad alipokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Kundi la Mayahudi lilikuja kwa Mtume ﷺ likasema, "Tueleze baadhi ya mambo ambayo hayajui isipokuwa Nabii tu." Akasema: "Niulizeni kuhusu chochote mkitakacho. Hata hivyo, chukueni ahadi kwa Allah, sawa na ahadi aliyoichukua Ya`qub kutoka kwa Wanawe, kuwa endapo nitakuelezeni jambo na mkabaini kuwa ni kweli, mtanifuata kwenye Uislamu." Wakasema, 'Tumekubali'. Mtume ﷺ akasema: "Niulizeni mnachotaka." Wakamuambia, "Tueleze juu ya mambo manne:-

- (1). Israil alijiharamishia aina gani ya vyakula?
- (2). Inakuwaje kutoka manii kwa mwanamke na mwanaume, na kila mmoja anachangiaje kuzaliwa mtoto wa kiume au wa kike?
- (3). Tueleze hali ya Mtume asiyejua kusoma wala kuandika kikasomwa "Ummi" anapokuwa usingizini?
- (4). Na nani Wali (mlinzi) wake miongoni mwa Malaika?"

Mtume ﷺ akachukua ahadi yao kuwa watamfuata akijibu maswali haya, na akanena: "Nakuulizeni kwa Jina la Yule Aliyemteremshia Musa Taurati! Je mnajua kuwa Israil aliugua maradhi makali? Maradhi yake yalipoendelea,

aliweka nadhiri kwa Allah kuwa kama Akimponya, atajiharamishia kinywaji na chakula alichokipenda zaidi. Chakula alichokuwa akikipenda sana ni nyama ya ngamia na kinywaji ni maziwa yake?" Wakasema, "Ndiyo, Wallahi!" Mtume ﷺ akasema, "Ewe Allah, kuwa shahidi dhidi yao." Kisha Mtume ﷺ akaendelea, "Nakuambieni kwa Jina la Allah تعالی, Ambaye hapana Mola Mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Yeye. Ambaye Alimteremshia Musa Taurati, hamjui kuwa manii ya mwanaume ni mazito na meupe na (mayai) ya mwanamke ni ya njano na mepesi? Iwapo moja ya majimaji yatakuwa yenye kutawala, mtoto atachukua jinsia na sura kwa uwezo wa Allah تعالی. Hivyo, iwapo Manii ya mwanaume ni zaidi ya mwanamke, mtoto atakuwa wa kiume kwa uwezo wa Allah تعالی na Iwapo mayai ya mwanamke ni zaidi ya mwanamume, mtoto atakuwa wa kike kwa uwezo wa Allah تعالی." Wakasema, 'Ndiyo'. Mtume ﷺ akasema, "Ewe Allah, kuwa shahidi dhidi yao." Kisha akasema, 'Nakuulizeni kwa Jina la Yule Aliyemteremshia Musa Taurati, Je, hamjui kuwa macho ya Mtume huyu asiyejua kusoma wala kuandika kikasomwa "ummi" hulala lakini moyo wake haulali?" Wakajibu, "Ndiyo, Wallahi!" Mtume ﷺ akasema, "Ewe Allah kuwa Shahidi." Wakasema, "Sasa tueleze juu ya walii wako miongoni mwa Malaika, kwani kwa hili ndipo tutaamua kukufuata au kujitenga nawe." Akajibu, 'Walii wangu ni jibril, na Allah تعالی Hajawahi kumtuma yeyote isipokuwa Jibrili ndiye walii Wake." Wakasema, "Kwa kuwa umemtaja huyo, tunaachana na wewe, kama ungemtaja mwingine tungelikufuata." Kutokana na hilo, Allah تعالی Aliteremsha Aya:

قُلْ مَنْ كَانِ عَدُوًّا لِّجِبْرِيلَ

"Sema: Aliye kuwa ni adui wa Jibril". (2:97)¹

Kauli ya Allah تعالی:

مِنْ قَبْلِ أَنْ تُنَزَّلَ التَّوْرَةُ

"Kabla hajjateremshwa Taurati."

Ina maana, Israil alijiharamishia kula nyama ya ngamia na kunywa maziwa yake kabla ya kushushwa Taurati. Kuna Minasaba mawili katika Mtiririko wa sehemu ya Ayah hii. Kwanza: Israil (Yaquub) عليه السلام alijiharamishia mambo mazuri kwa ajili ya Allah تعالی. Hili lilikuwa linaruhusiwa katika zama hizo, na kwa ajili hiyo inafaa kutajwa baada ya Kauli ya Allah تعالی,

¹ Ahmad 1:278.

لَنْ تَنَالُوا الْبِرَّ حَتَّى تُنْفِقُوا مِمَّا تُحِبُّونَ

“Kabisa hamtafikia wema mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda.”

Hii ndiyo Sharia tuliyowekewa, nayo ni kutoa katika utiifu wa Allah تعالی miongoni mwa vile avipendavyo mja na anavyovitamani kama Alivyosema,

وَأَتَى الْمَالَ عَلَى حُبِّهِ ذَوِي

“Na anawapa mali, kwa kupenda kwake.” (2:177) Na,

وَيُطْعَمُونَ أَلْطَعَامَ عَلَى حُبِّهِ

“Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake.” (76:8)

Pili, Baada ya Allah تعالی Kukanusha imani potofu ya Wakristo na itikadi yao potofu juu ya Masihi, na baada ya kubainika uongo wa tuhuma zao, na kudhihiri kwa ukweli na yakini katika jambo la Isa عليه السلام na mama yake, na namna Allah تعالی Alivyomuumba kwa Kudura na Utashi Wake, na Akamtuma kwa Wana wa Israil kuwalingania katika kumuabudu Mola wake Mtukufu. Hapa Allah تعالی Ameanza Kukanusha madai ya Mayahudi na Kubainisha kuwa *nasikh* na *mansukh* (kufuta hukumu kwa kuleta hukumu nyingine) waliyokana kuwa haipo na wala haijuzu, tayari ipo, kwani Allah تعالی Ametaja katika kitabu chao cha Taurati kuwa pale Nuh عليه السلام alipotoka katika Safina, Allah تعالی Alimruhusu kula nyama za aina zote za wanyama. Baadaye Israil (Yaqub) عليه السلام alijikataza nyama na maziwa ya ngamia; na wanawe walimfuata. Taurati baadaye ilikataza aina hii ya chakula na ikaongeza aina nyingine zilizokatazwa. Pia Allah تعالی Alimhalalishia Adam عليه السلام kuwaozesha watoto wake wa kike kwa kaka zao wa kiume, sharia hii iliharamishwa baadaye kisha Sharia ya Ibrahim عليه السلام ilimruhusu mwanamume kumfanya mjakazi kuwa mke mwenza, pamoja na mkewe muungwana, kama Ibrahim عليه السلام alivyofanya alipomchukua Hajar, wakati mkewe ni Sarah. Baadaye, Taurati iliharamisha Sharia hii. Kadhalika iliruhusiwa kuwaoa dada wawili wa baba na mama mmoja, kama Ya'qub عليه السلام alivyowaoa dada wawili kwa wakati mmoja. Baadaye, kaida hii iliharamishwa katika Taurati. Mifano yote hii imo ndani ya Taurati. Na hii ndio *Naskh Sharia* (Kufuata hukumu kwa kuleta hukumu nyingine). Kadhalika, ndivyo inavyokuwa Sharia Aliyoiweka kwa Isa عليه السلام, katika kuyahalalisha baadhi ya yaliyoharamishwa ndani ya Taurati. Basi, ni

kwa nini hawakumfuata Isa عليه السلام katika hali hii? Bali, Mayahudi walimkana na kumuasi Isa عليه السلام. Kadhalika yale ambayo Allah تعالى Alimtuma kwayo Muhammad ﷺ, ambayo ni Dini sahihi, njia iliyo sawa na mila ya baba yake, Ibrahim عليه السلام. Basi kwa nini hawaamini? Na Allah تعالى Amesema,

كُلُّ الطَّعَامِ كَانَ حَلَالًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ إِلَّا مَا حَرَّمَ إِسْرَائِيلُ عَلَى نَفْسِهِ مِنْ قَبْلِ أَنْ تُنزَلَ التَّوْرَةُ

“Kila chakula kilikuwa halali kwa Wana wa Israili isipo kuwa alichio jizullia Israili mwenyewe kabla haijateremshwa Taurati”. (3:93)

Maana yake: Kabla ya kuteremsha kwa Taurati, aina zote za vyakula vilikuwa halali, isipokuwa vile alivyojiharamishia Israil (Yaqub) عليه السلام mwenyewe. Kisha Allah تعالى Akasema,

قُلْ فَأْتُوا بِالتَّوْرَةِ فَاتْلُوهَا إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٩٤﴾

“Sema: Leteni Taurati muisome ikiwa nyinyi ni wasema kweli.”

Kwani Taurati inathibitisha tunachokieleza hapa. Kisha Allah تعالى Amesema

فَمَنْ أَفْتَرَى عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ مِنْ بَعْدِ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٩٥﴾

“Na wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu baada ya hayo, basi hao ndio madhalimu.” (3:94)

Maana yake: Wale watakaomuongopea Allah تعالى na kudai kuwa Aliwapangia siku ya Sabato na kushikamana na Taurati milele, na kwamba Allah تعالى Hakumpeleka Mtume mwingine ili awalinganie watu kwa Allah تعالى kwa kutumia uthibitisho na ushahidi, baada ya ubainisho huu wa kuwepo kwa kufuta hukumu kwa kufuata hukumu nyingine “Naskh” na kudhihiri kwa haya tuliyoyaelezea,

فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٩٥﴾

“Basi hao ndio madhalimu.” (3:94)

Kisha Allah تعالى Amesema,

قُلْ صَدَقَ اللَّهُ

“Sema: Mwenyezi Mungu Amesema kweli.” (3:95)

Maana yake: Ewe Muhammad ﷺ, sema kuwa Allah تعالى Amesema kweli katika yale Aliyowasilisha na Kuyawekea sheria ndani ya Qur’an,

فَاتَّبِعُوا مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿٩٥﴾

“Basi fuateni mila ya Ibrahim mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.” (3:95)

Kwa hiyo fuateni Dini ya Ibrahim عليه السلام ambayo Allah تعالى Ameitungia sheria ndani ya Qur’an, kupitia ulimi wa Muhammad ﷺ. Huu ni ukweli usio na shaka ndani yake, na njia iliyo sawa, na hapana Mtume aliyeleta njia iliyo kamili ya wazi na sahihi kuliko alivyofanya yeye. Allah تعالى Anasema katika Aya nyingine,

قُلْ إِنِّي هَدَيْتَنِي رَبِّيَ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ دِينًا قِيمًا مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ

الْمُشْرِكِينَ ﴿١٦١﴾

“Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Mlezi Ameniongoa kwenye njia iliyonyooka, Dini iliyo sawa kabisa, ambayo ndiyo mila ya Ibrahim aliyekuwa mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina”. (6:161)

Na Allah تعالى Akasema;

ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنْ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٦٢﴾

“Kisha Tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.” (16:123)

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٢٣﴾ فِيهِ آيَاتٌ بَيِّنَاتٌ

مَّقَامُ إِبْرَاهِيمَ ۗ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ ءَامِنًا ۗ وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ

سَبِيلًا ۗ وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿١٢٤﴾

96. Hakika Nyumba ya kwanza waliowekewa watu kwa ibada ni ile iliyoko Makka, iliyobarikiwa na yenye uwongofu kwa walimwengu wote.

97. Ndani yake zipo alama zilizowazi - za kuthibitisha utukufu na ubora wa msikiti huu - miongoni mwao ni kisimamo cha Ibrahim, na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani. Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kwendea. Na atakayekanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu.

Ka'bah ni Nyumba ya Kwanza Iliyowekwa kwa Ajili ya Ibada

Allah تعالی Amesema,

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ

**“Hakika Nyumba ya kwanza waliowekewa watu kwa ibada.”
(3:96)**

Hapa wanakusudiwa watu wote, kwa kufanya ibada zao na taratibu za kidini wanazunguka Al-Ka'abah (katika *Tawaf*), wanaswali kwa kuielekea na wanabaki katika eneo hilo kwa *Itikaf*.

لَلَّذِي بِبَكَّةَ

“Ni ile iliyoko Makka.” (3:96)

Maana yake: Ka'abah ambayo ilijengwa na Ibrahim Al-Khalil عليه السلام, ambaye makundi yote mawili, Mayahudi na Wakristo wanadai kuifuata dini yake. Hata hivyo, hawafanyi ibada ya Hajj katika Nyumba ambayo Ibrahim عليه السلام alijenga kwa Amri ya Allah تعالی, na kwayo aliwalingania watu waje kufanya Hajj. Kisha Allah تعالی Akasema,

مُبَارَكًا

“Yenye baraka.” (3:96),

Maana yake: Iliyobarikiwa.

وَهْدَىٰ لِلْعٰلَمِيْنَ ﴿٩٦﴾

“Na yenye uwongofu kwa walimwengu wote.” (3:96)

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه kuwa alisema, “Nilimuuliza, Ewe Mjumbe wa Allah! Ni Msikiti gani ulikuwa wa kwanza kujengwa juu ya ardhi?” Akanijibu, “*Al-Masjid Al-Haram.*” Nikauliza, “Kisha upi?” Alijibu, ‘*Al-Masjid Al-Aqsa.*’ Nikasema, “kuna tofauti ya muda gani kati ya ujenzi wa misikiti hiyo miwili?” Akajibu, “*Miaka Arobaini.*” Kisha akasema;

«ثُمَّ حَيْثُ أَذْرَكْتَ الصَّلَاةَ فَصَلِّ، فَكُلُّهَا مَسْجِدٌ»

“Mahali popote utakapoidiriki Swala swali hapo, kwani ardhi yote ni Msikiti.”¹

Pia Bukhari na Muslim wameipokea Hadithi hii.²

Sababu ya Makkah Kuitwa *Bakkah*, na Majina Mengine:

Allah تعالى Amesema,

لِلَّذِي بِبَكَّةَ

“...ni ile iliyoko *Bakkah*...”

Ilivyo mashuhuri ni kwamba Bakkah ni moja ya majina ya Makkah. Inasemekana kwamba iliitwa kwa jina la Bakkah kwa kuwa inawaliza (*Bukaa*, kulia, kutoa machozi), watu waliodhulumu na fedhuli, maana: Wanadhalilika, na wananyenyekea mbele yake. Pia Makkah iliitwa *Bakkah* kwa sababu watu hukusanyika humo. Mji wa Makkah una majina mengi, ambayo ni Makkah, *Bakkah*, *Al-Bayt Al-Atiq* (Nyumba ya Kale), *Al-Bayt Al-Haram* (Nyumba Takatifu), *Al-Balad Al-Amin* (Nyumba ya Amani), *Al-Ma'mun* (Salama). Majina mengine ya Makkah ni pamoja na *Umm Ruhm* (Mama wa Rehema), *Ummul-Qura* (Mama wa Miji), *Swalaah*, *Al-Arsh*, *Al-Qaadis*, kwa sababu hutakasa dhidi ya madhambi, *Al-Muqaddasah*, *An-Naasah*, *Al-Baasah*, *Al-Hatwimah*, *An-Nasaasah*, *Ar-Ra-as*, *Al-Kutha*, *Al-Baldah*, *Al-Baniyah* na *Al-Ka'bah*.

¹ Ahmad 5:150.

² Fat'hul Al-Bari 6:469. Muslim 1:370.

Makamu Ibrahim عليه السلام

Kauli ya Allah تعالى،

فِيهِ ءَايَاتٌ بَيِّنَاتٌ

“Ndani yake zipo Ishara zilizo wazi”.

Maana yake: Alama zilizo wazi kuwa Ibrahim عليه السلام ndiye aliyejenga Ka’abah na kuwa Allah تعالى Aliitukuza na Kuibariki. Kisha Allah تعالى Amesema،

مَقَامُ إِبْرَاهِيمَ

“Masimamio ya Ibrahim”.

Wakati jengo la Ka’bah liliponyanyuliwa, Ibrahim عليه السلام alisamama juu yake (*Maqam*) ili aweze kuinua ukuta juu zaidi, ambapo mwanaye Ismail عليه السلام alikuwa akimpa mawe. Ni vyema kutaja hapa kuwa *Maqam* ilikuwa karibu kabisa na Ka’bah. Baadaye, katika kipindi cha utawala wa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه aliihamisha *Maqam* upande wa mashariki, ili wale wanaofanya *Tawaf* kuizunguka Ka’bah waweze kupita kwa urahisi bila ya kuwabughudhi wanaosali karibu na *Maqam* baada ya kumaliza *Tawaf*. Kwani Allah تعالى Alituumuru tusali pembeni mwa *Maqam*, kwa Kauli Yake تعالى،

وَاتَّخِذُوا مِنْ مَّقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلًّى

“Na alipokuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia.”

(2:125)

Tumezitaja Hadithi zinazohusu mada hii hivyo hatuoni haja ya kuzirudia tena, shukrani zote zinamstahikia Allah تعالى. Al-Awfi alisema kuwa, Ibn Abbas رضي الله عنهما aliitolea ufafanuzi Kauli ya Allah تعالى،

فِيهِ ءَايَاتٌ بَيِّنَاتٌ مَّقَامُ إِبْرَاهِيمَ

“Ndani yake zipo Ishara zilizo wazi Masimamio ya Ibrahim”.

Miongoni mwa alama hizo ni: *Maqam* na *Al-Mash’ar* (Al-Haram).¹ Mujahid alisema, “Alama za nyayo za Ibrahim kubaki juu ya *Maqam* ni alama iliyo

¹ At-Tabari 7:26.

wazi.”¹ Ilisimuliwa kuwa Umar bin Abdul-Aziz, Al-Hassan, Qatadah, As-Suddi, Muqatil bin Hayyan na wengineo walisema vivyo hivyo.² Abu Twalib alisema katika kaswida yake mashuhuri: “Na mahali alipokanyaga Ibrahim عليه السلام katika jiwe ni panyenyekevu, kwa miguu yake miwili isiyokuwa na viatu.”

Eneo Takatifu la *Al-Haram* ya Makkah ni Mahali pa Salama

Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا

“Na mwenye kuingia humo anakuwa katika amani.”

Maana yake: *Haram* ya Makkah ni mahali pa salama, pindi mwenye khofu atakapopaingia. Ndivyo pia, ilivyokuwa katika zama za *Jahiliyyah*. Ni sawa na alivyosema Al-Hassan Al-Basri رحمه الله تعالى na wengine, kwamba mtu aliweza kuua, kisha akajizungushia kipande cha sufu shingoni mwake na akaingia *Haram*. Na hata kama mtoto wa aliyeuawa angekutana naye, asingepambana naye, mpaka atakapondoka maeneo matakatifu. Allah تعالى Amesema:

أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّا جَعَلْنَا حَرَمًا آمِنًا وَيُتَخَطَّفُ النَّاسُ مِنْ حَوْلِهِمْ

“Je! Hawaoni ya kwamba Tumeifanya nchi takatifu ina amani, na hali watu wengine wananyakuliwa kote kwa majirani zao?”
(29:67)

Na Allah تعالى Amesema,

فَلْيَعْبُدُوا رَبَّ هَذَا الْبَيْتِ ۖ الَّذِي أَطْعَمَهُمْ مِنْ جُوعٍ وَآمَنَهُمْ مِنْ خَوْفٍ ۖ

“Basi nawamuabudu Mola Mlezi wa Nyumba hii, ambaye Anawalisha wasipate njaa, na Anawalinda na khofu.” (106:3-4)

Pia miongoni mwa yasiyoruhusiwa katika eneo la *Al-Haram* ni uwindaji na kuwatoa wanyama nje ya makazi yao (ili wawindwe), na kukata miti katika viunga vyake, na kukata nyasi zake, kama zilivyothibitisha hayo Hadithi za Mtume ﷺ na kauli za Masahaba. Sahih mbili zilinukuu (haya yakiwa maneno

¹ At-Tabari 7:27.

² Ibn Abu Hatim 2:412,413.

ya Muslim) kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Siku ya *Fat-h Makkah*, Mtume ﷺ alisema,

«لَا هِجْرَةَ، وَلَكِنْ جِهَادٌ وَبِئْتَهُ، وَإِذَا اسْتَنْفَرْتُمْ فَانْفِرُوا»

"Hapatakuwa na Hijra nyingine, lakini kuna Jihad na Nia. Endapo mtatakiwa kusonga mbele, basi songa mbele."

Alisema tena katika siku ya *Fat-h Makkah*,

«إِنَّ هَذَا الْبَلَدَ حَرَمُهُ اللهُ يَوْمَ خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ، فَهُوَ حَرَامٌ بِحُرْمَةِ اللهِ إِلَيَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَإِنَّهُ لَمْ يَحِلَّ الْقِتَالُ فِيهِ لِأَحَدٍ قَبْلِي، وَلَمْ يَحِلَّ لِي إِلَّا فِي سَاعَةٍ مِنْ نَهَارٍ، فَهُوَ حَرَامٌ بِحُرْمَةِ اللهِ إِلَيَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، لَا يُعْصَدُ شَوْكُهُ، وَلَا يُنْفَرُ صَبْدُهُ، وَلَا يَنْقَطُ لِقَطْعَتِهَا إِلَّا مَنْ عَرَفَهَا، وَلَا يُخْتَلَى خِلَاهَا»

"Kwa hakika! Allah Aliufanya mji huu (Makkah) kuwa mtakatifu tokea siku Alipoumba mbingu na ardhi, na umetukuzwa kwa amri ya Allah mpaka siku ya kiyama. Kupigana ndani ya mji wa Makkah haikuruhusiwa kwa yeyote kabla yangu na iliruhusiwa kwangu kwa muda wa saa chache katika mchana mmoja tu. Hapana shaka sasa ni pahala patakatifu kwa amri ya Allah mpaka siku ya Kiyama. Hairuhusiwi kung'oa kichaka hata kama cha miba, kuwinda wanyama wake, kuokota vitu vilivyopotea, isipokuwa kwa mwenye kuvitangaza, wala miti yake haing'olewi."

Abbas رضي الله عنه alisema, 'Isipokuwa nyasi limau, Ewe Mjumbe wa Allah, kwa kuwa zinatumika katika majumba na makaburi." Mtume ﷺ alisema:

«إِلَّا الْإِذْخِرَ»

*"Isipokuwa mchaichai."*¹

(Maana yake: Nyasi hizo zimeruhusiwa kung'olewa).

Pia Sahihi mbili zilinukuu kuwa Abu Shurayh Al-Adawi alisema kuwa alimuambia Amr bin Said wakati alipokuwa akipeleka vikosi Makkah (kupigana na Abdullah bin Az-Zubayr), "Ewe Jemedari! Niruhusu nikuambie aliyoyasema Mtume ﷺ siku iliyofuatia *Fat-h Makkah*. Masikio yangu yalimsikia

¹ Fat'hul Al-Bari 4:56 na Muslim 2:986.

Mtume ﷺ akizungumza. Mtume ﷺ baada ya kumtukuza na kumsifu Allah alisema:

«إِنَّ مَكَّةَ حَرَمَهَا اللَّهُ، وَلَمْ يُحَرِّمْهَا النَّاسُ، فَلَا يَجُلُّ لِأَمْرِىَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أَنْ يَسْفِكَ بِهَا دَمًا، وَلَا يَغْتَبِدَ بِهَا شَجَرَةً، فَإِنْ أَحَدٌ تَرَخَّصَ بِقِتَالِ رَسُولِ اللَّهِ ﷺ فِيهَا فَقُولُوا لَهُ: إِنَّ اللَّهَ أَذِنَ لِرَسُولِهِ وَلَمْ يَأْذَنْ لَكُمْ، وَإِنَّمَا أَذِنَ لِي فِيهَا سَاعَةً مِنْ نَهَارٍ، وَقَدْ عَادَتْ حُرْمَتُهَا الْيَوْمَ كَحُرْمَتِهَا بِالْأَمْسِ فَلْيُبَلِّغِ الشَّاهِدُ الْغَائِبَ».

“Hakika Allah تعالى Aliifanya Makkah kuwa Haram (tukufu) na wala si watu waliyoifanya tukufu. Kwa hiyo, yeyote anayemuamini Allah تعالى na Siku ya Mwisho, asimwage damu hapo, wala asikate miti yake. Endapo mtu atasababisha kuwa inaruhusiwa kwa kupigana Mjumbe wa Allah siku ya Fat’hi, muambie ni Allah تعالى Alimruhusu Mjumbe Wake na Hakukuruhusuni nyinyi.” Allah تعالى Aliniruhusu kwa saa chache, mchana ule wa Fat-h, na leo uharamu wake umerudi kama ulivyokuwa jana. Hivyo, aliehudhuria lazima amfikishie asie kuwepo.”

Abu Shurayh aliulizwa, “Amr alisema nini?” Akasema kuwa Amr alijibu, “Ewe Abu Shurayh! Katika hili mimi ninajua kuliko wewe, Makkah haimpi hifadhi mfanya dhambi, muuaji au mwizi.”¹

Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema, “Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«لَا يَجُلُّ لِأَحَدِكُمْ أَنْ يَحْمِلَ بِمَكَّةَ السَّلَاحَ»

“Si halali kwa mmoja wenu kubeba silaha ndani ya Makkah.”²

Muslim aliandika Hadithi hii.

Abdullah bin Adiyi bin Al-Hamra’ Az-Zuhri رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema alipokuwa amesimama katika sehemu inayoitwa Al-Hazwarah katika soko la Makkah,

«وَاللَّهِ إِنَّكَ لَخَيْرُ أَرْضِ اللَّهِ، وَأَحَبُّ أَرْضِ اللَّهِ إِلَى اللَّهِ، وَلَوْلَا أَنِّي أُخْرِجْتُ مِنْكَ مَا خَرَجْتُ»

¹ Muslim 2:987.

² Muslim 2:989.

“Wallah! Wewe ni ardhi bora ya Allah na ardhi ipendwayo mno na Allah. Na lau nisingekuwa nimetolewa hapa, nisingeondoka.”¹

Imamu Ahmad ndiye aliyekusanya Hadithi hii, na haya ni maneno yake. At-Tirmidhi, An-Nasai na Ibn Majah waliikusanya pia.² At-Tirmidhi aliitaja kuwa ni *“Hasan Sahih”*

Ufafanuzi Kuhusu Wajibu wa Kuhiji:

Allah تعالى Amesema,

وَلِلَّهِ عَلَى النَّاسِ حِجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا

“Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu imewawajibikia watu wahiji kwenye Nyumba hiyo, kwa yule awezae njia ya kuendea”.

Ayah hii imewajibisha kutekeleza Hajj. Zipo Hadithi nyingi zinazoitaja Hijja kuwa ni moja kati ya nguzo na misingi ya Uislamu, na hili linakubaliwa na Waislamu. Kwa mujibu wa maandiko na makubaliano ya wanazuoni. Ni faradhi kwa Muislamu baleghe kuhiji mara moja katika umri wake. Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ wakati mmoja alitoa khutuba na kusema,

«أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ فُرِضَ عَلَيْكُمُ الْحَجُّ فَحُجُّوا»

“Enyi watu! Mmefaradhishiwa Hajj, kwa hiyo tekelezeni Hajj.”

Halafu akanyamaza. Mtu mmoja akauliza: “Hivi ni kila mwaka Ewe Mjumbe wa Allah?” Mtume ﷺ alinyamaza kimya mpaka mtu yule alipolirejea suali lake mara tatu na kisha akasema,

«لَوْ قُلْتُ: نَعَمْ لَوَجَبَتْ وَلَمَّا اسْتَطَعْتُمْ»

“Lau ningesema ndiyo, ingewajibika, nanyi msingeweza”.

Kisha akasema,

¹ Ahmad 4:305.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 10:326; An-Nasai katika Al-Kubra 2:479 na Ibn Majah 2:1037.

«ذُرُونِي مَا تَرَكَتُكُمْ فَإِنَّمَا هَلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ بِكَثْرَةِ سُؤَالِهِمْ وَاخْتِلَافِهِمْ عَلَيَّ
أَنْبِيَائِهِمْ، وَإِذَا أَمَرْتُكُمْ بِشَيْءٍ فَأَتُوا مِنْهُ مَا اسْتَطَعْتُمْ، وَإِذَا نَهَيْتُكُمْ عَنْ شَيْءٍ فَدَعُوهُ»

*"Niacheni kama ninavyokuacheni, watu kabla yenu waliangamizwa kwa maswali yao mengi kwa Mtume wao na kubishana kwao na Mitume wao. Iwapo nitakuamuruni mfanye jambo, fanyeni kwa kiasi muwezavyo. Na nikikukatazeni jambo basi liacheni."*¹

Pia Muslim alinukuu vivyo hivyo.²

Maana ya: 'Kuweza njia' katika Aya: Kuna namna nyingi za uwezo wa kufanya safari." Kuna uwezo wa mtu mwenyewe binafsi na uwezo unaohusishwa na vitu vingine kama vilivyotajwa ndani ya vitabu vya *Fiqh*. Abu Isa At-Tirmidhi alinukuu kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, "Alisimama mtu na akamuuliza Mtume ﷺ, "Ewe Mjumbe wa Allah! Nani Hajji?" Akamjibu, "Yule ambaye nywele na nguo zake zimechafuka." Mtu mwingine akauliza, "Hijja ipi ni bora, Ewe Mjumbe wa Allah?" Akamjibu "Yenye Makelele (ya kumuomba Allah تعالى) na damu (ya kutoa sadaka)." Mtu mwingine akauliza, "Ni upi uwezo wa kufanya safari, Ewe Mjumbe wa Allah?" Akamjibu, "Kuwa na matumizi ya njiani na gharama za usafiri."³ Haya ni masimulizi yaliyokusanywa na Ibn Majah.⁴ Al-Hakim alisimulia kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu maana ya Kauli ya Allah تعالى,

مَنْ اسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا

"Kwa yule awezae njia ya kuendea." (3:97)

Kwamba, "Ni nini maana ya awezaye njia ya kuendea?" Mtume ﷺ alijibu: "Ni kuwa na chakula cha kutosha, na kipando (gharama za safari)". Al-Hakim alieleza kuwa isnadi ya upokezi wa Hadithi hii ni Sahih, kwa sharti ya Muslim katika Sahih yake, lakini sahihi mbili hazikuikusanya.⁵ Ahmad alinukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Ahmad 2:508.

² Muslim 2:975.

³ Tuhfat Al-Ahwadhi 8:348

⁴ Ibn Majah 2:96.

⁵ Al-Hakim 1:442.

«مَنْ أَرَادَ الْحَجَّ فَلْيَتَعَجَّلْ»

“Mwenye kutaka Hajj, basi aharakishe.”¹

Abu Daudi pia alikusanya Hadith hii.²

Mwenye Kukanusha Nguzo ya Hajj ni Kafiri

Allah تعالى Amesema;

وَمَنْ كَفَرَ فَإِنَّ اللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٧٧﴾

“Na atakayekanusha basi Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu.”

Ibn Abbas, Mujahid na wengineo رضي الله عنهم wameitolea maelezo Ayah hii kwa kusema, “Yeyote anayekanusha ulazima wa Hajj ni kafiri, na Allah تعالى ni Mkwasi zaidi kwani hamhitajii.” Al-Hafidh Abu Bakr Al-Ismaail رحمه الله تعالى Alinukuu kuwa ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema, “Yeyote anayemudu gharama za Hajj, lakini asitekeleze, basi na afe akiwa Yahudi au Mkristo.”³

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ لِمَ تَكْفُرُونَ بِقَايَتِ اللَّهِ وَاللَّهُ شَهِيدٌ عَلَىٰ مَا تَعْمَلُونَ ﴿٧٧﴾ قُلْ يَا أَهْلَ

الْكِتَابِ لِمَ تَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ مَن ءَامَنَ تَبِعُوهَا فَوَجًّا وَأَنْتُمْ شُهَدَاءُ ۗ وَمَا اللَّهُ

بِغَفْلٍ ۗ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٧٧﴾

98. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Kwa nini mnakanusha ishara za Mwenyezi Mungu, na ilhali kuwa Mwenyezi Mungu ni Shahidi kwa yote mnayoyatenda?

99. Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Kwa nini mnamzuilia aliyeamini Njia ya Mwenyezi Mungu mkiitafutia kosa, na hali nyinyi mnashuhudia? Na Mwenyezi Mungu si Mwenye kughafilika na mnayoyatenda.

¹ Al-Hulyah 9:202 Ina isnadi ya upokezi iliyo sahihi ikimrejea Umar.

² Ahmad 1:225.

³ Abu Dawud 2:350.

Kukaripiwa Watu wa Kitabu kwa Kukufuru na Kuzuia Watu Njia ya Allah تعالی

Katika aya hii Allah تعالی Anawakaripia Watu wa Kitabu wanaokataa ukweli, wakikana Aya za Allah تعالی na kuzuia wanaotaka kufuata na kuamini njia Yake, japo wanajua alichotumwa nacho Mjumbe ﷺ ni ukweli kutoka kwa Allah تعالی. Walijifunza haya kutoka kwa Mtume Mwarabu, asiyejua kusoma wala kuandika kikasomwa “Ummi” wa kabila la Hashimi Makkah, bwana wa wana wa Adam, Mtume wa Mwisho na Mjumbe wa Mola wa mbinguni na ardhini. Allah تعالی Aliwaonya Wana wa Israil kwa mwenendo huu, akieleza kuwa Yeye ni Shahidi kwa kila wafanyalo, wakionesha kukana ilimu waliyofikishiwa na Mitume. Walikanusha na wakakataa na kumkana Mtume yule ambaye waliamriwa kutoa bishara njema juu ya kuja kwake. Allah تعالی Anaeleza kuwa Yeye Hapitwi na wanayofanya, na Atawalipa kwa matendo yao,

يَوْمٌ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ ﴿٨٨﴾

“Siku ambayo kwamba mali hayatofaa kitu wala wana.” (26:88)

* * *

يَتَّيِبُهَا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا اِنْ تَطِيعُوا فَرِيْقًا مِّنَ الَّذِيْنَ اُوتُوْا
 الْكِتٰبَ يَرْدُّوْكُمْ بَعْدَ اِيْمٰنِكُمْ كٰفِرِيْنَ ﴿١٠١﴾ وَكَيْفَ تَكْفُرُوْنَ
 وَاَنْتُمْ تُتْلٰى عَلَيْكُمْ ءَايٰتُ اللّٰهِ وَفِيْكُمْ رَسُوْلُهُ ؕ وَمَنْ
 يَعْتَصِمْ بِاللّٰهِ فَقَدْ هُدِيَ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿١٠٢﴾ يٰٓاَيُّهَا
 الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا اتَّقُوا اللّٰهَ حَقَّ تَقٰوَاتِهِ وَلَا تَمُوْنُوْا اِلَّا وَاَنْتُمْ
 مُّسْلِمُوْنَ ﴿١٠٣﴾ وَاَعْتَصِمُوْا بِحَبْلِ اللّٰهِ جَمِيْعًا وَلَا تَفَرَّقُوْا
 وَاذْكُرُوْا نِعْمَتَ اللّٰهِ عَلَيْكُمْ اِذْ كُنْتُمْ اَعْدَآءَ بَيْنَ
 قُلُوْبِكُمْ فَاَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ اِخْوٰنًا وَكُنْتُمْ عَلٰى شَفَا حُفْرَةٍ
 مِّنَ النَّارِ فَاَنْقَذَكُمْ مِّنْهَا ؕ كَذٰلِكَ يُبَيِّنُ اللّٰهُ لَكُمْ ءَايٰتِهِ
 لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُوْنَ ﴿١٠٤﴾ وَلَتَكُنْ مِّنْكُمْ اُمَّةٌ يَدْعُوْنَ اِلٰى الْخَيْرِ
 وَيَأْمُرُوْنَ بِالْعُرُوْفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ ؕ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ
 الْمُفْلِحُوْنَ ﴿١٠٥﴾ وَلَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ تَفَرَّقُوْا وَاخْتَلَفُوْا
 مِنْ بَعْدِ مَا جَآءَهُمُ الْبَيِّنٰتُ ؕ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ عَذٰبِ عَظِيْمٍ
 ﴿١٠٦﴾ يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوْهُ وَتَسْوَدُّ وُجُوْهُ ؕ فَاَمَّا الَّذِيْنَ اَسْوَدَّتْ
 وُجُوْهُهُمْ اَكْفَرْتُمْ بَعْدَ اِيْمٰنِكُمْ فَذُوْقُوا الْعَذٰبَ بِمَا كُنْتُمْ
 تَكْفُرُوْنَ ﴿١٠٧﴾ وَاَمَّا الَّذِيْنَ اَبْيَضَّتْ وُجُوْهُهُمْ فِى رَحْمَةِ اللّٰهِ
 هُمْ فِيْهَا خٰلِدُوْنَ ﴿١٠٨﴾ تِلْكَ ءَايٰتُ اللّٰهِ نَتْلُوْهَا عَلَيْكَ
 بِالْحَقِّ ؕ وَمَا اللّٰهُ يُرِيْدُ ظُلْمًا لِّلْعٰلَمِيْنَ ﴿١٠٩﴾ وَاَللّٰهُ مَا فِى
 السَّمٰوٰتِ وَمَا فِى الْاَرْضِ ؕ وَاِلٰى اللّٰهِ تُرْجَعُ الْاَمْوٰرُ ﴿١١٠﴾

يَتَّيِبُهَا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا اِنْ تَطِيعُوا فَرِيْقًا
 مِّنَ الَّذِيْنَ اُوتُوْا الْكِتٰبَ يَرْدُّوْكُمْ بَعْدَ
 اِيْمٰنِكُمْ كٰفِرِيْنَ ﴿١٠١﴾ وَكَيْفَ تَكْفُرُوْنَ
 وَاَنْتُمْ تُتْلٰى عَلَيْكُمْ ءَايٰتُ اللّٰهِ
 وَفِيْكُمْ رَسُوْلُهُ ؕ وَمَنْ يَعْتَصِمْ بِاللّٰهِ
 فَقَدْ هُدِيَ اِلٰى صِرَاطٍ مُّسْتَقِيْمٍ ﴿١٠٢﴾

100. Enyi mlioamini! Mkiwatii baadhi ya waliopewa Kitabu watakurudisheni kuwa makafiri baada ya Imani yenu.

101. Na vipi mkufuru hali nyinyi mnasomewa Aya za Mwenyezi Mungu na Mtume yuko kati yenu? Na mwenye kushikamana na Mwenyezi Mungu basi huyo ameingozwa kwenye njia iliyo nyooka.

Waislamu Wametahadhariwa Kuwatii Watu wa Kitabu

Allah تعالى Anawatahadharisha waumini kutowatii Watu wa Kitabu, wanao-waonea inda Anawaonya waumini kwa neema walizo-jaaliwa na Allah تعالى kwa

kumpeleka Mjumbe wake ﷺ kama Allah تعالى Alivyosema:

وَدَّ كَثِيرٌ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ يَرُدُّونَكُمْ مِن بَعْدِ إِيمَانِكُمْ كُفَّارًا حَسَدًا مِّنْ عِندِ
أَنْفُسِهِمْ

“Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanatamani lau wange kurudisheni nyinyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu, kwa ajili ya uhasidi uliomo ndani ya nafsi zao.” (2:109)

Katika Aya hii Allah تعالى Amesema,

إِنْ تُطِيعُوا فَرِيقًا مِّنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ يَرُدُّوكُم بَعْدَ إِيمَانِكُمْ كَافِرِينَ ﴿١٠٩﴾

“Mkiwatii baadhi ya waliopewa Kitabu watakurudisheni kuwa makafiri baada ya Imani yenu.” (3:100)

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَكَيْفَ تَكْفُرُونَ وَأَنْتُمْ تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ آيَاتُ اللَّهِ وَفِيكُمْ رَسُولُهُ

“Na vipi mkufuru hali nyinyi mnasomewa Aya za Mwenyezi Mungu na Mtume yuko kati yenu?” (3:101)

Maana yake: Ukafiri uko mbali nanyi kuwafikia, kwani Aya za Allah تعالى Zinateremshwa kwa Mjumbe Wake ﷺ mchana na usiku, na anazisoma na kuzifikisha kwenu. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

وَمَا لَكُمْ لَا تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالرَّسُولِ يَدْعُوكُمْ لِتُؤْمِنُوا بِرَبِّكُمْ وَقَدْ أَخَذَ مِيثَاقَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ

مُؤْمِنِينَ ﴿٥٧﴾

“Na mna nini hata hamumuamini Mwenyezi Mungu na hali Mtume anakuiteni mumuamini Mola wenu Mlezi? Naye amekwisha chukua ahadi yenu, ikiwa nyinyi ni Waumini”. (57:8)

Hadithi inaelezea kuwa, siku moja Mtume ﷺ aliwauliza Masahaba zake,

«أَيُّ الْمُؤْمِنِينَ أَعْجَبُ إِلَيْكُمْ إِيْمَانًا؟» قالوا: الملائكة. قال: «وَكَيْفَ لَا يُؤْمِنُونَ وَهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ؟» وذكروا الأنبياء، قال: «وَكَيْفَ لَا يُؤْمِنُونَ وَالْوَحْيُ يَنْزِلُ عَلَيْهِمْ؟» قالوا: فنحن. قال: «وَكَيْفَ لَا تُؤْمِنُونَ وَأَنَا بَيْنَ أَظْهُرِكُمْ؟» قالوا: فأبي الناس أعجب إيمانًا؟ قال: «قَوْمٌ يَجِئُونَ مِن بَعْدِكُمْ يَجِدُونَ صُحُفًا يُؤْمِنُونَ بِمَا فِيهَا»

"Ni muumini yupi anakuvutieni imani yake?" Wakajibu: "Malaika". Akasema, "Kwa nini wasiamini, nao wako na Mola wao?" Wakataja Mitume, na Mtume ﷺ akasema, "Kwanini wasiamini na ambapo wahyi uliteremshwa kwao?" Wakasema, "Basi ni sisi." Akasema, "kwanini msiamini na mimi niko miongoni mwenu?" Wakauliza, "Kumbe basi ni nani mwenye kuvutia imani?", Akasema, "Ni watu watakuja baada yenu ambao watakuta vitabu na wataviamini."¹

Kisha Allah ﷻ Akasema,

وَمَنْ يَعْصِمْ بِاللَّهِ فَقَدْ هُدِيَ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿١٠١﴾

"Na mwenye kushikamana na Mwenyezi Mungu basi huyo ameongozwa kwenye njia iliyonyooka." (3:101)

Maana yake: Pamoja na haya, kumuamini na kumtegemea Allah ﷻ ndio msingi wa kufikia uongofu sahihi na kuwa mbali na njia ya upotofu. Pia ni wasila wa kupata uongofu na ni njia ya kupita na kufikia malengo adilifu.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٠٢﴾ وَأَعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا ۗ وَأَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا وَكُنْتُمْ عَلَىٰ شَفَا حُفْرَةٍ مِنَ النَّارِ فَأَنْقَذَكُمْ مِنْهَا كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ ءَايَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٠٣﴾

102. Enyi mliaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu.

103. Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile mlivyokuwa nyinyi kwa nyinyi maadui Naye Akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema Yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto, Naye Akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu Anakubainishieni Ishara Zake ili mpate kuongoka."

¹ At-Tabarani 4:22,23 Pia Taz. Ahmad 4:106.

Ni Nini Maana ya Haki ya Kumcha Allah تعالى

Ibn Abu Hatim رضي الله عنه alinukuu kuwa Abdullah bin Mas'ud رحمه الله تعالى aliitolea maelezo Aya:

اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ

“Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha.”

“Kuhakikisha kuwa Anatiiwa na Haasiwi, Anakumbukwa na wala Hasahauliwi na Anashukuriwa na Hakufuriwi.”¹ Hadithi hii ina isnadi ya mapokezi sahihi mpaka kwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه. Al-Hakim alikusanya Hadithi hii katika *Mustadrak* wake, kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه, ambaye alipokea kutoka kwa Mtume ﷺ. Al-Hakim anasema, “Ni sahihi kwa mujibu wa vigezo vya Mashekhe wawili (Bukhari na Muslim), lakini wao hawakuiandika.”² Hivi ndivyo alivyosema, lakini inaonesha kuwa ni kauli ya Abdullah bin Mas'ud, na Allah تعالى Ndiye Mjuzi Zaidi. Pia ilisimuliwa kuwa Anas رضي الله عنه alisema, “Mja hatamcha Allah تعالى kama inavyostahili mpaka atakapouhifadhi ulimi wake.”³ Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تُمُونَنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٠٢﴾

“Wala msife ila nanyi ni Waislamu.”

Maana yake: Dumuni katika Uislamu wakati wa uzima wenu na wakati wa usalama wenu, ili mfe mkiwa Waislamu. Allah تعالى Mwingi wa Rehema Amefanya Uamuzi Wake kuwa: Atakavyoishi mtu ndivyo atakavyokufa na atafufuliwa hivyo. Tunaomba hifadhi ya kutokufa nje ya Uislamu. Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Mujahid alisema, “Watu walikuwa wakizunguka Nyumba Takatifu hali ya kuwa Ibni Abbas رضي الله عنهما akiwa amekaa huku ameshika bakora. Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema, Mtume ﷺ aliisoma Kauli ya Allah تعالى,

اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ

“Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha.” (3:102)

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ وَلَا تُمُونَنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٠٢﴾

“Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu.” (3:102)

¹ Ibn Abu Hatim 2:446.

² Al-Hakim 2:294.

³ Ibn Abu Hatim 2:448.

Kisha Akasema.

«وَلَوْ أَنَّ قِطْرَةً مِنْ الرِّزْقِمْ قُطِرَتْ لِأَمْرَتْ عَلَى أَهْلِ الْأَرْضِ عَيْسَتَهُمْ، فَكَيْفَ بِمَنْ
لَيْسَ لَهُ طَعَامٌ إِلَّا الرِّزْقُومُ؟»

“Kwa hakika lau tone la Zaqqum (mti uliopo Motoni) litaanguka (ardhini), kitaharibu maisha ya watu duniani. Hali itakuwaje kwa wale ambao hawana chakula isipokuwa ni Zaqqum?”¹

Hivi ndivyo alivyonukuu At-Tirmidhi, An-Nasai, Ibn Majah, Ibn Hibban katika Sahih yake na katika *Mustadrak* wa Al-Hakim. At-Tirmidhi amesema; “Hassan Sahih” ambapo Al-Hakim alisema, “Imetimiza masharti ya Sahih Mbili lakini hawakuinukuu.”² Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Jabir رضي الله عنه alisema kuwa siku tatu kabla ya kufariki Mtume ﷺ alimsikia akisema;

«لَا يَمُوتَنَّ أَحَدُكُمْ إِلَّا وَهُوَ يُحْسِنُ الظَّنَّ بِاللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Asife mmoja wenu bali awe na dhana nzuri kwa Allah Aliyetukuka, na Kutakasika.”³

Pia Muslim aliinukuu hadithi hii.⁴ Sahih Mbili zilinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«يَقُولُ اللهُ: أَنَا عِنْدَ ظَنِّ عَبْدِي بِي»

“Allah تعالى Anasema, “Mimi nipo kwenye dhana ya mja wangu kwangu.”⁵

Amri ya Kushikamana na Kamba ya Allah تعالى na Umuhimu wa Umoja:

Baadaye Allah تعالى Amesema,

وَأَعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا

“Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane.”

¹ Ahmad 1:300.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 7:307; An-Nasai katika Al-Kubra 6:313; Ibn Majah 2:1446; Ibn Hibban 9:278; Al-Hakim 2:294.

³ Ahmad 3:315.

⁴ Muslim 4:2205.

⁵ Fat’hul Al-Bari 13:395, na Muslim 4:2061

Ilisemwa kuwa maana ya,

يَحْتَبِلُ اللَّهَ

“Kamba ya Mwenyezi Mungu.”

Inahusu ahadi ya Allah تعالى. Kama Alivyosema katika aya ifuatayo,

ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةُ أَيْنَ مَا نُقِفُوا إِلَّا بِحَبْلٍ مِّنَ اللَّهِ وَحَبْلٍ مِّنَ النَّاسِ

“Wamepigwa na udhalili popote wanapokutikana, isipokuwa wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu.”
(3:112)

Kwa Kurejea Ahadi na Mikataba ya Amani, Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تَفَرَّقُوا

“Wala msifarikiane.” Amewaamrisha kuwa wamoja na Amewakataza kutengana. Kuna Hadithi nyingi ambazo zinawataka watu kushikamana katika *Jama'ah* (mkusanyiko wa waumini) na zinakataza mfarakano. Muslim alinukuu kuwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنهما alisema,

«إِنَّ اللَّهَ يَرْضَى لَكُمْ ثَلَاثًا، وَيَسْخَطُ لَكُمْ ثَلَاثًا: يَرْضَى لَكُمْ أَنْ تَعْبُدُوهُ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا، وَأَنْ تَعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا، وَأَنْ تَتَّصِحُوا مَنْ وَّلَاهُ اللَّهُ أَمْرَكُمْ. وَيَسْخَطُ لَكُمْ ثَلَاثًا: قَيْلٌ وَقَالَ، وَكَثْرَةُ السُّؤَالِ، وَإِضَاعَةُ الْمَالِ»

“Allah Anaridhia kwenu matatu, na Anachukia kwenu matatu, Anawaridhia mumuabudu bila Kumshirikisha, na chochote, Na Mshikamane nyote na kamba ya Allah wala msifarikiane, na Mumpe nasaha yeyote aliyechaguliwa na Allah kuwa kiongozi wenu. Na Anachukia kwenu mambo matatu: Unaposema, Ilisemwa, na Fulani alisema (maneno mengi ya porojo), na wingi wa maswali na kupoteza mali.”¹ Kauli Yake Allah تعالى,

وَأَذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا

“Na kumbukeni Neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile mlivyokuwa nyinyi kwa nyinyi maadui Naye Akaziunganisha nyoyo zenu; kwa Neema Yake mkawa ndugu”.

¹ Muslim 3:1340.

Aya hii iliteremshwa kuwahuu Aws na Khazraj katika zama za Jahiliyyah, Aws na Khazraj walikuwa na mapigano ya mara kwa mara enzi za Ujahili, walichukiana, walihasiimiana na wakahisiana vibaya, wakasababisha migongano na vita vikazuka baina yao. Allah تعالى Alipoleta Uislamu, wale waliosilimu walibadilika na kuwa ndugu wanaopendana kwa Rehema za Allah تعالى, wakawa na mshikamano kwa ajili ya Allah تعالى na wakasaidiana kwa uadilifu na ucha Mungu.

Allah تعالى Amesema;

وَإِنْ يُرِيدُوا أَنْ يَخْدَعُوكَ فَإِنَّ حَسْبَكَ اللَّهُ ۗ هُوَ الَّذِي أَيَّدَكَ بِنَصْرِهِ
وَبِالْمُؤْمِنِينَ ۗ وَالْفَ بَيْنَ قُلُوبِهِمْ ۗ لَوْ أَنْفَقْتَ مَا فِي الْأَرْضِ حَمِيعًا مَّا أَلْفَتْ
بَيْنَ قُلُوبِهِمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ أَلْفَ بَيْنَهُمْ ۗ

“Kwani Yeye Ndiye Aliye kuunga mkono kwa Nusura Yake na kwa Waumini. Na Akaziunga nyoyo zao. Na lau wewe ungelitoa vyote viliomo duniani usingeliweza kuziunga nyoyo zao, lakini Mwenyezi Mungu Ndiye Aliyewaunganisha.” (8:62-63)

Mpaka mwisho wa Aya. Kabla ya Uislamu, imani yao ya ukafiri iliwafanya kusimama ukingoni mwa shimo la Moto, lakini Allah تعالى Aliwaokoa kutokana nao kwa kuwaongoza katika imani ya Uislamu. Mtume ﷺ aliwakumbusha Ansar (kutoka Aws na Khazraj) hali yao hiyo waliyokuwa nayo alipokuwa akigawa ngawira za vita vya Hunayn. Wakati huo, baadhi ya Ansar hawakuridhika na mgawanyo wa ngawira, kwa kuwa hawakupata mgao huo. Mtume ﷺ aligawa kwa kufuata maelekezo ya Allah تعالى. Baada ya kujitokeza lawama hizo Mtume ﷺ alitoa hotuba na kusema,

«يَا مَعْشَرَ الْأَنْصَارِ أَلَمْ أَجِدْكُمْ ضَلَّالًا فَهَدَاكُمْ اللَّهُ يَا، وَكُنْتُمْ مُتَفَرِّقِينَ فَأَلْفَمَكُمْ اللَّهُ
يَا، وَعَالَةً فَأَغْنَاكُمْ اللَّهُ يَا؟»

“Enyi kundi la Ansar! Sikuwakuteni katika upotovu Allah تعالى Akawaongozeni kwa sababu yangu? Hamkuwa mmefarakana kabla na Allah تعالى Akawaunganisha kwa sababu yangu? Hamkuwa masikini na Allah تعالى Akakutajirisheni kwa sababu yangu?”

Kila Mtume ﷺ alipouliza swali walijibu, “Kwa hakika Allah تعالى na Mjumbe wake wametukirimu.”¹

وَلَتَكُنَّ مِنْكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى الْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَأُولَئِكَ هُمُ
 الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠١﴾ وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَفَرَّقُوا وَاخْتَلَفُوا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ
 وَأُولَئِكَ هُمُ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٠٢﴾ يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوهٌ وَتَسْوَدُّ وُجُوهٌ فَأَمَّا الَّذِينَ اسْوَدَّتْ
 وُجُوهُهُمْ أَكْفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿١٠٣﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ
 أَبْيَضَتْ وُجُوهُهُمْ فَفِي رَحْمَةِ اللَّهِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١٠٤﴾ تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ تَتْلُوهَا عَلَيْكَ
 بِالْحَقِّ وَمَا اللَّهُ يُرِيدُ ظُلْمًا لِلْعَالَمِينَ ﴿١٠٥﴾ وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَإِلَى اللَّهِ
 تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿١٠٦﴾

104. Na uwe kutokana na nyinyi umma unaolingania kheri na unao amrisha mema na unakataza maovu. Na hao ndio waliofanikiwa.

105. Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kukhitalifiana baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi. Na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa.

106. Siku ambayo nyuso zitanawiri na nyuso zitasawijika. Ama hao ambao nyuso zao zitasawijika wataambiwa: Je! Mlikufuru baada ya kuamini kwenu? Basi onjeni adhabu kwa vile mliyokuwa mnakufuru.

107. Ama wale ambao nyuso zao zitanawiri watakuwa katika Rehema ya Mwenyezi Mungu. Wao humo watadumu.

108. Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu Tunakusomea kwa haki. Na Mwenyezi Mungu Hataki Kuwadhulumu walimwengu.

109. Na kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini ni cha Mwenyezi Mungu; na mambo yote yatarejea kwa Mwenyezi Mungu’.

¹Sahihi Al-Bukhari (4330) na Sahihi Muslim (1061).

Amri ya Kuwaita Watu “Da’wah” kwa Allah

Allah تعالیٰ Amesema,

وَلَتَكُنَّ مِنْكُمْ أُمَّةٌ

“Na uwe kutokana na nyinyi umma”.

Ambao wanalingania katika uadilifu, wanaamrisha yote yaliyo mema, na wanakataza maovu kama Alivyoamrisha Allah تعالیٰ,

وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠١﴾

“Na hao ndio waliofanikiwa”.

Adh-Dhahhak alisema, “Ni kundi maalumu la Masahaba na kundi mahususi la wapokezi baada yao. Ikiwa ni pamoja na Mujahidina na wanazuoni (Ulamaa).”¹

Makusudio ya Ayah hii, ni kuwa lazima liwepo kundi katika Ummah wa Kiislamu la kutekeleza jukumu hili, japokuwa ni wajibu kwa kila mmoja katika Ummah huu, kwa mujibu wa uwezo wake. Muslim alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ رَأَى مِنْكُمْ مُنْكَرًا فَلْيُغَيِّرْهُ بِيَدِهِ، فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِلِسَانِهِ، فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِقَلْبِهِ، وَذَلِكَ أَضْعَفُ الْإِيمَانِ»

“Mwenye kuona uovu, basi abadilisha kwa mkono wake. Iwapo atashindwa basi kwa ulimi wake. Iwapo atashindwa basi kwa moyo wake, na huo ni udhaifu wa imani.”

Katika mapokezi mengine, Mtume ﷺ alisema,

«وَلَيْسَ وَرَاءَ ذَلِكَ مِنَ الْإِيمَانِ حَبَّةُ خَرْدَلٍ»

*“Hapana nyuma ya hapo, hata yenye uzito wa punje ya khardali.”*²

Imamu Ahmad alimnukuu Hudhayfah bin Al-Yaman رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ At-Tabari 7:92.

² Muslim 1:69,70.

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَتَأْمُرُنَّ بِالْمَعْرُوفِ، وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ، أُوْلَئِكَ اللَّهُ أَنْ يَنْعَثَ عَلَيْكُمْ عِقَابًا مِنْ عِنْدِهِ، ثُمَّ لَتَدْعُهُنَّ فَلَا يَسْتَجِيبُ لَكُمْ»

“Naapa kwa Ambaye nafsi yangu imo Mkononi Mwake! Mtaamrisha mema na mtakataza maovu, vinginevyo Allah Atawateremshia adhabu kutoka Kwake. Kisha, Mtamuomba msaada, lakini Hatakubali maombi yenu.”¹

Pia At-Tirmidhi aliipokea Hadithi hii na kuiita, ‘Hasan.’² Kuna hadithi na Aya nyingi juu ya maudhui haya, ambazo zitaelezwa baadaye.

Makatazo Juu ya Mfarakano:

Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ تَفَرَّقُوا وَاخْتَلَفُوا مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَهُمُ الْبَيِّنَاتُ

“Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kukhitalifiana baada ya kuwafikia hoja zilizo wazi.”

Katika Aya hii Allah تعالى Ameukataza Ummah huu kufarakiana na kukhitalifiana kama Mataifa yaliyopita kabla yao. Mataifa hayo yalitelekeza kuamrisha mema na kukataza mabaya, japo walikuwa na ushahidi wa kuwa kufanya hivyo ni wajibu.

Imamu Ahmad alinukuu kuwa Abu Amir Abdullah bin Luhay alisema, “Tulifanya ibada ya Hajj pamoja na Muawiyah bin Abu Sufyan رضي الله عنه. Tulipowasili Makkah, alisimama baada ya kusali Dhuhr na akasema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ أَهْلَ الْكَيْبَاتَيْنِ افْتَرَقُوا فِي دِينِهِمْ عَلَى ثِنْتَيْنِ وَسَبْعِينَ مِلَّةً، وَإِنَّ هَذِهِ الْأُمَّةَ سَتَقْتَرِقُ عَلَى ثَلَاثٍ وَسَبْعِينَ مِلَّةً - يَغْنِي الْأَهْوَاءَ - كُلُّهَا فِي النَّارِ إِلَّا وَاحِدَةً - وَهِيَ الْجَمَاعَةُ - وَإِنَّهُ سَيَخْرُجُ فِي أُمَّتِي أَقْرَامٌ تَجَارِي بِهِمْ تِلْكَ الْأَهْوَاءُ كَمَا يَتَجَارَى الْكَلْبُ بِصَاحِبِهِ، لَا يَبْقَى مِنْهُ عِرْقٌ وَلَا مَفْصِلٌ إِلَّا دَخَلَهُ»

¹ Ahmad 5:38.

² Tuhfatu Al-Ahwadh 6:390.

“Hakika Watu wa Vitabu Viwili (Mayahudi na Manasara) waligawanyika katika mapote sabini na mawili. Ummah huu utagawika katika mapote sabini na matatu, yaani hawaa, yote yataingizwa Motoni isipokuwa moja, nalo ni Jama`ah. Na katika umma wangu kutakuwa na watu ambao matamania yatawalaghai wao, kama mbwa anavyolaghaiwa na anayemfuga; hapana mshipa au kiungo kitakachosalimika, bali kitauingia.”

[Baadaye Muawiyah رضى الله عنه alisema], “Wallahi, Enyi Waarabu! Iwapo nyinyi hamtayafuata yaliyoletwa kwenu na Mtume ﷺ, watu wengine wasiokuwa waarabu hawatoshikamana nayo kabisa.”¹ Hadithi sawa na hiyo ilinukuliwa na Abu Dawud² kutoka kwa Ahmad bin Hanbal na Muhammad bin Yahya.”

Matunda ya Mshikamano na Madhara ya Mfarakano Siku ya Kiyama:

Allah تعالى Amesema,

يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوهٌُ وَتَسْوَدُّ وُجُوهٌُ

“Siku ambayo nyuso zitanawiri na nyuso zitasawijika.”

Siku ya Kufufuliwa, hapa ni pale nyuso za watu wa *Sunnah wal Jam`ah* zitametameta kwa weupe, na nyuso za watu wa Bid`ah na waliofarikiana zitakuwa nyeusi. Aliyeeleza maana hiyo ni Ibn Abbas رضى الله عنهما³ Allah تعالى Amesema,

فَأَمَّا الَّذِينَ أَسْوَدَّتْ وُجُوهُهُمْ أَكْفَرْتُمْ بَعْدَ إِيمَانِكُمْ

“Ama hao ambao nyuso zao zitasawijika wataambiwa: Je! Mlikufuru baada ya kuamini kwenu?”

Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Hao ni wanafiki.”⁴

فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنْتُمْ تَكْفُرُونَ ﴿١٠١﴾

“Basi onjeni adhabu kwa vile mlivyokuwa mnakufuru.”

¹ Ahmad 4:102.

² Abuu Daudi 5:5.

³ Ibn Abu Hatim 2:464.

⁴ Ibn Abuu Hatim 2:465. Isnadi yake ni ya kubuni Taz. “Mizanul Al-Itidali” 3:346.

Na wasifu huu unamstahiki kila Kafiri.

﴿١٧﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ أَبْيَضَتْ وُجُوهُهُمْ فِى رَحْمَةِ اللَّهِ هُمْ فِىهَا خَالِدُونَ

“Ama wale ambao nyuso zao zitanawiri watakuwa katika rehema ya Mwenyezi Mungu. Wao humo watadumu.”

Peponi ambapo wataishi milele na hawatotamani kuondolewa.

Abu Isa At-Tirmidhi katika kuitafsiri Aya hii, alinukuu kutoka kwa Abuu Ghalib alisema, Abu Umamah رضى الله عنه aliona vichwa (vya watu wa madhehebu ya *Khawarij*) vimening'inizwa katika mitaa ya Damascus.¹ Alitoa maoni kwa kusema, “Mbwa wa Motoni ni watu wabaya waliouwawa chini ya mbingu. Watu wazuri waliokufa ni wale waliowaua hawa.” Kisha akasema,

يَوْمَ تَبْيَضُّ وُجُوهٌُ وَتَسْوَدُّ وُجُوهٌُ

“Siku ambayo nyuso zitanawiri na nyuso zitasawijika.”

Mpaka mwisho wa Aya. Nilimuambia Abu Uma'ma رضى الله عنه, “Je, uliyasikia haya kutoka kwa Mjumbe wa Allah?” Alijibu, “Kama nisingemsikia Mtume ﷺ mara moja, mbili, tatu, nne, alihasabu mpaka mara saba, nisingewasimulia.” At-Tirimidhi alisema, “Hadithi hii ni Hasan.”² Ibn Majah na Ahmad walinukuu kama hivyo hivyo.³ Kisha Allah تعالى Akasema,

تِلْكَ آيَاتُ اللَّهِ تَتْلُوهَا عَلَيْكَ

“Hizi ni Aya za Mwenyezi Mungu ? Tunakusomea.”

Maana yake: “Hizi ni Aya za Allah تعالى, Ushahidi Wake na dalili ambazo Tunakuteremshia, Ewe Muhammad.”

بِالْحَقِّ

“Kwa haki.” Inayofanya kufahamika ukweli halisi wa dunia na kiyama,

﴿١٨﴾ وَمَا اللَّهُ يُرِيدُ ظُلْمًا لِّلْعَالَمِينَ

“Na Mwenyezi Mungu Hataki Kuwadhulumu walimwengu.”

¹ At-Tabarani 8:267. Pia Musnadi wa Ahmad 5:253.

² Tuhfatu Al-Ahwadhi 8:351.

³ Ibn Maja 1:62 na Ahmad 5:256.

Ni kweli Allah تعالى si Mwenye kuwadhulumu bali, Yeye ni Mtawala Muadilifu Ambaye Ana Uwezo wa kufanya kila kitu, Mwenye Ilimu ya kila kitu. Hivyo, Hahitaji Kudhulumu viumbe Wake, na kwa sababu hii Alisema baada ya hapo,

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ

“Na kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini ni cha Mwenyezi Mungu”.

Wote ni waja Wake na ni milki Yake,

وَاللّٰهُ تَرْجِعُ الْاُمُوْرَ

“Na mambo yote yatarejea kwa Mwenyezi Mungu”.

Kwa hiyo Yeye Ndiye Muamuzi kuhusu mambo ya maisha ya dunia na ya akhera, na Yeye Ndiye Mwenye Mamlaka ya juu kabisa ya dunia na akhera.

* * *

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ
 وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَوْ ءَامَنَ أَهْلُ
 الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ مِمَّنْهُمُ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمْ
 الْفَاسِقُونَ ﴿١١٠﴾ لَنْ يَضُرُّوكُمْ إِلَّا أَذًى ط وَإِنْ يُقْتَلُوا
 يُولُوكُمْ الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُبْصَرُونَ ﴿١١١﴾ ضَرَبْتَ عَلَيْهِمْ
 الذِّلَّةَ أَيْنَ مَا تَفَقَّهُوا إِلَّا يَحْتَلِرُ مِنَ اللَّهِ وَحَتَلِرُ مِنَ النَّاسِ
 وَبَاءَ وَبِغَضِبِ مِنَ اللَّهِ وَضَرَبْتَ عَلَيْهِمُ الْمَسْكَتَةَ ذَٰلِكَ
 بِأَنَّهُمْ كَانُوا يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ
 حَقِّ ذَٰلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿١١٢﴾ * لَيْسُوا
 سَوَاءً ط مِنَ أَهْلِ الْكِتَابِ أُمَّةٌ قَائِمَةٌ يَتْلُونَ آيَاتِ اللَّهِ ءَانَاءَ
 اللَّيْلِ وَهُمْ يَسْجُدُونَ ﴿١١٣﴾ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ
 وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُسْرِعُونَ
 فِي الْخَيْرَاتِ وَأُولَٰئِكَ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١١٤﴾ وَمَا يَفْعَلُوا مِنْ
 خَيْرٍ فَلَنْ يُكْفَرُوهُ وَاللَّهُ عَلَيْهِمُ بِالْمُتَّقِينَ ﴿١١٥﴾

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ
 تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ
 الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ * وَلَوْ
 ءَامَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْرًا
 لَهُمْ مِمَّنْهُمُ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمْ
 الْفَاسِقُونَ ﴿١١٠﴾ لَنْ يَضُرُّوكُمْ إِلَّا
 أَذًى ط وَإِنْ يُقْتَلُوا يُولُوكُمْ
 الْأَدْبَارَ ثُمَّ لَا يُبْصَرُونَ ﴿١١١﴾
 ضَرَبْتَ عَلَيْهِمُ الذِّلَّةَ أَيْنَ مَا تَفَقَّهُوا
 إِلَّا يَحْتَلِرُ مِنَ اللَّهِ وَحَتَلِرُ مِنَ النَّاسِ
 وَبَاءَ وَبِغَضِبِ مِنَ اللَّهِ وَضَرَبْتَ عَلَيْهِمُ
 الْمَسْكَتَةَ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا
 يَكْفُرُونَ بِآيَاتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ
 الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقِّ ذَٰلِكَ بِمَا
 عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿١١٢﴾

110. "Nyinyi mmekuwa bora ya umma waliotolewa kwa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa Watu wa Kitabu nao wameamini ingekuwa bora kwao. Wapo miongoni mwao waumini, lakini wengi wao wapotovu.

111. Maadui hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na tena hawatanusuriwa.

112. Wamepigwa na udhalili popote wanapokutwa, ila wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu. Na wakastahiki ghadhabu ya

Mwenyezi Mungu, na wamepigwa na unyonge. Hayo ni kwa sababu walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakiwaua Manabii pasina haki; hayo ni kwa sababu waliasi na walikuwa wakiruka mipaka”.

Ubora wa Ummah wa Muhammad ﷺ kwa zama zote

Allah تعالیٰ Anaeleza kuwa Ummah huu wa Muhammad ﷺ ndio Bora ya Ummah zingine. Allah تعالیٰ Alisema;

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

“Nyinyi mmekuwa bora ya umma waliotolewa kwa watu.” Bukhari alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alitoa maoni juu ya Aya hii, “(Nyie Waislamu, ni) ummah bora kuliko ummah zote, unawaleta huku wamefungwa minyororo shingoni (wameshikwa katika vita) na baadaye kusilimu.”¹ Hadithi sawa na hiyo ilisemwa na Ibn Abbas, Mujahid, Atiyah, Al-Awf, Ikrimah, Ataa na Ar-Rabi bin Anas رضي الله عنهم kuwa,

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ

“Nyinyi mmekuwa bora ya umma waliotolewa kwa watu.” Maana yake: Watu bora kuliko watu wengine.² Maana ya Aya ni kuwa Ummah wa Muhammad ﷺ, ni waadilifu zaidi na ni watu wenye manufaa kwa watu wengine. Hivyo aliwaelezea sifa zao,

تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ

“Kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu”.

Ahmad, At-Tirmidhi, Ibn Majah, na Al-Hakim wamemnukuu Hakim bin Muawiyah bin Haydah alisimulia kuwa baba yake alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَنْتُمْ تُؤْفُونَ سَبْعِينَ أُمَّةً، أَنْتُمْ خَيْرُهَا، وَأَنْتُمْ أَكْرَمُ عَلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

“Nyie mnatosheleza mataifa sabini, nyie ni wabora wao, na nyie ni watukufu zaidi mbele ya Allah.”³

¹ Fat’h Al-Bari 8:72.

² Ibn Abu Hatim 2:472,473.

³ Ahmad 5:3 na Tuhfat Al-Ahwadhi 8:352 na Ibn Majah 2:1433.

Hii ni Hadithi mashuhuri ambayo Tirmidhi alilitaja kuwa 'Hassan' na ambayo pia ilipokelewa kutoka kwa Mu`adh bin Jabal na Abu Said رضي الله عنهما. Ummah wa Muhammad ﷺ ulifikia kiwango hicho cha kheri kwa sababu ya Mtume wake, Muhammad ﷺ kiumbe wa Allah تعالى anayeheshimika zaidi na Mtume aliyetukuzwa na Allah تعالى. Allah تعالى Alimtuma Muhammad ﷺ na sharia iliyokamilika ambayo hakupewapo Mtume mwingine au Mjumbe kabla yake. Katika sharia ya Muhammad ﷺ amali chache zinachukua nafasi za amali nyingi ambazo mataifa mengine walitenda. Kwa mfano, Imamu Ahmad alinukuu kuwa Ali bin Abu Talib رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alisema,

«أَعْطَيْتُ مَا لَمْ يُعْطَ أَحَدٌ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ»

"Nilipewa ambacho hakupewa yoyote miongoni mwa mitume kabla yangu."

Tukauliza, "Ewe Mjumbe wa Allah! Nini hicho?" Akatujibu,

«نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ، وَأَعْطَيْتُ مَفَاتِيحَ الْأَرْضِ، وَسُمِّيتُ أَحْمَدَ، وَجُعِلَ التُّرَابُ لِي طَهُورًا، وَجُعِلَتْ أُمَّتِي خَيْرَ الْأُمَّةِ»

"Nilipewa ushindi kwa hofu. Nilipewa funguo za ardhi. Niliitwa Ahmad. Ardhi ilifanywa kitoharisho changu, (kwa kuswalia na kutayamamu kwayo) na Ummah wangu ulifanywa ummah bora."¹

Isnadi ya Hadithi hii ni Hasan. Kuna Hadithi nyingi ambazo tutazitaja hapa. Sahihi mbili zilinukuu kutoka kwa Az-Zuhri kutoka kwa Said bin Al-Musayyib alisema kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alimsimulia alisema, "Nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

«يَدْخُلُ الْجَنَّةَ مِنْ أُمَّتِي زُمْرَةٌ وَهُمْ سَبْعُونَ أَلْفًا، نُصِيءُ وَجُوهُهُمْ إِضَاءَةٌ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ» فقال أبو هريرة: فقام عكاشة بن محصن الأسدي يرفع نمرة عليه، فقال: يا رسول الله، ادع الله أن يجعلني منهم، فقال رسول الله ﷺ: «اللَّهُمَّ اجْعَلْهُ مِنْهُمْ» ثم قام رجل من الأنصار فقال: يا رسول الله! ادع الله أن يجعلني منهم، فقال: «سَبَقَكَ بِهَا عُكَّاشَةُ»

¹ Ahmad 1:98.

“Kundi la watu elfu sabini katika Ummah wangu wataingia Peponi, huku nyuso zao zikimetameta kama mwezi mpevu,” Abu Hurairah akaendelea kusema: “Ukasha bin Mihsani Al-Asadi alisimama na kusema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Muombe Allah niwe mmoja wao.” Mtume akasema, “Ewe Mwenyezi Mungu! Mjaalie awe ni miongoni mwao,” Mtu mmoja katika Ansar pia akasimama na kusema, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Muombe Allah niwe mmoja wao.’ Mtume akasema, ‘Ukasha amekulia kwa hilo (yaani amekutangulia).”¹

Hadithi Zingine Zinazoonisha Uboru wa Ummah huu wa Muhammad ﷺ, Pamoja na Utukufu Wake kwa Allah تعالى na Kwamba ndio Ummah bora Duniani na Akhera

Imamu Ahmad alinukuu kutoka kwa Ja'bir رضي الله عنه kwamba yeye, “Alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنِّي لَأَرْجُو أَنْ يَكُونَ مَنْ يَتَّبِعُنِي مِنْ أُمَّتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ رُبْعَ الْجَنَّةِ» قال: فكبرنا، ثم قال: «أَرْجُو أَنْ يَكُونُوا ثُلُثَ النَّاسِ» قال: فكبرنا، ثم قال: «أَرْجُو أَنْ تَكُونُوا الشُّطْرَةَ»

“Hakika mimi nataraji ya kuwa wale watakaonifuata katika umma wangu watakuwa robo ya wakazi wa Peponi. Tukasema ‘Allahu Akbar.’ Kisha akasema, “Nataraji watakuwa theluthi ya watu.” Tukasema, ‘Allahu Akbar’ Kisha akasema, “Nataraji mtakuwa nusu.”²

Imamu Ahmad aliinukuu Hadithi hii kwa isnadi nyingine ya upokezi,³ na Hadithi hii imefikia vigezo vya Muslim katika *Sahih* yake. Katika *Sahih* Mbili, ilinukuliwa kuwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alisema, “Mtume ﷺ alituambia,

«أَمَا تَرْضَوْنَ أَنْ تَكُونُوا رُبْعَ أَهْلِ الْجَنَّةِ؟»

“Je, Mnaridhia kuwa robo ya watu wa peponi?”

Tukasema, ‘Allahu Akbar! Akaongeza,

¹ Fat'hul Al-Bari 11:134 na Muslim 1:197.

² Ahmad 3:346.

³ Ahmad 3:383.

«أَمَا تَرْضَوْنَ أَنْ تَكُونُوا تُلَّتْ أَهْلُ الْجَنَّةِ؟»

"Je, Mnaridhia kuwa theluthi ya watu wa Peponi?"

Tukasema, *Allahu Akbar!* Akasema,

«إِنِّي لَأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا شَطْرَ أَهْلِ الْجَنَّةِ؟»

"Nataraji mtakuwa nusu ya watu wa Peponi."¹

Hadithi nyingine, Imamu Ahmad alinukuu kuwa Buraydah رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَهْلُ الْجَنَّةِ عَشْرُونَ وَمِائَةٌ صَفٌّ، هَذِهِ الْأُمَّةُ مِنْ ذَلِكَ تَمَانُونَ صَفًّا»

"Watu wa Peponi wako katika safu mia na ishirini, Ummah huu utachukua themanini kati ya hizo."²

Pia Imamu Ahmad alikusanya Hadithi hii kupitia isnadi ya upokezi tofauti.³ At-Tirmidhi alikusanya Hadithi hii, na akasema, "Hadithi hii ni *Hasan*."⁴ Ibn Majah pia aliandika.⁵

Abdur-Razzaq alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضى الله عنه alisema kuwa, Mtume ﷺ alisema,

«نَحْنُ الْأَجْرُونَ الْأَوَّلُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، نَحْنُ أَوَّلُ النَّاسِ دُخُولًا الْجَنَّةَ، يَبْدَأُ نَهْمٌ أَوْتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِنَا وَأَوْتِنَاهُ مِنْ بَعْدِهِمْ، فَهَدَانَا اللَّهُ لِمَا اخْتَلَفُوا فِيهِ مِنَ الْحَقِّ، فَهَذَا الْيَوْمُ الَّذِي اخْتَلَفُوا فِيهِ، النَّاسُ لَنَا فِيهِ بَيْعٌ، غَدَاً لِلْيَهُودِ، وَلِلنَّصَارَى بَعْدَ غَدِي»

"Sisi (Waislamu) ni wa mwisho wa mwanzo siku ya Kiyama, na watu wa mwanzo kuingizwa Peponi, japokuwa mataifa yaliyotangulia yalipewa Vitabu kabla yetu na sisi baada yao. Allah Alituongoza kwenye haki ambayo wao walitofautiana. Kwa hii siku ambayo

¹ Fat'hul Al-Bari 11:385 na Muslim 1:200.

² Ahmad 5:355.

³ Ahmad 5:347.

⁴ Tuhfat Al-Ahwadhi 7:256.

⁵ Ibn Majah 2:134.

walitofautiana ndani yake, na watu wote wanatuunga mkono katika hili, kesho ni ya Mayahudi (Jumamosi) na Wakristo ni kesho kutwa (Jumapili)."

Bukhari na Muslim walikusanya Hadithi hii.¹ Muslim alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«نَحْنُ الْأَجْرُونَ الْأَوَّلُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، نَحْنُ أَوَّلُ مَنْ يَدْخُلُ الْجَنَّةَ»

"...Sisi (Waislamu) ni wa mwisho (kuja), lakini (tutakuwa) wa mwanzo Siku ya Kiyama, sisi ni wa watu wa kwanza kuingia Peponi..."

Mpaka mwisho wa Hadithi.² Hadithi hizi na nyingine zinakubali maana ya Aya,

كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ
بِاللَّهِ

"Nyinyi mmekuwa bora ya umma waliotolewa kwa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu". (3:110)

Kwa hiyo, yeyote miongoni mwa Ummah mwenye sifa hizi, atakuwa pamoja nao katika wasifu huu. Qatadah alisema, tuliambiwa kuwa Umar bin Al-Khattab رضى الله عنه alikwenda Hajj na kuwaona watu wanafanya haraka, aliisoma Aya hii, kisha alisema, "Yeyote anayependa kuwa miongoni mwa Ummah huu, basi atekeleze masharti yaliyowekwa na Allah تعالى katika Aya hii."³ Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliandika Hadith hii. Watu miongoni mwa Ummah huu ambao hawatafikia sifa hizi, watakuwa kama watu wa Kitabu ambao walikosolewa na Allah تعالى, Aliposema,

كَانُوا لَا يَتَنَاهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ فَعَلُوهُ

"Walikuwa hawakatazani maovu waliyokuwa wakiyafanya". (5:79)

¹ Al-Bukhari 896, 3486,3487 na Muslim 855.

² Muslim 855.

³ At-Tabari 7:102 Isnadi yake ni dhaifu.

Hii ndiyo sababu iliyosababisha Allah تعالى Kuupamba Ummah wa Kiislamu na sifa Alizozitaja. Aliwakosoa Watu wa Kitabu na Akawafanyia istihizai, Akisema,

وَلَوْءَا مَنَّ أَهْلُ الْكِتَابِ

“Na lau kuwa Watu wa Kitabu, nao wameamini”.

Kitabu kile alichoteremshiwa Muhammad ﷺ,

لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ مِّنْهُمْ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ الْفَاسِقُونَ ﴿١١٠﴾

“Ingelikuwa bora kwao. Wapo miongoni mwao waumini, lakini wengi wao wapotovu”.

Kwa hiyo wachache tu ndio wanao muamini Allah تعالى na katika kile kilichoteremshwa kwenu na kilichoteremshwa kwao. Wengi wao wanafuata upotofu, ukafiri na maasi.

Bishara Njema kwa Waislamu ya Kupata Ushindi na Nusra juu ya Mayahudi na Wakristo (Ahlul Kitab)

Allah تعالى Anawaeleza khabari njema waja Wake waumini kuwa ushindi na utawala utakuwa wao dhidi ya makafiri, watu wa Kitabu na mushirikina, Allah تعالى Alisema,

لَنْ يَضُرُّكُمْ إِلَّا أذىٌ ۖ وَإِنْ يُقْتَلُواكُمْ يُؤَلُّوْكُمْ أَلَدْبَارًا ثُمَّ لَا يُنصَرُونَ ﴿١١١﴾

“Maadui hawatakudhuruni ila ni maudhi tu. Na wakipigana nanyi watakupeni mgongo, na tena hawatanusuriwa”.

Haya ndiyo yaliyojiri katika vita vya Khaybar, Allah تعالى Aliwadhalilisha na kuwaaibisha Mayahudi. Kabla ya hapo, Mayahudi wa Madinah, makabila ya Qaynuqa, Nadhir na Quraydhah nao walifedheheshwa na Allah تعالى. Hali hiyo pia iliwapata Wakristo baadaye katika maeneo ya Shamu mpaka hapo Isa عليه السلام, mwana wa Maryam, atakaposhuka wakiwa katika hali hii (juu ya ukweli, ulio wazi na ushindi). Isa عليه السلام ataongoza wakati huo kwa Sharia ya Muhammad ﷺ atavunja msalaba, ataua Nguruwe, kufuta Jizya na kuridhia Uislam peke yake. Kisha Allah تعالى Amesema,

ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الذَّلِيلَةُ أَيْنَ مَا تُقِفُوا إِلَّا بِحَبْلِ مِنَ اللَّهِ وَحَبْلِ مِنَ النَّاسِ

“Wamepigwa na udhalili popote wanapokutwa, isipokuwa wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu”.

Maana yake: Allah تعالى Amewadhhalilisha na Kuwafedhehesha popote watakapokuwa, na hawatasalimika kamwe,

إِلَّا بِحَبْلِ مِنَ اللَّهِ

“Isipo kuwa wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu”.

Maana yake: Chini ya *Dhimmah* kutoka kwa Allah تعالى ambayo inawataka kulipa Jizya (kodi kwa Waislamu) na kuwafanya kuwa watiifu wa sheria ya Kiislamu.

وَحَبْلِ مِنَ النَّاسِ

“Na kamba ya watu”.

Maana yake: Ahadi kutoka kwa watu, kama ahadi ya ulinzi na usalama kutoka kwa watu, kama ilivyo katika mikataba na mateka pindi wakipewa ahadi ya usalama kwa mmojawapo wa Waislamu, japo mwanamke, kadhalika mtumwa, kutokana na moja ya kauli za maulamaa. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa, Kauli ya Allah تعالى

إِلَّا بِحَبْلِ مِنَ اللَّهِ وَحَبْلِ مِنَ النَّاسِ

“Isipo kuwa wakishika kamba ya Mwenyezi Mungu na kamba ya watu.”

Maana yake ni: “Kwa ahadi ya kutoka kwa Allah تعالى na ya kutoka kwa watu.”¹ Maneno sawa na haya yalisemwa na Mujahid, Ikrimah, Ata Adh - Dhahhak, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi na Ar-Rabi bin Anas.² Kauli ya Allah تعالى,

وَيَأْتُو بِغَضَبٍ مِنَ اللَّهِ

“Na wakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Wamekasirikiwa na Allah تعالى, ambayo ni stahili yao.

¹ At-Tabari 7:112.

² Ibn Abu Hatim 2:480 - 481.

وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ الْمَسْكَنَةُ

“Na wamepigwa na unyonge.”

Maana yake: Walistahiki kwa amri na sharia. Baadaye Allah تعالى Amesema,

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَانُوا يَكْفُرُونَ بِغَايَتِ اللَّهِ وَيَقْتُلُونَ الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقِّ

“Hayo ni kwa sababu walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakiwaua Manabii pasina haki.”

Maana yake: Kilichowafanya kufikia hapo ni ukorofi, upinzani na husuda, ndio maana malipo yao yakawa kudhalilishwa, kufedheheshwa katika maisha yote ya dunia na akhera. Allah تعالى Amesema,

ذَٰلِكَ بِمَا عَصَوْا وَكَانُوا يَعْتَدُونَ ﴿١١٠﴾

“Hayo ni kwa sababu waliasi na walikuwa wakiruka mipaka”.

Maana yake: Kilichowafanya wazikane Aya za Allah تعالى na kuwaua Mitume Wake, ni ukweli kuwa walizidisha maasi kwa kufanya aliyoyaharamisha na wakachupa mipaka katika sharia za Allah تعالى. Tunamuomba Allah تعالى Atuhifadhi na mwenendo kama huu, na Allah Ndiye Anayeombwa msaada.

* * *

* لَيْسُوا سَوَاءً ۗ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ أُمَّةٌ قَائِمَةٌ يَتْلُونَ آيَاتِ
 اللَّهِ ءِانَاءَ اللَّيْلِ وَهُمْ يَسْجُدُونَ ﴿١١٦﴾ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ
 وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ
 وَيُسْرِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ وَأُولَئِكَ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١١٧﴾
 وَمَا يَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَلَنْ يُكْفَرُوهُ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْمُتَّقِينَ
 ﴿١١٨﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَنْ تُغْنِيَ عَنْهُمْ أَمْوَالُهُمْ وَلَا
 أَوْلَادُهُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا ۗ وَأُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا
 خَالِدُونَ ﴿١١٩﴾ مَثَلُ مَا يُنْفِقُونَ فِي هَذِهِ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا
 كَمَثَلِ رِيحٍ فِيهَا صِرٌّ أَصَابَتْ حَرْثَ قَوْمٍ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ
 فَأَهْلَكَتَهُ ۗ وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّهُ وَلَٰكِن أَنفُسُهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١٢٠﴾
 يٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا بَطَانَةً مِّنْ دُونِكُمْ لَا
 يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُؤًا مَا عَيْتُمْ قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَاءُ مِنْ
 أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ ۗ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ ۗ
 إِن كُنتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١٢١﴾ هَتَأْتُمْ أُولَاءَ يُحِبُّوهُمْ وَلَا يُحِبُّونَكُمْ
 وَتُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ كُلِّهِ وَإِذَا لُفُوكُمْ قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَوْا
 عَضُّوا عَلَيْكُمُ الْأَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ ۗ قُلْ مُوتُوا بِغَيْظِكُمْ ۗ إِنَّ
 اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١٢٢﴾ إِن تَمَسَّكُمُ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ
 وَإِن تُصِيبْكُمْ سَيِّئَةٌ يَفْرَحُوا بِهَا ۗ وَإِن نَّصِرُوا وَتَوَقَّعُوا لَا
 يَضُرُّكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا ۗ إِنَّ اللَّهَ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿١٢٣﴾

* لَيْسُوا سَوَاءً ۗ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ أُمَّةٌ
 قَائِمَةٌ يَتْلُونَ آيَاتِ اللَّهِ ءِانَاءَ اللَّيْلِ
 وَهُمْ يَسْجُدُونَ ﴿١١٦﴾ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ
 وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ
 وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُسْرِعُونَ فِي
 الْخَيْرَاتِ وَأُولَئِكَ مِنَ الصَّالِحِينَ
 ﴿١١٧﴾ وَمَا يَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَلَنْ
 يُكْفَرُوهُ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْمُتَّقِينَ
 ﴿١١٨﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَنْ تُغْنِيَ
 عَنْهُمْ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ مِنَ اللَّهِ
 شَيْئًا ۗ وَأُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۗ هُمْ فِيهَا
 خَالِدُونَ ﴿١١٩﴾ مَثَلُ مَا يُنْفِقُونَ فِي
 هَذِهِ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَثَلِ رِيحٍ
 فِيهَا صِرٌّ أَصَابَتْ حَرْثَ قَوْمٍ ظَلَمُوا
 أَنفُسَهُمْ فَأَهْلَكَتَهُ ۗ وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّهُ
 وَلَٰكِن أَنفُسُهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١٢٠﴾

113. Wote hao si sawa sawa. Miongoni mwa Watu wa Kitabu wamo watu waliosimama baraabara, wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku, na pia wanasujudu.

114. Wanamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wanaamrisha mema na wanakataza maovu na wanakimbilia katika mambo ya kheri. Na hao ndio miongoni mwa watenda mema.

115. Na kheri yoyote wanayoifanya hawatanyimwa malipo yake. Na Mwenyezi Mungu Anawajua wachamungu.

116. Hakika wale waliokufuru hazitawafaa kitu mali zao wala watoto wao mbele ya Mwenyezi Mungu Na hao ndio watu wa Motoni - humo watadumu.

117. Mfano wa vile wanavyovitoa katika uhai wao wa duniani ni kama upepo ambao ndani yake ipo baridi ya barafu, ukalisibu shamba la watu waliodhulumu nafsi zao, ukaliteketeza. Na Mwenyezi Mungu Hakuwadhulumu, bali wao wenyewe wanadhulumu nafsi zao.

Ubora wa Waliosilimu katika Ahlul Kitab

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى na wengineo, ikiwa ni pamoja na Al-Awfi ambaye alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, alisema; Aya hizi ziliteremshwa kuhusu viongozi katika Watu waliopewa Kitabu waliosilimu. Kwa mfano: kuna Abdullah bin Salam, Asad bin Ubayd, Tha'labah bin Sa'yah, Usayd bin Sa'yah, na wengine. Aya hii inamaanisha kwamba wale miongoni mwa Watu wa Kitabu waliokaripiwa na Allah تعالى mwanzoni si sawa na wale Waliosilimu. Ndio maana Allah تعالى Akasema,

❖ لَيْسُوا سَوَاءً

“Wote hao si sawa sawa.” (3:13).¹

Wote hawalingani, na kwa hakika, kuna waumini na pia kuna waasi miongoni mwao, kama Allah تعالى Alivyosema,

مِنَ أَهْلِ الْكِتَابِ أُمَّةٌ قَائِمَةٌ

“Miongoni mwa Watu wa Kitabu wamo watu waliosimama baraabara.”

¹ Al-Muharrirul-Wajiz 1:492.

Wanatekeleza amri zilizomo ndani ya kitabu cha Allah تعالى, wanashikamana na Sharia Zake na wanamfuata Mtume Wake Muhammad ﷺ. Kwa hiyo aina hii ya watu iko katika mstari ulionyooka,

يَتْلُونَ آيَاتِ اللَّهِ ءَانَاءَ اللَّيْلِ وَهُمْ يَسْجُدُونَ ﴿١١٦﴾

“Wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku, na pia wanasujudu.”

Husimama usiku kwa ajili ya *Tahajjud*, na wanasoma Qur'an katika Swala zao,

يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَيَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُسْرِعُونَ
فِي الْخَيْرَاتِ وَأُولَئِكَ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿١١٧﴾

“Wanamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wanaamrisha mema na wanakataza maovu na wanakimbilia katika mambo ya kheri. Na hao ndio miongoni mwa watenda mema”.

Hii ndio aina ile ile ya watu waliotajwa mwishoni mwa Sura;

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِمْ خَشِيعِينَ لِلَّهِ

“Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu wapo wanaomuamini Mwenyezi Mungu na yaliyoteremshwa kwenu na yaliyoteremshwa kwao, wakimnyenyekea Mwenyezi Mungu.” (3:199)

Ndio maana Allah تعالى Amesema hapa:

وَمَا يَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَلَنْ يُكْفَرُوهُ

“Na kheri yoyote wanayoifanya hawatanyimwa malipo yake”. Maana yake: Allah تعالى Hatozipoteza amali zao njema. Bali Atawalipa malipo bora kabisa.

وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِالْمُتَّقِينَ ﴿١١٨﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anawajua wachamungu”. Kwani hapana amali ya mtu yeyote Asiyofahamu, wala hapana amali njema ambayo itapotea. Allah تعالى Anawataja wapagani wasioamini kwa Kusema:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا لَنْ تُغْنِيَ عَنْهُمْ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا

“Hakika wale waliokufuru hazitawafaa kitu mali zao wala watoto wao mbele ya Mwenyezi Mungu”

Maana yake: Hakuna kitakachobadilisha mateso na adhabu ya Allah تعالى kuwafikia iwapo atataka kuwaadhibu,

وَأُولَئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١١٦﴾

“Na hao ndio watu wa Motoni - humo watadumu.”

Ubainifu wa Hatima ya Sadaqa za Makafiri:

Baada ya hapo, Allah تعالى Alipiga mfano wa kile wanachokitoa makafiri katika maisha ya dunia, kama walivyosema Mujahid, Al-Hasan na As-Suddi.¹

Allah تعالى Alisema;

مَثَلُ مَا يُنْفِقُونَ فِي هَذِهِ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَثَلِ رِيحٍ فِيهَا صِرٌّ

“Mfano wa vile wanavyovitoa katika uhai wao wa duniani ni kama upepo ambao ndani yake ipo baridi ya barafu”.

Maana yake ni: Upepo wenye baridi kali, kama walivyosema, Ibn Abbas, Ikrimah, Said bin Jubayr, Al-Hasan, Qatadah, Adh-Dhahak, Ar-Rabi bin Anas na wengineo رضي الله عنهم.² Ata alisema kuwa maana yake ni baridi na theluji.³ Ibn Abbas na Mujahid pia wanasimulia kuwa, “swirrun” maana yake ni ‘moto’.⁴ Hii maana ya mwisho haipingani na maana tulizozitaja hapo juu, kwa sababu hali ya ubaridi mkali, hasa inapoambatana na theluji, huchoma mimea na mazao, na kuleta athari sawa na ya moto katika mimea.

أَصَابَتْ حَرْثَ قَوْمٍ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ فَأَهْلَكَتَهُ

“Ukalisibu shamba la watu waliodhulumu nafsi zao, ukaliteketeza.”
(3:117)

¹ Ibn Abu Hatim 2:493.

² Ibn Abu Hatim 2:494, 495.

³ Ibn Abu Hatim 2:496.

⁴ Ibn Abu Hatim 2:495.

Kwa kuliunguza. Aya hii inataja maafa yanayoyafika mazao yaliyo tayari kuvunwa, inayaangamiza kwa kuyachoma na kumnyima mwenyewe wakati anayahitaji sana. Hii ni sawa na hali ya makafiri, kwani Allah تعالى Huyaharibu malipo ya amali zao njema hapa duniani, kama Anavyoangamiza mazao ya mkosaji kwa sababu ya dhambi zake. Hivyo kazi zao hazikujengwa juu ya msingi imara,

﴿١١٧﴾ وَمَا ظَلَمَهُمُ اللَّهُ وَلَٰكِن أَنفُسُهُمْ يَظْلِمُونَ

“Na Mwenyezi Mungu hakuwadhulumu, bali wao wenyewe wanadhulumu nafsi zao.” (3:117)

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا بَطَانَةً مِّن دُونِكُمْ لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُؤًا مَا عَيْنُكُمْ قَدِ بَدَتِ
 الْبَغْضَاءَ مِّنْ أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ إِن كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ
 ﴿١١٨﴾ هَتَأْتُمْ أُوْلَاءَ يُحِبُّوهُمْ وَلَا يُحِبُّونَكُمْ وَتُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ كُلِّهِ وَإِذَا لَقُوكُمْ قَالُوا ءَامَنَّا
 وَإِذَا خَلَوْا عَضُوا عَلَيْكُمُ الْآتَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ قُلْ مُوتُوا بِغَيْظِكُمْ إِنَّا اللَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ
 الصُّدُورِ ﴿١١٩﴾ إِن مَّمَسَّكُمْ حَسَنَةٌ تَسُؤْهُمْ وَإِن تُصِبْكُمْ سَيِّئَةٌ يَفْرَحُوا بِهَا وَإِن تَصَبَرُوا
 وَتَتَّقُوا لَا يَضُرُّكُمْ كَيْدُهُمْ شَيْئًا إِنَّا اللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطٌ ﴿١٢٠﴾

118. Enyi mlioamini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi. Hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yanayokudhuruni. Imekwishafichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayoficha vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekwisha kubainishieni Ishara ikiwa nyinyi mtayatia akilini.

119. Hivyo basi nyinyi ndio mnawapenda watu hao, wala wao hawakupendeni. Nanyi mnaviamini Vitabu vyote. Na wanapokutana nanyi husema: Tumeamini. Na wanapokuwa peke yao wanakuumieni vidole kwa chuki. Sema: Kufeni kwa chuki yenu!

120. Hakika Mwenyezi Mungu Anayajua yaliomo vifuani. Ikikupateni kheri huwaudhi. Na ikikupateni shari wanafurahia. Na nyinyi mkisubiri na mkajizuilia, hila zao hazitakudhuruni kitu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyazunguka yote wayatendayo.

Kukatazwa Kuwafanya Makafiri Kuwa Marafiki Vipenzi

Allah تعالى Amewaharamishia waja wake waumini kuwafanya wanafiki kuwa washauri wao, wanawaambia siri zao na yale wanayoyapanga dhidi ya adui zao. Wanafiki wanajaribu kwa kadri ya uwezo wao kuleta mkanganyiko kwa kuwapinga na kutafuta namna ya kuwadhuru waumini kwa njia yoyote wawezayo, kwa kutumia uovu, na njia batili walizo nazo. Wanawatakia waumini hali mbaya na maisha magumu. Allah تعالى Amesema,

لَا تَتَّخِذُوا بِطَانَةَ مِّن دُونِكُمْ

“Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi.” Maana yake: Msiwafanye wafuasi wa dini nyingine kuwa waelekezaji na washauri. Msiri wa mtu ni yule ambaye anaweza kuzifikia siri zake za ndani kabisa. Bukhari na An-Nasai na wengineo walimnukuu Abu Said رضي الله عنه akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا بَعَثَ اللَّهُ مِنْ نَبِيٍّ وَلَا اسْتَخْلَفَ مِنْ خَلِيفَةٍ إِلَّا كَانَتْ لَهُ بِطَانَتَانِ: بِطَانَةٌ تَأْمُرُهُ بِالْخَيْرِ وَتَحُضُّهُ عَلَيْهِ، وَبِطَانَةٌ تَأْمُرُهُ بِالسُّوءِ وَتَحُضُّهُ عَلَيْهِ، وَالْمَعْصُومُ مَنْ عَصَمَ اللَّهُ»

“Allah Hakuwahi kumtuma Mtume yoyote wala Hakumteua Khalifa yoyote ila alikuwa na washauri wa aina mbili, mmoja anayemuamuru kufanya mambo mema na kumhimiza juu ya hayo, na mwingine anayemuamuru kufanya maovu na anahimiza ayafanye. Na wale waliopewa hifadhi na Allah ndio waliohifadhika.”¹

Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abu Ad-Dihqanah alisema, “Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه aliambiwa, “kuna kijana kutoka watu wa Hirah (Iraqi, ambao walikuwa wakristo) ambaye ni mwandishi mahiri. Kwanini humteui kuwa Mwandishi?” Umar رضي الله عنه alijibu, “Nitakuwa nachukua ushauri kutoka kwa makafiri.”²

Aya hii na athari ya Umar رضي الله عنه inathibitisha ukweli kuwa Waislamu hawaruhusiwi kuwatumia *Ahl Adh-Dhimmah* watu wasiokuwa Waislamu wanaishi katika nchi za Kiislamu kwa kulipa jizya na kutii kanuni zake, kuandika masuala yanayoathiri mambo ya Waislamu na kuzitoa siri zao, kwani wanaweza kuwapa siri hizo Makafiri wenzao. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

¹ Fat’hul Al-Bari 13:201 na An-Nisai 7:158.

² Ibn Abu Hatim 2:500.

لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُؤًا مَّا عَنِتُّمْ

“Hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yanayo kudhuruni.” (3:118)

Kisha Allah تعالى Amesema,

قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَاءُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تُخْفِي صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ

“Imekwishafichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayo ficha vifua vyao ni makubwa zaidi”.

Maana yake: Uadui unadhihiri kwenye nyuso zao na kutoka katika yale wanayo yatamka baadhi ya wakati, vile vile, uadui walionao dhidi ya Waislamu na watu wake katika nyoyo zao. Ukweli huu uko wazi kwa kila mtu mwenye uelewa mzuri.

Kwa hiyo Allah تعالى Amesema,

قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ إِن كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١١٩﴾

“Tumekwisha kubainishieni Ishara ikiwa nyinyi mtayatia akilini.”

Kisha Kauli ya Allah تعالى,

هَاتَانِتُمْ أَوْلَاءِ تُحِبُّونَهُمْ وَلَا نُحِبُّونَكُمْ

“Hivyo basi nyinyi ndio mnawapenda watu hao, wala wao hawakupendeni”. (3:119)

Maana yake: Enyi Waumini! Mnawapenda wanafiki kwa sababu ya wao kudhihirisha imani? Mnawapenda kwa hilo? Lakini ukweli na uhakika ni kuwa hawakupendeni kwa dhahiri na kwa siri.

وَتُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ كُلِّهِ

“Nanyi mnaviamini Vitabu vyote.”

Maana yake: Hamna shaka na sehemu yoyote ya Kitabu cha Allah تعالى, wakati wanafiki wana shaka kubwa na kitabu hicho na kinawachanganya. Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

وَتُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ كُلِّهِ

“Nanyi mnaviamini Vitabu vyote.”

Maana yake: Mnaamini Kitabu chenu, Kitabu chao, na Vitabu vilivyopita, ambapo wanafiki hawaamini Kitabu chenu, na kwa sababu hii wanastahili kuchukiwa nanyi baada ya wao kuwachukieni.¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alikusanya kauli hii,

وَإِذَا لَقَوْكُمْ قَالُوا ءَامَنَّا وَإِذَا خَلَوْا عَضُّوا عَلَيْكُمُ الْأَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ

“Na wanapokutana nanyi husema: Tumeamini. Na wanapokuwa peke yao wanakuumieni vidole kwa chuki”.

Neno *Anamil*, lina maana ncha za vidole, kama alivyosema Qatadah.¹ Hii ni tabia ya wanafiki kuwaonesha waumini imani na mapenzi wanapokuwa nao kumbe ndani mwao wako kinyume na wanayoyadhihirisha. Hii ndiyo hali halisi kama Anavyoielezea Allah تعالى:

وَإِذَا خَلَوْا عَضُّوا عَلَيْكُمُ الْأَنَامِلَ مِنَ الْغَيْظِ

“Na wanapokuwa peke yao wanakuumieni vidole kwa chuki.”

Hii ni chuki ya hali ya juu. Kisha Allah تعالى Akasema,

قُلْ مَوْتُوا بِغَيْظِكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١١٦﴾

“Sema: Kufeni kwa chuki yenu! Hakika Mwenyezi Mungu Anayajua yaliomo vifuanī”.

Kwani vyovyote mtakavyowafanyia inda waumini na kuwaghadhibikia, jueni kuwa Allah تعالى Atatimiza Neema Yake kwa waja Wake na Ataikamilisha Dini Yake, Atauinua juu utajo Wake na kuidhihirisha Dini Yake. Kwa hiyo, Enyi wanafiki kufeni kwa ghadhabu,

إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١١٦﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Anayajua yaliomo vifuanī”.

¹ At-Tabari 7:149.

² At-Tabari 7:153.

Allah تعالی Ana ujuzi ulio kamili katika yale mnayoyaficha katika nyoyo zenu na vifua vyenu na ghadhabu, inda na chuki mlizonazo dhidi ya waumini, Allah تعالی Atawaadhibu kwa yote haya hapa duniani, kwa kufanya matokeo yawe kinyume na mnavyotarajia. Na siku ya Kiyama mtapata adhabu kali ya Motoni ambapo mtakaa humo milele. Baada ya hapo, Allah تعالی Amesema,

إِنْ تَمَسَسْتُمْ حَسَنَةً تَسْوَهُمْ وَإِنْ تَصَبَّحْتُمْ سَيِّئَةً يَفْرَحُوا بِهَا

“Ikikupateni kheri huwaudhi. Na ikikupateni shari wanafurahia”.

(3:122)

Hali hii inatilia mkazo kiwango cha uadui ambacho wanafiki wanacho dhidi ya Waumini. Iwapo waumini watafurahia mavuno mazuri, ushindi, kuungwa mkono na kuongezeka idadi yao, wanafiki wanachukizwa. Waislamu wanapopatwa na ukame, au wanaposhindwa na maadui zao, kwa Amri ya Allah تعالی, kama ilivyotokea katika vita vya Uhud, wanafiki walifurahia. Hivyo Allah تعالی Anawaambia Waja Wake waumini kuwa:

وَإِنْ تَصَبَّرُوا وَتَتَّقُوا لَأَيُّرُكُمْ كَيْدَهُمْ شَيْئًا

“Na nyinyi mkisubiri na mkajizuilia, hila zao hazita kudhuruni kitu.”

Allah تعالی Anawaongoza waumini katika usalama dhidi ya sharia za udhalimu wa watu waovu, na njama zao, kwa kuwataka warejeele subira, kumcha Allah تعالی na kumuamini Yeye. Allah تعالی Anawashinda maadui wa waumini, na wakati huo huo waumini hawana nguvu wala uwezo ila kutoka Kwake. Lolote Analoliridhia Allah تعالی huwa, na lolote Asiloliridhia haliwi. Hapana litokealo katika Miliki Yake isipokuwa Ameliamua na ni kwa mujibu wa makadirio Yake. Kwa hakika yeyote atakayemtegemea Allah تعالی, Allah تعالی Atamtosheleza.

Kisha Allah تعالی Ametaja kisa cha Uhud, na mtihani aliowaonjesha waumini na jinsi Alivyowabainisha waumini na wanafiki na akabainisha subira ya wenye subira pale Aliposema:



وَإِذْ غَدَوْتَ مِنْ أَهْلِكَ تُبَوِّئُ
 الْمُؤْمِنِينَ مَقْعِدَ لِلْقِتَالِ وَاللَّهُ سَمِيعٌ
 عَلِيمٌ ﴿١٢١﴾ إِذْ هَمَّتْ طَآئِفَتَانِ
 تَفْشَلَا وَاللَّهُ وَلِيُّهُمَا وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٢٢﴾
 وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ فَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ
 تَشْكُرُونَ ﴿١٢٣﴾ إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ أَلَنْ يَكْفِيَكُمْ أَنْ
 يُمِدَّكُمْ رَبُّكُمْ بِثَلَاثَةِ آفَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُرْسَلِينَ ﴿١٢٤﴾ بَلَى
 إِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا وَيَأْتُوكُمْ مِنْ فَوْرِهِمْ هَذَا يُمِدِّدْكُمْ
 رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ آفَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُسَوِّمِينَ ﴿١٢٥﴾ وَمَا
 جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَى لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ قُلُوبُكُمْ بِهِ وَمَا
 النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿١٢٦﴾ لِيَقْطَعَ طَرَفًا
 مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَوْ يَكْبِتَهُمْ فَيَنْقَلِبُوا خَآئِبِينَ ﴿١٢٧﴾ لَيْسَ
 لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ أَوْ يُعَذِّبُهُمْ فَلِإِنَّهُمْ
 ظَالِمُونَ ﴿١٢٨﴾ وَاللَّهُ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ
 يَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿١٢٩﴾

وَإِذْ غَدَوْتَ مِنْ أَهْلِكَ تُبَوِّئُ
 الْمُؤْمِنِينَ مَقْعِدَ لِلْقِتَالِ وَاللَّهُ سَمِيعٌ
 عَلِيمٌ ﴿١٢١﴾ إِذْ هَمَّتْ طَآئِفَتَانِ
 مِنْكُمْ أَنْ تَفْشَلَا وَاللَّهُ وَلِيُّهُمَا وَعَلَى
 اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٢٢﴾ وَلَقَدْ
 نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ فَاتَّقُوا
 اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢٣﴾

121. Na pale ulipotoka asubuhi, ukaacha ahali zako uwapange Waumini kwenye vituo kwa ajili ya vita - na Mwenyezi Mungu Anasikia na Anajua.

122. Makundi mawili miongoni mwenu yaka ingiwa na woga kuwa watashindwa - na hali Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wao; na Waumini

wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.

123. Na Mwenyezi Mungu Alikwishakunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge. Basi mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kushukuru'.

Maelezo Juu ya Vita vya Uhud:

Kwa muijibu wa wanazuoni wengi, Aya hizi zinaelezea tukio la Vita vya Uhud, Maulamaa hao ni Ibn Abbas, Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi na wengineo رضي الله عنهم.¹ Vita ya Uhud vilipangwa siku ya Jumamosi, katika mwezi wa Shawwal, mwaka wa tatu wa Hijrah.

Ikrimah alisema kuwa Vita vya Uhud vilipiganwa siku ya jumamosi, katikati ya mwezi wa *Shawwal*, na Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote.

Sababu ya Kutokea Vita vya Uhud:

Washirikina walipata kipigo na baadhi ya watukufu wao waliuawa katika vita ya Badr. Msafara ulioongozwa na Abu Sufyan (kabla ya Badr) ulirejea Makkah salama, pamoja na mali yake, watoto wao waliuawa katika vita vya Badr na viongozi waliobaki walimuambia Abu Sufyaan, "Tumia mali hii kwa kugharamia matayarisho ya vita kumpinga Muhammad!" Hivyo mali yote waliitoa kwa kazi hiyo.

Hivyo walitayarisha majeshi yao pamoja na kushirikisha makabila ya Ahbash yanayoishi katika viunga vya Makkah. Walikusanya askari elfu tatu na wakatembea mpaka walipopiga kambi jirani na Uhud wakielekea Madinah. Mtume ﷺ alisalisha Ijmaa, na alipomaliza, alisali swala ya maiti kwa ajili ya mtu mmoja katika Bani An-Najari aliyetitwa Malik bin Amr رضي الله عنه.

Kisha Mtume ﷺ aliwataka ushauri Waislamu, ama wawafuate makafiri Uhud au wajiwekee ngome Madinah? Abdullah bin Ubayy (mkuu wa wanafiki) alishauri wabaki Madinah, akasema kuwa iwapo makafiri wataizingira Madinah, uvamizi huo hautowasaidia. Aliongeza kuwa kama wataamua kuizingira Madinah, wanaume watakabiliana nao uso kwa uso, ambapo wanawake na watoto watawatupia mawe kutoka juu ya vichwa vyao, na kama wakiamua kurejea Makkah waterejea ilhali wameshindwa.

Hata hivyo, baadhi ya Masahaba hasa wale ambao hawakupigana vita ya Badr, waliwashauri Waislam watoke na kwenda Uhud kuwakabili makafiri.

¹Ibn Hatim 2:510.

Mtume ﷺ aliingia nyumbani kwake akavaa nguo ya vita na kutoka. Masahaba wakawa na hofu na kuulizana, “Je, tumemlazimisha Mtume ﷺ kutoka?” Wakasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Iwapo unataka, tutabakia Madinah.” Mtume ﷺ akasema,

«مَا يَتَّبِعِي لِنَبِيِّ إِذَا لَيْسَ لَأَمْتُهُ أَنْ يَرْجِعَ حَتَّىٰ يَحْكُمَ اللَّهُ لَهُ»

“Haifai kwa Mtume akishavaa mavazi ya vita kisha aweke chini silaha zake, lazima apigane hadi Allah Atakapohukumu.”

Mtume ﷺ alitoka na jeshi la Masahaba elfu moja. Na walipofika eneo la Shawt, Abdullah bin Ubayy aliligawa jeshi hilo kwani alirejea Madinah pamoja na theluthi ya jeshi, akidai kukasirishwa na kitendo cha Mtume ﷺ kukataa rai yake. Yeye na wafuasi wake walisema, ‘kama tungalijua kuwa utapigana leo, tungekufuateni. Lakini hatudhani kuwa mtapigana leo.” Mtume ﷺ alitembea mpaka akafika kwenye vilima katika maeneo ya Uhud na mlima wa Uhud ukiwa nyuma yao. Mtume ﷺ alisema,

«لَا يُقَاتِلُنَّ أَحَدًا حَتَّىٰ تَأْمُرَهُ بِالْقِتَالِ»

“Asipigane mmoja wenu mpaka nitakapoamrisha kupigana.”

Mtume ﷺ alijitayarisha tayari kwa vita, na jeshi lake lilikuwa na askari mia saba. Alimteua Abdullah bin Jubayr رضي الله عنه kutoka Bani Amr bin Awf, kuwaongoza wapiga mishale ambao walikuwa hamsini. Mtume ﷺ akawaambia,

«انْفُضُّوا الْخَيْلَ عَنَّا، وَلَا نُؤَاتِيَنَّ مِنْ قِبَلِكُمْ، وَالزُّمُومَا مَكَانَكُمْ، إِنْ كَانَتِ النَّوْبَةُ لَنَا أَوْ عَلَيْنَا، وَإِنْ رَأَيْتُمُونَا تَحْطِفْنَا الطَّيْرُ فَلَا تَبْرَحُوا مَكَانَكُمْ»

“Wawekeni wapanda farasi mbali nasi, na wala msishambuliwe kutoka upande wenu. Bakini katika sehemu zenu iwapo tutashinda au kushindwa. Na hata mkituona tukinyofolewa na ndege msiondoke sehemu zenu.”

Mtume ﷺ alivaa diraya mbili na alimpa bendera Mus’ab bin Umayr رضي الله عنه kutoka Bani Abd Ad-dar.

Mtume ﷺ aliwaruhusu mabarobaro kushiriki katika vita, na wengine aliwazuia, ambao aliwatumia katika vita vya Khandaki baada ya miaka miwili. Maquraish

walikusanya majeshi yenye askari elfu tatu na wapanda farasi mia mbili upande wa kulia walimweka Khalid bin Al-Walidi, na upande wa kushoto Ikrimah Ibn Abu Jahl. Walilipa bendera kabila la Bani Abd Ad-Dar. Allah Akipenda, tutavielezea vita hivi kwa urefu zaidi baadaye. Kwenye aya hii Allah Amesema,

وَإِذْ غَدَوْتَ مِنْ أَهْلِكَ تُبَوِّئُ الْمُؤْمِنِينَ مَقْعِدًا لِلْقِتَالِ

“Na pale ulipotoka asubuhi, ukaacha ahali zako uwapange Waumini kwenye vituo kwa ajili ya vita.” (3:121)

Akiwapangia maeneo tofauti, akiligawa jeshi upande wa kulia na kushoto na akiwaweka pale walipoamrisha.

وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu Anasikia na Anajua.” (3:121)

Anasikia wayasemayo na Anajua wanayoyaficha ndani ya nyoyo zao.

Kisha Allah تعالى Akasema,

إِذْ هَمَّتْ طَّائِفَتَانِ مِنْكُمْ أَنْ تَفْشَلَا

“Makundi mawili miongoni mwenu yakaingiwa na woga kuwa watashindwa”. (2:122)

Bukhari alipokea kutoka kwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema, Ayah,

إِذْ هَمَّتْ طَّائِفَتَانِ مِنْكُمْ أَنْ تَفْشَلَا

“Makundi mawili miongoni mwenu yakaingiwa na woga kuwa watashindwa”. (2:122)

Iliteremshwa kwetu sisi, (makabila mawili) Bani Harith na Bani Salamah. Na sisi hatulipendi hilo. Sufiani aliwahi kusema: Nisingefurahi kama isingeteremshwa, kwa sababu Allah تعالى Alisema ndani yake,

وَاللَّهُ وَرِثَتُهَا

“Na Mwenyezi Mungu Akawa mlinzi wa yote mawili hayo.”¹

¹ Fat’hul Al-Bari 8:63.

Muslim alipokea Hadith hii kutoka kwa Sufyan bin Uyaynah.¹

Waumini Wanakumbushwa Juu ya Ushindi Katika vita vya Badr, licha ya uchache wa wapiganaji na silaha. Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ

“Na Mwenyezi Mungu Alikwisha kunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge.” (3:123)

Maana yake: Wakati wa vita ya Badr, ambayo ilitokea siku ya Ijumaa, mwezi Kumi na saba Ramadhani, mwaka wa pili wa *Hijrah*.

Siku ya Badr inajulikana kama *Yawm Al-Furqan* (siku ya uongofu), ambayo kwayo Allah تعالى Aliwapa ushindi Waislamu na Akaudhalilisha na kuuangamiza ushirikina. Japokuwa Waislamu walikuwa wachache. Idadi ya Waislamu ilikuwa ni mia tatu na kumi na tatu, wakiwa na farasi wawili na ngamia sabini. Waliosalia walikuwa askari wa miguu bila zana za kivita za kutosha. Jeshi la adui lilikuwa na askari kati ya mia tisa na elfu moja, wakiwa na nguo za vita na silaha za kutosha, farasi walioandaliwa na zana mbalimbali. Hata hivyo, Allah تعالى Alimpa ushindi Mjumbe wake ﷺ, Akaupa nguvu Wahyi Wake, na Akazitia nuru nyuso za Mtume ﷺ na wafuasi wake. Pia Allah تعالى Alimdhaliilisha Shetani na jeshi lake. Kwa sababu hii Allah تعالى Aliwakumbusha waja Wake waumini na kundi la wachamungu juu ya upendeleo huu.

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ

“Na Mwenyezi Mungu Alikwishakunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge.”

Wakati huo mlikuwa wachache, Aya hii ina wakumbusha kuwa ushindi unatoka kwa Allah تعالى Pekee, sio kwa sababu ya jeshi kubwa na zana za kutosha pamoja na maandalizi. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine,

وَيَوْمَ حُنَيْنٍ إِذْ أَعْجَبَتْكُمْ كَثْرَتُكُمْ فَلَمْ تُغْنِ عَنْكُمْ شَيْئًا

“Na siku ya Hunayni ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni kitu”. (9:25) Mpaka Kauli Yake,

¹ Muslim 4:1948.

وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢١﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu.”
(9:27)

Badr ni eneo lililo kati ya Makkah na Madinah na ni maarufu kwa kisima chenye jina lake, ambacho kilipewa jina la Badr kutokana na Badr bin An-Nariyn, mtu aliyechimba kisima hicho.

فَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢٢﴾

“Basi mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kushukuru.” (3:123)

Maana yake: Kutekeleza majukumu ya utiifu Wake.

إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ أَلَنْ يَكْفِيَكُمْ أَنْ يُمَدِّدَ رَبُّكُمْ بِثَلَاثَةِ آفَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُتَرَلِّينَ ﴿١٢٤﴾ بَلَىٰ إِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا وَيَأْتُوكُم مِّن فَوْرِهِمْ هَذَا يُمَدِّدْكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ آفَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُسَوِّمِينَ ﴿١٢٥﴾ وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ قُلُوبُكُم بِهِ ۗ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿١٢٦﴾ لِيَقْطَعَ طَرَفًا مِّنَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَوْ يَكْبِتَهُمْ فَيَنْقَلِبُوا خَائِبِينَ ﴿١٢٧﴾ لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ أَوْ يُعَذِّبَهُمْ فَإِنَّهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٢٨﴾ وَاللَّهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ يَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢٩﴾

124. “Ulipowaambia Waumini: Je, haitakutosheni ikiwa Mola wenu Atakusaidieni kwa Malaika elfu tatu walioteremshwa?”

125. Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamungu na hata maadui wakikutokeeni Kwa ghafla, basi hapo Mola wenu Mlezi Atakusaidieni kwa Malaika elfu tano wanaoshambulia kwa nguvu.

126. Na Mwenyezi Mungu Hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na ili nyoyo zenu zipate kutua. Na msaada hautoki isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.

127. Haya ni kwa ajili aliangamize kundi katika waliokufuru, au awanyongeshe na kuwadhalilisha wapate kurejea nyuma hali ya kushindwa kwa unyonge.

128. Wewe huna lako jambo katika haya - ama Atawahurumia au Atawaadhibu, kwani wao ni madhaalimu.

129. Na ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi. Yeye Humsamehe na Humuadhibu Amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mwenye Kurehemu’.

Msaada wa Allah تعالى kwa Kuwatuma Malaika

Wanazuoni wa Tafsir wametofautiana iwapo ahadi iliyomo katika Aya hii ilihusu tukio la Vita vya Badr au Uhud. Zipa rai mbili kuhusu hili:

Rai ya Kwanza:

Rai ya kwanza inasema kuwa Kauli ya Allah تعالى:

إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ

“Ulipowaambia Waumini.” (3:124)

Inahusishwa na Kauli Yake,

وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ

“Na Mwenyezi Mungu Alikwisha kunusuruni katika Badr’.” (3:123)

Hii ilipokelewa kutoka kwa Hasan Al-Basri, Amr Ash-Shabi, Rabi bin Anas na wengineo.¹ Pia Ibn Jarir رحمه الله تعالى alikubaliana na rai hii. Abbad bin Mansur alisema kutoka kwa Hasan kuwa Kauli ya Allah تعالى,

إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ أَلَنْ يَكْفِيَكُمْ أَنْ يُعِدَّكُمْ رَبُّكُمْ بِثَلَاثَةِ آفَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ

“Ulipowaambia Waumini: Je, haitakutosheni ikiwa Mola wenu Atakusaidieni kwa Malaika elfu tatu?”. (3:24)

Ni kuhusu Vita vya Badr.² Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى naye aliipokea kauli hii.

¹ Ibn Abu Hatim 519-521.

² At-Tabari 7:174.

Kisha Abu Hatim رحمه الله تعالى alipokea kuwa Amr bin Ash-Shabi alisema, “Siku ya Badr, Waislamu walipokea habari kuwa Kurz bin Jabir (kiongozi maarufu wa kabila) alitaka kuwasaidia washirikina, na habari hii iliwapa taabu, hivyo Allah تعالى Akateremsha,

أَلَنْ يَكْفِيَكُمْ أَنْ يُمِدَّكُمْ رَبُّكُمْ بِثَلَاثَةِ أَلْفٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُزْلِينَ

“Je, haitakutosheni ikiwa Mola wenu Atakusaidieni kwa Malaika elfu tatu walioteremshwa?”. Mpaka,

مُسَوِّمِينَ

“Wanaoshambulia kwa nguvu”. (3:125)

Akasema: “Taarifa za kushindwa kwa washirikina (katika Badr) zilipofika kwa Kurz hakupeleka tena msaada, hivyo Allah تعالى Hakuwaongezea nguvu Waislamu kwa kuwapa Malaika elfu tano.”¹

Ama Ar-Rabii bin Anas, alisema, “Allah تعالى Aliwasaidia Waislamu kwa kuwapa Malaika elfu moja, kisha idadi ikafikia elfu tatu, kisha elfu tano.”² Iwapo mmoja atauliza, kwa mujibu wa rai hii, tutawezaje kuunganisha kati ya Aya hii na Kauli ya Allah تعالى juu ya Badr.

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّي مُمِدُّكُمْ بِالْفِ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ مُرَدِّينَ

“Mlipokuwa mkimuomba msaada Mola wenu Mlezi, naye aka kujibuni kuwa: Kwa yakini Mimi nitakusaidieni kwa Malaika elfu wanaofuatana mfululizo.” (8:9)

إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima.”

Tumesema kuwa, elfu moja waliotajwa hapa haisigani na elfu tatu waliotajwa katika Ayah (3:124) hapo juu. Neno “Kwa kufuatana” Maana: Wanafuatana linaonyesha walianza elfu moja kisha wakaongezeka zaidi. Aya mbili hapo juu (8:9 na 3:124) ni sawa kwa maana na inaelekea kuwa zote zilihusu vita

¹ Ibn Abu Hatim 2:520.

² At-Tabari 7:178.

vya Badr, kwa sababu Malaika hawakupigana isipokuwa katika vita vya Badr, kama ushahidi unavyoonesha. Allah تعالى Mjuzi zaidi.

Kauli ya Allah تعالى،
بَلَىٰٓ إِن تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا

“Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamungu.” (3:125)

Maana yake: Iwapo mtasubiri wakati wa kupigana na adui, na wakati huo huo mkiniogopa Mimi na kutii Amri Zangu. Hasan, Qatadah, Ar-Rabi na As-Suddi walisema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

وَيَأْتُوكُمْ مِّن فَوْرِهِمْ هَنَدًا

“Na hata maadui wakikutokeeni kwa ghafla.” (3:125)

Maana yake: Kwa mwelekeo wao huu.¹ Al-Awfi alisema kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Ayah hii ina maana, “katika safari yao hii.” Pia imesemwa kuwa ina maana, ‘kutokana na hasira zao hizi.’²

Rai ya Pili:

Rai ya pili inaeleza kuwa ahadi iliyotajwa hapa (kuhusiana na Malaika kushiriki katika vita) inahusishwa na Kauli ya Allah تعالى،

وَإِذْ غَدَوْتَ مِنْ أَهْلِكَ تُبَوِّئُ الْمُؤْمِنِينَ مَقْعِدًا لِلْقِتَالِ

“Na pale ulipotoka asubuhi, ukaacha ahali zako uwapange Waumini kwenye vituo kwa ajili ya vita.” (3:121)

Hiyo ni siku ya Uhud. Hata hivyo, Malaika hawakuja kuwasaidia Waislamu katika Uhud, kwa sababu Allah تعالى Aliweka sharti،

بَلَىٰٓ إِن تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا

“Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamungu.” (3:125)

Waislamu hawakuwa na subra katika Uhud. Bali walikimbia na kwa ajili hiyo hawakusaidiwa hata na Malaika mmoja. Kauli ya Allah تعالى،

¹ Ibn Abu Hatim 2:523,524.

² At-Tabari 7:182.

وَيَأْتُوكُمْ مِّن قَوْرِهِمْ هَذَا يُمَدِّدْكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ آلْفٍ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ مُسَوِّمِينَ ﴿١٢٥﴾

“Na hata maadui wakikutokeeni kwa ghafla, basi hapo Mola wenu Mlezi Atakusaidieni kwa Malaika elfu tano wanaoshambulia kwa nguvu.” (3:125)

Maana yake: Wenye Kutiwa Alama. Abu Is-haq As-Subay’i رحمه الله تعالى alisema, kutoka kwa Harithah bin Mudarrib kutoka kwa Ali bin Abu Talib رضي الله عنه alisema, “Malaika walikuwa wamevaa sufu nyeupe¹ katika Badr. Pia Malaika walikuwa na alama maalumu katika tosi za farasi wao.” Mak-hul alisema: “Walikuwa na alama za vilemba.” Ibn Marduwayh رحمه الله تعالى amesimulia katika Hadithi ya Abdi Al-Qodus kutoka kwa Ibn Abbasi عنهما رضي الله عنهما amesema: Mtume ﷺ amesema katika Kauli Yake.

مُسَوِّمِينَ

“Wanaoshambulia kwa nguvu.”

Maana yake: “Waliotiwa alama. Na alama za Malaika katika siku ya Badr ilikuwa ni vilemba vyeusi, na katika Hunayn vilemba vyekundu.” Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa, “Malaika hawakupigana isipokuwa katika siku ya Badr.”² Ibn Abu Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa, Yahya bin ‘Abbad alieleza kuwa Az-Zubayr رضي الله عنه alivaa kilemba cha rangi ya manjano kilichofungwa fundo siku ya Badri, basi Malaika wakawashukia huku wakiwa wamevaa vilemba vya rangi hiyo.”³

Allah تعالى Amesema,

وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ قُلُوبُكُم بِهِ ۗ

“Na Mwenyezi Mungu Hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na ili nyoyo zenu zipate kutua.” (3:126)

Aya hii ina maana, “Allah تعالى Aliwateremshia Malaika na Akawaelezeni juu ya kushuka kwao ili Kuwashajiisha na Kuwaliwaza na Kuzituliza nyoyo zenu. Lazima mjue kuwa ushahidi hutoka kwa Allah تعالى; na kama Angetaka,

¹ Ibn Abu Hatim 2:525. Isnadi yake ina dosari.

² Ibn Abu Shaybah 14:354.

³ Ibn Abu Hatim. 2:527.

Angewashinda maadui zenu hata nyie bila kupigana na maadui zenu. Kwa mfano, Allah تعالى Alisema baada ya Kuwaamrisha waumini wapigane,

فَإِذَا لَقِيتُمْ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَخْتَمْتُمُوهُمُ فَشُدُّوا الْوَتَاقَ فَمَا مَثًّا بَعْدُ
وَمَا فِدَاءً حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوَّارَهَا ۗ ذَٰلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَانتَصَرَ مِنْهُمْ وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَ
بَعْضَكُمْ بِبَعْضٍ ۗ وَالَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَنْ يُضِلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٤٧﴾ سَيَسْأَلُهُمْ
بِأَهْمِهِمْ ﴿٤٨﴾ وَيُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ ﴿٤٩﴾

“Basi mnapowakuta waliokufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe. Ndio hivyo. Na lau angeli taka Mwenyezi Mungu Angeliwashinda Mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu Akutieni mitihani nyinyi kwa nyinyi. Na waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu Hatazipoteza amali zao. Atawaongoza na Awatengezee hali yao. Na Atawaingiza katika Pepo Aliyowajuulisha.” (47:4-6)

Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema hapa,

وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ قُلُوبُكُمْ بِهِ ۗ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ الْعَزِيزِ
الْحَكِيمِ ﴿١٢٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu Hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na ili nyoyo zenu zipate kutua. Na msaada hautoki isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.” (3:126)

Aya hii ina maana “Allah تعالى ni Mwenye Nguvu Ambaye Uwezo Wake Hauwezi kudhoofishwa, na Mwenye Hikima katika Sharia Zake na Maamuzi Yake yote.”

Kisha, Allah تعالى Alisema,

لِيَقْطَعَ طَرَفًا مِّنَ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Haya ni kwa ajili Awakate sehemu katika waliokufuru.” (3:127)

Ina maana, Amewaamrisha kutekeleza Jihad na kupigana, kutokana na hikima Aliyonayo katika kila jambo. Kisha Allah تعالى Anataja matokeo mbalimbali ya kupigana Jihadi dhidi ya makafiri. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema,

لِيَقْطَعَ طَرَفًا

“Haya ni kwa ajili Awakate.” (3:127)

Maana yake: Kusababisha sehemu ya umma kuangamia.

مِنَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَوْ يَكْتُمُونَ

“Sehemu katika waliokufuru, au Awahizi wapate kurejea nyuma.” (3:127)

Kuwadhilisha na kuwalazimisha kurejea na hasira zao, baada ya kushindwa kuyafikia malengo yao ya kuwadhuruni. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

أَوْ يَكْتُمُونَ فَيَنْقَلِبُوا خَائِبِينَ ﴿١٢٧﴾

“Au Awahizi wapate kurejea nyuma nao wamepwelewa.” (3:127)

Maana yake: Warejee nyuma bila kufikia malengo yao. Kisha Allah تعالى Anataja kauli inayothibitisha kuwa Yeye Pekee Ndiye Anayetoa Maamuzi ya duniani na kesho Akhera bila msaidizi.

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Wewe huna lako jambo katika haya.” (3:128)

Maana yake: “Shauri lote liko katika Mkono Wangu.” Pia Allah تعالى Amesema,

فَإِنَّمَا عَلَيْكَ الْبَلْغُ وَعَلَيْنَا الْحِسَابُ ﴿١٢٨﴾

“Juu yako wewe ni kufikisha ujumbe na juu yetu ni hisabu.” (13:40)

Na Amesema tena,

* لَيْسَ عَلَيْكَ هُدَاهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَن يَشَاءُ

“Si juu yako wewe kuwaongoa, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye.” (2:272)

Na Amesema tena,

إِنَّكَ لَا تَهْدِي مَنْ أَحْبَبْتَ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يَشَاءُ

“Kwa hakika wewe humuongoi umpendaye, lakini Mwenyezi Mungu Humuongoa Amtakaye.” (28:56)

Muhammad bin Is-haq رحمه الله تعالى alisema juu ya Kauli ya Allah تعالى.

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Wewe huna lako jambo katika haya.”

Maana yake: “Huna ruhusa ya kutoa hukumu yako kwa waja Wangu ila kwa kufuata zile hukumu Nilizokuamrisha uwahukumu kwazo.”¹ Kisha Allah تعالى Akataja mafungu mengine yaliyobakia.

أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ

“Ama Atawahurumia.” Kwa wale waliokuwa nayo miongoni mwa ukafiri na Kuwaongoza wao baada ya upotofu.

أَوْ يُعَذِّبُهُمْ

“Au Atawaadhibu.” Hapa duniani na Akhera kwa sababu ya kukufuru kwao na madhambi yao. Na kwa kuzingatia hilo Amesema,

فَإِنَّهُمْ ظَالِمُونَ

“Kwani wao ni madhalimu.” Na hivyo, wanastahili hiyo adhabu. Bukhari aliandika kutoka kwa Salim bin Abdullah kutoka kwa baba yake alimsikia Mtume ﷺ akisema - alipoinua kichwa chake kutoka katika rukuu ya pili ya Swala ya Fajr. “Ewe Allah! Mlaani fulani na fulani.” Baada ya kusema: “Sami` Allahu Liman Hamidahu Rabbana wa lakal- Hamd.” Baada ya hapo Allah تعالى Akateremsha Aya hii,

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ أَوْ يُعَذِّبُهُمْ فَإِنَّهُمْ ظَالِمُونَ

“Wewe huna lako jambo katika haya - ama Atawahurumia au Atawaadhibu, kwani wao ni madhalimu.” (3:128)²

¹ At-Tabari 7:195.

² Fat’hul Al-Bari 8:73.

Hadithi hii ilipokewa pia na Nasai.¹ Imamu Ahmad alipokea kuwa Salim bin Abdullah alisema kuwa baba yake alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«اللَّهُمَّ الْعَنْ فُلَانًا، اللَّهُمَّ الْعَنْ الْحَارِثَ بْنَ هِشَامٍ، اللَّهُمَّ الْعَنْ سُهَيْلَ بْنَ عَمْرٍو،
اللَّهُمَّ الْعَنْ صَفْوَانَ بْنَ أُمَيَّةَ»

“Ewe Allah Mlaani fulani na fulani! Ewe Allah! Mlaani Harith bin Hisham. Ewe Allah! Mlaani Suhayl bin Amr. Ewe Allah! Mlaani Safwan bin Umayyah.”

Baadaye, Aya hii iliteremshwa;

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ أَوْ يُعَذِّبَهُمْ فَإِنَّهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٢٨﴾

“Wewe huna lako jambo katika haya - ama Atawahurumia au Atawaadhibu, kwani wao ni madhalimu.” (3:128)

Watu wote hao walisamehewa baada ya kusilimu baadaye.²

Bukhari alipokea kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kuwa alisema: Mtume ﷺ alikuwa anapotaka kuomba dua dhidi ya yeyote au kumuomba dua ya Nusra husoma *Qunut* baada ya ruku, na huenda (Abu Hurairah رضي الله عنه) alisema kuwa: Mtume ﷺ alikuwa akiomba baada ya kusema, *“Sami Allah Liman Hamidah, Rabbana wa lakal-Hamd.”* Husoma dua hii,

«اللَّهُمَّ أَنْجِ الْوَلِيدَ بْنَ الْوَلِيدِ، وَسَلْمَةَ بْنَ هِشَامٍ وَعَيْشَةَ بْنَ أَبِي رَبِيعَةَ،
وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ، اللَّهُمَّ اشْدُدْ وِطْأَتَكَ عَلَى مُضَرَ، وَاجْعَلْهَا عَلَيْهِمْ سِنِينَ
كَيْفِي يُوسُفَ»

“Ewe Allah Muokoe Walid bin Al-Walid, Salamah bin Hisham, ‘Ayyash bin Abu Rabiah na watu dhaifu na wasiojiweza miongoni mwa waumini. Ewe Allah! Kuwa mgumu kwa kabila la Mudhar na wajaalie ukame kama ukame zama za Yussuf.”

Aliomba dua hii kwa sauti. Na wakati mwingine aliomba wakati wa Sala ya Fajr, kwa kusema, *“Ewe Allah! Mlaani mtu fulani na fulani,...”* huku akitaja baadhi ya makabila ya Kiarabu. Baadaye, Allah تعالی Aliteremsha,

¹An-Nasai katika Al-Kubra 6:314.

²Ahmad 2:93.

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Wewe huna lako jambo katika haya.” (3:128)¹

Bukhari alisema; Humaid na Thabit walisema, Anas bin Malik رضي الله عنه alisema: Mtume ﷺ alijeruhiwa, katika vita vya Uhud, akasema:

«كَيْفَ يُفْلِحُ قَوْمٌ سَجَّوْا نَبِيَّهُمْ؟»

“Vipi watu wataongoka hali wamempasua Mtume wao.”

Ikashushwa Aya,

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ

“Wewe huna lako jambo katika haya.” (3:128)²

Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa, Meno ya mbele ya Mtume ﷺ yalivunjika wakati wa vita vya Uhud na pia alijeruhiwa katika bapa la uso wake mpaka damu ilichuruzika usoni mwake. Mtume ﷺ akasema,

«كَيْفَ يُفْلِحُ قَوْمٌ فَعَلُوا هَذَا بِنَبِيِّهِمْ، وَهُوَ يَدْعُوهُمْ إِلَى رَبِّهِمْ عَزَّ وَجَلَّ؟»

“Vipi watu wataongokewa baada ya kumfanyia hivi Mtume wao, ambaye anawalingania kwa Mola wao Aliyetukuka?”

Allah تعالى Akateremsha,

لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ أَوْ يَتُوبَ عَلَيْهِمْ أَوْ يُعَذِّبُهُمْ فَإِنَّهُمْ ظَالِمُونَ ﴿١٢٨﴾

“Wewe huna lako jambo katika haya - ama Atawahurumia au Atawaadhibu, kwani wao ni madhalimu.”³

Pia Muslim alikusanya Hadithi hii.⁴ Kisha Allah تعالى Amesema:

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

“Na ni vya Mwenyezi Mungu vyote vilivyomo katika mbingu na vilivyomo katika ardhi”. (3:129)

¹ Bukhari 4560.

² Fat'hul Al-Bari 7:365.

³ Ahmad 3:99.

⁴ Muslim 1791.

Kwa hakika kila kitu ni milki ya Allah تعالى na watu wote ni watumwa na wako Mkononi Mwake.

يَغْفِرُ لِمَن يَشَاءُ وَيُعَذِّبُ مَن يَشَاءُ

“Yeye Humsamehe na Humuadhibu Amtakaye.” (3:129)

Uamuzi ni Wake na hapana wa kukataa Uamuzi Wake. Allah تعالى Haulizwi kwa Ayafanyayo, wao wataulizwa,

وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mwenye Kurehemu.”

* * *

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوا الرِّبَا أَضْعَافًا مُضَاعَفَةً
 ٥ وَأَتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٣٠﴾ وَأَتَّقُوا النَّارَ الَّتِي
 أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿١٣١﴾ وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ
 تُرْحَمُونَ ﴿١٣٢﴾ * وَسَارِعُوا إِلَى مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ
 وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾
 الَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّاءِ وَالضَّرَّاءِ وَالْكَبِيمِ الْغَيْظِ
 وَالْعَافِينَ عَنِ النَّاسِ ۗ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٣٤﴾
 وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَحِشَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ
 فَاسْتَغْفَرُوا لِذُنُوبِهِمْ وَمَن يَغْفِرَ الذُّنُوبَ إِلَّا اللَّهُ وَلَمْ
 يُصِرُّوا عَلَىٰ مَا فَعَلُوا وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٣٥﴾ أُولَٰئِكَ
 جَزَاؤُهُم مَّغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَجَنَّاتٌ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ
 خَالِدِينَ فِيهَا ۖ وَنِعْمَ أَجْرُ الْعَامِلِينَ ﴿١٣٦﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوا
 الرِّبَا أَضْعَافًا مُضَاعَفَةً ٥ وَأَتَّقُوا اللَّهَ
 لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿١٣٠﴾ وَأَتَّقُوا النَّارَ
 الَّتِي أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿١٣١﴾ وَأَطِيعُوا
 اللَّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ
 ﴿١٣٢﴾ * وَسَارِعُوا إِلَى مَغْفِرَةٍ مِّن
 رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ
 وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾
 الَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّاءِ وَالضَّرَّاءِ
 وَالْكَبِيمِ الْغَيْظِ وَالْعَافِينَ عَنِ
 النَّاسِ ۗ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ
 ﴿١٣٤﴾ وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَحِشَةً أَوْ
 ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا
 لِذُنُوبِهِمْ وَمَن يَغْفِرَ الذُّنُوبَ إِلَّا
 اللَّهُ وَلَمْ يُصِرُّوا عَلَىٰ مَا فَعَلُوا وَهُمْ
 يَعْلَمُونَ ﴿١٣٥﴾ أُولَٰئِكَ جَزَاؤُهُم
 مَّغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَجَنَّاتٌ تَجْرِي
 مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۖ وَنِعْمَ
 أَجْرُ الْعَامِلِينَ ﴿١٣٦﴾

130. Enyi mlioamini! Msile riba mkizidisha juu kwa juu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kufanikiwa.

131. Na uogopeni Moto ambao umeandaliwa kwa ajili ya makafiri.

132. Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa.

133. Na yakimbilieni maghufira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyowekwa tayari kwa wachamungu.

134. Ambao hutoa wanapokuwa na wasaa na wanapokuwa na dhiki, na wanajizua ghadhabu, na wasamehevu kwa watu; na Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao wema;

135. Na ambao pindi wafanyapo uchafu au wakajidhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na wakamuomba msamaha kwa dhambi zao - na nani anayefuta dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu? - na wala hawaendelei na waliyoyafanya na hali wanajua.

136. Hao malipo yao ni msamaha kwa Mola wao Mlezi, na Bustani zipitazo mito kati yake. Humo watadumu, na mwema mno ujira wa watendao”.

Kuharamishwa Riba Moja kwa Moja:

Allah تعالى Amewaharamishia waja Wake kujishughulisha na *Riba* na kutaka riba kutokana na mitaji yao kama walivyokuwa wakifanya katika Jahiliyyah.

Mfano wakati wa kulipa deni, mkopeshaji alimuambia mkopaji, “Lipa sasa, au deni lako litakuwa na *riba*.”

Ana hiari kulipa au aongezewe muda wa mkopo, na kiwango kiongezoke, itaendelea hivyo kila mwaka, kiasi deni dogo huongezeka mpaka kuwa kubwa.

Pia Allah تعالى Anawaamrisha waja Wake kumcha Yeye ili waweze kufanikiwa hapa duniani na Akhera.

Pia Allah تعالى Anawakhofisha na Moto na Anawaonya wauogope kwa Kusema,

وَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴿١٣٠﴾ وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

“Na uogopeni Moto ambao umeandaliwa kwa ajili ya makafiri. Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa”.
(3:131- 132)

Kuhimiza Kufanya Mema Ambapo Malipo Yake ni Pepo

Allah تعالى Anawahimiza waja Wake kufanya amali njema na kupupia kufanya vitendo vya utiifu. Allah تعالى Amesema,

﴿ وَسَارِعُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ أُعِدَّتْ

لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٣﴾

“Na yakimbilieni maghufira ya Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi, iliyowekwa tayari kwa wachamungu”. (3:133)

Maana yake: Kama Pepo ilivyoandaliwa kwa wachamungu Moto nao uliandaliwa kwa ajili ya Makafiri. Kauli ya Allah تعالى .

عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ

“Upana wake ni mbingu na ardhi”. (3:133)

Anawazindua watu kujua ukubwa wa Pepo kama Alivyoelezea sifa ya matakia ya peponi.

بَطَّأَيْنَا مِنْ إِسْتَبْرَقٍ

“Yenye bitana ya hariri nzito.” (55:54),

Kama *bitana* iko hivyo itakuwaje dhahiri yake? Pia imeelezwa Pepo inalingana kwa upana na urefu kwa sababu ni Quba chini ya Arshi - Upana na Urefu wa Quba au mviringo ni sawa kwa vipimo.

Hili linaungwa mkono na yaliyomo ndani ya *Sahih* aliposema;

﴿ إِذَا سَأَلْتُمُ اللَّهَ الْجَنَّةَ فَمَا سَأَلُوهُ الْفِرْدَوْسَ، فَإِنَّهُ أَعْلَى الْجَنَّةِ، وَأَوْسَطُ الْجَنَّةِ، وَمِنْهُ تَنْجَرُ أَنْهَارُ الْجَنَّةِ، وَسَقْفُهَا عَرْشُ الرَّحْمَنِ ﴾

“Mtakapomuomba Allah pepo, Muombeni Firdaus, kwani hiyo ndiyo Pepo ya juu zaidi na pepo ya kati na kati, na kutoka humo kunachimbuka mito ya Peponi, na juu yake kuna Arshi ya Rahmaan (Allah).”¹

Aya hii (3:133). hapo juu ni sawa na Kauli ya Allah تعالى katika *Surat Al-Hadid*,

¹ Fat’hul Al-Bari 6:14.

سَابِقُوا إِلَىٰ مَغْفِرَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

“Kimbilieni msamaha wa Mola wenu Mlezi, na Pepo ambayo upana wake ni kama upana wa mbingu na ardhi.” (57:21)

Al-Bazzar رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Abu Hurayrah , alisema kuwa mtu alikuja kwa Mtume ﷺ na akamuuliza: unasemaje kuhusu Kauli ya Allah تعالى ,

وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا كَعَرْضِ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ

“Na Pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi”. (3:133)

“Uko wapi basi Moto?” Mtume ﷺ akajibu,

«أَرَأَيْتَ اللَّيْلَ إِذَا جَاءَ لَيْسَ كُلُّ شَيْءٍ، فَأَيُّ النَّهَارِ؟»

“Unaonaje Usiku unapokuja hugubika kila kitu, hivyo mchana uko wapi?”

Kwa hiyo moto uko pale anapopataka Allah تعالى, kisha Mtume ﷺ akasema:-

«وَكَذَلِكَ النَّارُ تَكُونُ حَيْثُ شَاءَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ،»

“Vile vile Moto utakuwa pale anapopataka Allah Aliyetukuka.”¹

Hadithi hii ina maana mbili

Ya kwanza:

Tukiwa hatuoni usiku wakati wa mchana, haina maana kuwa mchana haupo mahala pengine, japokuwa hatuoni. Hii ni kama Jahannam, ipo pale Allah تعالى Atakapo iwe. Pili: maana ya pili ni mchana unapodhihiri upande mmoja wa dunia, na usiku huwepo upande mwingine. Vivyo hivyo Pepo, kwani ipo kileleni mwa mbingu na chini ya Arshi. Upana wa Pepo ni kama ulivyoielezwa na Allah تعالى,

عَرْضُهَا السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ

“Upana wa mbingu na ardhi.” (57:21)

Upande mwingine, Moto uko chini kabisa. Kwa hiyo Pepo kuwa pana sawa na mbingu na ardhi haikhitilafiani na ukweli kuwa Moto upo popote Allah تعالى Atakapo. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi,

¹ Kashful - Astaar 3:43 Sahihi Hibbani 1:306 na Al-Mustadrak 1:36.

Allah تعالى Amesema Alipokuwa Akieleza sifa za watu wa Peponi,

الَّذِينَ يُنْفِقُونَ فِي السَّرَّاءِ وَالضَّرَّاءِ

“Ambao hutoa wanapokuwa na wasaa na wanapokuwa na dhiki.”
(3:134)

Wanatoa katika nyakati za tabu na za raha wakati mtu ana nguvu au vinginevyo, ana siha au mgonjwa, na katika hali zote, kama Allah تعالى Alivyosema katika Aya nyingine,

الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ سِرًّا وَعَلَانِيَةً

“Wale wanaotoa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri.”
(2:274)

Maana yake: haliwashughulishi wao jambo lolote wakaacha ucha Mungu na kumtii Allah تعالى na kutoa kwa kumridhisha Yeye tu na kuwafanyia ihsani viumbe wake wakiwemo ndugu zao wa karibu na watu wengine yote hayo ni katika wema. Kauli ya Allah تعالى,

وَالْكٰظِمِينَ الْغَيْظَ وَالْعَافِينَ عَنِ النَّاسِ

“Na wanajizua na ghadhabu, na wasamehevu kwa watu”. (3:134)

Na wanapokuwa na hasira, wanaidhibiti hasira yao na hawaipatilizi. Bali huwasamehe hata wale wanaowaudhi. Imamu Ahmad alipokea kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَيْسَ الشَّدِيدُ بِالصُّرَعَةِ، وَلَكِنَّ الشَّدِيدَ الَّذِي يَمْلِكُ نَفْسَهُ عِنْدَ الْغَضَبِ»

“Shujaa si yule anayewaangusha watu kwa mieleka. Mtu shujaa ni yule anayeizua nafsi yake wakati wa ghadhabu.”¹

Hadithi hii pia imeandikwa katika Sahih Mbili.² Imamu Ahmad alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ أَنْظَرَ مُعْسِرًا أَوْ وَضَعَ لَدَىٰ وَقَاهُ اللَّهُ مِنْ قَبْلِ جَهَنَّمَ، أَلَا إِنَّ عَمَلَ الْجَنَّةِ حَزَنٌ بِرَبْوَةٍ - ثَلَاثًا - أَلَا إِنَّ عَمَلَ النَّارِ سَهْلٌ بِسَهْوَةٍ. وَالسَّعِيدُ مَنْ وَقِيَ الْفِتْنَ، وَمَا مِنْ جِرْعَةٍ أَحَبَّ إِلَى اللَّهِ مِنْ جِرْعَةٍ غَنِيظٍ يَكْظُمُهَا عَبْدٌ، مَا كَظَمَهَا عَبْدٌ لَهِ إِلَّا مَلَأَ جَوْفَهُ إِيْمَانًا»

¹ Ahmad 2:236.

² Fat'hul Al-Bari 10:535 na Muslim 4:2014.

*"Mwenye kumpa mdaiwa muda wa kulipa au kumsamehe, Allah atamuokoa na moto wa Jahannam. Fahamuni ya kuwa amali za Peponi, ziko juu ya kilima, na amali za Motoni ni rahisi kuzifikia kwani ziko chini. Mtu mwema ni yule aliyeepushwa na mitihani. Kwa hakika, hapana fundo lipendezalo zaidi kwa Allah kuliko fundo la hasira analolidhibiti mtu wakati wa hasira, na mja halidhibiti kwa ajili ya Allah, isipokuwa nafsi yake itajazwa Imani."*¹

Hadithi hii isnadi yake ni nzuri, haina wapokezi wasioaminika, na maana yake ni nzuri.

Imamu Ahmad alipokea kuwa Sahl bin Mu'adh bin Anas alisema kuwa baba yake alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ كَظَمَ غَيْظًا وَهُوَ قَادِرٌ عَلَى أَنْ يُفِذَهُ دَعَاهُ اللَّهُ عَلَى رُؤُوسِ السُّحُلَاتِ حَتَّى يُخَيَّرَهُ مِنْ أَيِّ الْحُورِ شَاءَ»

*"Mwenye kudhibiti ghadhabu naye alikuwa na uwezo wa kuitekeleza, Allah Atamuita mbele ya viumbe watashuhudia mpaka atakapomchagua Huriliai yoyote amtakaye."*² (wanawake wazuri wenye macho makubwa yanayovutia).

Abu Dawud, At-Tirmidhi na Ibn Majah waliikusanya Hadithi hii, ambayo At-Tirmidhi aliitaja kuwa *"Hasan Gharib"*.

Ibn Marduwyahi رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Umar رضي الله عنهما, Mtume ﷺ alisema,

«مَا تَجَرَّعَ عَبْدٌ مِنْ جَرَعَةٍ أَفْضَلَ أَجْرًا مِنْ جَرَعَةٍ غَيْظٍ كَظَمَهَا ابْتِغَاءَ وَجْهِ اللَّهِ»

*"Hajamezapo mja fundo bora zaidi kwa ujira kuliko fundo la hasira analolidhibiti kwa kutaka radhi za Allah."*³

Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Ibn Majah رحمه الله تعالى nao waliikusanya Hadithi hii.⁴ Allah تعالى Amesema,

¹ Ahmad 1:327.

² Ahmad 3:438, 440; Abu Dawud 5:137 Tuhfat Al-Ahwadhi 6:139; Ibn Majah 2:1400.

³ Ahmad 2:128.

⁴ Ibn Majah 2:1401.

وَالْكَاظِمِينَ الْغَيْظَ وَالْعَافِينَ

“Na wanajizuia na ghadhabu.”

Maana yake: Hawawaghadhibikii watu. Bali wanajizuia kuwadhuru na wanasubiri malipo kutoka kwa Allah تعالى Mwenye Cheo. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَالْعَافِينَ عَنِ النَّاسِ

“Na wasamehevu kwa watu.”

Wanawasamehe wale wanaowadhulumu. Kwa hiyo, hawawi na kinyongo ndani ya mioyo yao, na huu ni mwenendo mzuri juu ya muktadha huu. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

وَاللَّهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

“Na Mwenyezi Mungu Huwapenda wafanyao wema.” (3:134)

Tabia hii nzuri nayo ni aina ya *Ihsan* (wema katika Dini). Kuna Hadithi inayosema,

«ثَلَاثٌ أَقْسِمُ عَلَيْهِنَّ: مَا نَقَصَ مَالٌ مِنْ صَدَقَةٍ، وَمَا زَادَ اللَّهُ عَبْدًا بِعَفْوٍ إِلَّا عِزًّا،
وَمَنْ تَوَاضَعَ لِلَّهِ رَفَعَهُ اللَّهُ»

“Ninaapa juu ya mambo matatu, mali haijapungua kwa kutoa sadaka, na Allah Hamzidishii mja kwa kusamehe isipokuwa utukufu, na anayenyenyekea kwa ajili ya Allah, Allah Anampandisha cheo.”

Allah تعالى Amesema,

وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَجِيحَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا لِذُنُوبِهِمْ

“Na ambao pindi wafanyapo uchafu au wakajidhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na wakamuomba msamaha kwa dhambi zao”. (3:135)

Kwa hiyo wanapofanya dhambi wanaifuatishia na mambo mazuri na kuomba msamaha. Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Hurayra رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

¹ Ahmad 4:231.

«إِنَّ رَجُلًا أَدْتَبَ ذَنْبًا فَقَالَ: رَبِّ إِنِّي أَدْتَبْتُ ذَنْبًا فَاغْفِرْهُ، فَقَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: عَبْدِي عَمِلَ ذَنْبًا فَعَلِمَ أَنَّ لَهُ رَبًّا يَغْفِرُ الذَّنْبَ وَيَأْخُذُ بِهِ، قَدْ غَفَرْتُ لِعَبْدِي، ثُمَّ عَمِلَ ذَنْبًا آخَرَ فَقَالَ: رَبِّ إِنِّي عَمِلْتُ ذَنْبًا فَاغْفِرْهُ، فَقَالَ تَبَارَكَ وَتَعَالَى: عَلِمَ عَبْدِي أَنَّ لَهُ رَبًّا يَغْفِرُ الذَّنْبَ وَيَأْخُذُ بِهِ، قَدْ غَفَرْتُ لِعَبْدِي، ثُمَّ عَمِلَ ذَنْبًا آخَرَ فَقَالَ: رَبِّ إِنِّي عَمِلْتُ ذَنْبًا فَاغْفِرْهُ لِي، فَقَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: عَلِمَ عَبْدِي أَنَّ لَهُ رَبًّا يَغْفِرُ الذَّنْبَ وَيَأْخُذُ بِهِ، قَدْ غَفَرْتُ لِعَبْدِي، ثُمَّ عَمِلَ ذَنْبًا آخَرَ فَقَالَ: رَبِّ إِنِّي عَمِلْتُ ذَنْبًا فَاغْفِرْهُ لِي، فَقَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: عَلِمَ عَبْدِي أَنَّ لَهُ رَبًّا يَغْفِرُ الذَّنْبَ وَيَأْخُذُ بِهِ، أَشْهَدُكُمْ أَنِّي قَدْ غَفَرْتُ لِعَبْدِي فَلْيَعْمَلْ مَا شَاءَ»

"Mtu mmoja alifanya dhambi na akasema, 'Ewe Mola! Nimefanya dhambi, nisamehe' Allah تعالی Akasema, 'Mja wangu amefanya dhambi na akajua kuwa anaye Mola Ambaye Husamehe makosa na Kuadhibu kwa makosa hayo. Nimemsamehe mja wangu.'" Kisha alifanya dhambi nyingine na akasema, 'Ewe Mola! Nimefanya dhambi, nisamehe!'" Allah تعالی Akasema, 'Mja wangu amejua kuwa ana Mola Anayesamehe makosa na Anayeadhibu aliyefanya dhambi Nimemsamehe mja Wangu.' Kisha akafanya dhambi nyingine na akasema 'Ewe Mola! Nimefanya dhambi, nisamehe!'" Allah تعالی Akasema, 'Mja wangu anajua kuwa ana Mola Anayesamehe makosa na Kuadhibu wakosaji. Nakushuhudisheni kuwa Mimi Nimemsamehe Mja wangu, hivyo muacheni afanye atakalo.'¹ Masimulizi sawa na hayo yamo katika sahihi.²

Abdur-Razzaq رضي الله عنه alipokea kutoka kwa Anas bin Malik رحمه الله تعالی alisema, "Niliambiwa kuwa Aya hii iliposhuka,

وَالَّذِينَ إِذَا فَعَلُوا فَحِشَةً أَوْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ ذَكَرُوا اللَّهَ فَاسْتَغْفَرُوا لِذُنُوبِهِمْ

"Na ambao pindi wafanyapo uchafu au wakajidhulumu nafsi zao humkumbuka Mwenyezi Mungu na wakamuomba msamaha kwa dhambi zao." (3:135)

Iblis (shetani) alilia. Na Kauli Yake Allah تعالی,³

¹ Ahmad 2:296.

²Fat'hul Bari 13:474.

³Abdur Razzaq 1:133.

وَمَنْ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا اللَّهُ

“Na nani anayefuta dhambi isipokuwa Mwenyezi Mungu?”.

Maana yake: hapana anaye samehe dhambi ila Allah تعالی. Allah تعالی Amesema,

وَلَمْ يُصِرُّوا عَلَىٰ مَا فَعَلُوا وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٣٥﴾

“Na wala hawaendelei na waliyoyafanya na hali wanajua.”

Kwani hutubia dhambi zao, wanarejea kwa Allah تعالی bila kukawia, hawadumu kwenye dhambi, na hata kama makosa yao yatakariri lakini hufanya toba kwa madhambi hayo. Allah تعالی Amesema hapa,

وَهُمْ يَعْلَمُونَ ﴿١٣٥﴾

“Na hali wanajua.”

Mujahid na Abdullah bin Ubayd bin Umayr walisema kuwa maana ya, **“Na hali wanajua”** ni, “Yeyote ambaye anayetubia madhambi yake, Allah تعالی Humkubalia toba yake.” Vivyo hivyo, Allah تعالی Amesema,

أَلَمْ يَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ هُوَ يَقْبَلُ التَّوْبَةَ عَنْ عِبَادِهِ

“Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu Anapokea toba ya waja wake.” (9:104)

Na kisha Akasema:

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١٣٦﴾

“Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake, kisha akaomba maghufira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghufira, Mwenye Kurehemu”. (4:110)

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Abdillahi bin Amri رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa alisema siku moja akiwa juu ya Mimbari;

«ارْحَمُوا تَرْحَمُوا، وَاعْفِرُوا يُغْفَرَ لَكُمْ، وَئِلَّ لِأَقْمَاعِ الْقَوْلِ، وَئِلَّ لِلْمُصْرِينَ الَّذِينَ يُصِرُّونَ عَلَىٰ مَا فَعَلُوا وَهُمْ يَعْلَمُونَ»

“Wahurumieni watu, nanyi mtahurumiwa, takeni msamaha, mtasamehewa. Ole wao wanaosikia maneno, kisha wasiyazingatie, Ole wao wale wanaoendelea na kudumu juu ya dhambi walizo-zifanya hali ya kuwa wanajua.”

Hadithi ameinukuu Imamu Ahmad peke yake.

Na mfano wa Aya kama hii ni nyingi sana. Kisha Allah تعالى Alisema baada ya ufafanuzi huu.

أُولَئِكَ جَزَاءُ هُم مَّغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ

“Hao malipo yao ni msamaha kwa Mola wao Mlezi.” (3:136)

Ni malipo kutokana na wao kuwa na sifa hizi,

مَّغْفِرَةٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَجَنَّتْ نُجْرَىٰ مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Ni msamaha kwa Mola wao Mlezi, na Bustani zipitazo mito kati yake”.

Ikiwa na kila aina ya kinywaji.

خَالِدِينَ فِيهَا

“Humo watadumu”. Na milele.

وَنِعْمَ أَجْرُ الْعَمَلِينَ ﴿١٣٦﴾

“Na mwema mno ujira wa watendao”.

Katika sehemu hii ya Aya, Allah تعالى Anaisifu Pepo.

* * *

قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِكُمْ سُنَنٌ فَمَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ
 كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكَذِّبِينَ ﴿١٣٧﴾ هَذَا بَيَانٌ لِلنَّاسِ وَهُدًى
 وَمَوْعِظَةٌ لِّلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٨﴾ وَلَا تَهِنُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَنْتُمْ
 الْأَعْلَوْنَ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٣٩﴾ إِنْ يَمَسُّكُمْ فَزَعٌ فَقَدْ
 مَسَّ الْقَوْمَ فَزَعٌ مِثْلُهُ ۗ وَتِلْكَ الْأَيَّامُ نُدَاوِلُهَا بَيْنَ النَّاسِ
 وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَيَتَّخِذَ مِنْكُمْ شُهَدَاءَ ۗ وَاللَّهُ لَا
 يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿١٤٠﴾ وَلِيُمَحِّصَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَيَمْحَقَ
 الْكٰفِرِينَ ﴿١٤١﴾ أَمْرٌ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا
 يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٢﴾
 وَلَقَدْ كُنْتُمْ تَمَنَّوْنَ الْوَمُوتَ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَلْفَوْهُ فَقَدْ رَأَيْتُمُوهُ
 وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿١٤٣﴾ وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ
 قَبْلِهِ الرُّسُلُ ۗ أَفَلَا يَنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ أُنْقَلَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ ۗ وَمَنْ
 يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقْبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا ۗ وَسَيَجْزِي اللَّهُ
 الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾ وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَنْ تَمُوتَ إِلَّا بِإِذْنِ
 اللَّهِ كِتَابًا مُّوجَّلًا ۗ وَمَنْ يُرِدْ ثَوَابَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا
 وَمَنْ يُرِدْ ثَوَابَ الْآخِرَةِ نُؤْتِهِ مِنْهَا ۗ وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ
 ﴿١٤٥﴾ وَكَأَيِّنْ مِنْ نَبِيٍّ قُتِلَ مَعَهُ رِبِّيُونَ كَثِيرٌ فَمَا وَهَنُوا
 لِمَا أَصَابَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَمَا ضَعُفُوا وَمَا اسْتَكَانُوا ۗ وَاللَّهُ
 يُحِبُّ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٦﴾ وَمَا كَانَ قَوْلَهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا رَبَّنَا
 اغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَإِسْرَافَنَا فِي أَمْرِنَا وَثَبِّتْ أَقْدَامَنَا وَانصُرْنَا
 عَلَى الْقَوْمِ الْكٰفِرِينَ ﴿١٤٧﴾ فَآتَاهُمُ اللَّهُ ثَوَابَ الدُّنْيَا
 وَحَسَنَ ثَوَابِ الْآخِرَةِ ۗ وَاللَّهُ يُحِبُّ الْحَسَنِينَ ﴿١٤٨﴾

قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِكُمْ سُنَنٌ فَمَسِيرُوا فِي
 الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ
 الْمُكَذِّبِينَ ﴿١٣٧﴾ هَذَا بَيَانٌ لِلنَّاسِ
 وَهُدًى وَمَوْعِظَةٌ لِّلْمُتَّقِينَ ﴿١٣٨﴾
 وَلَا تَهِنُوا وَلَا تَحْزَنُوا وَأَنْتُمْ الْأَعْلَوْنَ
 إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٣٩﴾ إِنْ
 يَمَسُّكُمْ فَزَعٌ فَقَدْ مَسَّ الْقَوْمَ فَزَعٌ
 مِثْلُهُ ۗ وَتِلْكَ الْأَيَّامُ نُدَاوِلُهَا بَيْنَ
 النَّاسِ وَلِيَعْلَمَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا
 وَيَتَّخِذَ مِنْكُمْ شُهَدَاءَ ۗ وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ
 الظَّالِمِينَ ﴿١٤٠﴾ وَلِيُمَحِّصَ اللَّهُ الَّذِينَ
 ءَامَنُوا وَيَمْحَقَ الْكٰفِرِينَ ﴿١٤١﴾ أَمْرٌ
 حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ
 اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ
 الصَّابِرِينَ ﴿١٤٢﴾ وَلَقَدْ كُنْتُمْ تَمَنَّوْنَ
 الْوَمُوتَ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَلْفَوْهُ فَقَدْ
 رَأَيْتُمُوهُ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿١٤٣﴾

137. Kabla yenu yamepita
 matokeo mengi ya kuadhi-
 biwa umma; basi tembeeni
 katika ulimwengu muangalie
 vipi ulikuwa mwisho wa
 wanaokanusha.

138. Hii ni bayana kwa watu wote, na ni uwongofu, na mawaidha kwa wachamungu.

139. Wala msinyongee, wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini.

140. Kama yamekupatani majeraha, basi na hao watu wengine yamewapata majeraha mfano wa haya. Na siku za namna hii Tunaweletea watu kwa zamu, ili Mwenyezi Mungu Awapambanue walioamini na Awateue miongoni mwenu mashahidi. Na Mwenyezi Mungu Hawapendi madhaalimu;

141. Na pia ili Mwenyezi Mungu Awasafishe walioamini na Awafutilie mbali makafiri.

142. Je! Mnadhani mtaingia Peponi na hali Mwenyezi Mungu hajawapambanua wale miongoni mwenu waliopigana Jihadi, na hajawapambanua waliosubiri?

143. Na nyinyi mlikuwa mkitamani mauti kabla hamjakutana nayo. Basi sasa mmekwisha yaona na huku mnayatazama.

Hekima ya Kushindwa Waislamu katika Vita vya Uhud:

Allah تعالى Anawaelezea waja wake waumini ambao walishindwa katika vita vya Uhud, ikiwa ni pamoja na kuuwawa mashahidi sabini.

قَدْ خَلَّتْ مِنْ قَبْلِكُمْ سُنَنٌ

“Kabla yenu yamepita matokeo mengi ya kuadhibiwa umma”.

Yaliwakuta kama haya umma zilizotangulia kabla yenu miongoni mwa wafuasi wa Mitume. Ndiyo maana mwisho wao ukawa mwema na mwisho mbaya (wa kushindwa) ukawa kwa makafiri. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

فَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَانظُرُوا كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُكْذِبِينَ ﴿١٧٧﴾

“Basi tembeeni katika ulimwengu muangalie vipi ulikuwa mwisho wa wanaokanusha”. Baadaye Akasema,

هَذَا بَيَانٌ لِلنَّاسِ

“Hii ni bayana kwa watu wote.

Maana yake: Qur'an inaelezea mambo kwa uwazi wake na jinsi gani mataifa yaliyotangulia yalivyoishi na maadui zao.

وَهُدًى وَمَوْعِظَةً

“Na ni uwongofu, na mawaidha.”

Kuwa Qur'an ina habari za watu waliopita kabla yenu. Kisha Akasema:

وَهُدًى

“Ni uwongofu.” Kwa nyoyo zenu.

وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ

“Na mawaidha kwa wachamungu.”

Anawakemea wasifanye yaliyokatazwa na yaliyoharamishwa. Baada ya hapo Allah تعالى Anawafarijii waumini kwa Kusema,

وَلَا تَهِنُوا

“Wala msilegee.” Kwa sababu ya hayo yaliyowapata,

وَلَا تَحْزَنُوا وَأَنْتُمْ الْأَعْلَوْنَ إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ

“Wala msihuzunike, kwani nyinyi ndio wa juu mkiwa ni Waumini!”

Kwa uhakika, ushindi wa mwisho na furaha itakuwa kwenu, Enyi waumini.

إِنْ يَمَسُّكُمْ فَرْحٌ فَقَدْ مَسَّ الْقَوْمَ فَرْحٌ مِّثْلُهُ

“Kama yamekupatani majeraha, basi na hao watu wengine yamewapata majeraha mfano wa haya.” (3:140),

Kwa hiyo, kama mlipata majeraha na baadhi yenu kuuawa, basi adui zenu nao walipata majeraha na maafa yanayofanana na hayo.

وَتِلْكَ الْأَيَّامُ نُدَاوِلُهَا بَيْنَ النَّاسِ

“Na siku za namna hii Tunaweletea watu kwa zamu.”

Na baadhi ya wakati – kwa hekima – Tunamruhusu adui kuwashinda japokuwa mwisho mwema ni wenu. Na kwa hilo Allah تعالى Amesema,

وَلْيَعْلَمْ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا

“Ili Mwenyezi Mungu Awapambanue walioamini.” (3:140)

Maana yake: “Ili Tumjue mwenye subira wakati wa kupigana na maadui.”
Hivyo ndivyo alivyotafsiri Ibn Abbas رضي الله عنهما.

وَيَتَّخِذَ مِنْكُمْ شُهَدَاءَ

“Na Awateue miongoni mwenu mashahidi.” (3:140)

Wale watakaouawa katika njia Yake Allah تعالى na wanatoa maisha yao kwa kutaka Radhi Zake.

وَاللَّهُ لَا يُحِبُّ الظَّالِمِينَ ﴿١٤١﴾ وَلِيُمَخِّصَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا

“Na Mwenyezi Mungu Hawapendi madhalimu, na pia ili Mwenyezi Mungu Awasafishe walioamini.” (3:140-141)

Kwa kuwasamehe dhambi zao kama wanazo. Vinginevyo Allah تعالى Atawapandisha daraja zao kwa mujibu wa madhara waliyoyapata. Kauli ya Allah تعالى,

وَيَمْحَقَ الْكٰفِرِينَ ﴿١٤٢﴾

“Na Awafutilie mbali makafiri.”

Kwani ni ada yao wanapopata ushindi, kuchupa mipaka na kufanya uharibifu. Mwenendo huu ndio sababu ya kuangamizwa kwao, kuhiliki, kufutika na kufa kabisa. Kisha Allah تعالى Amesema,

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ الضَّالِّينَ ﴿١٤٣﴾

“Je! Mnadhani mtaingia Peponi na hali Mwenyezi Mungu Hajawapambanua wale miongoni mwenu waliopigana Jihadi, na Hajawapambanua waliosubiri?” (3:142)

Aya hii inauliza, hivi mnadhani kuwa mtaingizwa Peponi bila kwanza kutahiniwa kwa vita na mashaka? Allah تعالى Amesema katika Surat Al-Baqarah,

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَأْتِكُمْ مَثَلُ الَّذِينَ خَلَوْا مِنْ قَبْلِكُمْ مَسْتَهْمِ الْأَسَافَةِ

وَالضَّالِّينَ وَزُلُّوا

“Mnadhani kuwa mtaingia Peponi, bila ya kukujieni kama yaliyo waja wale waliopita kabla yenu? Iliwapata shida na madhara na wakatikiswa.” (2:214).

Allah تعالى Amesema,

الْمَرْءُ أَحْسِبَ النَّاسُ أَنْ يُتْرَكَ أَنْ يَقُولُوا ءَامَنَّا وَهُمْ لَا يُفْتَنُونَ ﴿٢١٤﴾

“Alif Lam Mim (A.L.M.). Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema: Tumeamini. Nao wasijaribiwe?” (29:1-2)

Kwa sababu hii Amesema hapa,

أَمْ حَسِبْتُمْ أَنْ تُدْخَلُوا الْجَنَّةَ وَلَمَّا يَعْلَمِ اللَّهُ الَّذِينَ جَاهَدُوا مِنْكُمْ وَيَعْلَمَ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٢﴾

“Je! Mnadhani mtaingia Peponi na hali Mwenyezi Mungu Hajawapambanua wale miongoni mwenu waliopigana Jihadi, na Hajawapambanua waliosubiri?” (3:142)

Maana yake: Hamtaipata Pepo mpaka mtakapojaribiwa; na Allah تعالى Anamjua miongoni mwenu aliyepambana na kupigana katika njia Yake na wenye subira mbele za maadui. Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ كُنْتُمْ تَمَنَّوْنَ أَلْمَوْتَ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَلْقَوْهُ فَقَدْ رَأَيْتُمُوهُ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿١٤٣﴾

“Na nyinyi mlikuwa mkitamani mauti kabla hamjakutana nayo. Basi sasa mmekwishayaona na huku mnayatazama”. (3:143)

Ayah inatangaza, “Enyi waumini! Kabla ya siku hii, mlitaka kukabiliana na maadui na mlikuwa na ghera ya kupigana nao. Lile mlilolitaka limejiri, basi piganeni nao na muwe na subira.’ Imeandikwa katika Sahih Mbili kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا تَتَمَنَّوْا لِقَاءَ الْعَدُوِّ، وَسَلُّوْا اِلٰهَ الْعَافِيَةِ، فَاِذَا لَقِيْتُمُوْهُمْ فَاصْبِرُوْا، وَاعْلَمُوْا اَنَّ الْجَنَّةَ تَحْتَ ظِلَالِ السُّيُوفِ»

“Msitamani kukabiliana na adui na muombeni Allah afya, kwa hiyo mkikabiliana nao, subirini na jueni kuwa Pepo iko chini ya vivuli vya mapanga.”¹

¹Fat’hul Bari 6:181 na Muslim 3:1362.

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema hapa,

فَقَدَّ رَأَيْتُمُوهُ

“Basi sasa mmekwishayaona.”

Kifo, mlíkiona pale panga zilipodhihiri; visu viliponolewa, na mikuki ilipo kingama na askari waliposimama safu tayari kwa vita. Wana falsafa wanaielezea taswira iliyopo katika Aya hii, na jambo la kufikirika “*khayali*” Yaani kueleza kitu kisichoonekana (cha kufikirika) mpaka kikafanana na vitu halisi. Kama vile kufikiria urafiki wa Mbuji na Kondoo au kama ulivyo uadui wao na mbwa mwitu.

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَلَا يَنْفَكُونَ مِمَّا قَدْ كَانُوا فِيهَا وَهُمْ لَا يَخْتَفُونَ ۚ
 وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَى عَقْبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ ﴿١٣٧﴾ وَمَا كَانَ
 لِنَفْسٍ أَنْ تَمُوتَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ كَتَبْنَا مُؤَجَّلَاتٍ لَهَا وَمَنْ يُرِدْ ثَوَابَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا وَمَنْ
 يُرِدْ ثَوَابَ الْآخِرَةِ نُؤْتِهِ مِنْهَا وَسَنَجْزِي الشَّاكِرِينَ ﴿١٣٨﴾ وَكَأَيِّنْ مِنْ نَبِيٍّ قُتِلَ مَعَهُ رِبِّيُّونَ
 كَثِيرٌ فَمَا وَهَنُوا لِمَا أَصَابَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَمَا ضَعُفُوا وَمَا اسْتَكَانُوا ۗ وَاللَّهُ يُحِبُّ الصَّابِرِينَ
 ﴿١٣٩﴾ وَمَا كَانَ قَوْلُهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَإِسْرَافَنَا فِي أَمْرِنَا وَثَبِّتْ أَقْدَامَنَا
 وَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿١٤٠﴾ فَآتَاهُمُ اللَّهُ ثَوَابَ الدُّنْيَا وَحَسَنَّ ثَوَابَ الْآخِرَةِ
 وَاللَّهُ يُحِبُّ الْحَسِينَ ﴿١٤١﴾

144. Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma? Na atakayegeuka akarudi nyuma huyo hatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Atawalipa wanao mshukuru.

145. Na haiwezi nafsi kuwa ife ila kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu kama ilivyoandikwa ajali yake. Na mwenye kutaka malipo ya duniani Tutampa; na mwenye kutaka malipo ya Akhera Tutampa. Na Tutawalipa wenye kushukuru.

146. Na Manabii wangapi walipigana na pamoja nao Waumini wengi wenye ikhlasi! Hawakufanya woga kwa yaliyowasibu katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakudhoofika wala hawakuwa wanyonge. Na Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaosubiri.

147. Wala kauli yao haikuwa ila ni kusema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie madhambi yetu na kupondoka kwetu kupitia kiasi katika mambo yetu, na isimamishe imara miguu yetu na Utunusuru tuwashinde kaumu ya makafiri.

148. Basi Mwenyezi Mungu Akawapa malipo ya duniani na bora ya malipo ya Akhera. Na Mwenyezi Mungu Anawapenda wafanyao mema.

Maelezo Juu ya Uvumi wa Kufa Mtume ﷺ katika Vita vya Uhud. Na Ubainifu wa Msimamo Sahihi wa Kati wa Kufa Kwake.

Baadhi ya Waislamu walipokimbia katika vita vya Uhud na baadhi yao kuuawa. Shetani alipiga makelele, "Muhammad ameuawa." Na Ibn Qam-ah alirejea kwa mushirikina na kudai, "Nimemuua Muhammad." Kauli hii iliwavunja moyo Waislamu wengi.

Baadhi ya Waislamu, waliamini uvumi huo, wakadhani kuwa Mtume ﷺ alikuwa ameuawa kweli, wakidai kuwa hili linawezekana kujiri, kwani Allah تعالی alisema kuwa hili lilitokea kwa Mitume mingi kabla. Kwa hiyo, hali hiyo ilizifanya azma za Waislamu zidhoofike na hawakushiriki kwa nguvu kwenye vita. Kwa sababu hii Allah تعالی Alimteremshia wahyi Mjumbe Wake,

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ

"Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwisha pita kabla yake Mitume".

Jukumu lake ni kufikisha ujumbe wa Allah تعالی, na anaweza kuuawa akiwa katika jambo hilo, kama ilivyowatokea Mitume wengi kabla.

Ibn Abi Najih رحمه الله تعالی alisema kuwa baba yake alisema, mtu miongoni mwa Muhajirin alimpita mtu miongoni mwa Ansari akitokwa na damu (wakati wa Uhud) na akamuambia, "Ewe Bwana fulani! Unajua kuwa Muhammad

ameuawa?" Yule Ansari akajibu, "Hata kama Muhammad ﷺ angekuwa ameuawa, kwa hakika ameshafikisha Ujumbe. Kwa hiyo itetee Dini yako."

Aya iliteremshwa,

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ

"Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume".

Hadithi hii ilikusanywa na Al-Hafiz, Abu Bakar Al-Bayhaqi رحمه الله تعالى katika kitabu *Dalail An-Nabuwwah*.¹

Baadaye Allah تعالى Alisema huku akiwakosoa walioingiwa na udhaifu (baada ya kupata habari hiyo ya kifo).

أَفَايُن مَاتَ أَوْ قُتِلَ أُنْقَبْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ

"Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma?"

Mtarudi mlikotoka muwe tena makafiri,

وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَىٰ عَقْبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٨﴾

"Na atakayegeuka akarudi nyuma huyo hatamduru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Atawalipa wanao mshukuru."

Wanaoshukuru ni wale waliomtii Allah تعالى, wakaihami Dini yake na wakamfuata Mjumbe wake ama hai au amekufa. Sahih, *Musnad na Suna* zilikusanya isnadi mbalimbali zikielezea kuwa Abubakar رضي الله عنه alisoma Aya hii wakati Mtume ﷺ alipokufa. Bukhari alipokea kutoka kwa Aisha رضي الله عنها alisema kuwa Abubakar رضي الله عنه alikuja huku amepanda farasi wake kutoka nyumbani kwake - As-Sunj. Alishuka, akaingia Msikitini na hakusema na yeyote mpaka alipoingia chumbani mwa Aisha رضي الله عنها na akaenda moja kwa moja kwa Mtume ﷺ, ambaye alifunikwa kwa blanketi. Abubakar رضي الله عنه alimfunua uso wake, akapiga magoti na kum-busu, kisha akawa analia na kutangaza,

¹ *Dalail An-Nabuwwah* 3:248, Mapokezi haya ni *Mursal*.

“Baba yangu na mama yangu watolewe muhanga kwa ajili yako! Allah تعالی Hatokusababishia vifo viwili! Umekufa kifo ulichoandikiwa.”

Az-Zuhr kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alipokea kuwa; kisha Abubakar رضي الله عنه akatoka nje, wakati Umar رضي الله عنه akiwahutubia watu, na Abubakar رضي الله عنه akamtaka akae chini lakini Umar رضي الله عنه alikataa, na watu wakamsikiliza Abubakar رضي الله عنه na kumuacha Umar رضي الله عنه. Abubakar رضي الله عنه alisema, “Yeyote aliyekuwa akimuabudu Muhammad ﷺ, kwa hakika Muhammad ﷺ amefariki dunia, lakini yule aliyekuwa akimuabudu Allah تعالی basi Allah تعالی Yuko Hai na Hatokufa abadani.” Allah تعالی Amesema,

وَمَا مُحَمَّدٌ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ أَفَإِنْ مَاتَ أَوْ قُتِلَ انْقَلَبْتُمْ عَلَى أَعْقَابِكُمْ
وَمَنْ يَنْقَلِبْ عَلَى عَقْبَيْهِ فَلَنْ يَضُرَّ اللَّهَ شَيْئًا وَسَيَجْزِي اللَّهُ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٨﴾

“Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume. Je, akifa au akauwawa ndiyo mtageuka mrudi nyuma? Na atakayegeuka akarudi nyuma huyo hatamduru kitu Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Atawalipa wanao mshukuru.”

Msimulizi aliongeza, “Wallahi ilikuwa kama ndio mara ya kwanza Aya ile inateremshwa pale Abubakar رضي الله عنه alipoisoma, na tena kila aliyeisikia alianza kuisoma.” Said bin Al-Musayyib alisema kuwa Umar رضي الله عنه alisema, “Wallah! Nilipomsikia Abubakar رضي الله عنه akiisoma Aya hii, miguu yangu iliishiwa nguvu na nikaanguka chini.”¹

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَنْ تَمُوتَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ كِتَابًا مُؤَجَّلًا ﴿١٤٩﴾

“Na haiwezi nafsi ife ila kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu kama ilivyoandikwa ajali yake.”

Maana yake: hapana anayekufa ila kwa Uamuzi wa Allah تعالی, baada ya kumaliza kipindi alichandikiwa na Allah تعالی. Kwa sababu hii Allah تعالی Amesema,

¹Fat’hul Al-Bari 7:751.

كِتَابًا مُّوجَّلاً^١

“Kama ilivyoandikiwa ajali yake”. Ambayo ni sawa na Kauli Yake,

وَمَا يُعَمَّرُ مِنْ مُّعَمَّرٍ وَلَا يُنْقَصُ مِنْ عُمُرِهِ إِلَّا فِي كِتَابٍ

“Na wala hapawi umri mwenye umri mrefu, wala hapunguziwi katika umri wake, ila yamo hayo katika Kitabu.” (35:11)

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ طِينٍ ثُمَّ قَضَىٰ أَجَلًا^٢ وَأَجَلٌ مُّسَمًّى عِنْدَهُ

“Yeye Ndiye Aliyekuumbeni kwa udongo, kisha Akakuhukumieni ajali, na muda maalumu uko kwake tu.” (6:2)

Aya hii (3:145) inawashajihisha watu waoga na kuwaandaa washiriki katika vita, kwani kufanya hivyo, au kukwepa vita hakupunguzi, wala kuongeza muda wa kuishi. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kutoka kwa Habib bin Subhan alisema kuwa Mtu mmoja miongoni mwa Waislamu aitwae, Hujri bin Adiy, alisema katika vita, “Kitu gani kinawazuieni kuvuka mto huu wa Dijla (Euphrates) kuwaendea maadui?” Kisha alisoma:

وَمَا كَانَ لِنَفْسٍ أَنْ تَمُوتَ إِلَّا بِإِذْنِ اللَّهِ كِتَابًا مُّوجَّلاً^٣

“Na haiwezi nafsi ife ila kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu kama ilivyoandikwa ajali yake.” (3:145)

Kisha alivuka mto akimpanda farasi wake, na alipovuka Waislamu walimfuata. Adui walipowaona, walianza kupiga kelele, “*Diwani* (Kiuajemi, ni ifriti mkubwa), na wakakimbia.”¹ Allah تعالى Amesema:

وَمَنْ يُرِدْ ثَوَابَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا وَمَنْ يُرِدْ ثَوَابَ الْآخِرَةِ نُؤْتِهِ مِنْهَا

“Na mwenye kutaka malipo ya duniani Tutampa; na mwenye kutaka malipo ya Akhera Tutampa”.

Kwa hiyo, Aya inatangaza kuwa, yeyote anayefanya amali kwa ajili ya maisha ya dunia, atavuna kile Allah تعالى Alichomuandikia. Hata hivyo hatakuwa na hisa Akhera. Na Yeyote anayefanya amali kwa ajili ya Akhera, Allah تعالى

¹ Ibn Hatim 2:584.

Atampa fungu lake Kiyama, pamoja na yale Atakayompa hapa duniani. Kwa kauli sawa na hiyo, Allah تعالى Amesema,

مَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الْآخِرَةِ نَزِدْ لَهُ فِي حَرْثِهِ ۗ وَمَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الدُّنْيَا نُؤْتِهِ مِنْهَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ نَصِيبٍ ﴿٢٠﴾

“Mwenye kutaka mavuno ya Akhera Tutamzidishia katika mavuno yake, na mwenye kutaka mavuno ya duniani Tutampa katika hayo, lakini katika Akhera hana fungu.” (42:20)

Na Allah تعالى Amesema,

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَنْ نُرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ يَصَلِّيهَا مَذْمُومًا مَدْحُورًا ﴿١٧﴾ وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ سَعْيُهُمْ مَشْكُورًا ﴿١٨﴾

“Anayetaka yapitayo upesi upesi, Tutafanya haraka kumletea hapa hapa Tunayoyataka kwa Tumtakaye. Kisha Tumemuekea Jahannamu; ataingia humo hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa na kufurushwa. Na anayeitaka Akhera, na akazifanyia juhudi amali zake, naye ni Muumini, basi hao juhudi yao itakuwa ni ya kushukuriwa.” (17:18-19)

وَسَنَجْزِي الشَّاكِرِينَ ﴿١٤﴾

“Na Tutawalipa wenye kushukuru”

Maana yake: Tutawalipa kwa Rehma na Huruma zetu, hapa duniani na Akhera, kila mmoja kulingana na kiwango chake cha kushukuru na ukubwa wa amali yake. Kisha Allah تعالى Anawafariji waumini kutokana na madhara waliyopata katika Uhud,

وَكَأَيِّن مِّن نَّبِيٍّ قَاتَلَ مَعَهُ رِيشُونَ كَثِيرٌ

“Na Manabii wangapi walipigana na pamoja nao Waumini wengi wenye ikhlasi!” (3:146)

Ilisemwa kuwa Aya hii ina maana kuwa Mitume wengi na wafuasi wao waliuawa siku zilizopita. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amechagua rai hii. Ilisemwa pia kuwa Aya hii ina maana Mitume wengi walishuhudia wafuasi wao wakifariki dunia mbele yao. Pamoja na hayo, Ibn Ishaq رحمه الله تعالى ametoa maelezo mengine katika Sirah yake, akisema kuwa Aya hii ina maana, "Mitume wengi waliuawa, na walikuwa na wafuasi wengi ambao maamuzi yao haya-kuwadhoofisha baada ya kufariki dunia Mitume yao, hawakuwa dhalili mbele ya adui. Kukhasirika na kuumia kwao katika Jihad katika njia ya Allah تعالى na kwa ajili ya Dini yao na hakukuwavunja moyo." Huu ndio ustahamilivu.

وَاللَّهُ يُحِبُّ الصَّابِرِينَ ﴿١٣٧﴾

"Na Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaosubiri."

As-Suhayli aliyaunga mkono maelezo haya na akayatetea kwa uwezo wake wote. Rai hii inaungwa mkono na Kauli ya Allah تعالى.

مَعْدُرَ رَبِّيُونَ كَثِيرٌ ﴿١٣٨﴾

"Pamoja nao waumini wengi wenye ikhlasi!"

Katika kitabu chake juu ya vita, Al-Amawi alitaja maelezo haya tu kuhusu Aya hii.

Sufyan Ath-Thawri رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Mas'ud عنه رضي الله alisema kuwa,

رَبِّيُونَ كَثِيرٌ ﴿١٣٩﴾

"Waumini wengi wenye ikhlasi!" Mradi wake, maelfu.¹ Ibn Abbas, Mujahid, Said bin Jubayr, Ikrim Al-Hasan, Qatadah, As-Suddi, Ar-Rabi na Ata Al-Khurasani رضي الله عنهم walisema kuwa neno *Ribbiyyan* lina maana, makundi ya watu.² Abdur - Razzaq alisimulia kutoka kwa Ma'mmar kutoka kwa Al-Hasan alisema kuwa,

رَبِّيُونَ كَثِيرٌ ﴿١٤٠﴾

"Waumini wengi wenye ikhlasi!"

Maana yake: Wanazuoni wengi. Pia alisema kuwa muradi wake ni wanazuoni wachamungu na wastahamilivu.

¹ Al-Tabari 7:266.

² Ibn Abi Hatim 2:587-588.

فَمَا وَهَنُوا لِمَا أَصَابَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَمَا ضَعُفُوا وَمَا اسْتَكَانُوا^١

“Hawakufanya woga kwa yaliyowasibu katika njia ya Mwenyezi Mungu, wala hawakudhoofika wala hawakuwa wanyonge.”

Qatadah na Ar-Rabi bin Anas walisema kuwa,

وَمَا ضَعُفُوا

“Wala hawakudhoofika.” Ina maana, baada ya kuuawa kwa Mtume wao.¹

وَمَا اسْتَكَانُوا

“Na hawakuwa wanyonge.” Mradi wake, wala hawakufadhaishwa, ambapo As-Suddi na Ibn Zayd walisema, ina maana hawakujisalimisha kwa adui.

وَاللَّهُ يُحِبُّ الصَّابِرِينَ ﴿١٤٦﴾ وَمَا كَانَ قَوْلُهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَإِسْرَافَنَا فِي

أَمْرِنَا وَتُبِّتْ أَقْدَامَنَا وَانصُرْنَا عَلَى الْقَوْمِ الْكَافِرِينَ ﴿١٤٧﴾

“Na Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaosubiri. Wala kauli yao haikuwa ila ni kusema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie madhambi yetu na kupita kwetu kiasi katika mambo yetu, na isimamishe imara miguu yetu na Utunusuru tuwashinde kaumu ya makafiri.”
(3:146-147).

Maana yake: Hawakuwa na maneno mengi isipokuwa hayo.

فَقَاتِلْهُمْ اللَّهُ تَوَّابٌ أَلَدُنْيَا

“Basi Mwenyezi Mungu Akawapa malipo ya Dunia.” (3:148)

Ushindi, mafanikio na mwisho mwema,

وَحُسْنِ ثَوَابٍ آخِرَةٍ

“Na bora ya malipo ya Akhera.”

وَاللَّهُ يُحِبُّ الْحَسِنِينَ ﴿١٤٨﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anawapenda wafanyao mema.”

¹ Abu Hatim 2:591.

يَتَّأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَطِيعُوا الَّذِينَ كَفَرُوا
يُرُدُّوكُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ فَتَنْقَلِبُوا خَاسِرِينَ ﴿١٤٩﴾ بَلِ اللَّهُ
مَوْلَانِمْ ۖ وَهُوَ خَيْرُ النَّاصِرِينَ ﴿١٥٠﴾ سَنُلْقِي فِي قُلُوبِ
الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ بِمَا أَشْرَكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ
سُلْطَانًا ۖ وَمَأْوَهُمُ النَّارُ ۖ وَبِئْسَ مَتْوَى الظَّالِمِينَ ﴿١٥١﴾
وَلَقَدْ صَدَقَكُمُ اللَّهُ وَعْدَهُ إِذْ تَحُسُّونَهُم بِإِذْنِهِ ۖ
حَتَّىٰ إِذَا فَشِلْتُمْ وَتَنَزَّعْتُمْ فِي الْأَمْرِ وَعَصَيْتُمْ مِمَّن بَعْدَ مَا
أَرْزَكُم مَّا تُحِبُّونَ ۖ مِنْكُمْ مَّن يُرِيدُ الدُّنْيَا وَمِنْكُمْ
مَّن يُرِيدُ الآخِرَةَ ۖ ثُمَّ صَرَفَكُمْ عَنْهُمْ لِيَبْتَلِيَكُمْ ۖ وَلَقَدْ عَفَا
عَنْكُمْ ۗ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥٢﴾ * إِذْ
تُضْعَدُونَ وَلَا تَلَوْنَهَا عَلَىٰ أَحَدٍ ۖ وَالرَّسُولُ
يَدْعُوكُمْ فِي أَخْرَجِكُمْ فَأَتَيْتُمُ عَمَّا بَعَرِ لِكَيْلًا
تَحْزَنُوا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا مَا أَصَبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ خَبِيرٌ
بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٥٣﴾

149. Enyi mlioamini! Ikiwa mtawatii waliokufuru watakurudisheni nyuma, na hapo mtageuka kuwa wenye kupata hasara.

150. Bali Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wenu, Naye Ndiye bora wa wasaidizi.

151. Tutazitia khofu nyoyo za waliokufuru kwa vile walivyomshirikisha Mwenyezi Mungu na washirika ambao hakuwateremshia hoja yoyote. Na makazi yao ni Motoni; na maovu yaliyoje maskani ya wenye kudhulumu!

يَتَّأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَطِيعُوا
الَّذِينَ كَفَرُوا يُرُدُّوكُمْ عَلَىٰ
أَعْقَابِكُمْ فَتَنْقَلِبُوا خَاسِرِينَ ﴿١٤٩﴾ بَلِ
اللَّهُ مَوْلَانِمْ ۖ وَهُوَ خَيْرُ النَّاصِرِينَ ﴿١٥٠﴾
سَنُلْقِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ
كَفَرُوا الرُّعْبَ بِمَا أَشْرَكُوا بِاللَّهِ مَا
لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ سُلْطَانًا ۖ وَمَأْوَهُمُ النَّارُ ۖ
وَبِئْسَ مَتْوَى الظَّالِمِينَ ﴿١٥١﴾
وَلَقَدْ صَدَقَكُمُ اللَّهُ وَعْدَهُ إِذْ
تَحُسُّونَهُم بِإِذْنِهِ ۖ حَتَّىٰ إِذَا
فَشِلْتُمْ وَتَنَزَّعْتُمْ فِي الْأَمْرِ وَعَصَيْتُمْ
مِمَّن بَعْدَ مَا أَرْزَكُم مَّا تُحِبُّونَ ۖ
مِنْكُمْ مَّن يُرِيدُ الدُّنْيَا وَمِنْكُمْ
مَّن يُرِيدُ الآخِرَةَ ۖ ثُمَّ صَرَفَكُمْ
عَنْهُمْ لِيَبْتَلِيَكُمْ ۖ وَلَقَدْ عَفَا عَنْكُمْ ۗ

وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥٢﴾

* إِذْ تُضْعَدُونَ وَلَا تَلَوْنَهَا عَلَىٰ

أَحَدٍ ۖ وَالرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ فِي

أَخْرَجِكُمْ فَأَتَيْتُمُ عَمَّا بَعَرِ لِكَيْلًا

تَحْزَنُوا عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ

وَلَا مَا أَصَبَكُمْ ۗ وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا

تَعْمَلُونَ ﴿١٥٣﴾

152. Na Mwenyezi Mungu Alikutimilizieni miadi Yake, vile mlivyo kuwa mnawaua kwa Idhini Yake, mpaka mlipolegea na mkazozana juu ya amri, na mkaasi baada ya Yeye Kukuonesheni mliyo yapenda. Wapo miongoni mwenu wanaotaka dunia, na wapo miongoni mwenu wanaotaka Akhera. Kisha Akakutengeni nao (maadui) ili Akujaribuni. Naye sasa Amekwisha Kusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila juu ya Waumini.

153. Pale mlipokuwa mkikimbia mbio wala hamumsikilizi yeyote, na Mtume anakuiteni, yuko nyuma yenu. Mwenyezi Mungu Akakupeni dhiki juu ya dhiki, ili msisikitike kwa yaliyokukoseeni wala kwa yaliyokusibuni. Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za yote mnayoyatenda.

Katazo la Kuwatii Makafiri; na Ubainifu wa Sababu ya Yaliyotokea katika Uhud Kuhusu Kunusurika na Kushindwa:

Allah تعالی aliwaonya waja Wake waumini dhidi ya kuwatii makafiri na wanafiki, kwa sababu utii huo utasababisha kukhasirika hapa duniani na kesho Akhera. Kutokana na hilo Allah تعالی Anasema

﴿إِنْ تُطِيعُوا الَّذِينَ كَفَرُوا يُرْدُوكُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ فَتَنْقَلِبُوا حَسْرِينَ﴾

“Ikiwa mtawatii waliokufuru watakurudisheni nyuma, na hapo mtageuka kuwa wenye kukhasiri”. (3:149)

Kisha Allah تعالی Amewaamrisha waumini kumtii Yeye, Awe Mlinzi wao watake msaada Wake na kumtegemea Yeye. Allah تعالی Amesema

﴿بَلِ اللَّهِ مَوْلَانِكُمْ ۖ وَهُوَ خَيْرُ النَّاصِرِينَ﴾

“Bali Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wenu, Naye Ndiye Mbora wa wasaidizi”. (3:150)

Baadaye Allah تعالی Anawapa bishara njema kuwa Atatia hofu katika nyoyo za maadui ili wawaogope Waislamu na wawe na hisia za kuwa dhalili mbele ya Waislamu, kwa sababu ya ukafiri na ushirikina wao. Na Allah تعالی Anawangojelea adhabu kubwa akhera.

Allah تعالی Amesema,

سَنُلْقِي فِي قُلُوبِ الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ بِمَا أَشْرَكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ سُلْطَانًا
وَمَاؤْنَهُمُ النَّارُ وَيُسَّ مَثْوَى الظَّالِمِينَ ﴿١٥١﴾

“Tutazitia khofu nyoyo za waliokufuru kwa vile walivyomshirikisha Mwenyezi Mungu na washirika ambao hakuwateremshia hoja yoyote. Na makazi yao ni Motoni; na maovu yaliyoje maskani ya wenye kudhulumu!”(3:151)

Kwa nyongeza, imeandikwa katika Sahihi mbili kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema

«أُعْطِيتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ قَبْلِي: نُصِرْتُ بِالرُّعْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ، وَجُعِلَتْ لِي الْأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهْرًا، وَأُجِلَّتْ لِي الْعَنَائِمُ، وَأُعْطِيتُ السَّفَاعَةَ، وَكَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ خَاصَّةً وَيُبْعَثُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً»

“Nilipewa vitu vitano ambavyo hakupewapo yoyote miongoni mwa Mitume kabla yangu. Nilinusuriwa na hofu masafa ya mwezi mmoja, ardhi imefanywa kwangu kuwa Msikiti na sehemu ya kujitoharisha, niliruhusiwa kuchukua ngawira, nilipewa uombezi wa watu, na ilikuwa Mtume akitumwa kwa watu wake, na mimi nimetumwa kwa watu wote.”¹

Allah تعالى Amesema,

وَلَقَدْ صَدَقَكُمُ اللَّهُ وَعْدَهُ

“Na Mwenyezi Mungu Alikutimilizieni miadi Yake,...” (3:152)

Mwanzoni mwa mchana wa siku ya Uhud

إِذْ تَحْسُونَهُمْ

“Vile mlivyokuwa mnawauwa.”

Maana yake: Mkiwachinja maadui zenu,

بِإِذْنِهِ

“Kwa Idhini Yake.” Kwa kuwaruhusu kuwatendea hayo.

¹ Fat’hul Al-Bari 1:519 na Muslim 1:370.

حَتَّىٰ إِذَا فَشِلْتُمْ

“Mpaka mlipolegea.”

Ibn Jurayj رحمه الله تعالى alisema, Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa “Al-Fashal” Maana yake, “woga.”¹

وَتَنَزَعْتُمْ فِي الْأَمْرِ وَعَصَيْتُمْ

“Na mkazozana juu ya Amri, na mkaasi.” (3:152)

Mfano wake ni lile kosa lililofanywa na watupa mishale mlimani.

مِنْ بَعْدِ مَا أَرْسَلْنَاكُمْ مَا تُحِبُّونَ

“Baada ya Yeye Kukuonesheni mliyoyapenda.” (3:152)

Maana yake: Ushindi dhidi ya makafiri.

مِنْكُمْ مَنْ يُرِيدُ الدُّنْيَا

“Wapo miongoni mwenu wanaotaka dunia.”

Ikiwazungumzia wale walioamua kwenda kukusanya ngawira walipowaona maadui wakishindwa,

وَمِنْكُمْ مَنْ يُرِيدُ الْآخِرَةَ ۖ ثُمَّ صَرَفَكُمْ عَنْهُمْ لِيَبْتَلِيَكُمْ

“Na wapo miongoni mwenu wanaotaka Akhera. Kisha Akakutengeni nao (maadui) ili Akujaribuni.”

Aya hii ina maana, Allah تعالى Aliwapa ushindi maadui ili Akujaribuni, Enyi waumini, na Akupeni mtihani,

وَلَقَدْ عَفَا عَنْكُمْ

“Naye sasa amekwisha kusameheni.”

Aliwasamehe kwa kosa hilo mlilotenda, kwa sababu washirikina walikuwa wengi na wenye zana za kutosha, ambapo Waislamu walikuwa wachache na vifaa vichache. Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

¹ At - Tabari 7:291.

Bukhari alipokea kuwa Al-Bara رضي الله عنه alisema. "Tulipambana na washirikina siku ya Uhud na Mtume ﷺ alimteua Abdullah bin Jubayr رضي الله عنه kuwa kamanda wa watupa mishale. Alimuagiza, "Bakini katika sehemu zenu, hata kama mkiona tumewashinda, msiondoke katika sehemu zenu. Na iwapo mtaona wametushinda msikimbilie kutusaidia." Makafiri walikimbia tulipopambana nao, na tuliwaona wanawake wao wakikimbilia mlimani huku wakipandisha nguo zao huku wakiacha wazi magoti na miguu yao. Hivyo, wafuasi wa Abdullah bin Jubayr رضي الله عنه walisema, "Ngawira ngawira." Abdillah bin Jubair alisema: 'Niliwanasahi kuhusu maneno ya Mtume, walikataa na kuondoka katika maeneo yao.' Hawakumsikiliza, na walipogura kutoka maeneo yao, Waislamu walishindwa na sabini miongoni mwao waliuawa. Abu Sufyan alipiga kelele, "Je Muhammad ni miongoni mwao hawa watu?" Mtume ﷺ akasema 'Msimjibu!' Kisha akauliza, 'Je, Mtoto wa Abu Quhafa (Abubakar) yupo miongoni mwa watu hawa?' Mtume ﷺ akasema, 'Msimjibu!' Akauliza tena, 'Je mtoto wa Al-Khattab (Umar رضي الله عنه) alikuwepo pamoja na watu hawa? Ama kuhusu watu hawa, wamekwishauawa kwani kama wangekuwa hai wangenijibu." Umar رضي الله عنه hakuweza kujizuia na akamuambia Abu Sufyan, "Umesema uongo, Ewe adui wa Allah! Hakika waliobakishwa na Allah wanatosha kukuadabisha." Abu Sufyan, akasema, "Limetukuka sanamu la Hubal." Mtume ﷺ aliwaambia Maswahaba wake, "Mjibuni!" Wakauliza!" "Tutamuambia nini?" Akasema, 'Semeni, Allah تعالى Ametukuka na Mtukufu zaidi.' Abu Sufyan akasema, "Tuna Al-Uzza, nanyi hamna Uzza." Mtume ﷺ akawaambia, 'Mjibuni!, Wakamuuliza, 'Tumuambieje?' Akawaambia, 'Semeni, Allah تعالى ni Mlinzi wetu nanyi hamna mlinzi.' Abu Sufyan akasema, 'Ushindi wetu leo ni kisasi cha ushindi wenu katika Vita vya Badri, na katika vita, ushindi huwa haufahamiki na pande zinazopigana hupokezana ushindi. Mtawaona baadhi ya watu wenu wamekatwa katwa viungo, japokuwa sikuwataka watu wangu, wafanye hivyo, hata hivyo sisikitiki kwa tendo lao hilo." Bukhari pekee ndiye aliyeipokea Hadithi hii kwa njia hii ya upokezi.¹

Muhammad bin Is'haq رحمته الله تعالى alisema kuwa, Abdullah bin Az - Zubayr alisimulia kuwa Az-Zubayri bin Al-Awwam رضي الله عنه alisema, 'Wallahi! Nilimuona mtumishi wa kike na mjakazi wa Hindu (mke wa Abu Sufyan)

¹ Fat'hul Al-Bari 7:405.

walipofunua miguu yao na kukimbia. Wakati huo haikuhitajika juhudi ndogo wala kubwa ili kuwakamata. Hata hivyo, wapiga mishale walishuka juu ya mlima maadui walipokimbia kutoka uwanja wa vita, wakitaraji kukusanya ngawira. Waliacha wazi safu yetu ya nyuma kwa wapanda farasi wa Jeshi la Makafiri, ambao waliitumia fursa hiyo kutushambulia kutoka kwa nyuma. Kisha mtu mmoja alipiga kelele, '*Muhammad ameuwawa!*'. Hivyo tulirudi nyuma na makafiri wakatufuata, baada ya kuwaua waliobeba bendera yao, na hakuna aliyethubutu kuisogelea bendera mpaka wakati huo. Baadaye Muhammad bin Is'haq رحمه الله تعالى alisema, "Bendera ya makafiri iliachwa chini mpaka Amrah bint Al-zama Al-Harithiyah alipoikota na kuwapa Maquraish ambao waliibeba. Allah تعالى Amesema:

ثُمَّ صَرَفَكُمْ عَنْهُمْ لِيَبْتَلِيَكُمْ

"Kisha Akakutengeni nao (maadui) ili Akujaribuni." (3:152)

Ibn Is'haq رحمه الله تعالى amesema, 'Nimehadithiwa na Al-Qasim bin Abdul-Rahman bin Rafi, mmoja katika kabila la Bani Adiy bin An-Najar, ambaye alisema Anas bin An - Nadhir ami yake Anas bin Malik alikwenda kwa Umar Bin Al-Khattwab رضي الله عنه na Talha bin Ubaydullah رضي الله عنه pamoja na watu katika Muhajirun na Ansar ikiwa wameshakutana na kipigo, akawaauliza, 'Nini kinachowahuzunisha?' Wakajibu, 'Mtume ﷺ ameuawa.' Akawaambia, 'Kama ni hivyo nini faida ya kuishi baada ya kifo chake? Simameni mfie katika alichofia!" Kisha akakabiliana na adui, akapigana hadi alipouawa.¹ Bukhari alipokea kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema, "Ami yangu Anas bin An - Nadhir na hakushiriki vita vya Badr, alisema, 'Sikuwepo katika vita vya mwanzo Mtume ﷺ alipopigana na wapagani. *Wallah!* Endapo Allah تعالى Atanipa fursa ya kupigana nikiwa na mjumbe wa Allah, basi Allah تعالى Ataona ushujaa wangu katika vita.' Siku ya Uhud wakati Waislamu walipogezwa migongo na kukimbia, alisema, "Ewe Allah! Ninaomba radhi kwako kwa hili walilolifanya Waislamu, na ninajitakasa na waliyoyafanya mapagani!' Kisha akasonga mbele huku ameinua upanga wake, na Sa'd bin Mu'adh رضي الله عنه alipokutana naye alimuambia, 'Ewe Sa'd bin Muadh! Uko wapi! Peponi! Naisikia harufu ya pepo ikitokea Mlima Uhud na akasonga mbele, akipigana na akauawa. Tulikuta

¹ Ibn Hisham 3:88.

zaidi ya majeraha themanini ya mapanga na mishale kwenye mwili wake, ambao ulikatwakatwa vibaya sana, na hapana aliyemtambua isipokuwa dada yake, na aliweza kwa kuangalia vidole vyake." Hii ni Hadithi iliyopokewa na Bukhari.¹ Pia Muslim alipokea sawa na hadithi hii kutoka kwa Thabit رضي الله عنه kutoka kwa Anas رضي الله عنه.²

Matatizo Yaliyowapata Baadhi ya Waislamu katika Vita vya Uhud

Allah تعالى Amesema,

﴿ إِذْ تَضَعُ دُونَكَ وَلَا تَلُودَنَّ عَلَى أَحَدٍ ﴾

"Pale mlipokuwa mkikimbia mbio wala hamumsikilizi yeyote."

Na Allah تعالى Aliwafanya makafiri wawaache baada ya nyie kupanda Mlima ili kuwakimbia maadui zenu. Al-Hasan, Qatadah walisema kuwa *Tus'iduna* ina maana ya "Kukwea mlima."³

﴿ وَلَا تَلُودَنَّ عَلَى أَحَدٍ ﴾

"Wala hamumsikilizi yeyote."

Maana yake: Hamkumsikiliza yeyote kutokana na mshituko na woga.

﴿ وَالرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ فِي أَخْرَانِكُمْ ﴾

"Na Mtume anakuiteni, yuko nyuma yenu."

Kwani mlimuacha nyuma, wakati alipokuwa akiwataka muache kuwakimbia maadui na warejee katika medani ya vita kuendelea na mapigano. As-Suddi alisema, "Makafiri walipozishambulia safu za Waislamu wakati wa Vita vya Uhud na kuwashinda, baadhi ya Waislamu walikimbilia Madinah, ambapo wengine walipanda mlima Uhud, na wakasimama juu ya jabali." Mtume ﷺ akawa anawaita, *'Njooni kwangu, enyi waja wa Allah!'* Allah تعالى Ametaja kupanda kwao Mlima na kuwa Mtume ﷺ aliwataka warejee na Akasema,

¹ Fat'hul Al-Bari 7:411.

² Muslim Na. 3:1512.

³ Ibn Abu Hatim 2:609.

﴿ إِذْ تُصْعِدُونَ وَلَا تَلْوُونَ عَلَىٰ أَحَدٍ وَالرَّسُولُ يَدْعُوكُمْ فِيٰ أُخْرَانِكُمْ ﴾

“Pale mlipokuwa mkikimbia mbio wala hamumsikilizi yeyote, na Mtume anakuiteni, yuko nyuma yenu.” (3:153)¹

Pia Ibn Abbas, Qatadah, Ar-rabi na Ibn Zayd رضي الله عنهم walinena sawa na hayo²

Ansar na Muhajirin Walivyomhami Mtume ﷺ Siku ya Uhud.

Bukhari alipokea kutoka kwa Qays bin Abi Hazim alisema kuwa, “Niliuona mkono wa Talha umepooza, kwa sababu ya kumkinga Mtume ﷺ kwa mkono huo.” Yaani, siku ya Uhud.³ Imeandikwa katika Sahih Mbili kuwa Abu Uthman An-Nahdi alisema, “Katika siku ya Uhud siku ambayo Mtume ﷺ alipigana, Talha bin Ubaydullah na Sa’d ndiyo pekee waliobaki na Mtume.”⁴

Sa’id bin Al-Musayyib alisema, “Nilimsikia Sa’d bin Abi Waqqas رضي الله عنه akisema “Mtume ﷺ alinipa mishale siku ya Uhud na kaniambia, “*Tupa, hata baba yangu na mama yangu naweza kuwatoa fidia kwa ajili yako!*” Bukhari aliipokea Hadithi pia.⁵

Sahihi mbili ziliandika kuwa Sa’d bin Abi Waqqas رضي الله عنه alisema, “Katika siku ya Uhud, niliwaona watu wawili wamevaa nguo nyeupe, mmoja yuko upande wa kulia wa Mtume ﷺ na mwingine kushotoni ambao wakimhami Mtume ﷺ kwa bidii kubwa. Sikuwahi kuwaona watu hao kabla au baada ya siku ile. Yaani malaika Jibril عليه السلام na Mika’il عليه السلام.”⁶ Abu Al-As’wad alisema kuwa, Urwah bin Az-Zubayr رضي الله عنه alisema, “Ubayy bin Khalaf ndugu wa Bani Jumah aliapa akiwa Makkah kuwa angemuua Mtume ﷺ. Mtume ﷺ alipopewa habari ya kiapo hicho, alisema, “*Bali, nitamuua mimi, Allah Akiniridhia.*” Siku ya Uhud, Ubayy alikuja akiwa amevaa nguo za chuma na akinadi, ‘Hakuna ushindi, iwapo Muhammad atasalimika.’ Kisha alielekea

¹ Al-Tabari 7:301.

² Al-Tabari 7:303.

³ Fat’hul Al-Bari 7:416 .

⁴ Bukhari Na. 4055 na Muslim (2306).

⁵ Bukhari Na. 4055.

⁶ Bukhari Na. 4054 na Muslim 2306.

alipokuwa Mtume ﷺ kwa nia ya kumuua, lakini Mus'ab bin Umayr رضي الله عنه, kutoka Bani Abd Ddar alimzuia na kumkinga Mtume ﷺ kwa kiwiliwili chake, na hapo Mus'ab bin Umayr رضي الله عنه aliuawa. Mtume ﷺ aliona shingo ya Ubayy kati ya ngao na kofia ya chuma, akamjua kisha akamchoma kwa mkuki wake kupitia uwazi ule, na Ubayy alianguka chini kutoka katika farasi wake. Hata hivyo hakuna damu iliyochuruzika kutoka katika jeraha lake. Walikuja jamaa zake na kumbeba huku akilia kwa mngurumo kama ng'ombe dume, nao wakamuambia: 'Woga wa nini? Umepatwa na mkwaruzo kidogo tu.'

Ubayy akawatajia kiapo cha Mtume alichopa kuwa, '*Bali mimi nitamuua Ubayy!*' Kisha akasema, 'Naapa kwa Yule ambaye roho yangu iko Mikononi Mwake! Iwapo kilichonipiga kingewapiga watu wa *Dhul - Majaz* (soko la kale kabla ya Uislamu), wote wangekufa.' Kisha akafa na kuingizwa Motoni. Hadithi hii ameipokea Mussa bin Uqbah katika masimulizi yake kuhusu vita - *Al-Maghazi* kutoka kwa Az - Zuhri na kutoka kwa Said bin Al - Musayyib imepokewa Hadithi kama hii.

Imeandikwa ndani ya Sahih mbili kuwa alipoulizwa kuhusu majeraha aliyopata Mtume ﷺ katika Uhud, Sahl bin Sa'd رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ yalivunjwa, meno yake ya mbele na kofia yake ya chuma ilipigwa akiwa ameivaa. Mpaka, Fatimah, bint wa Mtume ﷺ alipoona damu inazidi kutoka kwa kuoshwa kwa maji mikononi mwake, alichukua mkeka, akauchoma moto na akayapaka majivu kwenye majeraha ya Mtume ﷺ na hapo damu iliacha kuvuja."¹

Allah تعالى Amesema:

فَأَثْبِكُمُ غَمًّا يَغْمِرُ

***"Mwenyezi Mungu Akakupeni dhiki juu ya dhiki."* (3:153)**

Alikutieni huzuni juu ya huzuni. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Huzuni ya kwanza ilitokana na kushindwa, hasa ilipovumishwa kuwa Muhammad ﷺ aliuawa. Huzuni ya pili ni pale washirikina walipopanda mlima na kuwashambulia Waislamu na Mtume ﷺ akasema, '*Ewe Allah! Wao hawastahiki kuwa juu yetu.*' Abdul - Rahman bin Awf رضي الله عنه alitafsiri kuwa, 'Huzuni ya kwanza ni kwa sababu ya kushindwa na ya pili ni ya wakati tetesi kuwa

¹ Bukhari 2911, 4075 na Muslim 1790.

Muhammad ﷺ alikuwa ameuawa, hili kwao lilikuwa baya kabisa kuliko kushindwa." Ibn Marduwyah alipokea riwaya hizo mbili. Mujahid na Qatadah walisema, "Huzuni ya kwanza ni pale waliposikia kuwa Muhammad ﷺ alikuwa ameuawa na huzuni ya pili ni kwa waliouawa na kujeruhiwa." Pia ilipokewa kutoka kwa Qatadah na Ar - Rabi bin Anas kuwa walisema ilikuwa kinyume chake. As-Suddi alisema kuwa, 'Huzuni ya kwanza ni kwa sababu ya ushindi na ngawira walizozikosa, ya pili ni maadui kuwa juu yao (juu ya mlima)."

Allah تعالیٰ Amesema,

لَيْسَ مَا فَاتَكُمْ

"Ili msisikitike kwa yaliyo kukoseni."

Kwa kukosa ngawira na kuwashinda maadui zenu.

وَلَا مَا أَصَبَكُمْ

"Wala kwa yaliyo kusibuni."

Maumivu na vifo, kama Ibn Abbas, 'Abdur – Rahman bin 'Awf, Al-Hasan. Qatadah na As-Suddi رضي الله عنهم walivyonena hayo.¹

* * *

¹ Ibn Abi Hatim 2:613.

ثُمَّ أَنْزَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ بَعْدِ الْغَمِّ أَمَنَةً
 نِعَاسًا يَغْشَى طَائِفَةً مِنْكُمْ ط وَطَائِفَةٌ
 قَدْ أَهَمَّتْهُمْ أَنْفُسُهُمْ يَظُنُّونَ بِاللَّهِ
 غَيْرَ الْحَقِّ ظَنَّ الْجَاهِلِيَّةِ ط يَقُولُونَ
 هَلْ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ مِنْ شَيْءٍ ط قُلْ إِنْ
 الْأَمْرُ كُلُّهُ لِلَّهِ ط تَخْفُونَ فِي أَنْفُسِهِمْ مَا
 لَا يُبْدُونَ لَكُمْ ط يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا
 مِنْ الْأَمْرِ شَيْءٌ مَا قُتِلْنَا هَاهُنَا ط قُلْ لَوْ
 كُنْتُمْ فِي بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ الَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ
 الْقَتْلُ إِلَى مَضَاجِعِهِمْ ط وَلِيَبْتَلِيَ اللَّهُ مَا
 فِي صُدُورِكُمْ وَلِيُمَحِّصَ مَا فِي قُلُوبِكُمْ ط
 وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١٥٤﴾
 إِنَّ الَّذِينَ تَوَلَّوْا مِنْكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ
 إِنَّمَا أَسْتَرْلَهُمُ الشَّيْطَانُ بِبَعْضِ مَا كَسَبُوا ط
 وَلَقَدْ عَفَا اللَّهُ عَنْهُمْ إِنْ اللَّهُ
 غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿١٥٥﴾ يَتَأَيُّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا
 لَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ كَفَرُوا وَقَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ
 إِذَا ضَرَبُوا فِي الْأَرْضِ أَوْ كَانُوا غُرَى
 لَوْ كَانُوا عِنْدَنَا مَا مَاتُوا وَمَا قُتِلُوا لِيَجْعَلَ
 اللَّهُ ذَلِكَ حَسْرَةً فِي قُلُوبِهِمْ ط وَاللَّهُ يُخَيِّئُ
 وَيُمِيتُ ط وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١٥٦﴾
 وَلَئِنْ قُتِلْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ مُتُّمْ
 لَمَغْفِرَةٌ مِنَ اللَّهِ وَرَحْمَةٌ خَيْرٌ مِمَّا يَجْمَعُونَ ﴿١٥٧﴾
 وَلَئِنْ مِتُّمْ أَوْ قُتِلْتُمْ لَإِلَى اللَّهِ تُحْشَرُونَ ﴿١٥٨﴾

ثُمَّ أَنْزَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ بَعْدِ الْغَمِّ أَمَنَةً
 نِعَاسًا يَغْشَى طَائِفَةً مِنْكُمْ ط وَطَائِفَةٌ
 قَدْ أَهَمَّتْهُمْ أَنْفُسُهُمْ يَظُنُّونَ بِاللَّهِ
 غَيْرَ الْحَقِّ ظَنَّ الْجَاهِلِيَّةِ ط يَقُولُونَ
 هَلْ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ مِنْ شَيْءٍ ط قُلْ إِنْ
 الْأَمْرُ كُلُّهُ لِلَّهِ ط تَخْفُونَ فِي أَنْفُسِهِمْ مَا
 لَا يُبْدُونَ لَكُمْ ط يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا
 مِنْ الْأَمْرِ شَيْءٌ مَا قُتِلْنَا هَاهُنَا ط قُلْ لَوْ
 كُنْتُمْ فِي بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ الَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ
 الْقَتْلُ إِلَى مَضَاجِعِهِمْ ط وَلِيَبْتَلِيَ اللَّهُ مَا
 فِي صُدُورِكُمْ وَلِيُمَحِّصَ مَا فِي قُلُوبِكُمْ ط
 وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١٥٤﴾
 إِنَّ الَّذِينَ تَوَلَّوْا مِنْكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ
 إِنَّمَا أَسْتَرْلَهُمُ الشَّيْطَانُ بِبَعْضِ مَا كَسَبُوا ط
 وَلَقَدْ عَفَا اللَّهُ عَنْهُمْ إِنْ اللَّهُ غَفُورٌ
 حَلِيمٌ ﴿١٥٥﴾ يَتَأَيُّبُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَكُونُوا
 كَالَّذِينَ كَفَرُوا وَقَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ إِذَا
 ضَرَبُوا فِي الْأَرْضِ أَوْ كَانُوا غُرَى لَوْ كَانُوا
 عِنْدَنَا مَا مَاتُوا وَمَا قُتِلُوا لِيَجْعَلَ اللَّهُ
 ذَلِكَ حَسْرَةً فِي قُلُوبِهِمْ ط وَاللَّهُ يُخَيِّئُ
 وَيُمِيتُ ط وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١٥٦﴾
 وَلَئِنْ قُتِلْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ مُتُّمْ
 لَمَغْفِرَةٌ مِنَ اللَّهِ وَرَحْمَةٌ خَيْرٌ مِمَّا يَجْمَعُونَ
 ﴿١٥٧﴾ وَلَئِنْ مِتُّمْ أَوْ قُتِلْتُمْ لَإِلَى اللَّهِ
 تُحْشَرُونَ ﴿١٥٨﴾

154. Kisha baada ya dhiki Alikuteremshieni utulivu - usingizi ambao ulifunika kundi moja kati yenu. Na kundi jengine nafsi zao ziliwashughulisha hata wakamdhania Mwenyezi Mungu dhana isiyokuwa ya haki, dhana ya kijinga. Wakisema: Hivyo tuna lolote sisi katika jambo hili? Sema: Mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Wanaficha katika nafsi zao wasiyokubainishia

Wanasema: Lau ingelikuwa tuna lolote katika jambo hili tusingeliwa hapa. Sema: Hata mngelikuwa majumbani mwenu, basi wangelitoka walioandikiwa kufa, wakenda mahali pao pa kuangukia wafe.(Haya ni hivyo) ili Mwenyezi Mungu Ayajaribu yaliyomo vifuani mwenu, na Asafishe yaliyomo nyoyoni mwenu. Na Mwenyezi Mungu Anayajua yaliyomo vifuani.

155. Hakika wale waliorudi nyuma miongoni mwenu siku yalipopambana majeshi mawili, Shetani ndiye aliyewatelezesha kwa sababu ya baadhi ya makosa waliyoyafanya; na Mwenyezi Mungu Amekwishawasamehe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mpole.

Amani ya Usingizi Ilivyowashukia Waumini Wakati wa Vita na Woga Ulivyowaingia Wanafiki

Allah تعالیٰ Anawakumbusha waja Wake juu ya Neema Zake Alizowateremshia, utulivu na usingizi uliwafudikiza huku wakiwa wamebeba silaha zao na wakihisi dhiki na huzuni. Kwa hali kama hii, usingizi ni rehma na unabeba maana ya utulivu na amani. Kwa mfano, Allah تعالیٰ Amesema katika *Surat Al-Anfal* kuhusu vita vya Badri,

إِذْ يُغَشِّيكُمُ اللَّعَاسُ أَمَّاتًا

“Alipokufunikeni kwa usingizi uwe ni uaminisho kutoka Kwake.” (8:11)

Bukhari alipokea kutoka kwa Anasi رضي الله عنه kutoka kwa Abu Talhah رضي الله عنه alisema, “Nilikuwa miongoni mwa waliofunikwa na usingizi wakati wa vita vya Uhud. Upanga wangu ulidodondoka mara kadha, unaanguka ninauokota, kisha unaanguka tena nami ninauokota tena.”¹ Bukhari aliihusanya Hadithi hii kuhusu masimulizi ya vita bila *isnad*. Na katika kitabu cha Tafsiri pamoja na *isnad*.² At-Tirmidhi, An-Nasai na Al-Hakim walipokea kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa Abu Talhah رضي الله عنه alisema, “Siku ya Uhud nilinyanyua kichwa changu na nikamuona kila mtu ameanguka kichwa kwa kusinzia.” Hii ni kauli ya At-Tirmidhi ambaye aliitaja kuwa “*Hasan*”³

¹ Fat’hul Al-Bari 7:22

² Fat’hul Al-Bari 8:76 Tuhfatul Al-Ahwadhi 8:358

³ Tuhfatul Al-Ahwadh 8:358. Annasai katika Al-Kubra 6:349 na Al-hakim 2:297.

Sahih."¹ An Nasai pia aliipokea Hadithi hii kutoka kwa Anas رضي الله عنه aliyesema kuwa Abu Talha رضي الله عنه alisema, "Nilikuwa miongoni mwa wale waliopatwa na usingizi."²

Kundi la pili lilitajwa katika Ayah ni wanafiki wao hushughulishwa na nafsi zao tu na hiyo ni kutokana na woga walionao na kutopenda haki,

يُظُنُّونَ بِاللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ ظَنَّ الْجَاهِلِيَّةِ

"Wakamdhanja Mwenyezi Mungu dhana isiyokuwa ya haki, dhana ya kijinga." (3:154)

Kwani ni wazandiki na watu wenye mashaka na wasiwasi juu ya Allah تعالى Aliyejuu. Allah تعالى Amesema,

ثُمَّ أَنْزَلَ عَلَيْكُمْ مِنْ بَعْدِ الْغَمِّ أَمْنَةً نُبُوءًا يُغْنِيكُمْ عَنْ طَآئِفَةٍ مِّنْكُمْ

"Kisha baada ya dhiki Alikuteremshieni utulivu - usingizi ambao ulifunika kundi moja kati yenu." (3:154)

Kundi hilo ni lile la watu wenye imani, uhakika, msimamo na kumtegemea (Allah تعالى) ambao wana uhakika wa kupewa ushindi pamoja na Mtume ﷺ na kukidhi malengo yake. Ndio maana Allah تعالى Akasema,

وَطَآئِفَةٌ قَدْ أَهَمَّتْهُمْ أَنفُسُهُمْ

"Na kundi jingine nafsi zao ziliwashughulisha". (3:154)

Wao hawakufunikwa na usingizi kwa sababu ya woga, wahka na hofu waliyokuwa nayo.

يُظُنُّونَ بِاللَّهِ غَيْرَ الْحَقِّ ظَنَّ الْجَاهِلِيَّةِ

"Hata wakamdhanja Mwenyezi Mungu dhana isiyokuwa ya haki dhana ya kijinga." (3:154)

Kama Allah تعالى Alivyosema katika aya nyingine

بَلْ ظَنَّكُمْ أَنْ لَنْ يَنْقَلِبَ الرَّسُولُ وَالْمُؤْمِنُونَ إِلَىٰ أَهْلِيهِمْ أَبَدًا

"Lakini mlidhani kwamba Mtume na Waumini hawatarudi kabisa kwa ahali zao." (48:12)

¹ An-Nasai katika Al-Kubra 6:349.

Kundi hili lilidhani kuwa kushindwa waislamu siku ile ina maana washirikina walifikia malengo yao na kuwa Uislamu na Ummah wake wameangamia. Hii ndiyo hali halisi ya watu wenye wasiwasi na shaka, wanapofikiwa na madhila, wanatawaliwa na fikra mbovu. Kisha Allah تعالی Akawaelezea kuwa,

يَقُولُونَ

“**Wakisema.**” Katika hali hii,

هَلْ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ مِنْ شَيْءٍ

“**Hivyo tuna lolote sisi katika jambo hili?**” Allah تعالی Alisema:

قُلْ إِنَّ الْأَمْرَ كُلَّهُ لِلَّهِ يُخْفُونَ فِي أَنْفُسِهِمْ مَا لَا يُبْدُونَ لَكَ

“**Sema: Mambo yote ni ya Mwenyezi Mungu. Wanaficha katika nafsi zao wasiyokubainishia.**”

Kisha Akafasiri na Kueleza yale waliyokuwa wakiyaficha katika nafsi zao kwa Kauli Yake تعالی,

يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ مَا قُتِلْنَا هَاهُنَا

“**Wanasema: Lau ingelikuwa tuna lolote katika jambo hili tusinge uliwa hapa.**”

Maana yake: Walimficha mazungumzo hayo Mtume ﷺ. Ibn Is'haq رحمه الله تعالی alipokea kutoka kwa Abdullah bin Azi - Zubayr رضي الله عنهما kutoka kwa Az-Zubayr رضي الله عنه alisema, “Nilikuwa pamoja na Mtume ﷺ, wakati hofu ilipozidi na Allah تعالی Akatuletea usingizi (wakati wa vita vya Uhud). Wakati huo, sote (isipokuwa wanafiki) tulikuwa tukitikisa vichwa kwa usingizi. *Wallahi!* Kama nilikuwa ndotoni, nilisikia kauli ya Mua'tib bin Qushayr. Nilimsikia huku nikiwa kama ninaota ndoto akisema, “Tungekuwa na jambo la kufanya na shauri hili, hapana mmoja wetu angeuawa hapa.” Niliyahifadhi kwa moyo maneno haya ambayo Allah تعالی Aliyataja baadaye Alipoteremsha Kauli Yake,

يَقُولُونَ لَوْ كَانَ لَنَا مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ مَا قُتِلْنَا هَاهُنَا

“**Wanasema: Lau ingelikuwa tuna lolote katika jambo hili tusinge uliwa hapa.**”

Hadithi hii imepokewa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی¹. Allah تعالی Amesema,

¹ Ibn Abi Hatim 2:620.

قُلْ لَوْ كُنْتُمْ فِي بُيُوتِكُمْ لَبَرَزَ الَّذِينَ كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقَتْلُ إِلَى مَضَاجِعِهِمْ

“Sema: Hata mngelikuwa majumbani mwenu, basi wangelitoka walioandikiwa kufa, wakenda mahali pao pa kuangukia wafe.”

Maana yake: Hiyo ndio Qadar Aliyoikadiria Allah تعالى na ni Hukumu ya lazima isiyoepukika wala mtu hawezi kuikimbia. Kauli ya Allah تعالى,

وَلِيَبْتَلِيَ اللَّهُ مَا فِي صُدُورِكُمْ وَلِيُمَحَّصَ مَا فِي قُلُوبِكُمْ

“Ili Mwenyezi Mungu Ayajaribu yaliyomo vifuani mwenu, na Asafishe yaliyomo nyoyoni mwenu.”

Ili Awajaribu kwa yale yaliyojiri juu yenu na Aweze kutofautisha kati ya wema na wabaya na Aweke wazi suala la waumini wa kweli na wanafiki kutokana na maneno yao na matendo yao.

وَاللَّهُ عَلِيمٌ بِذَاتِ الصُّدُورِ ﴿١٥٤﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anayajua yaliyomo vifuani”.

Na yaliyofichwa nyoyoni miongoni mwa nia na siri.

Waumini Waliokimbia Vita vya Uhud na Namna walivyosamehewa:

Kisha Allah تعالى Amesema

إِنَّ الَّذِينَ تَوَلَّوْا مِنْكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ إِنَّمَا اسْتَزَلَّهُمُ الشَّيْطَانُ بِبَعْضِ مَا كَسَبُوا

“Hakika wale waliorudi nyuma miongoni mwenu siku yalipopambana majeshi mawili, Shet’ani n diye aliyewatelezesha kwa sababu ya baadhi ya makosa waliyoyafanya;...” (3:155)

Hiyo ni kwa sababu ya makosa yao yaliyopita kama walivyosema baadhi ya Salaf kuwa, “Hakika malipo ya aliyetenda wema ni kulipwa wema na hakika aliyetenda maovu ni kulipwa maovu baada yake.” Kisha Allah تعالى Akasema,

وَلَقَدْ عَفَا اللَّهُ عَنْهُمْ

“Na Mwenyezi Mungu Amekwisha wasamehe.” Maana yake: Kwa kule kukimbia kwao.

إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ حَلِيمٌ ﴿١٥٤﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe, Mpole.”

Anasamehe makosa, Anawahurumia na Anawasamehe viumbe Wake. Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Shaqiq kwamba, “Abdur-Rahmani bin Awf رضي الله عنه alikutana na Al-Walid bin Uqbah رضي الله عنه. Walid رضي الله عنه alimuuliza, “Kwa nini unamsema vibaya ‘Uthman رضي الله عنه, kiongozi wa Waumini?” Abdur-Rahman رضي الله عنه alimjibu, “Muambie sikukimbia siku ya Uhud.” ‘Asim رضي الله عنه alisema: “Sio Uhud tu kadhalika kutega katika vita vya Badri na kuacha kufuata mwenendo wa Khalifa Umar رضي الله عنه.” Amesema: “Hivyo aliondoka na kwenda kumuhabarisha Uthman رضي الله عنه. Akasema, naye akajibu ‘Sikukimbia Vita vya Uhud! Vipi anilaumu kwa kosa ambalo Allah تعالى Ameshalisamehe, pale Aliposema:

إِنَّ الَّذِينَ تَوَلَّوْا مِنْكُمْ يَوْمَ الْتَقَى الْجَمْعَانِ إِنَّمَا اسْتَزَلَّهُمُ الشَّيْطَانُ بِبَعْضِ مَا كَسَبُوا ۗ
وَلَقَدْ عَفَا اللَّهُ عَنْهُمْ ۗ

“Hakika wale waliorudi nyuma miongoni mwenu siku yalipopambana majeshi mawili, Shetani ndiye aliyewatelezesha kwa sababu ya baadhi ya makosa waliyoyafanya; na Mwenyezi Mungu Amekwishawasamehe.”

Ama kuhusu kauli yake, nilibaki nyumbani badala ya kushiriki Badr, nilikuwa nikimuuguza Ruqqayah رضي الله عنها, bintiye Mjumbe wa Allah, mpaka alipofariki dunia. Na Mtume ﷺ alinipa fungu kutokana na ngawira za Badr, na yeyote anayepewa ngawira na Mtume ﷺ nae huwa ameshiriki katika vita. Ama kuhusu kauli yake kuwa nilitelekeza Sunnah ya Umar رضي الله عنه, wala sikuweza kudumisha. Mimi na yeye hatuiwezi. ‘Nenda na muwasilishie majibu haya.’¹

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ كَفَرُوا وَقَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ إِذَا ضَرَبُوا فِي الْأَرْضِ أَوْ
كَانُوا غُزًى لَوْ كَانُوا عِنْدَنَا مَا مَاتُوا وَمَا قُتِلُوا لِيَجْعَلَ اللَّهُ ذَلِكِ حَسْرَةً فِي قُلُوبِهِمْ ۗ وَاللَّهُ
سَخِيءٌ وَيْمِيءٌ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١٥٥﴾ وَلَئِنْ قُتِلْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ مُتُّمْ لَمَغْفِرَةٌ مِّنَ
اللَّهِ وَرَحْمَةٌ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ ﴿١٥٦﴾ وَلَئِنْ مُتُّمْ أَوْ قُتِلْتُمْ لَإِلَى اللَّهِ تَحْشُرُونَ ﴿١٥٧﴾

¹ Ahmad 1:68.

156. Enyi mlioamini! Msiwe kama wale waliokufuru na wakawasema ndugu zao waliposafiri katika nchi au walipo kuwa vitani: Wangelikuwa kwetu wasingelikufa na wasingeliuwawa. Ili Mwenyezi Mungu Afanye hayo kuwa ni majuto katika nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu Huhuisha na Hufisha. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona myatendayo.

157. Na pindi mkiuliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, au mkifa, hakika maghufira na rehema zitokazo kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko yote wanayoyakusanya.

158. Na mkifa au mkiuliwa ni kwa Mwenyezi Mungu ndio mtakusanywa.

Makatazo Juu ya kujifananisha na Makafiri kwa Kuitakidi Mtu kufa bila ya Utashi wa Allah تعالى

Allah تعالى Amewakataza waja wake waumini kufuata amali potofu za makafiri, ambazo zipo katika kauli zao kuhusu waliokufa safarini na vitani kwa kusema: "Kama wasingesafiri, wasingefikwa na maafa."

Allah تعالى Amesema,

يٰۤاَيُّهَا الَّذِيْنَ ءَامَنُوْا لَا تَكُوْنُوْا كَالَّذِيْنَ كَفَرُوْا وَقَالُوْا لِاٰخُوْنٰهُمْ

"Enyi mlioamini! Msiwe kama wale waliokufuru na wakawasema ndugu zao". (3:156)

Kuhusu ndugu zao waliokufa,

اِذَا ضَرَبُوْا فِي الْاَرْضِ

"Waliposafiri katika nchi."

Waliosafiri kwa ajili ya biashara au shughuli nyinginezo.

اَوْ كَانُوْا غُرٰى

"Au walipokuwa vitani." Au kushiriki katika vita.

لَوْ كَانُوْا عِنْدَنَا

"Wangelikuwa kwetu." Katika makazi yetu.

مَا مَاتُوا وَمَا قُتِلُوا

“Wasingelikufa na wasingeliuwawa.”

Wasingeuawa wakiwa safarini au kuuawa vitani. Kauli ya Allah تعالى،

لِيَجْعَلَ اللَّهُ ذَلِكَ حَسْرَةً فِي قُلُوبِهِمْ

“Ili Mwenyezi Mungu Afanye hayo kuwa ni majuto katika nyoyo zao”.

Maana yake: Allah تعالى Amejalia fikra potofu nyoyoni mwao ili huzuni na majonzi ya kufa na kuulizwa kwao yazidi kuwa makubwa, kisha Allah تعالى Aliwakanusha kwa Kusema:

وَاللَّهُ نَحِيءٌ وَيُؤْمِتُ

“Na Mwenyezi Mungu Huhuisha na Hufisha”.

Maana yake: Viumbe wote wapo Mikononi Mwake, na mambo yote hurejeshwa Kwake, hawi hai mtu au kufa isipokuwa ni kwa Utashi Wake na Uweza Wake. Na umri wa mtu yeyote hauongezeki au kupungua ila kwa Hukumu Yake na Uweza Wake.

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١٥٧﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona myatendayo.”

Maana yake: Elimu na Ujuzi Wake unaangazia viumbe Vyake vyote, hakijifichi kitu chochote katika harakati za mambo yao. Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَلَيْنَ قُتِلْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ مُتُّمْ لِمَغْفِرَةٍ مِّنَ اللَّهِ وَرَحْمَةٍ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ ﴿١٥٨﴾

“Na pindi mkiuliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu, au mkifa, hakika maghufira na rehema zitokazo kwa Mwenyezi Mungu ni bora kuliko yote wanayoyakusanya.” (3:157)

Hili linaashiria ya kuwa kufa au kuuliwa kwa ajili ya Dini ya Allah, ni njia ya kupata Rehema za Allah تعالى، Msamaha Wake na Ridhaa Yake. Na hilo ni bora zaidi kuliko kubakia katika dunia na kuburudika na anasa zake zenye kuondoka. Kisha Allah تعالى Akahabarisha ya kuwa kila anayekufa au kuuliwa marejeo yake yatakuwa kwa Allah تعالى. Hivyo, Atamlipa kulingana na amali yake, ikiwa ni kheri atavuna kheri, na kama shari atavuna shari. Allah تعالى Amesema,

وَلَيْنَ مُتُّمٍ أَوْ قَتَلْتُمْ لِأَلَى اللَّهِ تَحْشُرُونَ ﴿١٥٨﴾

“Na mkifa au mkiuliwa ni kwa Mwenyezi Mungu ndio mtakusanywa.” (3:158)

* * *

فِيمَا رَحِمَةٍ مِنَ اللَّهِ لِنْتَ لَهُمْ ۗ وَلَوْ كُنْتَ فَظًا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَأَنْفَضُوا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ ۗ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

إِنْ يَنْصُرْكُمُ اللَّهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمْ ۗ وَإِنْ يَخَذِلْكُمْ فَمَنْ ذَا الَّذِي يَنْصُرْكُمْ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٦٠﴾

وَمَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَنْ يَغُلَّ ۗ وَمَنْ يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ ثُمَّ تُوَفَّى كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦١﴾

أَفَمَنْ أَتَّبَعَ رِضْوَانَ اللَّهِ كَمَنْ بَاءَ بِسَخَطٍ مِنَ اللَّهِ وَمَاؤَلَّهُ جَهَنَّمَ ۗ وَيُفْسِقُ الْفِئْتِمَةَ ۗ هُمْ دَرَجَاتٌ عِنْدَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿١٦٢﴾

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْ أَنْفُسِهِمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿١٦٣﴾

159. Basi ni kwa sababu ya Rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangelikukimbia. Basi wasamehe, na waombe maghufira, na shauriana nao katika mambo. Na ukishakata shauri basi mtegemea Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaomtegemea.

160. Akikunusuruni Mwenyezi Mungu hapana wa kukushindenii, na Akikutupeni ni nani, basi,

فِيمَا رَحِمَةٍ مِنَ اللَّهِ لِنْتَ لَهُمْ ۗ وَلَوْ كُنْتَ فَظًا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَأَنْفَضُوا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ ۗ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

إِنْ يَنْصُرْكُمُ اللَّهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمْ ۗ وَإِنْ يَخَذِلْكُمْ فَمَنْ ذَا الَّذِي يَنْصُرْكُمْ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٦٠﴾

وَمَا كَانَ لِنَبِيٍّ أَنْ يَغُلَّ ۗ وَمَنْ يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ ثُمَّ تُوَفَّى كُلُّ نَفْسٍ مَّا كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦١﴾

أَفَمَنْ أَتَّبَعَ رِضْوَانَ اللَّهِ كَمَنْ بَاءَ بِسَخَطٍ مِنَ اللَّهِ وَمَاؤَلَّهُ جَهَنَّمَ ۗ وَيُفْسِقُ الْفِئْتِمَةَ ۗ هُمْ دَرَجَاتٌ عِنْدَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ ﴿١٦٢﴾

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِنْ أَنْفُسِهِمْ يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ وَيُزَكِّيهِمْ وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ لَفِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿١٦٣﴾

baada yake Yeye atayekunusuruni? Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.

161. Na haiwezekani kwa Nabii yeyote kufanya khiyana. Na atakayefanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyoyafanyia khiyana, kisha kila mtu atalipwa kwa aliyoyachuma, kwa ukamilifu; wala hawatadhulumiwa.

162. Je! Aliyeyafuata ya kumridhisha Mwenyezi Mungu ni kama yule aliyestahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na makazi yake yakawa Jahannamu? Napo ni mahala pabaya pa kurejea.

163. Hao wana vyeo mbali mbali kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyaona yote wayatendayo.

164. Hakika Mwenyezi Mungu Amewafanyia wema mkubwa Waumini vile Alivyowaletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe, Anayewasomea Aya Zake, na Anawatakasa, na Anawafunza Kitabu na hikima, ijapokuwa kabla ya hapo walikuwa katika upotovu ulio wazi.

Miongoni mwa Sifa za Mtume wetu Muhammad ﷺ ni Huruma na Upole

Allah تعالی Anamsemesha Mtume Wake, Akimsifia yeye na waumini, katika kulainisha moyo wake kwa umma wake wenye kufuata amri yake na kuacha makatazo yake na kuyafanya vizuri matamshi yake kwa wao.

فِيمَا رَحْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ لَئِن لَّهُمْ

“Basi ni kwa sababu ya Rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao.” (3:159)

Ni kitu gani kilichokufanya wewe uwe laini kwao, lau kama isingelikuwa Rehema ya Allah تعالی kwako wewe na wao. Hasan Al-Basri رحمه الله تعالی alisema, “kwa hakika hii ndiyo tabia ambayo Allah تعالی Alimtuma nayo Muhammad ﷺ. Na aya inafanana na Kauli ya Allah تعالی,

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ

بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

“Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayokutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma.” (9:128)

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَلَوْ كُنْتَ فَظًا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَأَنَّفَضُوا مِنْ حَوْلِكَ

“Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangelikukimbia.” (3:159)

Ugumu unaokusudiwa hapa ni wa maneno, ndiyo maana baada ya hapo Amesema,

غَلِيظَ الْقَلْبِ

“Mwenye moyo mgumu.” (3:159)

Kama ungekuwa na maneno mabaya na msusuwavu wa moyo juu yao wangelikukimbia na kukuacha. Pamoja na hayo Allah تعالى Aliwakusanya ukawa nao, na Allah تعالى Akakufanya mpole na mwema, ili nyoyo zao zikuzowee.” Kama Abdullah bin Amri alivyosema kuwa alisoma wasifu wa Mtume ﷺ katika vitabu vilivyotangulia, “Sio mkali wala mkatili, hakuwa mpunjufu sokoni, hakuwa analipiza ubaya kwa aliyemfanyia mabaya. Bali husamehe na kuwaachia wenye makosa.”¹

Amri ya kufanya Shura na kufungamana Nayo

Kutokana na anuani hiyo. Allah تعالى Amesema,

فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ

“Basi wasamehe, na waombee maghufira, na shauriana nao katika mambo.” (3:159)

Mtume ﷺ alikuwa akiwataka ushauri Maswahaba zake, kuhusu mambo mbalimbali, ili kuituliza mioyo yao. Kwa sababu hiyo walitekeleza kwa ghera maamuzi yote waliyoyafikia. Kwa mfano, kabla ya vita vya Badr, aliwauliza Masahaba zake juu ya Waislamu kuukata msafara wa biashara ulioongozwa

¹ Fat’hul Al-Bari 8:449.

na Abu Sufyan. Wakamuambia, "Ewe Mjumbe wa Allah! Lau kama unataka kuvuka bahari, tuko tayari kuvuka pamoja nawe, na kama unataka kusonga mbele kuelekea *Barkul - Ghimad* tutakuwa pamoja nawe, na wala hatusemi kama kaumu ya Musa عليه السلام walivyomuambia Musa عليه السلام, 'Nenda wewe na Mola wako ukapigane sisi hapa tumejipumzisha, lakini tunasema 'sisi tupo pamoja nawe mbele yako, kulia na kushotoni kwako, tuko tayari kupigana.'" Mtume ﷺ aliwauliza pia rai ya kuhusu mahali pa kupiga kambi katika Badri. Al-Mundhir bin Amr alishauri wapige kambi jirani na maadui kwani alitaka kufa shahidi.

Ama kuhusu vita vya Uhud, Mtume ﷺ aliwataka shauri Masahaba ima wabaki katika ngome ya mji wa Madinah au watoke kwenda kuwakabili maadui? Wengi wao wakaomba watoke kumkabili adui, naye alifanya hivyo. Pia alichukua ushauri wao siku ya Khandaq juu ya kufanya mkataba wa amani na baadhi ya makabila ya Al-Ahzab kwa malipo ya theluthi moja ya matunda ya Madina. Hata hivyo, Sa'ad bin Ubadah na Sa'd bin Mua'dh رضي الله عنهما walikataa pendekezo hilo na Mtume ﷺ alifuata ushauri wao. Mtume ﷺ aliwashauri wao iwapo wawashambulie washirikina siku ya Hudaybiyya, na Abubakar رضي الله عنه alipinga akisema, "Hatukuja hapa kupigana na yeyote. Bali tumekuja kutekeleza ibada ya "Umrah" Mtume ﷺ alikubali ushauri huo. Kadhalika Mtume ﷺ alitaka ushauri siku ya Ifk (shutuma za uongo dhidi ya mama Aisha رضي الله عنها), Mtume ﷺ aliwaambia, "*Enyi Waislamu! Nipeni ushauri juu ya baadhi ya watu waliomzulia mke wangu (Aishah). Naapa kwa Allah, sijui kama kuna uovu wowote kwa mke wangu, nifahamisheni hao waliomtuhumu mke wangu ni akina nani? Naapa kwa Allah mimi ninachojua kwa mke wangu yeye ni mtu msafi.*"¹

Ali na Usama رضي الله عنهما walimpa ushauri wa kutengana na mama Aisha رضي الله عنها. Mtume ﷺ alikuwa akiwashauri Masahaba wake katika vita na mambo mengine. Ibn Majah amenukuu kutoka kwa Abuu Hurayra رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema;

«الْمُسْتَشَارُ مُؤْتَمَرٌ»

"Mwenye kutakwa ushauri ni mwenye kutumainiwa"²

¹ Al-Bukhari (4757).

² Ibn Maja 2:1233.

Imepokewa na Abu Dawud, At-Tirmidhi, na An - Nasai ameipa daraja la Hasan.¹

Utegemezi kwa Allah تعالی ni Baada ya Ushauri

Kauli ya Allah تعالی,

فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ

“Na ukishakata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu.” (3:159)

Unapowataka wao ushauri, na ukajenga azma, basi mtegemee Allah تعالی katika jambo hilo.

إِنَّ اللَّهَ سَجِبُ الْمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Huwapenda wanaomtegemea.” (3:159)

Na Kauli Yake Allah تعالی,

إِنْ يَنْصُرْكُمُ اللَّهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمْ ۗ وَإِنْ يَخَذِلْكُمْ فَمَنْ ذَا الَّذِي يَنْصُرْكُمْ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَعَلَى

اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٦٠﴾

“Akikunusuruni Mwenyezi Mungu hapana wa kukushindeni, na Akikutupeni ni nani, basi, baada yake Yeye atayekunusuruni? Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.” (3:160)

Kisha Allah تعالی Akawaamuru wao kumtegemea Yeye tu, Akasema

صَبْرًا إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَكِيمِ ﴿١٦١﴾

“Na hakukuwa kunusuriwa isipokuwa kwa Allah. mwenye Nguvu na Mwenye Hikima” (3:126)

Na hili ni kama Kauli Yake Allah تعالی Iliyotangulia,

وَعَلَى اللَّهِ فَلْيَتَوَكَّلِ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١٦٢﴾

“Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu.” (3:160)

¹ Abuu Daudi 5/345 na Tuhfatu Al-Ahwadh 9:109.

Hiana na Hadaa Katika Vita si Katika Sifa za Mtume ﷺ

Allah تعالى Amesema,

وَمَا كَانَ لِنَبِيِّ أَنْ يُغْلَ

“Na haiwezekani kwa Nabii yeyote kufanya khiyana.”

Ibn Abbas, Mujahid, Al-Hasan na wengineo رضي الله عنهم, wamesema: “Hamtakikani kwa Mtume kufanya khiyana.”¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kwamba: Aya hii ilishuka kuhusu nguo nyekundu ya Hariri iliyopotea siku ya vita vya Badri. Baadhi ya watu wakasema: Huenda Mtume ﷺ ameichukua, wakakithirisha kuzungumza hilo, Allah تعالى Akateremsha.

وَمَا كَانَ لِنَبِيِّ أَنْ يُغْلَ وَمَنْ يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Na haiwezekani kwa Nabii yeyote kufanya khiyana. Na atakaye fanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyoyafanyia khiyana.” (3:161)²

Kama hivyo amepokea Abu Daudi na Tirmidhi, na akasema: Hadithi hii ina daraja la *Hassan Gharib*.³ Na huu ni utakaso kwa Mtume kuhusu njia zote za kufanya khiyana. Na anafikisha amana na kugawa Ngawira na nyinginezo. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَمَا كَانَ لِنَبِيِّ أَنْ يُغْلَ وَمَنْ يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ثُمَّ تُوَفَّى كُلُّ نَفْسٍ مَّا

كَسَبَتْ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦١﴾

“Haiwezekani kwa Nabii yeyote kufanya khiyana. Na atakayefanya khiyana, atayaleta Siku ya Kiyama aliyoyafanyia khiyana, kisha kila mtu atalipwa kwa aliyoyachuma, kwa ukamilifu; wala hawatadhulumiwa.” (3:161)

Aya hii ina makaripio makali na vitisho dhidi ya *Ghulul* (kuiba ngawira), pia kuna Hadithi zinazokataza mwenendo huu. Imam Ahmad alipokea kuwa Abu Malik A-Ashjai رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Ibn Abi Hatim 2:37.

² At - Tabari 7:348.

³ Abu Dawud 4:280, Tuhfat Al-Ahwadhi 8:359.

«أَعْظَمُ الْغُلُولِ عِنْدَ اللَّهِ ذِرَاعٌ مِنَ الْأَرْضِ، تَجِدُونَ الرَّجُلَيْنِ جَارَيْنِ فِي الْأَرْضِ -
 أو فِي الدَّارِ - فَيَقْطَعُ أَحَدُهُمَا مِنْ حَظِّ صَاحِبِهِ ذِرَاعًا، فَإِذَا افْتَطَعَهُ، طَرَفَهُ مِنْ سَبْعِ
 أَرْضِينَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

*"Khiyana (Ghulul) iliyo mbaya (kuiba) mbele ya Allah, ni dhiraa ya ardhi, yaani utapowakuta majirani wawili katika ardhi au nyumba na mmoja wao anampokonya mwenzake dhiraa moja ya Ardhi. Atakapoichukua atafungwa nacho katika ardhi saba mpaka siku ya Kiyama."*¹

Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Abu Humayd As-Said kuwa amesema Mtume ﷺ alimteua mtu kutoka kabila la Al-Azd anayeitwa Ibn Lutbiyyah kukusanya Zakah. Aliporejea alisema, "Hiki kipande ni chako na hiki nimepewa zawadi." Mtume ﷺ alisimama juu ya Mimbari na kusema,

«مَا بَالُ الْعَامِلِ نَبَعْتُهُ فَيَجِيءُ فَيَقُولُ: هَذَا لَكُمْ، وَهَذَا أَهْدِي لِي، أَفَلَا جَلَسَ فِي
 بَيْتِ أَبِيهِ وَأُمِّهِ فَيَنْظُرُ أَيُّهُدَىٰ إِلَيْهِ أَمْ لَا؟ وَالَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ، لَا يَأْتِي أَحَدٌ مِنْكُمْ
 مِنْهَا بِشَيْءٍ إِلَّا جَاءَ بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ رَقَبَتِهِ، إِنْ كَانَ بَعِيرًا لَهُ رُغَاءٌ، أَوْ بَقْرَةً لَهَا
 خُوَارٌ، أَوْ شَاةً تَبْعُرُ، ثُمَّ رَفَعَ يَدَيْهِ حَتَّىٰ رَأَيْنَا عَفْرَةَ يُبْطِئُ، ثُمَّ قَالَ: «اللَّهُمَّ هَلْ
 بَلَغَتْ» ثَلَاثًا.

"Ana nini mtumishi tumemtuma kukusanya (Zaka) aliporejea alisema, "Hili ni fungu lenu na hili nimepewa zawadi. Kwa nini hakubaki kwa baba yake au mama yake aone kama angepewa zawadi au la? Kwa Yule Ambaye nafsi yangu imo Mkononi Mwake, yeyote anayechukua chochote kwa batili katika Zaka, atakibeba katika shingo yake siku ya Kiyama; kama ikiwa ni ngamia atakoroma, iwapo ni ng'ombe atalia, na iwapo ni Kondoo atalia kikondoo. Kisha Mtume ﷺ alinyanyua mikono yake mpaka tukaona weupe wa makwapa yake na akasema mara tatu, "Ewe Allah! Nimefikisha" Hilo alisema Mtume ﷺ mara tatu.

¹ Ahmad 4:140 Isnadi yake ina dosari.

Hisham bin Urwah رضى الله عنه aliongeza kuwa Abu Humayd baada ya kusikia maneno hayo ya Mtume ﷺ alisema, 'Jicho langu limeona na sikio langu limesikia, na muulizeni Zayd bin Thabit.'" "Imeandikwa katika Sahihi Mbili"¹

Abuu Isa At-Tirmidhi amesimulia katika mlango wa hukumu na sharia, kutoka kwa Muadhi bin Jabal رضى الله عنه kuwa amesema: Mtume ﷺ alinituma kwenda Yemen, nilipoanza kuondoka nyuma yangu alinitumia ujumbe nikarudishwa, akasema:

«لِهَذَا دَعَوْتُكَ فَاْمُضِ لِعَمَلِكَ»

"Kwa ajili hii nimekuacha, basi endelea na kazi yako?"

وَمَنْ يَغْلُلْ يَأْتِ بِمَا غَلَّ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

"Na atakayefanya Khiyana atayaleta Siku ya Kiyama aliyofanyia khiyana."

«أَتَذَرِي لِمَ بَعَثْتُ إِلَيْكَ؟ لَا نُصِيبَنَّ شَيْئًا بِغَيْرِ إِذْنِي، فَإِنَّهُ غُلُولٌ»

"Unajua kwanini nimekuita? usichukue chochote bila idhini yangu, kwani itakuwa khiyana."² At-Tirmidhi alisema, "Hadithi hii ni Hasan Gharib."

Zaidi ya hayo, Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه akisema, Mtume ﷺ alisimama miongoni mwetu na akataja jambo la kufanya Ghulul akaeleza ukubwa wake. Kisha akasema,

«لَا أَلْفَيْنَ أَحَدَكُمْ يَجِيءُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَى رَقَبَتِهِ بَعِيرٌ لَهُ رُغَاءٌ، فَيَقُولُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ اغْنِنِي، فَأَقُولُ: لَا أَمْلِكُ لَكَ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا، قَدْ أْبْلَغْتُكَ، لَا أَلْفَيْنَ أَحَدَكُمْ يَجِيءُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَى رَقَبَتِهِ فَرَسٌ لَهَا حَمْحَمَةٌ، فَيَقُولُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ اغْنِنِي، فَأَقُولُ: لَا أَمْلِكُ لَكَ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا، قَدْ أْبْلَغْتُكَ، لَا أَلْفَيْنَ أَحَدَكُمْ يَجِيءُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَى رَقَبَتِهِ صَامِتٌ، فَيَقُولُ: يَا رَسُولَ اللَّهِ اغْنِنِي، فَأَقُولُ: لَا أَمْلِكُ لَكَ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا، قَدْ أْبْلَغْتُكَ»

¹ Ahmad 5:423, Bukhari Na. 2597, 7174; Muslim Na.1832.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 4:564.

“Sitapenda kuona yoyote anakuja siku ya kiama na shingoni mwake kuna ngamia mwenye kutoa sauti, huku anasema, ‘Ewe Mtume wa Allah niokoe.’ Nitasema, ‘Sikumilikii chochote kwa Allah تعالیٰ, hakika nimekufikishia.’ Sitapenda kuona yoyote anakuja siku ya kiama na shingoni mwake kuna farasi anayeunguruma, huku anasema, ‘Ewe Mtume wa Allah niokoe.’ Nitasema: ‘Sikumilikii chochote kwa Allah تعالیٰ, hakika nimekufikishia.” Sitapenda kuona yoyote anakuja siku ya kiama shingoni mwake ana kipande cha ardhi kinatetemeka, huku anasema, ‘Ewe Mtume wa Allah niokoe.’ Nitasema, ‘Sikumilikii chochote kwa Allah تعالیٰ. Hakika nimekufikishia, sitapenda kuona yoyote anakuja siku ya kiama na huku shingoni mwake anakoroma, anasema, ‘Ewe Mtume wa Allah niokoe.’ Nitasema, ‘Similiki chochote kwa Allah تعالیٰ, hakika nimekufikishia”.¹ Hadithi hii imepokewa katika sahihi.²

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه kuwa amesema, siku ya vita vya Khaibar kundi moja la Masahaba wa Mtume ﷺ lilikuja kwake na kusema: ‘Fulani amekufa shahidi na Fulani amekufa shahidi.’ hadi walipokuwa wakimtaja mtu mmoja, wakasema naye amekufa shahidi. Mtume ﷺ akasema:

«كَلَّا إِنِّي رَأَيْتُهُ فِي النَّارِ فِي بُرْدَةٍ عَلَّهَا - أَوْ عَبَاءَةٍ -»

“Hasha, Hakika mimi nimemuona motoni kwa ajili ya kikoi, alichoghushi, au kijibao.”

Kisha Mtume ﷺ akasema,

«يَا ابْنَ الْخَطَّابِ، اذْهَبْ فَتَادِ فِي النَّاسِ: إِنَّهُ لَا يَدْخُلُ الْجَنَّةَ إِلَّا الْمُؤْمِنُونَ»

“Ewe Ibn Al-Khattab nenda ukawatangazie watu, ya kuwa hawatoingia peponi isipokuwa waumini.”

Akasema Umar رضي الله عنه: ‘Nikatoka kuwaendea watu na kuwatangazia ya kuwa hatoingia peponi yeyote isipokuwa muumini.’ Hivyo ndivyo alivyoinukuu Muslim

¹ Ahmad 2:426.

² Fat’hul Al-Bari 6:214, Muslim 3:1416.

na Tirmidh. Kisha akasema: Hadithi hii ina daraja la Hasan sahihi. Allah تعالى Amesema,

أَفَمَنْ اتَّبَعَ رِضْوَانَ اللَّهِ كَمَنْ بَاءَ بِسَخَطٍ مِّنَ اللَّهِ وَمَأْوَهُ جَهَنَّمَ ۚ وَيَسَّ الْأَبْصَارُ

“Je! Aliyeyafuata ya kumridhisha Mwenyezi Mungu ni kama yule aliyestahiki Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na makazi yake yakawa Jahannamu? Napo ni mahala pabaya pa kurejea.” (3:162)

Maana yake: Hawi sawa yule anayetaka Radhi za Allah تعالى, kwa kufuata Sharia Yake, hivyo akastahiki Ridhaa ya Allah تعالى na Thawabu Zake nyingi, na akaepushwa na balaa la Adhabu Yake. Na mtu ambaye anastahiki Ghadhabu za Allah تعالى na ikawa hana njia ya kujiepusha nazo, na makazi yake siku ya kiyama ni Jahanamu, nayo ni makazi maovu. Na aya kama hizi zipo nyingi sana ndani ya Qur'an kama Kauli Yake Allah تعالى:

۞ أَفَمَنْ يَعْلَمُ أَنَّمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِن رَّبِّكَ الْحَقُّ كَمَنْ هُوَ أَعْمَى

“Je! Anayejua ya kwamba yaliyoteremshwa kwako kutoka kwa Mola Wako Mlezi ni Haki ni sawa na aliye kipofu?...” (13:19)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

أَفَمَنْ وَعَدَّنَهُ وَعَدًّا حَسَنًا فَهُوَ لَنَقِيهِ كَمَنْ مَّتَعْنَهُ مَتَاعَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

“Je! Yule Tuliye muahidi ahadi nzuri, tena naye akayapata, ni kama Tuliye mstarehesha kwa starehe za maisha ya duniani,...” (28:61)

Kisha Allah تعالى Amesema,

هُمُ دَرَجَاتٌ عِنْدَ اللَّهِ

“Hao wana vyoe mbali mbali kwa Mwenyezi Mungu.” (3:163)

Maana yake ni kwamba: Watu wema na waovu, wapo katika daraja tofauti, kama Hasani Al-Basri رحمه الله تعالى na Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى walivyosema.¹ Abu Ubaydah na Al-Kisai walisema kuwa Aya hii inaelezea

¹ Ibn Abuu Hatim 2:646 na At-Tabari 7/367.

madaraja, yaani kuna madaraja mbalimbali ya makazi ya Peponi. Hali kadhalika kuna madaraja mbalimbali ya makazi ya Motoni. Katika Aya nyingine Allah تعالی Anasema,

وَلِكُلِّ دَرَجَاتٍ مِّمَّا عَمِلُوا

“Na wote wana daraja mbali mbali kutokana na yale waliyo yatenda.” (6:132)

Baadaye Allah تعالی Anasema,

وَاللَّهُ بَصِيرٌ بِمَا يَعْمَلُونَ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuyaona yote wayatendayo.” (3:163)

Na Atawalipa au Kuwaadhibu, na Hatowapunguzia amali zao njema, wala Kuongeza amali mbovu. Bali kila mmoja atahukumiwa kwa mujibu wa amali zake.

Kutumwa kwa Nabii Wetu Muhammad ﷺ ni Neema Kubwa

Allah تعالی Amesema,

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ

“Hakika Mwenyezi Mungu Amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyowaletea Mtume aliye miongoni mwao wenyewe.” (3:164)

Maana yake: Kutokana nao, ili iwe sahala kwao kuzungumza nao, kumuuliza maswali, kuamiliana naye na kunufaika naye. Kama Allah تعالی Alivyosema;

وَمِنْ آيَاتِهِمْ أَنِ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنفُسِكُمْ أَزْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا

“Na katika ishara Zake ni kuwa Amekuumbieni wake kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao.” (30:21)

Maana yake: Kutokana na jinsi yenu. Na Allah تعالی Amesema,

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ إِلَهُ وَاحِدٌ

“Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja.” (18:110)

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لِيَأْكُلُوا الطَّعَامَ وَيَشْرَبُونَ فِي الْأَسْوَاقِ[۝]

“Na hatukuwatuma kabla yako Mitume wowote ila kwa hakika na yakini walikuwa wakila chakula, na wakenda masokoni.”
(25:20)

Na Allah تعالی Amesema,

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رَجُلًا نُوحِيَ إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَى[۝]

“Na hatukuwatuma Mitume kabla yako isipo kuwa wanaume tulio wafunulia wahyi miongoni mwa watu wa mijini.” (12:109)

Rehema za Allah تعالی zimekuwa timilifu kwa kule kumtuma kwake Mjumbe wake ﷺ toka miongoni mwao, ili wawasiliane naye na kumuuliza maana ya Maneno ya Allah تعالی. Ndio Allah تعالی Akateremsha aya ifuatayo:

وَيُزَكِّيهِمْ

“Anayewasomea Aya zake.” (3:164)

Maana yake: Qur'an.

يَتْلُوا عَلَيْهِمْ آيَاتِهِ

“Na anawatakasa.” (3:164)

Maana yake: Anawaamuru wao kutenda mema, na anawakataza na machafu, ili nafsi zipate kutakasika, na zitwahirike na uchafu na madhambi ambayo walikuwa wakiyafanya kipindi cha ushirikina na ujahili wao.

وَيُعَلِّمُهُمُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ

“Na anawafunza Kitabu na hekima.” (3:164)

Maana yake: Qur'an na Sunna.

وَإِنْ كَانُوا مِنْ قَبْلُ

“Ijapokuwa kabla ya hapo.” (3:164)

Maana yake: kabla ya Mtume huyu.

لَيْفَى ضَلَّالِ مُبِينٍ ﴿١٦٤﴾

“Walikuwa katika upotovu ulio wazi” (3:164)

Maana yake: Walikuwa katika upotovu na ujinga wa wazi kwa kila mtu.

* * *

أَوْلَمَّا أَصَبْتُمْ مُمْسِيَةً قَدْ أَصَبْتُمْ مَثَلِيهَا قُلْتُمْ أَنَّى هَذَا قُلْ
 هُوَ مِنْ عِنْدِ أَنْفُسِكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٦٥﴾
 وَمَا أَصَبْتُمْ يَوْمَ الْأَتْقَى الَّذِي تَجْمَعَانِ فَيُؤْذِنُ اللَّهُ وَلِيَعْلَمَ
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٦٦﴾ وَلِيَعْلَمَ الَّذِينَ نَافَقُوا وَقِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا
 فَيَقُولُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ ادْفَعُوا قَالُوا لَوْ نَعْلَمُ قِتَالًا
 لَأَتَّبَعْنَكُمْ هُمْ لِلْكَافِرِ يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلْإِيمَانِ
 يَقُولُونَ بِأَفْوَاهِهِمْ مَا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا
 يَكْتُمُونَ ﴿١٦٧﴾ الَّذِينَ قَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أِطَاعُونَا
 مَا قُتِلُوا قُلْ فَادْرَأُوا عَنْ أَنْفُسِكُمُ الْمَوْتَ إِنْ كُنْتُمْ
 صَادِقِينَ ﴿١٦٨﴾ وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا
 بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٩﴾ فَرِحِينَ بِمَا آتَاهُمُ
 اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَاسْتَنْبِشُوا بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُوا بِهِمْ مِنْ
 خَلْفِهِمْ أَلَّا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٧٠﴾ *
 يَسْتَنْبِشُونَ بِنِعْمَةِ مِنَ اللَّهِ وَفَضْلِهِ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ
 الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٧١﴾ الَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِلَّهِ وَالرَّسُولِ مِنْ بَعْدِ
 مَا أَصَابَهُمُ الْقَرْحُ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا مِنْهُمْ وَاتَّقُوا أَجْرٌ عَظِيمٌ
 ﴿١٧٢﴾ الَّذِينَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ إِنَّ النَّاسَ قَدْ جَمَعُوا لَكُمْ
 فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَانًا وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ
 الْوَكِيلُ ﴿١٧٣﴾ فَأَنْقَلَبُوا بِنِعْمَةِ مِنَ اللَّهِ وَفَضْلِهِ لَمْ
 يَمَسْسْهُمْ سُوءٌ وَاتَّبَعُوا رِضْوَانَ اللَّهِ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَظِيمٍ
 ﴿١٧٤﴾ إِنَّمَا ذَلِكُمُ الشَّيْطَانُ يُخَوِّفُ أَوْلِيَاءَهُ فَلَا تَخَافُوهُمْ
 وَخَافُوا إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٧٥﴾

أَوْلَمَّا أَصَبْتُمْ مُمْسِيَةً قَدْ أَصَبْتُمْ
 مَثَلِيهَا قُلْتُمْ أَنَّى هَذَا قُلْ هُوَ مِنْ
 عِنْدِ أَنْفُسِكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ
 قَدِيرٌ ﴿١٦٥﴾ وَمَا أَصَبْتُمْ يَوْمَ
 الْأَتْقَى الَّذِي تَجْمَعَانِ فَيُؤْذِنُ
 اللَّهُ وَلِيَعْلَمَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٦٦﴾
 وَلِيَعْلَمَ الَّذِينَ نَافَقُوا وَقِيلَ
 لَهُمْ تَعَالَوْا فَيَقُولُوا فِي سَبِيلِ
 اللَّهِ أَوْ ادْفَعُوا قَالُوا لَوْ نَعْلَمُ
 قِتَالًا لَأَتَّبَعْنَكُمْ هُمْ لِلْكَافِرِ
 يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلْإِيمَانِ
 يَقُولُونَ بِأَفْوَاهِهِمْ مَا لَيْسَ فِي
 قُلُوبِهِمْ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا
 يَكْتُمُونَ ﴿١٦٧﴾ الَّذِينَ قَالُوا
 لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أِطَاعُونَا
 مَا قُتِلُوا قُلْ فَادْرَأُوا عَنْ أَنْفُسِكُمْ
 الْمَوْتَ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٦٨﴾

165. Nyinyi - ulipokusibuni
 msiba ambao nyinyi
 mmekwishawatia mara
 mbili mfano wa huo -
 mnasema: Umetoka wapi
 huu? Sema: Huo umetoka
 kwenu wenyewe. Hakika

Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.

166. Na yaliyokusibuni siku yalipopambana majeshi mawili yalikuwa kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu, na ili Awajue Waumini.

167. Na ili Awapambanue waliokuwa wanafiki, wakaambiwa: Njooi mpigane katika njia ya Mwenyezi Mungu au linden. Wakasema: Tungejua kuna kupigana bila shaka tungekufuateni. Wao siku ile walikuwa karibu na ukafiri kuliko Imani. Wanasema kwa midomo yao yasiyokuwamo nyoyoni mwao. Na Mwenyezi Mungu Anajua kabisa wanayoyaficha.

168. Hao ndio waliowaambia ndugu zao na wao wenyewe wakakaa kitako: Lau wengeli tutii wasingeliuliwa. Sema: Ziondoleeni nafsi zenu mauti kama mnasema kweli.

Sababu ya Yaliyowasibu Siku ya Uhud na Hekima Yake

Allah تعالى Anasema,

أَوْلَمَّا أَصَبْتَكُمْ مُصِيبَةً

“Nyinyi - ulipokusibuni msiba.”

Nao ni ule ambao uliwakuta waislamu siku ya vita vya Uhudi kwa kuuliwa miongoni mwao watu sabiini.

قَدْ أَصَبْتُمْ مِثْلَهَا

“Ambao nyinyi mme kwisha watia mara mbili mfano wa huo.” (3:165)

Maana yake: Wakati wa vita vya Badri, kwani waliwaua maadui zao sabiini na kuwafanya mateka sabiini.

قُلْتُمْ أَنِي هَذَا

“Mnasema : Umetoka wapi huu?”

Kwa maana, kushindwa kumepatikana vipi?

قُلْ هُوَ مِنْ عِنْدِ أَنْفُسِكُمْ

“Sema: Huo umetoka kwenu wenyewe.”

Ibn Abuu Hatim amenukuu kutoka kwa Umar bin Al-Khattab رضى الله عنه kuwa amesema, ilipokuwa siku ya Uhud, mwaka uliofuata baada ya vita vya Badri, waliadhibiwa Waislamu kwa makosa waliyoyafanya ya kuchukua fidia kutoka kwa makafiri siku ya Badri. Hivyo basi, Waislamu sabiini waliuliwa na baadhi ya Masahaba wa Mtume ﷺ walikimbia katika safu ya mapambano, Mtume ﷺ meno yake ya mbele yalivunjwa, na kichwa chake kilipasuliwa na damu ikaanza kuchuruzika usoni mwake. Allah تعالى Akateremsha;

أَوْلَمَّا أَصَبْتُمْ مِصْبَةَ قَدْ أَصَبْتُمْ مِثْلَهَا فَلَمْ أُنِي هَذَا قُلْ هُوَ مِنْ عِنْدِ أَنْفُسِكُمْ

“Nyinyi - ulipokusibuni msiba ambao nyinyi mmekwisha watia mara mbili mfano wa huo - mnasema: Umetoka wapi huu? Sema: Huo umetoka kwenu wenyewe” (3:165)

Kwa sababu mlichukua fidia. Zaidi ya hayo, Muhammad bin Ishaq, Ibn Jurayj, Ar-Rabi bin Anas na As-Suddi walisema kuwa Aya hii,

هُوَ مِنْ عِنْدِ أَنْفُسِكُمْ

“Huo umetoka kwenu wenyewe...”

Maana yake: Nyie wapiga mishale mliasi amri ya Mtume ﷺ ya kuacha nafasi zenu baada ya kuamriwa na Mtume ﷺ kuwa msishuke kutoka kwenye nafasi yenu.

إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٦٥﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.”

Yeye Allah تعالى Hufanya Atakalo na Huamua Atakalo, na hapana wa kuzuia Uamuzi Wake. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَمَا أَصَابَكُمْ يَوْمَ التَّغْيِ الْجَمْعَانِ فَبِإِذْنِ اللَّهِ

“Na yaliyokusibuni siku yalipopambana majeshi mawili yalikuwa kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu.” (3:166)

Miongoni mwa hayo ni: Kumkimbia adui, kufanikiwa na adui kuua baadhi yenu na kuwajeruhi wengi, haya yote yalijiri kwa Utashi wa Allah تعالى na Amri Zake zenye Hikima timilifu.

Allah تعالی Akasema:

وَلْيَعْلَمَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٦٦﴾

“Na ili awajue Waumini.” (3:166)

Maana yake: Wale ambao walisubiri, kuthibiti na wala hawakutetereka.

وَلْيَعْلَمَ الَّذِينَ نَافَقُوا وَقِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا قَاتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ ادْفَعُوا قَالُوا لَوْ نَعْلَمُ

فِتْنَالَا لَاتَّبَعَنَّكُمْ

“Na ili Awapambanue walio kuwa wanafiki, wakaambiwa: Njooi mpigane katika njia ya Mwenyezi Mungu au lindeni. Wakasema: Tungelijua kuna kupigana bila ya shaka tungelikufuateni.” (3:167)

Maana yake: Wafuasi wa Abdallah bin Ubay bin Salul waliorejea naye Madinah kabla ya vita. Baadhi ya waumini waliwafuata na wakawashajiisha kurejea kwenye uwanja wa vita. Na kwa ajili hiyo Allah تعالی Amesema,

أَوْ ادْفَعُوا

“Au lindeni”, ili idadi ya Waislamu iongezeke, kama Ibn Abbas, Ikrimah, Said bin Jubayr, Ad-Dhahhak, Abu Salih, Al-Hasan na As-Suddi رضي الله عنهم walivyoeleza. Al-Hasan bin Salih alisema, sehemu hii ya Ayah ina maana tusaidiane kwa dua, ambapo wengine wanasema ina maana lindeni vituo vyenu. Hata hivyo walisema:

لَوْ نَعْلَمُ فِتْنَالَا لَاتَّبَعَنَّكُمْ

“Tungelijua kuna kupigana bila ya shaka tungelikufuateni.”

Mujahid amesema hapa wanachokusudia: Kama tungejua kutatokea vita tungewafuata, lakini tunaamini hakutakuwa na mapigano. Allah تعالی Amesema,

هُمْ لِلْكَفْرِ يَوْمَئِذٍ أَقْرَبُ مِنْهُمْ لِلْإِيمَانِ

“Wao siku ile walikuwa karibu na ukafiri kuliko Imani.”

Wametoa hoja kuhusu Aya hii, kuwa mazingira mara nyingi ndio yanayombadilisha mtu, hivyo anakuwa wakati mwengine yupo karibu zaidi na ukafiri na wakati mwengine anakuwa karibu zaidi na Imani. Hiyo ni kutokana na Kauli Yake,

يَقُولُونَ بِأَفْوَاهِهِمْ مَا لَيْسَ فِي قُلُوبِهِمْ

“Wanasema kwa midomo yao yasiyo kuwamo nyoyoni mwao.”

Kwani wanatamka kauli wasizoamini ukweli wake kama vile walivyosema,

لَوْ نَعْلَمُ قِتَالًا لَا تَبَعَنَّكُمْ

“Tungelijua kuna kupigana bila ya shaka tungelikufuateni.”

Walijua kwa yakini kuwa jeshi la makafiri limepokuja kutoka mji wa mbali wakiwaghadhibikia Waislamu, kulipiza kisasi cha watu wao waliouwa na Waislamu katika Badr. Makafiri hawa walikuja kwa wingi kuliko Waislamu, hivyo ni dhahiri kuwa bila shaka vita vitatokea.

Kwa ajili hiyo Allah تعالی Amesema,

وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا يَكْتُمُونَ ﴿١٦٧﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anajua kabisa wanayoyaficha.”

Kauli ya Allah تعالی,

الَّذِينَ قَالُوا لِإِخْوَانِهِمْ وَقَعَدُوا لَوْ أَطَاعُونَا مَا قُتِلُوا

“Hao ndio waliowaambia ndugu zao na wao wenyewe wakakaa kitako: Lau wengelitutii wasingeliuliwa.”

Kama wangesikiliza ushauri wetu wa kubakia humu mjini bila ya kutoka wasingekuwa miongoni mwa waliouawa. Allah تعالی Amesema,

قُلْ فَادْرَأُوا عَنْ أَنْفُسِكُمُ الْمَوْتَ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٦٨﴾

“Sema, Ziondoleeni nafsi zenu mauti kama mnasema kweli.”

Maana yake: Ikiwa kubaki nyumbani kunaokoa kuuawa au kufa, basi hamtokufa. Bali kifo kitawajia hata mkijificha katika ngome imara, basi ziondoleeni nafsi zenu mauti kama mnasema kweli. Mujahid alipokea kutoka kwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه akisema, “Aya hii (3:168) iliteremshwa kwa Abdullah bin Ubayy bin Salul, (Mkuu wa Wanafiki).”¹

¹ At-Tabari 7:383 Isnadi yake ina dosari. Taz. Taqribu At-Tahdhib (2925).

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٠﴾ فَرِحِينَ
 بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ وَدَسْتَبْشِرُونَ بِالَّذِينَ لَمْ يَلْحَقُوا بِهِمْ مِنْ خَلْفِهِمْ أَلَّا خَوْفٌ
 عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿١٦١﴾ * يَسْتَبْشِرُونَ بِنِعْمَةِ مِنَ اللَّهِ وَفَضْلِهِ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ
 أَجْرَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٦٢﴾ الَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِلَّهِ وَالرَّسُولِ مِنْ بَعْدِ مَا أَصَابَهُمُ الْقَرْحُ لِلَّذِينَ
 أَحْسَنُوا مِنْهُمْ وَاتَّقُوا أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿١٦٣﴾ الَّذِينَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ إِنَّ النَّاسَ قَدْ جَمَعُوا لَكُمْ
 فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَانًا وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ ﴿١٦٤﴾ فَانْقَلَبُوا بِنِعْمَةِ مِنَ
 اللَّهِ وَفَضْلِهِ لَمْ يَمَسْسِهِمْ سُوءٌ وَاتَّبَعُوا رِضْوَانَ اللَّهِ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَظِيمٍ ﴿١٦٥﴾ إِنَّمَا
 ذَلِكُمْ الشَّيْطَانُ يُخَوِّفُ أَوْلِيَاءَهُ فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُوا مِنِّي إِنْ كُنْتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٦٦﴾

169. Wala kabisa usiwadhania waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi.

170. Wanafurahia Aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa Fadhila Yake, na wanawashangilia wale ambao bado hawajajiunga nao, walio nyuma yao, ya kwamba haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.

171. Wanashangilia Neema na Fadhila za Mwenyezi Mungu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu Hapotezi ujira wa Waumini,

172. Waliomuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya kwisha patwa na majeraha - kwa waliofanya wema miongoni mwao na wakamchamungu utakuwa ujira mkubwa -

173. Walioambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Mwenyezi Mungu Anatutosha, Naye ni Mbora wa kutegemewa.

174. Basi wakarudi na Neema na Fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya liliowagusa, na wakafuata yanayomridhisha Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kuu.

175. Hakika huyo ni Shetani anawatia khofu marafiki zake, basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini.

Fadhila za Mashahidi

Allah تعالی Anaeleza kuwa japokuwa Mashahidi wameuawa hapa duniani, lakini roho zao ni hai na zinapata riziki katika makazi ya milele.

Katika sahihi yake, Muslim alipokea kutoka kwa Masruq ambaye alisema "Tulimuuliza Abdullah juu ya Aya hii,

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٠﴾

"Wala kabisa usiwadhania waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi."

Alisema, Tulisema tulimuuliza Mtume ﷺ swali hilo hilo, akasema:

«أَرَوَّاحُهُمْ فِي جَوْفِ طَيْرٍ خُضِرٍ، لَهَا فَنَادِبِلٌ مُعَلَّقَةٌ بِالْعَرْشِ، نَسْرُحٌ مِنَ الْجَنَّةِ حَيْثُ شَاءَتْ، ثُمَّ تَأْرِي إِلَيَّ تِلْكَ الْقَنَادِبِلِ، فَاطَّلَعَ إِلَيْهِمْ رَبُّهُمْ اِطْلَاعَةً فَقَالَ: هَلْ تَسْتَهْوُونَ شَيْئًا؟ فَقَالُوا: أَيُّ شَيْءٍ نَسْتَهْوِي وَنَحْنُ نَسْرُحُ مِنَ الْجَنَّةِ حَيْثُ شِئْنَا؟ فَفَعَلَ ذَلِكَ بِهِمْ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ، فَلَمَّا رَأَوْا أَنَّهُمْ لَنْ يَتْرُكُوا مِنْ أَنْ يُسْأَلُوا، قَالُوا: يَا رَبِّ نُرِيدُ أَنْ تَرُدَّ أَرْوَاحَنَا فِي أَجْسَادِنَا حَتَّى نَقْتَلَ فِي سَبِيلِكَ مَرَّةً أُخْرَى، فَلَمَّا رَأَى أَنْ لَيْسَ لَهُمْ حَاجَةٌ، تَرَكُوا»

"Roho zao zimo ndani ya Tumbo la ndege wa kijani mwenye taa, zinazoning'inia kwenye Arshi (ya Allah تعالی) na wanarandaranda ndani ya Pepo kama wapendavyo. Kisha hurejea kwenye hizo taa. Allah تعالی Huwaangalia na Kuwauliza, 'Je mnahitaji kitu?' Wanajibu, "Tutake nini zaidi, ambapo tunatembea ndani ya Pepo kama tutakavyo?". Allah تعالی Aliwauliza swali hilo mara tatu, na walipotanabahi kuwa Ataendelea Kuwauliza mpaka wampe jibu, wakamuambia, 'Ewe Mola Mlezi, Tunatarajia roho zetu zirejeshwe kwenye miili yetu ili tuuawe tena katika njia Yako. Allah تعالی Alijua kuwa hawakuwa na ombi jingine, hivyo Aliwaacha."¹

¹ Muslim 3:1502.

Kuna masimulizi sawa na haya kutoka kwa Anas na Abu Said رضي الله عنهما. Imam Ahmad alimnukuu Anas رضي الله عنه akisema kuwa Mtume ﷺ alisema:

«مَا مِنْ نَفْسٍ تَمُوتُ، نَهَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ، بِسُرِّهَا أَنْ تَرْجِعَ إِلَى الدُّنْيَا، إِلَّا الشَّهِيدُ، فَإِنَّهُ بِسُرِّهِ أَنْ يَرْجِعَ إِلَى الدُّنْيَا يُقْتَلُ مَرَّةً أُخْرَى، لِمَا يَرَى مِنْ فَضْلِ الشَّهَادَةِ»

"Hapana nafsi iliyokufa na yenye kheri mbele ya Allah تعالى، ingependelea kurejea kwenye maisha ya duniani ila shahidi، angenda kurejea duniani ili afe shahidi tena، kwa kile alichoonja katika utukufu aupatao shahidi." Muslim alikusanya Hadithi hii.¹

Imam Ahmad رضي الله عنه amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisema،

«لَمَّا أُصِيبَ إِخْوَانُكُمْ بِأَحَدٍ، جَعَلَ اللَّهُ أَرْوَاحَهُمْ فِي أَجْوَابِ طَبِيرِ خُضْرٍ، تَرِدُ أَنْهَارَ الْجَنَّةِ، وَتَأْكُلُ مِنْ ثَمَارِهَا، وَتَأْوِي إِلَى قَنَادِيلَ مِنْ ذَهَبٍ فِي ظِلِّ الْعَرْشِ، فَلَمَّا وَجَدُوا طَيْبَ مَسَرِّبِهِمْ وَمَأْكَلِهِمْ، وَحُسْنَ مَتَقَلَّبِهِمْ قَالُوا: يَا لَيْتَ إِخْوَانَتَنَا يَعْلَمُونَ مَا صَنَعَ اللَّهُ لَنَا، لَيْتَلَا يَزْمِدُوا فِي الْجِهَادِ، وَلَا يَنْكَلُوا عَنِ الْحَرْبِ، فَقَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: أَنَا أَبْلَغُهُمْ عَنْكُمْ»

"Ndugu zenu walipouawa katika Uhud، Allah تعالى Alizitia roho zao ndani ya tumbo la ndege wa kijani ambao wanavinjari katika mito ya Peponi na wanakula matunda yake. Kisha wanarejea kwenye taa za dhahabu zinazoning'inia katika kivuli cha Arshi. Wanapoonja ladha ya vyakula، vinywaji na makazi mazuri، na mwisho mwema. Wanasema، "Laiti ndugu zetu wangeelewa Aliyotufanyia Allah تعالى wasingeacha Jihadi wala wasingekimbia mapigano." Allah تعالى Akawaambia، 'Nitawafikishia khabari hizi kwa niaba yenu.'

Allah تعالى Aliteremsha Aya hii na nyengine،

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزَقُونَ ﴿١٦٩﴾

"Wala kabisa usiwadhania waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai، wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi." (3:169)²

¹ Ahmad 3:126، Muslim 1877.

² Ahmad 1:265.

Kama hivyo amepokea Ahmad, Qatadah, Ar-Rabi na Adh-Dhahhak walisema kuwa Aya hizi ziliteremshwa kuhusiana na mashahidi wa Uhud.¹ Abubakar Ibn Marduwyah رضي الله عنه alipokea kutoka kwa Jabir bin Abdullah قال تعالى akisema, "Mtume ﷺ siku moja aliniangalia na kuniambia, "Ewe Jabir! Kwanini unahuzunika?" Nikajibu, 'Ewe Mtume ﷺ Baba yangu alikufa shahidi na ameacha madeni na watoto." Akajibu,

«أَلَا أُخْبِرُكَ؟ مَا كَلَّمَ اللَّهُ أَحَدًا قَطُّ إِلَّا مِنْ وَرَاءِ حِجَابٍ، وَإِنَّهُ كَلَّمَ أَبَاكَ كِفَاحًا»،
قال علي: الكفاح: المواجهة «قَالَ: سَلَنِي أُعْطِكَ. قَالَ: أَسَأَلُكَ أَنْ أُرَدَّ إِلَى
الدُّنْيَا فَأُقْتَلَ فِيكَ ثَانِيَةً، فَقَالَ الرَّبُّ عَزَّ وَجَلَّ: إِنَّهُ قَدْ سَبَقَ مِنِّي الْقَوْلُ: إِنَّهُمْ إِلَيْهَا
لَا يَرْجِعُونَ. قَالَ: أَيُّ رَبِّ فَأَبْلِغْ مَنْ وَرَائِي»

"Waonaje, nikupe khabari kuwa Allah تعالى Hajawahi Kuzungumza na mtu yoyote isipokuwa nyuma ya pazia? Hata hivyo Alizungumza na baba yako moja kwa moja Akamwambia, 'Niombe na Nitakujibu'. Akasema, 'Ninaomba nirejeshwe duniani ili niuawe katika njia Yako. Mola Mlezi, Alisema, 'Nilisema neno kuwa hawatarejeshwa katika maisha ya dunia.' Akasema, 'Ewe Mola Mlezi! Nifikishie khabari kwa wale niliowaacha nyuma".

Kwa ajili hiyo Allah تعالى Aliteremsha,

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا

"Wala kabisa usiwadhania waliouliwa katika njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti." (3:156)²

Imam Ahmad alipokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الشُّهَدَاءُ عَلَى بَارِقٍ نَهْرٍ بِبَابِ الْجَنَّةِ، فِي قُبَّةِ حَضْرَاءَ، يَخْرُجُ عَلَيْهِمْ رِزْقُهُمْ مِنْ
الْجَنَّةِ بُكْرَةً وَعَشِيًّا»

"Mashahidi wapo katika ukingo wa mto kwenye mlango wa peponi, ndani yake kuna kuba la kijani, riziki yao inatokea peponi, asubuhi na jioni."

¹ At-Tabari 7:389-390.

² Dala'il An - Nubuwwah, cha Al-Bayhaqi 3:299.

Ahmad¹ na Ibn Jarir² walipokea Hadithi hii, ambayo ina isnadi nzuri ya upokezi. Inaonesha kuwa mashahidi wako wa aina nyingi, baadhi wanavinjari Peponi, na baadhi hukaa jirani na mto huu wenye mlango wa kuingilia Peponi. Aidha yamkini hapo kwenye mto ndio pahala pa kukutania roho za mashahidi na hupata mahitajio ya mchana na usiku, na Allah تعالی ni Mjuzi Zaidi.

Imam Ahmad رحمه الله تعالی alipokea Hadithi yenye bishara njema kwa kila muumini kuwa roho yake itakuwa Peponi, ikivinjari humo na kula matunda yake, wakifurahia starehe zake na kuonja utukufu walioandaliwa na Allah تعالی. Hadithi hii ina isnadi ya kipekee iliyo sahihi ambayo ni pamoja na Maimamu watatu kati ya Wanne. Imamu Ahmad رحمه الله تعالی aliipokea Hadithi hii kutoka kwa Muhammad bin Idris Ash-Shafi رحمه الله تعالی ambaye aliipokea kutoka kwa Abdulrahman bin Kaab bin Malik ambaye baba yake alisema kuwa Mjumbe ﷺ alisema.

«نَسَمَةُ الْمُؤْمِنِ طَائِرٌ يَغْلُقُ فِي شَجَرِ الْجَنَّةِ حَتَّى يَرْجِعَهُ اللَّهُ إِلَى جَسَدِهِ يَوْمَ يَبْعَثُهُ»

*"Roho ya muumini huwa ni ndege anayekula kutokana na miti ya Peponi, mpaka Allah تعالی Anapoirejesha katika mwili wake wakati Atakapomfufua."*⁴

Katika Hadithi hii inaeleza kuwa: Roho ya muumini ina umbo lifananalo na ndege katika Pepo. Ama roho za mashahidi ni kama tulivyoona katika maelezo yaliyotangulia ziko katika matumbo ya ndege wa kijani, nazo ni mfano wa nyota ukilinganisha na roho za waumini wengine wa kawaida, zinaruka zenyewe. Tunamuomba Allah تعالی Mkarimu Azithibitisha Imani zetu. Kauli ya Allah تعالی

فَرِحِينَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ

"Wanafurahia Aliyowapa Mwenyezi Mungu."

Inathibiti kuwa mashahidi ambao waliouawa katika njia ya Allah تعالی, wako hai kwa Allah تعالی, wamependezewa kwa sababu ya ukarimu na furaha waipatayo. Pia wanawabashiria ndugu zao, ambao watauawa katika njia ya Allah تعالی baada yao kuwa watakutana nao. Hawa mashahidi hawana khofu kwa yatakayokuja na hawana huzuni kwa waliyoyaacha nyuma. Tunamuomba

¹ Ahmad 1:266.

² At-Tabari 7:387.

³ Ahmad 3:455.

Allah تعالی Aturidhie Pepo. Sahihi mbili zimepokea kutoka kwa Anas رضي الله عنه, kisa cha Maswahaba sabiini wa Kiansari ambao waliuawa katika *Biir Ma'unah* katika mchanga mmoja alimuomba Allah تعالی katika Qunut katika kila Sala dhidi ya wale waliowaua akiwalaani na kuwaomba maangamizo. Anas رضي الله عنه alisema, "Sehemu ya Qur'an iliteremshwa ikiwajadili wao, lakini baadaye ilifutwa: 'Wafikishieni watu wetu kuwa tulikutana na Allah تعالی na Alikuwa radhi nasi na Alituridhisha.'"¹ Baadaye Allah تعالی Akasema,

﴿ يَسْتَبْشِرُونَ بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ وَأَنَّ اللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجْرَ الْمُؤْمِنِينَ ﴾

"Wanashangilia Neema na Fadhila za Mwenyezi Mungu, na ya kwamba Mwenyezi Mungu Hapotezi ujira wa Waumini" (3:171)

Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالی alisema yafuatayo, "Walipendezwa na kuridhishwa kwa sababu ya ahadi ya Allah تعالی iliyotekelezwa na kwa malipo waliyopata." Abdur Rahman bin Zayd bin Aslam alisema, "Aya hii inawaenea waumini wote, mashahidi na wengineo. Ni nadra Allah Kutaja Neema na Malipo Aliyowapa Mitume ﷺ bila Kulifuatilia hilo na kile Alichowaruzuku waumini baada yao."

Maelezo ya Vita vya *Hamra Al-Asad* na Fadhila za Walioshiriki

Allah تعالی Alisema,

﴿ الَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِلَّهِ وَالرَّسُولِ مِنْ بَعْدِ مَا أَصَابَهُمُ الْقَرْحُ ﴾

"Waliomuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya kwisha patwa na majeraha." (3:172)

Hili lilijiri siku ya *Hamra Al-Asad*. Baada ya washirikina kuvuna walichopata kwa Waislamu (katika Uhud), walianza kurejea nyumbani, lakini mara walipofika njiani waliingia na majuto: Kwa nini hawakuwamaliza watu wa Madina na kuangamiza Jeshi lake kuifanya vita hiyo iwe ndiyo ya mwisho. Mtume ﷺ alipopata khabari hizi, aliwaamuru Waislamu wawafuate kwa nyuma, ili kuwapa khofu katika mioyo yao na kuwaonesha kuwa Waislamu walikuwa bado wana nguvu ya kupigana. Mtume ﷺ aliwaruhusu wale waliokuwepo

¹ Fat'hul Al-Bari 7:445, Muslim 1:468.

katika Uhud kufuatana naye, isipokuwa Jabir bin Abdullah Al-Ansar رضي الله عنه, kama tutakavyobainisha hilo. Waislamu walihamasishana japokuwa walikuwa bado wakitibu majeraha, kwa kumtii Allah تعالى na Mtume ﷺ. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ikrima kuwa alisema, “Washirikina waliporejea (Makkah) baada ya Uhud walisema, “Hamkumuua Muhammad wala kuwakusanya mateka wa kike ni tendo baya mlilolifanya. Turejeeni tena!!” Mtume ﷺ aliposikia habari hizi aliandaa majeshi ya Waislamu na wakaondoka mpaka alipofika *Hamra Al-Asad* au *Biiri Abu Uyaina*. Mushirikina walisema, ‘Bali tutarudi mwaka ujao.’ Mtume ﷺ alirejea (Madinah), na hii ilichukuliwa kuwa ni *Ghazwah* (vita). Allah تعالى Aliteremsha,

الَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِلَّهِ وَالرَّسُولِ مِنْ بَعْدِ مَا أَصَابَهُمُ الْقَرْحُ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا مِنْهُمْ وَاتَّقُوا

أَجْرٌ عَظِيمٌ

“Waliomuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya kwisha patwa na majeraha - kwa waliofanya wema miongoni mwao na wakamchamungu utakuwa ujira mkubwa.” (3:172)¹

Bukhari alipokea kutoka kwa Aisha رضي الله عنها, alimuambia Urwah رضي الله عنه kuhus Aya;

الَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِلَّهِ وَالرَّسُولِ

“Waliomuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume”.

“Binamu yangu! Baba zako, Az-Zubayr na Abubakr رضي الله عنهما walikuwa miongoni mwao. Baaada ya Mtume ﷺ kufikwa na madhila katika Uhud na Washirikina kurejea, alichelea kuwa washirikina wangerejea na akasema, ‘Nani atawafuata?’ Watu *sabini*, ikiwa ni pamoja na Az-Zubayr na Abubakar walijitolea kuwafuata.” Hadithi hii ilipokewa na Bukhari peke yake.² Na Kauli ya Allah تعالى,

الَّذِينَ قَالَ لَهُمُ النَّاسُ إِنَّ النَّاسَ قَدْ جَمَعُوا لَكُمْ فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَانًا

“Walioambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani.” (3:173)

¹ An-Nasaai Al-Kubra Na. 11083.

² Bukhari (4077).

Ina maana, wale waliowatisha watu, wakisema kuwa makafiri wamejikusanya dhidi yenu, ili kuwajengea hofu, lakini hili halikuogopwa, bali, walimuamini Allah تعالى na wakataka msaada Wake kwa kusema,

وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ ﴿١٧٣﴾

“Wakasema: Mwenyezi Mungu Anatutosha, Naye ni M-bora wa kutegemewa.” (3:173)

Bukhari alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما,

حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ ﴿١٧٣﴾

“Mwenyezi Mungu Anatutosha, Naye ni M-bora wa kutegemewa.”

Nabii Ibrahim عليه السلام aliyasema haya alipotupwa katika moto, Nabii Muhammad ﷺ alilisema hili watu waliposema, “Kwa hakika watu wamejikusanya dhidi yako, kwa hiyo, waogope.” Lakini liliwaongezea Imani, na wakasema, “Allah تعالى Anatutosha sisi na Ndiye M-bora wa Kutukidhiia haja zetu.”² Abubakar Ibn Marduwyah رحمه الله تعالى alipokea kuwa Anas Bin Maliki رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ aliambiwa siku ya Uhud, “Kwa hakika, watu wamejikusanya dhidi yako, kwa hiyo waogope.” Baadaye, Allah تعالى Aliteremsha Aya (3:173). Na kwa kuzingatia hilo. Allah تعالى Amesema,

فَأَنْقَلَبُوا بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ لَّمْ يَمَسَّهِمْ سُوءٌ

“Basi wakarudi na Neema na Fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa.” (3:174)

Walipomtegemea Allah تعالى, Allah تعالى Alizituliza hofu zao, Aliziangamiza njama za maadui zao, na Waislamu walirejea katika ardhi yao.

بِنِعْمَةٍ مِّنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ لَّمْ يَمَسَّهِمْ سُوءٌ

“Kwa Neema na Fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa.” (3:174)

¹ Fat’hul Al-Bari 8:77.

Wakasalimika kutokana na njama mbovu walizopanga maadui zao,

وَاتَّبِعُوا رِضْوَانَ اللَّهِ وَاللَّهُ ذُو فَضْلٍ عَظِيمٍ ﴿١٦٥﴾

“Na wakafuata yanayomridhi Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Fadhila kuu.”

Al-Bayhaqi alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

فَأَنْقَلَبُوا بِنِعْمَةٍ مِنَ اللَّهِ وَفَضْلٍ

“Basi wakarudi na Neema na Fadhila za Mwenyezi Mungu.”

“**Neema.**” ni kule kuokolewa. “**Fadhila**” ni msafara uliopita siku hizo katika msimu wa Hajj. Hivyo Mtume ﷺ alinunua na kuuza na kupata faida, aliyowagawia Masahaba.”¹ Kisha Allah تعالى Akasema,

إِنَّمَا ذَلِكُمُ الشَّيْطَانُ يُخَوِّفُ أَوْلِيَاءَهُ

“Hakika huyo ni Shetani anawatia khofu marafiki zake”.

Muradi wake ni kuwa wanaokukukhofisheni ni wasaidizi wa shetani na wanajifanya wana nguvu na silaha kali za kiwango cha juu. Kisha Allah تعالى Amesema,

فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُوا مِنِّي إِن كُنتُمْ مُؤْمِنِينَ ﴿١٦٦﴾

“Basi msiwaogope, bali Niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini.”

Maana yake: “kama Shetani anawaleta fikra za woga, basi nitegemeeni Mimi na kimbilieni Kwangu. Kwa hakika, Nitawatosheni na Kuwafanya washindi juu yao.” Vivyo hivyo, Allah تعالى Amesema,

أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ ۗ وَيُخَوِّفُونَكَ بِالَّذِينَ مِن دُونِهِ

“Je! Mwenyezi Mungu si wa Kumtosheleza mja wake? Na ati wanakutishia kwa hao wenginewe wasiokuwa Yeye”. (39:36).

Hadi Kauli ya Allah تعالى,

¹ Dala ‘il u An – Nubuwwah 3:318.

قُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ عَلَيْهِ يَتَوَكَّلُ الْمُتَوَكِّلُونَ ﴿٧٨﴾

“Sema: Mwenyezi Mungu Anamtosheleza, Kwake Yeye wategemee wanaotegemea.” (39:38)

Allah تعالى Amesema,

أَسْتَحْوَذَ عَلَيْهِمُ الشَّيْطَانُ فَأَنسَهُمْ ذِكْرَ اللَّهِ ۚ فَأُولَٰئِكَ حِزْبُ الشَّيْطَانِ ۗ أَلَا إِنَّ حِزْبَ الشَّيْطَانِ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿٧٩﴾

“Shetani amewatawala na akawasahaulisha kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hao ndio kundi la Shetani. Kweli hakika kundi la Shetani ndilo lenye kukhasirika.” (58:19)

Na Amesema tena Allah تعالى,

كَتَبَ اللَّهُ لَأَغْلِبَنَّ أَنَا وَرُسُلِي ۗ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٨٠﴾

“Mwenyezi Mungu Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.” (58:21)

Allah تعالى Amesema,

فَقَاتِلُوا أَوْلِيَاءَ الشَّيْطَانِ ۗ إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا ﴿٧٧﴾

“Basi piganeni na marafiki wa Shetani. Hakika hila za Shetani ni dhaifu.” (4:76)

Na Amesema tena Allah تعالى,

وَلَيَنصُرَنَّ اللَّهُ مَن يَنصُرُهُ ۗ

“Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu Humsaidia yule anayemsaidia Yeye”. (22:40) Na Amesema tena Allah تعالى,

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ

“Enyi mliaoamini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu Naye Atakunusuruni.” (47:7)

Na Amesema tena Allah تعالى،

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾ يَوْمَ لَا
يَنْفَعُ الظَّالِمِينَ مَعَذِرَتُهُمْ ۖ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ ﴿٥٢﴾

“Hakika bila ya shaka Sisi Tunawanusuru Mitume Wetu na walio amini katika uhai wa duniani na siku wataposimama Mashahidi, Siku ambayo hautawafaa madhalimu udhuru wao, nao watapata laana, na watapata makazi mabaya kabisa.” (40:51-52)

* * *

وَلَا يَخْزِيكَ الَّذِينَ يُسْرِعُونَ فِي الْكُفْرِ إِنَّهُمْ لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا يُرِيدُ اللَّهُ أَلَّا يَجْعَلَ لَهُمْ حَظًّا فِي الْآخِرَةِ ۗ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٧٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ اشْتَرُوا الْكُفْرَ بِالْإِيمَانِ لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٧﴾ وَلَا يَخْسِبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا أَلَّا يَكْفُرُوا إِنَّهُمْ لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٨﴾ وَلَا يَخْسِبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا أَلَّا يَكْفُرُوا إِنَّهُمْ لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٩﴾ مَا كَانَ اللَّهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتَّىٰ يَمِيزَ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ ۗ وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُطْلِعَكُمْ عَلَى الْغَيْبِ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَجْتَبِي مِن رُّسُلِهِ مَن يَشَاءُ ۖ فَتَقَائِمُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۗ وَإِن تَوَلَّيْتُمْ ۖ سَيُطَوَّقُونَ مَا مَخَّلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَاللَّهُ يَمِيزُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١٨٠﴾

وَلَا يَخْزِيكَ الَّذِينَ يُسْرِعُونَ فِي الْكُفْرِ إِنَّهُمْ لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا يُرِيدُ اللَّهُ أَلَّا يَجْعَلَ لَهُمْ حَظًّا فِي الْآخِرَةِ ۗ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٧٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ اشْتَرُوا الْكُفْرَ بِالْإِيمَانِ لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٧﴾ وَلَا يَخْسِبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا أَلَّا يَكْفُرُوا إِنَّهُمْ لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٨﴾ وَلَا يَخْسِبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا أَلَّا يَكْفُرُوا إِنَّهُمْ لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٧٩﴾ مَا كَانَ اللَّهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتَّىٰ يَمِيزَ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ ۗ وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُطْلِعَكُمْ عَلَى الْغَيْبِ وَلَكِنَّ اللَّهَ يَجْتَبِي مِن رُّسُلِهِ مَن يَشَاءُ ۖ فَتَقَائِمُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۗ وَإِن تَوَلَّيْتُمْ ۖ سَيُطَوَّقُونَ مَا مَخَّلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَاللَّهُ يَمِيزُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١٨٠﴾

176. Wala wasikuhuzunishe wale wanaokimbilia ukafirini. Hakika hao hawamdhuru kitu Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Anataka Asiwawekee sehemu yoyote katika Akhera, na yao wao adhabu kubwa.

177. Hakika wale walionunua ukafiri kwa Imani hawatamdhuru kitu Mwenyezi Mungu, na yao wao ni adhabu chungu.

178. Wala wasidhani wale wanaokufuru kwamba huu muhula Tunaowapa ni kheri kwao. Hakika Tunawapa muhula wazidi madhambi. Na wana wao kwao adhabu ya kuwadhalilisha.

179. Haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwaacha Waumini katika hali mliyonyo mpaka Apambanue wabaya na wema. Wala haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kukujuulisheni mambo ya ghaibu. Lakini Mwenyezi Mungu Humteua katika Mitume Wake Amtakaye. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mitume Yake. Na mkiamini na mkamchamungu mtakuwa na ujira mkubwa.

180. Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika Fadhila Zake kuwa ni kheri kwao. Bali hiyo ni shari kwao. Watafungwa kongwa za yale waliyoyafanyia ubakhili Siku ya Kiyama. Na urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za yote myatendayo.

Kumfariji Mtume ﷺ

Allah تعالی Alimuambia Mtume wake ﷺ

وَلَا تَحْزَنْكَ الَّذِينَ يُسْرِعُونَ فِي الْكُفْرِ

“Wala wasikuhuzunisha wale wanaokimbilia ukafirini.” (3:176)

Kutokana na ukubwa wa mapenzi ya Mtume ﷺ kutaka watu wawe Waislamu alikuwa akihuzunishwa na makafiri waliokuwa wanakhitari ukafiri, kukengeuka na kwenda kinyume.

Ndiyo maana Allah تعالی Akasema: Hayo yasikuhuzunisheni kwani,

إِنَّهُمْ لَنْ يَصُورُوا اللَّهَ شَيْئًا يُرِيدُ اللَّهُ أَلَّا يَجْعَلَ لَهُمْ حِطًّا فِي الْآخِرَةِ

“Hakika hao hawamduru kitu Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Anataka Asiwawekee sehemu yoyote katika Akhera.”

Kwani aliamua kwa Qadari Yake na Hikima Yake kuwa hawatopata hisa yoyote siku ya Kiyama,

وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ

“Na wana wao adhabu kubwa.”

Allah تعالى Alizungumza kuhusu makafiri,

إِنَّ الَّذِينَ أَشْرَوْا كُفُرُوا بِالْإِيمَانِ

“Hakika wale walionunua ukafiri kwa Imani.”

Maana yake: Walibadilisha Uislamu wakaendeleza ukafiri.

لَنْ يَضُرُّوا اللَّهَ شَيْئًا

“Hawamdhuru kitu Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Wanazidhuru nafsi zao.

وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Na wao wana adhabu chungu.” (3:177)

Na Amesema tena Allah تعالى.

وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ مَا نُمَلِّهِمْ هُمْ خَيْرٌ لَّأَنْفُسِهِمْ ۚ إِنَّمَا نُمَلِّهِمْ لِيَزِدُوا إِثْمًا وَهُمْ

عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿١٧٨﴾

“Wala wasidhani wale wanaokufuru kwamba huu muhula Tunaowapa ni kheri yao. Hakika Tunawapa muhula wazidi madhambi. Na yao wao ni adhabu ya kuwadhalilisha.” (3:178)

Kauli hii ni sawa na Kauli ingine ya Allah تعالى isemayo,

أَحْسَبُونَ أَنَّمَا نُمْدِدُهُمْ بِهِ مِنْ مَّالٍ وَبَنِينَ ﴿١٧٩﴾ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرَاتِ ۗ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿١٨٠﴾

“Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto. Ndio Tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.” (23:55-56)

Na kama Kauli Yake Allah تعالى,

فَدَرَنِي وَمَنْ يُكَذِّبْ بِهَذَا الْحَدِيثِ ۗ سَنَسْتَدْرِجُهُمْ مِنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٨١﴾

“Basi niache na wanaokadhibisha maneno haya! Tutawavutia kidogo kidogo kwa mahali wasipopajua.” (68:44)

وَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَأَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الدُّنْيَا وَتَزْهَقَ أَنْفُسُهُمْ
وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٨٥﴾

“Wala zisikupendezeshe mali zao na watoto wao. Mwenyezi Mungu Anataka Kuwaadhibu kwa hayo katika dunia; na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri.” (9:85)

Na Amesema tena Allah تعالى،

مَا كَانَ اللَّهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتَّىٰ يَمِيزَ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ

“Haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwaacha Waumini katika hali mliyo nayo mpaka Apambanue wabaya na wema.” (3:179)

Maana yake: Anaruhusu mtihani, na wakati wa mtihani huu rafiki zake wanabainika, adui zake kuumbuka, waumini wenye subira kutambulika, na wanafiki waovu kufichuka. Ayah hii inahusu tukio la Uhud, Allah تعالى Aliwatahini waumini katika vita hiyo kufahamu imani zao, uvumilivu, subira, ukakamavu na utii wao, kwa Allah تعالى na Mtume ﷺ. Na kwa mtihani huo Allah تعالى Alifichua wanafiki kwa kupinga kwao Jihadi na kwenda kinyume na Amri ya Allah تعالى na Mtume ﷺ. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

مَا كَانَ اللَّهُ لِيَذَرَ الْمُؤْمِنِينَ عَلَىٰ مَا أَنْتُمْ عَلَيْهِ حَتَّىٰ يَمِيزَ الْخَبِيثَ مِنَ الطَّيِّبِ

“Haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kuwaacha Waumini katika hali mliyo nayo mpaka Apambanue wabaya na wema.” (3:179)

Mujahid alitoa maelezo kuwa: “Allah تعالى aliwapambanulia siku ya Uhud.”¹ Na Qatadah alisema: “Allah تعالى Aliwatofautisha katika utekelezaji wa Jihad na Hijrah.”² Baadae Allah تعالى Alisema,

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُطْلِعَكُمْ عَلَى الْغَيْبِ

“Wala haiwi kwa Mwenyezi Mungu Kukujuulisheni mambo ya ghaibu.” (3:179)

¹ At - Tabari 7:424.

² At - Tabari 7:424.

Maana yake: Hamjui Ilimu ya Allah تعالى juu ya viumbe Wake ili mtofautishe kati ya waumini na wanafiki, ila kwa kuweka sababu zinazodhihirisha hayo. Kauli ya Allah تعالى,

وَلَكِنَّ اللَّهَ يَجْتَبِي مِنْ رُسُلِهِ مَنْ يَشَاءُ

“Lakini Mwenyezi Mungu Humteua katika Mitume Wake Amtakaye.” (3:179)

Ni kama Kauli Yake Allah تعالى,

عَلَيْمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهَرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿١٧٦﴾ إِلَّا مَنِ ارْتَضَىٰ مِنْ رَسُولٍ فَإِنَّهُ يَسْلُكُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَيَمْنِ حَلْفِيهِ رِصْدًا ﴿١٧٧﴾

“Yeye Ndiye Mwenye Kujua ya siri, wala Hamdhihirishii yeyote siri yake, isipokuwa Mtume Wake Aliyemridhia. Naye huyo Humwekea walinzi mbele yake na nyuma yake.” (72:26-27)

Kisha Allah تعالى Amesema,

فَقَامُوا بِاللَّهِ وِرْسُلِهِ^٤

“Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mitume Yake.”

Mtiini Allah تعالى na Mtume ﷺ na shikamaneni na sheria Alizokuandikieni.

وَإِنْ تَوَلَّيْتُمْ فَأَعْرَابٌ فَلَكُمْ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿١٧٩﴾

“Mkiamini na mkamchamungu mtakuwa na ujira mkubwa.” (3:179)

Shutuma Dhidi ya Ubakhili na Onyo Kali Dhidi Yake.

Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخُلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَّهُمْ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَّهُمْ

“Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika Fadhila Zake kuwa ni kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao.” (3:180)

Kwa hiyo, bakhili asidhani kuwa kulimbikiza kwake mali kutamsaidia. Bali,

kutamdhuru katika dini yake na hata katika dunia yake pia. Kisha Allah تعالى Anaeleza matokeo ya fedha alizokusanya bakhili siku ya kufufuliwa kwa Kusema,

سَيُطَوَّقُونَ مَا كَانُوا بِمِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Watafungwa kongwa za yale waliyoyafanyia ubakhili Siku ya Kiyama.” (3:180)

Bukhari amenukuu Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema, Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ آتَاهُ اللَّهُ مَالًا فَلَمْ يُؤَدِّ زَكَاتَهُ، مَثَلٌ لَهُ شُجَاعًا أَفْرَعُ، لَهُ زَبِيَّانٍ، يُطَوَّقُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، يَأْخُذُ بِلَهْزِمَتَيْهِ - يَغْنِي بِشِدْقَيْهِ - يَقُولُ: أَنَا مَالِكٌ، أَنَا كَنْزُكَ»

“Mtu yeyote aliyepewa mali na Allah na asiitolee Zaka yake hiyo, basi (siku ya kufufuliwa) mali yake itageuzwa joka la kiume lenye kipara, lenye sumu, lenye madoa meusi mawili juu ya macho yake. Nyoka atajiviringisha kwenye shingo yake na atamuuma mashavu yake na kutangaza, ‘Mimi ni mali yako, mimi ni hazina yako.”

Kisha baada ya kusema maneno hayo Mtume ﷺ alisoma Aya hii,

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَبْخُلُونَ بِمَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ هُوَ خَيْرًا لَّهُمْ بَلْ هُوَ شَرٌّ لَّهُمْ

“Wala wasidhani wale ambao wanafanya ubakhili katika Aliyo wapa Mwenyezi Mungu katika Fadhila Zake kuwa ni Kheri yao. Bali hiyo ni shari kwao”. (3:180)

Alisoma mpaka mwisho wa Aya.¹ Ameipokea Al-Bukhari peke yake, Muslim hajaipokea. Ibn Hibban pia ameandika Hadithi hii katika Sahihi yake.² Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Abdullah رضي الله عنه akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا مِنْ عَبْدٍ لَا يُؤَدِّي زَكَاتَ مَالِهِ إِلَّا جُعِلَ لَهُ شُجَاعٌ أَفْرَعٌ يَتَّبِعُهُ، يَغْرُ مِنْهُ وَهُوَ يَتَّبِعُهُ، يَقُولُ: أَنَا كَنْزُكَ»

“Hakuna mja yoyote asiyetoa Zakah ya mali yake, isipokuwa zitageuzwa umbile la nyoka dume, mwenye kipara, mwenye sumu

¹ Fat’hul Al-Bari 8:78.

² Ibn Hibban 5:107.

ambaye atamfuata Mtu naye atamkimbia, nyoka ataendelea kumfuata na kunadi, 'Mimi ni hazina yako.'

Kisha Abdullah رضى الله عنه alisoma Aya ya ushahidi juu ya hilo isemayo,

سَيُطَوَّقُونَ مَا نَخُلُوا بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Watafungwa kongwa za yale waliyoyafanyia ubakhili Siku ya Kiyama.”¹

Hadithi hii ilipokewa na At-Tirmidhi,² An-Nasai,³ na Ibn Majah⁴ At - Tirmidhi amesema ni “*Hassan Sahihi*” Kauli ya Allah تعالى,

وَلِلَّهِ مِيرَاثُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Urithi wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu.” Maana yake:

وَأَنْفِقُوا مِمَّا جَعَلَكُمْ مُسْتَحْلِفِينَ فِيهِ

“Na toeni katika Alivyo kufanyeni nyinyi kuwa ni waangalizi wake”.
(57:7)

Ni, kwa kuwa mambo yote marejeo yake ni kwa Allah تعالى, basi jitangulizieni katika mali zenu yatakayowanufaisha siku ya kiyama.

وَاللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ

“Na Mwenyezi Mungu Anazo khabari za yote myatendayo.”

Anazonia nia zenu na dhamira zenu.

* * *

¹ Ahmad 1:377.

² Tuhfatul Al-Ahwadhi 8:393.

³ An-Nasaai katika Al-Kubra 6:317.

⁴ Ibn Majah 2:568.

لَقَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ سَنَكْتُبُ مَا قَالُوا وَقَتْلَهُمُ الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقٍّ وَنَقُولُ ذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿١٨١﴾ ذَلِكَ بِمَا قَدَّمْتُمْ أَيْدِيكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَامٍ لِلْعَبِيدِ ﴿١٨٢﴾ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ عَهْدٌ إِلَيْنَا إِلَّا نُوْثِرُ لِرَسُولٍ حَتَّىٰ يَأْتِينَا بَقُرْبَانٍ تَأْكُلُهُ النَّارُ قُلْ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّن قَبْلِي بِالْبَيِّنَاتِ وَبِالذِّكْرِ فَلَمَّا قَتَلْتُمُوهُمْ إِنَّ كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٨٣﴾ فَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَ رَسُولٌ مِّن قَبْلِكَ جَاءُوا بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ وَالْكِتَابِ الْمُنِيرِ ﴿١٨٤﴾ كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَإِنَّمَا تُوَفَّوْنَ أَجُورَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَمَن زُحِرَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿١٨٥﴾ * لَيَبْلُوَنَّ فِي أَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ وَلِتَسْمَعَنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا أَذًى كَثِيرًا ۗ وَإِن تَصَبَرُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ ذَلِكَ مِّن عِزِّ الْأُمُورِ ﴿١٨٦﴾

لَقَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ سَنَكْتُبُ مَا قَالُوا وَقَتْلَهُمُ الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقٍّ وَنَقُولُ ذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿١٨١﴾ ذَلِكَ بِمَا قَدَّمْتُمْ أَيْدِيكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَامٍ لِلْعَبِيدِ ﴿١٨٢﴾ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ عَهْدٌ إِلَيْنَا إِلَّا نُوْثِرُ لِرَسُولٍ حَتَّىٰ يَأْتِينَا بَقُرْبَانٍ تَأْكُلُهُ النَّارُ قُلْ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّن قَبْلِي بِالْبَيِّنَاتِ وَبِالذِّكْرِ فَلَمَّا قَتَلْتُمُوهُمْ إِنَّ كُنتُمْ صَادِقِينَ ﴿١٨٣﴾ فَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَ رَسُولٌ مِّن قَبْلِكَ جَاءُوا بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ وَالْكِتَابِ الْمُنِيرِ ﴿١٨٤﴾

181. Mwenyezi Mungu Amekwishasikia kauli ya

waliosema: Mwenyezi Mungu ni masikini, na sisi ni matajiri. Tumeyaandika waliyoyasema, na pia kuwaua kwao Manabii bila ya haki, na Tutawaambia Siku ya Kiyama: Onjeni adhabu ya yenye kuunguza.

182. Haya ni kwa sababu ya iliyotanguliza mikono yenu, na kwamba Mwenyezi Mungu si Mwenye Kuwadhulumu waja,

183. Waliosema: Mwenyezi Mungu Ametuahidi tusimuamini Mtume yeyote mpaka atuletee kafara inayoteketezwa na moto. Waambie: Walikujieni

Mitume kabla yangu kwa hoja zilizo wazi na kwa hayo mnayo-sema, basi kwa nini mkawaua ikiwa mlikuwa wakweli?

184. Na wakikukanusha basi walikanushwa Mitume wengine kabla yako waliokuja na hoja waziwazi na Vitabu vyenye hikima, na Kitabu chenye nuru.

Onyo la Allah تعالیٰ kwa Washirikina

Said bin Jubayr alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنها alisema, wakati iliposhuka Kauli ya Allah تعالیٰ,

مَنْ ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيَضَعِفُهُ لَهُ أَضْعَافًا كَثِيرَةً

“Ni nani atakayemkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema ili Amzidishie mzidisho mwingi.” (2:245)

Mayahudi walisema: Muhammad, Mungu wako amekuwa fakiri kwani Anaomba mkopo toka kwa viumbe Wake. Hapo Allah تعالیٰ Aliteremsha Kauli Yake:

لَقَدْ سَمِعَ اللَّهُ قَوْلَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ فَقِيرٌ وَنَحْنُ أَغْنِيَاءُ

“Mwenyezi Mungu Amekwishesikia kauli ya waliosema: Mwenyezi Mungu ni masikini, na sisi ni matajiri.”

Hadithi hii ilikusanywa na Marduwyah na Ibn Abi Hatim. Kauli ya Allah تعالیٰ,

سَنَكْتُبُ مَا قَالُوا

“Tumeyaandika waliyoyasema.”

Ndani yake mna karipio na onyo, karipio hilo limefuatia baada ya Kauli Yake تعالیٰ,

وَقَتَلَهُمُ الْآلِئِيَاءَ بِغَيْرِ حَقٍّ

“Na pia kuwaua kwao Manabii bila ya haki.”

Hivi ndivyo wasemavyo juu ya Allah تعالیٰ na hivi ndivyo wanavyowatendea Mitume Wake. Allah تعالیٰ Atawalipa malipo mabaya na kwa hilo Allah تعالیٰ Amesema,

وَتَقُولُ ذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿١٨١﴾ ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمْت أَيْدِيكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَّامٍ

لِّلْعَبِيدِ ﴿١٨٢﴾

“Na Tutawaambia Siku ya Kiyama: Onjeni adhabu ya kuungua. Haya ni kwa sababu ya iliyotanguliza mikono yenu, na kwamba Mwenyezi Mungu si Mwenye Kuwadhulumu waja.”

Wataambiwa hivyo kwa lugha ya kebehi, dharau, kunyanyaswa n.k. kama njia ya adhabu.

Allah تعالى Alisema,

الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ عٰهَدَ إِلَيْنَا آلا نُوْمِنُ لِرَسُولٍ حَتَّىٰ يَأْتِنَنَا بُعْرَابَانِ تَأْكُلُهُ النَّارُ

“Waliosema: Mwenyezi Mungu Ametuahidi tusimuamini Mtume yeyote mpaka Atuletee kafara inayoteketezwa na moto.”

Allah تعالى Alikanusha madai yao yaliyopo katika Vitabu vyao, Allah تعالى Alichukua ahadi kutoka kwao wamuamini Mjumbe pekee ambaye miujiza yake ni pamoja na kushuka moto kutoka juu ambao uliteketeza sadaka iliyotolewa na mmoja wa wafuasi wa Mjumbe wa umma huo, kama Ibn Abass رضي الله عنهما na Al-Hasan walivyotaja. Allah تعالى Alijibu,

قُلْ قَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّن قَبْلِي بِالْبَيِّنَاتِ

“Waambie: Walikujieni Mitume kabla yangu kwa hoja zilizo wazi.”

Maana yake: Walikuja kwa hoja mbali mbali, dalili na ushahidi

وَبِالَّذِي قُلْتُمْ

“Na kwa hayo mnayo sema.”

Maana yake: Moto unavyokula sadaka zinazokubaliwa.

فَلَمَّا قَتَلْتُمُوهُمْ

“Basi kwa nini mkawaua.”

Kwa nini mliwakataa Mitume hawa mkawakadhibisha, mkawakengeuka, mkawakaidi na hata kuwaua,

﴿١٨٢﴾ إِنَّ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

“Ikiwa mlikuwa wakweli?”,

Kama ni kweli mnafuata ukweli, na mnawatii Mitume? Kisha Allah تعالى Anamtuliza Mtume wake ﷺ kwa kumuambia

﴿١٨٣﴾ فَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقَدْ كُذِّبَ رَسُولٌ مِّن قَبْلِكَ جَاءُوا بِالْبَيِّنَاتِ وَالزُّبُرِ وَالْكِتَابِ الْمُنِيرِ ﴿١٨٣﴾

“Na wakikukanusha basi walikanushwa Mitume wengine kabla yako waliokuja na hoja waziwazi na Vitabu vyenye hikima, na Kitabu chenye nuru.”

Muradi wake, usihuzunike kwa kuwa wamekukana, kwani una mifano kwa Mitume waliokuja kabla yako. Mitume hao walikataliwa japokuwa walikuwa na dalili zilizo wazi, ushahidi, na alama zisizopingika.

وَالزُّبُرِ

“Vyenye hikima.”

Zaburi ni kati ya Vitabu vitakatifu walivyoteremshiwa Mitume kutoka Mbinguni kama suhufu.

﴿١٨٤﴾ وَالْكِتَابِ الْمُنِيرِ ﴿١٨٤﴾

“Na Kitabu chenye nuru.” Kwa uthibitisho na ufafanuzi.

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ وَإِنَّمَا تُوَفَّوْنَ أَجُورَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَمَن زُحِرَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿١٨٥﴾ * لَتَبْلُؤَنَّ فِي أَمْوَالِكُمْ وَأَنفُسِكُمْ وَلَتَسْمَعُنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا أَذًى كَثِيرًا وَإِن تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ ذَلِكَ مِّن عَزْمِ الْأُمُورِ ﴿١٨٦﴾

185. Kila nafsi itaonja mauti. Na bila ya shaka mtapewa ujira wenu kamili Siku ya Kiyama. Na atakayeepushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu. Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu.

186. Hapana shaka yoyote mtapata misukosuko katika mali zenu na nafsi zenu, na bila ya shaka yoyote mtasikia udhia mwingi kutoka kwa waliopewa Kitabu kabla yenu na washirikina. Na ikiwa mtasubiri na mkamchamngu basi hakika hayo ni katika mambo ya kuazimia.

Kila Nafsi Itaonja Kifo.

Allah تعالی Ametoa Kauli ya jumla inayojumuisha viumbe wote kuwa kila nafsi hai itaonja kifo. Katika Kauli nyengine. Allah تعالی Amesema,

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهَ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾

“Kila kilioko juu yake kitatoweka. Na Atabakia Mwenyewe Mola Wako Mlezi Mwenye Utukufu na Ukarimu.” (55:26-27)

Yeye Allah تعالی Pekee Ndiye wa milele ambaye hafi, ambapo majini na binadamu wanakufa pia na malaika, wachukuzi wa Arshi ya Allah تعالی na atakayedumu milele na milele ni Allah تعالی. Yeye Atasalia na kuwa wa Mwisho kama Alivyokuwa wa Mwanzo. Aya hii inawaliwaza viumbe wote, kwa kuwa kila nafsi inayoishi duniani itakufa. Muda wa kuishi unapokoma na wana wa Adam hawatokuwa na kizazi kipya, hivyo dunia hii itafikia kikomo, Allah تعالی Ataamrisha siku ya Ufufuo ianze. Kisha Allah تعالی Atawalipa viumbe kwa amali zao, ima ndogo au kubwa, nyingi au chache. Kwa hakika Allah تعالی Hatomdhulumu yeyote hata uzito wa chembe ndogo. Na kwa sababu hiyo Amesema,

وَإِنَّمَا تُوفَّرُ أَبْجُورَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Na bila ya shaka mtapewa ujira wenu kamili Siku ya Kiyama.”

Kufaulu kutakuwa ni kwa nani siku hiyo?

Allah تعالی Amesema,

فَمَنْ زُحِرَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ

“Na Atakayeepushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu.”

Muradi wake, yeyote atakayesalimika na Jahannam, akaokolewa nayo na akaingizwa Peponi, atakuwa amefuzu kufuzu kukubwa. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى, alipokea kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa alisema Mtume ﷺ alisema,

«مَوْضِعُ سَوْطٍ فِي الْجَنَّةِ خَيْرٌ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا فِيهَا، اقْرَأُوا إِن شِئْتُمْ»

“Eneo la mjeledi Peponi ni bora kuliko dunia na vilivyo ndani yake, someni mkipenda.”

فَمَنْ رُحِزَ عَنِ النَّارِ وَأُدْخِلَ الْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ

“Na atakayeepushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu.”

Hadithi hii ilikusanywa katika Sahihi Mbili, lakini ikiwa na Isnad tofauti na bila nyongeza (ya Aya).¹ Abu Hatim Ibn Hibban رحمه الله تعالى aliandika ndani ya Sahihi² yake bila nyongeza kama alivyofanya Al-Hakim رحمه الله تعالى katika Mustadrak wake.³ Allah تعالى Amesema,

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿٦٦﴾

“Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu.”

Maana yake: Kudunisha thamani ya maisha ya dunia na kudhalilisha umuhimu wake. Kuwa maisha haya ni mafupi, madogo na yenye kikomo, kama Allah تعالى Alivyosema:

بَلْ تُؤْتِرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٦٦﴾ وَالْآخِرَةَ خَيْرٌ وَأَبْقَى ﴿٦٧﴾

“Lakini nyinyi mnakhiari maisha ya dunia!, na Akhera ni bora na yenye kudumu zaidi.” (87:16-17) Na Akasema tena Allah تعالى,

وَمَا أُوتِيتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَمَتَّعُ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا وَزَيَّنْتُهَا وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْقَى

“Na chochote mlichopewa ni matumizi ya maisha ya dunia na pambo lake. Na yaliyoko kwa Mwenyezi Munugu ndio bora na yatakayo baki zaidi.” (28 :60)

¹ Fat’hul Bari 6:100.

² Ibn Hibban 9:252.

³ Al-Hakim 2:299

Hadithi inasema,

«وَاللَّهُ مَا الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا كَمَا يَغْمِسُ أَحَدُكُمْ أَصْبَعَهُ فِي الْيَمِّ، فَلْيَنْظُرْ بِمَ تَرْجِعُ إِلَيْهِ»

“Wallah! Maisha ya dunia ukiyalinganisha na ya Akhera si chochote, ni sawa na mtu anapotia kidole ndani ya bahari, atazame kidole chake kitatoka na maji mengi kiasi gani?”¹

Qatadah aliitolea maelezo Kauli ya Allah تعالى،

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا مَتَاعُ الْغُرُورِ ﴿١٨٦﴾

“Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu.”

Ni Maisha yanayofurahisha, ninaapa kuwa: Hapana muabudiwa mwingine ila Allah تعالى، furaha ya duniani itatoweka kwa watu. Kwa hiyo kuwa mtiifu kwa Allah تعالى kutokana na furaha hii kama unaweza. Kwa hakika hakuna nguvu za kufanya utiifu isipokuwa kutoka kwa Allah تعالى.”

Muumini Anajaribiwa na Anasikia Maudhi Kutoka kwa Adui

Allah تعالى Amesema،

﴿لَتَبْلُؤُنَّ فِي أَمْوَالِكُمْ وَأَنْفُسِكُمْ﴾

“Hapana shaka yoyote mtapata misukosuko katika mali zenu na nafsi zenu.” (3:186)

Kama Alivyosema katika aya nyingine،

﴿وَلَتَبْلُؤُنَّكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ﴾

“Hapana shaka Tutakujaribuni kwa chembe ya khofu na njaa, na upungufu wa mali na watu na matunda.”

Kwa hiyo, muumini atajaribiwa katika mali yake, nafsi yake, watoto wake na aila yake. Muumini atajaribiwa kwa kulingana na kiwango cha imani yake, endapo imani yake ina nguvu mtihani wake utakuwa mkubwa.

¹ Muslim 2858 na Tirmidhy 2324.

وَلَتَسْمَعُنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا أَذًى كَثِيرًا

“Na bila ya shaka yoyote mtasikia udhia mwingi kutokana na walio pewa Kitabu kabla yenu na washirikina maudhi mengi.”

Allah تعالى Aliwaambia waumini baada ya kuwasili Madinah kabla ya Badri alipokuwa akiwaliwaza kutokana na madhara yaliyowakuta kutoka kwa watu wa Kitabu na Washirikina; huku akiwataka wawe wasamehevu, wenye subira na msamaha mpaka Allah تعالى Atakapowapa faraja.

وَإِن تَصَبِرُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ ذَلِكَ مِن عَزْمِ الْأُمُورِ

“Na ikiwa mtasubiri na mkamchamungu basi hakika hayo ni katika mambo ya kuazimia”. (3:186)

Bukhari alipokea kutoka kwa Usamah bin Zayd رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alipanda juu ya Punda aliyetandikwa na alimbeba Usamah bin Zayd nyuma yake katika safari ya kumpa pole Sa'd bin Ubadah رضي الله عنه katika Kitongoji cha Bani Al-Harith bin Al-Khazraj, na hili lilijiri kabla ya vita vya Badri. Mtume ﷺ aliupita mkusanyiko ambamo Abdullah bin Ubbay bin Salul alikuwa mmoja wao, kabla Abdullah bin Ubayy kuwa Muislamu. Mjumuiko huo ulikuwa na Waislamu mbalimbali, bali pia washirikina, waliokuwa wakiabudia masanamu na baadhi ya Mayahudi. Pia Abdullah bin Rawahah رضي الله عنه alijumuika nao. Mtume ﷺ alipomfikia Abdullah bin Ubayy, Punda alitifua vumbi likawaangukia kile kikundi. Abdullah bin Ubayy aliziba pua yake kwa kilemba chake na akasema, 'Usitutumilie vumbi.' Mtume ﷺ aliwatolea salamu, akawalingania kumkubali Allah تعالى na aliwasomea baadhi ya Aya za Qur'an. Abdullah bin Ubayy alitamka kumuambia, 'Ewe Bwana! Hapana hotuba nzuri kuliko hiyo kama unalosema ni kweli. Hata hivyo usitughasi katika majilisi yetu. Rejea masikani kwako, yeyote atakayekujia, msimulie ngano zako,' Abdullah bin Rawahah رضي الله عنه alisema, 'Ewe Mjumbe wa Allah junge na kikao chetu kwani tunaridhia hilo.' Waislamu, washirikina na Mayahudi walifokeana na wakafikia hali ya kutaka kupigana. Mtume ﷺ aliendelea kuwanyamazisha mpaka akafanikiwa kuwatuliza.

Mtume ﷺ aliondoka akiwa juu ya Punda wake na alifika kwa Sa'd bin Ubadah رضي الله عنه, na kumuambia, 'Ewe Sa'd! Je umesikia maneno aliyosema Abu

Hubbab (Abdullah bin Ubayy)? Amesema kadha wa kadha! Sa'd رضي الله عنه akajibu, 'Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Msamehe na mvumilie. Naapa kwa Allah تعالى Aliyekuteremshia Kitabu, Allah تعالى Ametuletea ukweli kupitia kwako wakati watu wa mji huu walikaribia kumteua kuwa Mfalme. Allah تعالى Aliyabadilisha yote hayo kwa ukweli Aliokupa. Likamghadhibisha sana na hii ndio sababu ya kuwa na hali hiyo uliyomuona nayo." Mtume ﷺ alimsamehe. Kwa hakika Mtume ﷺ na Masahaba zake walikuwa wakiwasamehe washirikina na watu wa Kitabu, kama Allah تعالى Alivyowaamrisha, na walikuwa wakivumilia madhara waliyoyapata. Allah تعالى Amesema,

وَلَتَسْمَعَنَّ مِنَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِن قَبْلِكُمْ وَمِنَ الَّذِينَ أَشْرَكُوا أَذًى كَثِيرًا

"Na bila ya shaka yoyote mtasikia udhia mwingi kutokana na waliopewa Kitabu kabla yenu na washirikina." (3:186)

Na Allah تعالى Amesema,

وَدَّ كَثِيرٌ مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَوْ يَرُدُّونَكُمْ مِن بَعْدِ إِيمَانِكُمْ كُفَّارًا حَسَدًا مِّنْ عِنْدِ
أَنْفُسِهِمْ مِّنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمُ الْحَقُّ فَاعْفُوا وَاصْفَحُوا حَتَّىٰ يَأْتِيَ اللَّهُ بِأَمْرِهِ

"Wengi miongoni mwa watu wa Kitabu wanatamani lau wange kurudisheni nyinyi muwe makafiri baada ya kuamini kwenu, kwa ajili ya uhasidi uliomo ndani ya nafsi zao, baada ya kwisha wapambanukia Haki. Basi sameheni na wachilieni mbali mpaka Mwenyezi Mungu Atapoleta Amri Yake."

Mtume aliendelea kuwasamehe makafiri kama alivyoamrisha na Allah تعالى mpaka Allah تعالى Alipomuamuru kuwapiga (Makafiri). Mtume ﷺ alipopigana vita vya Badri, na Allah تعالى Akawaua kwa mkono wake, Vigogo wa makafiri wa Kiquraish, Abdullah bin Ubayy bin Salul na washirikina wanaoabudu masanamu waliokuwa naye walisema, 'Kadhia hii imeshinda, na wakamfuata Mtume ﷺ na wakashilimu."¹ Kwa hiyo, kila mtu anayesimamia ukweli anaamrisha mema na kukataza maovu atapata misukosuko. Katika hali hizo hakuna jambo bora zaidi ya kuwa na subira katika njia ya Allah تعالى, kumuamini Yeye, na kurejea Kwake.

¹ Bukhari 4566 na Muslim 1798.

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ فَنَبَذُوهُ وَرَاءَ ظُهُورِهِمْ وَأَشْرَوْا بِهِ مِمَّا قَلِيلًا ۗ فَبِئْسَ مَا يَشْتَرُونَ ﴿١٨٧﴾ لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَفْرَحُونَ بِمَا أُوتُوا وَيُحِبُّونَ أَنْ يُحْمَدُوا بِمَا لَمْ يَفْعَلُوا فَلَا تَحْسَبَنَّهُمْ بِمَفَازَةٍ مِنَ الْعَذَابِ ۗ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٨٨﴾

وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٨٩﴾

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٩٠﴾ الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَذَا بَطْلًا سُبْحَانَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٩١﴾ رَبَّنَا إِنَّكَ مَن تُدْخِلِ النَّارَ فَقَدْ أَخْرَجْتَهُ ۗ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن أَنْصَارٍ ﴿١٩٢﴾ رَبَّنَا إِنَّا سَمِعْنَا مُنَادِيًا يُنَادِي لِلْإِيمَانِ أَنْ ءَامِنُوا بِرَبِّكُمْ فَآمَنَّا ۗ رَبَّنَا فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَكَفِّرْ عَنَّا سَيِّئَاتِنَا وَتَوَفَّنَا مَعَ الْأَبْرَارِ ﴿١٩٣﴾ رَبَّنَا وَءَاتِنَا مَا وَعَدْتَنَا عَلَىٰ رُسُلِكَ وَلَا تُخْزِنَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ إِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْوَعْدَ ﴿١٩٤﴾ فَاسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ أَنِّي لَا أُضِيعُ عَمَلَ عَمَلٍ مِّنْكُمْ مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ ۗ بَعْضُكُمْ مِّنْ بَعْضٍ ۗ فَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَأُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأُودُوا فِي سَبِيلِي وَقُتِلُوا وَقُتِلُوا لَأَكْفِرَنَّ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَأُدْخِلَنَّهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرَىٰ مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ ثَوَابًا مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْنُ الثَّوَابِ ﴿١٩٥﴾

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْتُمُونَهُ فَنَبَذُوهُ وَرَاءَ ظُهُورِهِمْ وَأَشْرَوْا بِهِ مِمَّا قَلِيلًا ۗ فَبِئْسَ مَا يَشْتَرُونَ ﴿١٨٧﴾ لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَفْرَحُونَ بِمَا أُوتُوا وَيُحِبُّونَ أَنْ يُحْمَدُوا بِمَا لَمْ يَفْعَلُوا فَلَا تَحْسَبَنَّهُمْ بِمَفَازَةٍ مِنَ الْعَذَابِ ۗ وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١٨٨﴾

وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿١٨٩﴾

187. Na pale Mwenyezi Mungu Alipofungamana na waliopewa Kitabu kuwa: Lazima mtawabainishia watu, wala hamtokificha, walikitupa nyuma ya migongo yao, na wakanunua kwacho thamani duni. Basi ni kiovu hicho walichonunua.

188. Usiwadhania kabisa wale wanaofurahia waliyoyafanya, na wakapenda kusifiwa kwa wasiyo-yatenda, usiwadhania kuwa watasalimika na adhabu. Yao wao ni adhabu chungu.

189. Na Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.

Shutuma kwa watu wa Kitabu juu ya Kuvunja Ahadi na kuficha Ukweli

Katika Ayah hii, Allah تعالى Anawashutumu watu wa Kitabu, ambao alichukua ahadi kwao kwa kauli ya Mitume wao, kuwa watamuamini Muhammad ﷺ na kumuelezea kwa watu ili wamtambue na wamfuate atakapotumwa. Hata hivyo walificha ukweli huu na wakakhitari faida na mafanikio machache badala ya malipo ya hapa duniani na Akhera waliyoahidiwa. Huku ni kupoteza muamala na ni biashara mbovu. Aidha Aya hizi zinawaonya wanazuoni wasiige tabia zao, ili wasikhasirike na kuwa kama wao. Kwa hiyo, wanazuoni wanatakiwa kueneza elimu yenye manufaa waliyonayo wakishajiisha amali zilizo njema. Pia wanatahadharishwa dhidi ya kuficha sehemu ya elimu yao. Hadithi inaeleza kuwa Mtume ﷺ amesema.

«مَنْ سئِلَ عَنْ عِلْمٍ فَكْتَمَهُ، أَلْجِمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِلِجَامٍ مِنْ نَارٍ»

“Mwenye kuuulizwa juu ya elimu, akaficha atafungwa lijamu ya moto siku ya kiama.”¹

Shutuma kwa watu wa Kitabu Juu ya Udanganyifu wao na Kupenda Kusifiwa kwa Yale ambayo Hawakuyatenda.

Kauli ya Allah تعالى،

لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَفْرَحُونَ بِمَا أَتَوْا وَيُحِبُّونَ أَنْ يُحْمَدُوا بِمَا لَمْ يَفْعَلُوا

“Usiwadhanie kabisa wale wanaofurahia waliyoyafanya, na wakapenda kusifiwa kwa wasiyoyatenda.”

Inawahusu wale wanaojionesha, kujisifia na kudai kufanya wasiyoyafanya. Sahihi mbili zimeandika kuwa Mtume ﷺ alisema،

«الْمُتَسَبِّعُ بِمَا لَمْ يُعْطَ، كَلَّاسِ تَوْبِي زُورٍ»

“Mtu atakayejipamba na sifa asizokuwa nazo, mfano wake ni kama mtu aliyevaa nguo mbili za uongo.”²

¹At - Tabarany 8:401.

²Muslim Na. 2129.

Sahih pia imeandika,

«مَنْ ادَّعَى دَعْوَةَ كَاذِبَةٍ لِيَتَكْتَرَّ بِهَا، لَمْ يَزِدْهُ اللهُ إِلَّا قِلَّةً»

*"Mtu yeyote anayejivisha sifa za uongo, ili apate kujinufaisha, Allah hatamzidishia isipokuwa kuwa duni."*¹

Imam Ahmad alipokea kuwa Marwan alimuambia mlinzi wake Rafi aende kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na amuambie; "Endapo kuna mtu miongoni mwetu anafurahia alichofanya na anapenda kusifiwa kwa lile ambalo hakulifanya atapewa adhabu kali, basi sote tutaadhibiwa vikali." Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Aya hii iliteremshwa kuhusu watu wa Kitabu."

Kisha alisoma Aya ifuatavyo:-

وَإِذْ أَخَذَ اللَّهُ مِيثَاقَ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ لَتُبَيِّنُنَّهُ لِلنَّاسِ وَلَا تَكْفُمُونَهُ فَنَبَذُوهُ وَرَاءَ ظُهُورِهِمْ وَأَشْرَتُوا بِهِمْ مِمَّا قَلِيلًا فَيَتَسَّ مَا يَشْتَرُونَ ﴿١٨٧﴾

"Na pale Mwenyezi Mungu Alipofungamana na waliopewa Kitabu kuwa: Lazima mtawabainishia watu, wala hamtokificha, walikitupa nyuma ya migongo yao, na wakanunua kwacho thamani duni. Basi ni kiovu hicho walichonunua."

Kisha Ibn Abbas رضي الله عنهما akasoma,

لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَفْرَحُونَ بِمَا أَتَوْا وَمُحِبُّونَ أَنْ تُحْمَدُوا بِمَا لَمْ يَفْعَلُوا

"Usiwadhania kabisa wale wanaofurahia waliyoyafanya, na wakapenda kusifiwa kwa wasiyoyatenda." (3:188)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Mtume ﷺ aliwauliza kuhusu jambo, na wakamficha ukweli wake, na wakampa jibu lisilo sahihi.

Waliondoka baada ya kujikoga na kufurahia mbele yake kwa sababu walimjibu, hivyo walijifanya wamefarijika kwa kumficha ukweli aliotaka kuufahamu."²

¹ Bukhari 6105, 6652 na Muslim 1:104.

² Ahmad 1:298.

Hadithi hii imepokelewa na Bukhari,¹ Muslim,² At-Tirmidhy,³ na An-Nasa'i.⁴ Hadithi hii ilipokelewa kutoka kwa Abu Said Al-Khudry رضي الله عنه, alisema, "Katika zama za Mtume ﷺ, wakati Mjumbe ﷺ alipokwenda vitani, baadhi ya wanafiki walibaki nyumbani na wakafurahia kutofuatana na Mtume ﷺ vitani. Mtume ﷺ aliporudi kutoka vitani walimuomba radhi na kuapa kuwa walikuwa na nyudhuru na wakataka wasifiwe kwa lile walilolifanya.

Hivyo Allah تعالى Aliteremsha,

لَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ يَفْرَحُونَ بِمَا أَتَوْا وَيُحِبُّونَ أَنْ يُحْمَدُوا بِمَا لَمْ يَفْعَلُوا

"Usiwadhania kabisa wale wanaofurahia waliyoyafanya, na wakapenda kusifiwa kwa wasiyoyatenda."

Mpaka mwisho wa Aya. Na Muslim alipokea Hadithi sawa na hiyo.⁵ Allah تعالى Amesema,

فَلَا تَحْسَبَنَّاهُمْ بِمَفَازَةٍ مِنَ الْعَذَابِ

"Usiwadhania kuwa watasalimika na adhabu."

وَلَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

"Yao wao ni adhabu chungu."

Kisha Allah تعالى Amesema:

وَلِلَّهِ مُلْكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

"Na Ufalme wa mbingu na ardhi ni wa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu."

Yeye ni Mmiliki wa kila kitu, Ana Uwezo wa Kutenda kila Akitakacho hapana kinachoweza kuepa Uwezo Wake. Hivyo, mcheni Yeye, wala msikengeuke na jihadharini na Ghadhabu na Kisasi Chake. Yeye ni Mkuu kabisa, hakuna mkuu zaidi Yake, na Yeye ni Muweza wa yote, hakuna muweza zaidi Yake.

¹ Fat'hul Bari 8:81

² Muslim 8.:2143

³ Tuhfat ul Al-Ahwadhi 8:66.

⁴ An-Nasai katika Al-Kubra 6:318

⁵ Bukhari 4567 na Muslim 2777

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٨٧﴾
 الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ
 رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَذَا بَطْلًا سُبْحَانَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٨٨﴾ رَبَّنَا إِنَّكَ مَن تُدْخِلِ النَّارَ
 فَقَدْ أَخْرَجْتَهُ ط وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن أَنْصَارٍ ﴿١٨٩﴾ رَبَّنَا إِنَّنا سَمِعنا مُنَادِيًا يُنَادِي لِلْإِيمَانِ أَنْ
 ءَامِنُوا بِرَبِّكُمْ فَآمَنَّا ؕ رَبَّنَا فَاغْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا وَكَفِّرْ عَنَّا سَيِّئَاتِنَا وَتَوَفَّنَا مَعَ الْأَبْرَارِ ﴿١٩٠﴾
 رَبَّنَا وَإِنَّا مَآ وَعَدْتُنَا عَلَىٰ رُسُلِكَ وَلَا نَجْزِيكَ يَوْمَ الْقِيَمَةِ إِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْوَعْدَ ﴿١٩١﴾

190. Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili,

191. Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto.

192. Mola wetu Mlezi! Hakika Unayemtia Motoni umemdhaliisha; na waliodhulumu hawana wasaidizi.

193. Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumemsikia mwenye kuita anatuitia katika Imani kwamba: Muaminini Mola wenu Mlezi; nasi tukaamini. Basi tusamehe madhambi yetu, na Utufutie makosa yetu, na Utufishe pamoja na watu wema.

194. Mola wetu Mlezi! Na Utupe Uliyotuahidi kwa Mitume wako, wala Usitudhalishe Siku ya Kiyama. Hakika Wewe Huvunji miadi.

Dalili za Tauhid kwa Watu Wenye Akili, Sifa Zao, Kauli Zao na Dua Zao.

Allah تعالى Amesema,

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi.” (3:190)

Inahusu mbingu, kuinuka kwake na upana wake mkubwa, ardhi na ukubwa wa eneo lake na uzito wake, na sura za kustaajabisha za sayari zinazozunguka,

bahari, milima, majangwa, miti, mimea, matunda, wanyama, vyuma na vitu vingine venye faida kama vile rangi, harufu, ladha na chembe za asili

وَأَخْتَلَفَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ

“Na kukhitalifiana usiku na mchana.” (3:190)

Vikipishana kwa urefu, kwa mfano, baadhi ya wakati, mmoja wao huwa mrefu kuliko mwingine, au mfupi kuliko mwingine na hulingana wakati mwingine, na hali hiyo hujirejea kila mara, na yote haya hujiri kwa ridhaa ya Allah تعالى, Mwingi wa Hikima. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema

لَا يَسْتَلِ الْأُولَى الْأُخْرَى ۗ

“Ziko Ishara kwa wenye akili.” Inahusu wenye uwezo wa kufikiri na akili timamu ambao wanatafakari juu ya ukweli wa mambo, na sio kama viziwi na mabubu ambao hawana uelewa. Allah تعالى Aliwazungumzia kama ifuatavyo:-

وَكَايْنٍ مِّنْ آيَاتٍ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَمُرُونَ عَلَيْهَا وَهُمْ عَنْهَا مُعْرِضُونَ ۗ وَمَا

يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُشْرِكُونَ ۗ

“Na ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipitia, na hali ya kuwa wanazipuuzwa. Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina.” (12:105-106)

Kisha Allah تعالى Anawaelezea wale wenye akili nzuri. Kwa Kusema,

الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ

“Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala.” (3:191)

Kama ilivyothibiti katika sahihi Bukhari kutoka kwa Imrani bin Huswain رضي الله عنه, kwamba Mtume ﷺ amesema:

«صَلِّ قَائِمًا، فَإِنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَقَاعِدًا، فَإِنْ لَمْ تَسْتَطِعْ فَعَلَىٰ جَنْبٍ»

“Swali ukiwa umesimama, na ikiwa huwezi, swali ukiwa umekaa, kama huwezi, ukiwa umelala kwa ubavu.”¹

¹ Fat’hul Al-Bari 2:684.

Watu hawa humkumbuka Allah تعالى katika hali zote, katika mioyo yao, kauli, dhamira na ndimi zao.

وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Na hufikiri katika kuumbwa mbingu na ardhi...” (3:191)

Wanafahamu yaliyomo mbinguni na ardhini katika hekima zinazothibitisha Nguvu za Muumba, Uwezo, Elimu, Hikima, Utashi na Huruma Yake.

Allah تعالى Anashutumu wale wasiotafakari kuhusu Uumbaji Wake, ambao ni ushahidi wa kuwepo Kwake, Sifa Zake, Shariah, Kanuni Zake na ishara Zake.

Allah تعالى Amesema,

وَكَايِنٍ مِّنْ آيَاتٍ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَمُرُّونَ عَلَيْهَا وَهُمْ عَنْهَا مُعْرِضُونَ ﴿١٩١﴾ وَمَا يُؤْمِنُ أَكْثَرُهُمْ بِاللَّهِ إِلَّا وَهُمْ مُّشْرِكُونَ ﴿١٩٢﴾

“Na ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipitia, na hali ya kuwa wanazipuuza. Na wengi katika wao hawamuamini Mwenyezi Mungu pasina kuwa ni washirikina”. (12:105-106)

Kisha Allah تعالى Anawasifu waja Wake wenye akili. Amesema:

الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi”.

Wakiomba dua kwa kusema,

رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَذَا بَطْلًا

“Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure”.

Hukuviumba viumbe hivi kwa masikhara au kwa mchezo. Bali, Uliwaumba kwa ukweli, ili Kuwalipa wafanyao maovu, na kuwajazi wanaotenda amali njema kwa malipo yaliyo bora.

Kisha Waumini wa kweli humtakasa Allah na kukanusha kuwa hufanya jambo kwa mzaha na bila malengo kwa kusema,

سُبْحَانَكَ

“Umetakasika!”

Maana yake: Huwezi Kuumba kitu bila kusudi maalumu.

فَقِنَّا عَذَابَ النَّارِ

“Basi tukinge na adhabu ya Moto.”

Maana yake: “Ewe Uliyeumba viumbe kwa ukweli na haki, Ambaye Huna upungufu, au Kufanya mambo bila lengo maalumu, tuokoe kutokana na mateso ya Moto kwa Uweza Wako na Nguvu Zako. Tuongoze kufanya amali njema Unazoziridhia, ambazo kwazo Utatuingiza Pepo inayofurahisha na Utuokoe kutokana na adhabu yako kali.”

Baadae waliomba Dua, wakisema:

رَبَّنَا إِنَّكَ مَن تَدْخِلِ النَّارَ فَقَدْ أَخْرَجْتَهُ

“Mola wetu Mlezi! Hakika Unayemtia Motoni Umemdhalilisha”.

Kwa Kumfedhehesha na Kumnyongesha mbele ya watu siku ya Kiyama.

وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن أَنْصَارٍ

“Na waliodhulumu hawana wasaidizi.”

Katika siku ya Kiyama, hakuna wa kuwaokoa na adhabu Yako. Kwa hiyo hapana wa kukwepa Uliloliamua juu yao.

رَبَّنَا إِنَّنَا سَمِعْنَا مُنَادِيًا يُنَادِي لِلْإِيمَانِ

“Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tumemsikia mwenye kuita akiitia Imani”.

Mlinganiaji kwenye Imani, maana Mtume ﷺ,

أَن ءَامِنُوا بِرَبِّكُمْ فَآمَنَّا

“Kwamba: Muaminini Mola wenu Mlezi; nasi tukaamini”.

Maana anasema, Muaminini Mola wenu, tukaamini. Kwa maana: Tuliitikia wito wake na tukamfuata,

رَبَّنَا فَاعْفِرْ لَنَا ذُنُوبَنَا

“Ewe Mola wetu, basi tusamehe madhambi yetu.”

Tusamehe dhambi zetu kutokana na imani yetu na kumtii Mtume Wako

وَكَفِّرْ عَنَّا سَيِّئَاتِنَا

“Na Utufutie makosa yetu.” Yale yaliyo baina yetu na wewe.

وَتَوْفِنَا مَعَ الْأَبْرَارِ ﴿١٨٧﴾

“Na Utufishe pamoja na watu wema.” Tujumuishe na watu wema.

رَبَّنَا وَإِنَّا مَا وَعَدْتَنَا عَلَىٰ رُسُلِكَ

“Mola wetu Mlezi! Na Utupe Uliyotuahidi kwa Mitume wako.”

Kwa kuwaamini Mitume wako. Au maana yake ni, tupe Uliyotuahidi kupitia kauli za Mitume yako. Na maana hii ndiyo dhahiri zaidi.

وَلَا تُخْزِنَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Wala usituhizi Siku ya Kiyama.” Mbele ya viumbe wote.

إِنَّكَ لَا تُخْلِفُ الْوَعْدَ ﴿١٨٨﴾

“Hakika Wewe huvunji miadi.”

Kwa hakika, Ahadi Uliyotoa kwa Mitume wako, ikiwa ni pamoja nasi kufufuliwa na kusimama mbele Yako, hakika bila ya shaka itatimia. Ilikuwa ada ya Mtume ﷺ kusoma Aya kumi za mwisho za Surah Al-Imrani katika *Qiyamu Layli (Tahajjud)*. Bukhari alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, ‘Usiku mmoja nililala nyumbani kwa shangazi yangu Maimuna, Mtume ﷺ alizungumza na mkewe kwa muda, kisha akaenda kulala. Ilipofika theluthi ya usiku, alisimama, akaangalia mbinguni na kusoma,

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٨٩﴾

“Hakika katika Kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili.”

Kisha Mtume ﷺ alisimama, akatawadha, akapiga mswaki akaswali rakaa kumi na moja. Bilal رضي الله عنه alipomaliza kuadhini, Mtume ﷺ aliswali rakaa mbili, akatoka kwenda Msikitini na kuswalisha swala ya Subhi.¹

Hadithi hii pia ameipokea Muslim.² Ibn Marduwayhi رحمه الله تعالى alipokea kuwa 'Ata alisema, "mimi, Ibn Umar na Ubay bin Umayr tulikwenda kwa Mama Aisha رضي الله عنها tukaingia chumbani kwake, kati yetu na yeye kulikuwa na pazia, akasema, "Ewe Ubayd! Kwa nini hututembelei? Akamjibu, "Mshairi alisema, "Zuru kwa nafasi utapendwa zaidi." Ibn Umar رضي الله عنهما aliulizwa, "Tueleze jambo ambalo halikuwa la kawaida ulilolishuhudia kwa Mtume ﷺ." Alilia na kusema, "Mambo yake yote yalikuwa ya kushangaza. Usiku mmoja alinisogelea mpaka ngozi yake ikagusana na yangu akasema, 'Ngoja nimuabudu Mola wangu.' Nikasema, 'Wallahi! Napenda kuwa karibu yako. Pia Napenda unavyomuabudu Mola wako! Alitumia kiriba cha maji kutawadhia, lakini hakutumia maji mengi. Alisimama kuswali na alilia mpaka ndevu zake ziliroa kwa machozi. Alisujudu na alilia mpaka ardhi ikaroa machozi. Kisha alilala ubavu akalia. Bilali alipokuja kumuamsha swala ya Asubuhi, alimuuliza, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Kinakuliza nini, na Allah تعالى Amekusamehe dhambi zako zilizopita na zijazo?" Mtume ﷺ akamjibu,

«وَيُحَاكُّ يَا بِلَالُ، وَمَا يَمْنَعُنِي أَنْ أَبْكِي، وَقَدْ أَنْزَلَ عَلَيَّ فِي هَذِهِ اللَّيْلَةِ»

'Ewe Bilal! nini kitanizuia kulia wakati usiku wa leo nimeteremshiwa Aya hii.'

إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَأَخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٩٠﴾

"Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili." (3:190)

Kisha akasema,

«وَيُنِيلُ لِمَنْ قَرَأَهَا وَلَمْ يَتَفَكَّرْ فِيهَا»

"Ole wao wanaoisoma bila mazingatio ndani yake."³

¹ Fat'hul Al-Bari 8:83.

² 1:134 Muslim 1:530.

³ Ibn Hibban (620).

فَأَسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ أَنِّي لَا أُضِيعُ عَمَلَ عَمَلٍ مِّنْكُمْ مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْتِىٰٓ بِعَعْضِكُمْ مِّنْ بَعْضٍ
 فَأَلَّذِينَ هَاجَرُوا وَأُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ وَأُوذُوا فِي سَبِيلِي وَقَاتَلُوا وَقُتِلُوا لَأُكَفِّرَنَّ عَنْهُمْ
 سَيِّئَاتِهِمْ وَلَأُدْخِلَنَّهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ نَوَآبًا مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْنُ

التَّوَابِ ﴿١٩٥﴾

195. "Mola Mlezi wao, Akayakubali maombi yao Akajibu: Hakika Sipotezi matendo ya mtendaji miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke, kwani ni nyinyi kwa nyinyi. Basi waliohama, na waliotolewa makwao, na wakateswa katika njia Yangu, na wakapigana, na wakauliwa, kwa yakini Mimi Nitawafutia makosa yao, na kwa yakini Nitawaingiza katika bustani zinazopita mito kati yake. Hayo ndiyo malipo yanayotoka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Kwake yapo malipo mema kabisa."

Allah تعالى Hujibu Dua za Watu Wenye Akili

Allah تعالى Amesema,

فَأَسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ

"Mola Mlezi wao, Akayakubali maombi yao akajibu."

Alipokea maombi yao. Said bin Mansur alipokea kutoka kwa Salamah رضي الله عنها, mtu miongoni mwa watu wa ukoo wa Ummu Salamah رضي الله عنها alisema, "Ummu Salamah رضي الله عنها alisema, Ewe Mjumbe wa Allah! Allah تعالى Hajawataja wanawake kuhusiana na Hijrah.' Allah تعالى Akateremsha Aya hii,

فَأَسْتَجَابَ لَهُمْ رَبُّهُمْ أَنِّي لَا أُضِيعُ عَمَلَ عَمَلٍ مِّنْكُمْ مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْتِىٰٓ

"Mola Mlezi wao, Akayakubali maombi yao Akajibu: Hakika Sipotezi matendo ya mtendaji miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke."

Ansar wanataja kuwa, 'Ummu Salamah رضي الله عنها ni mwanamke wa kwanza kuhamia kwao."¹ Al-Hakim alikusanya Hadithi hii katika *Mustadrak*² wake na

¹Said Bin Mansur 3:1136.

²Al-Hakim 2:300.

akasema, “Ni sahihi kwa sharti ya Al-Bukhari lakin *Shaikhani* (Bukhari na Muslim hawakuikusanya.” Kauli ya Allah تعالى،

أَنْتَى لَا أُضِيعُ عَمَلَ عَمَلٍ مِّنْكُمْ مِّنْ ذَكَرٍ أَوْ أَنْتَى

“Hakika Sipotezi matendo ya mtendaji miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke.”

Inaelezea jibu walilopewa na Allah تعالى kuwa hapana amali ya mja itakayopotea. Bali, Atamlipa kwa ukamilifu kila mmoja kwa mujibu wa amali zake. Kauli Yake،

بَعْضُكُمْ مِّنْ بَعْضٍ ط

“Kwani ni nyinyi kwa nyinyi.”

Maana yake: Nyote nyinyi katika kulipwa thawabu Zangu mpo sawa.

فَالَّذِينَ هَاجَرُوا

“Basi waliohama.”

Kwa kuhama ardhi ya shirki na kwenda Ardhi ya Imani na kuwaacha nyuma wapenzi wao, ndugu na majirani،

وَأُخْرِجُوا مِنْ دِيَارِهِمْ

“Na waliotolewa makwao.”

Wakati washirikina walipowatesa na kuwalazimisha kuhama miji yao, ndio maana Akasema،

وَأُودُوا فِي سَبِيلِي

“Na wakateswa katika Njia Yangu.”

Kosa lao kubwa mble ya watu, ni kwa kuwa walimuamini Allah تعالى Pekee. Katika Aya sawa na hiyo, Allah تعالى Amesema،

مُخْرِجُونَ الرُّسُولَ وَإِيَّاكُمْ أَنْ تَتُومِنُوا بِاللَّهِ رَبِّكُمْ

“Wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu mnamuamini Mwenyezi Mungu.” (60:1)

Na Allah تعالى Amesema,

وَمَا نَقَمُوا مِنْهُمْ إِلَّا أَنْ يُؤْمِنُوا بِاللَّهِ الْعَزِيزِ الْحَمِيدِ ﴿٨٥﴾

“Na hawakuona baya lolote kwao ila kuwa wakimuamini Mwenyezi Mungu, Mwenye Nguvu, Msifiwa.” (85:8)

Kauli ya Allah تعالى,

وَقَاتِلُوا وَقَاتِلُوا

“Na wakapigana, na wakauliwa.” (3:195)

Inahusu walio daraja la juu katika waja, ni yule anayepigana kwa ajili ya Allah تعالى na anakufa katika harakati huku uso wake ukiwa umefunikwa na damu na mavumbi. Imelandikwa katika Sahihi kuwa mtu mmoja alisema,

يا رسول الله، أرايت إن قتلت في سبيل الله صابراً محتسباً مقبلاً غير مدبر، أيكفر الله عني خطاياي؟ قال: «نعم» ثم قال: «كيف قلت؟» فأعاد عليه ما قال، فقال: «نعم، إلا الدين، قاله لي جبريل أيضاً»

“Ewe Mjumbe wa Allah! Unaonaje kama nikiuawa katika njia ya Allah! Nikawa ni mwenye subira, mwenye kutarajia, nikishambulia, bila kurudi nyuma, Je Allah Atanisamehe madhambi yangu?” Mtume ﷺ akamjibu, ‘Ndiyo, isipokuwa mwenye deni, kwani Jibril ameniletea wahyi sasa hivi.’¹

Hii ndiyo sababu Allah تعالى Akasema,

لَا تُكْفِرَنَّ عَنْهُمْ سَيِّئَاتِهِمْ وَلَا أُدْخِلْنَهُمْ جَنَّةٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“Kwa yakini Mimi Nitawafutia makosa yao, na kwa yakini Nitawaingiza katika bustani yanayopita mito kati yake”. (3:195)

Ndani ya Pepo ambapo kuna mito ya vinywaji anuwai - maziwa, asali, mvinyo, na maji safi. Kuna vitu ambavyo jicho halijapata kuona, na hapana sikio lililosikia na hapana moyo uliopata kuwaza (vifurahishavyo Peponi).

¹ Muslim 3:1501

Kauli ya Allah تعالى،

ثَوَابًا مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ

“Hayo ndiyo malipo yanayotoka kwa Mwenyezi Mungu”.

Inathibitisha uwezo Wake, kwani Muweza na Mkuu, Hutoa jaza ya Kustaajibisha. Kauli ya Allah تعالى،

وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْنُ الثَّوَابِ ﴿١٩٥﴾

“Na Mwenyezi Mungu Kwake yapo malipo mema kabisa.” (3:195)

Kwa wale watendao amali njema.

* * *

لَا يَغُرُّكَ تَقَلُّبُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي الْبِلَدِ ۗ مَتَّعَ قَلِيلٌ ۗ
 ثُمَّ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ۗ لَكِنَّ الَّذِينَ اتَّقَوْا
 رَبَّهُمْ هُمْ جَنَّتْ حَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا
 نُزُلًا مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ ۗ وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ لِلْأَبْرَارِ ۗ وَإِن
 مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَمَا
 أُنزِلَ إِلَيْهِمْ خَشِعِينَ لِلَّهِ لَا يَشْتُرُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ نَمَنًا قَلِيلًا ۗ
 أُولَئِكَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ
 الْحِسَابِ ۗ يَتَأَيَّأُ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَصْبَرُوا وَصَابَرُوا
 وَرَابَطُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ۗ

لا يَغُرُّكَ تَقَلُّبُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي
 الْبِلَدِ ۗ مَتَّعَ قَلِيلٌ ثُمَّ مَأْوَاهُمْ
 جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ۗ لَكِنَّ
 الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ هُمْ جَنَّتْ حَجْرِي
 مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا
 نُزُلًا مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ ۗ وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ
 لِلْأَبْرَارِ ۗ

196. Kabisa kusikudanganye kubakia kutangatanga kwa walio kufuru katika nchi.

197. Hiyo ni starehe ndogo. Kisha makazi yao yatakuwa Jahannamu. Na ni mahali pabaya mno pa kupumzikia.

198. Lakini waliomcha Mola wao Mlezi watapata bustani zinazopita mito kati yake. Watadumu humo. Hayo ni makaribisho yao yatokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na vilioko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kwa watu wema.

Tahadhari Dhidi ya Kughurika Tabia za Wapenda Dunia na Kubainisha Malipo ya Waja Wema

Allah تعالیٰ Amesema, msiwahusudu makafiri, wanaofurahia maisha na kufaidi hapa duniani. Muda si mrefu watayapoteza yote hayo na watabaki na amali zao mbovu, kwa hakika Tunawapa muda ambao unawahadaa, ambapo,

مَتَّعَ قَلِيلٌ ثُمَّ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ الْمِهَادُ ۗ

“Hiyo ni starehe ndogo. Kisha makazi yao yatakuwa Jahannamu. Na ni mahali pabaya mno pa kupumzikia.” (3:197)

Aya hii ni sawa na Aya nyingine, isemayo:

مَا مَجْدُلٌ فِي آيَاتِ اللَّهِ إِلَّا الَّذِينَ كَفَرُوا فَلَا يَغْرُوكَ تَقَاتِيمٌ فِي الْبَلَدِ ﴿٤٠﴾

“Hawazibishi Ishara za Mwenyezi Mungu ila waliokufuru; basi kusikudanganye wewe kutangatanga kwao katika nchi.” (40:4)

قُلْ إِنَّ الَّذِينَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾ مَتَّعَ فِي الدُّنْيَا ثُمَّ

إِلَيْنَا مَرْجِعُهُمْ ثُمَّ نُذِيقُهُمُ الْعَذَابَ الشَّدِيدَ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ ﴿٧٠﴾

“Sema: Hao wanaomzulia uwongo Mwenyezi Mungu hawatafanikiwa. Hiyo ni starehe ya katika dunia tu, kisha marejeo yao ni Kwetu. Tena Tutawaonjesha adhabu kali kwa sababu ya kukufuru kwao.” (10:69-70)

Na Allah تعالی Amesema,

تُمتِعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٣١﴾

“Tunawastarehesha kwa uchache, kisha Tutawasukuma kwenye Adhabu ngumu.” (31:24)

Na Allah تعالی Amesema,

فَمَهْلٍ الْكَافِرِينَ أَمْهَلُهُمْ رُوْبَدًا ﴿٨٦﴾

“Basi wape muhula makafiri - wape muhula pole pole.” (86:17)

Maana yake: Kidogo kidogo. Na Allah تعالی Amesema,

أَفَمَنْ وَعَدْنَاهُ وَعْدًا حَسَنًا فَهُوَ لَاقِيهِ كَمَنْ مَتَّعْنَاهُ مَتَّعَةً ثُمَّ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ثُمَّ هُوَ يَوْمَ

الْقِيَامَةِ مِنَ الْمُحْضَرِينَ ﴿٦١﴾

“Je! Yule Tuliymuahidi ahadi nzuri, tena naye akayapata, ni kama Tuliymstarehesha kwa starehe za maisha ya duniani, na kisha Siku ya Kiyama akawa miongoni mwa wanaohudhurishwa?” (28:61)

Hali ndio hiyo, Allah تعالی Alivyomaliza Kutaja hali za Makafiri katika dunia, na Akataja mafikio yao Motoni, baada ya hapo Alisema,

لَيْكِنَ الَّذِينَ اتَّقَوْا رَبَّهُمْ هُمْ جَنَّتْ نَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا نُزُلًا مِّنْ عِنْدِ
اللَّهِ

“Lakini walio mcha Mola wao Mlezi watapata bustani zinazopita mito kati yake. Watadumu humo. Hayo ni makaribisho yao yatokayo kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Ni ukaribisho utokao kwa Allah تعالى kwa uhakika,

وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ لِّلْأَبْرَارِ ﴿١٩٦﴾

“Na vilioko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kwa watu wema.”

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alimnukuu Abu Ad - Dardai رضي الله عنه akinena, “Mauti ni bora kwa kila muumini. Mauti ni bora kwa kila kafiri, na wasionisadikisha basi wasome Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ لِّلْأَبْرَارِ ﴿١٩٦﴾

“Na vilioko kwa Mwenyezi Mungu ni bora kwa watu wema.”

Na Kauli Yake,

وَلَا يَحْسَبَنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّمَا نُمَلِّهِمْ خَيْرٌ لَّا أَنفُسِهِمْ إِنَّمَا نُمَلِّهِمْ لِيَزِدُوا إِيمَانًا وَهُمْ
عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿١٩٧﴾

“Wala wasidhani wale wanaokufuru kwamba huu muhula Tunao wapa ni kheri yao. Hakika Tunawapa muhula wazidi madhambi. Na yao wao ni adhabu ya kuwadhalilisha.” (3:178)¹

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْكُمْ وَمَا أُنزِلَ إِلَيْهِمْ خَشِيعَةً لِلَّهِ لَا
يَشْتَرُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا ۗ أُولَٰئِكَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ
الْحِسَابِ ﴿١٩٨﴾ يٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَصْبِرُوا وَصَابِرُوا وَرَابِطُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ
تُفْلِحُونَ ﴿١٩٩﴾

¹ At-Tabari 7:496 Isnadi yake ina dosari. Taz. “At-Tarikh Asswaghir” 2:173. Kadhalika Taz. “Al-Jarhuwattadi” 7:182.

199. Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu wapo wanaomuamini Mwenyezi Mungu na yaliyoteremshwa kwenu na yaliyoteremshwa kwao, wakimnyenyekea Mwenyezi Mungu. Hawabadili Aya za Mwenyezi Mungu kwa thamani duni. Hao wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.

200. Enyi mlioamini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa.

Mustakbali wa Baadhi ya watu wa Kitabu na Malipo Yao

Allah تعالى Anaelezea kuwa baadhi ya Watu wa Kitabu wanamuamini yeye kwa dhati na kwa yale aliyokuja nayo Muhammad ﷺ, Sanjari na kuamini yaliyomo ndani ya Vitabu Vitakatifu, na wanamtii Yeye na ni wanyenyekevu mbele ya Allah تعالى.

لَا يَشْتَرُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا

“Hawabadili Aya za Mwenyezi Mungu kwa thamani duni”. (3:199)

Kwani hawafichi yale wanayoyafahamu kuhusu ruwaza njema juu ya sifa bainifu za Muhammad ﷺ, Utume wake, na sifa bainifu za Ummah wake. Bila shaka, hawa ndiyo watu bora miongoni mwa Watu wa Kitabu, ima ni Mayahudi au Wakristo. Allah تعالى Amesema ndani ya Surat Al-Qasas,

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِهِمْ هُمْ بِهِ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٤﴾ وَإِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ قَالُوا ءَأَمَّا

بِهِ إِنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّنَا إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلِهِ مُسْلِمِينَ ﴿٥٥﴾ أُولَٰئِكَ يُؤْتَوْنَ أَجْرَهُمْ مَرَّتَيْنِ بِمَا

صَبَرُوا

“Wale Tuliowapa Kitabu kabla yake wanakiamini hiki. Na wanapo somewa wanasema: Tunaiamini. Hakika hii ni Haki inayotoka kwa Mola wetu Mlezi. Hakika sisi kabla yake tulikuwa ni Waislamu, tulionyenyekea. Basi hao watapewa ujira wao mara mbili kwa walivyovumilia”. (28:52 -54). Allah تعالى Amesema,

الَّذِينَ آتَيْنَاهُمُ الْكِتَابَ يَتْلُونَهُ حَقَّ تِلَاوَتِهِ أُولَٰئِكَ يُؤْمِنُونَ بِهِ

“Wale Tuliowapa Kitabu, wakakisoma kama ipasavyo kusomwa, hao ndio kweli wanakiamini.” (2:121)

Kisha Allah تعالى Akasema tena,

وَمِن قَوْمِ مُوسَىٰ أُمَّةٌ يَهْتَدُونَ بِالْحَقِّ وَبِهِ يَعْذِرُونَ ﴿١٩٦﴾

“Na katika kaumu ya Musa lipo kundi linaowaongoa watu kwa haki na kwa haki wanafanya uadilifu”. (7:159)

Na Allah تعالى Amesema,

لَيْسُوا سَوَاءً ۗ مِمَّنْ أَهْلِلِ الْكِتَابِ أُمَّةٌ قَائِمَةٌ يَتْلُونَ آيَاتِ اللَّهِ ۗ أَنَاءَ اللَّيْلِ وَهُمْ يَسْجُدُونَ ﴿١٩٧﴾

“Wote hao si sawa sawa. Miongoni mwa Watu wa Kitabu wamo watu waliosimama barabara, wanasoma Aya za Mwenyezi Mungu nyakati za usiku, na pia wanasujudu”. (3:113)

Na Allah تعالى Amesema,

قُلْ ءَامِنُوا بِهِ أَوْ لَا تُؤْمِنُوا ۗ إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِن قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ

لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا ﴿١٩٨﴾ وَيَقُولُونَ سُبْحٰنَ رَبِّنَا ۗ إِن كَانَ وَعْدَ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿١٩٩﴾ وَيَخِرُّونَ

لِلْأَذْقَانِ يَبْكُونَ وَيَزِيدُهُمْ خُشُوعًا ﴿٢٠٠﴾

“Sema: aminini au msiamini. Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake, wanaposomewa hii, huanguka kifudifudi wanasujudu. Na wanasema: Subhana Rabbina, Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika Ahadi ya Mola wetu Mlezi lazima itimizwe! Na huanguka kifudifudi na huku wanalia, na inawazidisha unyenyekevu.” (17:107 – 109)

Baadhi ya Mayahudi wanazo sifa hizi lakini ni wachache sana. Kwa mfano, Abdullah bin Salam na wanaofanana nae ambao hawazidi watu kumi, hao ndio walioamini katika viongozi wa Kiyahudi. Kwa upande wa Wakristo wengi wao wanaongoka na wanafata haki kama Alivyosema Allah تعالى,

* لَتَجِدَنَّ أَشَدَّ النَّاسِ عَدَاوَةً لِلَّذِينَ ءَامَنُوا ۗ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا ۗ وَلَتَجِدَنَّ

أَقْرَبَهُمْ مَّوَدَّةً لِلَّذِينَ ءَامَنُوا ۗ الَّذِينَ قَالُوا ۗ إِنَّا نَصْرِي

“Hakika utawakuta waliokuwa wakali zaidi kuliko watu wote katika uadui kwa walioamini ni Mayahudi na washirikina. Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanaosema: Sisi ni Manasara.” (5:82),

Mpaka Kauli Yake Allah تعالى،

فَأَثْبَهُمُ اللَّهُ بِمَا قَالُوا جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا

“Basi Mwenyezi Mungu Atawalipa, kwa yale waliyoyasema, Bustani zipitazo mito katikati yake; humo watadumu.” (5:85)

Na kwa kuzingatia hilo, katika Aya hii Allah تعالى Amesema,

أُولَئِكَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ

“Hao wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi.” (3:199)

Ja'far bin Abi Talib رضي الله عنه alipomsomea An-Najash, Mfalme wa Ethiopia akiwa pamoja na mapadri na makasisi, *Surat Maryam* (sura ya 19), wote walilia mpaka ndevu zao zikaroa machozi.¹

Sahih mbili zimeandika kuwa alipofariki dunia An-Najash. Mtume ﷺ aliwaarifu Masahaba juu ya msiba huo na akasema,

إِنَّ أَخَا لَكُمْ بِالْحَيْثَةِ قَدْ مَاتَ، فَصَلُّوا عَلَيْهِ

“Ndugu yenu huko Ethiopia amekufa, kwa hiyo basi mswalieni”.

Alitoka yeye na Maswahaba wakaenda jangwani akawapanga safu na wakamswalia.² Ibn Abi Najih alisimulia kutoka kwa Mujahid alisema kuwa,

وَأَنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ

“Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu.” (3:199)

Inawahusu waliosilimu katika *Ahlu Kitaab*.³ 'Abbad bin Mansur alisema kuwa alimuuliza Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

¹ Ibn Hisham 1:357.

² Fat'hul Al-Bari 7:230, Muslim 2:657.

³ At - Tabari 7:499.

وَأَنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ لَمَنْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ

“Hakika miongoni mwa Watu wa Kitabu aliyemuamini Mwenyezi Mungu”. (3:199)

Hassan رحمه الله تعالى alisema, “Hao ni Watu wa Kitabu waliokuwepo kabla ya kuja Muhammad ﷺ na waliukubali Uislamu. Allah تعالى Aliwalipa maradufu kwa imani waliokuwa nayo kabla ya Muhammad ﷺ na kwa kumuamini Muhammad ﷺ (baada ya kutumwa kuwa Mtume).” Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliziandika kauli zote mbili. Sahihi zimeandika kutoka kwa Abu Musa رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«ثَلَاثَةٌ يُؤْتَوْنَ أَجْرَهُمْ مَرَّتَيْنِ»

“Watu watatu watalipwa ujira wao maradufu.”¹

Akawataja miongoni mwao,

أَوْرَجُلٌ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ آمَنَ بِنَبِيِّهِ وَأَمَرَ بِي

“Miongoni mwao ni mtu katika watu wa Kitabu aliyemuamini Mjumbe wake na akaniamini mimi.”

Kauli ya Allah تعالى،

لَا يَشْتَرُونَ بِعَايَتِ اللَّهِ ثَمَنًا قَلِيلًا

“Hawabadili Aya za Mwenyezi Mungu kwa thamani duni.” (3:199)

Maana yake: Hawafichi elimu waliyo nayo, kama walivyofanya wale waliolaaniwa miongoni mwao. Bali wanatoa elimu kwa wengine bila ujira, na kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

أُولَئِكَ لَهُمْ أَجْرُهُمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ إِنَّ اللَّهَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿١٩٩﴾

“Hao wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu.” (3:199)

Mujahid alielezea Aya hii,

¹ Fat’hul Al-Bari 6:169 Muslim 1:134.

سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿١٩٩﴾

“Mwepesi wa kuhisabu.” (3:199)

Maana yake: Mwepesi wa kuhifadhi hesabu. Abuu Hatim رحمه الله تعالى ameipokea na wengineo.

Amri ya kuvumilia na Kudumu katika Ibada

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَصْبِرُوا وَصَابِرُوا وَرَابِطُوا

“Enyi mlioamini! Subirini, na shindaneni katika kusubiri.” (3:200)

Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, ‘Waumini wameamuriwa kuwa na subira katika Dini ambayo Allah تعالى Amewachagulia, yaani Uislamu. Hawaruhusiwi kuitelekeza katika wakati wa raha au wa shida, wa utulivu au wa maafa, mpaka watakapokufa katika Uislamu. Aidha wameamrisha kuvumilia dhidi ya maadui zao, wale wanaoficha ukweli kuhusu dini yao.”¹ Maelezo sawa na haya yametolewa na wanazuoni kadhaa miongoni mwa *Salaf*.

Ama kuhusu neno “*Murabata*” maana yake ni kudumu katika pahala pa ibada na kuvumilia. Aidha maana nyingine ni kusubiri Sala baada ya Sala. Kama Ibn Abbas, Sahl Bin Hunaif na Muhammad bin Ka'b Al-Qurazi na wengineo رضي الله عنهم walivyonenena. Ibn Hatim رحمه الله تعالى alikusanya Hadithi ambayo pia ilikusanywa na Muslim na An-Nasai kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alisema:

«أَلَا أُخْبِرُكُمْ بِمَا يَمْحُو اللَّهُ بِهِ الْخَطَايَا، وَيَرْفَعُ بِهِ الدَّرَجَاتِ؟ إِسْبَاغُ الرُّضُوءِ عَلَى الْمَكَارِهِ، وَكَثْرَةُ الْخُطَا إِلَى الْمَسَاجِدِ، وَانْتِظَارُ الصَّلَاةِ بَعْدَ الصَّلَاةِ، فَذَلِكَ الرِّبَاطُ، فَذَلِكَ الرِّبَاطُ، فَذَلِكَ الرِّبَاطُ»

“Je nikuhabarisheni ambayo kwayo Allah تعالى Hufuta madhambi na kupandisha daraja? Ni kueneza udhu katika kipindi cha shida na kupiga hatua nyingi kwenda Masjid, na kusubiri Sala baada ya Sala: kwani hii ndiyo Ribat yenu, hii ndiyo Ribat yenu, hii ndiyo Ribat yenu (kwa maana kuifunga nafsi katika utiifu).”²

¹ Muslim 1:219, An-Nasai 1:89.

² At-Twabari 7:502.

Aidha wanasema kuwa *Murabatah* kama ilivyo katika Aya hapo juu, muradi wake ni vita dhidi ya adui, na kutawala malindo ya nje ya Waislamu kwa kuwalinda na uvamizi wa maadui wasiingie maeneo ya Waislamu. Kuna Hadithi nyingi zinazohimiza *Murabata* na zinataja ujira wake.

Bukhari alipokea katika sahihi yake kutoka kwa Sahli bin Sa'd As-Saidi رضي الله عنه kwamba Mtume ﷺ alisema,

«رِبَاطُ يَوْمٍ فِي سَبِيلِ اللَّهِ خَيْرٌ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا عَلَيْهَا»

“Kujifunga Siku moja katika njia ya Allah تعالى ni bora kuliko maisha ya dunia na vilivyomo ndani yake.”¹

Muslim alipokea kutoka kwa Salman Al-Farisi رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«رِبَاطُ يَوْمٍ وَلَيْلَةٍ خَيْرٌ مِنْ صِيَامِ شَهْرٍ وَصِيَامِهِ، وَإِنْ مَاتَ جَرَى عَلَيْهِ عَمَلُهُ الَّذِي كَانَ يَغْمَلُهُ، وَأَجْرِي عَلَيْهِ رِزْقُهُ، وَأَمِنْ النَّفْسَانِ»

“Kujifunga siku moja katika njia ya Allah kwa mchana na usiku ni bora kuliko saumu mwezi mzima na kisimamo chake. Na mtu akifa katika hali hiyo, amali alizokuwa akizifanya zitaendelea kuongezwa katika hesabu yake, na ataendelea kupata riziki yake, na ataepushwa na adhabu ya kaburi.”²

Imamu Ahmad alipokea kutoka kwa Fadalab bin Ubaydi رضي الله عنه alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema.

«كُلُّ مَيِّتٍ يُخْتَمُ عَلَيْهِ عَمَلُهُ إِلَّا الَّذِي مَاتَ مُرَابِطًا فِي سَبِيلِ اللَّهِ، فَإِنَّهُ يُنْبِئُ لَهُ عَمَلُهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، وَبِأَمْرِ فِتْنَةِ الْقَبْرِ»

“Kila maiti, anahitimishwa amali zake, isipokuwa yule atakayekufa katika ithibati kwa ajili ya Allah, kwani matendo yake yataendelea kuongezeka mpaka siku ya Kiama, na atasalimika na fitina za kaburini.”³

¹ Muslim 1913.

² Ahmad 6:20.

³ Abu Dawud 3:20, Tahfat Al-Ahwadhi 5:249.

Hadithi hii ni sawa na iliyokusanywa na Abu Dawud na At-Tirmidhi, ambao wameitaja kuwa "Hasan Sahih."¹ Ibn Hibban naye aliikusanya Hadithi hii katika Sahih yake.

At-Tirmidhi alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«عَيْنَانِ لَا تَمْسُهُمَا النَّارُ: عَيْنٌ بَكَتْ مِنْ خَشْيَةِ اللَّهِ، وَعَيْنٌ بَاتَتْ تُحْرُسُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

"Macho mawili hayataguswa na Moto: Jicho lililolia kwa kumcha Allah na jicho lililokesha kufanya doria katika njia ya Allah."²

Bukhari aliandika kwenye sahihi yake kutoka kwa Abu Hurayra رضي الله عنه kuwa alisema Mtume ﷺ alisema,

«تَعِسَ عَبْدُ الدِّينَارِ وَعَبْدُ اللِّزَمِ وَعَبْدُ الخَمِيصَةِ، إِنْ أُعْطِيَ رَضِي، وَإِنْ لَمْ يُعْطَ سَخَطَ، تَعِسَ وَأَنْتَكَسَ، وَإِذَا شَبِكَ فَلَا انْتَمَسَ، طُوبَى لِعَبْدٍ آخِذٍ بِعِنَانِ قَرَسِيهِ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، أَشَعَتْ رَأْسُهُ، مُعَبَّرَةٌ قَدَمَاهُ، إِنْ كَانَ فِي الْحِرَاسَةِ كَانَ فِي الْحِرَاسَةِ، وَإِنْ كَانَ فِي السَّاقَةِ كَانَ فِي السَّاقَةِ، إِنْ اسْتَأْذَنَ لَمْ يُؤْذَنَ لَهُ، وَإِنْ سَمِعَ لَمْ يُسْمَعْ»

"Ameangamia mtumwa wa Dinari, na mtumwa wa Dirham au Khamisa (nguo): kwani anaridhia akipewa vitu hivyo, na anapokosa, anavunjika moyo. Mtu wa aina hiyo amehiliki na kuangamia, na anapochomwa na mwiba, hapati mtu wa kumchomoa. Pepo ni stahiki ya yule anayeshika hatamu za farasi wake, anajitahidi katika njia ya Allah, nywele zake zikiwa timtim na miguu yake imejaa vumbi: anapoteuliwa kuwa mlinzi mstari wa mbele anakuwa mlinzi mzuri, anaridhika na nafasi yake kwa roho nyeupe, na anapoteuliwa kuwa mlinzi wa nyuma (katika jeshi) huikubali nafasi hiyo kwa moyo mkunjufu; na aombapo ruhusa, hapewi, na anapomtakia uombezi mtu mwingine maombi yake hayakubaliwi."³

¹ Ibn Hibban 7:69.

² At-Tirmidhi 1639.

³ Bukhari Na. 2886.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alipokea kuwa Zayd bin Aslam alisema, Abu Ubaydah رضي الله عنه alimuandikia "Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه na akamdokezea kuwa Warumi walikuwa wakikusanya majeshi yao dhidi ya Waislamu. Umar رضي الله عنه alimjibu, "Ama baadu" Kwa hakika kwa matatizo na shida yoyote itakayompata muumini Allah تعالى baada yake ataleta faraja; na uzito mmoja hautashinda faraja mbili (*Fainna maal-usri yusra inna maal-usri yusra*) na kwa hakika katika kitabu Chake Allah تعالى Anasema,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَصْبِرُوا وَصَابِرُوا وَرَابِطُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٢٠٠﴾

"Enyi mliaoamini! Subirini, na shindaneni kusubiri, na kuweni macho, na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa." (3:200)¹

Al-Hafiz Ibn Asakir رحمه الله تعالى aliandika katika wasifu wa Abdullah ibn Al-Mubarak, kuwa Muhammad bin Ibrahim bin Abi Sukaina alisema, "Tulipokuwa Tarsus, Abdullah bin Al-Mubarak alinifanyia Imla shairi hili nilipokuwa namuaga. Alinituma nilipeleka shairi kwa Al-Fudhayl bin Iyad katika mwaka wa mia moja na sabiini katika riwaya nyingine mwaka mia moja na sabiini na saba akasema, 'Ewe unayefanya ibada, utatuona, utatanabahi kuwa mnafanya mzaha katika ibada. Yeyote atakayeleta shahidi kuwa shavu lake lina chozi, afahamu kuwa shingo zetu zimeloa damu yetu. Yeyote anaye wachosha farasi wake bila lengo lolote, ajue kuwa farasi wetu wamechoshwa vitani. Mnasikia harufu ya uturi ambao manukato yetu ni mmemeko wa mikuki na harufu ya vumbi la mahandaki (Vitani). Tulisimuliwa katika hotuba ya Mtume wetu ﷺ, na kauli za kweli zisizo na ghibiba. Vumbi linalotimuliwa na farasi wa Allah na linaloingia kwenye mianzi ya pua ya mtu haitajumuishwa na moshi wa moto mkali. Kitabu hiki cha Allah kinazungumza nasi kuwa shahidi si mtu aliyekufa, na ukweli uliomo ndani ya Kitabu cha Allah hauwezi kukanushwa." Nilikutana na Al-Fudayl bin Iyad ndani ya Msikiti Mtakatifu na nikamkabidhi barua. Alipoisoma, macho yake yalitoka machozi na akasema, 'Abu Abdur-Rahman (Abdullah bin Al-Mubarak), amesema kweli na amenipa ushauri wa dhati. Kisha akaniuliza, 'Je unaandika Hadithi?' Nilimjibu, 'Ndiyo' Akaniambia, 'Andika Hadithi hii iwe zawadi kwa kuniletea barua kutoka kwa Abdul-Rahman.' Kisha akanisomea kwa Imla. Mansur bin Al-Mutamir alitusimulia kuwa Abu Sahil

¹ At - Tabari 7:503.

alipokea kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa mtu mmoja aliuliza, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Nifundishe amali njema ambayo itanipa malipo sawa na mpiganaji Jihad katika njia ya Allah!' Mtume ﷺ akamuambia,

«هَلْ تَسْتَطِيعُ أَنْ تُصَلِّيَ فَلَا تُفْتَرُ، وَتَصُومَ فَلَا تُفْطِرُ؟»

"Unaweza kuswali mfululizo bila kuacha na kufunga bila kufungua?"

Yule mtu akasema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Simudu." Mtume ﷺ akamuambia,

«فَوَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَوْ طُوِّفَتْ ذَلِكَ مَا بَلَغْتَ الْمُجَاهِدِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، أَوْ مَا عَلِمْتَ أَنَّ فَرَسَ الْمُجَاهِدِ لَيْسَتْ فِي طَوْلِهِ، فَيُكْتَبُ لَهُ بِذَلِكَ الْحَسَنَاتُ»

"Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake!, lau ungeweza hilo, usingewafikia wapiganaji Jihadi katika njia ya Allah. Unajua kuwa farasi wa anayepigana Jihadi anamchumia Mmiliki wake thawabu madhali anaishi, kwa hiyo anaandikiwa mema"¹

Allah تعالى Akasema baadae:

وَاتَّقُوا اللَّهَ

"...na mcheni Mwenyezi Mungu..." (3:200)

Kuhusu mambo yake yote na hali zote. Kwa mfano Mtume ﷺ alimuambia Muadh عنه رضي الله alipomtuma Yemen,

«إِنِّي اللَّهُ حَيْثُمَا كُنْتُ، وَأَتَّبِعِ السَّيِّئَةَ الْحَسَنَةَ تَمَحُّهَا، وَخَالِيَ النَّاسَ بِخُلُقِي حَسَنٍ»

"Mche Allah popote utakapokuwa, na ovu lifuatishe na jema litalifuta, na amiliana na watu kwa tabia njema."²

Allah تعالى Amesema,

لَعَلَّكُمْ تَفْلِحُونَ ﴿٢٠٠﴾

"Ili mpate kufanikiwa." (3:200)

¹ Ahmad 5:236. Kadhalika Tz. Tarekhe Damashqi 34:307. Pia Tz. "Siyaru Alaami Anubalaai" Isnadi yake ina dosari. Tz. "Lisanu Al-Mizaan" 6:248.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:123.

Katika maisha ya dunia na akhera Ibn Jarir رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى alipokea kuwa Muhammad bin Ka'b Al-Qurazi alikuwa akisema kutokana na Kauli ya Allah تَعَالَى،

وَأَتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٢٠٠﴾

“Na mcheni Mwenyezi Mungu, ili mpate kufanikiwa.” (3:200)

Muradi wake, “Mcheni Allah تَعَالَى katika yale yaliyo baina yetu, ili mpate fanaka mtakapokutana nami kesho.”¹

Tafsiri ya *Surat Al-Imran* inaishia hapa, Shukrani zote ni za Allah تَعَالَى na tunamuomba tufe tukiwa katika njia ya Qur'an na Sunnah, Amin.

* * *

¹ At-Tabari 7:510

Tafsiri ya Suratu An-Nisai'

Sura ya 4

Iliteremshwa Madinah

Al-Awfi alipokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, *Suratu An-Nisa* iliteremshwa Madina. Ibn Marduwyah رحمه الله تعالى alipokea kauli kama hiyo kwa Abdullah bin Az-Zubayr na Zayd bin Thabit. Al-Hakim aliandika katika *Mustadrak* yake kuwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنهما alisema, "Kuna Aya tano ndani ya *Surat An-Nisa* nazipenda kuliko maisha ya dunia na vyote vilivyomo ndani yake. Nazo ni:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ

"Hakika Mwenyezi Mungu Hadhulumu hata uzito wa chembe moja." (4:40)

إِنْ تَجْتَنِبُوا كَبَائِرَ مَا تُهِنُونَ عَنْهُ

"Mkiyaepuka makubwa mnayokatazwa." (4:31)

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

"Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehe kushirikishwa, na Husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye." (4:48)

وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ جَاءُوكَ

"...Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangelikuja..." (4:64)

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٦٥﴾

"Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake, kisha akaomba maghira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghufira, Mwenye Kurehemu." (4:110)

Kisha akasema *Sanad* yake ni sahihi. Ama kuhusu Abdur Rahman kupokea kutoka kwa babake, wanazuoni wametofautiana. Al-Hakim alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, "Niulizeni juu ya *Surat An-Nisai* kwani nilijifunza Qur'an nilipokuwa mdogo." Al-Hakim alisema, "Hadithi hii ni sahihi kwa masharti ya masheikh wawili wa hadithi (Bukhari na Muslim) ijapokuwa hawakuikusanya."¹

¹ Al-Hakim 2:301.

سُورَةُ النِّسَاءِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يَتَّيِبُهَا لِلنَّاسِ أَنْ يَقُولُوا رَبُّكُمْ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ
 وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَنَسَاءً كَثِيرًا وَنِسَاءً وَأَقْبُوا
 اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ
 رَقِيبًا ﴿١﴾ وَءَاتُوا الْيَتَامَىٰ أَمْوَالَهُمْ وَلَا تَتَّبِعُوا الْحَبِيسَ
 بِالطَّيِّبِ وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَهُمْ إِلَىٰ أَمْوَالِكُمْ إِنَّهُ كَانَ حُوبًا
 كَبِيرًا ﴿٢﴾ وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَىٰ فَانكِحُوا مَا
 طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مَتًى وَثَلُثَ وَرُبِعَ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا
 تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ذَلِكَ أَدْنَىٰ أَلَّا
 تَعُولُوا ﴿٣﴾ وَءَاتُوا النِّسَاءَ صَدَقَاتِنَّ حِجَلَهُنَّ فَإِنْ ظَنَنْتُمْ
 عَنْ شَيْءٍ مِنْهُ نَفْسًا فَكُلُوهُ هَنِيئًا مَرِيئًا ﴿٤﴾ وَلَا تَوْتُوا
 السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَمًا وَارْزُقُوهُمْ فِيهَا
 وَاكْسُوهُمْ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَعْرُوفًا ﴿٥﴾ وَابْتَلُوا الْيَتَامَىٰ
 حَتَّىٰ إِذَا بَلَغُوا النِّكَاحَ فَإِنْ ءَانَسْتُمْ مِنْهُمْ زُجْدًا فَادْفَعُوا
 إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ وَلَا تَأْكُلُوهَا إِسْرَافًا وَبِدَارًا أَنْ يَكْبَرُوا وَمَنْ
 كَانَ غَنِيًّا فَلْيَسْتَعْفِفْ وَمَنْ كَانَ فَقِيرًا فَلْيَأْكُلْ بِالْمَعْرُوفِ
 فَإِذَا دَفَعْتُمْ إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ فَأَشْهِدُوا عَلَيْهِمْ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ

حَسِيبًا ﴿٦﴾

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi
 wa Rehema Mwenye
 Kurehemu

يَتَّيِبُهَا لِلنَّاسِ أَنْ يَقُولُوا رَبُّكُمْ الَّذِي
 خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا
 زَوْجَهَا وَنَسَاءً كَثِيرًا وَنِسَاءً وَأَقْبُوا
 اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ
 بِهِ وَالْأَرْحَامَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ
 رَقِيبًا ﴿١﴾

"Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi Aliyekuumbeni kutokana na nafsi (asli) moja, na Akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na Akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka wawili hao. Na Mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye Kwaye mnao - mbana, na (muwatazame) jamaa zenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuhifadhi matendo yenu." (4:1)

Amri ya Kuwa na Taqwa, inakumbusha Kuumbwa na Kuwatendea wema jamaa.

Allah تعالى Amewakalifisha viumbe Wake kumcha Yeye kwa kumuabudu Yeye Pekee bila mshirika. Aidha Anawakumbusha Uweza Wake, kuwa Aliwaumba wote kutokana na mtu mmoja Adam عليه السلام.

وَحَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا

“Na Akamuumba mkewe kutoka nafsi (asli) ile ile.”

Hawwa, aliumbwa kwa ubavu wa kushoto wa nyuma wa Adam عليه السلام alipokuwa amelala. Adam عليه السلام alipoamka na kumuona Hawwa, alimpenda na kuchuruka, na Hawwa naye yalimsibu hayo hayo. Hadithi sahihi inaeleza,

«إِنَّ الْمَرْأَةَ خُلِقَتْ مِنْ ضِلْعٍ، وَإِنَّ أَعْوَجَ شَيْءٍ فِي الضِّلْعِ أَغْلَاهُ، فَإِنْ ذَهَبَتْ نُفَيْمُهُ كُسْرَتُهُ، وَإِنْ اسْتَمْتَعَتْ بِهَا اسْتَمْتَعَتْ بِهَا وَفِيهَا عَوَجٌ»

“Hakika Mwanamke aliumbwa kutokana na ubavu, kwa hakika sehemu iliyopinda zaidi katika ubavu ni juu yake, hivyo ukitaka kuunyoosha, utauvunja, lakini ukiuacha kama ulivyo utabaki umepinda.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

وَوَتَّ مِّنْهَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً

“Na Akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi.”

Muradi wake ni kuwa Allah تعالى Aliumba kutokana na Adam عليه السلام na Hawwa, wanaume na wanawake wengi na Akawaeneza duniani kote wakiwa na maumbile, sifa bainifu, rangi na kujua lugha mbalimbali. Khatima yao ni kurejea kwa Allah تعالى na kuhesabiwa. Kisha Allah تعالى Amesema:

وَاتَّقُوا اللَّهَ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ

“Na Mcheni Mwenyezi Mungu Ambaye Kwaye mnaombana, na (muwatazame) jamaa zenu.”

¹ Fat'hul Al-Bari 6:418.

Jilinde kwa Mola wako kwa amali za kumnyenyekea Yeye. Ibrahimu, Mujahid na Al-Hasan wamesema,

الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ وَالْأَرْحَامَ

“Ambaye Kwaye mnaombana, na (muwatazame) jamaa zenu..”

Hii inawakusudia baadhi ya watu wasemao, “Nakuomba kwa Jina la Allah تعالى na kwa Jina la *Ar-Rahim*.¹ Adh-dhahhak alisema, “Mcheni Allah تعالى Ambaye Kwake mnaahidiana na mnafungiana mikataba.”² Na “Heshimu sana udugu wa kuzaliwa kwa kutoukata udugu huo bali muudumishe na muuheshimu.” Kama walivyosema Ibn Abbas, Ikrima, Mujahid, Al-Hassan, Adh-dhahhak na Ar-Rabi رضي الله عنهم.³ Kauli Yake Allah تعالى,

إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuhifadhi matendo yenu.”

Maana yake: Anayaona matendo yako yote, na Anazona hali zako zote. Katika Ayah nyingine Allah تعالى Amesema;

وَاللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kushuhudia kila kitu.” (58:6)

«اعْبُدِ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ، فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ، فَإِنَّهُ يَرَاكَ»

“Muabudu Allah kama Unamuona, na hata kama humuoni Yeye Anakuona.”⁴

Sehemu hii ya Aya inashajiisha utambuzi kuwa Allah تعالى wakati wote Anayaona yanayotendeka bila kupitwa na kitu. Allah تعالى Ametaja kuwa Alimuumba binadamu kutokana na baba na mama mmoja, ili wahurumiane wao kwa wao na wawasaidie madhalili miongoni mwao.

¹ At-Tabari 7:519.

² At-Tabari 7:518.

³ At-Tabari.

⁴ Fat’hul Al-Bari 1:140.

Katika sahihi yake, Muslim alipokea kuwa Jarir bin Abdullah Al-Bajali رضي الله عنه alisema kuwa ujumbe kutoka Mudar ulikuja kwa Mtume ﷺ na aliona hali zao kuwa walivaa nguo chakavu za sufi kutokana na umaskini. Baada ya Sala ya *Dhuhr* Mtume ﷺ alisimama na kutoa hotuba na akasoma,

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ

“Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi Aliyekuumbeni kutokana na nafsi (asli) moja, na Akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile...”

Mpaka mwisho wa Aya. Mtume ﷺ pia aliwasomea,

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَلْتَنْظُرْ نَفْسٌ مَا قَدَّمَتْ لِغَدٍ

“Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie inayoyatanguliza kwa ajili ya Kesho...” (59:18)

Pia aliwahimiza kutoa Sadaka alisema,

تَصَدَّقْ رَجُلٌ مِنْ دِينَارِهِ، مِنْ دِرْهَمِهِ، مِنْ صَاعِ بُرٍّ، مِنْ صَاعِ تَمْرِهِ

“Mtu hutoa Sadakah kutokana na Dinari yake, Dirham yake, Pishi yake ya ngano na pishi yake ya tende....” Na akataja hadithi kamili.¹

Hadithi hii pia, ilikusanywa na Ahmad na wakusanyaji wa *Sunan* kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه katika khutuba ya Haja.²

وَأَتُوا آلَيْتَنِي أَمْوَالَهُمْ طُ وَلَا تَتَّبِعُوا الْخَنِيثَ بِالطَّيِّبِ طُ وَلَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَهُمْ إِلَىٰ أَمْوَالِكُمْ ؕ
 إِنَّهُ كَانَ حُوبًا كَبِيرًا ﴿١٠﴾ وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي آلَيْتَنِي فَأَنْكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ
 النِّسَاءِ مَتَىٰ وَتَلَّتْ وَرَبَعٌ طُ فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةٌ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ؕ ذَلِكَ
 أَدْبَىٰ أَلَّا تَعُولُوا ﴿١١﴾ وَأَتُوا النِّسَاءَ صَدَقَاتِهِنَّ بِحِلَّةٍ طُ فَإِنْ طِبْنَ لَكُمْ عَنْ شَيْءٍ مِنْهُ نَفْسًا
 فَكُلُوهُ هَنِيئًا مَرِيئًا ﴿١٢﴾

¹ Muslim 2:705.

² Ahmad 4:358, An – Nisai 5:75, Ibn Majah 1:74.

2. Na wapeni mayatima mali yao. Wala msibadilisha kibaya kwa kizuri. Wala msile mali zao pamoja na mali zenu. Hakika yote hayo ni Dhambi kubwa.

3. Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtowafanyia mayatima uadilifu, basi oeni mnao wapenda katika wanawake, wawili au watatu au wanne. na mkiogopa kuwa hamuwezi kufanya uadilifu, basi mmoja tu, au wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki. Kufanya hivi ndiko kutapelekea kutotelekeza haki zao.

4. Na wapeni wanawake mahari yao hali ya kuwa ni kipawa. Lakini wakikutunukieni kitu katika mahari, kwa radhi yao, basi kuleni katika vizuri na vyenye kutia afya.

Ulinzi wa Mali za Mayatima

Allah تعالى Ameamuru mayatima wakabidhiwe mali zao zote wanapofikia baleghe na Ameharamisha kuitumia au kupora sehemu yake. Hivyo amesema

وَلَا تَتَّبِعُوا الْاٰخِيْنَ بِالطَّيْبِ

“..Wala msibadilisha kibaya kwa kizuri..”

Said bin Al-Musayyib na Az-Zuhri wameeleza, “Usibadili mnyama wako dhaifu kwa mnyama wake mnono.”¹ Ibrahim An-Nakhai na Adh-Dhahhak wameeleza yafuatayo, “Usibadili kitu kibaya kwa kizuri.”² As-Suddi alisema, “Mmoja wao (Mlezi wa yatima) anachukua Kondoo mnono katika mali ya yatima na badala yake anaweka Kondoo mkondefu, huku akisema ‘Kondoo kwa Kondoo.’ Aidha anachukua Dirham halisi na kuibadili kwa Dirham bandia, akisema ‘Dirham kwa Dirham.’³ Kauli ya Allah تعالى

وَلَا تَاْكُلُوْا اَمْوَالَهُمْ اِلَىٰ اَمْوَالِكُمْ

“Wala msile mali zao pamoja na mali zenu.”

¹ At-Tabari 7:525.

² At-Tabari 7:525.

³ At-Tabari 7:526.

Maana yake: Msichanganye, ili msile na mali zao, kama Mujahid, Said bin Jubayr, Muqatil bin Hayyan, As-Suddi na Sufyan bin Hussin رضي الله عنهم walivyoeleza. Yaani, msichanganye mkala wote.¹ Allah تعالى Amesema,

إِنَّهُ كَانَ حُوبًا كَبِيرًا ﴿٦﴾

“Hakika yote hayo ni dhambi kubwa.”

Ni dhambi kubwa kulingana na Ibn Abbas رضي الله عنهما.² Haya yamepokewa pia kutoka kwa Mujahid, Ikrimah, Said bin Jubayr, Al-Hassan, Ibn Sirin, Qatadah, Muqatil bin Hayyan, Adh-Dhahhak, Abu Malik, Zayd bin Aslam na Abu Sinaan.³ Maana ya hapo juu ni kuwa kuchanganya mali yako na yao ni dhambi kubwa na kosa kubwa, hivyo jiepusha nayo.

Kuharamishwa Kuoia Mayatima kwa Kuwapa Mahari Duni

Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي آلَيْتِنِي فَأَنْكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ مَتَّقُوا

“Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtowafanyia mayatima uadilifu, basi oeni mnao wapenda katika wanawake, wawili...”

Allah تعالى Anaamuru kuwa mmoja wenu anayemlea yatima wa kike na anachelea kuwa asingeweza kumpa mahari yenye hadhi yake, basi analazimika kumuoa mwanamke mwingine ambao wako wengi; na Allah تعالى Hakumkwaza kwa hilo. Bukhari alipokea kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Kuna mtu alikuwa akimlea yatima wa kike na kisha akamuoa, japokuwa hakuwa na hamu ya kumuoa. Alichanganya mali ya mwanamke yule na yake na akahodhi mali yote. Baadaye Aya hii iliteremshwa kwa sababu ya kadhia hii.

وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا

“Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtowafanyia uadilifu.”

¹ At-Tabari 7:528.

² At-Tabari 7:530.

³ At-Tabari 7:530.

Bukhari alipokea kutoka kwa Urwah bin Az-Zubair رضى الله عنه alisema kuwa alimuuliza Aisha رضى الله عنها kuhusu maana ya Kauli ya Allah تعالى isemayo,

وَأِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَىٰ

“Na ikiwa mnaogopa kuwa hamtowafanyia mayatima uadilifu.”

Akasema, “Ewe mpwa wangu! Kauli hii inamhusu yatima wa kike anayeishi na mlezi anayetumia mali yake.”¹ Mali yake na uzuri wake vinaweza kushawishi kumuoa bila kumpa mahari ya kutosha ambayo angepewa na mchumba mwingine. Hivyo walezi wa aina hiyo wamezuiwa kuwaoa mayatima wa aina hiyo mpaka wawafanyie uadilifu na kuwapa mahari iliyo stahili yao; vinginevyo wameamrisha kuoa wanawake wengine.” Aishah رضى الله عنها aliongeza kusema kuwa, “Baada ya kushuka Ayah hii, watu waliendelea kumuuliza Mtume ﷺ (Juu ya kuoa mayatima) Allah تعالى Alishusha Aya ifuatayo:

وَبَسْتَفْتُونَكَ فِي النِّسَاءِ

“Wanakuuliza nini sharia ya wanawake.” (4:127)

Akasema, Kauli ya Allah تعالى katika Aya hii.

وَتَرَعْبُونَ أَنْ تَنْكِحُوهُنَّ

“Na mnapenda kuwaoa..” (4:127)

Inahusu mlezi hokusudii kuoa yatima anayemlea, ama kwa kuwa hana mali au si mzuri. Walezi walizuiwa kuoa yatima wazuri wenye mali bila kuwatendea uadilifu kama walivyojiweka mbali kuoa wasiokuwa na mali nyingi au wasiokuwa na uzuri.”²

¹ Fat’hul-Bari 8:88.

² Fat’hul-Bari 8:88.

Kuishia Kuo Wake Wanne

مَتْنِي وَتَلْتِ وَرَبْعَ

“Wawili au watatu au wane.” (4:3)

Maana yake: Oeni wanawake wengi kama mtakavyo miongoni mwa wasichana yatima, wawili, watatu au wane. Tunalazimika kutaja Kauli ya Allah تعالى katika Aya nyingine,

جَاعِلِ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا أُولِي أَلْبَانٍ مَّتْنِي وَتَلْتِ وَرَبْعَ

“Aliyewafanya Malaika kuwa wajumbe wenye mbawa, mbili- mbili, na tatu- tatu, na nne-nne.”

Haimaanishi malaika wengine hawana zaidi ya mbawa nne, upo ushahidi kuwa baadhi ya malaika wana mbawa zaidi. Hata hivyo wanaume wameharamishwa kuo zaidi ya wake wane, kama Ayah inavyoamuru, kwani Aya imebainisha idadi ya wake waliyoruhusiwa kuo, kama Ibn Abbas رضي الله عنهما na wanazuoni wengi walivyotaja. Iwapo ruhusa ingekuwa ni zaidi ya wake wane, Aya ingetaja hivyo.

Imam Ahmad alimnukuu Salim akisema, baba yake alisema, Ghailan bin Salamah Ath-Thaqafi alikuwa na wake kumi aliposilimu, Mtume ﷺ akamuambia, “Chagua wane wowote kati yao na wataliki waliosalia.” (Alikataa) Na katika utawala wa Umar رضي الله عنه, Ghailan aliwataliki wakeze waliosalia na akawagaia wanawe utajiri wake. Khabari hii ilipomfikia Umar رضي الله عنه, alimuambia Ghailan, “Nadhani shetani ameufikishia moyo wako taarifa ya kukaribia kifo chako, kwa kuwa shetani labda kuna aliyoyasikia wakati wa kusikiliza mazungumzo ya siri, inawezekana pia hautaishi kipindi kirefu. Wallah! Lazima uwarejee wakezo na uchukue mali zako, la sivyo nitachukua zote na kuamuru kaburi lako lirujumiwe, kama lilivyorujumiwa kwa wenzi wako.” Shafii, Tirmidhi, Ibn Majah, Daraqutni na Bayhaq waliikusanya hadithi hii mpaka kauli ya Mtume ﷺ, “Chagua yeyote kati ya wane.” Ahmad pekee ndiye aliyekusanya masimulizi kamili ya Hadithi hii.²

¹ Fat'h ulAl-Bari 1:140.

² Ahamd 2:14, Al-Umm 5:49, At-Tirmidhi Na.1128, Ibn Majah Na.1953, Ad-Daraqutni.

Hivyo ingekuwepo ruksa ya wanaume kuoa wanawake zaidi ya wane wakati mmoja basi Mtume ﷺ angemruhusu Ghilan kubakiza zaidi ya wane katika wakeze, kwani alisilimu pamoja nao. Mtume ﷺ alipomuambia abakize wane na awataliki waliobaki, inaashiria kuwa wanaume hawatakiwi kuwa na wake zaidi ya wane kwa wakati mmoja kwa hali yoyote iwayo. Endapo amri hii inaruhusu waliokuwa na wake zaidi ya wane wakati wa kusilimu, hivyo amri hii inahusu pia kutooa zaidi ya wanawake wane.

Kutosheka Kuoa Mke Mmoja kwa Kuchelea Kukosekana Uadilifu kwa Wakeze.

Kauli ya Allah تعالى،

فَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تَعْدِلُوا فَوَاحِدَةً أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ

“Na mkiogopa kuwa hamuwezi kufanya uadilifu, basi mmoja tu, au wale ambao mikono yenu ya kulia imewamiliki.”

Aya inaamuru kuwa kama unachelea kutofanya uadilifu kwa mke zaidi ya mmoja, basi oa mmoja tu au jitosheleze na suria (mjakazi) kwani si lazima kuwatendea wote sawa, bali imependekezwa. Hivyo mtu akiweza ni vizuri na akishindwa, hapana madhara juu yake.

Katika Aya nyingine Allah تعالى Amesema,

وَلَنْ تَسْتَطِيعُوا أَنْ تَعْدِلُوا بَيْنَ النِّسَاءِ وَلَوْ حَرَصْتُمْ

“Wala hamtaweza kufanya uadilifu baina ya wake, hata mkikakamia.” (4:129)

ذَلِكَ أَدَّتْ أَلَّا تَعُولُوا ﴿٤٠﴾

“Kufanya hivi ndiko kutapelekea msiwadhulumu.”

Muradi wake ni kutokudhulumu. Ibn Abi Hatim, Ibn Marduwyah na Abu Hatim Ibn Hibban katika Sahih yake aliandika kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, Mtume ﷺ alisema kuwa Aya،

ذَلِكَ أَدَّتْ أَلَا تَعُولُوا ﴿٦﴾

“Kufanya hivi ndiko kutapelekea msiwadhulumu.”

Maana yake: kutodhulumu.¹ Hata hivyo Abi Hatim alisema kuwa baba yake alisema, Hadithi hii kusemwa inatoka kwa Mtume ﷺ ni makosa kwani ilipokelewa kutoka kwa Aishah رضي الله عنها na sio Mtume ﷺ.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Abbas, Aishah, Mujahid, Ikrimah, Al-Hassan, Abu Malik, Abu Rizin, An-Nakhai, Ash-Shabi, Adh-Dhahhak, Ata Al-Khurasani, Qadatadah, As-suddi na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم kuwa “*Ta’ulu* maana yake ni kukengeuka (dhidi ya haki).”²

Kutoa Mahari ni Wajibu

Ali bin Abi Talhah alimsikia Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, *Nihlah* katika Kauli ya Allah.

وَأَتُوا النِّسَاءَ صَدُقَاتِهِنَّ نِحْلَةً

“Na wapeni wanawake mahari yao.” Inakusudiwa mahari.³

Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى alipokea kwa Az-Zuhri kuwa Urwah alisema Aisha رضي الله عنها alisema, “*Nihlah* ni wajibu.” Ibn Jurayrj aliongeza: ‘iliyoainishwa.⁴ Ibn Zayd alisema, “Katika lugha ya kiarabu, *Nihlah* ni kitu cha lazima. Hivyo Allah تعالى Anatuamrisha Msioe hadi muwape wake zenu haki zao.” Baada ya Mtume ﷺ hapana mwingine aliyeruhusiwa kuoza mwanamke mpaka atoe mahari wala si kwa ahadi za uongo katika mahari iliyokusudiwa.”⁵ Hivyo mwanaume anatakiwa kumpa mahari mkewe kwa moyo safi kama zawadi. Na mke akimpa sehemu au mahari yote kwa hiyari, mume anaruhusiwa kuipokea na ni halali yake katika mazingira haya. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

¹ Ibn Hibban 6:134.

² At - Tabari 7:549–551.

³ At - Tabari 7:553.

⁴ At - Tabari 7:553.

⁵ At - Tabari 7:553.

فَإِنْ طِبْنَ لَكُمْ عَنْ شَيْءٍ مِّنْهُ نَفْسًا فَكُلُوهُ هَنِيئًا مَّرِيئًا ﴿١٦﴾

“Lakini wakikutunukieni kitu katika mahari, kwa radhi yao, basi kuleni kiwashuke kwa raha”.

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ الَّتِي جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ قِيَمًا وَارْزُقُوهُمْ فِيهَا وَاكْسُوهُمْ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَّرْهُوفًا ﴿١٧﴾ وَابْتَلُوا الَّذِينَ آمَنُوا حَتَّىٰ إِذَا بَلَغُوا النِّكَاحَ فَإِنْ آنَسْتُمْ مِنْهُمْ رُشْدًا فَادْفَعُوا إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ وَلَا تَأْكُلُوهَا إِسْرَافًا وَبِدَارًا أَنْ يَكْبَرُوا ۚ وَمَنْ كَانَ غَنِيًّا فَلْيَسْتَعْفِفْ ۚ وَمَنْ كَانَ فَقِيرًا فَلْيَأْكُلْ بِالْمَعْرُوفِ ۚ فَإِذَا دَفَعْتُمْ إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ فَأَشْهِدُوا عَلَيْهِمْ ۗ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ

حَسِيبًا ﴿١٨﴾

5. Wala msiwape wasio na akili mali yenu ambayo Mwenyezi Mungu Ameyajaalia yawe msimamo wa maisha yenu. Walisheni katika hayo na muwavike, na msemi nao maneno mazuri.

6. Na wajaribuni mayatima mpaka wafike umri wa kuoa. Mkiwaona ni werevu, basi wapeni mali yao. Wala msiyale kwa fujo na pupa kwa kuwa watakuja kuwa watu wazima. Na aliye kuwa tajiri na ajizuilie, na aliyefakiri basi na ale kwa kadiri ya haja. Na mtakapo wapa mali yao washuhudisheni. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mhasibu.

Kuzuia Mali ya Mtu Mbahirifu

Allah تعالی Ameharamisha kumuacha kutumia mali apendavyo asiye na busara au akili, Allah تعالی Ameifanya mali kuwa njia ya kuwakimu watu. Kuna wakati sheria hii hutumika kwa watoto wadogo ambao kwa umri wao si rahisi kufanya uamuzi wa busara. Pia katika hali ya umajinuni, tabia mbovu na udhaifu wa kiakili au kidini. Pia masuala ya ufilisi wakati mdai anataka kuchukua mali za mdaiwa zilizo chini ya mfilisi na deni haliwezi kulipwa kwa fedha zake kwa kuwa hazitoshelezi. Adh-Dhahhak alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa Allah تعالی Amesema,

وَلَا تُؤْتُوا السُّفَهَاءَ أَمْوَالَكُمُ

“Wala msiwape wasio na akili mali yenu.”

Wanakusudiwa watoto na wanawake.¹ Kauli hii pia ilisemwa na Ibn Mas'ud, Al-Hakam bin Uyaynah, Al-Hassan na Adh-Dhahhak رضي الله عنهم, “Wanawake na watoto.”² Said bin Jubayr رضي الله عنه alisema kuwa, “Wasio na busara” maana yake mayatima.³ Mujahid, Ikrimah na Qatadah wamesema, “Ni wanawake.”⁴

Amri ya Kuwapa Matumizi Wasio na Busara kwa Uadilifu

Allah تعالى Amesema,

وَأَرْزُقُوهُمْ فِيهَا وَاكْسُوهُمْ وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَعْرُوفًا ﴿٥٠﴾

“Walisheni katika hayo na muwavike, na msem nao maneno mazuri.”

Ali bin Abi Talhan alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitupa maelezo yafuatayo, usitoe mali yako aliyokupa Allah تعالى uwe msimamizi kwayo, kwa ajili ya kujikimu wewe binafsi pamoja na mke au watoto wako. Bali itunze mali yako na uwe msimamizi, na uwanunulie chakula, uwape malazi na mahitaji mengine.⁵ Mujahid alisema kuwa Aya,

وَقُولُوا لَهُمْ قَوْلًا مَعْرُوفًا ﴿٥٠﴾

“Na msem nao maneno mazuri.”

Muradi wake ni wema na kudumisha mahusiano mazuri. Ayah hii tukufu inawaamrisha kuamiliana vizuri kwa vitendo chini ya uangalizi wako. Inatakiwa kuwanunulia nguo na mahitaji mengine na kuwatendea mema - kama kuzungumza nao kwa lugha nzuri.

¹ At - Tabari 7:562.

² At - Tabari 7:562.

³ At - Tabari 7:563.

⁴ At - Tabari 7:564.

⁵ At - Tabari 7:570.

Kuwakabidhi Mayatima Mali yao Wanapofika Baleghe

Allah تعالى Amesema,

وَأَبْتَلُوا أَلْيَتَنِي

“Na wajaribuni mayatima.”

Maana yake: Jaribuni maarifa yao. Kama walivyosema Ibn Abbas, Mujahid, Hassan, As-Suddi na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم.²

حَتَّىٰ إِذَا بَلَغُوا النِّكَاحَ

“Mpaka wafike umri wa kuoa.”

Umri wa baleghe kwa mujibu wa Mujahid,³ kwa mujibu wa wanazuoni wengi, baleghe huanza mtoto anapoota na kumwaga.

Katika Sunan yake Abu Dawud aliandika kuwa Ali رضي الله عنه alisema, ‘Niliyahifadhi maneno haya kutoka kwa Mtume ﷺ,

«لَا يَتِمُّ بَعْدَ اِخْتِلَامٍ، وَلَا صُمَاتٍ يَوْمَ إِلَى اللَّيْلِ»

“Hapana yatima baada ya baleghe wala kula kiapo cha kunyamaza kutwa nzima mpaka usiku.”⁴

Katika hadithi nyingine, Aisha رضي الله عنها na Masahaba wengine wa Mtume ﷺ walisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«رُفِعَ الْقَلَمُ عَنْ ثَلَاثٍ، عَنِ الصَّبِيِّ حَتَّىٰ يَحْتَلِمَ، وَعَنِ النَّائِمِ حَتَّىٰ يَسْتَيْقِظَ، وَعَنِ الْمَجْنُونِ حَتَّىٰ يُبِينَ»

“Kalamu imeinuliwa kwa amali za watu watatu, mtoto mpaka afikie baleghe, aliyelala mpaka aamke na mwendawazimu mpaka azinduke.”⁵

¹ At - Tabari 7:574.

² At - Tabari 7:575.

³ Abu Dawud 3:293.

⁴ Abu Dawud 4:558 – 560.

Umri wa miaka kumi na mitano unachukuliwa kuwa umri wa Baleghe katika sahihi mbili, imeandikwa kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, "Nilipelekwa mbele ya Mtume ﷺ siku ya mkeshwa wa vita vya Uhud, nilipokuwa na umri wa miaka kumi na nne, hakuniruhusu kushiriki katika vita hivyo. Lakini nilipelekwa mbele yake siku ya mkeshwa wa vita vya Al-Khandaq nilipokuwa na umri wa miaka kumi na mitano, na aliniruhusu kwenda vitani. Hadithi hii ilipomfikia Umar bin Abdul Azizi رحمه الله تعالى alisema, "Hii ndiyo tofauti kati ya mtoto na mtu mzima."¹

Kuna rai tofauti kuwa nywele za kinena ni alama ya utu uzima, na rai iliyosibu ni kuwa ni dalili. Sunnah inaunga mkono rai hii kwa kulingana na Hadithi iliyokusanywa na Imam Ahmad² kutoka kwa Atiyah Al-Qarazi ambayo alisema, "Tulifikishwa mbele ya Mtume ﷺ siku ya Quraidha. Yeyote aliyekuwa na nywele za kinena aliuawa na asiyekuwa nazo aliachwa huru, nilikuwa miongoni mwa wale wasiokuwa nazo, hivyo niliachwa huru." Wakusanyaji wanne wa Sunan walikusanya Hadithi sawa na hii.³ At-Tirmidhi amesema ni "*Hadithi sahih*". Kauli ya Allah تعالى,

فَإِنْ ءَأَسْتُمْ مِنْهُمْ رُشْدًا فَادْفَعُوا إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ

"Mkiwaona ni werevu, basi wapeni mali yao..."

Said bin Jubayr alisema, kipande hiki cha Ayah kina maana, ukiwaona wana msimamo mzuri wa dini na werevu wa kutunza fedha. Maneno kama haya yalipokewa na Ibn Abbas رضي الله عنهما, Hassan Al-Basri رحمه الله تعالى na wengine katika Maimamu.⁴ Wanazuoni wa Fiqh wanasema kuwa mtoto anapokuwa mwerevu na mwenye maadili mazuri na mtunzaji wa fedha, anastahili kukabidhiwa fedha zilizokuwa zinatunzwa na Mwangalizi.

¹ Bukhari Na.2664, Muslim Na.1868.

² Ahmad 4:310.

³ Abu Dawud 4:561, Tuhfat Al-Ahwadhi 2:207; An-Nasai katika Al-Kubra 5:181.

⁴ At - Tabari 7:576.

Waangalizi Masikini Wanaruhusiwa Kutumia kwa Hekima Mali za Mayatima Zilizo chini ya Uangalizi Wao Ili Kufidia Kazi ya Kuzitunza

Allah تعالی Amesema,

وَلَا تَأْكُلُوهَا إِسْرَافًا وَبِدَارًا أَنْ يَكْبُرُوا

“Wala msiyale kwa fujo na pupa kwa kuwa watakuja kuwa watu wazima.”

Allah تعالی Anaamrisha kuwa fedha za mayatima zisitumiwe vibaya.

إِسْرَافًا وَبِدَارًا

“Kwa fujo na pupa.” Kwa kuchelewa kuwa watakuwa watu wazima. Allah تعالی pia Anaamrisha,

وَمَنْ كَانَ غَنِيًّا فَلْيَسْتَعْفِفْ

“Na aliyekuwa tajiri na ajizuilie...” Hivyo, mlezi ambaye ni tajiri na ahitaji mali za yatima asichukue chochote kama malipo.

وَمَنْ كَانَ فَقِيرًا فَلْيَأْكُلْ بِالْمَعْرُوفِ

“Na aliyekwa fakiri basi na ale kwa kadiri ya ada.”

‘Aya hii iliteremshwa kuhusu waangalizi wa mayatima na inahusu kazi yoyote afanyayo kwa mali ya mayatima.’¹ Bukhari alikusanya hadithi hii.² Imam Ahmad aliandika kuwa Amr Bin Shu‘ayb alisema kuwa baba yake alimuambia kuwa, kuna mtu alimuuliza Mtume ﷺ, “Sina fedha lakini ninamlea yatima.’ Mtume ﷺ akasema,

«كُلْ مِنْ مَالِ يَتِيمِكَ غَيْرَ مُسْرِفٍ وَلَا مُبَدِّرٍ وَلَا مُتَأَنِّلٍ مَالًا، وَمِنْ غَيْرِ أَنْ تَقِيَّ مَالَكَ - أَوْ قَالَ - تَقْدِي مَالَكَ بِمَالِهِ»

“Kula katika mali ya yatima wako bila kufanya Israfu au ubadhirifu wala kuchanganya mali yake na yako na bila kuikinga mali yako, (au amesema) kuikomboa mali yako kwa hesabu ya mali yake (yatima).”³

¹ At - Tabari 7:593.

² Fat’hul Al-Bari 8:89.

³ Ahmad 2:215, 216.

Allah تعالى Amesema,

فَإِذَا دَفَعْتُمْ إِلَيْهِمْ أَمْوَالَهُمْ

“Na mtakapo wapa mali yao.”

Baada ya kuwa watu wazima, na mkawaona kuwa watambuzi basi,

فَأَشْهَدُوا عَلَيْهِمْ

“Washuhudizieni.”

Allah تعالى Anaamuru waangalizi wa Yatima kuwakabidhi waliofikia utu uzima, mbele ya mashahidi, ili mmoja wao asije kanusha kupokea fedha. Allah تعالى Amesema,

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ حَسِيبًا

“Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mhasibu.”

Maana yake: Allah تعالى Anatosha kuwa shahidi. Mhasibu na Muangalizi wa kazi wafanyazo kwa yatima, na wanapowakabidhi mali zao, ima kamili au pungufu. Kwa hakika Allah تعالى Anajua yote hayo. Katika sahihi Muslim aliandika kuwa Mtume ﷺ alisema,

يَا أَبَا ذَرٍّ إِنَّي أَرَاكَ ضَعِيفًا ، وَإِنِّي أَحِبُّ لَكَ مَا أَحِبُّ لِنَفْسِي ، لَا تَأْمُرَنَّ عَلَيَّ اثْنَيْنِ ،
لَا ثَلَاثِينَ مَالًا يَتِيمٍ

“Ewe Abu Dharr! Hakika nakuona u-dhaifu na nakupendelea ninalolipendelea nafsi yangu. Usiwe kiongozi wa wawili wala usisimamie mali ya yatima.”¹

* * *

¹ Muslim 3:1458.

لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ وَلِلنِّسَاءِ
 نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ أَوْ
 كَثُرٌ ۗ نَّصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿٧﴾ وَإِذَا حَضَرَ الْقِسْمَةَ أُولُو
 الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينُ فَأَرزُقُوهُمْ مِنْهُ وَقُولُوا لَهُمْ
 قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٨﴾ وَلْيَخْشَ الَّذِينَ لَوْ تَرَكَوْا مِنْ خَلْفِهِمْ
 ذُرِّيَّةً ضِعْفًا خَافُوا عَلَيْهِمْ فَلْيَتَّقُوا اللَّهَ وَلْيَقُولُوا قَوْلًا
 سَدِيدًا ﴿٩﴾ إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا
 إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا ۖ وَسَيَصْلَوْنَ سَعِيرًا ﴿١٠﴾
 يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ الْإُنثَىٰ ۚ
 فَإِنْ كُنَّ نِسَاءً فَوْقَ اثْنَتَيْنِ فَلَهُنَّ ثُلُثَا مَا تَرَكَ ۚ وَإِنْ كَانَتْ
 وَاحِدَةً فَلَهَا النِّصْفُ ۚ وَلِأَبَوَيْهِ لِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا الشُّدُسُ
 مِمَّا تَرَكَ إِنْ كَانَ لَهُ وَلَدٌ ۚ فَإِنْ لَمْ يَكُنْ لَهُ وَلَدٌ وَوَرِثَهُ
 أَبَوَاهُ فَلِأُمِّهِ الثُّلُثُ ۚ فَإِنْ كَانَ لَهُ إِخْوَةٌ فَلِأُمِّهِ الشُّدُسُ ۚ مِنْ
 بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِي بِهَا أَوْ دَيْنٍ ۚ ءَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ لَا تَدْرُونَ
 أَيُّهُمُ أَقْرَبُ لَكُمْ نَفْعًا ۚ فَرِيضَةٌ مِنَ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ
 عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١١﴾

لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ
 وَالْأَقْرَبُونَ وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ
 الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ مِمَّا قَلَّ مِنْهُ
 أَوْ كَثُرٌ ۗ نَّصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿٧﴾ وَإِذَا
 حَضَرَ الْقِسْمَةَ أُولُو الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ
 وَالْمَسْكِينُ فَأَرزُقُوهُمْ مِنْهُ وَقُولُوا
 لَهُمْ قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٨﴾ وَلْيَخْشَ
 الَّذِينَ لَوْ تَرَكَوْا مِنْ خَلْفِهِمْ ذُرِّيَّةً
 ضِعْفًا خَافُوا عَلَيْهِمْ فَلْيَتَّقُوا اللَّهَ
 وَلْيَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٩﴾ إِنَّ
 الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا
 إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا ۖ
 وَسَيَصْلَوْنَ سَعِيرًا ﴿١٠﴾

7. Wanaume wana sehemu katika wanayoyaacha wazazi na jamaa walio karibia. Na wanawake wanayo sehemu katika waliyo yaacha wazazi na

jamaa walio karibia. Ikiwa kidogo au kingi. Hizi ni sehemu zilizofaridhiwa.

8. Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na masikini, wapeni katika hayo mali ya urithi, na semeni nao maneno mema.

9. Na wachelee wale ambao lau kuwa na wao wangeliacha nyuma yao watoto wanyonge wangeliwakhofia. Basi nao wamche Mwenyezi Mungu, na waseme maneno waliyo sawa.

10. Hakika wanaokula mali ya mayatima kwa dhulma, hapana shaka yoyote wanakula matumboni mwao moto, na wataingia Motoni.

Amri ya Kurithisha na Kuwapa Kidogo Waliohudhuria ambao Sio Warithi

Said Bin Jubayr na Qatadah walisema, "Mushirikina walikuwa wakiwapa wanaume Watu wazima mirathi na kuwahini wanawake na watoto. Allah تعالى Akateremsha,

لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ

"Wanaume wana sehemu katika wanayoyaacha wazazi na jamaa waliokaribia."

Basi, kila mmoja ni sawa katika Uamuzi wa Allah تعالى katika mirathi, ila mafungu yao hutofautiana kulingana na ukaribu na marehemu, iwe jamaa, mke/mume n.k. ibn Marduwayhi رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa kwa Jabir رضي الله عنه kuwa, "Umm Kujjah alikwenda kwa Mtume ﷺ akamuambia; 'Ewe Mjumbe wa Allah! Nina mabinti wawili waliofiwa na baba yao, na hawamiliki chochote!" Allah تعالى Akateremsha Aya hii;

لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ

"Wanaume wana sehemu katika wanayoyaacha wazazi na jamaa waliokaribia."

Tutataja hadithi hii tutakapoelezea Aya mbili za mirathi, Allah تعالى ni Mjuzi wa yote.¹ Allah تعالى Amesema,

وَإِذَا حَضَرَ الْقِسْمَةَ

"Na wakati wa kugawanya wakihudhuria." Wale wasio na hisa katika mirathi,

وَأَلْيَتَنِي وَالْمَسْكِينُ

"Na mayatima na masikini,..." Waliohudhuria wakati wa kugawanywa kwa mirathi, wapewe sehemu ya mirathi.² Bukhari ameandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya,

¹ Abu Dawud 3:314.

² Fat 'hul Al-Bari 8:90.

وَإِذَا حَضَرَ الْقِسْمَةَ أُولُو الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسْكِينُ

“Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na masikini,” Haijanasikhiwa.¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema Ayah hii bado inafaa na lazima itumike.² Ath-Thawri رحمه الله تعالى alisema kuwa Ibn Abi Najih alisimulia kutoka kwa Mujahid kuwa utekelezaji wa Aya hii ni, ‘kuwa inahitajika kwa warithi kutoa na kuwapa chochote ambacho nyoyo zao zitaridhia kutoa.’³ Maelezo sawa na hayo yalipokelewa kutoka kwa Ibn Masoud, Abu Musa, Abdur-Rahman bin Abubakri, Abu Al-Aliyah, Ash-shabi na Al-Hassan رضي الله عنهم.⁴ Ibn Sirin, Said bin Jubayr, Makhulul, Ibrahim An-Nakhai, Atwa bin Abi - Rabah, Az-Zuhri na Yahya bin Ya’amar walisema kutoa huko ni faradhi. Ilisemwa vilevile kuwa hii ni kwa wasiya aliousia maiti. Wengine wanasema kuwa ilinasikhiwa. Al-Awfi aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Aya hii.

وَإِذَا حَضَرَ الْقِسْمَةَ

“Na wakati wa kugawanya wakihudhuria”

Inakusudia ugawaji Mirathi. Hivyo, ndugu walio maskini, mayatima, na maskini wanahudhuria ugawaji mirathi, ambayo wakati mwingine ni nyingi, nyoyo zao zitatamani kupata fungu, kwa kumuona kila anayestahiki kugawiwa mirathi akipata fungu lake, ilhali wao hawana matumaini, na bado hawapewi chochote. Inaamrisha kuwa wapewe fungu katika mirathi kama kitendo cha kuwafanyia wema, sadaka na kuwahurumia.

Kuangalia Usawa Katika Mirathi (Wasia)

Allah تعالى Anasema,

وَلْيَخْشَ الَّذِينَ لَوْ تَرَكَوْا مِنْ خَلْفِهِمْ

“Na wachelee wale ambao lau kuwa na wao wangeliacha nyuma yao watoto.”

¹ At - Tabari 8:8.

² At - Tabari 8:8.

³ At - Tabari 8:8.

⁴ Hadithi zinazohusu kushushwa kwa aya hii hazina daraja ya sahihi.

Ali bin Abi Twalha amepokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, kipande hiki cha aya kinamhusu mtu ambaye yuko karibu na kufa na anatoa wasia mbaya katika mirathi na anakusudia kuwadhuru baadhi ya warithi halali, Allah تعالى Anaamrisha mwenye kuusia wasia huo amuogope Allah تعالى¹, mfano wake imepokewa kutoka kwa Mujahid na wengi wengine².

Sahihi mbili zimepokea kuwa wakati Mtume ﷺ alipomtembelea Sa`ad bin Abi Waqqaas رضي الله عنه wakati wa ugonjwa wake uliokuwa ukimsumbua, alimuambia Mtume ﷺ, 'Ewe Mtume ﷺ nina utajiri na sina wa kunirithi isipokuwa binti yangu, je naweza kutoa sadaka theluthi mbili ya mali yangu?' Akamjibu, "hapana" Akauliza. "Je nusu?" Mtume ﷺ akasema, "hapana" Saad akauliza "Je! theluthi?" Mtume ﷺ akasema,

«الثُّلُثُ، وَالثُّلُثُ كَثِيرٌ»

"Theluthi, na theluthi ni nyingi."

Mtume ﷺ kisha akasema,

«إِنَّكَ أَنْ تَذَرَ وَرَثَتَكَ أَغْنِيَاءَ خَيْرٌ مِنْ أَنْ تَذَرَهُمْ عَالَةً يَتَكَفَّمُونَ النَّاسَ»

"Hakika wewe kuwaacha watoto wako matajiri ni bora kuliko kuwaacha masikini wanawaomba watu".³

Onyo Kali Dhidi ya Wale Wanaotumia Mali za Mayatima

Pia ilisemwa kuwa aya hiyo:

وَلَا تَأْكُلُوهَا إِسْرَافًا وَبِدَارًا أَنْ يَكْبُرُوا

"Wala msiyale kwa fujo na pupa kwa kuwa watakuja kuwa watu wazima."

Inamaanisha kuwa na Taqwa ya Allah تعالى wakati wa kutunza mali za mayatima; kama Ibn Jarir رحمه الله تعالى alivyomsikia Al-Awfi ambaye alipokea maelezo haya kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما. Hii ni rai nzuri inatiwa nguvu kwa onyo

¹ At-Tabari 8:19.

² At-Tabari 8:19.

³ Fat'h Al-Bari 8:89.

linalofuata dhidi ya kula mali za mayatima kwa dhuluma. Katika hali hii inamaanisha kuwa kama utakavyotaka watoto wako watendewe haki baada yako basi na wewe watendee haki watu pindi utakapopewa majukumu ya kuwatunza.

Allah تعالى amesema kuwa wale ambao wanadhulumu kwa kula mali za mayatima watakula moto ndani ya matumbo yao; hivi ndivyo Allah تعالى Alivyosema:

إِنَّ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ أَمْوَالَ الْيَتَامَىٰ ظُلْمًا إِنَّمَا يَأْكُلُونَ فِي بُطُونِهِمْ نَارًا وَسَيَصْلَوْنَ

سَعِيرًا ﴿٧﴾

“Hakika wanaokula mali ya mayatima kwa dhulma, hapana shaka yoyote wanakula matumboni mwao moto, na wataingia Motoni.”

Inamaanisha pindi utakapokula mali za mayatima bila haki utakuwa umekula moto tu ambao utakuwasha siku ya ufufuo [kiyama].

Imepokewa na sahih mbili kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema;

«اجْتَنِبُوا السَّبْعَ الْمُوبِقَاتِ»

“Jiepusheni na madhambi saba yenye kuangamiza.”

Watu wakamuuliza, “Ewe Mtume ﷺ! Ni yapi hayo?” Akajibu,

«الشُّرْكَ بِاللهِ، وَالسُّخْرُ، وَفَتْلُ النَّفْسِ الَّتِي حَرَّمَ اللهُ إِلَّا بِالْحَقِّ، وَأَكْلُ الرِّبَا، وَأَكْلُ مَالِ الْيَتِيمِ، وَالتَّوَلَّى يَوْمَ الرَّحْفِ، وَقَذْفُ الْمُحْضَنَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ الْغَائِلَاتِ»

“Kumshirikisha Mwenyezi Mungu, uchawi, kuaa nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Ameiharamisha kuiua isipokuwa kwa haki (yake), kula riba, kula mali ya mayatima, kukimbia siku ya mapigano, na kuwasingizia wanawake waumini walioghafilika.”¹

¹ Fat-h Al-Bari 5:462, Muslim 1:92.

يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثِيَّاتِ ۚ فَإِنَّ كُنَّ نِسَاءً فَوْقَ اثْنَتَيْنِ فَلَهُنَّ ثُلُثَا مَا تَرَكَ ۚ وَإِنْ كَانَتْ وَاحِدَةً فَلَهَا النِّصْفُ ۚ وَلِأَبَوَيْهِ لِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا أَلْسُدُسٌ مِّمَّا تَرَكَ إِنْ كَانَ لَهُ وَوَلَدٌ ۚ فَإِنْ لَمْ يَكُنْ لَهُ وَلَدٌ وَوَرِثَهُ أَبُوَاهُ فَلِلْمُتَّكِئَةِ ۚ فَإِنْ كَانَ لَهُ إِخْوَةٌ فَلِلْمُتَّكِئَةِ أَلْسُدُسٌ ۚ مِنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصَىٰ بِهَا أَوْ دِينٍ ۚ ءَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ لَا تَدْرُونَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ لَكُمْ نَفْعًا فَرِيضَةٌ مِنَ اللَّهِ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١١﴾

11. "Mwenyezi Mungu Anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili. Na ikiwa wanawake zaidi ya wawili, basi watapata thuluthi mbili za alichokiacha maiti. Lakini ikiwa mtoto mwanamke ni mmoja, basi fungu lake ni nusu. Na wazazi wake wawili, kila mmoja wao apate sudusi ya alichokiacha, ikiwa anaye mtoto. Akiwa hana mtoto, na wazazi wake wawili wamekuwa ndio warithi wake, basi mama yake atapata thuluthi moja. Na akiwa anao ndugu, basi mama yake atapata sudusi. Haya ni baada ya kutolewa alichokiacha au kulipa deni. Baba zenu na watoto wenu, nyinyi hamjui ni nani baina yao aliye karibia zaidi kwenu kwa manufaa. Hiyo ni Sharia iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu. Bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye Hekima."

Kuamrisha Mirathi na Kuhimizwa Kujifunza Elimu Yake.

Ayah hii, na ya mwisho katika surah hii zina elimu ya *Al-Faraidh* (Mirathi) Elimu ya *Al-Faraidh* inapatikana ndani ya Ayat hizi tatu na kutoka katika hadithi juu ya somo hili. Imetiliwa nguvu kujifunza elimu hii hususani mambo mahsusali yaliyotajwa ndani ya Aya hizo. Ibn Uaynah alisema; Maarifa juu ya *Al-Faraidh* iliitwa ni nusu ya elimu, kwa sababu inawahusu watu wote.

Sababu za Kushushwa Aya 4:11

Alipoelezea Aya hii, Bukhari aliandika kuwa Jabir bin Abdullah رضى الله عنه alisema Mtume ﷺ alikuja kwangu kwa miguu akifuatana na Abubakar رضى الله عنه katika makazi ya Banu Salamah, hali ya kuwa wakitembea kwa miguu na Mtume ﷺ

alinikuta sina fahamu. Aliomba maji, akatawadhia, kisha akanimwagia, na nikapata fahamu. Nikamuambia, "Uniamuru niifanyie nini mali yangu, ewe Mjumbe wa Allah?" Baadaye Aya hii iliteremshwa,

يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثِيَّاتِ

"Mwenyezi Mungu Anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili."

Hivi ndivyo ilivyopokelewa na Muslim² na An-Nasai.³ Pia wakusanyaji sita wa Hadithi waliikusanya hadithi hii.⁴

Hadithi Nyingine Iliyopokelewa kutoka kwa Jabir رضي الله عنه Inayoelezea Sababu za Kuteremshwa Aya 4:11.

Ahmad alipokea kutoka kwa Jabir رضي الله عنه kuwa alisema "Mkewe Sa'ad Bin Ar-Rabi alifika kwa Mtume ﷺ na akamuambia, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Hawa ni mabint wawili wa Sa'ad Bin Ar-Rabi, aliyekuwa pamoja nawe na kuuliwa shahidi katika Uhud. Ammi yao alichukua mali yao na hokusaza chochote kwa ajili yao." Mtume ﷺ akasema "Allah Ataamua juu ya kadhia hii." Aya kuhusu mirathi iliteremshwa baadaye na Mtume ﷺ alimtumia ujumbe Ammi yao akimuamuru,

«أَعْطِ ابْنَتِي سَعْدِ التَّائِبِينَ، وَأُمَّهُمَا التُّمْنَ، وَمَا بَقِيَ فَهُوَ لَكَ»

"Wape mabint wa Sa'ad theluthi mbili ya mali ya baba yao, na moja ya nane, mpe mama yao yao, na kitakachosalia ni chako."⁵

Abu Dawud,⁶ Al-Tirmidhi⁷ na Ibn Majah⁸ waliikusanya Hadithi hii. Hata hivyo ni dhahiri kuwa hadithi ya kwanza kutoka kwa Jabir رضي الله عنه ilikuwa juu ya

¹ Fat'hul Al-Bari 8:91.

² Muslim 3:1235.

³ An-Nasai katika Al-Kubra 6:320.

⁴ Fat'hul Al-Bari 1:118; 8:91, Muslim 3:1234; Abu Dawud 3:308; Tuhfat Al-Ahwadhi 8:368, An-Nasai 1:77, Ibn Majah 2:911.

⁵ Ahmad 3:352.

⁶ Abu Dawud 3:314.

⁷ Tuhfatul Al-Ahwadhi 6:267.

⁸ Ibn Majah 2:908.

suala la Aya ya mwisho ya Surah (4:176 kuliko 4:11), kwani wakati wa tukio hilo, Jabir رضي الله عنه alikuwa na dada na hakuwa na mabinti wala wazazi wa kumrithi, pamoja na hayo tumeitaja Hadithi hapa kama alivyofanya Bukhari. Hadithi ya pili kutoka kwa Jabir inafanana na sababu ya kuteremka aya hii.

Watoto Hurithishwa kwa Kuzingatia Wanaume Wanapata Sehemu Mbili na Wanawake Wanapata Sehemu Moja ya Mirathi.

Allah تعالى Amesema,

يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثِيَّاتِ

“Mwenyezi Mungu Anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili.”

Allah تعالى Anaamrisha; watendeeni haki watoto wenu. Watu katika enzi za Jahiliyyah, walikuwa wakiwapa watoto wa kiume lakini sio wa kike. Kwa hiyo Allah تعالى Amefaradhisha wote; wanaume na wanawake wapate fungu katika mirathi, japokuwa fungu la mwanaume ni sawa na mafungu mawili ya mwanamke; kuna tofauti kwa sababu wanaume wanahitaji kuzikimu familia, kufanya miradi ya kibiashara, kufanya kazi na kutimiza majukumu yao.

Hivyo wanaume wanapata mafungu mawili ya mirathi ya yale wayapatayo wanawake.

Kauli ya Allah تعالى,

يُوصِيكُمُ اللَّهُ فِي أَوْلَادِكُمْ لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثِيَّاتِ

“Mwenyezi Mungu Anakuusieni juu ya watoto wenu: Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili.”

Inathibitisha ukweli kuwa Allah تعالى ni Mrehemevu sana kwa watoto kuliko walivyo wazazi wao. Anawaamuru wazazi wawatendee uadilifu wana wao.

Hadithi sahihi inaeleza kuwa mjakazi alikuwa akimtafuta mwanae na alipompata alimkumbatia, akamnyonyesha na kumsafisha, baada ya kuona hili Mtume ﷺ aliwaambia Masahaba zake,

«أَتُرُونَ هَذِهِ طَارِحَةً وَلَدَهَا فِي النَّارِ وَهِيَ تَقْدِرُ عَلَى ذَلِكَ؟»

“Mnadhani mwanamke huyo anaweza kumtupia motoni mwanae kwa hiari yake?, ingawa uwezo wa kufanya hivyo anao?”

Wakamjibu, “Hapana, Ewe Mtume ﷺ.” Akasema,

«قَوْلَ اللَّهِ نَحْمُ أَرْحَمُ بِعِبَادِهِ مِنْ هَذِهِ بِوَلَدِهَا»

“Wallah! Allah Anawahurumia zaidi waja wake kuliko mama huyu anavyomhurumia mtoto wake.”¹

Bukhari alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, Desturi (katika zama za Jahiliya) kama kuna mali ya marehemu, wangelirithi kwa usia wa marehemu. Kisha Allah تعالى alifuta kila alichousia kwa mujibu wa mila na desturi na Akafaradhisha kuwa mwanaume apate mara mbili ya mirathi ya mwanamke, na kwa kila mzazi apate sudusi (1/6), na mke apate moja ya nane (1/8) au robo (1/4) na mume apate nusu au robo (1/4).²

Fungu la Mabinti Wanapokuwa Peke Yao.

Allah تعالى Amesema,

فَإِنْ كُنَّ نِسَاءً فَوْقَ آئْتِنَيْنِ فَلَهُنَّ ثُلُثَا مَا تَرَكَ

“Ikiwa wanawake zaidi ya wawili, basi watapata thuluthi mbili za alichu kiacha marehemu.”

Tunalazimika kutaja hapa kuwa badhi ya watu wanasema kuwa Ayah imekusudia mabinti wawili tu, na kuwa neno “zaidi” halihitajiki ambapo sio kweli. Hapana kitu ndani ya Qur’an ambacho hakifai au ni zaidi. Ingekuwa Ayah inazungumza wanawake wawili tu, ingesema, “Mafungu ya wote wawili ni theluthi mbili.”

Ama kwa mabinti, wawili au zaidi, hukumu ya kupata theluthi mbili ilitokana na Aya hii. Kadhalika kupitia hukumu ya aya ya mwisho katika sura hii iliyozeleza kuwa dada wawili wanapata theluthi mbili. Allah تعالى Amehukumu kuwa dada wanapata theluthi mbili. Kama dada wawili wanapata theluthi mbili, basi mabinti wawili wana haki zaidi ya kupata theluthi mbili. Pia tumetaja hadithi

¹ Muslim 4:2109.

² Fat’hul Al-Bari 8:93.

huko nyuma iliyosimuliwa na Jabir رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ aliamuru theluthi mbili iwe ni fungu la mabinti wawili wa Sa'ad bin Ar-Rabi رضي الله عنه. Hivyo hii imethibitishwa ndani ya Kitabu na Sunnah. Kadhalika Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ كَانَتْ وَاحِدَةً فَلَهَا النِّصْفُ

“Lakini akiwa mtoto mwanamke ni mmoja, basi fungu lake ni nusu.”

Kama ingekuwa mabinti wawili wanapata nusu basi aya ingelitaja hilo. Lakini kwa kupewa binti mmoja akiwa peke yake fungu la nusu hii imeonesha kuwa mabinti wawili wako katika hukumu sawa na mabinti watatu (Yaani watapata 2/3 ya mali) theluthi mbili. Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi.

Mafungu ya Wazazi katika Mirathi.

Allah تعالى Amesema,

وَلِأَبْوَيْهِ لِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا الشُّدُوسُ

“Na wazazi wake wawili, kila mmoja wao apate sudusi.”

Kuwepo kwao kutapunguza kasma ya mama, lakini wao hawatorithi. Iwapo kuna kaka mmoja fungu la mama litasalia kuwa theluthi moja, lakini fungu lake litapungua iwapo kuna kaka zaidi ya mmoja. Wanazuoni wanasema kuwa, “sababu ya kupunguzwa kasma ya mama kutoka theluthi kuwa sudusi ni kwa kuwa baba ndiye anayewasaidia kaka na dada wa marehemu katika mambo ya Harusi, kwa kutumia gharama zake. Wakati mama hatumii mali yake katika kuwaozesha.” Rai hii ina mashiko.

Kutanguliza Deni, Kisha Wasia, Kabla ya Urithi.

Allah تعالى Anasema,

مِنْ بَعْدِ وَصِيٍّ يُوصِي بِهَا أَوْ دِينٍ

“Haya ni baada ya kutolewa alichu usia au kulipa deni.”

Wanazuoni wa *Salaf* na *Khalaf* wanakubaliana kulipa madeni kufanywa kabla ya kutekeleza Wasia, na hili liko wazi kwa wale wanaozisoma Ayah kwa idhari. Kisha Allah تعالى Akasema,

ءَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ لَا تَدْرُونَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ لَكُمْ نَفَعًا

“Baba zenu na watoto wenu, nyinyi hamjui ni nani baina yao aliye karibu zaidi kwenu kwa manufaa...”

Maana yake: Tumepanga mafungu kwa wazazi na watoto kinyume na ada ya Jahiliyyah na mwanzoni mwa Uislamu, ambapo urithi ungekwenda kwa watoto na wazazi wangepata hisa iwapo waliusiwa, kama Ibn Abbas رضي الله عنهما alivyotaja. Allah تعالى Alifuta ada hii Akafaradhisha mafungu mahususi kwa watoto na wazazi. Mmoja wenu anaweza kupata manufaa duniani au akhera kutokana na wazazi wake, ambapo asingeweza kupata kutoka kwa watoto wake kinyume chake pia kinayumkinika. Allah تعالى Amesema,

ءَابَاؤُكُمْ وَأَبْنَاؤُكُمْ لَا تَدْرُونَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ لَكُمْ نَفْعًا

“Baba zenu na watoto wenu, nyinyi hamjui ni nani baina yao aliye karibu zaidi kwenu kwa manufaa...”

Kwa kuwa manufaa yanaweza kutoka kwa mmoja au jamaa au jamaa wengine. Tumepanga kasma maalumu kwa kila mmoja, Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi;

فَرِيضَةٌ مِّنَ اللَّهِ

“Hiyo ni Sharia iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Mafungu hayo ya mirathi tuliyoyataja na ambayo huwapa warithi mafungu makubwa kuliko wengine, ni Amri kutoka kwa Allah تعالى Aliyoamua na kufaradhishwa.

إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١١﴾

“Bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye hekima.”

Ambaye kila kitu Amekipa nafasi yake na kila mmoja Amempa hisa iliyomstahiki.

* * *

* وَلَكُمْ نِصْفُ مَا تَرَكَ أَزْوَاجُكُمْ إِن لَّمْ يَكُن لَّهُنَّ وَلَدٌ
 ۚ فَإِن كَانَ لَّهُنَّ وَلَدٌ فَلَكُمْ أَلْرُبْعُ مِمَّا تَرَكَنَّ مِن
 بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِيَنَّ بِهَا أَوْ دِينٍ ۗ وَلَهُنَّ أَلْرُبْعُ مِمَّا
 تَرَكَتُمْ إِن لَّمْ يَكُن لَّكُمْ وَلَدٌ ۚ فَإِن كَانَ لَكُمْ وَلَدٌ
 فَلَهُنَّ أَلْثُمُن مِمَّا تَرَكَتُمْ ۚ مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ تُوصُونَ بِهَا
 أَوْ دِينٍ ۗ وَإِن كَانَ رَجُلٌ يُورَثُ كَلِئَلَةً أَوْ امْرَأَةً وَوَلَهُ أَخٌ
 أَوْ أُخْتٌ فَلِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا أَلْسُدُسٌ ۚ فَإِن كَانُوا أَكْثَرَ
 مِن ذَٰلِكَ فَهُمْ شُرَكَآءُ فِي أَلْثُمَتِ ۚ مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصَى
 بِهَا أَوْ دِينٍ غَيْرِ مُضَآرٍّ ۗ وَصِيَّةٌ مِّنَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَلِيمٌ ﴿١٢﴾
 تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ ۗ وَمَن يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ
 جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا أَلْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ
 وَذَٰلِكَ أَلْفَوْزٌ أَلْعَظِيمُ ﴿١٣﴾ وَمَن يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ
 وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ عَذَابٌ
 مُّهِينٌ ﴿١٤﴾

* وَلَكُمْ نِصْفُ مَا تَرَكَ أَزْوَاجُكُمْ
 ۚ إِن لَّمْ يَكُن لَّهُنَّ وَلَدٌ ۚ فَإِن كَانَ
 لَهُنَّ وَلَدٌ فَلَكُمْ أَلْرُبْعُ مِمَّا
 تَرَكَنَّ ۚ مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِيَنَّ
 بِهَا أَوْ دِينٍ ۗ وَلَهُنَّ أَلْرُبْعُ مِمَّا
 تَرَكَتُمْ إِن لَّمْ يَكُن لَّكُمْ وَلَدٌ ۚ
 فَإِن كَانَ لَكُمْ وَلَدٌ فَلَهُنَّ أَلْثُمُن
 مِمَّا تَرَكَتُمْ ۚ مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ تُوصُونَ
 بِهَا أَوْ دِينٍ ۗ وَإِن كَانَ رَجُلٌ يُورَثُ
 كَلِئَلَةً أَوْ امْرَأَةً وَوَلَهُ أَخٌ أَوْ أُخْتٌ
 فَلِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا أَلْسُدُسٌ ۚ
 فَإِن كَانُوا أَكْثَرَ مِن ذَٰلِكَ فَهُمْ
 شُرَكَآءُ فِي أَلْثُمَتِ ۚ مِن بَعْدِ وَصِيَّةٍ
 يُوصَى بِهَا أَوْ دِينٍ غَيْرِ مُضَآرٍّ ۗ وَصِيَّةٌ
 مِّنَ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَلِيمٌ ﴿١٢﴾

12. "Na fungu lenu ni nusu walichoacha wake zenu ikiwa hawana mtoto. Wakiwa na mtoto basi fungu lenu ni robo ya walichoacha, baada ya wasia waliyo usia au kulipa deni. Na wake zenu watapata robo mlichokiacha, ikiwa hamna mtoto. Mkiwa mna mtoto basi sehemu yao ni thumni ya mlichokiacha, baada ya wasia mliousia au kulipa deni. Na ikiwa mwanamume au mwanamke anayerithiwa hana mtoto wala wazazi, lakini anaye ndugu mume au ndugu mke, basi kila mmoja katika hawa atapata sudusi. Na wakiwa zaidi kuliko hivyo basi watashirikiana katika thuluthi, baada ya wasia ulio usiwa au kulipa deni, pasipo kuleta dhara. Huu ndio wasia uliotoka kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mpole".

Mirathi ya Wanandoa

Allah تعالى Anamuambia mume, utapata nusu ya kila kilichoachwa na mkeo atakapofariki dunia na hakuwa na mtoto. Pindipo angekuwa na mtoto, utapata robo ya kile alichokiacha, baada ya kulipa mali aliyoachiwa ambayo iliandikwa wasia au madeni yake. Tulitangulia kusema, karadha hulipwa mwanzo kisha wasia na baadaye mirathi. Wanazuoni wote wanakubaliana katika hili. Kanuni hii inawahusu pia watoto na wajukuu, hata kama ni vilembwe (au hata vizazi vya mbali). Allah تعالى Amesema,

وَلَهُنَّ الْرُّبُعُ مِمَّا تَرَكْتُمْ

“Na wake zenu watapata robo ya mlichokiacha.”

Na iwapo kuna mke zaidi ya mmoja, wote watagawana robo au moja ya nane apatayo mke. Kabla ya hapo tulieleza Kauli ya Allah تعالى,

مِّنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ تُوصُونَ بِهَا

“Baada ya wasia mliusia.”

Maana ya Kalalah

Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ كَانَ رَجُلٌ يُورَثُ كَلِالَةً

“Na ikiwa mwanamume au mwanamke anayerithiwa hana mtoto.”

Kalalah ni mnyumbulisho wa *Ikli*; taji livaliwalo kichwani. Maana ya *Kalalah* katika Ayah hii ni warithi wa mtu wanaotoka katika daraja la pili la ndugu. Ash-Shabi ameandika kuwa Abubakar As-Siddiq رضي الله عنه aliulizwa juu ya *Kalalah*, akajibu, “Nitatoa rai yangu kuhusu hilo, na ikiwa nimesibu, basi usahihi huo ni kutoka kwa Allah تعالى. Hata hivyo kama rai yangu si sahihi litakuwa ni kosa langu kwa sababu ya juhudi za shaytan, na Allah تعالى pamoja na mjumbe wake hawahusiki nalo, *kalalah* inahusu mtu asiye na wazazi wala watoto. “Umar رضي الله عنه alipochaguliwa kuwa Khalifah, alisema, “Nachelea kusigana na rai ya Abubakari رضي الله عنه.”¹ Hadithi hii iliandikwa na Ibn Jarir na wengine.

¹ At - Tabari 8:55-57.

Katika Tafsiri yake Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Nilikuwa miongoni mwa watu wa mwisho kumuona Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه na nikamsikia akisema, "Uliyoyasema ni maoni sahihi.' Nikamuuliza, "Kwani nilisema nini?" Akajibu, "Kuwa *Kalalah* muradi wake ni mtu asiye na mtoto au wazazi."¹ Hii pia ni rai ya Ali bin Abi Talib, Ibn Masud, Ibn Abbas, Zayd bin Thabit, Ash-Shabi, An-Nakhai, Al-Hassan Al-Basri, Qatadah, Jabir bin Zayd na Al-Hakam رضي الله عنهم.² Aidha hii ni rai ya watu wa Madina, Kufah, Basrah na Mafakihi saba,³ Maimamu wanne na wanazuoni wengi wa zama zilizopita na za sasa. Imepelekea baadhi ya wanazuoni kutamka kuwa ni rai iliyokubaliwa na wengi.

Hukumu Kuhusu Watoto wa Mama ambao Hakuwazaa na Marehemu

Allah تعالى Amesema:

وَلَهُدَّ أَخٌ أَوْ أُخْتٌ

"Lakini anaye ndugu mume au ndugu mke..."Maana yake kutoka upande wa mama, kama walivyosema baadhi ya *Salaf*, ikiwa ni pamoja na Sa'd bin Abi Waqqas رضي الله عنه. Kadhalika Qatadah alisema kuwa hii ni kauli ya Abubakar As-Siddiq رضي الله عنه.

فَلِكُلِّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا آلسُدُسُ فَإِن كَانُوا أَكْثَرَ مِن ذَٰلِكَ فَهُمْ شُرَكَاءُ فِي الثُّلُثِ

"Basi kila mmoja katika hawa atapata sudusi. Na wakiwa zaidi kuliko hivyo basi watashirikiana katika thuluthi."

Kuna tofauti baina ya kaka wa kambo kutoka kwa mama na warithi waliosalia. Wanarithi pamoja na yule aliyewaunganisha (kuwafikisha) katika urithi, yaani mama. Pili, wanaume na wanawake katika wao wanapata kasma iliyo sawa. Tatu, wana mafungu katika mirathi endapo mali ya marehemu itarithiwa kwa *kalalah*. Kwani hawana fungu pindipo maiti amemuacha Baba, Babu, Mtoto au Mjukuu. Nne, hawapati zaidi ya thuluthi, bila kujali idadi yao ya wanaume na wanawake. Kauli ya Allah تعالى,

¹ At - Tabari 8:59.

² At - Tabari 8:55 – 57.

³ Sa'id bin Al-Musayyib (Alikufa 94 H); 'Ur'wah bin Az-Zubayr (alikuwa 94 H) Abu Bakar bin Abdur-Rahman bin Al-Harith bin Hisham Al-Mukhazumi (alikuwa 94 H); Ubaydullah bin Abdullah bin Zayd bin Thabit (Alikufa 99 H); Al-Qasim bin Muhammad bin Abu Bakar (Alikufa 104 H); Sulayman bin Yasar (Alikufa 107 H).

مِنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصِي بِهَا أَوْ دَيْنٍ غَيْرِ مُضَارٍّ

“Baada ya wasia ulio usiwa au kulipa deni, pasipo kuleta dhara.”

Maana yake: Hati ya wasia iwe ya kiuadilifu na isilete madhara, kama kuwapokonya baadhi ya warithi haki zao zote au sehemu au kuzidisha viwango Alivyoamrisha Allah تعالى kwa baadhi ya warithi. Atakayefanya hivyo atakuwa amepinga Maamuzi ya Allah تعالى kuhusu ugawaji. Hadithi sahihi inasema, Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ اللَّهَ قَدْ أَعْطَى كُلَّ ذِي حَقٍّ حَقَّهُ فَلَا وَصِيَّةَ لِي وَارِثٍ»

“Hakika Allah Amempa kila mwenye haki, haki yake. Kwa hiyo hapana wasia kwa mrithi.”¹

تِلْكَ حُدُودُ اللَّهِ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ يُدْخِلْهُ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

خَالِدِينَ فِيهَا ۚ وَذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ ﴿١٣﴾ وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدَّ

حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ عَذَابٌ مُهِينٌ ﴿١٤﴾

13. Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anaye mtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Yeye atamtia katika Pepo zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na huko ndiko kufuzu kukubwa.

14. Na anayemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akaipindukia mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) Atamtia Motoni adumu humo, na atapata adhabu ya kudhalilisha.

Indhari Dhidi ya Kuchupa Mipaka ya Mirathi

Maana yake ni kuwa *Faraidh* na kasma hizi Alizoziweka Allah تعالى kwa warithi ni kwa mujibu wa ukuruba wa mahusiano na marehemu na mahitajio yao na kukosekana kwake. Hivyo msitende kinyume na hayo. Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ

“Na anaye mtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake.”

¹ Abu Dawud Na.2870, At-Tirmidhi Na.2121, 2122; An-Nasai Na.3673, Ibn Majah Na.2712 na 2713.

Kuhusu mirathi, na hapunguzi wala kuongeza mafungu yaliyopangwa kwa kutumia hila na mizonge. Bali ameiacha vile Alivyoihukumu na kuigawa Allah تعالى. Kiila mmoja anampa kasma yake kama Alivyoamuru Allah تعالى na Kuthibitisha.

يُدْخِلُهُ جَنَّتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ وَذَٰلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ
 ﴿١٣﴾ وَمَنْ يَعِصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَيَتَعَدَّ حُدُودَهُ يُدْخِلْهُ نَارًا خَالِدًا فِيهَا وَلَهُ
 عَذَابٌ مُهِينٌ ﴿١٤﴾

“...Yeye Atamtia katika Pepo zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na huko ndiko kufuzu kukubwa. Na anaye muasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akaipindukia mipaka Yake, (Mwenyezi Mungu) Atamtia Motoni adumu humo, na atapata adhabu ya kudhalilisha.”

Hii ni kwa sababu alitengua Aliyofaradhisha Allah تعالى na akakanusha Hukumu Yake. Kwa hakika, huu ni mwenendo wa watu wasioridhia namna Alivyoamua Allah تعالى, na kwa ajili hiyo Allah تعالى Atawaadhibu kwa Kuwadhalilisha katika adhabu chungu ya milele.

Imam Ahmad aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa, Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْخَيْرِ سَبْعِينَ سَنَةً، فَإِذَا أَوْصَى حَافٍ فِي وَصِيَّتِهِ،
 فَيُخْتَمُ لَهُ بِشَرِّ عَمَلِهِ، فَيَدْخُلُ النَّارَ، وَإِنَّ الرَّجُلَ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الشَّرِّ سَبْعِينَ سَنَةً،
 فَيَعْدِلُ فِي وَصِيَّتِهِ فَيُخْتَمُ لَهُ بِخَيْرِ عَمَلِهِ فَيَدْخُلُ الْجَنَّةَ»

“Hakika Mtu anayefanya amali njema kwa miaka sabini, lakini unapofika wakati wa kuandaa wasia huingia makosani. Hivyo kazi yake ya mwisho huwa mbovu, na hivyo hutupwa Motoni. Mtu anaweza kutenda amali za watu waovu kwa miaka sabini, hata hivyo akifanya uadilifu katika wasia wake. Amali yake ya mwisho ikawa ni njema, na kwa ajili hiyo ataingizwa Peponi.”

Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Soma, kama ukipenda,

تَلَاكَ حُدُودَ اللَّهِ

“Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu.” Mpaka,

عَذَابٌ مُّهِينٌ

“Adhabu ya kudhalilisha.”¹

«إِنَّ الرَّجُلَ لَيَعْمَلُ - أَوْ الْمَرْأَةُ - بِطَاعَةِ اللَّهِ سِتِينَ سَنَةً، ثُمَّ يَحْضُرُهُمَا الْمَوْتُ،
فِيضَارَانِ فِي الْوَصِيَّةِ، فَتَجِبُ لَهُمَا النَّارُ»

“Hakika mwanamume au mwanamke watamtii Allah kwa miaka sitini. Kisha watafikiwa na mauti, watakhini katika wasia na hivyo kuingizwa Motoni.”

Kisha Abu Hurayrah رضي الله عنه akasoma:

مِنْ بَعْدِ وَصِيَّةٍ يُوصَى بِهَا أَوْ دَيْنٍ غَيْرِ مُضَارٍ

“Baada ya wasia ulio usiwa au kulipa deni, pasipo kuleta dhara.”

Mpaka

وَذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

“Na huko ndiko kufuzu kukubwa.”²

Pia ameipokea At-Tirmidhi³ na Ibn Majah,⁴ na At-Tirmidhi amesema, *“Hasan Gharib.”* Upokezi wa Imam Ahmad juu ya Hadithi hiyo ni kamilifu zaidi na timilifu.

* * *

¹ Ahmad 2:274.

¹ Abu Dawud 3:288.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:304.

³ Ibn Majah 2:902.

وَأَلَّتِي يَأْتِينَ الْفَاحِشَةَ مِنْ نِسَائِكُمْ فَاسْتَشْهَدُوا عَلَيْهِنَّ
 أَرْبَعَةً مِنْكُمْ فَإِنْ شَهِدُوا فَأَمْسِكُوهُنَّ فِي الْبُيُوتِ حَتَّى
 يَتَوَفَّيَهُنَّ الْمَوْتُ أَوْ يَجْعَلَ اللَّهُ لَهُنَّ سَبِيلًا ﴿١٥﴾ وَالَّذِينَ
 يَأْتِيهِمَا مِنْكُمْ فَكَاذُوهُمَا فَإِنْ تَابَا وَأَصْلَحَا فَأَعْرِضُوا
 عَنْهُمَا إِنَّ اللَّهَ كَانَ تَوَّابًا رَحِيمًا ﴿١٦﴾ إِنَّمَا التَّوْبَةُ عَلَى
 اللَّهِ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السُّوءَ بِجَهْلَةٍ ثُمَّ يَتُوبُونَ مِنْ قَرِيبٍ
 فَأُولَئِكَ يَتُوبُ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٧﴾
 وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ حَتَّى إِذَا حَضَرَ
 أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ إِنِّي تُبْتُ الْفَنِّ وَلَا الَّذِينَ يَمُوتُونَ
 وَهُمْ كُفَّارٌ أُولَئِكَ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٨﴾ يَأْتِيهَا
 الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرْتُوا النِّسَاءَ كَرْهًا وَلَا
 تَعْضُلُوهُنَّ لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَا ءَاتَيْتُمُوهُنَّ إِلَّا أَنْ يَأْتِيَنَّ
 بِفَحِشَةٍ مُبِينَةٍ وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ فَإِنْ كَرِهْتُمُوهُنَّ
 فَعَسَى أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَيَجْعَلَ اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيرًا ﴿١٩﴾

وَأَلَّتِي يَأْتِينَ الْفَاحِشَةَ مِنْ
 نِسَائِكُمْ فَاسْتَشْهَدُوا عَلَيْهِنَّ أَرْبَعَةً
 مِنْكُمْ فَإِنْ شَهِدُوا فَأَمْسِكُوهُنَّ
 فِي الْبُيُوتِ حَتَّى يَتَوَفَّيَهُنَّ الْمَوْتُ أَوْ
 يَجْعَلَ اللَّهُ لَهُنَّ سَبِيلًا ﴿١٥﴾ وَالَّذِينَ
 يَأْتِيهِمَا مِنْكُمْ فَكَاذُوهُمَا فَإِنْ
 تَابَا وَأَصْلَحَا فَأَعْرِضُوا عَنْهُمَا إِنَّ
 اللَّهَ كَانَ تَوَّابًا رَحِيمًا ﴿١٦﴾

15. Na amba wanafanya uchafu miongoni mwa wanawake wenu, washuhudilieni watu wane katika nyinyi. Watakaposhuhudia, basi wazuieni majumbani mpaka wafishwe na mauti au Mwenyezi Mungu Awatolee njia nyingine.

16. Na wawili kati yenu wafanyao hayo waadhibuni. Na wakitubia wakatengenea basi waacheni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kupokea toba, Mwenye Kurehemu.

Amri ya Kumzuilia Mzinifu Mwanamke Nyumbani Kwake, Hukumu hii Ilifutwa Baadaye.

Mwanzoni mwa Uislamu, mwanamke aliyezini na ikathibiti kuwa amezini, alizuiwa nyumbani kwake asitoke mpaka afikwe na mauti.

Allah تعالى Amesema,

وَأَلَّتِي يَأْتِينَ الْفَاحِشَةَ مِنْ نَسَائِكُمْ فَاسْتَشْهِدُوا عَلَيْهِنَّ أَرْبَعَةً مِّنْكُمْ ۖ فَإِن شَهِدُوا
فَأَمْسِكُوهُنَّ فِي الْبُيُوتِ حَتَّىٰ يَتَوَفَّيَهُنَّ الْمَوْتُ أَوْ يَجْعَلَ اللَّهُ لَهُنَّ سَبِيلًا ﴿١٥﴾

“Na ambao wanafanya uchafu miongoni mwa wanawake wenu, washuhudizieni watu wane katika nyinyi. Watakaposhuhudia, basi wazuieni majumbani mpaka wafishwe na mauti au Mwenyezi Mungu Awatolee njia nyingine.”

“Njia nyingine.” kama ilivyotajwa katika aya ni naskhi ya hukumu iliokuja baadaye. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Hukumu ya mwanzo ilikuwa ni hiyo mpaka Allah تعالى Aliposhusha Surat Nuur (sura ya 24) ambayo ilifuta hukumu hiyo na badala yake ikawa kumpiga viboko (mzinifu asiyeoa au asiyeolewa) au kurujumiwa mpaka kufa (mzinifu aliyeoa au kuolewa).”

Pia ilipokewa kutoka kwa Ikrimah, Said bin Jubayr, Al-Hasan, Ata Al-Khurasani, Abu Salih, Qatada, Zayd bin Aslam na Adh-Dhahhak, alisema kuwa hukumu hii ilifutwa na hili ni jambo lenye kuwafikiwa. Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه alisema, “Wakati wahyi ukimshukia Mtume ﷺ ulimuathiri na kupata kishindo kwa huo Wahyi na uso wake ulionesha alama ya uchovu.”

“Siku moja Allah تعالى Alimteremshia wahyi, na Mtume ﷺ alipoondokewa na machovu, alisema,

«خُذُوا عَنِّي، فَذَجَعَلَ اللَّهُ لَهُنَّ سَبِيلًا، الثَّيْبُ بِالثَّيْبِ، وَالْبِكْرُ بِالْبِكْرِ، الثَّيْبُ جَلْدٌ
بِائَةٍ، وَرَجْمٌ بِالْحِجَارَةِ، وَالْبِكْرُ جَلْدٌ مِائَةً ثُمَّ نَفِي سَنَةٍ»

“Chukueni kutoka kwangu: Allah Amewafanyia njia nyingine kwa asiyeoa na asiyeolewa. Aliyeoa au kuolewa atapigwa bakora mia moja na atarujumiwa mpaka afe, ambapo asiyeoa na asiyeolewa wataandikwa bakora mia na kisha kuhamishwa kwa mwaka.”¹

Muslim na wakusanyaji wengine wa sunan waliandika kuwa Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Ahmad 5:317.

«خُذُوا عَنِّي خُذُوا عَنِّي، قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لَهِنَّ سَيْلًا، الْبِكْرُ بِالْبِكْرِ جَلْدٌ مِائَةٌ وَتَغْرِيْبٌ
غَامٌ، وَالتَّيْبُ بِالتَّيْبِ جَلْدٌ مِائَةٌ وَالرَّجْمُ»

“Chukueni kutoka kwangu, chukueni kutoka kwangu. Allah Kawafanyia njia nyingine. Wasiooa au kuolewa wanacharazwa bakora mia moja na kuhamishwa kwa mwaka mmoja, ambapo walio oa au kuolewa wanapigwa bakora mia moja na kupigwa mawe mpaka wafe.”¹ At-Tirmidhi amesema ni “Hassan sahih”.

Allah تعالی Anasema,

وَالَّذَانِ يَأْتِيْنَهَا مِنْكُمْ فَكَادُوْهُمَا

“Na wawili kati yenu wafanyao hayo waadhibuni.”

Maana yake: Wawili miongoni mwao watakaofanya uovu wataadhibiwa. Ibn Abbas na Said bin Jubayr رضي الله عنهما na wengine pia wamesema kuwa adhabu hii ni pamoja na kuwalaani, kuwazomea na kuwapiga kwa makubadhi.² Hii ndiyo iliyokuwa hukumu mpaka Allah تعالی Alipoibadili na kuja hukumu ya kupiga bakora au kurujumu, kama ilivyoenezwa. Mujahid anasema, “Iliteremshwa kuhusu kadhia ya wanaume wawili.”³ Kama alikuwa akizungumzia watu wakifanya Liwati, na Allah تعالی Ndiye Mjuzi wa yote. Wakusanyaji wa Sunan waliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ رَأَىئُمُوهُ يَعْْمَلُ عَمَلٌ لُّوطٍ، فَاقْتُلُوا الْفَاعِلَ وَالْمَفْعُولَ بِهِ»

“Mtakayemshika anafanya amali ya kaumu Lut (Liwati) muuweni mtenda na mtendewa.”⁴

Allah تعالی Amesema,

فَإِنْ تَابَا وَأَصْلَحَا

“Na wakitubia wakatengenea.” Kwa kuwacha vitendo viovu na baada ya hapo wakafanya amali njema.

¹ Muslim 3:1316, Abu Dawud 4:570, Tuhfat Al-Ahwadhi 4:705, An-Nasai katika Al-Kubwa 4:270, Ibn Majah 2:852.

² At - Tabari 8:85.

³ At - Tabari 8:82.

⁴ Abu Dawud 4:607, Tuhfat Al-Ahwadhi 5:21, An-Nasai katika Al-Kubwa 4:322, Ibn Majah 2:856.

فَأَعْرِضُوا عَنْهُمَا

"Basi waacheni."

Msiwasimange, msiwasumbue baada ya hapo, kwani Yule atubiaye ni sawa na mtu asiye na dhambi.

إِنَّ اللَّهَ كَانَ تَوَّابًا رَّحِيمًا ﴿١٧﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kupokea toba, Mwenye Kurehemu."

Hadithi ifuatayo imethibiti kuwa ni Sahihi ndani ya Sahihi Mbili:

«إِذَا زَنْتَ أُمَّةً أَحَدِكُمْ، فَلْيَجْلِدْهَا الْحَدَّ، وَلَا يَنْزُبْ عَلَيْهَا»

*"Atakapozini mjakazi wa mmoja wenu, atandikwe bakora na asisumbuliwe baadaye."*¹

Kisha asifedheheshwe kwa aliyoyafanya baada ya adhabu hiyo, kwa sababu fimbo alizotandikwa zinafuta madhambi aliyoyafanya.

إِنَّمَا التَّوْبَةُ عَلَى اللَّهِ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السُّوءَ بِجَهْلَةٍ ثُمَّ يَتُوبُونَ مِنْ قَرِيبٍ فَأُولَئِكَ يَتُوبُ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٨﴾
وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ
السَّيِّئَاتِ حَتَّى إِذَا حَضَرَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ إِنِّي تُبْتُ الْفَنَ وَلَا الَّذِينَ يَمُوتُونَ
وَهُمْ كُفَّارٌ ﴿١٩﴾ أُولَئِكَ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿٢٠﴾

17. Hakika toba inayokubaliwa na Mwenyezi Mungu ni ya wale wafanyao uovu kwa ujinga, kisha wakatubia kwa haraka. Hao ndio Mwenyezi Mungu Huwakubalia toba yao, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na ni Mwenye Hekima.

18. Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yakamfikia mmoja wao mauti, kisha hapo akasema: Hakika mimi sasa nimetubia. Wala wale wanaokufa na hali wao ni makafiri. Hao Tumewaandalia adhabu chungu.

¹ Fat'hul Al-Bari 4:491 na Muslim 3:1338.

Kukubaliwa kwa Toba ya Mja Kabla Mtu Hajaanza Kutapatapa na Umauti.

Allah تعالى Anaeleza kuwa Anapokea toba ya mja anayekosea bila ya kujua kisha akatubia, kabla hajamuona Malaika mtoa roho, kabla roho yake haijatoka kooni au kabla hajaanza kutapatapa. Mujaahid na wengine wanasema, "Mwenye kumuasi Allah تعالى bila kukusudia au kwa kukusudia bila kujua basi huyo ni jahili mpaka ajiondoshe kwenye madhambi hayo."¹ Qatadah alisema kuwa Abu Al-Aliya alisimulia kuwa swahaba wa Mtume ﷺ walikuwa wakisema, "Kila dhambi anayotenda mja huifanya kwa ujinga."² Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliinukuu. Abdur-Razzaq alisimulia, Ma'mar alisema kuwa Qatadah alisema, "Maswahaba wa Mtume ﷺ walikubaliana kuwa kila kosa lifanywalo kwa kudhamiria au vinginevyo limefanywa kwa ujinga."³ Ibn Jurayr رحمه الله تعالى alisema, "Abdullah bin Kathir alinisimulia kuwa Mujahid alisema, "Kila anayemuasi Allah تعالى ni mjinga wakati anapoasi." Ibn Jurayj alisema, "Ata bin Abu Rubah aliniambia Khabari kama hii."⁴ Abu Salih alisema, Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, "Mtu hufanya makosa kwa ujinga."⁵ Ali bin Abi Talhan aliandika, Ibn Abbas رضي الله عنهما aliielezea Aya hii,

ثُمَّ يَتُوبُونَ مِنْ قَرِيبٍ

"Kisha wakatubia kwa haraka." Ni kama baina yake na kumuona *Malakul Mawt* - Malaika mtoa roho."⁶ Adh-Dhahhak alisema, "Kila jambo kabla ya kifo ni la karibu."⁷ Hasan Al-Basri alizungumzia kuhusu,

ثُمَّ يَتُوبُونَ مِنْ قَرِيبٍ

"Kisha wakatubia kwa haraka". "Kabla pumzi yake ya mwisho haijapita kwenye koo lake."⁸ Ikrima alisema, "Dunia yote ni ya muda mfupi."⁹ Imam Ahmad aliandika kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ At – Tabari 8:89.

² At – Tabari 8:89.

³ Abdur-Razzaq 1:151.

⁴ At – Tabari 8:90.

⁵ At – Tabari 8:90.

⁶ At – Tabari 8:94.

⁷ At – Tabari 8:94.

⁸ At – Tabari 8:96.

⁹ At – Tabari 8:94.

«إِنَّ اللَّهَ يَقْبَلُ تَوْبَةَ الْعَبْدِ مَا لَمْ يُغْرِغْ»

"Hakika Allah Hupokea toba ya mja kabla roho haijafika kooni,"¹

Hadithi hii pia ameipokea At-Tirmidhi,² Ibn Majah,³ At-Tirmidhi amesema, *"Hasan Gharib."* Ibn Majah amesema: ilisimuliwa kutoka kwa Abdullah bin Amr. Hata hivyo, sahihi ni kuwa Abdullah bin Umar bin Al-Khattab رضي الله عنهما ndiye msimulizi wa hadithi hii. Allah تعالى Amesema,

فَأُولَئِكَ يَتُوبُ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٧﴾

"Hao ndio Mwenyezi Mungu Huwakubalia toba yao, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na ni Mwenye Hikima."

Kwa hakika, matumaini ya kuishi yanapokatika, Malaika wa mauti hujongea karibu na roho kufikia kwenye koo, inasogea kwenye kifua kisha inafika katika koromeo, pahala ambapo inavutwa nje taratibu. Ikifika hapo hapana toba inayokubaliwa wala hakuna kurudi nyuma. Allah تعالى Amesema,

وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ حَتَّىٰ إِذَا حَضَرَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ إِنِّي

تُبْتُ الْعَن

"Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yakamfikia mmoja wao mauti, kisha hapo akasema: Hakika mimi sasa nimetubia."

Hii ni sawa na Kauli nyingine ya Allah تعالى

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَحَدُّهُ

"Walipoiona Adhabu Yetu walisema: Tumemuamini Mwenyezi Mungu kuwa ni wa Pekee." (40:84)

Ni kama Alivyohukumu Allah تعالى kuwa toba ya watu wa duniani haitopokelewa watakapoona jua linapochomoza kutoka Magharibi kama Allah تعالى Alivyosema;

¹ Ahmad 5:174.

² At - Tabarani Katika As-Saghir 3308, Al-Hilyah 8:125. Hadithi hii ni sahihi na inaipa nguvu hadithi iliyopita.

يَوْمَ يَأْتِي بَعْضُ آيَاتِ رَبِّكَ لَا يَنْفَعُ نَفْسًا إِيْمَانُهَا لَمْ تَكُنْ ءَامَنَتْ مِن قَبْلُ أَوْ كَسَبَتْ فِي
إِيْمَانِهَا خَيْرًا^١

“Siku zitakapo fika baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi, kuamini hapo hakutumfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake, au amefanya kheri katika Imani yake.” (6:158)

Allah تعالى Amesema,

وَلَا الَّذِينَ يَمُوتُونَ وَهُمْ كُفَّارٌ

“Wala wale wanao kufa na hali wao ni makafiri.” Hivyo, kafiri anapokufa katika ukafiri au ushirikina, majonzi yake na toba yake haitamnusuru. Hata akitaka kujikomboa, hata angeijaza dunia dhahabu, Allah تعالى Asingeikubali, Ibn Abbas, Abu Al-Aliyah na Ar-Rabiy bin Anas رضى الله عنهم walisema kuwa Aya hii,

وَلَا الَّذِينَ يَمُوتُونَ وَهُمْ كُفَّارٌ

“Wala wale wanaokufa na hali wao ni makafiri.”

Iliteremshwa kwa ajili ya Washirikina. Imam Ahmad aliandika kuwa Usamah bin Salman alisema, Abu Dharr رضى الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ اللَّهَ يَقْبَلُ تَوْبَةَ عَبْدِهِ - أَوْ يَغْنَبُ لِعَبْدِهِ - مَا لَمْ يَفْعَ الْحِجَابُ»

“Hakika Allah تعالى Anapokea toba ya mja wake, au Anamsamehe mja wake madhali hijabu haijatoka.”

Walimuuliza, “Na nini maana ya kutoka kwa Hijab?” Aliwajibu,

«أَنْ تَخْرُجَ النَّفْسُ وَهِيَ مُشْرِكَةٌ»

“Roho ya mmoja wenu inapotolewa akiwa bado mshirikina.”¹

Kwa ajili hii Allah تعالى Amesema,

أُولَئِكَ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٥٨﴾

“Hao Tumewaandalia Adhabu chungu.” Yaani Adhabu kali na ya kuumiza milele.

¹ Ahmad 5:174.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ
 تَرْتُوا النِّسَاءَ كَرِهًا ^ط وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ
 لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَا ءَاتَيْتُمُوهُنَّ إِلَّا أَنْ
 يَأْتِيَنَّ بِفَحِشَةٍ مُّبِينَةٍ ^ع وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ^ف فَإِنْ
 كَرِهْتُمُوهُنَّ فَعَسَى أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَيَجْعَلَ اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا
 كَثِيرًا ﴿١٩﴾ وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَسْبَدَالَ زَوْجٍ مَكَانَ
 زَوْجٍ وَءَاتَيْتُمْ إِحْدَهُنَّ قِنطَارًا فَلَا تَأْخُذُوا مِنْهُ شَيْئًا ^ع
 أَتَأْخُذُونَهُ بِهْتِنًا وَإِنَّمَا مِيبِنًا ﴿٢٠﴾ وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ
 وَقَدْ أَفْضَى بَعْضُكُمْ إِلَى بَعْضٍ وَأَخَذْتُمْ مِنْكُمْ
 مِيثَاقًا غَلِيظًا ﴿٢١﴾ وَلَا تَنْكِحُوا مَا نَكَحَ ءَابَاؤُكُمْ
 مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ ^ع إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً
 وَمَقْتًا وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٢٢﴾ حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ
 وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ
 الْأَخِ وَبَنَاتُ الْأَخِ وَأُمَّهَاتُكُمُ اللَّاتِي أَرْضَعْنَكُمْ
 وَأَخَوَاتُكُمْ مِنَ الرِّضَاعِ وَأُمَّهَاتُ نِسَائِكُمْ
 وَزَوَّجَاتُكُمُ اللَّاتِي فِي حُجُورِكُمْ مِنَ نِسَائِكُمُ اللَّاتِي
 دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَإِنْ لَمْ تَكُونُوا دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ
 عَلَيْكُمْ وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ وَأَنْ
 تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ ^ع إِنَّ اللَّهَ
 كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٢٣﴾

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ
 تَرْتُوا النِّسَاءَ كَرِهًا ^ط وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ
 لِتَذْهَبُوا بِبَعْضِ مَا ءَاتَيْتُمُوهُنَّ إِلَّا
 أَنْ يَأْتِيَنَّ بِفَحِشَةٍ مُّبِينَةٍ ^ع وَعَاشِرُوهُنَّ
 بِالْمَعْرُوفِ ^ف فَإِنْ كَرِهْتُمُوهُنَّ فَعَسَى
 أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَيَجْعَلَ اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا
 كَثِيرًا ﴿١٩﴾ وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَسْبَدَالَ
 زَوْجٍ مَكَانَ زَوْجٍ وَءَاتَيْتُمْ
 إِحْدَهُنَّ قِنطَارًا فَلَا تَأْخُذُوا مِنْهُ
 شَيْئًا ^ع أَتَأْخُذُونَهُ بِهْتِنًا وَإِنَّمَا
 مِيبِنًا ﴿٢٠﴾ وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ
 أَفْضَى بَعْضُكُمْ إِلَى بَعْضٍ وَأَخَذْتُمْ
 مِنْكُمْ مِيثَاقًا غَلِيظًا ﴿٢١﴾ وَلَا
 تَنْكِحُوا مَا نَكَحَ ءَابَاؤُكُمْ مِنَ
 النِّسَاءِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ ^ع إِنَّهُ كَانَ
 فَحِشَةً وَمَقْتًا وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٢٢﴾

19. Enyi mlio amini! Si halali kwenu kuwarithi wana-wake kwa nguvu. Wala msiwazuie kwa madhara ili muwapokonye baadhi ya mlivyowapa isipokuwa

wakifanya uovu uliowazi. Na kaeni nao kwa wema, na ikiwa mmewachukia, basi huenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu Ametia kheri nyingi ndani yake.

20. Na mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke, na hali mmoja wao mmempa chungu ya mali, basi msichukue katika hayo kitu chochote. Je, mtachukua kwa dhulma na kosa lilio wazi?

21. Na mtachukuaje na ilhali mmekwisha ingiliana nyinyi kwa nyinyi, na wao wanawake wamechukua kwenu ahadi iliyo madhubuti?

22. Wala msiwaoe wake walio waoa baba zenu, ila yaliyokwisha pita. Hakika huo ni uchafu na chukizo na ni njia mbaya.

Maana ya 'Kurithi Wanawake kwa Nguvu':

Bukhari amepokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alivyoielezea Aya ifuatayo:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرِثُوا النِّسَاءَ كَرِهًا

"Enyi mlio amini! Si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu."

Alisema: Walikuwa, pindi alipokufa mtu basi Mawalii wake ndio waliokuwa wenye haki zaidi juu ya mkewe. Mwenye kutaka alimuoza na vinginevyo walimuoza, na pengine hawakumuozesha kwani wao walikuwa na haki zaidi kumtendea hayo kuliko nduguze.

Aya hiyo ikateremshwa juu ya jambo hilo,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَرِثُوا النِّسَاءَ كَرِهًا

"Enyi mlio amini! Si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu."¹

¹ Fat'hul Al-Bari 8:93.

Wanawake Wasidhuriwe

Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَعْضُلُوهُنَّ لِتَذَهَبُوا بِبَعْضِ مَا آتَيْتُمُوهُنَّ

“Wala msiwadhikishe ili muwapokonye baadhi ya mlivyowapa.”

Allah تعالى Ameamrisha, “Wala msiwadhikishe wanawake ili wakurejesheni mahari yote au sehemu yake, au kusabilia haki zake kwa kutezwa nguvu au kugandamizwa.” Kauli ya Allah تعالى,

إِلَّا أَنْ يَأْتِيَنَّ بِفَحِشَةٍ مُّبِينَةٍ

“Isipo kuwa wakifanya uchafu ulio wazi.”

Ibn Mas’ud, Ibn Abbas, Sa’id bin Al-Musayyib, Ash-Sha’bi Hasan Al-Basri, Muhammad bin Sirin, Said bin Jubayr, Mujahid, Ikrimah, Ata Al-Khurasani, Adh-Dhahhak, Abu Qilabah, Abu Salih, As-Suddi, Zayd bin Aslam na Said bin Abi Hilal رضي الله عنهم walisema kuwa hii inahusu zinaa. Ina maana kuwa endapo mke atazini, unaruhusiwa kudai mahari uliyompa. Aidha unaruhusiwa kumkera mpaka arejeshe mahari na umuache kwa kujikomboa (*Khul’u*).¹ katika Surah al-Baqarah, Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَأْخُذُوا بِمَا آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا إِلَّا أَنْ تَخَافَا أَلَّا يُقِيمَا حُدُودَ اللَّهِ

“Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa wake zenu, ila ikiwa wote wawili wakiogopa ya kwamba hawataweza kushikamana na mipaka ya Mwenyezi Mungu.” (2:229)

Ibn Abbas, Ikrimah na Adh-dhahhak رضي الله عنهم walisema kuwa *Fahishah* iliyo wazi inakusudiwa kuasi na kukengeuka.² Ibn Jarir رحمه الله تعالى alichagua rai ya jumla, inayojumuisha maana zote, uzinzi, kuasi, kukengeuka, matusi, ukatili na kadhalika. Muradi wake ni kuwa anaruhusiwa kumkera mkewe anapofanya moja ya vitendo hivi mpaka atakaposamehe haki zake zote au sehemu yake na kisha kumtaliki, rai hii ni sahihi, na Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote.

¹ At-Tabari 115:117.

² At-Tabari 8:117.

Amri ya Kukaa na Wanawake kwa Wema.

Allah تعالیٰ Anasema;

وَعَاشِرُوهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ

"Na kaeni nao Kwa wema."

Kwa kuzungumza nao vizuri, kuwatendea mema na kukunjua uso na kutabasamu kwa kadri ya uwezavyo, kama unavyopenda utendewe.

وَهُنَّ مِثْلُ الَّذِي عَلَيْهِنَّ بِالْمَعْرُوفِ

"Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao." (2:228)

Mtume ﷺ amesema,

«خَيْرُكُمْ خَيْرُكُمْ لِأَهْلِيهِ، وَأَنَا خَيْرُكُمْ لِأَهْلِي»

*"Mbora wenu ni yule aliye bora kwa ahli yake, hapana shaka mimi ni mbora wenu kwani ni mbora kwa ahli yangu."*¹

Mtume ﷺ alikuwa mwema, mcheshi, na akicheza na wakeze, mwenye huruma, akiwakimu vizuri na kucheka nao. Mtume ﷺ alikuwa akishindana mbio na Mwana Aisha رضي الله عنها, Mama wa waumini, kama dalili ya mapenzi. Aisha رضي الله عنها alisema, "Mtume ﷺ alishindana nami na nikamshinda katika mbio. Hii lilijiri kabla ya kuwa mzito na baadaye nilishindana naye, na akanishinda." Alisema,

«هَذِهِ بَيْتُكَ»

*"Ushindi huu kwa ushindi ule."*²

Mtume ﷺ alipokuwa kwa mmoja wa wakeze, baadhi ya wakati, wake zake wote walikusanyika hapo na kula pamoja chakula, na baada ya hapo walirejea majumbani kwao. Yeye na mkewe walilala kitanda kimoja, na alivua nguo zake za nje na kusalia na nguo ya ndani. Mtume ﷺ alikuwa akizungumza na mke wa zamu baada ya kusali isha na kabla ya kwenda kulala. Allah تعالیٰ Amesema,

¹ Tuhfatul Al-Ahwadhi 10:394.² Abu Dawud 3:66.

لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ

“Hakika nyinyi mnyo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu.” (33:21)

Allah تعالی Amesema,

فَإِنْ كَرِهْتُمُوهُنَّ فَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَجَعَلَ اللَّهُ فِيهِ خَيْرًا كَثِيرًا ۝

“Na ikiwa mmewachukia, basi huenda mkakichukia kitu, na Mwenyezi Mungu Ametia kheri nyingi ndani yake.”

Allah تعالی Anasema kuwa subira yenu ambayo imejidhihirisha kwa kukaa na wake mnaowachukia, ina malipo makubwa hapa duniani na Akhera. Ibn Abbas رضي الله عنهما ameieleza Ayah hii, “Kuwa mume anamhurumia mkewe na Allah تعالی Anamjaalia kupata mtoto na mtoto huyu anakuwa mwema.” Hadithi sahihi inasema,

«لَا يَفْرَكُ مُؤْمِنٌ مُؤْمِنَةً، إِنْ سَخِطَ مِنْهَا خُلْفًا، رَضِيَ مِنْهَا آخَرَ»

“Muumini mwanaume asimchukie muumini mwanamke. Akichukia tabia yake moja, atairidhia kwake tabia nyingine.”¹

Kuharamishwa Jambo la Kutaka Kurudishiwa Mahari Kutoka kwa Mke

Allah تعالی Amesema,

وَإِنْ أَرَدْتُمْ أَنْ تَبْدُلُوا زَوْجَ مَكَاتٍ زَوْجٍ وَآتَيْتُمْ إِحْدَهُنَّ فِنْطَارًا فَلَا تَأْخُذُوا مِنْهُ

شَيْئًا ۚ أَتَأْخُذُونَهُ بِهَيْعَتِنَا وَإِنَّمَا مَيْبِنَا ۝

“Na mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke, na hali mmoja wao mmempa chungu ya mali, basi msichukue katika hayo kitu chochote. Je, mtachukua kwa dhulma na kosa lilio wazi?” (4:20)

Ayah inaamuru: Mmoja wenu akitaka kumtaliki mke au kuo mwingine, hatakiwi kuchukua au kudai sehemu ya mahari aliyompa mke wa kwanza, hata kama ni *Qintar*. Tumeeleza maana ya *Qintar* katika Tafsiri ya *Surah Al-Imran*, hakuna

¹ Muslim 1:1091.

haja kuirejea hapa. Ayah hii ni dalili ya kufaa mahari kuwa mali nyingi na kiwango cha kuridhisha. 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alikataza mahari kubwa, ila baadaye alibadili msimamo wake. Imam Ahmad alimnukuu Abu Al-Ajfa As-Sulami akisema, alimsikia 'Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه akisema, "Msifanye isirafu katika kuwapa mahari wanawake, kama tabia hii ingekuwa na heshima au Taqwa, basi Mtume ﷺ angekuwa na haki zaidi kuliko nyie kuitekeleza." Mtume ﷺ hakupata kumpa mkewe yeyote au bintiye aliyepokea mahari zaidi ya waqia kumi na mbili.¹ Hata inafikia Mtu kupata mitihani katika kulipa mahari kubwa, ikapelekea kujenga uhasama na mkewe. Na kumsumbulia mkewe, "Nimelipa mahari kubwa!" Ahmad² na wapokezi wengine wa Sunan waliipokea Hadithi hii kupitia Isnadi anuwai,³ na At-Tirmidhi ameipa daraja la "Hassan sahih".

Al-Hafidh Abu Ya'la رحمه الله تعالى aliandika kuwa Masruq alisema, "Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisimama juu ya Mimbari ya Mtume ﷺ na akasema, "Enyi Watu! Kwa nini mnawapa mahari kubwa wanawake?" Mtume ﷺ na Masahaba zake walikuwa wakilipa mahari mpaka Dirham mia nne au chini ya hiyo. Kama kulipa mahari kubwa ingekuwa sehemu ya uchamungu au heshima, basi Mtume ﷺ angetuongoza kutekeleza ada hii. Kwa hiyo, sitaki kusikia mtu akitoa mahari Dir'ham mia nne." Kisha akashuka kutoka katika mimbari, lakini mwanamke wa Kiquraish aliweka pingamizi kwa 'Umar رضي الله عنه na akamuambia, 'Ewe Kiongozi wa Waumini! Umewazuia watu kuwapa mahari wanawake zaidi ya Dirham mia nne?" Alijibu, 'Ndiyo.' Akamuambia, "Hujasikia Aliyoshusha Allah تعالى ndani ya Qur'an?" Akamuuliza, 'Sehemu gani?' Akamuambia, "Hujasikia Kauli ya Allah تعالى,

وَأَتَيْنَهُمْ إِحْدَثَهُنَّ قِنطَارًا

"Na hali mmoja wao mmempa chungu ya mali."

Akasema, "Ewe Allah! Nisamehe..." Kisha akarejea na kusimama juu ya mimbari, akasema, 'Nilikukatazeni kutoa mahari zaidi ya Dir'ham mia nne. Hivyo kila mmoja atoe kiasi apendacho." Isnadi ya Hadithi hii ina nguvu.⁵

¹ Takriban Dirham 400.

² Ahmad 1:40.

³ Muqbil bin Hadi amezipata daraja ya Dhaifu kisa hiki, na ile Ripoti kutoka kwa 'Umar.

⁴ Abu Dawud 2:582: Tuhfat ulAl-Ahwadhi 4:255, An-Nasa'I 6:117, Ibn Majah 1:601.

⁵ Abu Dawud 2:582: Tuhfat ulAl-Ahwadhi 4:255, An-Nasa'I 6:117, Ibn Majah 1:601.

وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ أَفْضَىٰ بَعْضُكُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ

“Na mtachukua je na ilhali mmekwisha ingiliana nyinyi kwa nyinyi.”

Utachukua je mahari kutoka kwa mwanamke uliye jamii naye? Ibn Abbas, Mujahid, As-Suddi na wengineo رضي الله عنهم walisema kuwa hii ina maana kukutana kimwili.¹ Sahihi mbili zimerikodi kuwa Mtume ﷺ aliwaambia watu wawili wenye kulaaniana mara tatu baada ya kumaliza *Mula'ana*,²

«اللَّهُ يَعْلَمُ أَنَّ أَحَدَكُمَا كَاذِبٌ، فَهَلْ مِتَّ كَمَا تَابِ؟»

“Allah Anajua kuwa mmoja wenu ni mwongo, hivyo je kuna mmoja wenu anayetaka kutubia?”

Mtume aliyakariri maneno haya mara tatu. Mtu mmoja akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Mali zangu, akikusudia mahari aliyompa mkewe,” Akamjibu,

«لَا مَالَ لَكَ، إِنْ كُنْتَ صَدَقْتَ عَلَيَّهَا فَهَوَ بِمَا اسْتَحَلَلْتَ مِنْ قَرَجِهَا، وَإِنْ كُنْتَ كَذَبْتَ عَلَيَّهَا فَهَوَ أَبْعَدُ لَكَ مِنْهَا»

“Huna mali: Kama ni wewe uliyenena kweli, mahari ni malipo ya kumuingilia mwanamke. Endapo wewe ndiye uliyesema urongo, hivyo fedha hii iko mbali nawe.”³

Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ أَفْضَىٰ بَعْضُكُمْ إِلَىٰ بَعْضٍ وَأَخَذَ مِنْكُمْ مِيثَاقًا غَلِيظًا ﴿٤٠﴾

“Na mtachukua je na ilhali mmekwisha ingiliana nyinyi kwa nyinyi, na wao wanawake wamechukua kwenu ahadi iliyo madhubuti?”

Maana yake: ndoa, kwa mujibu wa Ibn Abbas, Mujahid na Sa'id bin Jubayr رضي الله عنهم.⁴ Katika Sahihi yake, Muslim amemnukuu Jabir عنه رضي الله عنه akisema, Mtume ﷺ alipokuwa akitoa hotuba katika Hija ya kuaga, alisema,

¹ At - Tabari 8:126.

² Rejea Surat An-Nur 24:6 – 9.

³ *Fat'hul Al-Bari* 9:366 na Muslim 2:1131.

⁴ At-Tabari 8:129.

وَاسْتَرْضُوا بِالنِّسَاءِ خَيْرًا، فَإِنَّكُمْ أَخَذْتُمُوهُنَّ بِأَمَانِ اللَّهِ، وَاسْتَخْلَلْتُمْ نُزُوجَهُنَّ بِكَلِمَةِ اللَّهِ،

“Kaeni vizuri na wanawake, kwani mmewachukua ni amana kutoka kwa Allah تعالی na mkapata haki ya kuwaingilia kwa kalima ya Allah تعالی.”¹

Kuharamishwa Kumuoia Mke wa Baba na Hukumu ya Wenye Kulikiuka Hilo.

وَلَا تَنْكِحُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُمْ مِنَ النِّسَاءِ

“Wala msiwaoe wake walio waoa baba zenu.”

Allah تعالی Ameharamisha kuwaoa wanawake waliokuwa wake wa baba zenu, ili kuwaheshimu na kuwaadhimisha baba zenu, kwa kuwazuia watoto wao kujamiiana na wake zao baada ya kufariki dunia. Mwanamke huwa mahramu wa mtoto wa kiume wa mume wake mara tu baada ya kufungwa ndoa, wanazuoni wanaafikiana katika hili.

Ibn Jarir رحمه الله تعالی alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliyesema, katika enzi za Jahiliyyah, watu walikuwa wakikataza yale yaliyoharamishwa na Allah تعالی (yahasuyo ndoa) isipokuwa kumuoa mama wa kambo na kuwaoa dada wawili kama wake wenza. Allah تعالی Aliteremsha,

وَلَا تَنْكِحُوا مَا نَكَحَ آبَاؤُكُمْ

“Wala msiwaoe wake walio waoa baba zenu.” Na

وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ

“Na kuwaoa pamoja dada wawili.” (4:23)²

Kauli kama hiyo iliripotiwa kutoka kwa Ata na Qatadah.³ Kwa hiyo iliyotajwa na Ayah imeharamishwa kwa Ummah huu, ni jambo la fedheha na kosa kubwa.

إِنَّهُ كَانَ فَنِجْشَةً وَمَقْتًا وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٢٣﴾

“Hakika huo ni uchafu na uchukizo na ni njia mbaya.”

¹ Muslim 2:889.

² At - Tabari 8:132.

³ At - Tabari 8:132 – 134.

Allah تعالى Amesema katika Aya nyingine.

وَلَا تَقْرَبُوا أَلْفَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ

“Wala msikaribie mambo machafu, yanayoonekana, na yanayo fichikana.” (6:151) na,

وَلَا تَقْرَبُوا الزَّيْنَىٰ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿١٧﴾

“Wala msikaribie uzinzi. Hakika huo ni uchafu na njia mbaya.” (17:32)

Katika Aya hii (2:22) Allah تعالى Ameongeza

وَمَقْتًا

“...na uchukizo...” Maana yake: Kubughudhi. Ni dhambi pekee inayopelekea mtoto kumchukia baba yake baada ya kuoa mkewe. Ni kawaida kwa anayeoa kuchukia waliomuoa mwanamke huyo kabla. Hii ndio moja ya sababu, Mama wa Waumini hawakuruhusiwa kuolewa baada ya kufa Mtume ﷺ. Hakika wao ni Mama wa Waumini madhali waliolewa na Mtume ﷺ ambaye ni kama baba wa waumini. Pamoja na hayo, haki ya Mtume ﷺ ni kubwa zaidi kuliko ya baba, na mapenzi yake yanakuja kabla ya mapenzi ya mtu binafsi, rehema na amani za Allah zimshukie.

Ata bin Abi Rabah, alisema kuwa Aya,

وَمَقْتًا

“...na chukizo...” Muradi wake, Allah تعالى Atamchukia

وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿١٧﴾

“...na ni njia mbaya...”, Kwa wale wanaokhitari njia hii, basi hii ni njia mbaya. Kwa hiyo wale wenye mwendo huo watakuwa wamefanya kitendo cha kuritadi na hivyo wanastahili adhabu kali ya kuuawa na kunyang'anywa mali zao na kufanywa *Fayi* ni mali iliyopatikana bila ya kupigana vita ambayo itapelekwa kwenye *Baitul Mali*. Imam Ahmad na wakusanyaji wa Sunan waliandika kwa Isnadi mbalimbali kuwa Al-Bara bin Azib alisema kuwa Mjomba wake Abu

¹ Ahmad 4:290; Abu Dawud 4:609; Tuhfat Al-Ahwadhi 4:598; An-Nasai katika Al-Kubra 4:296; Ibn Majah 2:869.

Burdan alitumwa na Mtume ﷺ kwa mtu aliyemuoa mama yake wa kambo ili akamuue na kumnyang'anya mali zake.¹

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ الْأَخِ
وَبَنَاتُ الْأَخْتِ وَأُمَّهَاتُكُمُ اللَّيِّئِ أَرْضَعْتَكُمْ وَأَخَوَاتُكُم مِّنَ الرَّضَاعَةِ وَأُمَّهَاتُ
نِسَائِكُمْ وَرَبِّبَاتِكُمُ اللَّيِّئِ فِي حُجُورِكُمْ مِّنْ نِّسَائِكُمُ اللَّيِّئِ دَخَلْتُم بِهِنَّ فَإِنْ لَّمْ تَكُونُوا
دَخَلْتُم بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ وَخَالَاتُكُمُ اللَّيِّئِ أُمَّهَاتُكُمْ وَأَصْلَابُكُمْ وَأَنْ
تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأَخْتَيْنِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٣١﴾

23. "Mmeharimishiwa mama zenu, na binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na khaalati zenu, na binti wa ndugu wa mume, na binti wa dada, na mama zenu waliokunyonyesheni, na dada zenu kwa kunyonya, na mama wa wake zenu, na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia. Ikiwa hamkuwaingilia basi hapana lawama juu yenu. (Pia mmeharimishwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu. Na kuwaoa pamoja dada wawili isipokuwa yale yaliyo kwisha pita. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe Mwenye Kurehemu."

Kubainisha Wanawake Maharim; Walioharamishwa Kuwaoa Milele, na wa Muda Maalum.

Ayah hii tukufu ndio inayoainisha faraja za ukuruba wa wanawake ambao mmoja wenu hapaswi kumuoa kutokana na uhusiano wa kinasaba, kunyonya ziwa moja na ukwe. Ibn Hatim رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, alisema (Allah تعالى Amesema), "Nimewaharamishia aina saba za ndugu wa damu na za nasaba kwa kuoa." Kisha Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema Aya hii,

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ

"Mmeharimishiwa mama zenu, na binti zenu, na dada zenu."

¹ At - Tabari 8:142.

At-Tabari رحمه الله تعالى aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Daraja saba za nasaba na za damu na daraja za uhusiano wa ndoa ni haramu." Kisha alisoma,

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمْ أُمَّهَاتُكُمْ وَبَنَاتُكُمْ وَأَخَوَاتُكُمْ وَعَمَّاتُكُمْ وَخَالَاتُكُمْ وَبَنَاتُ الْأَخِ
وَبَنَاتُ الْأُخْتِ

"Mmeharimishiwa mama zenu, na binti zenu, na dada zenu, na shangazi zenu, na khaalati zenu, na binti wa ndugu wa mume, na binti wa dada."

Na hizi ni aina za uhusiano wa kinasaba.¹ Kauli ya Allah تعالى,

وَأُمَّهَاتُكُمُ اللَّاتِي أَرْضَعْنَكُمْ وَأَخَوَاتُكُم مِّنَ الرَّضَاعَةِ

"Na mama zenu waliokunyonyesheni, na dada zenu kwa kunyonya."

Maana yake: Kama ilivyo haramu kumuoa mama yako mzazi, hali kadhalika mama yako wa kunyonya.

Bukhari na Muslim waliandika kuwa Aishah رضي الله عنها, Mama wa Waumini, alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ الرِّضَاعَةَ تُحَرِّمُ مَا تُحَرِّمُ الْوِلَادَةُ»

"Hakika kunyonya kunaharamisha kile kilichoharamishwa na kizazi."

Katika mapokezi mengine yaliyopokelewa na Muslim,

«يُحَرِّمُ مِنَ الرِّضَاعَةِ مَا يُحَرِّمُ مِنَ النَّسَبِ»

"Kunyonya kunaharamisha yanayoharamishwa na nasaba."²

Kunyonya kusikofikia mara tano hakuzuii kuoana. Ndani ya sahihi yake, Muslim aliandika kuwa, Aishah رضي الله عنها alisema Miongoni mwa Ayah za Qur'an zilizoteremshwa, ni kauli isemayo, "Kunyonya mara kumi kunasababisha kuzuiwa kuoana. Baadaye ilinasikhiwa na tano, na Mtume ﷺ alifariki dunia hali aya hii iliendelea kusomwa kama sehemu ya Qur'an."³

¹ At -Tabari 8:141.

² Fat'hul Al-Bari 9:43 na Muslim 2:1068.

³ Muslim 2:1075.

Hadithi ilisimuliwa na Sahlah Bint Suhayl رضي الله عنها kuwa Mtume ﷺ alimuamuru amnyonyeshe Salim mara tano.¹ Salim ni ni mtoto aliyepewa uhuru na Abu Hudhaifah رضي الله عنه. Tunasisitiza kuwa kunyonyesha kuliko tajwa hapa lazima kuwe kabla ya kufikia umri wa miaka miwili, kama tulivyosema tulipokuwa tukielezea Aya ndani ya *Surat Al-Baqarah*, (2:233).

يُرِضَعْنَ أَوْلَادَهُنَّ حَوْلَيْنِ كَامِلَيْنِ لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يُمَّ الرِّضَاعَةَ

“Wawanyonyeshe watoto wao miaka miwili kamili kwa anaye taka kutimiza kunyonyesha...” (2:233)

Haramu Kuwaoa Mama Wakwe na Binti zao.

Allah تعالى Anasema,

وَأَمَهتُ نِسَائِكُمْ وَرَبَائِكُمْ الَّتِي فِي حُجُورِكُمْ مِّنْ نِّسَائِكُمُ الَّتِي دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَإِنْ لَّمْ تَكُونُوا دَخَلْتُمْ بِهِنَّ فَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ

“Na mama wa wake zenu, na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia. Ikiwa hamkuwaingilia basi hapana lawama juu yenu.”

Ama mama wa mke anakuwa haramu kuolewa na mkwe baada ya ndoa kutimia, bila kujali kuwa mkwe alimuingilia bintiye au la. Ama kwa binti wa mke, anakuwa haramu kwa baba wa kambo baada ya kukutana kimwili na mama yake. Endapo atamtaliki mama yake kabla ya jimai, anaruhusiwa kumuoa binti yake.

Hivyo Allah تعالى Amesema,

وَرَبَائِكُمُ الَّتِي فِي حُجُورِكُمْ

“Na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu.”

Hii ni khasa juu ya kuwaoa watoto wa kambo.

¹ Abu Dawud 2:550.

Mtoto wa Kambo ni Haramu Kuolewa Hata Kama Hakuwa katika Ulinzi wa Baba Yake wa Kambo.

Allah تعالى Amesema,

وَرَبِّبُكُمْ أَلَيْبِي فِي حُجُورِكُمْ

“Na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu.”

Wanazuoni walio wengi wamedhukuru kuwa binti wa kambo si ruhusa kuolewa na baba yake wa kambo (aliyetimiza ndoa na mama yake) kama alikuwa au hajakuwa chini ya ulinzi wake. Sahihi mbili zimeandika kuwa Umm Habibah رضي الله عنها alisema, “Ewe Mtume ﷺ Muoe dada yangu, binti wa Abu Sufyan (na katika mapokezi mengine ‘Azzah bint Abu Sufyani),

«أَوْ نُجِيبَنَّ ذَلِكَ؟» قالت: نعم. لست لك بمخلية، وأحب من شاركتني في خيرٍ أختي، قال: «فإِنَّ ذَلِكَ لَا يَجِلُّ لِي». قالت: فإنا نتحدث أنك تريد أن تنكح بنت أبي سلمة، قال: «بِئْسَ أُمَّ سَلَمَةَ؟» قالت: نعم. قال: «إِنَّهَا لَوْ لَمْ تَكُنْ رَبِّبَتِي فِي حَجْرِي مَا حَلَّتْ لِي، إِنَّهَا لَبِئْسَ أُخِي مِنَ الرِّضَاعَةِ، أَرْضَعْتَنِي وَأَبَا سَلَمَةَ تُؤَيِّبُهُ، فَلَا تَعْرِضَنَّ عَلَيَّ بَنَاتِكُنَّ وَلَا أَخَوَاتِكُنَّ»

“Unapenda hivyo?” Akajibu, “Ndiyo, Hakuna mbadala napenda dada yangu kushirikiana amali njema.” Na Mtume ﷺ akajibu, “Sijaruhusiwa kufanya hivyo.” Akamuambia, “Tuliambiwa unataka kumuoa binti wa Umm Salamah?” Akajibu, “Ndiyo.” Akasema, “Hata kama hakuwa mtoto wangu wa kambo na katika ulinzi wangu, bado hairuhusiwi kwani ni mpwa wangu kwa kunyonya, Thuwaibah alininyonyesha na Abu Salamah, hivyo usinitolee bintizo au dadazo niwaoe.”¹

Katika mapokezi mengine kutoka kwa Bukhari.

«إِنِّي لَوْ لَمْ أَتَزَوَّجْ أُمَّ سَلَمَةَ مَا حَلَّتْ لِي»

“Kama nisingemua Umm Salamah, bintiye asingeruhusiwa kuolewa nami.”²

¹ Fat ' hul Al-Bari 9:64 na Muslim 2:1073.

² Fat ' hul Al-Bari 9:62.

Hivyo Mtume ﷺ alidhukuru kuwa ndoa yake na Umm Salamah رضي الله عنها ilikuwa ndio sababu ya kuharamishwa huko.

Maana ya “Kuingilia”

Maana ya Kauli ya Allah تعالى،

الَّتِي دَخَلْتُمْ بِهِنَّ

“...Wake zenu mliowaingilia...”

Muradi wake kujamiiana nao, kwa mujibu wa Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengineo.¹

Kuharamishwa Kuwaoa Wake wa Watoto Halisi, Si wa Watoto wa Kupanga.

Allah تعالى Amesema،

وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ

“(Pia mmeharimishwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu.”

Basi, mmeharamishiwa kuoa wake wa watoto wenu, ila sio wake wa watoto wenu wa kupanga, kwani kupanga watoto ilikuwa ni ada ya Jahiliyyah،

فَلَمَّا قَضَى زَيْدٌ مِّنْهَا وَطَرًا زَوَّجْنَاكَهَا لِكَيْ لَا يَكُونَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ حَرَجٌ فِي أَزْوَاجِ

أَدْعِيَّاهُمْ

“Basi Zaid alipokwisha haja naye Tulikuoza wewe, ili isiwe taabu kwa Waumini kuwaoa wake wa watoto wao wa kupanga...”(33:37)

Ibn Jurayr رحمه الله تعالى alisema، “Nilimuuliza Ata kuhusu kauli hii،

وَحَلَائِلُ أَبْنَائِكُمُ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ

“(Pia mmeharimishwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu.”

¹At - Tabari 7:526.

Alisema, "Tulielezwa kuwa Mtume ﷺ alipomuona mtalaka wa Zayd (ambaye alikuwa ni mtoto wa kupanga wa Mtume ﷺ kabla tabia hii kuharamishwa na Uislamu) Mushirikina wa Makkah walimkosa. Allah تعالی Akashusha ayah hizi:

وَحَلَّتِ بِكُمْ أَبْنَاءُ الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ

"(Pia mmeharimishwa) wake wa watoto wenu waliotoka katika migongo yenu."

وَمَا جَعَلَ أَدْعِيَاءَكُمْ أَبْنَاءَكُمْ

"Wala hakuwafanya watoto wenu wa kupanga kuwa ni wana wenu khasa." (33:4)

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ

"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu." (33:40)

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی aliandika kuwa Hasan bin Muhammad alisema, "Aya hizi zinajumuisha,

وَحَلَّتِ بِكُمْ أَبْنَاءُكُمْ

"...(Pia mmeharimishwa) Wake wa watoto wenu.."

وَأُمّهتُ نِسَابَكُمْ

"Na (Mmeharamishiwa kuo) mama wa wake zenu." Aidha haya ni maelezo ya Tawus, Ibrahim, Az-zuhri na Makhul. Ina maana aya hizi mbili zinawajumuisha aina hizi za wanawake, ima ndoa zao zilikamilika au la ambako inakuwa haramu muda tu ndoa inapofungwa, na kuna muwafaka katika rai hii.

Utatanishi na Majibu Yake

Kukiulizwa kwanini mke wa mtoto wa kunyonya ameharamishwa kumuoa kama isemavyo kauli ya Jopo la wanazuoni (*Jamhur*) ambapo huyo si mke wa mtoto wake wa kumzaa? Jibu ni kama walivyoeleza wanazuoni wengi hata kama hawana uhusiano wa damu. Kauli yake Mtume ﷺ,

«يُحْرَمُ مِنَ الرِّضَاعِ مَا يُحْرَمُ مِنَ النَّسَبِ»

"Kunyonya kunazuia kilichozuiwa na udugu wa damu."¹

¹ Muslim 2:1072.

Kuharamishwa Kuoia dada Wawili kwa Wakati Mmoja.

وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ

“Na kuwaoa pamoja dada wawili isipokuwa yale yaliyokwisha pita.”

Maana yake: Mmezuiwa kuwaoa dada wawili kwa mpigo kama wake wenza au wajakazi, isipokuwa kwa yale yaliyojiri zama za Jahiliyyah, ambayo Tumeyafuta na Kuyasamehe, na hakuna khususiya katika hilo kama Alivyosema Allah تعالى,

لَا يَذُوقُونَ فِيهَا الْمَوْتَ إِلَّا الْمَوْتَةَ الْأُولَىٰ

“Humo hawataonja mauti ila mauti yale ya kwanza,...” (44:56)

Ina maana kuwa, kamwe hawataonja mauti. Kwa hiyo hapana anayeruhusiwa kuwa na dada wawili kama wake wenza, kwa mintarafu ya wanazuoni wa Maswahaba, wafuasi wao, na maimamu wa kale na wa leo. Wote wamedhukuru kuwa kukusanya dada wawili kama wake wenza ni haramu, na yeyote anayesilimu akiwa na wake wenza ambao ni dada anakhiyarishwa kumpa talaka mmoja na kubaki na mmoja wao. Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Adh-Dhahak bin Fayruz kutoka kwa baba yake kuwa alisema, “Nilisilimu nikiwa na wake wenza, dada wawili, na Mtume ﷺ aliniamuru nimaliki mmoja wao.”¹

* * *

¹ Ahmad 4:232.

* وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ
 كَتَبَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ ۗ وَأُحِلَّ لَكُمْ مَا وَرَاءَ ذَلِكَ أَنْ
 تَبْتَغُوا بِأَمْوَالِكُمْ مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسْفِحِينَ ۗ فَمَا
 اسْتَمْتَعْتُمْ بِهِ مِنْهُنَّ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ فَرِيضَةً ۗ وَلَا
 جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا تَرَضَيْتُمْ بِهِ مِنْ بَعْدِ الْفَرِيضَةِ ۗ إِنَّ
 اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٢٤﴾ وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ مِنْكُمْ
 طَوْلًا أَنْ يَنْكِحَ الْمُحْصَنَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ فَمِنْ مَا
 مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِنْ فَتَيَاتِكُمُ الْمُؤْمِنَاتِ ۗ وَاللَّهُ أَعْلَمُ
 بِإِيمَانِكُمْ بَعْضُكُمْ مِنْ بَعْضٍ ۗ فَانكِحُوهُنَّ بِإِذْنِ أَهْلِيهِنَّ
 وَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ ۗ مُحْصَنَاتٍ غَيْرَ
 مُسْفِحَاتٍ وَلَا مُتَّخِذَاتِ أَحْدَانٍ ۗ فَإِذَا أَحْصَيْتُمْ
 أَنْتُمْ بِفَحِشَةٍ فَعَلَيْهِنَّ نِصْفُ مَا عَلَى الْمُحْصَنَاتِ
 مِنَ الْعَذَابِ ۗ ذَلِكَ لِمَنْ حَشَى الْعَنَتَ مِنْكُمْ ۗ وَأَنْ
 تَضَرُّوا خَيْرٌ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٥﴾

* وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا
 مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ كَتَبَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ ۗ
 وَأُحِلَّ لَكُمْ مَا وَرَاءَ ذَلِكَ أَنْ
 تَبْتَغُوا بِأَمْوَالِكُمْ مُحْصِنِينَ غَيْرَ
 مُسْفِحِينَ ۗ فَمَا اسْتَمْتَعْتُمْ بِهِ
 مِنْهُنَّ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ فَرِيضَةً ۗ
 وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا تَرَضَيْتُمْ بِهِ
 مِنْ بَعْدِ الْفَرِيضَةِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا
 حَكِيمًا ﴿٢٤﴾

24. Na Wanawake wenye
 waume, isipokuwa walio-
 milikiwa na mikono yenu ya
 kulia. Ndiyo Sharia ya
 Mwenyezi Mungu juu yenu.
 Na mmehalalishiwa wasio-
 kuwa hao, mtafute kwa
 mali yenu kwa kuowa
 wanawake wenye kujilinda
 na machafu na sio wazinifu.
 Kama mnavyostarehe nao,

basi wapeni mahari yao kwa kuwa ni wajibu. Wala hapana lawama juu yenu
 kwa mtakachokubaliana baada ya kutimiza wajibu. Hakika Mwenyezi Mungu
 ni Mwenye Kujua na Mwenye Hikima.

Kuharamishwa *Muhsanat* Watakapokuwa Chini ya Milki

Allah تعالى Amesema,

﴿وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ﴾

“Na Wanawake wenye waume, isipokuwa waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia.”

Muradi wa aya hii ni kuwa mmezuiwa kuwaoa wanawake ambao wamesha-olewa.

﴿إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ﴾

“Isipokuwa waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia.”

Isipokuwa wale mnaowapata vitani kwani mnaruhusiwa kuwaingilia wanawake hao baada ya kuthibitisha kuwa si wajawazito. Aya hii ilishuka kwa ajili hiyo. Imam Ahmad aliandika kuwa Abu Said Al-Khudri رضي الله عنه alisema, “Tuliwateka baadhi ya wanawake katika eneo la Awtas ambalo walikuwa wameolewa, na hatukutaka kuwaingilia kwa sababu walikuwa na waume. Hivyo tulimuuliza Mtume ﷺ kadhia hii, na Aya hii iliteremshwa,

﴿وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ﴾

“Na Wanawake wenye waume, isipokuwa waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia.”

Hivyo tuliwaingilia kimwili wanawake hao.”¹ Haya ni maneno aliyoyakusanya Al-Tirmidh², An-Nasai³, Ibn Jarir⁴ na Muslim katika sahihi yake.⁵ Kauli ya Allah

تعالى،

﴿كَتَبَ اللَّهُ عَلَيْكُمْ﴾

“Ndiyo Sharia ya Mwenyezi Mungu juu yenu.” Maana yake: Kuharamishwa huku kumelazimishwa juu yenu, kwa hiyo shikamana na Kitabu cha Allah تعالى، msichupe mipaka Yake, na ushikamane na Sharia na Amri Zake.

¹ Ahmad 3:72.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 4:282.

³ An-Nasai katika Al-Kubra 3:308.

⁴ At - Tabari 8:153.

⁵ Muslim 2:1080

Kuhalalishiwa Wanawake Wasiokuwa Hao Waliotajwa

Allah تعالى Amesema,

وَأُحِلَّ لَكُمْ مَا وَرَاءَ ذَلِكَ

“Na mmehalalishiwa wasiokuwa hao.”

Tafsiri yake ni kuwa mmeruhusiwa kuoa wanawake minghairi ya wale waliotajwa hapa, kama Ata na wengine walivyotaja.¹

أَنْ تَبْتَغُوا بِأَمْوَالِكُمْ مُحْصِينَ غَيْرَ مُسْفِحِينَ

**“Mtafute kwa mali yenu kwa kuowa
Wenye kujilinda na machafu na sio wazinifu.”**

Maana yake: Unaruhusiwa kutumia mali yako kuoa mpaka wake wanne na kununua wajakazi kama upendavyo kwa njia za halali.

مُحْصِينَ غَيْرَ مُسْفِحِينَ

“Wenye kujilinda na machafu na sio wazinifu.” Kauli ya Allah تعالى,

فَمَا اسْتَمْتَعْتُمْ بِهِ مِنْهُنَّ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ فَرِيضَةً

“Kama mnavyostarehe nao, basi wapeni mahari yao kwa kuwa ni wajibu.”

Maana yake: Kustarehe nao kimwili, kuwapa mahari yao stahili kama fidia. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Anasema,

وَكَيْفَ تَأْخُذُونَهُ وَقَدْ أَفْضَى بَعْضُكُمْ إِلَى بَعْضٍ

“Na mtachukuae na ilhali mmekwisha ingiliana nyinyi kwa nyinyi.”

وَأْتُوا النِّسَاءَ صِدْقَتِهِنَّ خِلَّةً

“Na wapeni wanawake mahari yao ya kuwa ni kipawa.” na,

وَلَا يَحِلُّ لَكُمْ أَنْ تَأْخُذُوا مِمَّا آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا

“Wala si halali kwenu kuchukua chochote mlichowapa wake zenu..” (2:229)

¹ At-Tabari 8/172.

Maelezo Juu ya Ndoa ya *Mut'ah* na Uharamu wake

Ibn Abbas, Ubayy bin Ka'ab, Sa'id bin Jubayr na As-Suddi رضي الله عنهم walikuwa wakisoma aya hii namna hii,

"Famastamta'tum bihi Minhunna ilaa Ajalin Musammah Faatuhunna ujurahunna faridhwah." (Usomaji huu sio mashuhuri umeongezwa neno '*ilaa Ajalin Musammah*').

Mujahid alisema,

فَمَا أَسْتَمْتَعْتُمْ بِهِ مِنْهُنَّ فَفَاتُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ فَرِيضَةً

"Kama mnavyostarehe nao, basi wapeni mahari yao kwa kuwa ni wajibu."

Iliteremshwa kwa mintarafu ya ndoa ya *Mut'ah*.¹ *Mut'ah* ni ndoa inayoisha katika muda uliopangwa kabla. Katika Sahihi Mbili, imeandikwa kuwa Amiril-Muuminina Ali bin Abi Talib رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alikataza ndoa ya *Mut'ah* na kula nyama ya punda wa mjini (anayefugwa) katika vita ya Khaibar."² Zaidi ya hayo, katika Sahih yake, Muslim aliandika kuwa Ar-Rabi bin Subrah bin Ma'bad Al-Juhani alisema kuwa baba yake alisema kuwa alifuatana na Mtume ﷺ siku ya kutekwa Makkah, na Mtume ﷺ alisema,

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ! إِنِّي كُنْتُ أَذْنُتُ لَكُمْ فِي الْأَسْتِمْتَاعِ مِنَ النِّسَاءِ، وَإِنَّ اللَّهَ قَدْ حَرَّمَ ذَلِكَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، فَمَنْ كَانَ عِنْدَهُ مِنْهُنَّ شَيْءٌ فَلْيُخَلِّ سَبِيلَهُ، وَلَا تَأْخُذُوا بِمَا آتَيْتُمُوهُنَّ شَيْئًا»

"Enyi watu niliwaruhusu kuoa wanawake kwa ndoa ya Mut'ah kabla ya leo. Sasa Allah Ameiharamisha mpaka siku ya Kiyama. Kwa hiyo iwapo kuna mmoja wenu ana mke wa Mut'ah amruhusu aondoke, na msichukue chochote katika vile mlivyowapa."³

Kauli ya Allah تعالى،

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا تَرَاضَيْتُمْ بِهِ مِنْ بَعْدِ الْفَرِيضَةِ

"Wala hapana lawama juu yenu kwa mtakachokubaliana baada ya kutimiza waajibu."

¹ At – Tabari 8:178.

² Fat'hul Al-Bari 9:590, Muslim 2:1027.

³ Muslim 2:1025.

Inafanana na Kauli Yake nyingine,

وَأَتُوا النِّسَاءَ صَدَقْتِهِنَّ نِحْلَةً

“Na wapeni wanawake mahari yao ya kuwa ni kipawa”

Tafsiri ya Ayah hii: Ukimpa mahari kisha akarudisha yote au sehemu yake huna kosa, naye pia hana dhara. Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema, “Al-Hadhrami alisema, baadhi ya wanaume wanapanga kima cha mahari, lakini baadaye wanapata matatizo ya uchumi.” Akasema, “Basi hapana makosa juu yenu, Enyi watu, kuhusu maafikiano ya pamoja ya kima kuamuliwa.”¹ Maana yake: Endapo atasamehe sehemu ya mahari, hivyo nyie wanaume mnaruhusiwa kukubali. Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٢٥﴾

“Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kujua na Mwenye Hikima”

Inafaa hapa, baada ya Allah تعالى Kutaja kukatazwa huko.

وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ مِنْكُمْ طَوْلًا أَنْ يَنْكِحَ الْمُحْصَنَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ فَمِنْ مَا مَلَكَتْ
 أَيْمَانُكُمْ مِنْ فَتْيَتِكُمْ الْمُؤْمِنَاتِ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِكُمْ بَعْضُكُمْ مِنْ بَعْضٍ فَانكِحُوهُنَّ
 بِإِذْنِ أَهْلِهِنَّ وَأَتُوهُنَّ أَجُورَهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ مُحْصَنَاتٍ غَيْرِ مُسْفِحَاتٍ وَلَا مُتَّخِذَاتِ
 أَخْدَانٍ فَإِذَا أُحْصِنَ فَإِنَّ أَتَيْتَ بِفَنِحْشَةٍ فَعَلَيْتَ نِصْفَ مَا عَلَى الْمُحْصَنَاتِ مِنْ
 الْعَذَابِ ذَلِكَ لِمَنْ خَشِيَ الْعَنَتَ مِنْكُمْ وَأَنْ تَصْبِرُوا خَيْرٌ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ ﴿٢٥﴾

25. Na asiyeweza kati yenu kupata mali ya kuolea wanawake wa kiungwana Waumini, na aoe katika vijakazi Waumini iliyo wamiliki mikono yenu ya kulia. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa imani yenu. Nyinyi mmetokana wenyewe kwa wenyewe. Basi waoeni kwa idhini ya watu wao, na wapeni mahari yao kama ada, wawe wanawake wema, si makahaba wala si mahawara. Na wanapo olewa kisha wakafanya uchafu basi adhabu yao itakuwa ni nusu ya adhabu waliyowekewa waungwana. Hayo ni kwa yule miongoni mwenu anayeogopa kuingia katika zinaa. Na mkisubiri ndio bora

¹ At - Tabari 8:180.

kwenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.” (4:25).

Kujuzu Jambo la Kuoa Mjakazi kama Mtu Hawezi Kuoa Mwanamke Huru.

Allah تعالى Amesema wale wasio na uwezo,

مِنْكُمْ طَوَّالًا

“Kupata mali.” Uwezo wa kifedha,

أَنْ يَنْكِحَ الْمُحْصَنَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ

“Ya kuolea wanawake wa kiungwana Waumini.”

Maana yake: Waumini walio huru, waliojilinda na waaminifu.

فَمِنْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِّنْ فِتْيَانِكُمُ الْمُؤْمِنَاتِ

“Na aoe katika vijakazi Waumini iliyo wamiliki mikono yenu ya kulia.”

Maana yake: Wanaruhusiwa kuoa wajakazi waumini wanaomilikiwa na Waumini.

وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِكُمْ بَعْضُكُمْ مِّنْ بَعْضٍ

“Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa imani yenu. Nyinyi mmetokana wenyewe kwa wenyewe.”

Allah تعالى ni Mjuzi wa siri za vitu vyote, bali nyie binadamu mnafahamu mambo yaliyo dhahiri tu. Kisha Allah تعالى Amesema,

فَأَنْكِحُوهُنَّ بِإِذْنِ أَهْلِهِنَّ

“Basi waoeni kwa idhini ya watu wao.” Inaonesha kuwa bwana ndiye walii anayehusika na mjakazi, na hivyo hawezi kuolewa bila idhini yake. Bwana pia anahusika na ni walii wa Mtumwa wake (mwanaume) na hawawezi kuoana bila idhini yake. Hadithi inaelezea,

«أَيُّمَا عَبْدٍ تَزَوَّجَ بِغَيْرِ إِذْنِ مَوْلَاهُ، فَهُوَ غَايِرٌ»

“Mtumwa yeyote anayeo bila ya idhini ya Bwana wake ni kahaba.”¹

¹ Abu Dawud 2:563.

Ikiwa kijakazi anamilikiwa na mwanamke, basi ataozeshwa na mtu mwingine kwa idhini yake.

«لَا تُزَوِّجُ الْمَرَأَةَ الْمَرَأَةَ، وَلَا الْمَرَأَةَ نَفْسَهَا، فَإِنَّ الزَّانِيَةَ هِيَ الَّتِي تُزَوِّجُ نَفْسَهَا»

"Mwanamke hamuozeshi mwanamke mwenzie, au mwenyewe isipokuwa mzinifu ndiye hujjozesha."¹

وَأَتَوْهُنَّ أَجُورَهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ

"Na wapeni mahari yao kama ada."

Tafsiri yake ni kuwa walipeni mahari yao kwa uadilifu na msibakize kitu kwa kuwadhalilisha kwa kuwa ni watumwa wanaomilikiwa. Kauli ya Allah تعالى،

مُحْصَنَاتٍ

"Wawe wanawake wema..."

Maana yake: Ni wanawake wanaojiheshimu ambao si wazinzi. Kwa ajili hiyo Allah تعالى Amesema,

غَيْرِ مُسْلِفَاتٍ

"...Si makahaba.."

Akiwakusudia wanawake wazinzi ambao hawajiepushi na uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa na wale wanaowataka. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa wanawake wazinifu ni makahaba, ambao hawamkatai yeyote anayewataka. Ambapo,

وَلَا مُتَّخِذَاتِ أَحْدَانٍ

"Wala si waliowekwa kinyumba."

Inakusudiwa kuwa na marafiki wa kiume.² Hadithi sawa na hiyo ilisimuliwa na Abu Hurayrah, Mujahid, Ash-Shabii, Adh-dhahhak, Al-Ata Khurasani, Yahya bin Abi Kathir, Muqatil bin Hayyan na As-Suddi.³ Wote walisema kuwa ni marafiki wa kiume.

¹ Ibn Majah 1:606

² At - Tabari 8:193.

³ At - Tabari 8:194.

Adhabu ya Mjakazi Mzinifu ni Nusu ya Mwanamke Huru Asiyeolewa,

Allah تعالى Amesema,

فَإِذَا أَحْصِنَّ فَإِنَّ أَتَيْنَ بِفَدْحِشَةٍ فَعَلَيْهِنَّ نِصْفُ مَا عَلَى الْمُحْصَنَاتِ مِنَ الْعَذَابِ

“Na wanapoolewa kisha wakafanya uchafu basi adhabu yao itakuwa ni nusu ya adhabu waliyowekewa waungwana.”

Muradi wa ‘Uungwana’ (mtumwa aliyeachwa huru) hapa ni kuozechwa, kwani muelekeo wa Aya unatoa dalili juu yake. Kauli ya Allah,

وَمَنْ لَّمْ يَسْتَطِعْ مِنْكُمْ طَوْلاً أَنْ يَنْكِحَ الْمُحْصَنَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ فَمَنْ مَّا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِّن فَتَيَاتِكُمُ الْمُؤْمِنَاتِ

“Na asiyeweza kati yenu kupata mali ya kuolea wanawake wa kiungwana Waumini, na aoe katika vijakazi Waumini iliyo wamiliki mikono yenu ya kulia.”

Kwa hiyo, kwa kuwa Aya tukufu ni kuhusu vijakazi waislamu hivyo,

فَإِذَا أَحْصِنَّ

“Na wanapoolewa.” Inaturejesha wakati (vihakazi Waislamu) wanapoolewa, kama walivyosema Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine.¹ Kauli ya Allah تعالى,

نِصْفُ مَا عَلَى الْمُحْصَنَاتِ مِنَ الْعَذَابِ

“Basi adhabu yao itakuwa ni nusu ya adhabu waliyowekewa waungwana.”

Muradi wake ni adhabu ambayo inaweza kugawika, mfano mijeledi inayohisabika na sio *Rajm* kupigwa mawe. Allah تعالى Ndiye Ajuaye. Kauli ya Allah تعالى,

ذَلِكَ لِمَنْ خَشِيَ الْعَنَتَ مِنْكُمْ

“Hayo ni kwa yule miongoni mwenu anayeogopa kuingia katika zinaa.”

¹ At - Tabari 8:202.

Inaonesha kuwa kuoa mjakazi madhali mtu anatimiza masharti husika ni kwa wale tu wanaochelea kupoteza heshima yao na wanashindwa kujizuia kufanya zinaa. Katika mazingira hayo magumu, mtu anaruhusiwa kuoa mjakazi hata hivyo ni aula zaidi kujizuia kuoa mjakazi na kuvuta subira, vinginevyo watoto watakuwa wa Bwana wa Mjakazi. Allah تعالى Anasema,

وَأَنْ تَصْبِرُوا خَيْرٌ لَّكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٥﴾

“Na mkisubiri ndio bora kwenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusamehe na Mwenye Kurehemu.”

* * *

يُرِيدُ اللَّهُ لِيُبَيِّنَ لَكُمْ وَيَهْدِيَكُمْ
 سُنَنَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَيَتُوبَ
 عَلَيْكُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٢٦﴾ وَاللَّهُ يُرِيدُ أَنْ
 يَتُوبَ عَلَيْكُمْ وَيُرِيدُ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الشَّهَوَاتِ أَنْ
 تَمِيلُوا مِيلًا عَظِيمًا ﴿٢٧﴾ يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُخَفِّفَ
 عَنكُمْ ۖ وَخَلَقَ الْإِنْسَانَ ضَعِيفًا ﴿٢٨﴾ يَتَأْتِيهَا
 الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ
 بِالْبَاطِلِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً عَنْ
 تَرَاضٍ مِّنْكُمْ ۖ وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ۚ إِنَّ
 اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٩﴾ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ
 عُذُوْنَا وَظَلْمًا فَسَوْفَ نُضَلِّهِ نَارًا ۚ
 وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٣٠﴾ إِنْ
 تَجْتَنِبُوا كَبَائِرَ مَا تُنْهَوْنَ عَنْهُ
 نُكَفِّرْ عَنكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَنُدْخِلْكُمْ
 مُدْخَلًا كَرِيمًا ﴿٣١﴾ وَلَا تَتَمَنَّوْا مَا
 فَضَّلَ اللَّهُ بِهِ بَعْضَكُمْ عَلَى بَعْضٍ
 لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا كَتَبْنَا ۗ
 وَلِلنِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا كَتَبْنَا ۚ
 وَسَأَلُوا اللَّهَ مِنْ فَضْلِهِ ۗ إِنَّ
 اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٢﴾
 وَلِكُلِّ جَعَلْنَا مَوَالِيَ مِمَّا
 تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ ۚ
 وَالَّذِينَ عَقَدَتْ أَيْمَنُكُمْ
 فَفَاتُوهُمْ نَصِيْبَهُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ
 كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدًا ﴿٣٣﴾

يُرِيدُ اللَّهُ لِيُبَيِّنَ لَكُمْ وَيَهْدِيَكُمْ
 سُنَنَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَيَتُوبَ
 عَلَيْكُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٢٦﴾ وَاللَّهُ يُرِيدُ أَنْ
 يَتُوبَ عَلَيْكُمْ وَيُرِيدُ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الشَّهَوَاتِ أَنْ
 تَمِيلُوا مِيلًا عَظِيمًا ﴿٢٧﴾ يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُخَفِّفَ
 عَنكُمْ ۖ وَخَلَقَ الْإِنْسَانَ ضَعِيفًا ﴿٢٨﴾

26. Mwenyezi Mungu Anataka Kukubainishieni na Kukuongozeni nyendo za waliokuwa kabla yenu, na (Anapenda) Kukukha fishieni. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye Hekima.

27. Na Mwenyezi Mungu Anataka kukutakaseni kutokana na madhambi, na wanaotaka kufuata mata-manio wanataka mkenge-uke makengeuko makubwa.

28. Mwenyezi Mungu Anataka Kukupunguzieni taabu, na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.

Allah تعالیٰ Anawaeleza waumini yale Aliyoyahalalisha na yale Aliyoyaharamisha katika surah hii na nyinginezo.

وَيَهْدِيكُمْ سُنَنَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ

“Na Kukuongozeni nyendo za waliokuwa kabla yenu.”

Maana yake: Unyoofu wao na namna ya kutii Amri Azipendazo na Anazoziridhia.

وَيَتُوبَ عَلَيْكُمْ

“...na (Anapenda) Kukukhafishieni..”

Maana yake: Madhambi na makosa,

وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

“ Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye Hekima.”

Maana yake: Katika Amri, Sheria, na Vitendo. Na Kauli ya Allah تعالى,

وَيُرِيدُ الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الشَّهَوَاتِ أَنْ تَمِيلُوا مَيْلًا عَظِيمًا

“Na wanaotaka kufuata matamanio wanataka mkengeuke makengeuko makubwa.”

Inadhihirisha kuwa wafuasi wa shetani katika Mayahudi, Wakristo, Mushirikina na wazunifu wanatamani mngochukua njia potofu badala ya njia sahihi,

يُرِيدُ اللَّهُ أَنْ يُخَفِّفَ عَنْكُمْ

“Mwenyezi Mungu Anataka Kukupunguzieni taabu.”

Maana yake: Katika Sheria Zake, Amri, kila Alichoharamisha na Anachowaamrisha. Kwa sababu hii ndio maana Allah تعالى Akawaruhusu wanaume huru kuoja wajakazi kwa masharti fulani, kama walivyodhukuru Mujahid na wenziwe.¹

وَخُلِقَ الْإِنْسَانُ ضَعِيفًا

“Na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.”

Ndio maana katika hali hii, amefanyiwa amri nyepesi sababu ya udhaifu wake. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Tawus, alisema kuwa,

¹ At - Tabari 8:172.

وَحُلِقَ الْإِنْسَانُ ضَعِيفًا ﴿٢٦﴾

“Na mwanaadamu ameumbwa dhaifu.”

“Kuhusu wanawake.”¹ Waki'i amesema, “Akili ya mwanaume huruka pale anapokuwa na wanawake.”

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً عَن
تَرَاضٍ مِّنْكُمْ ؕ وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ ؕ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٧﴾ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ
عَدُوًّا وَظُلْمًا فَسَوْفَ نُصَلِّبُهُ نَارًا ؕ وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٢٨﴾ إِنْ تَجْتَنِبُوا
كَبَائِرَ مَا نُهَيْتُمْ عَنْهُ نُكْفِّرْ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَنُدْخِلْكُمْ مُدْخَلًا كَرِيمًا ﴿٢٩﴾

29. Enyi mlioamini! Msiliane Mali yenu kwa dhulma, isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana wenyewe. Wala msijiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwarehemuni.

30. Na mwenye kutenda hayo kwa uadui na udhalimu, basi huyo Tutamwingiza Motoni. Na hilo ni jepesi kwa Mwenyezi Mungu.

31. Mkiyaepuka makubwa mnayokatazwa, Tutakufutieni makosa yenu madogo, na Tutakingizeni mahali patukufu.

Kuharamishwa Mali iliyochumwa kwa Haramu

Allah تعالی Aliye juu ya vyote na Aliyetukuka zaidi, Anawakataza waja Wake dhidi ya kutwaa mali ya wengine kwa kutumia njia za batili, za hila na za haramu kama vile Riba, Kamari na njia nyingine zinazoonekana kuwa halali, lakini Allah تعالی Anayajua hayo uhakika wake, kuwa wahusika wanafanya riba.

Ibn Jarir رحمه الله تعالی aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo juu ya mtu anunuaye nguo na kusema kuwa, ‘akipenda atabaki nayo au atarejesha pamoja na Dirham za ziada.’ Amesema Ibn Jarir رحمه الله تعالی kuwa hivi ndivyo alivyokusudia Allah تعالی Aliposema,

¹At - Tabari 8:216.

لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ

“Wala Msiliane Mali yenu Kwa dhulma.”¹

Ali bin Abi Talha alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Allah تعالى Alipotoremsha,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ

“Enyi mlioamini! Msiliane Mali yenu Kwa dhulma.”

Baadhi ya waislamu walisema, Allah تعالى Ametukataza kula mali ya mtu mwingine kinyume cha sharia, na chakula ndio mali yetu iliyo bora kwa hiyo hapana yeyote miongoni mwetu anayeruhusiwa chakula cha mwingine. Baada ya hapo Allah تعالى Aliteremsha,

لَيْسَ عَلَى الْأَعْمَى حَرَجٌ

“Si vibaya kwa kipofu...”, mpaka mwisho wa aya (24:61),

Qatadah alisema vivyo hivyo. Allah تعالى Amesema,

إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً عَنْ تَرَاضٍ مِنْكُمْ

“Isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana wenyewe.”

Maana yake: Msirejee katika njia haramu za kupata mali. Hata hivyo si vibaya katika miamala ya kibiashara kati ya mnunuzi na muuzaji, kwa maridhiano kiasi ambacho fedha zinachumwa kihalali katika miamala hiyo na hiyo ikawa sababu ya kuchuma mali kama Alivyosema Allah تعالى katika Kauli Yake,

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ

“Wala usiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Amekataza isipokuwa kwa haki.” (6:151)

Na kama katika Kauli Yake nyingine,

¹At - Tabari 8:217.

لَا يَذُوقُونَ فِيهَا الْمَوْتَ إِلَّا الْمَوْتَةَ الْأُولَىٰ

“Humo hawataonja mauti ila mauti yale ya kwanza.” (44:56)

Mujahid alisema akiielezea aya hii,

إِلَّا أَنْ تَكُونَ تِجَارَةً عَن تَرَاضٍ مِّنْكُمْ

“Isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana wenyewe.”

Muradi wake ni kuwa, “kwa kuuza au kununua au kumpa mtu zawadi.” Ibn Jarir رحمه الله تعالى ameandika kauli hii.¹

Uchaguzi wa Kununua au Kuuza Kabla ya Kuachana Sehemu ya ‘Maridhiano ya Pande Mbili” katika Biashara.

Ridhaa katika kuaminiana kibiashara inafwatiwa pale pande zote zina khiari au kuvunja makubaliano kabla ya kuondoka.

Katika sahihi mbili imeandikwa kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْبَيْعَانِ بِالْخِيَارِ مَا لَمْ يَنْفَرَقَا»

“Wauziano (muuzaji na mnunuzi) wana haki ya kubadili maafikiano iwapo hawajatawanyika.”²

Kwa maandishi ya Bukhari Hadithi hii inasomeka,

«إِذَا تَبَايَعَ الرَّجُلَانِ فَكُلُّ وَاحِدٍ مِّنْهُمَا بِالْخِيَارِ، مَا لَمْ يَنْفَرَقَا»

“Watu wawili wanapouziana wana haki ya kubadilisha maamuzi madhali hawatakuwa wameachana.”³

¹ At - Tabari 8:221.

² Fat’hul Al-Bari 4:385; Muslim 3:1163.

³ Fat’hul Al-Bari 4:390.

Makatazo na Maonyo Dhidi ya Kuaa Nafsi

Allah تعالى Amesema,

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ

“Wala msijiuwe.”

Kwa kuvunja Amri ya Allah تعالى, kuangukia kwenye makatazo, makosa na kula mali za watu kwa batili,

إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٦﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwarehemuni.”

Kwa yale Aliyowaamuru kuyatenda na Aliyokukatazeni kujiepusha nayo.

Imam Ahmad amemnukuu Amr bin Al-As رضي الله عنه akisema, Mtume ﷺ alipokwenda kwenye vita ya *Dhat – As-Salasil*, niliota na kumwaga manii usiku uliokuwa na baridi sana na nikachelea kukoga nisije kufa. Hivyo nilitayamamu (kwa mchanga tohara) na nikakisalisha kikosi changu Sala ya Subhi. Niliporejea kwa Mtume ﷺ nilimueleza yaliyonitokea na akasema,

«يَا عَمْرُو! صَلَّيْتَ بِأَصْحَابِكَ وَأَنْتَ جُنُبٌ!»

“Ewe Amr! Umewaswalisha watu wako nawe una Janaba?”

Nilijibu, “Ewe Mjumbe wa Allah! Niliota nikamwaga manii usiku wenye baridi kali na nikachelea iwapo ningekoga ningekufa, na nikakumbuka Kauli ya Allah,

وَلَا تَقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٦﴾

“Wala msijiuwe. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwarehemuni.”

Hivyo nilitayamamu na kuswali. “Mtume ﷺ alitabasamu na hakunena lolote.” (Ahmad 4:203–204).

Hadithi hii imesimuliwa na Abu Dawud رضي الله عنه. (Abu Dawud 334). Ibn Marduwayah رحمه الله تعالى aliitaja Aya hii tukufu na kisha akaripoti kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ قَتَلَ نَفْسَهُ بِحَدِيدَةٍ، فَحَدِيدَتُهُ فِي يَدِهِ، يَجَأُ بِهَا بَطْنَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِي نَارِ جَهَنَّمَ،
خَالِدًا مُخَلَّدًا فِيهَا أَبَدًا، وَمَنْ قَتَلَ نَفْسَهُ بِسُمِّ فُسْمُهُ فِي يَدِهِ، يَتَحَسَّاهُ فِي نَارِ جَهَنَّمَ،
خَالِدًا مُخَلَّدًا فِيهَا أَبَدًا، وَمَنْ تَرَدَّى مِنْ جَبَلٍ فَقَتَلَ نَفْسَهُ، فَهُوَ مُتَرَدِّدٌ فِي نَارِ جَهَنَّمَ،
خَالِدًا مُخَلَّدًا فِيهَا أَبَدًا»

“Mwenye kujiuwa kwa chuma, basi zana hiyo itabakia mkononi mwake na kujipiga nayo ndani ya Moto wa Jahannamu milele. Yeyote atakayejiua kwa sumu, basi sumu yake ataishika mkononi na ataendelea kuinywa akiwa ndani ya moto wa Jahannam milele. Yeyote atakayejiuwa kwa kujitupa kutoka juu ya mlima, ataendelea kuanguka ndani ya Moto wa Jahannam milele.”

Hadithi hii iliandikwa pia katika Sahih Mbili (Al-Bukhari 5778 na Muslim 109), Abu Qilaabah alisema kuwa Thabit bin Adhahhak رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ قَتَلَ نَفْسَهُ بِشَيْءٍ، عُذِّبَ بِهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

“Yeyote atakayejiua kwa ala, ataadhibiwa nayo siku ya Kiyama.”

Hadithi hii imekusanywa na Al-Jamaa katika vitabu vyao. Ndio maana Allah تعالی Akasema,

وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ عُدْوَانًا وَظُلْمًا

“Na mwenye kutenda hayo kwa uadui na udhalimu”

Maana yake: Yeyote anayefanya lile lililokatazwa na Allah تعالی miongoni mwa kuchupa mipaka na dhuluma – ilhali akijua kuwa yamekatazwa na bado akadiriki kuyafanya.

فَسَوْفَ نُصَلِّيهِ نَارًا

“Basi huyo Tutamuingiza Motoni.”

Na haya ni maonyo makali na makamio thabiti. Kwa hiyo kila mtu mwenye akili lazima atahadhari nayo, hasa wale wanaosikia mawaidha na wakaya-zingatia.

Madhambi Madogo Yatasamehewa Iwapo Mtu Atajizuia na Madhambi Makubwa,

Allah تعالی Amesema,

إِن تَجْتَبِئُوا كِبَايِرَ مَا تَنْهَوْنَ عَنْهُ تُكْفِرَ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ

“Mkiyaepuka makubwa mnayokatazwa, Tutakufutieni makosa yenu madogo.”

Inakusudiwa kuwa, pindipo mtajiweka mbali na amali kubwa zilizo mbovu mlizokatazwa, “Tutawasamehe makosa madogo na Tutakuingizeni Peponi.” Kwa sababu hii Allah تعالی Amesema,

وَوَدَّخَلَّكُمْ مُدْخَلَ كَرِيمًا ﴿٥٥﴾

“Na Tutakuingizeni mahali patukufu.”

Zipo Hadithi nyingi juu ya Ayah hii tukufu. Imam Ahmad aliandika kuwa Salman Al-Farisi رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ aliniambia, “Je unajua maana ya siku ya Al-Jum’ah?” Nikajibu, “Ni siku ambayo Allah تعالی Alimuumba baba yetu (Adam); akasema,

«لَكِنْ أُذِرِي مَا يَوْمَ الْجُمُعَةِ، لَا يَتَطَهَّرُ الرَّجُلُ فَيُحْسِنُ طَهْرَهُ، ثُمَّ يَأْتِي الْجُمُعَةَ فَيَنْصِتُ حَتَّى يَفْضِيَ الْإِمَامُ صَلَاتَهُ، إِلَّا كَانَ كَفَّارَةً لَهُ مَا بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْجُمُعَةِ الْمُقْبِلَةِ، مَا اجْتَنِبَ الْمُقْتَلَةَ»

“Lakini najua mimi siku ya Jumua’ah. Yeyote atakayekoga kisha akajinadhifisha kwa kadri ya uwezo wake kisha akaelekea kuswali Al-Jumua’ah; na akawa kimya mpaka Imam akamaliza Swala, madhambi yake kati ya sasa na Ijumaa ijayo yatasamehewa, almuradi alijiepusha na madhambi makubwa.”

Bukhari aliandika hadithi kama hii aliyopokea kutoka kwa Salman رضي الله عنه.

Ufafanuzi wa Madhambi Saba Yaangamizayo

Katika Sahih Mbili, imeandikwa kuwa Abu Hurayrah رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«اجْتَنُوا السَّبْعَ الْمَوْبِقَاتِ»

“Jiepusheni na madhambi saba yaangamizayo.”

Watu walidodosa, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Ni yapi hayo?’ Alijibu,

«الشُّرْكَ بِاللهِ، وَقَتْلُ النَّفْسِ الَّتِي حَرَّمَ اللهُ إِلَّا بِالْحَقِّ، وَالسَّخْرِ، وَأَكْلُ الرِّبَا، وَأَكْلُ مَالِ الْيَتِيمِ، وَالتَّوَلَّى يَوْمَ الرَّحْفِ، وَقَذْفُ الْمُحْصَنَاتِ الْمُؤْمِنَاتِ الْعَافِيَاتِ»

“Kumshirikisha Mwenyezi Mungu, kuua nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Ameiharamisha isipokuwa kwa haki, uchawi, kula Riba, kula mali ya yatima, kukimbia siku ya vita, na kuwasingizia wanawake wema, ambao hawafikirii jambo ambalo litawatoa katika wema wao, na ni waumini wazuri.”¹

Hadithi Nyingine Inadhukuru Ushahidi wa Uongo

Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Anas bin Malik رضى الله عنه, aliyesema, Mtume ﷺ alitaja madhambi makubwa, alisema,

«الشُّرْكَ بِاللهِ، وَقَتْلُ النَّفْسِ، وَعُقُوقُ الْوَالِدَيْنِ»

“Kumshirikisha Mwenyezi Mungu, kuua nafsi na kuasi wazazi wawili.”

Akasema, akasoma,

«أَلَا أَنْبَيْتُكُمْ بِأَكْبَرِ الْكِبَايِرِ؟» قَالَ: «قَوْلُ الزُّورِ - أَوْ شَهَادَةُ الزُّورِ -»

“Je nikuelezeni kuhusu dhambi kubwa kuliko zote? Kauli ya uzushi au ushahidi wa uongo”

Shu’bah – mmoja wa wasimulizi wa Hadithi alisema, “Yamkini kwa maoni yangu, alisema, “Ushahidi wa urongo.”² Sahihi Mbili ziliandika Hadithi hii kutoka kwa Shu’bah aliyepokea kutoka kwa Anas رضى الله عنه.³

¹ Fat’hul Al-Bari 5:462, Muslim 2:92.

² Ahmad 3:131.

³ Fat’hul Al-Bari 10:419, Muslim 1:91.

Hadithi Nyengine.

Ndani ya Sahih Mbili iliandikwa kuwa Abdur - Rahman bin Abi Bukrah alinena kuwa baba yake alisema, "Mtume ﷺ alisema,

«أَلَا أُتَبِّئُكُمْ بِأَكْبَرِ الْكِبَائِرِ؟»

"Nikufahamisheni kuhusu kubwa zaidi ya madhambi?"

Tukajibu, "Ndiyo, Ewe Mjumbe wa Allah! Akasema

«الْإِشْرَاكُ بِاللَّهِ، وَعُقُوقُ الْوَالِدَيْنِ»

"Kumshirikisha Allah تعالى na kutowatazama wazazi wawili."

Alikuwa anamalizia akawa anashuka kisha akasimama na kusema,

«أَلَا وَشَهَادَةُ الزُّورِ، أَلَا وَقَوْلُ الزُّورِ»

"Jueni na ushahidi wa uongo, na tambueni na kauli ya uongo".

Na aliendelea kukariri na tukataraji asingeendelea.¹

Hadithi Nyingine Inayotaja Kuaa Mtoto.

Ndani ya Sahih Mbili, imeandikwa kuwa Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنه alinena, "Nilimuuliza, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Ni ipi dhambi kubwa zaidi?' Alijibu,

«أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ نِدَاءً وَهُوَ خَلَقَكَ»

"Kumfanyia Allah mshirika ilhali Yeye Peke Yake Ndiye Aliyekuumba".

Nikasema, "Kisha?" Akasema:

«أَنْ تُرَانِي حَلِيلَةَ جَارِكَ»

"Kuzini na mke wa jirani yako."²

Kisha akasoma:

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ

"Na wale wasio muomba mola mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu,..." (25:68) mpaka akafikia,

¹ Fat'hul Al-Bari 5:309, Muslim 1:91.

² Fat'hul Al-Bari 5:350, Muslim 1:90.

إِلَّا مَنْ تَابَ

“Isipokuwa waliotubu...” Hadithi Nyingine ni kutoka kwa Abdullah bin Amr رضي الله عنه na ndani yake imetajwa yamini ya urongo.

Imam Ahmad aliandika kuwa Abdillahi bin Amri رضي الله عنه alinena kuwa Mtume ﷺ alisema,

“Hakika kubwa zaidi ya madhambi ni Kumshirikisha Allah تعالى, kutowahudumia wazazi wawili - au kuua nafsi isiyo na hatia.” (Shubaha hakuwa na uhakika ni ipi moja wapo) - *na kiapo cha urongo.*¹ Alipokea Bukhari, At-Tirmidhi na An-Nasai.

Hadithi Nyengine ya Abdullah bin Amri رضي الله عنه juu ya kusababisha Wazazi Kutukanwa

Abdullah bin Amri رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ مِنْ أَجْبَرِ الْكَبَائِرِ أَنْ يَلْعَنَ الرَّجُلُ وَالِدَيْهِ»

“Hakika katika kubwa zaidi ya madhambi ni mtu kuwatukana wazazi wake.”

Wakauliza; “Inakuaje mtu akawatukana wazazi wake?” Akasema,

«يَسُبُّ الرَّجُلُ أَبَا الرَّجُلِ، فَيَسُبُّ أَبَاهُ، وَيَسُبُّ أُمَّهُ فَيَسُبُّ أُمَّهُ»

“Mtu anamtukana baba wa mtu, naye anamtukania babaye, na mtu anamtukana mama yake mtu, naye akamtukania mama yake.” Hadithi hii ni kwa mujibu wa kauli ya Muslim.² At-Tirmidhi alitaja kuwa ni “Sahih”

Na imethibiti katika Sahih kuwa Mtume ﷺ alisema,

«سَبَابُ الْمُسْلِمِ فُسُوقٌ، وَقِتَالُهُ كُفْرٌ»

“Kumtukana Muislamu ni ufuska na kumpiga ni Ukafiri.”³

¹ Ahmad 2:201; Bukhari 6675; Tuhfat Al-Ahwadhi 3021 na An-Nasai katika Al-Kubra 8:63.

² Muslim Na.90.

³ Bukhari 5973; Muslim 64.

وَلَا تَتَمَنَّوْا مَا فَضَّلَ اللَّهُ بِهِ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۚ لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا أَكْتَسَبُوا ۚ
وَاللِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا أَكْتَسَبْنَ ۚ وَسَأَلُوا اللَّهَ مِنْ فَضْلِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ

عَلِيمًا ﴿٣٢﴾

“Wala msitamani Alichowafadhili Mwenyezi Mungu baadhi yenu kuliko wengine. Wanaume wana fungu katika walivyovichuma, na wanawake wana fungu katika walivyovichuma. Na muombeni Mwenyezi Mungu Fadhila Zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.” (4:32)

Kukatazwa Kutamani Ambavyo Allah تعالی Amewafadhili Wengine:

Imam Ahmad aliandika kuwa Umm Salamah رضي الله عنها alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Wanaume wanakwenda vitani, lakini sisi hatuendi vitani, na tunapata nusu ya mirathi (ya wapatao wanaume).” Allah تعالی Alishusha,

وَلَا تَتَمَنَّوْا مَا فَضَّلَ اللَّهُ بِهِ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ

“Wala msitamani Alichowafadhili Mwenyezi Mungu baadhi yenu kuliko wengine.”¹

Aidha Tirmidhi aliandika Hadithi hii.² Kauli ya Allah تعالی,

لِلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا أَكْتَسَبُوا ۚ وَاللِّسَاءِ نَصِيبٌ مِّمَّا أَكْتَسَبْنَ

“Wanaume wana fungu katika walivyovichuma, na wanawake wana fungu katika walivyovichuma.”

Kwa mujibu wa Ibn Jarir رحمه الله تعالی, inaonesha kuwa kila mtu atachuma kulingana na kazi yake, atalipwa kama atafanya amali njema, na atapata mateso kama amali zake ni mbovu.

Ilisemwa pia kuwa Ayah hii inazungumzia mirathi, ikidhihirisha kila mmoja atapata stahiki yake ya mirathi, kama Alwaliby³ alivyopokea kutoka kwa Ibn Abbas. Kisha Allah تعالی Aliwaelekeza waja kwa yale yenye faida nao.

¹ Ahmad 6:322.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 8:375, 377.

³ Ali bin Abi Talhah.

وَسْئَلُوا اللَّهَ مِنْ فَضْلِهِ

“Na muombeni Mwenyezi Mungu Fadhila zake.”

Kwa hiyo, Ayah hii inaeleza, “Msitamani vitu walivyoruzukiwa zaidi wengine kuliko nyie, kwani haya ni maamuzi yaliyopitishwa na kutamani kwenu hakutabadili kitu (uamuzi). Hata hivyo, ‘Niombeni katika Fadhila Zangu na Nitakujaalieni, kwani Mimi ni Mkarimu na Mtoaji Zaidi.’” Kisha Allah تعالی Amesema,

إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٣﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

Maana yake: Allah تعالی Anajua yule anayestahili maisha ya dunia, na hivyo Humpa utajiri, na yule anayestahili ufukara Humfukarisha. Aidha Anajua anayestahili Akhera, na Humuongoza kutenda amali zitazomsaidia, na yeyote anayestahili kushindwa, Humzuia kufikia wema na yanayopelekea huko. Hivyo Allah تعالی Amesema,

إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٣﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

وَلِكُلِّ جَعَلْنَا مَوْلَىٰ مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ ۚ وَالَّذِينَ عَقَدَتْ أَيْمَنُكُمْ

فَقَاتُوهُمْ نَصِيحَةً ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدًا ﴿٣٣﴾

“Na kila mmoja Tumemuwekea warithi katika waliyoyaacha wazazi wawili na jamaa. Na mlio fungamana nao ahadi wapeni fungu lao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kila kitu.” (4:33)

Ibn Abbas, Mujahid, Said bin Jubayr, Abu Salih, Qatadah, Zayd bin Aslam, As-Suddi, Adh-dhahak, Muqatil bin Hayyan na wengineo رضي الله عنهم walizungumzia Kauli ya Allah تعالی,

وَلِكُلِّ جَعَلْنَا مَوْلَىٰ

“Na kila mmoja Tumemuwekea warithi.” Muradi wake, “warithi”¹ imepokewa pia Ibn Abbas رحمه الله تعالی alisema, ‘Mawali ni jamaa.’ Ibn Jarir رحمه الله تعالی alisema, “Waarabu humuita binamu Mawla.” Ibn Jarir رحمه الله تعالی aliendelea na Kauli ya Allah تعالی,

¹ At - Tabari 8:270–271.

مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ

"Katika waliyoyaacha wazazi wawili na jamaa."

Maana yake: Kutokana na aliyorithi kutoka kwa wazazi wake na jamaa zake. Kwa hiyo maana ya Ayah inakuwa: "Kwenu nyote, Enyi watu, tuliwateua jamaa (kama vile watoto) ambao baadaye watarithi yale mliyorithi kutoka kwa wazazi wenu na jamaa zenu."

وَالَّذِينَ عَقَدْتَ أَيْمَانُكُمْ فَفَاتُوهُمْ نَصِيهِمْ

"Na mliofungamana nao ahadi wapeni fungu lao."

Muradi wake, wale uliyochukua ahadi ya udugu, wape kasma yao ya mirathi kutimiza ahadi uliyowapa.

Allah تعالی Ameshuhudia ulipowaahidi na kuagana nao. Ada hii ilifuatwa mwanzoni mwa Uislamu, baadaye ilifutwa pale Waislamu walipotakiwa kutekeleza miadi yao ya udugu waliyoitoa, lakini wasifanye ahadi nyengine baada ya pale. Bukhari alipokea kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

وَلِكُلِّ جَعَلْنَا مَوَالِي

"Na kila mmoja Tumemuwekea warithi."

Maana yake: Warithi;

وَالَّذِينَ عَقَدْتَ أَيْمَانُكُمْ

"Na mlio fungamana nao ahadi."

Muhajirina walipofika Madina walikuwa wakiwarithi Ansaar kwa sababu ya uhusiano wa kidugu ulioanzishwa na Mtume ﷺ kati yao (Muhajirina na Ansar). Aya hii iliposhuka,

وَلِكُلِّ جَعَلْنَا مَوَالِي

"Na kila mmoja Tumemuwekea warithi."

Ilivunja (udugu wa agano kuhusu urathi)." Kisha akasema katika "Aya,

وَالَّذِينَ عَقَدَتِ أَيْمَانُكُمْ فَكَاثُرُهُمْ نَصِيحُهُمْ

“Na mlio fungamana nao ahadi wapeni fungu lao.”

“Ilibakia masuala ya ushirikiano, na mashauriano, ambapo mambo ya mirathi hayakuhusika na ikaruhusiwa kutoa wasia kwa mtu ambaye mwanzo alikuwa na haki ya kurithi.”¹ (Haki ya kurithi kwa fungamano).

* * *

¹ Fat’hul Al-Bari 8:96.

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ بِمَا فَضَّلَ اللَّهُ بَعْضَهُمْ
 عَلَى بَعْضٍ وَبِمَا أَنْفَقُوا مِنْ أَمْوَالِهِمْ ۚ فَالَّذِينَ
 قَنَبْتُمْ حَفِظْتُ لَهُمْ لِيُحْفَظُوا بِمَا حَفِظَ اللَّهُ ۗ وَالَّذِينَ
 تُخَافُونَ فِي الدِّينِ فَاعْلَمُوا أَنَّهُمْ لَكُمْ حِصْنٌ كَمَا
 أَنْفَقْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا
 حَكِيمًا ۗ وَأَصْرِبُوا فِي الْيَمِينِ ۗ وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ
 بَيْنِهِمَا فَابْتِغُوا حَكْمًا مِنَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا
 حَكِيمًا ۗ وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۗ
 وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۗ وَبِالزَّوْجَاتِ
 كَمَا أَنْفَقْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا
 حَكِيمًا ۗ فَخُورًا ۗ

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ بِمَا
 فَضَّلَ اللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ وَبِمَا
 أَنْفَقُوا مِنْ أَمْوَالِهِمْ ۚ فَالَّذِينَ
 قَنَبْتُمْ حَفِظْتُ لَهُمْ لِيُحْفَظُوا بِمَا حَفِظَ
 اللَّهُ ۗ وَالَّذِينَ تُخَافُونَ فِي الدِّينِ
 فَاعْلَمُوا أَنَّهُمْ لَكُمْ حِصْنٌ كَمَا
 أَنْفَقْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ۗ وَأَصْرِبُوا فِي
 الْيَمِينِ ۗ وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا
 فَابْتِغُوا حَكْمًا مِنَ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ۗ وَأَعْبُدُوا اللَّهَ
 وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۗ وَبِالْوَالِدَيْنِ
 إِحْسَانًا ۗ وَبِالزَّوْجَاتِ كَمَا أَنْفَقْتُمْ
 فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا
 حَكِيمًا ۗ فَخُورًا ۗ

34. "Wanaume ni wasi-
 mamizi wa wanawake, kwa
 kufadhiliwa na Mwenyezi
 Mungu baadhi yao na kwa
 mali yao wanayoyatoa.
 Basi wanawake wema ni
 wale wenye kutii na wanao
 jilinda hata katika siri kwa
 kuwa Mwenyezi Mungu

Ameamrisha wajilinde. Na ambao mnachelea kutoka katika utiifu wanasihini, muwahame katika malazi na wapigeni. Wakikut'iini msiwatafutie njia ya kuwadhi bure. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Aliye juu na Mkuu."

Allah تعالى Amesema,

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ

"Wanaume ni wasimamizi wa wanawake."

Maana yake, mwanaume ana dhima kwa mwanamke, naye ndiye anayemkimu, kumtunza na kumuongoza pale anapokengeuka.

بِمَا فَضَّلَ اللَّهُ بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ

“Kwa kufadhiliwa na Mwenyezi Mungu baadhi yao juu ya baadhi.”

Muradi wake ni kuwa, kwa sababu wanaume wamewazidi wanawake nao ni mahodari katika baadhi ya majukumu. Kwa sababu hii ndio maana Utume ulikuwa mahsusi kwa wanaume peke yao, vivyo hivyo baadhi ya nafasi za uongozi. Mtume ﷺ alisema,

«لَنْ يُغْلِبَ قَوْمٌ وَلَوْ أَمَرَهُمْ امْرَأَةٌ»

“Hawatafanikiwa watu wanaomtawalisha mwanamke kuwa kiongozi wao.”

Bukhari aliandika Hadithi hii.¹ Mfano wake ni kuwachagua wanawake kuwa majaji au katika nafasi za uongozi,

وَيَمَّا أَنْفَقُوا مِنْ أَمْوَالِهِمْ

“Na kwa mali yao wanayoyatoa.” Maana yake: Mahari, matumizi na gharama mbalimbali ambazo Allah ﷻ Amezishurutisha ndani ya Kitabu Chake na katika Sunnah za Mjumbe Wake kwa wanaume kutumia fedha katika kuwahudumia wanawake. Kwa sababu hii amechaguliwa kuwa mtunzaji wake, kama Allah ﷻ Alivyosema;

وَاللرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ

“Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao.”

Sifa za Mwanamke Muadilifu

Allah ﷻ Amesema,

فَالصَّالِحَاتُ

“Basi wanawake wema...” Wanawake,

قَانِتَاتٌ

“Ni wale wenye kutii.” Yaani wenye kuwatii waume zao kama alivyonena Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengine,²

¹ Fat'hul Al-Bari 7:732.

² At-Tabari 8:294.

حَفِظْتَ لِلْغَيْبِ

“Na wanao jilinda hata katika siri.”

As-Suddi na wengine wamesema muradi wake ni kuwa anajitahidi na analinda mali ya mumewe anapokuwa anatoka. Na Allah تعالى Anasema,

بِمَا حَفِظَ اللَّهُ

“Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Aameamrisha wajilinde.”

Maana yake: Mume aliyelindwa ni yule aliyehifadhiwa na Allah تعالى.¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«خَيْرُ النِّسَاءِ امْرَأَةٌ إِذَا نَظَرَتْ إِلَيْهَا سَرَّتْكَ، وَإِذَا أَمَرْتَهَا أَطَاعَتْكَ، وَإِذَا غَبَّتْ عَنْهَا حَفِظْتَكَ فِي نَفْسِهَا وَمَالِكَ»

“Mwanamke bora ni yule unapomtazama anakuliwaza, na unapomuamuru hukutii, na unapotoka hulinda heshima yako katika nafsi yake na mali yako.”

Baada ya hapo Mtume ﷺ alisoma Aya hii,

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ

“Wanaume ni wasimamaizi wa wanawake.” Mpaka mwisho.²

Imam Ahmad alipokea kuwa Abdur-Rahman bin Awf رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا صَلَّتِ الْمَرْأَةُ حَمْسَهَا، وَصَامَتْ شَهْرَهَا، وَحَفِظَتْ فَرْجَهَا، وَأَطَاعَتْ زَوْجَهَا، قِيلَ لَهَا: ادْخُلِي الْجَنَّةَ مِنْ أَيِّ الْأَبْوَابِ شِئْتَ»

“Pindi atakaposali mwanamke Sala zake tano, akafunga mwezi wa Ramadhani, akatunza heshima na tupu yake na akamtii mumewe, ataambiwa, “Ingia peponi kupitia mlango wowote uupendao.”³

¹ At - Tabari 8:295.

² At - Tabari 8:295.

³ Ahmad 1:191.

Kushughulikia Ujeuri wa Mke.

Allah تعالی Amesema,

وَأَلْتِي تَخَافُونَ ذُشُورَهُمْ.

“Na ambao mnachelea kutoka katika utiifu.”

Ina maana kuwa umuonapo mke anamvunjia heshima mumewe, kwa mfano anapojionesha kuwa yuko juu ya mumewe, anamchukia na kumbughudhi na kadhalika. Dalili hizi zikishajitokeza kwa mwanamke, mume anatakiwa amnasihi na kumkumbusha Adhabu ya Allah تعالی kwa kuwa mtovu wa adabu kwa mume. Bila shaka, Allah تعالی Alimuamrisha sababu ya haki zake zilizo kithiri na yote amtendeavyo. Mtume ﷺ alisema,

«لَوْ كُنْتُ امْرَأًا أَحَدًا أَنْ يَسْجُدَ لِأَحَدٍ، لَأَمَرْتُ الْمَرْأَةَ أَنْ تَسْجُدَ لِزَوْجِهَا، مِنْ عِظَمِ حَقِّهِ عَلَيْهَا»

“Kama ningekuwa wakuamuru mtu amsujudie mwengine, basi ningemuamuru mke amsujudie mumewe kutokana na ukubwa wa haki yake juu yake.”¹

Bukhari alipokea kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا دَعَا الرَّجُلُ امْرَأَتَهُ إِلَى فِرَاشِهِ فَأَبَتْ عَلَيْهِ، لَعَنَتَهَا الْمَلَائِكَةُ حَتَّى تُضْحِكَ»

“Mume akimtaka mke apande kitandani naye akakataa, malaika watamlaani usiku kucha hadi kupambazuke.”²

Muslim aliandika kwa maneno yafuatayo,

«إِذَا بَاتَتِ الْمَرْأَةُ هَاجِرَةً فِرَاشَ زَوْجِهَا، لَعَنَتَهَا الْمَلَائِكَةُ حَتَّى تُضْحِكَ»

“Endapo mke atahama kitanda cha mumewe, atalaaniwa na malaika mpaka kupambazuke.”³

Kwa ajili hiyo Allah تعالی Amesema,

وَأَلْتِي تَخَافُونَ ذُشُورَهُمْ.

“Na ambao mnachelea kutoka katika utiifu.”

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 4:313.

² Fat'hul Al-Bari 9:205.

³ Muslim 2:1059.

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَهْجُرُوهُمْ فِي الْمَضَاجِعِ

"Muwahame katika malazi..."

Ali bin Abi Talhan alisema, Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, "Kwa kuhama, maana yake, kutojamiiana naye, kumpa mgongo wakati wa kulala."¹ Wengine wamesema vivyo hivyo, As-Suddi, Adh-Dhahak, Ikrimah, na Ibn Abbas رضي الله عنهم, katika riwaya, kuna nyongeza, "Kutosema naye, kumnunia."² Katika Sunan na Musnad, wameandika; Muawiyah bin Haydah Al-Qushayri رضي الله عنه aliuliza, "Ewe Mtume wa Allah! Zipi haki za mke juu yetu?" Mtume ﷺ alisema,

«أَنْ تُطْعِمَهَا إِذَا طَعِمْتَ، وَتَكْسُوَهَا إِذَا اكْتَسَيْتَ، وَلَا تَضْرِبَ الْوَجْهَ، وَلَا تُقْبِخَ،
وَلَا تَهْجُرْ إِلَّا فِي الْبَيْتِ»

*"Kumlisha unapokula, kumvisha unapojinunulia nguo, kuepusha kumpiga usoni au kumshutumu, na kutomhama isipokuwa ndani ya nyumba."*³

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَضْرِبُوهُمْ

*"Na wapigeni."*⁴

Maana yake: Iwapo nasaha na kumpuuza kitandani hakuleti matunda yaliyotarajiwa, unaruhusiwa kumtia adabu bila kumpiga kwa nguvu. Muslim aliandika kuwa Jabir رضي الله عنه alisema wakati wa Hajj ya kuaga kuwa Mtume ﷺ alisema:

«وَاتَّقُوا اللَّهَ فِي النِّسَاءِ، فَإِنَّهُنَّ عِنْدَكُمْ عَوَايِنٌ، وَلَكُمْ عَلَيْهِنَّ أَنْ لَا يُوطِئَنَّ فُرْشَكُمْ أَحَدًا تَكَرَّهُوهُنَّ، فَإِنْ فَعَلْنَ ذَلِكَ فَاضْرِبُوهُنَّ ضَرْبًا غَيْرَ مُبْرِحٍ، وَلَهُنَّ عَلَيْكُمْ رِزْقُهُنَّ وَكِسْوَتُهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ»

¹At - Tabari 8:302.

²At - Tabari 8:302 – 304.

³Abu Dawud 2:606, An-Nasa'I katika Al-Kubra 5:375, Ibn Majah 1:593, Ahmad 5:3.

⁴Waislamu wanaitakidi kuwa Mtume ﷺ ndio kigezo bora na cha pekee katika maisha ya ndoa. Hakuna katika seerah rikodi ya aina yoyote ile hata dhaifi kuwa aliwapiga wakeze, watoto au wajukuu wake. Vizuri aya hii isomwe kwa mazingatio na tadaburi ya hai juu kwa kuangalia aya zinazofuatia, na mafundisho ya Mtume ﷺ yanayohusu maadli bora ya kishi na wenza wa maisha.

*"Mcheni Allah katika wanawake, kwani wao ni wasaidizi wenu. Haki yenu juu yao ni kutomkaribisha nyumbani msiyemtaka. Watakapo fanya hivyo, wapigeni pigo lisiloumiza. Na haki yao juu yenu, ni riziki yao na mavazi yao kwa wema."*¹

Ibn Abbas na wengine رضي الله عنهم walisema kuwa Ayah hii inahusu kupiga kusikoumiza.² Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema kuwa ina maana, kipigo chepesi kisicho athiri.³

Mwanamke Mtiifu kwa Mume Hapaswi Kubughudhiwa:

Allah تعالى Amesema,

فَإِنْ أَطَعْتَكُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِمْ سَبِيلًا

"...Wakikutiini msiwatafutie njia ya kuwaudhi bure." Maana yake: Mke anapomtii mume kama Alivyoamrisha na Allah تعالى, haimpasi mume kumuudhi mke. Kwa hiyo katika hali hii, mume hana haki ya kumpiga au kuhama kitanda cha mke. Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا كَبِيرًا ﴿٣٥﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Aliye Juu na Mkuu."

Hili ni karipio kwa wanaume pindi watakapochupa mipaka dhidi ya wake zao bila uhalali, basi Allah تعالى, Aliye juu ya kila kitu, Mkuu zaidi, na Mlinzi wao Atawalipizia wale wanaowatendea vibaya wake zao na kuwadhulumu,

وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْتَغُوا حَكْمًا مِّنْ أَهْلِهِ وَحَكْمًا مِّنْ أَهْلِهَا إِنْ يُرِيدَا إِصْلَاحًا

يُوفِّقِ اللَّهُ بَيْنَهُمَا إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا كَبِيرًا ﴿٣٥﴾

***"Na mkichelea kutakuwapo mfarakano baina ya mke na mume basi pelekeni muamuzi kutokana na jamaa za mume, na muamuzi kutokana na jamaa za mke. Wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu Atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye Habari."* (4:35)**

¹ Muslim 8:886.

² At - Tabari 8:314.

³ At - Tabari 8:316.

Kuteuliwa Wasuluhishi Wawili Inapokhofiwa Mfarakano baina ya Mume na Mke.

Mwanzo Allah تعالی Ametaja uasi wa mke. Kisha Ametaja hali ya pili nayo ni mambo yenye kupelekea hali ya kutengana kati ya wenza wawili. Allah تعالی Amesema,

وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْتَغُوا حَكْمًا مِّنْ أَهْلَيْهِ وَحَكْمًا مِّنْ أَهْلِهَا

“Na mkichelea kutakuwapo mfarakano baina ya mke na mume basi pelekeni muamuzi kutokana na jamaa za mume.”

Mafaqih (wanazuoni wa Fiqh) wanasema kunapotokea dalili za kufarakana kati ya mume na mke, hakimu humpa kadhia hiyo mtu muadilifu ili asuluhishe mgogoro huo ili kuzuia aliye dhalimu kati yao kutenda dhulma na kutokea madhara. Endapo tatizo litaendelea au kuzidi uhasama wao, kadhi atapeleka watu waadilifu mmoja kutoka familia ya mke na mwingine kutoka familia ya mume ili wakae nao na kulisikiliza shauri kisha waamue lililo bora kwao, kama ni kuendelea kuwa pamoja au kufarakana. Allah تعالی Anatoa kipaumbele kwa kuendelea kuishi pamoja na kwa ajili hiyo Amesema,

إِنْ يُرِيدَا إِصْلَاحًا يُوَفِّقِ اللَّهُ بَيْنَهُمَا

“Wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu Atawawezesha.”

Ali bin Abi Talhan alimnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, Allah تعالی Amemuamuru mtu muadilifu kutoka familia ya mume na mtu muadilifu kutoka familia ya mke wateuliwe waone ni nani kati yao ni mkosa. Pindipo mume ndiye aliyekosea atazuiliwa kuwa na mkewe na atapigwa faini. Iwapo mke ndiye mwenye makosa atabaki kwa mume na hatolipa faini. Endapo wasuluhishi wataamua ndoa iendelee au ivunjike, basi uamuzi wao utafuatwa. Watakapoamua ndoa iendelee na mmoja akakubali na mwingine akakataa, na mmoja wao akafariki dunia, basi aliyekubali atamrithi yule mwingine, ambapo mwenza aliyekataa hatomrithi yule aliye kubali.” Hadithi hii ameipokea Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.¹

Shaykh Abu Umar bin Abdul - Barr alisema, “Wanazuoni wameafikiana kwamba wasuluhishi wawili wasipokubaliana, basi haitokubaliwa kauli ya mwingine.

¹ At - Tabari 8:325.

Aidha wamekubaliana kuwa uamuzi wa wasuluhishi utiwe, hata kama mume na mke hawakuwateua kuwa mawakala. Hapa ni wakati mtakapoamua kuishi pamoja, lakini hawakubaliani ima kutii maamuzi au kuyakataa watakapoamua kuachana." Kisha anataja kuwa wengi wanashikilia rai kuwa uamuzi lazima ufuatwe, hata kama hawakumteua kufanya maamuzi.

• **وَأَعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا ۗ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ
وَالْمَسْكِينِ وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا
مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَن كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿٣٦﴾**

***"Muabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni wema wazazi wawili na jamaa na mayatima na masikini na jirani wa karibu na jirani wa mbali, na rafiki wa ubavuni na mpita njia, na walio milikiwa na mikono yenu ya kulia. Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wenye kiburi wanaojifakharisha."* (4:36)**

Amri ya Kumcha Allah تعالیٰ Pekee na Kuwatii Wazazi, Jamaa na Wengine:

Allah تعالیٰ Aameamuru kuabudiwa Yeye Pekee bila mshirika, kwa sababu Yeye Pekee Ndiye Muumbaji na Mlishaji Ambaye Huwateremshia neema na ukarimu waja wake katika hali zote ziwazo. Hivyo Anastahili Kupwekeshwa, bila kumshirikisha na chochote au yeyote miongoni mwa viumbe Wake katika ibada. Kama vile, Mtume ﷺ alivyomueleza Muadh رضي الله عنه

«أَتَدْرِي مَا حَقُّ اللَّهِ عَلَى الْعِبَادِ؟»

"Je Unajua haki za Allah kwa waja Wake?"

Muadh رضي الله عنه alijibu. "Allah تعالیٰ na Mjumbe wake ﷺ wanajua zaidi." Akasema,

«أَنْ يَعْبُدُوهُ وَلَا يُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا»

"Ni kumuabudu Yeye na wala wasimshirikishe na chochote." Kisha Mtume ﷺ alisema,

«أَتَدْرِي مَا حَقُّ الْعِبَادِ عَلَى اللَّهِ إِذَا فَعَلُوا ذَلِكَ؟ أَنْ لَا يُعَذِّبَهُمْ»

*"Je, unajua haki za waja kwa Allah, na wakizitekeleza Hatowaadhibu?"*¹

¹ Fat 'hul Al-Bari 13:359.

Kisha Allah تعالى Akawaamuru waja Wake kuwa watiifu kwa wazazi wao, kwani Allah تعالى Aliwafanya wazazi kuwa sababu ya waja kuumbwa, ambapo kabla ya hapo hawakuwepo. Allah تعالى Anaiunganisha amri ya kumuabudu Yeye na kuwatii wazazi katika sehemu nyingi. Kwa mfano, amesema,

أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلَوْلَا دَيْكَ

“..Nishukuru Mimi na wazazi wako...” (31:14) na

﴿ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَيَالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا

“Na Mola wako Mlezi Aameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema...” (17:23)

Allah تعالى baada ya kufaradhisha utu kwa wazazi wawili, Alifaradhisha kuwatendee wema jamaa, wanaume na wanawake. Hadithi inaelezea,

«الصَّدَقَةُ عَلَى الْمَسْكِينِ صَدَقَةٌ، وَعَلَى ذِي الرَّحْمِ صَدَقَةٌ وَصَلَةٌ»

“Sadaka aliyopewa masikini ni sadaka, na sadaka waliyopewa jamaa ni sadaqa yenye kuuunga na kuudumisha udugu (swilah).”¹

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَالْيَتَامَىٰ

“...na mayatima.”

Kwa sababu wamepoteza walezi ambao wangewatunza. Hivyo Allah تعالى Anaamrisha mayatima watendewe wema na wahurumiwe. Kisha Allah تعالى Akasema,

وَالْمَسْكِينِ

“Na masikini...”

Ambao wana mahitajio mbalimbali na hawana njia yeyote ya kujikimu. Kwa hiyo, Allah تعالى Anaamrisha wasaidiwe katika kupata mahitaji yao, katika hali ya kutosheleza, ambayo itamaliza kupungukiwa kwao. Tutafafanua zaidi ufukara na umasikini katika *Surah Baraatu* (9:60).

¹ Tuhfat Al-Ahwadhi 3:324.

Haki za Jirani:

Allah تعالى Amesema,

وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ

“Na jirani wa karibu na jirani wa mbali.”

Ali bin Abi Talhan alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ

“Na jirani wa karibu.” Maana yake: “Jirani ambaye pia ni ndugu,”¹ ambapo

وَالْجَارِ الْجُنُبِ

“Na jirani wa mbali.” Muradi wake, “ambaye hakuna baina yako na yeye ujamaa.”² Aidha imepokewa na Ikrimah, Mujahid, Maymum bin Mahran, Adh-Dhahaak, Zayd bin Aslam, Muqatil bin Hayyan na Qatadah walisema vivyo hivyo.³ Imepokewa kuwa Mujahid alisemea Kauli ya Allah تعالى,

وَالْجَارِ الْجُنُبِ

“Na jirani wa mbali.” Maana yake: “Swahiba katika safari.”⁴ Kuna Hadithi nyingi zinazoamrisha kuwatendea wema majirani, na tutazitaja baadhi yake hapa kwa msaada wa Allah تعالى.

Hadithi ya Kwanza

Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Abdullah bin Umar رضي الله عنه kuwa alisema Mtume ﷺ alisema,

«مَا زَالَ جِبْرِيلُ يُوصِينِي بِالْجَارِ حَتَّىٰ ظَنَنْتُ أَنَّهُ سَيَرُدُّنِي»

“Hakuacha Jibril kuniusia haki za jirani, mpaka nikadhania kuwa angemrithisha.”⁵ Sahihi Mbili zimeandika Hadithi hii.⁶

¹At - Tabari 8:335.

²At - Tabari 8:338.

³At - Tabari 8:335 – 336.

⁴At - Tabari 8:341.

⁵Ahmad 2:85.

⁶Fat'hul Al-Bari 10:455, Muslim 4:2025.

Hadithi ya Pili Sawa na ya Kwanza

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa Abdallah bin Amri bin Al-As رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا زَالَ جِبْرِيلُ يُوصِينِي بِالْجَارِ حَتَّى طَلَّتُ أَنَّهُ سَيُورُنِي»

"Hakuacha Jibril kuniusia haki za jirani, mpaka nikadhania kuwa angemrithisha".⁶

Abu Dawud na At-Tirmidhi waliandika Hadithi hii, ambayo At-Tirmidhi alisema kuwa ni 'Hasan Gharib' katika Isnad yake.⁷

Hadithi ya Tatu.

Imam Ahmad alinukuu kutoka kwa Abdallah bin Amri bin Al-Asi رضى الله عنه aliyesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«خَيْرُ الْأَصْحَابِ عِنْدَ اللَّهِ خَيْرُهُمْ لِصَاحِبِهِ، وَخَيْرُ الْجِيرَانِ عِنْدَ اللَّهِ خَيْرُهُمْ لِجَارِهِ»

"Wabora wa Marafiki mbele ya Allah ni mbora wao kwa mwenzie, na mbora wa majirani mbele ya Allah ni mbora wao kwa jirani yake."¹ At-Tirmidhi aliiandika Hadithi hii na kuitaja kuwa ni "Hasan Gharib."²

Hadithi ya Nne:

Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Al-Miqdad bin Al-Aswad رضى الله عنه aliyesema kuwa Mtume ﷺ aliwauliza Masahaba zake,

«مَا تَقُولُونَ فِي الزُّنَا؟»

"Mnasema nini kuhusu zina?"

Wakajibu, "Imeharamishwa, kwani Allah تعالى na Mjumbe Wake ﷺ wameiharamisha. Hivyo imeharamishwa mpaka siku ya Kiyama." Mtume ﷺ akasema:

¹ Ahmad 2:167.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 6:75.

«لَأَنْ يَزْنِيَ الرَّجُلُ بِعَشْرِ نِسْوَةٍ، أَيْسُرُ عَلَيْهِ مِنْ أَنْ يَزْنِيَ بِامْرَأَةِ جَارِهِ»

"Kuzini na mke wa jirani ni vibaya zaidi kuliko kuzini na wanawake kumi."

Kisha akawauliza,

«مَا تَقُولُونَ فِي السَّرِقَةِ؟»

"Mnasema nini kuhusu kuiba?"

Wakajibu, "Imeharamishwa, kwa kuwa Allah تعالی na Mjumbe Wake ﷺ wameiharamisha." Akasema,

«لَأَنْ يَسْرِقَ الرَّجُلُ مِنْ عَشْرَةِ آيَاتٍ، أَيْسُرُ عَلَيْهِ مِنْ أَنْ يَسْرِقَ مِنْ جَارِهِ»

"Endapo mtu atamuibia jirani, ni kosa kubwa kuliko kuiba katika nyumba kumi."¹ Hadithi imeandikwa na Ahmad peke yake.

Hadithi inayofanana na hiyo imeandikwa katika sahihi Mbili kutoka katika hadithi ya Ibn Mas'ud رضي الله عنهما aliyesema, "Nilimuuliza, "Ewe Mjumbe wa Allah! Ni Ipi Dhambi kubwa?" Alijibu,

«أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ يَدًا وَهُوَ خَلَقَكَ»

"Kumfanya Allah عزوجل kuwa na mshirika ambapo Yeye Pekee Ndiye Aliyekuumba."

Nikauliza, 'kisha?' Akasema,

«أَنْ تَقْتُلَ وَلَدَكَ خَشِيَةً أَنْ يَطْعَمَ مَعَكَ»

"Kumuua mwanao kwa kuchelea kula pamoja nawe."

Nikauliza, 'Kisha?' Akajibu,

«أَنْ تُزَانِيَ حَلِيلَةَ جَارِكَ»

"Kuzini na mke wa jirani yako."²

¹ Ahmad 6:8.

² Fat'hul Al-Bari 8:350, Muslim 1:90.

Hadithi ya Tano:

Imam Ahmad alinukuu kuwa Aisha رضي الله عنها alimuuliza Mtume ﷺ, "Nina majirani wawili, ni yupi mmoja wao nimpe zawadi?" Akajibu,

«إِلَى أَقْرَبِيهِمَا مِنْكَ يَا أَبَا»

"Jirani ambaye mlango wake uko karibu nawe."

Hadithi hii ilisimuliwa na Bukhari.¹ Mada hii tutaiielezea kwa urefu katika Tafsiri ya Surah Barah, Allah تعالى Akituwezesha.

Amri ya Kuwatendea Wema Watumwa na Watumishi:

Allah تعالى Amesema,

وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ

"Na waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia."

Hii ni amri ya kuwahurumia kwa sababu ya udhaifu wao na kutokuwa watumwa huru. Hadithi sahihi inasema kuwa wakati Mtume ﷺ akijiuguza kabla ya kutawafu, aliendelea kuunasihi Ummah.

«الصَّلَاةَ الصَّلَاةَ، وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ»

*"Hifadhini Sala, hifadhini Sala, na wanaomilikiwa na mikono yenu."*²

Aliyarejea maneno haya mpaka ulimi ukakoma kutikisika.

Imam Ahmad alipokea kutoka kwa Al-Miqdam bin Madyakarib رضي الله عنه akisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَا أَطْعَمْتَ نَفْسَكَ فَهُوَ لَكَ صَدَقَةٌ، وَمَا أَطْعَمْتَ وَلَدَكَ فَهُوَ لَكَ صَدَقَةٌ، وَمَا

أَطْعَمْتَ زَوْجَتَكَ فَهُوَ لَكَ صَدَقَةٌ، وَمَا أَطْعَمْتَ خَادِمَكَ فَهُوَ لَكَ صَدَقَةٌ»

*"Unachojilisha ni Sadaka kwako, unachowalisha wanao ni Sadaka kwako, unachomlisha mkeo ni Sadaka kwako na unachomlisha mtumishi wako ni Sadaqa kwako."*³

¹ Ahmad 6:175; Bukhari 6020.

² An - Nasai katika Al-Kubra 4:258.

³ Ahmad 4:131.

An-Nasai¹ aliandika Hadithi hii yenye Isnadi yenye uhakika, Shukrani zote zinamstahiki Allah تعالى.

Abdullah bin Amr رضي الله عنه alimuambia mlezi wake, "Umewapa watumwa chakula?" Akajibu, "Hapana". Ibn Amr رضي الله عنه akamuambia, 'Nenda ukawape kwani Mtume ﷺ amesema,

«كَفَى بِالْمَرْءِ إِثْمًا أَنْ يَخْسِرَ عَمَّنْ يَمْلِكُ قُوتَهُمْ»

"Inamtosha mtu kuwa na dhambi, kwa kutompa chakula anayemtegemea chakula chake." Ameipokea Muslim,² na Isnadi yake ni sahihi, Alhamdulillah.

Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لِلْمَمْلُوكِ طَعَامُهُ وَكِسْوَتُهُ، وَلَا يُكَلَّفُ مِنَ الْعَمَلِ إِلَّا مَا يُطِيقُ»

"Haki ya mtumwa ni chakula chake na kuvishwa kwake, na asikalifishwe kazi asiyooweza." Muslim pia ameirekodi Hadithi hii.³

Abu Hurayrah رضي الله عنه alisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِذَا أَتَى أَحَدَكُمْ خَادِمُهُ بِطَعَامِهِ، فَإِنْ لَمْ يُجْلِسْهُ مَعَهُ فَلْيَتَوَلَّهْ لُقْمَةً أَوْ لُقْمَتَيْنِ - أَوْ أُكْلَةً أَوْ أُكْلَتَيْنِ - فَإِنَّهُ وَلِيُّ حَرِّهِ وَعِلَاجِهِ»

*"Mtumishi anapomletea mmoja wenu chakula, kama hatoweza kukaa kula naye, basi ampe tonge moja au mawili au ampe mlo mmoja au miwili kwani yeye ndiye aliyekipika."*⁴

Maneno haya ni kwa mujibu wa mapokezi ya Bukhari.

Allah تعالى Hawapendi Wanaotakabari. Allah تعالى Amesema,

إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿٦٠﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wenye kiburi wanaojifakhiri."

¹ An-Nasai katika Al-Kubra 5:376.

² Muslim 2:692.

³ Muslim 3:1284.

⁴ Fat'hul Al-Bari 5:214, Muslim 3:1284.

Maana yake: Mtu anayejiona na kujifakharisha kwa wengine. Anadhani yeye ni bora kuliko wengine, hivyo kujiona juu yao, japo si lolote kwa Allah تعالى, na anachukiwa na wengine. Mujahid alitaja Kauli ya Allah تعالى.

﴿ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Hawapendi wenye kiburi wanaojifakhiri.”

Maana yake mjuba, ambapo,

﴿ فَخُورًا ﴾

“...**wanaojifakhiri.**” Maana yake: Anajivunia alichonacho badala ya kumshukuru Allah تعالى.¹ Aya hii inadhihirisha kuwa mtu kama huyo anawaringia watu kwa neema alizopewa na Allah تعالى, lakini kwa uhakika hamshukuru Allah تعالى kwa neema hiyo. Ibn Jarir aliandika; Abdullah bin Waqid Abu Raja Al-Hawawi alisema, “Utaona wenye maisha ya wastani pia wanajivuna na kujifakharisha.” Kisha akasoma,

﴿ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ ﴾

“Na waliomilikiwa na mikono yenu ya kulia.”

Utamuona asiye wajali wazazi wake, pia ni mjuvi na aliyepokwa. Kisha akasoma,

﴿ وَرَبًّا بَوْلَدِي وَلَمْ يَجْعَلْنِي جَبَّارًا شَفِيًّا ﴾

“Na nimtendee wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, mwovu.” (19:32).

Wakati mtu mmoja alimuambia Mtume ﷺ, “Ewe Mtume ﷺ niusie, Mtume ﷺ akasema,

﴿ إِيَّاكَ وَإِسْبَالَ الْإِزَارِ، فَإِنَّ إِسْبَالَ الْإِزَارِ مِنَ الْمَخِيلَةِ، وَإِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْمَخِيلَةَ، ﴾

“Jiepushe kurefusha kanzu (chini ya tindi ya mguu) kwani hii ni tabia ya ujuvi. Hapana shaka Allah Hapendi ujuvi.”²

* * *

¹ At - Tabari 8:350.

² Ahmad 5:64.

الَّذِينَ يَبْخُلُونَ وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ وَيَكْتُمُونَ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُهِينًا ﴿٣٧﴾ وَالَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ رِثَاءَ النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ وَمَنْ يَكُنِ الشَّيْطَانُ لَهُ قَرِينًا فَسَاءَ قَرِينًا ﴿٣٨﴾ وَمَاذَا عَلَيْهِمْ لَوْ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقَهُمُ اللَّهُ وَكَانَ اللَّهُ بِهِمْ عَلِيمًا ﴿٣٩﴾ إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۗ وَإِنْ تَكَ حَسَنَةً يُضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾ فَكَيْفَ إِذَا جِئْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ بِشَهِيدٍ وَجِئْنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ شَهِيدًا ﴿٤١﴾ يَوْمَئِذٍ يُودُّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَعَصُوا أَرْسُولَ لَوْ تَسَوَّىٰ بِهِمُ الْأَرْضُ وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٢﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرُبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغْتَسِلُوا ۗ وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِنْكُمْ مِنَ الْغَايِبِ أَوْ لَمْ تَمْسُتُمْ أَلَيْسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِرُءُوسِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُورًا ﴿٤٣﴾

الَّذِينَ يَبْخُلُونَ وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ وَيَكْتُمُونَ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ ۗ وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُهِينًا ﴿٣٧﴾ وَالَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ رِثَاءَ النَّاسِ وَلَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ وَمَنْ يَكُنِ الشَّيْطَانُ لَهُ قَرِينًا فَسَاءَ قَرِينًا ﴿٣٨﴾ وَمَاذَا عَلَيْهِمْ لَوْ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقَهُمُ اللَّهُ وَكَانَ اللَّهُ بِهِمْ عَلِيمًا ﴿٣٩﴾

37. Ambao wanafanya ubakhili na wanaamrisha watu ubakhili, na wanaficha Fadhila Alizowapa Mwenyezi Mungu. Na Tumewandalia makafiri adhabu ya fedheha.

38. Na ambao hutoa mali yao kwa kuonesha watu, wala hawamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho; na yule ambaye Shetani amekuwa ndiye rafiki yake, basi ana rafiki mbaya mno.

39. Na ingeliwadhuru nini wao lau wangelimuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wakatoa katika Aliyowaruzuku Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwajua vyema.

Karipio kwa Tabia ya Ubahili:

Allah تعالى Anawakemea watu wenye tabia ya ubahili ambao hawataki kutumia fedha (mali) zao kama Allah تعالى Alivyowaamrisha, kama vile kuwatendea wema wazazi na kuwahudumia jamaa, mayatima, maskini, jamaa ambaye pia ni jirani, msafiri mwenza, msafiri aliyeharibikiwa, watumwa na watumishi.

Mtume ﷺ alisema,

«وَأَيُّ ذَاءٍ أَدْرَأُ مِنَ الْبُخْلِ»

"Kuna maradhi gani yaliyo mabaya kuliko ubakhili?"¹

Aidha alisema:

«إِيَّاكُمْ وَالشَّحَّ، فَإِنَّهُ أَهْلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ، أَمْرُهُمْ بِالْقَطِيعَةِ فَتَقَطُّوا، وَأَمْرُهُمْ
بِالْفُجُورِ فَتَجْرُوا»

"Jihadhari na ubakhili kwani uliwaangamiza waliokuwa kabla yenu, kwani uliwaamuru kukata udugu, na wakaukata, na uliwaamuru kutenda dhambi na walifanya dhambi."²

Allah تعالى Amesema,

وَيَكْتُمُونَ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

"Na wanaficha Fadhila Alizowapa Mwenyezi Mungu."

Kwa hiyo mchoyo hashukuru neema za Allah تعالى, kwani hazioni athari zake, ima ni katika chakula chake, mavazi au avitoavyo.

Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

إِنَّ الْإِنْسَانَ لِرَبِّهِ لَكَنُودٌ ﴿٦١﴾ وَإِنَّهُمْ عَلَىٰ ذَٰلِكَ لَشٰهِدٌ ﴿٦٢﴾

"Hakika mwanaadamu ni mtovu wa fadhila kwa Mola wake Mlezi!, Na hakika yeye mwenyewe bila ya shaka ni shahidi wa hayo!"(100:6-7)

Kwa mwenendo na tabia.

¹ Al-Adab Al-Mufrad 83.

² Abu Dawud 2:324.

وَإِنَّهُ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيدٌ ﴿٣٧﴾

“Naye hakika bila ya shaka ana nguvu za kupenda mali!” (100:8)

Allah تعالی Amesema,

وَيَكْتُمُونَ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

“Na wanaficha Fadhila Alizowapa Mwenyezi Mungu.”

Na kwa sababu hii Aliwakemea,

وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُهِينًا ﴿٣٨﴾

“ Na Tumewaandalia makafiri adhabu ya fedheha.”

Ukafiri, ni kusitiri na kufunika, kwa hiyo Bakhili anaficha (anafunika) neema za Allah تعالی Alizomruzuku, na anazikana, kwani yeye ni kafiri wa neema za Allah تعالی Alizomneemesha. Na katika Hadithi Mtume ﷺ anasema,

إِنَّ اللَّهَ إِذَا أَنْعَمَ نِعْمَةً عَلَى عَبْدٍ، أَحَبَّ أَنْ يَظْهَرَ أَثَرَهَا عَلَيْهِ

“Allah تعالی Anapomneemesha mja, Hupenda Azione athari zake kwake.”

Baadhi ya *Salaf* wanaeleza kuwa ayah hii (4:37) inawazungumzia Mayahudi walioficha elimu waliyo kuwa nayo juu ya wasifu wa Muhammad ﷺ, na hapana shaka kuwa maana ya jumla inajumuisha na hili. Maneno ya dhahiri ya Ayah hii yanaonesha inaelezea unyimi wa fedha, japokuwa kufanya ubahili kwa kujua pia inayajumuisha. Ayah inazungumza, kuwakimu jamaa na wanyonge, kama Ayah baada yake isemavyo,

وَالَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ رِئَاءَ النَّاسِ

“Na ambao hutoa mali yao kwa kuonesha watu.”

Mwanzo Allah تعالی Anataja kuwa Atawaadhibu mabakhili wasiotumia mali zao, kisha Anawataja wanaotoa kwa riya ili wasifiwe kuwa ni wakarimu, sio kwa kupata radhi za Allah تعالی. Hadithi inasema kuwa watu watatu wa mwanzo kuliwa na moto ni mwanazuoni, mpiganaji na mtumiaji anayejiionesha kwa watu. Kwa mfano,

¹ At - Tabarani katika Al-Kabir 18:135.

«يَقُولُ صَاحِبُ الْمَالِ: مَا تَرَكْتُ مِنْ شَيْءٍ تُحِبُّ أَنْ يُنْفَقَ فِيهِ، إِلَّا أَنْفَقْتُ فِي سَبِيلِكَ، فَيَقُولُ اللَّهُ: كَذَبْتَ، إِنَّمَا أَرَدْتُ أَنْ يَقَالَ: جَوَادٌ، فَقَدْ قِيلَ»

"Tajiri atasema, 'Sikuacha sehemu ambayo kwayo Ulinitaka nitumie ila nilitumia katika njia Yako." Allah تعالى Atasema, "Mwongo, ulifanya hivyo ili isemwe kuwa, "Ni mtoaji. Na tayari imesemwa."

Maana yake: Ulipata malipo yako duniani, na hilo kwa hakika ndilo ulilolichuma kwa matendo yako.¹ Kwa sababu hiyo Allah تعالى Amesema,

وَلَا يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ

"Wala hawamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho;.."

Maana yake: Kwa hakika sababu iliyowafanya watende tendo lao hilo baya na kuacha utiifu kwa namna yake iliyo sahihi ni *Shaytan*. *Shaytan* aliwaghilibu kufanya vitendo viovu, badala ya kutenda amali njema kama inavyostahili kufanywa. *Shaytan* alihimiza akawahamasisha na akawaghilibu kwa kufanya maovu yaonekane kuwa mema,

وَمَنْ يَكُنِ الشَّيْطَانُ لَهُ قَرِينًا فَسَاءَ قَرِينًا ﴿٦٤﴾

"Na yule ambaye Shetani amekuwa ndiye rafiki yake, basi ana rafiki mbaya mno." Kisha Allah تعالى Amesema,

وَمَاذَا عَلَيْهِمْ لَوْ آمَنُوا بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَأَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقَهُمُ اللَّهُ

"Na ingeliwadhuru nini wao lau wangelimuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na wakatoa katika Aliyowaruzuku Mwenyezi Mungu?"

Maana yake: Watapata madhara gani kama watamuamini Allah تعالى, wakafuata njia sahihi, wakaacha riya na kuwa waadilifu, wakamtegemea Allah تعالى na wakasubiri Ahadi yake siku ya Kiyama, kwa wale watendao mema na wanatoa katika vile Alivyowaruzuku kama Apendavyo Allah تعالى na Kuridhia. Kauli ya Allah تعالى,

وَكَانَ اللَّهُ بِهِمْ عَلِيمًا ﴿٦٥﴾

"Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuwajua vyema."

¹ An-Nasai 6:24.

Muradi wake ni kuwa Anazijua dhamira zao, ima ni nzuri au mbaya. Kwa hakika Anajua wale wanaostahili taufiki, Naye Anawawafikisha, na Anawapa mwongozo. Anawaongoza kufanya amali adilifu ambazo Atazilipa. Aidha Anawajua wale wanaoshindwa na kutengwa na sehemu zake, ambayo inapelekea kushindwa hapa duniani na kesho Akhera. Tunakimbilia kwa Allah تعالى kuelekea mwisho mbaya.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۖ وَإِن تَكُ حَسَنَةً يُضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾
 فَكَيْفَ إِذَا جِئْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ بِشَهِيدٍ وَجِئْنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ شَهِيدًا ﴿٤١﴾ يَوْمَئِذٍ يُوَدُّ
 الَّذِينَ كَفَرُوا وَعَصَوُا الرَّسُولَ لَوْ تُسَوَّىٰ بِهِمُ الْأَرْضُ وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٢﴾

40. Hakika Mwenyezi Mungu Hadhulumu hata uzito wa chembe moja. Na ikiwa ni jambo jema basi Yeye Hulizidisha na Hutoa kutoka Kwake malipo makubwa.

41. Basi itakuwaje pindi Tukiwaletea kutoka kila umma shahidi, na Tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?

42. Siku hiyo waliokufuru na wakamuasi Mtume watatamani ardhi isawazishwe juu yao. Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote.

Allah تعالى Hamdhulumu Mja Wake Hata kwa Uzito wa Chembe ya Vumbi:

Allah تعالى Anaeleza kuwa Hawawadhulumu waja Wake siku ya kufufuliwa, hata kwa uzito wa punje ya khardali au chembe ya vumbi. Bali Allah تعالى Atawalipa kwa matendo yao mema na kuzidisha malipo. Kwa mfano Amesema,

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ

"Nasi Tutaweka mizani za uadilifu." (21:47)

Allah تعالى Anamuelezea Luqman kuwa alisema,

يَبْنِيٰٓ اِيۡنَهَاۙ اِنۡ تَكُ مِثۡقَالَ حَبۡبٍۭ مِّنۡ حَرۡدَلٍۭ فَتَكُنۡ فِيۡ صَخْرَةٍۭ اَوْ فِيۡ السَّمٰوٰتِ اَوْ فِيۡ الْاَرْضِ

يَأْتِ بِهَا اللّٰهُ

“Ewe mwanangu! Kikiwapo kitu cha uzito wa chembe ya khardali kikiwa ndani ya Jabali au ndani ya mbingu au ndani ya ardhi, basi Mwenyezi Mungu Atakileta.”

Allah تعالى Akasema,

يَوْمَئِذٍ يَصْدُرُ النَّاسُ أَشْتَاتًا لِيُرَوْا أَعْمَالَهُمْ ﴿٦٦﴾ فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٦٧﴾

وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٦٨﴾

“Siku hiyo watu watatoka kwa mfarakano wakaoneshwe vitendo vyao! Basi anayetenda chembe ya wema, ataona! Na anayetenda chembe ya Shari, ataona!” (99:6-8)

Sahih Mbili zimeandika Hadithi ndefu kuhusu kuombea ambako Abu Said al-Khudri رضي الله عنه amesimulia, na ambako Mtume ﷺ amesema,

«فَيَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: اِرْجِعُوا، فَمَنْ وَجَدْتُمْ فِي قَلْبِهِ مِثْقَالَ حَبَّةٍ خَرْدَلٍ مِنْ إِيمَانٍ، فَأَخْرِجُوهُ مِنَ النَّارِ»

“Allah تعالى Atasema, “Rejeeni, endapo mtamkuta mtu katika moyo wake ana iman i sawa na uzito wa chembe ya Khardali, mtoeni motoni.”

Katika mapokezi mengine, Allah تعالى Amesema,

وفي لفظ: «أَذْنَى أَذْنَى مِثْقَالَ ذَرَّةٍ مِنْ إِيمَانٍ، فَأَخْرِجُوهُ مِنَ النَّارِ، فَيُخْرِجُونَ خَلْقًا كَثِيرًا»

“Na katika tamshi lingine: Yeyote mwenye chembe ndogo, sana ya imani, mtoeni motoni. Na watawatoa watu wengi.”

Kisha Abu Saidi رضي الله عنه akasema, “Soma kama utaweza,

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ

“Hakika Mwenyezi Mungu Hadhulumu hata uzito wa chembe moja.”¹

¹ Fat'hul Al-Bari 13:413, Muslim 1:167.

Je, Washirikina Watapunguziwa Adhabu?

Said bin Jubayr alizungumzia Kauli ya Allah تعالى،

وَأَنَّ تَكُ حَسَنَةً يُضَعِفُهَا

“...Na ikiwa ni jambo jema basi Yeye hulizidisha...”

“Ama kwa kafiri atapunguziwa adhabu siku ya Ufufuo, lakini hatotolewa Motoni kamwe. Alitumia kama ushahidi Hadithi sahihi ambapo Al-Abbas رضي الله عنه alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Ami yako Abu Talib alikuwa akikulinda na kukuunga mkono, Je, umemsaidia kwa lolote?”

Mtume ﷺ alisema،

«نَعَمْ هُوَ فِي ضَخْضَاحٍ مِنْ نَارٍ، وَلَوْلَا أَنَا، لَكَانَ فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ»

“Ndiyo, yupo katika kina kifupi cha Motoni na kama siyo mimi angekuwa katika kina kirefu cha Moto (Darkil - asfal).”¹

Hata hivyo Hadithi hii inamhusu Abu Talib tu sio makafiri wengine. Ili kuunga mkono kauli hii, tutataja alichoandika Abu Dawud At - Tayalisi, katika *Musnad* kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema،

«إِنَّ اللَّهَ لَا يَطْلِمُ الْمُؤْمِنَ حَسَنَةً، يُثَابُ عَلَيْهَا الرِّزْقَ فِي الدُّنْيَا، وَيُجْزَى بِهَا فِي
الْآخِرَةِ، وَأَمَّا الْكَافِرُ فَيُطَلَمُ بِهَا فِي الدُّنْيَا، فَإِذَا كَانَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ لَمْ يَكُنْ لَهُ حَسَنَةٌ»

“Mwenyezi Mungu Hamdhulumu Muumini jema lake, hulipwa katika riziki yake duniani na hulipwa pepo Akhera. Ama kafiri, hulipwa riziki kwa mazuri atendayo, na kesho Akhera hana malipo yoyote.”²

¹ Bukhari Na.3883, 6208 na Muslim 209.

² Musnad Al-Tayalisi p47, Muslim 2808.

Malipo Makubwa Maana Yake Nini?

Abu Hurayrah, Ikrimah, Said bin Ubayr, Al-Hasan, Qatadah na Adh-Dhahak رضي الله عنهم walisema kuwa Kauli ya Allah تعالى،

وَوُتِّبَ مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٣٧﴾

“Na Hutoa Kutoka Kwake malipo makubwa.”

Inahusu Pepo, tunamuomba Allah Rehema Zake na Pepo Yake. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Abu Uthman An-Nahdi alisema, “Hapana mtu aliyefuatana na Abu Hurayrah رضي الله عنه zaidi yangu. Mwaka mmoja alinitangulia kwenda Hajj nami nilikwenda baada yake, yaani mwaka uliofuata, na nikawasikia watu wa Basra wakisema kuwa alisema alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنَّ اللَّهَ يَجْزِي بِالْحَسَنَةِ أَلْفَ أَلْفِ حَسَنَةٍ»

“Allah تعالى Huzidisha malipo ya amali njema kwa mema milioni.”

Hivyo nikasema, “Ole wako! Hapana mtu aliyefuatana na Abu Hurayrah رضي الله عنه zaidi yangu, na sijapatapo kumsikia akisimulia Hadithi hii. Nilipotaka kumkabili, nilikuta amekwisha kwenda kwa ajili ya Hajj hivyo nilimfuata kwenda kumuuliza juu ya Hadithi hii.”

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى naye aliandika Hadithi hii akitumia Isnad nyingine inayotufikisha kwa Abu Uthman. Katika mapokezi hayo, Abu Uthman alisema, “Nilimuambia, ‘Ewe Abu Hurayrah! Niliwasikia ndugu zangu wa Basra wakidai kuwa uliwasimulia kuwa ulimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنَّ اللَّهَ يَجْزِي بِالْحَسَنَةِ أَلْفَيْ أَلْفِ حَسَنَةٍ»

“Allah Hulipa amali njema kwa mema milioni.”

Abu Hurayrah رضي الله عنه akajibu, “Wallahi nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«إِنَّ اللَّهَ يَجْزِي بِالْحَسَنَةِ أَلْفَيْ أَلْفِ حَسَنَةٍ»

“Allah Hulipa jema kwa mema milioni.”

¹ Ahmad 2:215, 216.

Kisha akasoma Aya hii,

﴿٣٨﴾ فَمَا مَتَّعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ

"Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha ya Akhera ni chache.." (9:38)

Mtume wetu ﷺ Atakuwa Shahidi Dhidi ya au kwa Ajili ya Umma Wake Katika Siku ya Kiama, Wakati Ambapo Makafiri Watakapotamani Kufa.

Allah تعالى Anasema:

﴿٤١﴾ فَكَيْفَ إِذَا جِئْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ بِشَهِيدٍ وَجِئْنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ شَهِيدًا

"Basi itakuwaje pindi Tukiwaletea kutoka kila umma shahidi, na Tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?" (4:41)

Allah تعالى Anaelezea vitisho, mateso na magumu ya siku ya Kiyama, Akasema, itakuaje siku hiyo ambapo watakuwepo mashahidi kutoka kila taifa, yaani Mitume kama Allah تعالى Alivyosema:

﴿٦٩﴾ وَأَشْرَقَتِ الْأَرْضُ بِنُورِ رَبِّهَا وَوُضِعَ الْكِتَابُ وَجِئْنَا بِالنَّبِيِّينَ وَالشُّهَدَاءِ

"Na ardhi itang'ara kwa Nuru ya Mola wake Mlezi, na Kitabu kitawekwa, na wataletwa Manabii na mashahidi..." (39:69)

Bukhari alipokea kuwa Abdullah bin Masoud رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ aliniambia, 'Nisomee.' Nikamjibu, "Ewe Mjumbe wa Allah! Nikusomee Qur'an ilhali iliteremshwa kwako?" Akasema, 'Ndiyo, kwani napenda kuisikia ikisomwa na watu wengine.' Nilisoma Surat An-Nisa mpaka nilipofikia aya hii,

﴿٤١﴾ فَكَيْفَ إِذَا جِئْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ بِشَهِيدٍ وَجِئْنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ شَهِيدًا

"Basi itakuwaje pindi Tukiwaletea kutoka kila umma shahidi, na Tukakuleta wewe kuwa shahidi wa hawa?" (4:41)

Kisha akanambia, 'Sasa simama'. Niliona macho yake yakibubujika machozi." Kauli ya Allah تعالى,

يَوْمَئِذٍ يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَعَصَوُوا الرُّسُولَ لَوْ تُسَوَّىٰ بِهِمُ الْأَرْضُ وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٢﴾

“Siku hiyo waliokufuru na wakamuasi Mtume watatamani ardhi isawazishwe juu yao. Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote”. (4:42)

Maana yake: Watatamani ardhi ingelipasuka na kuwameza kwa sababu ya vitisho vya mahali pa mkutano na tahayari, idhilali na mateso watakapopata siku hiyo.

Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

يَوْمَ يَنْظُرُ الْمَرْءُ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ

“Siku ambayo mtu atakapoona yaliyotangulizwa na mikono yake.” (78:40)

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٣﴾

“Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote.”

Inaonesha kuwa watakiri kila walichokifanya na hawatoficha chochote.

Abdur - Razaq aliandika kuwa Said bin Jubayr alisema, Mtu alikuja kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما na akamuambia, ‘Kuna mambo ndani ya Qur’an yananichanganya.’ Ibn Abbas رضي الله عنهما akauliza, ‘Ni mambo gani uliyo na wasiwasi nayo ndani ya Qur’an?’ akasema, “Sio wasiwasi bali mambo yanayonichanganya!” Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema, “Niambie kilichokufanya uchanganyikiwe.’ Nikasema, ‘Nimesikia Kauli ya Allah تعالى,

ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فِتْنَتَهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا وَاللَّهِ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿٦٣﴾

“Kisha hautakuwa udhuru wao ila ni kusema: Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.” (6:23)

Lakini pia Amesema,

وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٢﴾

“Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote.” (4:42)

Kwa hakika walificha kitu. Ibn Abbas رضي الله عنهما akasema, ‘Ama Kauli ya Allah تعالى,

ثُمَّ لَمْ تَكُنْ فِتْنَتَهُمْ إِلَّا أَنْ قَالُوا وَاللَّهِ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿٢٣﴾

“Kisha hautakuwa udhuru wao ila ni kusema: Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.” (6:23)

Watakapotanabahi ya kwamba Allah تعالى Hasamehe siku ya Kiyama dhambi, isipokuwa kwa Waislamu, na kuwa Anasamehe dhambi hata zikiwa kubwa namna gani isipokuwa shirk, basi Mushirikina wataongopa watasema,

وَاللَّهُ رَبِّنَا مَا كُنَّا مُشْرِكِينَ ﴿٢٣﴾

“Wallahi! Mola wetu Mlezi! Hatukuwa washirikina.” (6:23)

Wakitaraji kuwa Allah تعالى Atawasamehe. Hata hivyo Allah تعالى Ataitia lakiri midomo yao, na mikono na miguu yao itafichua yote waliyokuwa wakiyafanya. Kisha,

يَوْمَئِذٍ يُودُّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَعَصُوا الرَّسُولَ لَوْ تُسَوَّىٰ بِهِمُ الْأَرْضُ وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٢﴾

“Siku hiyo waliokufuru na wakamuasi Mtume watatamani ardhi isawazishwe juu yao. Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote.” (4:42)¹

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرُبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا

عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغْتَسِلُوا^٢ وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ

أَوْ لَمَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوْهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ^٣

إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُورًا غَفُورًا ﴿٤٢﴾

¹ Abdur – Razzaq 1:160.

“Enyi mlio amini! Msikaribie Swala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayoyasema, wala hali mna janaba - isipo kuwa mmo safarini - mpaka mkoge. Na mkiwa wagonjwa, au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni, au mmewagusa wanawake. Na msipate maji, basi ukusudieni mchanga safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye Kughufiria.” (4:43).

Kuharamisha Kusogelea Sala Mtu Anapokuwa Amelewa au Ana Janabah

Allah تعالى Aliwakataza waja Wake waumini kusali wakati wamelewa, kwani wakiwa katika hali hiyo hawaelewi wakisemacho, na Akawakataza kwenda Masjid wakati wakiwa na janaba isipokuwa mtu anapopita Masjid kuingilia mlango mmoja na kutokea wa pili. Ayah hii ilishushwa kabla ya pombe kuharamishwa moja kwa moja, kama ilivyothibitishwa na Hadithi tuliyoitaja katika *Surat Al-Baqarah* tulipoelezea Kauli ya Allah تعالى,

﴿ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْخَمْرِ وَالْمَيْسِرِ ﴾

“Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari.” (2:219)

Katika Hadithi, Mtume ﷺ alimsomea Umar رضي الله عنه Ayah hii ambaye alisema, “Ewe Allah! Tueleze juu ya hukumu ya pombe kwa uwazi.” Ayah hii iliposhushwa (4:43). Mtume ﷺ alimsomea Umar رضي الله عنه, akaendelea kusema, “Ewe Allah! Tueleze hukumu ya *Khamr* (vileo) wazi wazi.” Baada ya hapo hawakunywa pombe karibu na wakati wa Sala. Baada ya Kauli hii ya Allah تعالى kuteremka,

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِنَّمَا الْخَمْرُ وَالْمَيْسِرُ وَالْأَنْصَابُ وَالْأَزْلَامُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ الشَّيْطَانِ

﴿ فَاجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴾

“Enyi mlio amini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufanikiwa.” (5:90) mpaka

فَهَلْ أَنْتُمْ مُنْتَهُونَ ﴿٣٧﴾

“Basi je, mmeacha? (5:91)¹

Umar رضي الله عنه akasema, “Tumewacha! Tumewacha!” Katika mapokezi mengine, wakati Ayah ndani ya *Surat An-Nisa* ilipotremshwa,

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرُبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ

“Enyi mlio amini! Msikaribie Swala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayoyasema.”

Wakati wa Sala, Mtume ﷺ alimtuma mtu anadi; “Mlevi yeyote haruhusiwi kuikaribia Sala.” Hivi kama ilivyokusanywa na Abu Dawud.²

Sababu za Kuteremshwa Kwake.

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alirekodi baadhi ya taarifa kuhusu tukio la kuteremshwa kwake; Sa'd رضي الله عنه alisema, “Ayat Nne ziliteremshwa kunihusu mimi. Mtu wa Ansar alitayarisha chakula na akawaita baadhi ya Muhajirin na Ansar, na tulikula na kunywa mpaka tukalewa. Kisha tukajisifia kwa vyeo vyetu. Kisha mtu mmoja alishika mfupa wa ngamia na kuijeruhi pua ya Sa'd رضي الله عنه na tendo hilo lilimkhofisha. Haya yalijiri kabla ya kuharamishwa *Khamr*, na baadaye Allah تعالى Aliteremsha,

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرُبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ

“Enyi mlio amini! Msikaribie Swala, hali mmelewa.”

Muslim aliiandika Hadithi hii,³ na wokusanyaji wa *Sunan* waliandika, isipokuwa Ibn Majah.⁴

¹ Ahmad 1:53.

² Abu Dawud 4:80.

³ Musnad At-Tayalisi: 28; Muslim 4:1878.

⁴ Abu Dawud 1773; Tuhfat Al-Ahwadhi 8:466, An-Nisai katika Al-Kubra 6:348.

Sababu Nyengine

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alisimulia kuwa Ali bin Talib رضي الله عنه alisema, "Abdur-Rahman bin Awf aliandaa chakula na alitualika kula pamoja na kunywa mvinyo. Tulipolewa na wakati wa Sala ukaingia walimuomba mmoja wetu awe Imam. Alisoma Sema, 'Enyi makafiri! Siabudu mnacho kiabudu, lakini tunaabudu mnachoabudu (rejea maneno sahihi katika Surah 109)." Allah تعالى Akateremsha.

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَقْرُبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ سُكَرَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ

"Enyi mlio amini! Msikaribie Swala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayoyasema."

Hadithi hii ilikusanywa na Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى na At-Tirmidhi رحمه الله تعالى ambayo waliipa daraja la "*Hasan sahih*."² Kauli ya Allah تعالى,

حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ

"Mpaka myajue mnayoyasema."

Huo ndio wasifu wa mlevi yaani anapokuwa hajui anayoyasema. Mtu anapolewa hufanya makosa katika kusoma na hatoweza kuwa na utulivu ndani ya Sala. Imam Ahmad رحمه الله تعالى aliandika kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

إِذَا نَعَسَ أَحَدُكُمْ وَهُوَ يُصَلِّي، فَلْيَنْصِرْ فَلَيْتِمَ، حَتَّىٰ يَعْلَمَ مَا يَقُولُ

"Mmoja wenu akisinzia na huku anasali, basi aende akalale ili aweze kutambua maana ya ayasemayo."³

Iliandikwa pia na Bukhari⁴ رحمه الله تعالى na An-Nisai⁵ katika رحمه الله تعالى mapokezi mengine ya Hadithi hii, Mtume ﷺ alisema,

¹ At – Tabari 8:378.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 8:380.

³ Ahmad 3:142.

⁴ Fat'hul Al-Bari 1:377.

⁵ An-Nisa' 1:215.

«فَلَعَلَّهُ يَذْهَبُ يَسْتَغْفِرُ فَيَسْبُ نَفْسُهُ»

“Pengine mtu alikusudia kuomba maghfira, lakini badala yake anajilaani.”¹

Allah تعالی Amesema,

وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّى تَغْتَسِلُوا

“Wala hali mna janaba - isipo kuwa mmo safarini - mpaka mkoge.”

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی alirekodi kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Kauli ya Allah تعالی,

وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّى تَغْتَسِلُوا

“Wala hali mna janaba - isipo kuwa mmo safarini - mpaka mkoge.”

Muradi wake ni kuwa, “Usiingie Masjid ukiwa na Janaba ila kama unapita tu, yaani unapita bila kukaa.”²

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی alisema alipokea pia kutoka kwa, Abdullah bin Mas’ud, Anas, Abu Ubaydah, Said bin Al-Musayyib, Abu Adh-duha, Ata, Mujahid, Masruq, Ibrahim An-Nakhai, Zayd bin Aslam, Abu Malik, Amr bin Dinar, Al-Hakam bi Utaybah, Ikrimah, Al-Hasan Al-Basri, Yahya bin Said Al-Ansari, Ibn Shibab na Qatadah رضي الله عنهم.³ Ibn Jarir رحمه الله تعالی alirekodi kuwa Yazid bin Abi Habib alitolea maelezo Kauli ya Allah تعالی,

وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ

“Wala hali mna janaba - isipo kuwa mmo safarini.”

Pindi baadhi ya Ansar ambao milango yao ilifungukia upande wa Masjid, walipokuwa na janaba na hawakuwa na maji na njia pekee ya kupata maji ilikuwa kupitia Masjid. Hivyo Allah تعالی Akateremsha,

¹ Fat’hul Al-Bari 1:375.

² At - Tabari 8:382.

³ At - Tabari 8:381-384.

وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ

“Wala hali mna janaba - isipo kuwa mmo safarini”¹

Kauli ya Yazid bin Abi Habib ni ripoti ya Bukhari iliyo ndani ya Sahihi yake kuwa Mtume ﷺ alisema,

«سُدُّوا كُلَّ خَوْخَةٍ فِي الْمَسْجِدِ إِلَّا خَوْخَةَ أَبِي بَكْرٍ»

“Fungeni milango yote inayoelekea msikitini, isipokuwa mlango wa Abubakar.”²

Hili ndilo aliloamrisha Mtume ﷺ kabla ya kufariki, akijua kuwa Abubakar رضي الله عنه atakuwa Khalifah baada yake, kuwa atahitaji kuingia Masjid mara kadha kushughulikia masuala ya Waislamu. Hata hivyo, Mtume ﷺ aliamrisha milango yote inayoingia Masjid ifungwe ila mlango wa Abubakar رضي الله عنه. Baadhi ya Watu wa *Sunan* waliandika kuwa Mtume ﷺ alisema mlango wa Ali رضي الله عنه uachwe wazi, lakini hili ni kosa, kilichomo ndani ya Sahihi ndicho sawa.

Katika Sahih ya Muslim aliandika kuwa Aisha رضي الله عنها alisema, “Mtume ﷺ aliniambia,

«نَأْوِلِي الْخُمْرَةَ مِنَ الْمَسْجِدِ»

“Niletee nguo kutoka Masjid.”

Nikamjibu, “Niko katika siku zangu.” Akaniambia,

«إِنَّ حَيْضَتِكَ لَيْسَتْ فِي يَدِكَ»

“Hedhi yako haiko mkononi mwako.”³

Muslim alipokea sawa na hiyo kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه.⁴ Hadithi hii inadhihirisha kuwa mwanamke anaruhusiwa kupita Masjid wakati akiwa na hedhi au nifasi, na Allah تعالى ni Mjuzi wa yote.

¹ At - Tabari 8:384. Isnadi sio Sahihi.

² *Fat'hul Al-Bari* 1:665.

³ Muslim 1:245.

⁴ Muslim 1:245.

Maelezo ya Tayamamu

Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَىٰ أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ أَوْ لَمَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ يَجِدُوا
مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا

“Na mkiwa wagonjwa, au mmo safarini, au mmoja wenu ametoka chooni, au mmewagusa wanawake - Na msipate maji, basi ukusudieni mchanga Safi.”

Ama kuhusu aina ya maradhi ambayo inaruhusiwa *Tayammum*, ni maradhi yanayohofiwa kuzidi kwa kutumia maji, ambayo yanaweza kudhuru sehemu ya mwili au kwa kufanya hivyo maradhi yataendelea. Baadhi ya wanazuoni wanasema kila aina ya maradhi inaruhusiwa *Tayammum* kwa kuwa Allah تعالى Amezungumzia kwa jumla. Ama kwa msafiri inafahamika, bila kujali masafa.

Kisha Allah تعالى Akasema,

أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنْكُمْ مِنَ الْغَائِطِ

“Au mmoja wenu ametoka chooni.”

Ghait kilugha maana yake ardhi tambarare, na sehemu hii ya Aya inakusudia najisi ndogo. Kisha Allah تعالى Amesema,

أَوْ لَمَسْتُمُ النِّسَاءَ

“Au mmewagusa wanawake.”

Ambayo ilisomwa *Lamastum* na *Laamastum*, ambayo ina maana kujamiiana. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema katika aya nyingine,

وَإِنْ طَلَقْتُمْوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ وَقَدْ فَرَضْتُمْهُنَّ فَرِيضَةً فَيَنْصِفْ مَا فَرَضْتُمْ

“Na mkiwapa talaka kabla ya kuwagusa, na mmekwisha wawekea hayo mahari makhsusi, basi wapeni nusu ya mahari mlioagana.”
(2:237) na,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا نَكَحْتُمُ الْمُؤْمِنَاتِ ثُمَّ طَلَقْتُمُوهُنَّ مِنْ قَبْلِ أَنْ تَمْسُوهُنَّ بِمَا
لَكُمْ عَلَيْهِنَّ مِنْ عِدَّةٍ تَعْتَدُونَهَا^ط

“Enyi mlio amini! Mkiwaoa wanawake, Waumini, kisha mkawapa talaka kabla ya kuwagusa, basi hamna eda juu yao mtakayo ihisabu.” (33:49)

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alizungumzia Kauli ya Allah تعالى،

أَوْ لَمَسْتُمُ النِّسَاءَ

“Au mmewagusa wanawake.” Ina maana ya jimai.¹

Iliripotiwa kuwa wafuatao wana rai sawa na hiyo, Ali, Ubayy bin Ka’b, Mujahid, Tawus, Al-Hasan, Ubayd bin Umayr, Said bin Jubayr, Ash-Sha’bi, Qatadah, na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم.² Allah تعالى Amesema,

فَلَمْ يَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا

“Na msipate maji, basi ukusudieni mchanga Safi.”

Ndani ya Sahih Mbili imeandikwa kuwa Imran bin Husayn رضي الله عنه alisema,

إن رسول الله ﷺ رأى رجلا معتزلا لم يصل في القوم فقال: «يا فلان ما منعك أن تُصلي مع القوم، أَلَسْتَ بِرَجُلٍ مُسْلِمٍ؟» قال: بلى، يا رسول الله! ولكن أصابني جنابة ولا ماء، قال: «عَلَيْكَ بِالصَّعِيدِ، فَإِنَّهُ يَكْفِيكَ»

“Mtume ﷺ alimuona mtu amejitenga na hakusali na watu. Akamuuliza, ‘Ewe fulani! Kitu gani kilichokuzuia kusali jamaa na wenzako, wewe si Muislamu?’ Akajibu, ‘kwanini?, Ewe Mjumbe wa Allah! Nina janaba na hapana maji!’ Akasema, ‘Tayammamu na mchanga safi na hiyo itakutosheleza.’”³

¹ At - Tabari 8:392.

² At - Tabari 8:392 – 393.

³ Fat’hul Al-Bari 1:545, Muslim 1:474.

Maana ya kilugha ya kiarabu ya *Tayammam* ni kukusudia jambo, kama Waarabu wasemavyo, "Allah تعالى Akusudie Ulinzi Wake kwako." Mchanga safi maana yake vumbi tu, kwa mujibu wa Kauli ya Allah تعالى (18:40). Kwa maana mchanga safi na mzuri. Katika Sahih Muslim amepokea kuwa, Hudhaifah bin Al-Yaman رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alisema,

«فُضِّلْنَا عَلَى النَّاسِ بِثَلَاثٍ: جُعِلَتْ صُفُونَا كَصُفُوفِ الْمَلَائِكَةِ، وَجُعِلَتْ لَنَا الْأَرْضُ كُلُّهَا مَسْجِدًا، وَجُعِلَتْ تُرَابُهَا لَنَا طَهُورًا، إِذَا لَمْ نَجِدِ الْمَاءَ»

*"Tumefadhilishiwa mambo matatu: safu zetu katika Swala zimefanywa kama safu za Malaika, ardhi yote kwetu imefanywa kuwa Masjid, na vumbi lake limefanywa kitoharisho chetu, tukikosa maji."*¹

Mtume ﷺ ametaja fadhila za vumbi kufanywa safi; na endapo kungekuwa na kitu chingine cha kuchukua nafasi ya *Tayammum*, angelikitaja. Kisafi hapa, imesemwa ni "halali" na imesemwa vile vile 'ambayo sio najisi' kama alivyopokea Imam Ahmad na wakusanyaji wa *Sunan*, isipokuwa Ibn Majah, waliandika kuwa Abu Dharr رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الصَّعِيدُ الطَّيِّبُ طَهُورٌ الْمُسْلِمِ، وَإِنْ لَمْ يَجِدِ الْمَاءَ عَشْرَ حِجَجٍ، فَإِذَا وَجَدَهُ فَلْيَمْسَهُ بِبَشْرَتِهِ، فَإِنَّ ذَلِكَ خَيْرٌ»

*"Ardhi safi ni tohara kwa Waislamu, hata kama hatopata maji kwa miaka kumi. Atakapoyapata maji basi ayatumie kwani ni bora kwa ngozi yake."*² At-Tirmidhi amesema ni *"Hasan Sahih"*

Kauli ya Allah تعالى,

فَامْسَحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ

"Mpake nyuso zenu na mikono yenu."

Inaashiria kuwa *Tayammum* ni badala ya udhu, sio kuosha viungo kama katika kutawadha. Hivyo inatosha katika *Tayammum* kufuta uso na mikono kwa

¹ Muslim 1:371.

² Ahmad 5:180; Abu Dawud 1:235; Tuhfatul Ahwadh 1:388; An-Nasa'I katika Al-Kubra 1:171.

makubaliano ya wanazuoni. Uso na mikono inafutwa kwa pigo moja juu ya mchanga, kama Imam Ahmad alivyonyuka kutoka kwa Abdur - Rahman bin Abbas kuwa alisema, mtu alikuja kwa Umar رضي الله عنه akamsali, "Nina Janaba, ila sina maji." Umar رضي الله عنه akasema, "Basi usiswali". Ammar رضي الله عنه alisema, "Hukumbuki, Ewe Amiri wa Waumini! Mimi nawe tulikuwa katika msafara wa kijeshi tulipopata janaba na hatukupata maji. Hamkusali, lakini nilijibiringisha kwenye mchanga na kisha nikasali. Tuliporejea kwa Mtume ﷺ, tulimuarifu kilichojiri, akaniambia,

«إِنَّمَا كَانَ بِكُمْ غَبْرَةٌ»

"Hakika imekutosha."

Na Mtume ﷺ alipiga mkono wake juu ya mchanga mara moja, akaupuliza na akafuta uso wake na mikono yake."¹ Ummah wa Waislamu minghairi ya mataifa mengine ulipendelewa kwa kuruhusiwa *Tayammum*. Katika Sahih Mbili ilinukuliwa kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أُعْطِيتُ خَمْسًا لَمْ يُعْطَهُنَّ أَحَدٌ قَبْلِي: نُصِرْتُ بِالرُّغْبِ مَسِيرَةَ شَهْرٍ، وَجُعِلَتْ لِي الْأَرْضُ مَسْجِدًا وَطَهْرًا، فَأَيُّمَا رَجُلٍ مِنْ أُمَّتِي أَدْرَكْتُهُ الصَّلَاةَ فَلْيُصَلِّ، وَفِي لَفْظٍ: «فَعِنْدَهُ طَهْرُهُ وَمَسْجِدُهُ، وَأَجَلْتُ لِي الْعَنَائِمَ، وَلَمْ تَحِلَّ لِأَحَدٍ قَبْلِي، وَأُعْطِيتُ الشَّفَاعَةَ، وَكَانَ النَّبِيُّ يُبْعَثُ إِلَى قَوْمِهِ، وَبُعِثْتُ إِلَى النَّاسِ عَامَّةً»

"Nimepewa mambo matano ambayo hakupewa yeyote kabla yangu: Nimenusuriwa kwa hofu masafa ya mwezi; na nimefanyiwa ardhi kuwa Msikiti na kutoharisho. Kwa hiyo, mtu yeyote katika Umma wangu amekutwa na Sala na asali. Na katika riwaya nyingine – atakuwa na cha kujitoharishia na Masjid. Ngawira za vita zilihalalishwa kwangu na haikuwa hivyo kwa walionitangulia. Nimepewa haki ya kuwaombea wafuasi wangu siku ya Kiyama. Kila Mtume alikuwa akitumwa kwa watu wake tu, lakini mimi nimetumwa kwa ulimwengu mzima."²

¹ Ahmad 2:265.

² *Fat'hul Al-Bari* 1:519, *Muslim* 1:370.

Aidha tudhukuru Hadithi ya Hudhaifah رضي الله عنه ambayo iliandikwa na Muslim,

«فُضِّلْنَا عَلَى النَّاسِ بِثَلَاثٍ، جُعِلَتْ صُفُوفُنَا كَصُفُوفِ الْمَلَائِكَةِ، وَجُعِلَتْ لَنَا
الْأَرْضُ مَسْجِدًا، وَتُرْبَتُهَا طَهْرًا، إِذَا لَمْ نَجِدِ الْمَاءَ»

“Tulipendelewa mambo matatu juu ya mataifa mengine. Safu zetu katika Sala zilifanywa kama safu za Malaika, ardhi yote tulifanyiwa Masjid, na vumbi lake lilifanywa tohara ambapo hapana maji.”¹

Allah تعالى Alisema katika Aya hii tukufu,

فَأَمْسُحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُورًا غَفُورًا ﴿٤٣﴾

“Mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu na Mwenye Kughufiria.”

Maana yake: Msamaha ni ruhusa ya *Tayammum* na kuswali baada yake mkikosa maji, ili kuwasahilishia mambo. Ayah hii inatukuza nafasi ya Swala, ni tukufu mno kiasi cha kutoswaliwa katika hali isiyo nzuri, kama ulevi, mpaka mtu ajue anachosema, au akiwa na janaba, mpaka akoge, au akienda haja mpaka atawadhe. Kuna udhuru mtu anapokuwa mgonjwa, au kukosekana maji. Katika hali hii, Allah تعالى Ameruhusu *Tayammum* kwa huruma na wema kwa waja Wake, ili kuwasahilishia na Kuwahurumia mambo, shukrani zote zinamstahiki Allah تعالى.

Sababu za Kuruhusiwa *Tayammum*

Bukhari alinukuu kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Tulisafiri na Mtume ﷺ mpaka tulipofika Al-Baydh au Dhat-ul-Jaysh, mahali ambapo mkufu wangu ulikatika na kupotea. Mtume ﷺ alibaki pale kuutafuta, pamoja na watu aliofuatana nao - sehemu haikuwa na chanzo cha maji, na wala watu hawakuchukuwa maji, hivyo watu walikwenda kwa Abubakar As-Siddiq رضي الله عنه na wakamuambia, ‘Huoni alichofanya Aishah! Amesababisha Mtume ﷺ na watu wengine kukaa pahala pasipo na chanzo cha maji na hatuna maji.’

¹ Muslim 1:371.

Abubakar رضي الله عنه alikuja ambapo Mtume ﷺ alikuwa amelala na kichwa chake ameegemeza juu ya paja langu. Akaniambia, umemzuia Mtume ﷺ na watu wengine pahala pasipo na maji na hakuna aliye na maji. Hivyo alinionya na akasema aliyojaaliwa na Allah تعالى kusema na akanipiga ubavu kwa mkono wake. Nilitikisika kwa maumivu, lakini Mtume ﷺ aliamka Alasiri ikaingia na hapakuwa na maji. Hivyo Allah تعالى Alishusha Aya ya *Tayammum*, na wote walitayamamu. Usayd bin Hudayr رضي الله عنه alisema, 'Ee familia ya Abubakar! Hii siyo mara ya kwanza mnabarikiwa. Kisha ngamia niliyempanda aliondoshwa alipokuwa na mkufu ukaonekana chini yake."¹

Imepokewa na Bukhari na Muslim ²



¹ *Fat'hul Al-Bari* 1:514.

² *Fat'hul Al-Bari* 7:24, 12:180 na Muslim 1:279.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيْبًا مِّنَ الْكِتَابِ يَشْتُرُونَ
 الضَّلٰلَةَ وَيُرِيدُونَ أَن تَضِلُّوا السَّبِيْلَ ﴿٤٤﴾ وَاللّٰهُ أَعْلَمُ
 بِأَعْدَابِكُمْ ۗ وَكَفَى بِاللّٰهِ وَلِيًّا وَكَفَى بِاللّٰهِ نَصِيْرًا ﴿٤٥﴾ مِّنَ
 الَّذِينَ هَادُوا تُحَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَن مَّوَاضِعِهِ وَيَقُولُونَ
 سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا وَاسْمِعْ غَيْرَ مَسْمُوعٍ وَرَاعِنَا لَيًّا بِأَلْسِنَتِهِمْ
 وَطَعْنَا فِي الدِّينِ ۗ وَلَوْ أَنَّهُمْ قَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَاسْمِعْ
 وَأَنْظِرْنَا لَكَانَ خَيْرًا هُمْ وَأَقْوَمَ وَلٰكِن لَّعَنَهُمُ اللّٰهُ بِكُفْرِهِمْ
 فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيْلًا ﴿٤٦﴾ يَتَأْتِيَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ
 ءَامِنُوا بِمَا نَزَّلْنَا مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ مِّن قَبْلِ أَن
 نَّطْمِسَ وُجُوْهَاً فَرُدَّهَا عَلٰى أَدْبَارِهَا أَوْ نَلْعَنَهُمْ كَمَا
 لَعْنَا أَصْحَابَ السَّبْتِ ۗ وَكَانَ أَمْرُ اللّٰهِ مَفْعُوْلًا ﴿٤٧﴾ إِنَّ
 اللّٰهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَن
 يَشَاءُ ۗ وَمَن يُشْرِكْ بِاللّٰهِ فَقَدِ افْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيْمًا ﴿٤٨﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيْبًا مِّنَ
 الْكِتَابِ يَشْتُرُونَ الضَّلٰلَةَ وَيُرِيدُونَ أَن
 تَضِلُّوا السَّبِيْلَ ﴿٤٤﴾ وَاللّٰهُ أَعْلَمُ
 بِأَعْدَابِكُمْ ۗ وَكَفَى بِاللّٰهِ وَلِيًّا وَكَفَى
 بِاللّٰهِ نَصِيْرًا ﴿٤٥﴾ مِّنَ الَّذِينَ هَادُوا
 تُحَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَن مَّوَاضِعِهِ وَيَقُولُونَ
 سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا وَاسْمِعْ غَيْرَ مَسْمُوعٍ
 وَرَاعِنَا لَيًّا بِأَلْسِنَتِهِمْ وَطَعْنَا فِي
 الدِّينِ ۗ وَلَوْ أَنَّهُمْ قَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا
 وَاسْمِعْ وَأَنْظِرْنَا لَكَانَ خَيْرًا هُمْ وَأَقْوَمَ
 وَلٰكِن لَّعَنَهُمُ اللّٰهُ بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُونَ
 إِلَّا قَلِيْلًا ﴿٤٦﴾

44. Huwaoni wale walio pewa sehemu ya Kitabu wananunua upotovu na wanakutakieni nanyi mptote njia?

45. Na Mwenyezi Mungu Anawajua vyema maadui zenu. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni Mlinzi, na Anatosha kuwa ni Mwenye Kukunusuruni.

46. Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahala pake, na husema: Tumesikia na tumeasi, na sikia bila ya kusikilizwa. Na husema: "Raai'naa", kwa kuzipotoa ndimi zao ili kuitukana Dini. Na lau kama wangelisema: Tumesikia na tumetii, na usikie na "Undhurna" (Utungalie), ingelikuwa ni kheri kwao na sawa zaidi. Lakini Mwenyezi Mungu Amewalaani kwa kufuru yao; basi hawaamini ila wachache tu.

Kuwarudi Mayahudi kwa Kuchagua Upotofu, Wakigeuza Maneno ya Allah تعالى na Wakiwadhihaki Waislamu:

Allah تعالى Anaeleza kuwa mayahudi, laana ya Allah تعالى ziwashukie mpaka siku ya Kiyama, wamekhiyari njia potofu badala ya uwongofu, na wakapuuza aliyoteremshiwa Mtume Muhammad ﷺ na Mola Wake. Pia walidharau elimu waliyorithi kutoka kwa Mitume iliyotangulia, kuhusu sifa bainifu za Muhammad ﷺ, kwa ajili ya maslahi machache tu ya kidunia.

يَسْتَرْوْنَ الضَّلَالَةَ وَيُرِيدُونَ أَنْ تَضِلُّوا السَّبِيلَ ﴿٤٤﴾

“Wananunua upotovu na wanakutakeni nanyi mpotee njia?”

Kwani wanataka mkanushe mliyoteremshiwa, Enyi Waumini, na muache kutekeleza muongozo na elimu yenye manufaa mliyonyayo.

وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِأَعْدَابِكُمْ

“Na Mwenyezi Mungu Anawajua vyema maadui zenu.”

Muradi wake, Allah تعالى Anajua zaidi maadui zenu, na Anawahadharisha dhidi yao.

وَكَفَى بِاللَّهِ وَلِيًّا وَكَفَى بِاللَّهِ نَصِيرًا ﴿٤٥﴾

“Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa ni Mlinzi, na Anatosha kuwa ni Mwenye Kukunusuruni.”

Yeye ni Mlinzi wa Kutosha kwa wale wanaokimbilia Kwake na Anatosha Kunusuru kwa wale wanaohitaji msaada Wake.

Kisha Allah تعالى Akasema,

مُخَرَّفُونَ الَّلَاكِمَ عَنْ مَوَاضِعِهِ

“Wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahala pake.”

Maana yake: Wanapotosha kwa makusudi maana ya Aya na wanayaelezea kwa namna nyingine kinyume na Allah تعالى Alivyokusudia.

وَيَقُولُونَ سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا

“Na husema: Tumesikia na tumeasi.”

Wakisema, 'Tumesikia uyasemayo, Ewe Muhammad, lakini hatukutii' kama walivyoeleza Mujahid na Ibn Zayd.¹

Hii ndio maana iliyokusudiwa na Aya, na inaeleza ukafiri wa Mayahudi, ufedhuli wao, na kupuuza kitabu cha Allah تعالى baada ya kukielewa, na huku wakielewa makosa na adhabu watakayopata kutokana na tabia yao.

وَأَسْمِعْ غَيْرَ مُسْمِعٍ

"Na sikia bila ya kusikilizwa."

Maana yake: Sikia maneno yetu, bila kusikilizwa, kama Adh-Dhahak alivyopokea kutoka kwa ibn Abbas رضي الله عنهما.² Hii ndio njia ya Mayahudi ya kudhihaki, Allah تعالى Awalani.

وَرَزَعْنَا لِيَأْ بِأَلْسِنَتِهِمْ وَطَعْنَا فِي أَلْدِينِ

"Na husema: "Raai'naa", kwa kuzipotoa ndimi zao ili kuitukana Dini."

Maana yake: Wamejidai kusema, 'Tusikilizeni, wanaposema, Ra'ina (tusi kwa Kihabrii, lakini kwa Kiarabu ina maana, 'Tusikilizeni). Hata hivyo nia yao ilikuwa kumtukana Mtume ﷺ. Tulitaja somo hili wakati wa kuelezea Kauli ya Allah تعالى,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ بَاءَ امْتُوا لَا تَقُولُوا رَزَعْنَا وَقُولُوا أَنْظَرْنَا

"Enyi mlioamini! Msiseme. Raainaa semeni Un-dhurna."

Kwa hiyo Allah تعالى Aliwazungumzia Mayahudi, ambapo wanasema yale ambayo ni kinyume na yale waliyoyaficha.

وَرَزَعْنَا لِيَأْ بِأَلْسِنَتِهِمْ وَطَعْنَا فِي أَلْدِينِ

"Kwa kuzipotoa ndimi zao ili kuitukana Dini."

Kwa sababu ya kumtukana Mtume ﷺ. Kisha Allah تعالى Amesema,

¹ At – Tabari 8:433.

² At – Tabari 8:434.

وَلَوْ أَنَّهُمْ قَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأَسْمَعُ وَأَنْظُرْنَا لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ وَأَقْوَمَ وَلَٰكِن لَّعَنَهُمُ اللَّهُ بِكُفْرِهِمْ
فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٤٦﴾

**“Na lau kama wangelisema: Tumesikia na tumetii, na usikie na
“Undhurna” (Utungalie), ingeli kuwa ni kheri kwao na sawa zaidi.
Lakini Mwenyezi Mungu Amewalaani kwa kufuru yao; basi
hawaamini ila wachache tu.”**

Maana yake: Mioyo yao iko mbali na uadilifu, kwa hiyo hapana chembe ya imani inayoingia. Mapema tulipoelezea Kauli ya Allah تعالى،

فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٤٦﴾

“Kwa hivyo ni kidogo tu wanayoyaamini.”

Maana yake: Hawana imani itakayowanufaisha.

يٰۤأَيُّهَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ ءَامِنُوا بِمَا نَزَّلْنَا مُصَدِّقًا لِّمَا مَعَكُمْ مِّن قَبْلِ أَن نَّطْمِسَ وُجُوهًا
فَنَرُودَهَا عَلَىٰ أَدْبَارِهَا أَوْ نَلْعَنَهُمْ كَمَا لَعَنَّا أَصْحَابَ السَّبْتِ ؕ وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا ﴿٤٧﴾ إِنَّ
اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَن يَشَاءُ ؕ وَمَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَىٰ
إِنَّمَا عَظِيمًا ﴿٤٨﴾

47. Enyi mliopewa Kitabu! Aminini Tuliyoateremsha yenye kusadikisha yale mliyo nayo, kabla hatujazigeuza nyuso Tukazipeleka kisogoni, au Tukawalaani kama Tulivyowalaani watu wa Sabato (Jumamosi). Na Amri ya Mwenyezi Mungu ni lazima ifanyike.

48. Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehe kushirikishwa, na Husamehe yaliyo duni ya hilo kwa Amtakaye. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu basi hakika amezua dhambi kubwa.

Kuwalingania Watu wa Kitabu Kuamini na Kuwaonya Kutofanya Kinyume Chake

Allah تعالی Anawaamrisha watu wa Kitabu kuamini yale Aliyoyateremsha kwa mja na Mjumbe wake, Muhammad ﷺ, Kitabu Kitakatifu ambacho kinawiana na habari walizokuwa nazo kuhusu Muhammad ﷺ.

Kisha Akawakhofisha,

مِن قَبْلِ أَنْ نَنْظِمَ وَجُوهًا فَتَرُدُّهَا عَلَيَّ أَدْبَارَهَا

“Kabla hatujazigeuza nyuso Tukazipeleka kisogoni.”

Al-Awf alisema, Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa ‘Kuzigeuza’ ina maana ya upotofu.

فَتَرُدُّهَا عَلَيَّ أَدْبَارَهَا

“Tukazipeleka kisogoni.”

Muradi wake, Tumeziweka nyuso zao kisogoni, na kuwafanya kutembea kinyume nyume na hivyo Tunamfanya mmoja wao kuwa na macho kisogoni.¹ Qatadah na Atiyah Al-Awf walisema kama hayo.² Hili linafanya adhabu kuwa kali zaidi, na hili fumbo alilofumba Allah تعالی kwa kudharau kwao ukweli, kukhiyari upotofu, kuacha njia iliyonyooka na kufuata njia potofu. Basi watu aina hiyo wanatembea kinyume nyume.

Vivyo hivyo, baadhi wameitaja Kauli ya Allah تعالی,

إِنَّا جَعَلْنَا فِي أَعْنَاقِهِمْ أَغْلَالًا فَهِيَ إِلَى الْأَذْقَانِ فَهُمْ مُقْمَحُونَ ﴿٨﴾ وَجَعَلْنَا مِنْ بَيْنِ أَيْدِيهِمْ سَدًّا

“Tumeweka makongwa shingoni mwao, yakawafika videvuni. Kwa hivyo vichwa vyao viko juu tu. Tumeweka kizuizi mbele yao...”
(36:8-9)

Hilo ni fumbo alilowapa Allah تعالی kwa Kupotoka kwao na Kujizuia na uwongofu.

¹ At - Tabari 8:440.

² At - Tabari 8:441.

Ka'b Al-Ahbar Alisilimu Baada ya Kusikia Aya (4:47).

Iliarifiwa kuwa Ka'b Al-Ahbar alisilimu baada ya kusikia Ayah (4:47). Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliandika kuwa Isa bin Al-Mughirah alisema: Tulikuwa na Ibrahim tulipozungumzia muda aliosilimu Ka'b. Alisema, Ka'b alisilimu wakati wa utawala wa Umar رضي الله عنه, kwani alipita Madinah alikusudia kuzuru *Baytul Maqdis*, na Umar رضي الله عنه akamuambia, "Silimu, Ewe Ka'b." Ka'b' akamjibu, 'Husomi Kitabu chako,

مَثَلُ الَّذِينَ حُمِّلُوا التَّوْرَةَ

"Mfano wa waliobebeshwa Taurati." (62:5) mpaka

أَسْفَارًا

"Vitabu vikubwa vikubwa." (62:5)

Mimi ni miongoni mwa wale waliopewa Taurati. Umar رضي الله عنه alimuacha naye Ka'b alikwenda Hims (Syria) na akamsikia mmoja wa wakati wake katika jamaa akisoma Aya huku amehuzunika,

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ ءَامِنُونَ بِمَا نَزَّلْنَا مُصَدِّقًا لِمَا مَعَكُمْ مِّن قَبْلِ أَنْ نَطْمِسَ وُجُوهًا

فَنَرُدَّهَا عَلَىٰ أَدْبَارَهَا

"Enyi mliopewa Kitabu! Aminini Tuliyoateremsha yenye kusadikisha yale mliyo nayo, kabla hatujazigeuza nyuso Tukazipeleka kisogoni."

Ka'b akasema, 'Naamini, Ewe Mola! Nasalimu, Ewe Mola.' Kwani alichelea kukutwa na kitisho hiki kisha alirejea Yemen kwa jamaa zake na akarejea nao wote wamesilimu.¹ Kauli ya Allah تعالى،

أَوْ نَلْعَنَهُمْ كَمَا لَعْنَا أَصْحَابَ السَّبْتِ

"Au Tukawalaani kama Tulivyowalaani watu wa Sabato (Jumaamosi)."

¹ At - Tabari 8:446.

Inahusu waliovunja utukufu wa Sabato, wakifanya hadaa, kwa lengo la kufanya kazi zaidi. Allah تعالى Aliwabadili sura zao kuwa za nyani na nguruwe, kama tutakavyofahamu katika maelezo ya *Surat Al-aaraf:7*. Kauli ya Allah تعالى،

وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا ﴿١٧﴾

“Na Amri ya Mwenyezi Mungu ni lazima ifanyike.”

Maana yake: Anapoamrisha kitu, hivyo hapana wa kukanusha au kukataa Amri Yake. Allah تعالى Hasamehi *Shirk* Isipokuwa baada ya Kutubia. Allah تعالى Amesema Yeye،

لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ

“Hasamehe kushirikishwa.”

Maana yake: Hatomsamehe mja atakapokutana Naye hali ya kuwa anamshirikisha Yeye،

وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ

“Na Husamehe yaliyo duni ya hilo.” Maana yake: madhambi،

لِمَنْ يَشَاءُ

“Kwa Amtakaye.” Maana yake: Kwa waja wake.

Imam Ahmad amemnukuu Abu Dharr رضي الله عنه akisema, Mtume ﷺ amesema،

«إِنَّ اللَّهَ يَقُولُ: يَا عَبْدِي مَا عَبْدَتَنِي وَرَجَوْتَنِي، فَإِنِّي غَافِرٌ لَكَ عَلَى مَا كَانَ فِيكَ، يَا عَبْدِي إِنَّكَ إِذَا لَقَيْتَنِي بِقُرَابِ الْأَرْضِ خَطِيئَةٌ مَا لَمْ تُشْرِكْ بِي، لَقَيْتَكَ بِقُرَابِهَا مَغْفِرَةٌ»

“Allah Amesema, ‘Ewe mja wangu! Utakapokuwa unaniabudu na kunitarajia, Nitakusamehe, uliokuwa nayo. Ewe Mja wangu! Utakapokutana Nami na ardhi imejaa madhambi na hukunishirikisha, Nitakulaki kwa madhambi yako kuwa maghufira.”

Ahmad pekee amepokea Hadithi kwa Isnad hii.¹ Imam Ahmad amenukuu kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه kuwa alisema, “Nilikuja kwa Mtume ﷺ akasema،

¹ Ahmad 5:154.

«مَا مِنْ عَتِيدٍ قَالٍ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ ثُمَّ مَاتَ عَلَى ذَلِكَ، إِلَّا دَخَلَ الْجَنَّةَ» قلت: وإن زنى وإن سرق؟ قال: «وإن زنى وإن سرق». قلت: وإن زنى وإن سرق؟ قال: «وإن زنى وإن سرق ثَلَاثًا»، ثم قال في الرابعة: «عَلَى رَعْمِ أَبِي دَرَّةٍ»

"Hapana mja yoyote aliyetamka, "Hapana muabudiwa ila Allah, na akafa katika imani hiyo, ila ataingia Peponi." Nikauliza, 'hata akizini na kuiba?' akasema, "Hata akizini na kuiba." Nikasema, "Hata akizini na kuiba? Akasema, "Hata akizini na kuiba." Mara ya nne, akasema, "Hata Abu Dharr akikataa."

Abu Dharr رضي الله عنه aliondoka akiburuza *Izariyake* akisema, 'Hata Abu Dharr رضي الله عنه akikataa.' Toka siku hiyo Abu Dharr رضي الله عنه alikuwa akisimulia Hadithi hii na kisha akiongeza, 'Hata kama Abu Dharr رضي الله عنه akikataa.'¹

Sahihi Mbili zimeandika.²

Al-Bazzar رحمه الله تعالى alimnukuu Ibn Umar رضي الله عنهما akisema, "Tulikuwa tukijizua kumuomba Allah تعالى Maghfira kwa tuliofanya dhambi kubwa mpaka tulipo msikia Mtume ﷺ akisoma,

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

"Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehe kushirikishwa, na Husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye."

Na kauli ya Mtume ﷺ,

«أَخْرَجْتُ شَفَاعَتِي لِأَهْلِ الْكِبَائِرِ مِنْ أُمَّتِي يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

"Nimeucheleweshwa uombezi wangu ili uwe ni kwa ajili ya kuwaombea watu wa Ummah wangu wenye madhambi makubwa siku ya Kiyama."³

¹ Ahmad 5:152.

² *Fat'hul Al-Bari* 10:294 na Muslim 1:95.

³ Kashf Al-Astar 4:84.

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ افْتَرَىٰ إِثْمًا عَظِيمًا ﴿٤٤﴾

“Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu basi hakika amezua dhambi kubwa.”

Ni sawa na Kauli Yake،

إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ ﴿٣١﴾

“Kwani hakika ushirikina bila ya shaka ni dhulma iliyo kubwa.”
(31:13)

Ndani ya sahihi Mbili iliandikwa kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisema, “Nilisema, Ewe Mjumbe wa Allah! Ni ipi dhambi kubwa?” Alijibu

«أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ نِدَاءً وَهُوَ خَلَقَكَ»

“Kumfanyia Allah تعالى mshirika ambapo Yeye Pekee Ndiye Aliyekuumba.”¹

Na alitaja Hadithi kamili.

* * *

¹ Fat'hul Al-Bari 8:350 na Muslim 1:90.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يُزَكُّونَ أَنْفُسَهُمْ ۗ بَلِ اللَّهُ يُرِيكُم مِّنْ يَشَاءُ وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٤٩﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ ۗ
 وَكَفَى بِمَنِ إِثْمًا مُّبِينًا ﴿٥٠﴾ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا
 مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْحِجَابِ وَالطَّافُوتِ وَيَقُولُونَ لِلَّذِينَ
 كَفَرُوا هَتُّؤَلَاءِ أَهْدَىٰ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا سَبِيلًا ﴿٥١﴾ أُولَٰئِكَ
 الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ ۗ وَمَن يَلْعَنِ اللَّهُ فَلَن نَّجِدَ لَهُ نَصِيرًا ﴿٥٢﴾ أَمْ
 هُمْ نَصِيبٌ مِّنَ الْمَلَكِ فَإِذَا لَا يُؤْتُونَ النَّاسَ نَقِيرًا ﴿٥٣﴾ أَمْ
 يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا ءَاتَاهُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ ۗ فَقَدْ ءَاتَيْنَا
 ءَالَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَءَاتَيْنَاهُم مَّلَكًا عَظِيمًا ﴿٥٤﴾
 فَوَعَّاهُمْ مِّنْ ءَمَانٍ بِيَمِينِهِمْ مِّنْ صَدِّعْتَهُ ۗ وَكَفَىٰ بِهِمْ سَعِيرًا
 ﴿٥٥﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِءَايَاتِنَا سَوَّفَ نُصَلِّبُهُمْ نَارًا كُلَّمَا نَضِجَتْ
 جُلُودُهُمْ بِدَلَنَتُهُمْ جُلُودًا غَيْرَهَا لِيَذُوقُوا الْعَذَابَ ۗ إِنَّ اللَّهَ
 كَانَ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٥٦﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
 سَنُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ
 هُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ ۗ وَنُدْخِلُهُمْ ظِلًّا ظَلِيلًا ﴿٥٧﴾ * إِنَّ اللَّهَ
 يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُم بَيْنَ النَّاسِ
 أَنْ تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ ۗ إِنَّ اللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُم بِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ
 سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٥٨﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا
 الرَّسُولَ وَأُولَى الْأَمْرِ مِنْكُمْ ۗ فَإِن تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوه إِلَى اللَّهِ
 وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ ذَلِكَ خَيْرٌ
 وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يُزَكُّونَ أَنْفُسَهُمْ ۗ بَلِ اللَّهُ يُرِيكُم مِّنْ يَشَاءُ وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٤٩﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ ۗ
 وَكَفَى بِمَنِ إِثْمًا مُّبِينًا ﴿٥٠﴾ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا
 مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْحِجَابِ وَالطَّافُوتِ وَيَقُولُونَ لِلَّذِينَ
 كَفَرُوا هَتُّؤَلَاءِ أَهْدَىٰ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا سَبِيلًا ﴿٥١﴾ أُولَٰئِكَ
 الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ ۗ وَمَن يَلْعَنِ اللَّهُ فَلَن نَّجِدَ لَهُ نَصِيرًا ﴿٥٢﴾

49. Jee huwaoni wale wanaodai kuwa ati wame-takasika? Bali Mwenyezi Mungu Humtakasa Amtakaye. Na hawata dhulumiwa hata kadiri ya kijiuzi kilichomo ndani ya uwazi wa kokwa ya tende.

50. Tazama vipi wanavyomzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na haya yatosha kuwa dhambi iliyo dhahiri.

51. Huwaoni wale walio-pewa sehemu ya Kitabu?

Wanaamini masanamu na Shet'ani! Na wanawasema waliokufuru, kuwa hao wameongoka zaidi katika njia kuliko Walioamini.

52. Hao ndio Mwenyezi Mungu Amewalaani. Na ambaye Mwenyezi Mungu Amemlaani basi hutamuona kuwa na mwenye kumnusuru.

Kuwakemea na Kuwalaani Mayahudi kwa Kujitangazia Utakasifu Kuamini Jibt na Twaghut

Al-Hasan na Qatadah walisema, "Aya hii,

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يُرْكُونَ أَنْفُسَهُمْ

"Jee huwaoni wale wanaodai kuwa ati wametakasika?"

Iliteremshwa kwa ajili ya Mayahudi na Wakristo, waliposema, "Sisi ni wana wa Allah na tunaopendwa Naye."¹ Aidha Ibn Zayd alisema, Aya hii iliteremshwa kuhusiana na kauli yao,

لَحْنًا أَبْتَنُوا لِلَّهِ وَأَحْبَبُوا

"Sisi ni wana wa Mwenyezi Mungu na vipenzi vyake." (5:18).

Na kauli yao nyingine,

لَنْ يَدْخُلَ الْجَنَّةَ إِلَّا مَنْ كَانَ هُودًا أَوْ نَصْرِيًّا

"Hataingia Peponi ila aliyekuwa Yahudi au Mkristo." (2:111)²

Kwa sababu hiyo Allah تعالی Amesema,

بَلِ اللَّهِ يُرْسِي مَنْ يَشَاءُ

".....Bali Mwenyezi Mungu Humtakasa Amtakaye."

Maana: Uamuzi wa jambo hili uko Mikononi mwa Allah تعالی Peke Yake kwa sababu Anajua ukweli na uhakika na siri za vitu vyote. Kisha Allah تعالی Amesema,

¹ At - Tabari 8:452.

وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٥٨﴾

“Na hawatadhulumiwa hata kadiri ya kijiuzi kilichomo ndani ya uwazi wa kokwa ya tende.”

Muradi wake ni kuwa, “Hamdhulumu yeyote katika malipo hata kama yalikuwa na uzito wa *Fatl*.” Ibn Abbas, Mujahid, Ikrimah, Ata, Al-Hasan, Qatadah na wengineo رضي الله عنهم miongoni mwa *Salaf* walisema kuwa *Fat-l* ina maana ya kijiuzi kilichomo ndani ya uwazi wa kokwa ya tende.”¹

Allah تعالى Amesema,

أَنْظُرْ كَيْفَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ

“Tazama vipi wanavyo mzulia uwongo Mwenyezi Mungu.”

Wakidai utakasifu, kuwa wao ni wana wa Allah تعالى wapendwao Naye, kauli yao,

لَنْ يَدْخُلَ الْجَنَّةَ إِلَّا مَنْ كَانَ هُودًا أَوْ نَصْرَى

“Hataingia Peponi ila aliyekuwa Yahudi au Mkristo.” (2:111)²

Kauli yao,

وَقَالُوا لَنْ تَمَسَّنَا النَّارُ إِلَّا أَيَّامًا مَعْدُودَةً

“Hautatugusa Moto ila kwa siku chache tu...” (2:80)

Na kutegemea kwao amali njema zilizofanywa na babu zao Allah تعالى Amehukumu kuwa matendo mema ya baba hayawasaidii watoto, Aliposema,

تِلْكَ أُمَّةٌ قَدْ خَلَتْ هَلْ أَمَّا كَسَبَتْ وَلَكُمْ مَّا كَسَبْتُمْ

“Hao ni watu waliokwisha pita. Wao watapata waliyoyachuma, na nyinyi mtapata mliyoyachuma...” (2:141)

Kisha Allah تعالى Aliposema,

وَكَفَىٰ بِهِمْ إِتْمَانًا

“Na haya yatosha kuwa dhambi iliyo dhahiri.”

¹At - Tabari 458,459.

²At - Tabari 8:453.

Maana yake: Urongo wao na uzushi vinatosha. Kauli ya Allah تعالى،

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ يُؤْمِنُونَ بِالْكِتَابِ وَأَلْفُتُونَ

“Huwaoni wale waliopewa sehemu ya Kitabu? Wanaamini masanamu na Shetani!”

Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Hassan bin Faid kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema, 'Jibt ni uchawi na *Twaghut* ni shetani."¹ Abu Nasr Ismail bin Hammad Al-Jawhar, mwanazuoni maarufu, alisema ndani ya kitabu chake *As-Sihah*, "Al-Jibt maana yake mungu – sanamu, mpiga ramli na mchawi." Ibn Abi Hatim aliandika kuwa, "Jabir bin Abdullah aliulizwa juu ya *Twaghut*, na alijibu, "Ni watabiri ambao wametumwa na shetani."² Mujahid alisema, " *Twaghut* ni shetani katika umbile la binadamu na wanamuendea kwa kutanzuliwa matatizo, naye ndie bwana wao."³ Imam Malik alisema, " *Twaghut* ni kila kitu kinachoabudiwa badala ya Allah تعالى Aliye juu na Mtukufu."

Makafiri Hawana Ubora Juu ya Waumini:

Allah تعالى Amesema,

وَيَقُولُونَ لِلَّذِينَ كَفَرُوا هَتُّؤُلَاءِ أَهْدَىٰ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا سَبِيلًا ﴿٥٦﴾

“Na wanawasema waliokufuru, kuwa hao wameongoka zaidi katika njia kuliko Walioamini.”

Wakiwapendelea makafiri kuliko Waislamu kwa sababu ya ujinga na uchache wa Dini yao na hali ya ukafiri na kukanusha Kitabu cha Allah تعالى ambacho kilikuwa mbele yao.

Ibn Abi Hatim aliandika kuwa Ikrimah alisema, "Huyeyi bin Akhtab na Ka'b bin Al-Ashraf (viongozi wa Kiyahud) waliwajia watu wa Makkah, wakawaambia: "Enyi (Mayahudi) ni watu wa Kitabu na Wasomi, tujulisheni sisi na Muhammad, wakasema, tupeni wasifu wenu na wa Muhammad, wakajibu, Tunaimarisha uhusiano na marafiki na aali, tunachinja ngamia (kuwapa masikini), tunawalipia wadaiwa na tunawapa maji mahujaji. Ama kuhusu Muhammad ﷺ, hana mtoto wa kiume, alivunja uhusiano na wezi waliowaibia

¹ At - Tabari 8:462.

² Ibn Abi Hatim 3:994.

³ At-Tabari 8:462.

mahujaji na kabila linalomfuata ni Ghifar. Hivyo nani bora zaidi, sisi au yeye?" Wakasema, 'Nye ni waadilifu zaidi na mmeongoza vema.' Kwa hiyo Allah تعالی Aliteremsha.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ

"Huwaoni wale waliopewa sehemu ya kitabu..."¹

Kisa hiki kilipokelewa kwa namna mbalimbali kutoka kwa Ibn Abbas na wengine miongoni mwa *Salaf* رضي الله عنهم.

Laana ya Allah تعالی kwa Mayahudi kwa Kuwasaidia Washirikina

Aya hii (4:52) ina laana kwa Mayahudi na inawaarifu kutokuwa na msaidizi duniani au siku ya Kiyama, sababu walitafuta msaada wa makafiri (waabudu masanamu). Walitumia (Aya 4:51) kuwaghilibu makafiri wawaunge mkono, na hatimaye walikusanya majeshi yao kwa ajili ya vita vya *Ahzaab*, na kumlazimisha Mtume ﷺ na Masahaba kuchimba mahandaki kuuzunguka mji wa Madina. Lakini Allah تعالی Aliwaokoa Waislamu kutokana na uovu wao,

وَرَدَّ اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا بِغَيْظِهِمْ لَمْ يَنَالُوا خَيْرًا وَكَفَى اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ الْقِتَالَ وَكَانَ اللَّهُ

قَوِيًّا عَزِيزًا ﴿٥٢﴾

"Na Mwenyezi Mungu Aliwarudisha nyuma makafiri juu ya ghadhabu yao; hawakupata kheri yoyote. Na Mwenyezi Mungu Amewatosheleza Waumini katika vita. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Uweza." (33:25)

أَمْ هُمْ نَصِيبٌ مِّنَ الْمُلْكِ فَإِذَا لَا يُؤْتُونَ النَّاسَ نَقِيرًا ﴿٥٣﴾ أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا

ءَاتَاهُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ ۗ فَقَدْ ءَاتَيْنَا آلَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَءَاتَيْنَاهُم مَّا لَمْ يَكُونُوا

عَالَمِينَ ﴿٥٤﴾ فَمِنْهُمْ مَّنْ ءَامَنَ بِهِ وَمِنْهُمْ مَّنْ صَدَّ عَنْهُ ۗ وَكَفَىٰ بِجَهَنَّمَ سَعِيرًا ﴿٥٥﴾

53. Au wanayo sehemu ya utawala? Basi hapo wasingewapa watu hata tundu ya kokwa ya tende.

54. Au wanawahusudu watu kwa yale Aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa Fadhila Yake? Basi Tuliwapa ukoo wa Ibrahim Kitabu na hikima na Tukawapa utawala mkubwa.

¹ Ibn Abi Hatim 3:994 na Tabari 5:133.

55. Basi wapo miongoni mwao waliyo yaamini, na wapo walio yakataa. Na Jahannamu yatosha kuwa ni moto wa kuwateketeza.

Ubakhili wa Husda ya Mayahudi

Allah تعالى Aliwasaili Mayahudi kama wana hisa katika utawala. Kauli hii ni kejeli kwani hawana hisa yoyote katika utawala. Kisha Allah تعالى Akawaelezea kuwa ni mabakhili.

فَإِذَا لَا يُؤْتُونَ النَّاسَ نَقِيرًا ﴿٥٧﴾

“Basi hapo wasingewapa watu hata tundu ya kokwa ya tende.”

Maana yake: Wangekuwa na sehemu katika milki na utawala, wesingempa mtu chochote, hasa Muhammad ﷺ, hata kama ingekuwa ni tundu ya kokwa ya tende, ambayo ndiyo maana ya *Naqir* kwa mintaarafu ya Ibn Abbas رضي الله عنهما na wengi wa wanazuoni. Aya hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

قُلْ لَوْ أَنْتُمْ تَمْلِكُونَ خَزَائِنَ رَحْمَةِ رَبِّي إِذًا لَأَمْسَكْتُمْ خَشْيَةَ الْإِنْفَاقِ

“Sema: Lau kuwa nyinyi mnazimiliki hazina za rehema za Mola Wangu Mlezi, basi hapana shaka mngelizuia kuzitumia kwa ajili ya kukhofu.” (17:100)

Maana yake: Kuchelea mwisho utakavyo kuwa, japokuwa hapana uwezekano huo. Hii inaonesha tabia yao ya uroho na ubakhili. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

وَكَانَ الْإِنْسَانُ قَتُورًا ﴿٥٨﴾

“Na mwanaadamu tangu hapo tabia yake ni mchoyo!” (17:100)

Maana yake, bakhili. Kisha Allah تعالى Akasema,

أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَى مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ

“Au wanawahusudu watu kwa yale Aliyowapa Mwenyezi Mungu.”

Unakusudiwa wivu wao dhidi ya Mtume ﷺ kwa kupewa utume mkubwa na Allah تعالى. Wivu wao uliwapelekea kumkana kwa sababu alikuwa Mwarabu na sio kutoka wana wa Israili.

At-Tabarani alimnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما aliyesema kuhusu Kauli ya Allah,

أَمْرًا تَحْسُدُونَ النَّاسَ

"Au wanawahusudu watu." Ibn Abbas رضي الله عنهما amesema, maana: "Sisi ni watu wa thamani, kuliko watu wengine."¹ Allah تعالى Amesema,

فَقَدْ ءَاتَيْنَا ءَالَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَءَاتَيْنَهُمْ مُلْكًا عَظِيمًا ﴿٤٩﴾

"Basi Tuliwapa ukoo wa Ibrahim Kitabu na hikima na Tukawapa utawala mkubwa."

Muradi wake, Tuliwapa utume makabila ya Wana wa Israil ambao ni katika wajukuu wa Ibrahim عليه السلام na Tukawateremshia vitabu. Mitume hao waliwatawala Mayahudi kwa mafundisho ya kitume, nayo ni Hikma, na Tuliwafanya wafalme katika wao. Hata hivyo.

فَمِنْهُمْ مَّنْ ءَامَنَ بِهِ

"Basi wapo miongoni mwao waliyoyaamini."

Maana yake: Kwa Muhammad ﷺ,

وَمِنْهُمْ مَّنْ صَدَّ عَنْهُ

"Na wapo waliyakataa."¹ Kwa hiyo, Makafiri wanakukadhibisha sana, na mbaya zaidi wako baidi na ukweli uliowaletea. Kwa sababu hii Allah تعالى Amewatisha,

وَكَفَىٰ لِحُجَّتِهِمْ سَعِيرًا ﴿٥٠﴾

"Na Jahannamu yatosha kuwa ni moto wa kuwateketeza."

Maana yake: Jahannam ni adhabu stahiki kwao kwa sababu ya ukafiri wao, uasi na kukengeuka Vitabu na Mitume ya Allah تعالى.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِءَايَاتِنَا سَوْفَ نُصَلِّبُهُمْ نَارًا كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُمْ بَدَّلْنَاهُمْ جُلُودًا غَيْرَهَا

لِيَذُوقُوا الْعَذَابَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٥١﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

سَنُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرَىٰ مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ هُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ ۗ

وَنُدْخِلُهُمْ ظِلًّا ظَلِيلًا ﴿٥٢﴾

¹ At - Tabari 8:482.

56. Hakika wale waliozikataa Ishara zetu Tutawaingiza Motoni. Kila zitapowiva ngozi zao Tutawabadilishia ngozi nyengine ili waionje hiyo adhabu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima.

57. Na wale walio amini na wakatenda mema Tutawaingiza katika Pepo zipitazo mito kati yake kwa kudumu humo milele. Huko watakuwa na wake waliotakasika, na Tutawaingiza katika vivuli vizuri kweli.

Adhabu ya Wale Wasioamini Vitabu na Mitume ya Allah تعالی

Allah تعالی Anaeleza adhabu ndani ya Moto wa Jahannam, kwa wale wanao kadhibisha Aya zake na wanazuia katika njia ya Mitume wake. Allah تعالی Amesema,

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِنَا

“Hakika wale waliozikataa Ishara Zetu.” Maana yake: Tutawaweka katika Moto ambao utaenea viungo vya miili yao yote. Kisha Allah تعالی Anasema kuwa adhabu yao na mateso yao ni ya kudumu. Allah تعالی Akasema,

كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُمْ بَدَّلْنَاهُمْ جُلُودًا غَيْرَهَا لِيَذُوقُوا الْعَذَابَ

“Kila zitapowiva ngozi zao Tutawabadilishia ngozi nyingine ili waionje hiyo adhabu.”

Al-A'mash alisema kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema, “Ngozi zao zitakapochomwa watapewa ngozi nyingine badala yake, na ngozi hii itakuwa nyeupe kama karatasi.”¹ Hadithi ilikusanywa na Ibn Hatim, ambaye naye aliandika kuwa Al-Hasan alisema,

كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُمْ

“Kila zitapowiva ngozi zao.” “Ngozi zao zitachomwa mara elfu sabini kila siku.” Husayn alisema Fudayl aliongeza kuwa Hisham alisema kuwa Al-Hasan pia alisema kuwa,

كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُمْ

“Kila zitapowiva ngozi zao.”

¹ At - Tabari 8:484.

Maana yake: "Kila Moto utakapoivisha ngozi zao na nyama kwisha, wataambiwa, rejeeni kama mlivyokuwa, na zitakuwa."¹

Mafikio ya Waja Wema Peponi na Neema Zake.

Allah تعالى Amesema,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَنُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا
أَبَدًا ط

"Na wale walioamini na wakatenda mema Tutawaingiza katika Pepo zipitazo mito kati yake kwa kudumu humo milele."

Inaelezea makazi ya wenye sururi ndani ya mabustani ya Eden, chini yake inapita mito katika eneo lote, nafasi ya kona, mahali popote itakapo. Wataishi ndani yake milele, na katu hawatahamishwa au kuondolewa, wala wao hawatapenda kugura kutoka humo. Allah تعالى Amesema,

هُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُطَهَّرَةٌ

"Huko watakuwa na wake waliotakasika."

Maana yake: Hawana hedhi wala nifasi, uchafu, tabia mbaya au dosari. Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Ayah hii ina maana, "wametakaswa na uchafu na mambo mabaya."² Ata, Al-Hasan, Adh-Dhahhak, An-Nakhai, Abu Salih, Atiyah, na As-Suddi³ walisema vivyo hivyo. Mujahid alisema kuwa hawaendi msalani, hawatemi mate, au kutoa manii na hawabebi mimba.' Kauli ya Allah تعالى,

وَنُدْخِلُهُمْ ظِلًّا ظَلِيلًا ﴿٥٧﴾

"Na Tutawaingiza katika vivuli vizuri kweli."

Maana yake: vipana, vikubwa, safi na kivuli jamala. Ibn Jarir رحمه الله تعالى aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ At - Tabari 8:485.

² At - Tabari 1:395.

³ Ibn Abi Hatim 1:92.

⁴ At- Tabari 8:489. Pia imerikodiwa na Ahmad na At-Tayalisi. Hadithi yenye maneno haya, 'Mti wa maisha ya milele' sio sahihi. Maneno mengine yaliyobaki ya Hadithi ni Sahihi na yamerekodiwa na Bukhari na wengineo.

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ لَشَجْرَةً يَسِيرُ الرَّايِبُ فِي ظِلِّهَا مِائَةَ عَامٍ لَا يَقْطَعُهَا : شَجْرَةُ الْخُلْدِ»

*"Kuna mti peponi, ambapo mpanda farasi anasafiri chini yake kwa miaka mia moja hatoumaliza. Ni mti wa Maisha ya Milele."*¹

«إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا

بِالْعَدْلِ إِنَّ اللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُمْ بِهِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٥٨﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe. Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu. Hakika haya Anayokuwaidhini Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona." (4:58)

Amri ya Kurejesha Amana kwa Yeyote Anayestahiki:

Allah تعالى Ameerisha kuwa amana zirejeshwe kwa wenyewe. Al-Hasan alisimulia kuwa Samurah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«أَدِّ الْأَمَانَةَ إِلَىٰ مَنْ اتَّيَمَّنَكَ، وَلَا تَخُنْ مَنْ خَانَكَ»

"Rejesha amana kwa yule aliyeziweka kwako, na usimkhini aliyekukhini."

Imam Ahmad na watu wa Sunan wameipokea Hadith hii.² Amri hii inahusu kila anachotakiwa mtu kukichunga, kama haki za Allah تعالى kwa waja wake. Kusali, Zakah, kufunga, adhabu kwa kutenda dhambi, viapo na kadhalika. Aidha amri hiyo inahusu, kuchunga haki za waja, kama vile amana wanazowekeana, pamoja na masuala aliyoaminiwa yasioandikwa. Allah تعالى Anaamrisha Kutekeleza amana zote. Wasiotekeleza amri hii duniani itatolewa katika amali zao Siku ya Kiyama. Imeandikwa ndani ya Sahih kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَتُؤَدَّنَ الْحُقُوفُ إِلَىٰ أَهْلِهَا حَتَّىٰ يُقْتَصَرَ لِلشَّاءِ الْجَمَاءِ مِنَ الْقَرْنَاءِ»

*"Haki zitarejeshwa kwa wenyewe, na hata kondoo asiye na pembe atalipiza kisasi kwa kondoo mwenye pembe."*³

¹ Ahmad 3:414; Abu Dawud 3:805; Tuhfat Al-Ahwadhi 4:479.

² Muslim 4:1997.

³ At-Tabari 8:492.

Ibn Jarir aliandika kuwa Ibn Jurayj aliizungumzia Aya hii, "Iliteremshwa kumhusu Uthman bin Talhan ambaye alimrejeshea Mtume ﷺ funguo za Al-Ka'bah na akaingia nazo Siku ya *Fat'hi Makkah*. Mtume ﷺ alipotoka alikuwa akisoma Aya,

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا ﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe."

Kisha alimuita Uthman na akamrejeshea funguo." Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisimulia pia kuwa Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alipotoka ndani ya Ka'bah, alikuwa akisoma Aya hii,

﴿ إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَنْ تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ أَهْلِهَا ﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Anakuamrisheni mzirudishe amana kwa wenyewe."

Naweza kujitoa muhanga kwa niaba ya baba na mama yangu, sijapata kuisikia Ayah hii kabla ya hapo."¹ Imetangaa kuwa yamkini hii ndio sababu ya kushushwa Ayah (4:58). Hata hivyo matumizi ya Ayah hii ni ya jumla iwe ni kwa sababu hiyo imeteremka au sababu nyingineyo; na kwa sababu hiyo Ibn Abbas رضي الله عنهما na Muhammad bin Hanafiyyah walisema, "Ayah hii inawahusu watu wema na watu waovu." Yaani ni amri inayomhusu kila mtu.

Amri Yakuwa Muadilifu Katika Hukumu.

Allah تعالى Amesema;

﴿ وَإِذَا حَكَمْتُمْ بَيْنَ النَّاسِ أَنْ تَحْكُمُوا بِالْعَدْلِ ﴾

"Na mnapo hukumu baina ya watu mhukumu kwa uadilifu."

Allah تعالى Anaamrisha kutenda haki wakati wa kutoa hukumu baina ya watu. Muhammad bin Ka'bi, Zayd bin Aslam na Shahr bin Hawshab walisema, "Ayah hii iliteremshwa kwa wale wenye mamlaka."² Ikiwa na maana wale wanao hukumu baina ya watu. Hadithi inasema,

¹ At - Tabari 8:490.

² At-Tabari 8:490.

«إِنَّ اللَّهَ مَعَ الْحَاكِمِينَ مَا لَمْ يُعْزِ، فَإِذَا جَارَ وَكَلَهُ اللَّهُ إِلَى نَفْسِهِ»

*"Allah تعالى Anamridhia hakimu madhali hadhulumu, na akifanya, Allah Atamuacha ajitegemee bila Msaada Wake."*¹

Na katika mapokezi mengine kauli inaendelea, "Siku moja kufanya hukumu ya haki ni sawa na ibada ya miaka arubaini."²

Allah تعالى Amesema,

إِنَّ اللَّهَ نِعْمًا يَعِظُكُمْ بِهِ

"Hakika haya anayo kuwaidhini Mwenyezi Mungu ni mazuri sana."

Maana yake: Anawaamrisheni kutekeleza amana na kuhukumu kwa uadilifu baina ya watu na mfano wa hayo katika Maamrisha Yake na Shariah Zake Timilifu na Tukufu zilizosheheni kila sehemu za konde la maisha.

إِنَّ اللَّهَ كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٥٩﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona."

Muradi wake ni kuwa, Anasikia kauli zenu na Anajua vitendo vyenu.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولَى الْأَمْرِ مِنْكُمْ ۗ فَإِن تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

59. "Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema."

¹ Ibn Majah 2:775.

² Al-Kanz 6:12.

Ulazima wa Kuwatii, Viongozi Katika Yasiyomuasi Allah:

أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولَى الْأَمْرِ مِنْكُمْ

"Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi."

"Iliteremshwa juu ya Abdullah bin Hudhaifah bin Qays bin Adi رضي الله عنه ambaye alitumwa na Mtume ﷺ katika safari ya kijeshi."¹ Kauli hii ilikusanywa na kikundi cha wapokezi wa Hadithi isipokuwa Ibn Majah.² At-Tirmidhi ameitaja kuwa, *"Hasan Gharib"*. Imam Ahmad alirekodi kuwa Ali رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alipeleka kikosi chini ya uongozi wa mtu kutoka Ansar. Walipoondoka, alighadhibika kutokana na sababu fulani na akawaambia, "Mtume ﷺ hakuwaamrisheni nyinyi kunitii mimi?" Wakajibu 'Ndiyo'. Akasema, "Kusanyeni kuni, kisha akakoka moto kwa kuni, huku akiwaambia, 'Nawaamrisha muingie ndani ya moto!' Walikuwa karibu waingie motoni, lakini kijana mmoja miongoni mwao, alisema, "Kimbieni kutoka katika Moto na muende kwa Mtume ﷺ. Msiwe na haraka, rejeeni." Kwa hiyo, waliporejea kwa Mtume ﷺ walimuambia yaliyojiri, na Mtume ﷺ alisema,

«لَوْ دَخَلْتُمُوهُمَا مَا خَرَجْتُمْ مِنْهَا أَبَدًا، إِنَّمَا الطَّاعَةُ فِي الْمَعْرُوفِ»

*"Kama mngeingia msingeweza kutoka humo Abadan. Utiifu ni kwa mambo yaliyo sawa na ya kheri tu."*³

Hadithi hii imeandikwa katika sahih Mbili.⁴ Abu Dawud aliandika kuwa Abdullah Ibin Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«السَّمْعُ وَالطَّاعَةُ عَلَى الْمَرْءِ الْمُسْلِمِ فِيمَا أَحَبَّ وَكَرِهَ، مَا لَمْ يُؤْمَرْ بِمَعْصِيَةٍ، فَإِذَا أُمِرَ بِمَعْصِيَةٍ فَلَا سَمْعَ وَلَا طَاعَةَ»

"Muislamu anatakiwa kusikia na kutii katika lile alipendalo na alichukialo, ila atakapoamrishwa kutenda maasia. Atakapoamrishwa kutenda maasia, hapa hapana kusikia au kutii."

¹ Fat'hul Al-Bari 8:101.

² Muslim 3:1465, Abu Dawud 3:92, Tuhfat Al-Ahwadhi 5:364 na An-Nasa' I 7:154.

³ Ahmad 1:82.

⁴ Fat'hul Al-Bari 7:655, Muslim 3:1469.

Hadithi hii imeandikwa katika Sahihi Mbili.¹ Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه alisema, "Tulimpa ahadi Mtume ﷺ ya kuwasikiliza na kuwatii (viongozi wetu) wakati wa matatizo, hata kama tumenyimwa hisa zetu stahiki; na kutoukanusha uongozi na watu wake waongofu." Mtume ﷺ alisema,

«إِلَّا أَنْ تَرَوْا كُفْرًا بَوَاحًا، عِنْدَكُمْ فِيهِ مِنَ اللَّهِ بَرْهَانٌ»

"Ila utakaposhuhudia kufr iliyo dhahiri, na ambayo mna dalili zilizo wazi kutoka kwa Allah."

Hadithi imeandikwa ndani ya Sahih Mbili.² Hadithi nyingine iliyosimuliwa na Anas رضي الله عنه inayosema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«اسْمَعُوا وَأَطِيعُوا، وَإِنْ أَمَرَ عَلَيْكُمْ عَبْدٌ حَبَشِيٌّ كَأَنَّ رَأْسَهُ زَيْبَةٌ»

"Sikilizeni na mtii (viongozi wenu), hata kama ni Mtumwa wa kihabeshi ambaye kichwa chake ni kama zabibu kavu amefanywa kiongozi wenu."

Bukhari alisajili Hadithi hii.³ Umm Al-Husayn رضي الله عنها alisema kuwa alimsikia Mtume ﷺ akiitoa hotuba wakati wa Hajj ya Kuaga, ambapo alisema,

«وَلَوْ اسْتُعْمِلَ عَلَيْكُمْ عَبْدٌ يَقُودُكُمْ بِكِتَابِ اللَّهِ، اسْمَعُوا لَهُ وَأَطِيعُوا»

"Hata kama mtumwa atateuliwa juu yenu, na akawatawala kwa kitabu cha Allah, basi msikilizeni na mumtii."

Muslim aliandika Hadithi hii.⁴ Katika mapokezi ya Muslim, Mtume ﷺ alisema,

«عَبْدًا حَبَشِيًّا مَجْدُوعًا»

"Hata kama mtumwa wa Kihabeshi ambaye amekakwa pua..."

Ndani ya Sahih Mbili iliandikwa kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Abu Dawud 2626, Bukhari 7144; Muslim 1839.

² Fat'hul Al-Bari 13:204, Muslim 3:470.

³ Fat'hul Al-Bari 13:130.

⁴ Muslim 1338.

«مَنْ أَطَاعَنِي فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ، وَمَنْ عَصَانِي فَقَدْ عَصَى اللَّهَ، وَمَنْ أَطَاعَ أَمِيرِي فَقَدْ أَطَاعَنِي، وَمَنْ عَصَى أَمِيرِي فَقَدْ عَصَانِي»

“Mwenye kunitii, amemtii Allah تعالى, na mwenye kuniasi, amemuasi Allah. Yeyote anayemtii kiongozi wangu, amenitii, na mwenye kumuasi kamanda wangu, ameniasi mimi.”¹

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

أَطِيعُوا اللَّهَ

“Mtiini Mwenyezi Mungu.”

Shikamaneni na kitabu Chake.

وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ

“Na mtiini Mtume.”

Shika maneni na sunnah zake.

وَأُولَى الْأَمْرِ مِنْكُمْ

“Na wenye madaraka katika nyinyi.”

Maana yake: Katika wanalowaamrisheni katika kumtii Allah تعالى kama mliyoamrishwa, na wala si katika kumuasi Allah تعالى, kwani hapana utii wa yeyote katika kumuasi Allah تعالى, kama tulivyoitaja Hadithi sahihi,

«إِنَّمَا الطَّاعَةُ فِي الْمَعْرُوفِ»

“Hakika utiifu ni katika mema .”²

¹ Fat'hul Al-Bari 13:119, na Muslim 3:1466.

² Fat'hul Al-Bari 13:130.

Ulazima wa Kurejesha Hukumu Katika Qur'an na Sunnah Wakati Mkizozana:

Allah تعالی Amesema,

فَإِنْ تَنَزَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ

“Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake.”

Mujahid na wengine katika *Salaf* walisema; Aya hii ina maana, “(Rejea) Kitabu cha Allah تعالی na Sunnah za Mtume Wake ﷺ.”¹

Hii ni amri ya Allah تعالی, kwa chochote wanachotofautiana, kubwa au dogo katika dini, wanatakiwa kurejea Qur'an na Sunnah kwa utatuzi wa tofauti hizo.

Allah تعالی Amesema,

وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِنْ شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ

“Na mkikhitalifiana katika jambo lolote, basi hukumu yake iko kwa Mwenyezi Mungu...” (42:10)

Basi, Qur'an na Sunna ikiamua lolote na likashuhudia ukweli, basi huo ni ukweli mtupu. Na hakuna baada ya haki ila upotofu. Ndio sababu Allah تعالی Akasema,

إِنْ كُنْتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

“Ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”

Aya inathibitisha kuwa wale wasioyarejesha masuala yao kwenye Kitabu na Sunnah kwa utatuzi wa migogoro yao, hao hawamuamini Allah تعالی au Siku ya Mwisho. Allah تعالی Amesema,

ذَلِكَ خَيْرٌ

“Hayo ndiyo bora zaidi.”

Muradi wake, kurejea kwenye Kitabu cha Allah تعالی na Sunnah za Mjumbe wake kwa maamuzi kwa migogoro mbalimbali ni bora,

¹ At-Tabari 8:504.

وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

“Na ndiyo yenye mwisho mwema.”

Maana yake: “Ana mwisho mwema.” Kama walivyoelekeza Suddi na wengineo,¹ ambapo Mujahid alisema, “Ina malipo bora.”² Ni maana mbili zenye kukurubiana.

* * *

¹ At - Tabari 8:462.

² Ibn Abi Hatim 3:994.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ
 ءَامَنُوا بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ
 وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ
 يَتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ
 وَقَدْ أُمِرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ
 وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ
 ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿٥٩﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ
 تَعَالَوْا إِلَى مَا أَنْزَلَ اللَّهُ
 وَإِلَى الرَّسُولِ رَأَيْتَ الْمُنَافِقِينَ
 يَصُدُونَ عَنْكَ صُدُودًا
 ﴿٦٠﴾ فَكَيْفَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ
 مُصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ
 ثُمَّ جَاءُوكَ يَخْلِفُونَ بِاللَّهِ
 إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا إِحْسَانًا
 وَتَوْفِيقًا ﴿٦١﴾ أُولَئِكَ
 الَّذِينَ يَعْلَمُ اللَّهُ مَا فِي
 قُلُوبِهِمْ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ
 وَعِظْهُمْ وَقُلْ لَهُمْ فِي
 أَنْفُسِهِمْ قَوْلًا بَلِيغًا ﴿٦٢﴾
 وَمَا أَرْسَلْنَا
 مِنْ رَسُولٍ إِلَّا لِيُطَاعَ
 بِإِذْنِ اللَّهِ وَلَوْ أَنَّهُمْ
 إِذْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ
 جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ
 وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ
 لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّابًا رَحِيمًا ﴿٦٣﴾
 فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ
 حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِي مَا شَجَرَ
 بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي
 أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ
 وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٦٤﴾

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ
 ءَامَنُوا بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ
 قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَنْ يَتَحَاكَمُوا إِلَى
 الطَّاغُوتِ وَقَدْ أُمِرُوا أَنْ يَكْفُرُوا بِهِ
 وَيُرِيدُ الشَّيْطَانُ أَنْ يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا
 بَعِيدًا ﴿٥٩﴾ وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا
 إِلَى مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَإِلَى الرَّسُولِ رَأَيْتَ
 الْمُنَافِقِينَ يَصُدُونَ عَنْكَ صُدُودًا
 ﴿٦٠﴾ فَكَيْفَ إِذَا أَصَابَتْهُمُ مُصِيبَةٌ
 بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ ثُمَّ جَاءُوكَ
 يَخْلِفُونَ بِاللَّهِ إِنْ أَرَدْنَا إِلَّا إِحْسَانًا
 وَتَوْفِيقًا ﴿٦١﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ يَعْلَمُ
 اللَّهُ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ
 وَعِظْهُمْ وَقُلْ لَهُمْ فِي أَنْفُسِهِمْ قَوْلًا
 بَلِيغًا ﴿٦٢﴾

60. Huwaoni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako? Wanataka wakahukumwi kwa njia ya upotofu, na hali wameamrisha wakatae hayo! Na Shetani anataka kuwapotezelea mbali.

61. Na wanapoambiwa: Njooi kwenye yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, na njooi kwa Mtume; utawaona wanafiki wanajitenga mbali na wewe utengaji mkubwa.

62. Basi inakuwaje unapowapata msiba kwa sababu ya yale iliyo tanguliza mikono yao? Hapo tena hukujia wakiapa kwa Mwenyezi Mungu wakisema: Hatukutaka ila wema na mapatano.

63. Hao ndio wale ambao Mwenyezi Mungu Anayajua yaliyomo ndani ya nyoyo zao. Basi waachilie mbali, uwape mawaidha na uwaambie maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao.

Kutoyarejesha Masuala ya Dini Kwenye Qur'an na Sunnan kwa Utatuzi ni Sifa Bainifu za Makafiri:

Allah تعالی Amewakemea wale wanaodai kuamini yale Allah تعالی Aliyomteremshia Mjumbe wake ﷺ na kwa Mitume wake wa mwanzo, lakini waliyarejesha mighairi ya Kitabu cha Allah تعالی na Sunnah za Mjumbe wake ﷺ kwa utatuzi wa migogoro mbalimbali. Imeelezwa kuwa sababu za kuteremshwa Ayah hii ni kuwa kulikuwa na mgogoro kati ya mtu wa Ansar na Myahudi, na Myahudi akasema, "Tulipeleke suala hili kwa Muhammad ﷺ ili atuhukumu." Hata hivyo Muislamu alisema, "Tulipeleke kwa Ka'b bin Al-Ashraf (Myahudi) atuamulie." Aidha imeelezwa kuwa Aya iliteremshwa juu ya baadhi ya wanafiki ambao walijifanya Waislamu, hata hivyo walikhiyari kuhukumiwa na kanuni za Jahiliyah. Zipo sababu zaidi ya hayo, Aya ina maana ya jumla, kama inavyowakaripia wote wasiorejesha mambo yao kwenye Qur'an na Sunnah kwa utatuzi na wanapendelea hukumu ya yale wanayochagua katika batili, ambayo ina landana na sifa bainifu za *Twaghut*.

Kwa sababu hii Allah تعالی Amesema,

يُرِيدُونَ أَنْ يُتَحَاكَمُوا إِلَى الطَّاغُوتِ

"Wanataka wakahukumiwe kwa njia ya upotofu."

Mpaka mwisho wa Aya,

يَصُدُّونَ عَنْكَ صُدُودًا

"Wanakukwepa kwa upinzani."

¹ At-Tabari 8:506.

² At-Tabari 8:506.

Maana yake: Wanakuzuia kama wale waliotakabari. Kauli ya Allah تعالى kuhusu washirikina.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ اتَّبِعُوا مَا أَنْزَلَ اللَّهُ قَالُوا بَلْ نَتَّبِعُ مَا وَجَدْنَا عَلَيْهِ آبَاءَنَا

“Na wanapoambiwa: Fuateni aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, husema: Bali tunafuata tuliyowakuta nayo baba zetu.” (31:21)

Kinyume na mwendo wa waumini waaminifu, kama wanavyoelezwa na Allah,

إِنَّمَا كَانَ قَوْلَ الْمُؤْمِنِينَ إِذَا دُعُوا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ لِيَحْكُمَ بَيْنَهُمْ أَنْ يَقُولُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿٥١﴾

“Haiwi kauli ya Waumini wanapoitwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu baina yao, ila ni kusema: Tumesikia, na tumetii!” (24:51)

Karipio la Wanafiki:

Akiwakaripia Wanafiki, Allah تعالى Amesema,

فَكَيْفَ إِذَا أَصَابْتَهُمْ مُصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ

“Basi inakuwaje unapowasibu msiba kwa sababu ya yale iliyo tanguliza mikono yao?”

Maana yake: Itakuwaje wakihi kuwa wamelazimika kuungana nanyi kwa maafa yaliyowapata kutokana na madhambi yao, basi watawahitajia nyinyi.

ثُمَّ جَاءُوكَ سَخِفُونَ بِاللَّهِ إِنَّ أَرْضَنَا إِلَّا إِحْسَنًا وَتَوْفِيقًا

“Hapo tena hukujia wakiapa kwa Mwenyezi Mungu wakisema: Hatukutaka ila wema na mapatano.”

Wakiomba radhi na kuapa kuwa walitaka wema na mapatano walipokwenda kwa wenzao kutatuliwa mambo badala ya Mtume ﷺ na sio kuwa waliamini hukumu mbadala, kama wanavyodai.

Allah تعالى Anawaelezea hayo katika Kauli Yake,

فَتَرَى الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يُسْرِعُونَ فِيهِمْ يَقُولُونَ خَشِيَ

“Utawaona wale wenye maradhi nyoyoni mwao wanakimbilia kwao wakisema: Tunakhofu.” (5:52) Mpaka

فَيُضْجِعُوا عَلَىٰ مَا أَسْرُوا فِي أَنفُسِهِمْ تَلْمِيزِينَ ﴿٥٢﴾

“Wakawa wenye kujuta kwa waliyoyaficha katika nafsi zao.” (5:52)

At-Tabarani aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, ‘Abu Barzah Al-Aslami alikuwa kuhani ambaye aliwasuluhisha Mayahudi katika mizozo yao. Waislamu walipomuendea kutanzuliwa migogoro yao, Allah تعالى Aliteremsha,

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ ءَامَنُوا بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ

“Huwaoni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyo teremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako?” Mpaka,

إِن أَرَدْنَا إِلَّا إِحْسَانًا وَتَوْفِيقًا ﴿٥٣﴾

“Hatukutaka ila wema na mapatano.”¹

Kisha Allah تعالى Amesema,

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يَعْلَمُ اللَّهُ مَا فِي قُلُوبِهِمْ

“Hao ndio wale ambao Mwenyezi Mungu Anayajua yaliyomo ndani ya nyoyo zao.”

Hawa watu ni wanafiki, na Allah تعالى Anajua yaliyomo nyoyoni mwao na Atawaadhibu bila uonevu, kwani hakuna kinachokwepa uoni wa Allah تعالى. Hivyo Ewe Muhammad! Acha Allah تعالى Akutosheleze katika hili, kwani Ndiye Ajuaye ya dhahiri yao na yaliyojificha. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

فَأَعْرَضَ عَنْهُمْ

“Basi waachilie mbali.”Maana yake: Usiwaadhibu kwa sababu ya yaliyo mioyoni mwao.

وَعَظَّمَهُمْ

“..uwape mawaidha..”

¹ At-Tabari 11:373.

Maana yake: Washauri dhidi ya uovu na uovu uliomo ndani ya nafsi zao.”

وَقُلْ هُمْ فِي أَنْفُسِهِمْ قَوْلًا بَلِيغًا ﴿٦٤﴾

“Na uwaambie maneno ya kuathiri na kuingia katika nafsi zao.”

Washauri, kati yako na wao, ukitumia maneno yanayoathiri ambayo huenda yakawasaidia.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ رَسُولٍ إِلَّا لِيُطَاعَ بِإِذْنِ اللَّهِ ۗ وَلَوْ أَنْتُمْ إِذْ ظَلَمْتُمْ أَنْفُسَكُمْ جَاءَتْكُمْ
فَأَسْتَغْفِرُوا اللَّهَ ۗ وَأَسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا اللَّهَ تَوَّابًا رَحِيمًا ﴿٦٥﴾ فَلَا وَرَبِّكَ لَا
يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِي مَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ
وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٦٦﴾

64. Na hatukumtuma Mtume yeyote ila atiiwe kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu. Na lau pale walipojidhulumu nafsi zao wangeli kujia, wakamuomba Mwenyezi Mungu msamaha, na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangelimkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu.

65. La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayotoa, na wanyenyekee kabisa.”

Ulazima wa Kumtii Mtume ﷺ

Allah تعالی Amesema,

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ رَسُولٍ إِلَّا لِيُطَاعَ

“Na hatukumtuma Mtume yeyote ila atiiwe.” Maana yake: Kumtii Mtume ni faradhi kwa waliopewa Mtume na Allah تعالی. Kauli ya Allah تعالی.

بِإِذْنِ اللَّهِ

“Kwa Idhini ya Mwenyezi Mungu.” Mujahid ameeleza kuwa, maana yake, “Hapana atakayetii ila kwa Idhini Yangu.” Ayah hii inadhihirisha kuwa Mitume wanatiiwa kwa kuzingatia Kauli ya Allah تعالی. Allah تعالی Anasema,

وَلَقَدْ صَدَقَكُمُ اللَّهُ وَعْدَهُ إِذْ تَحُسُّونَهُم بِإِذْنِهِ^ط

“Allah kwa hakika Alitimiza ahadi Yake kwenu pindi mlipowaadhibu kwa Idhini Yake.”

Maana yake: Kwa Amri Yake, Sharia, Utashi na kwa sababu Aliwapa ushindi juu yao. Kauli ya Allah,

وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ

“Na lau pale walipojidhulumu nafsi zao.” Anawaeleza wako saji na watendao maovu, wanapopotoka na kufanya makosa waende kwa Mtume ﷺ ili wamuombe Mtume ﷺ awaombe msamaha kwa Allah تعالى. Wakifanya hivyo, Allah تعالى Atawasamehe na Kuwapa Rehema Zake na Msamaha. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

لَوْ جَدُوا اللَّهَ تَوَّابًا رَحِيمًا ﴿٥٩﴾

“Wangelimkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kupokea toba na Mwenye Kurehemu.”

Mtu Hatokuwa Muumini Mpaka Ayarejeshe Masuala Yake kwa Mtume ﷺ na Kufuata Amri Zake.

Allah تعالى Amesema,

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِي مَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ

“La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayokhitalifiana.”

Allah تعالى Anaapa kwa Utukufu Wake na Utakasifu Wake, kuwa hapana atakayefikia kiwango cha imani mpaka atakapoyarejesha mambo yote kwa ufumbuzi kwa Mtume ﷺ. Kwa hiyo, lolote atakalo amuru Mtume ﷺ, ni ukweli mtupu ambao unatakiwa kufuatwa kwa ndani na nje. Allah تعالى Amesema,

ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٦٠﴾

“Kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa.”

¹ At - Tabari 8:516.

Maana: Wafuate hukumu yake bila kutilia shaka uamuzi wako, na wakiri moyoni na nje uamuzi wa Mtume ﷺ kwa kujisalimisha bila kukanusha au kukadhibisha.

Bukhari aliandika kuwa Urwah رضي الله عنه alisema, "Zubayr رضي الله عنه aligombana na mtu kuhusu kijito walichokuwa wakikitumia wote pamoja kunywesha shamba. Mtume ﷺ akamuambia Zubayr,

«اسقِ يَا زُبَيْرُ! ثُمَّ أَرْسِلِ الْمَاءَ إِلَى جَارِكَ»

"Ewe Zubayr! Mwangilia, kisha peleka maji kwa jirani yako."

Ansari alikasirika na kusema, 'Ewe Mtume wa Allah! Ni kwa sababu ni binamu yako?, Kutokana na hilo, uso wa Mtume ﷺ ulibadilkika rangi (kwa ghadhabu) na akasema,

«اسقِ يَا زُبَيْرُ! ثُمَّ اخْبِسِ الْمَاءَ حَتَّى يَرْجِعَ إِلَى الْجَدْرِ، ثُمَّ أَرْسِلِ الْمَاءَ إِلَى جَارِكَ»

"Mwangilia ewe Zubayri, na zuia maji mpaka yafikie kuta, Kisha, peleka maji kwa jirani yako."

Hivyo, Mtume ﷺ alimpa Az-Zubayr رضي الله عنه haki zake kamili wakati Ansaar walipomkasirisha. Kabla ya hapo, Mtume ﷺ alitoa hukumu sahihi, inayomfaida Az-Zubayr رضي الله عنه na Ansar. Az-Zubayr رضي الله عنه akasema, 'Nadhani Ayah ifuatayo iliteremshwa juu ya kadhia hii,

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ

"La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana"¹

Sababu Nyingine:

Katika Tafsiri ya Al-Hafiz Abu Ishaq Ibrahim bin Abdur-Rahman bin Ibrahim bin Duhayam رحمه الله تعالى aliandika kuwa Damrah alisimulia kuwa watu wawili walipeleka mashauri yao kwa Mtume ﷺ na akahukumu kuwa mmoja kati yao ndiyo aliyekuwa na haki. Yule aliyeshindwa akasema, 'Sikubaliani na hukumu hii.' Yule mwenziwe akamueleza, "Unataka nini basi?" Akajibu, "Twende zetu

¹ Fat'hul Al-Bari 8:103.

kwa Abubakar As-Siddiq رضي الله عنه, walikwenda kwa Abubakar رضي الله عنه na yule aliyeshinda kesi akasema, "Tulikwenda kwa Mtume ﷺ atuamulie mgogoro wetu na aliamua kuwa mimi ndiye mwenye haki." Abubakar رضي الله عنه akasema, "Uamuzi ni ule alioutoa Mtume ﷺ." Yule aliyeshindwa shaurini akakataa tena hukumu na akanena, "Twende zetu kwa Umar Al-Khattab رضي الله عنه." Walipofika kwa Umar رضي الله عنه, yule aliyeshinda katika kadhia ile, akasema, "Tulipeleka tatizo letu kwa Mtume ﷺ, nami ndiye niliyeshinda, lakini huyu Bwana hakukubaliana na maamuzi." Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alimuuliza mtu wa pili alikiri yaliyosemwa, Umar رضي الله عنه alikwenda nyumbani kwake na akatoka ameinua juu upanga wake. Akamkata kichwa mtu aliyekataa hukumu ya Mtume ﷺ na akamuua. Kwa hiyo Allah تعالى Akateremsha,

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ

"La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini."

* * *

¹Ad - Durr Al-Manthur 2:322. Hadithi hii haina daraja *Sahih*. Damrah hakuwa Sahaba.

وَلَوْ أَنَّا كَتَبْنَا عَلَيْهِمْ أَنْ اقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ أَوْ اخْرَجُوا مِنْ دِيَارِكُمْ مَا فَعَلُوهُ إِلَّا قَلِيلٌ مِنْهُمْ ۗ وَلَوْ أَنَّهُمْ فَعَلُوا بِهِ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ وَأَشَدَّ تَنْبِيهًُا ﴿٦٦﴾ وَإِذَا لَأَتَيْنَهُمْ مِنْ لَدُنَّا أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٦٧﴾ وَلَهَدَيْنَهُمْ صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٦٨﴾ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصَّادِقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ ۗ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ﴿٦٩﴾ ذَلِكَ الْفَضْلُ مِنَ اللَّهِ ۗ وَكَفَى بِاللَّهِ عِلْمًا ﴿٧٠﴾ يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَخَذُوا حِذْرَكُمْ فَانفَرُوا ثَبَاتٍ أَوْ أَنْفَرُوا جَمِيعًا ﴿٧١﴾ وَإِنْ مِنْكُمْ مَنْ لَيُبَطِّلُنَّ فَإِنْ أَصَابَكُمْ مُصِيبَةٌ قَالْ قَدْ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْنَا إِذْ لَمْ أَكُنْ مَعَهُمْ شَهِيدًا ﴿٧٢﴾ وَلَئِنْ أَصَابَكُمْ فَضْلٌ مِنَ اللَّهِ لَيَقُولُنَّ كَأَنْ لَمْ نَكُنْ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُ مَوَدَّةٌ يَلْبِغُنِي كُنْتُ مَعَهُمْ فَأَفُورَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧٣﴾ * فَلْيَقْبَلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يَشْرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا بِالْآخِرَةِ ۗ وَمَنْ يُقْبَلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلْ أَوْ يَغْلِبْ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٧٤﴾

وَلَوْ أَنَّا كَتَبْنَا عَلَيْهِمْ أَنْ اقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ أَوْ اخْرَجُوا مِنْ دِيَارِكُمْ مَا فَعَلُوهُ إِلَّا قَلِيلٌ مِنْهُمْ ۗ وَلَوْ أَنَّهُمْ فَعَلُوا مَا يُوعَظُونَ بِهِ لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ وَأَشَدَّ تَنْبِيهًُا ﴿٦٦﴾ وَإِذَا لَأَتَيْنَهُمْ مِنْ لَدُنَّا أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٦٧﴾ وَلَهَدَيْنَهُمْ صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٦٨﴾ وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصَّادِقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ ۗ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ﴿٦٩﴾ ذَلِكَ الْفَضْلُ مِنَ اللَّهِ ۗ وَكَفَى بِاللَّهِ عِلْمًا ﴿٧٠﴾

66. Na lau kuwa Tumewa-amrisha: Jiueni, au tokeni majumbani kwenu, wasi-

ngelifanya hayo ila wachache tu miongoni mwao. Na lau kama wangelifanya waliowaidhiwa ingelikuwa bora kwao na uthibitisho wa nguvu zaidi.

67. Na hapo Tungewapa malipo makubwa kutoka kwetu.

68. Na Tungeliwaongoa njia iliyonyooka.

69. Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!

70. Hiyo ni Fadhila itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kutosha.

Watu Wengi Hukataa Wanayoamrisha

Allah تعالى Anaeleza kuwa hata kama watu wangeamrisha kufanya yale waliyozuiwa kufanya, wengi wao wasingeikubali amri hii, kwa kuwa hali yao ya uovu ni kukataa kutii amri. Allah تعالى Anayajua yote ambayo hayajatokea, na itakuwaje endapo na wakati litakapothubutu.

Kwa sababu hii Allah تعالى Alisema,

وَلَوْ أَنَّا كَتَبْنَا عَلَيْهِمْ أَنْ اقْتُلُوا أَنْفُسَكُمْ

“Na lau kuwa Tumewaamrisha: Jiueni...”

Mpaka mwisho wa aya,

وَلَوْ أَنَّهُمْ فَعَلُوا مَا يُوعَظُونَ بِهِ.

“Na lau kama wangelifanya waliowaidhiwa.”

Muradi wake ni kuwa, kama wangelifanya waliyoamrisha, na wakajiepusha na yale waliyokatazwa,

لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ

“Ingelikuwa bora kwao...” kuliko kuasi na kufanya yaliyokatazwa,

وَأَشَدَّ تَثِيْبًا ﴿٦٦﴾

“Na uthibitisho wa nguvu zaidi.” Tasdiq yenye nguvu, kwa mujibu wa As-Suddi.

وَإِذَا لَأَتَيْنَهُمْ مِنْ لَدُنَّا

“Na hapo Tungewapa kutoka Kwetu.” Kutoka kwetu.

أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٦٧﴾

“Malipo makubwa.” Pepo.

وَلَهْدٍ يَنْهَاهُمْ صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿٦٨﴾

“Na Tungeliwaongoa njia iliyonyooka.” Hapa duniani na kesho Akhera.

Yeyote Atakayemtii Allah تعالى na Mjumbe wake ﷺ Atakuwa Pamoja na Waliokirimiwa Mbele ya Allah تعالى.

Kisha Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصَّادِقِينَ
وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ﴿٦٦﴾

“Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema.”

Hivyo, yeyote anayetekeleza yale aliyoyaamuru Allah تعالى na Mtume ﷺ na kujiepusha na yale yaliyokatazwa na Allah تعالى na Mtume ﷺ basi Allah تعالى Atamhakikishia makazi katika Nyumba Tukufu. Hapa Atamuweka pamoja na Mitume, na wale wenye daraja la *Siddiqiin* kisha mashahidi na kisha watu wema, ambao ni wema moyoni na katika matendo yao. Allah تعالى Amelisifu kundi hili,

وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ﴿٦٦﴾

“Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!”

Bukhari aliandika kuwa Aishah رضي الله عنها alisema, “Nilimsikia Mtume ﷺ akisema,

«مَا مِنْ نَبِيٍّ يَمْرُضُ إِلَّا خَيْرٌ بَيْنَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ»

“Kila Mtume anayepatwa na maradhi hukhiyarishwa baina ya maisha ya dunia na Akhera.”

Wakati Mtume ﷺ alipougua na kufuatwa na kifo chake, sauti yake ilikuwa dhaifu na nilimsikia akisema,

مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصَّادِقِينَ وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ

“Hao wa pamoja na wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema.”

Nikajua kuwa alipewa uchaguzi.”¹ Muslim aliandika Hadithi hii.²

Hadithi hii inaelezea maana ya Hadithi nyingine; Mtume ﷺ alisema kabla ya kufariki dunia:

«اللَّهُمَّ [فِي] الرَّفِيقِ الْأَعْلَى»

“Ewe Allah! Niwe katika rafiki wa juu.” Mara tatu kisha akakata roho, Rehema za Allah ziwe juu yake.³

Sababu za Kuteremshwa Aya hii Tukufu

Ibn Jarir رحمه الله تعالى amemnuuu Said bin Jubayr رضي الله عنه akisema, “Mtu katika Ansar alikuja kwa Mtume ﷺ akisononeka, Mtume ﷺ akamuuliza, “Mbona nakuona una huzuni?” Akajibu, ‘Ewe Mtume wa Allah! Nilikuwa natafakari jambo.” Mtume ﷺ akasema, “Ni jambo gani hilo?”, akasema, ‘Tunakuja kwako mchana na usiku, tunakuangalia na kukaa pembeni yako. Kisha utafufuliwa na Mitume, nasi hatutakuona. Mtume ﷺ hakusema kitu, Jibril عليه السلام alishuka na Aya hii.

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ

“Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii.”

Na Mtume ﷺ akampelekea Khabari njema yule mtu wa Ansari.⁴ Hadithi hii ni *Mursa*⁵ kutoka kwa Masruq, Ikrimah, Amir Ash-shabi, Qatadah na Ar-Rabi bin Anas. Haya ni masimulizi yenye isnadi iliyo bora. Abubakar bin Marduwyah aliandika na isnadi tofauti kutoka kwa Aishah رضي الله عنها, ambaye alisema, “Mtu alikuja kwa Mtume ﷺ akamuambia, “Ewe Mjumbe wa Allah! Nakupenda kuliko niipendavyo nafsi yangu, familia yangu na watoto wangu. Baadhi ya wakati niwapo nyumbani, nakukumbuka, na sisubiri mpaka nije kukuangalia

¹ *Fat’hul Al-Bari* 8:103.

² Muslim 4:1893.

³ Muslim 4:1894.

⁴ At - Tabari 8:534.

⁵ Isnadi yake haina jina la Sahaba aliyeipokea.

ninapotafakari kuhusu kifo changu na chako. Najua kuwa utakuwa na Mitume utakapoingia Peponi. Najua kuwa sitakuona nitakapoingia Peponi.' Mtume ﷺ hakumjibu mpaka Aya hii ilipotemshwa kwake,

وَمَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَأُولَئِكَ مَعَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ
وَالشُّهَدَاءِ وَالصَّالِحِينَ وَحَسُنَ أُولَئِكَ رَفِيقًا ﴿٦٦﴾

“Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wako pamoja na wale Aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema.”

Hadithi hii ilikusanywa na Al-Hafiz Abu Abdullah Al-Maqdisi رحمه الله تعالى ndani ya Kitabu chake, *Sifat Al-Jannah*, kisha akasema, “Sioni tatizo na isnadi yake.”¹ Na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi. Muslim aliandika kuwa Rabiah bin Ka’b Al-Aslami رضي الله عنه alisema, “Nilikuwa nalala kwenye nyumba ya Mtume ﷺ nikimletea maji ya kutawadhia na mahitajio mengine. Wakati mmoja aliniambia, ‘Niombe’ Nikamuambia, ‘Ewe Mjumbe wa Allah! Ninaomba niwe nawe Peponi.’ Akasema, ‘Jingine isipokuwa hili?’ Nikasema, ‘Hili tu.’ Akasema,

«فَأَعِنِّي عَلَى نَفْسِكَ بِكَثْرَةِ السُّجُودِ»

“Basi nisaidie, kwa kukithirisha sijida.”²

Imam Ahmad aliandika kuwa Amri bin Murrah Al-Juhani رضي الله عنه alisema, “Mtu alimjia Mtume ﷺ na akasema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Naapa kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى na kuwa wewe ni Mtume ﷺ, ninasali Sala tano na kutoa Zakah ya mali na kufunga mwezi wa Ramadhani.”

Mtume ﷺ akasema,

«مَنْ مَاتَ عَلَى هَذَا كَانَ مَعَ النَّبِيِّينَ وَالصِّدِّيقِينَ وَالشُّهَدَاءِ يَسُومَ الْفِيَامَةَ، مَكْدَا
-وَنُصَبَ أَصْبَعَيْهِ - مَا لَمْ يَغْرَقْ وَالِدَيْهِ»

¹ At - Tabarani Katika As-Saghir 3308, Al-Hilyah 8:125. Hadithi hii ni sahihi na inaipa nguvu hadithi iliyopita.

² Muslim 489.

“Atakaye kufa katika hali hii, atakuwa na Mitume, aliowaneemesha Allah, na Mashahidi siku ya Kiyama – hivi na akainua kidole chake – muda wa kuwa hawaasi wazazi wake.”¹ Ameipokea Ahmad pekee.

Habari kubwa kuliko hizi zimo katika Hadithi sahihi iliyomo ndani ya *Sahih* na *Musnad*, katika daraja ya *Mutawatir*, iliyosimuliwa na Masahaba wengi wa Mtume ﷺ. Mtume ﷺ aliulizwa juu ya mtu anayewapenda watu, lakini hadhi yake si sawa na yao.

Mtume ﷺ alisema,

«الْمَرْءُ مَعَ مَنْ أَحَبَّ»

“Mtu atakuwa na wale awapendao.”²

Anas رضي الله عنه alisema yafuatayo: “Waislamu waliifurahia sana Hadithi hii.” Katika riwaya nyingine, Anas رضي الله عنه alisema, “Nampenda Mtume ﷺ, Abubakar رضي الله عنه na Umar رضي الله عنه na nataraji Kuwa Allah تعالى Atanifufua pamoja nao, japokuwa sikufanya amali kama zao.”³

Allah تعالى Amesema,

ذَلِكَ أَلْفَضْلُ مِنِّي أَللَّهُ

“Hiyo ni Fadhila itokayo kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Itokayo kwa Allah تعالى kwa Fadhila Zake, kwani Yeye Ndiye Aliyewafadhili na sio amali zao.

وَكَفَى بِاللَّهِ عَلِيمًا

“ Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa Kutosha.”

Anawajua wanaostahili muongozo na ubainifu.

¹ *Jami' Al-Masanid was – Sunan* 10:77.

² Bukhari Na.6168, Muslim 1:90.

³ *Fat'hul Al-Bari* 7:51.

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا خُذُوا حِذْرَكُمْ فَانفِرُوا ثُبَاتٍ أَوْ اَنْفِرُوا جَمِيعًا ﴿٦٦﴾ وَإِنَّ مِنْكُمْ لَمَنْ لَيُبَطِّئَنَّ فَإِنْ أَصَابْتُمْ مِصْبَبًا قَالَ قَدْ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيَّ إِذْ لَمْ أَكُنْ مَعَهُمْ شَهِيدًا ﴿٦٧﴾
 وَلَئِنْ أَصَابَكُمْ فَضْلٌ مِّنَ اللَّهِ لَيَقُولَنَّ كَأَنْ لَّمْ تَكُنْ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُ مَوَدَّةٌ يَلْبِغْتَنِي كُتُّ مَعَهُمْ
 فَأَفُوزَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٦٨﴾ * فَلْيُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يَشْرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا
 بِالْآخِرَةِ ۗ وَمَنْ يُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلْ أَوْ يَغْلِبْ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٦٩﴾

71. Enyi mliaoamini! Chukueni hadhari yenu! Tokeni katika jihadi kwa makundi au mkiwa mbalimbali au tokeni nyote pamoja!

72. Na wapo katika nyinyi wanaokaa nyuma (wasende vitani, na huwakataza wenziwao wasende vitani). Na kama unakupateni msiba (kila mmoja) husema: Mwenyezi Mungu Amenineemesha ilivyokuwa sikuhudhuria pamoja nao.

73. Na ikikufikieni Fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu husema - kama kwamba hapakuwa mapenzi baina yenu naye: Laiti ningeli kuwa pamoja nao nikafanikiwa mafanikio makubwa.

74. Basi nawapigane katika njia ya Mwenyezi Mungu wale ambao wanaouza uhai wa dunia kwa Akhera. Na anayepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha akauliwa au akashinda basi Tutakuja mpa ujira mkubwa.¹

¹ Kuna rai tofauti katika Kauli Yake, "Wale ambao wanaouza uhai wa dunia kwa Akhera." inaweza kuwa na maana, "waliuza maisha ya dunia kwa maisha ya Akhera". au "walinunua maisha ya dunia kwa gharama ya maisha ya Akhera." Kwa hiyo ni amri kwa wenye imani ya kupigana, au amri kwa wenye mioyo iliyojaa imani, ambao wamenukuliwa katika Ayah iliyotangulia, kupigana kwa imani, sio kwa malipo ya kidunia. Watoa maoni wengi wameiona kama ilivyo katika mfano wa kwanza.

Umuhimu wa Kuchukua Tahadhari Dhidi ya Adui:

Allah تعالی Amewaamuru waja wake wema kuchukua tahadhari dhidi ya maadui zao, kwa kujiandaa na zana muhimu na mahitajio mengine, na kuongeza idadi ya vikosi kwa kupigana katika njia Yake.

ثُبَاتٍ

“Kwa vikosi.”

Ina maana, kikundi baada ya kikundi, kikosi baada ya kikosi, na msafara baada ya msafara. Ali binTalhan amemnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa,

فَأَنْفِرُوا ثُبَاتٍ

“Na mtoke kwa vikosi”,

Muradi wake, “kwa vikundi, vikosi baada ya vikosi vilivyotengana.”

أَوْ أَنْفِرُوا جَمِيعًا

“Au tokeni nyote pamoja!”

Maana yake: “Nyote pamoja.”² Hadithi sawa na hiyo, ilipokelewa kutoka kwa Majahid, Ikrimah, As-Suddi, Qatadah, Adh-Dhahaak, Ata Al-Khurasani, Muqatil bin Hayyan na Khusayf Al-Jizry.³

Kukataa Kujiunga na Jihad ni Dalili ya Unafiki:

Allah تعالی Amesema,

وَإِنَّ مِنْكُمْ لَمَنْ لَيُبْتَغِيَنَّ

“Na yupo kati yenu anayebakia nyuma.”

Mujahid na wengineo wamesema kuwa Ayah hii ilishushwa juu ya wanafiki.⁴ Muqatil bin Hayyan alisema kuwa,

¹ At – Tabari 8:537.

² At – Tabari 8:537 – 538.

⁴ At - Tabari 8:538.

لَيْبَطِينَ

"Anayebakia nyuma."

Maana yake: Anayebaki nyuma na hajiungi na Jihad. Pia inawezekana mtu huyo anabaki nyuma, wakati akiwashawishi wengine wasijiunge na Jihad. Kwa mfano, Abdullah bin Ubayy bin Salul, Allah تعالى Amlaani, alikuwa akibaki nyuma na akiwashawishi wengine wafanye kama yeye na wasijiunge na Jihad, kama walivyoeleza Ibn Jurayj رحمه الله تعالى na Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Kwa sababu hii Allah تعالى Alisema juu ya wanafiki, kuwa anapochelewa na kutojiunga na Jihad, Husema:

فَإِنْ أَصَبْتُمْ مُصِيبَةً

"..Na kama unakupateni msiba (kila mmoja) ..."

Maana yake: Kifo, ushahidi, au – kwa hikima ya Allah تعالى – kwa kushindwa na adui.

قَالَ قَدْ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيَّ إِذْ لَمْ أَكُنْ مَعَهُمْ شَهِيدًا ﴿٧٦﴾

"Husema: Allah Amenineemesha ilivyokuwa sikuhudhuria pamoja nao."

Maana yake: Maadam sikujiunga nao vitani. Kwa sababu anaiona hii ni moja ya fadhila za Allah تعالى kwake, bila kujua malipo ambayo angaliyapata kwa kuvumilia vita au kufa shahidi kama angeliuawa.

وَلَيْنَ أَصَابَكُمْ فَضْلٌ مِّنَ اللَّهِ

"Na ikikufikieni Fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu."

Kama vile ushindi na ngawira,

لَيَقُولَنَّ كَأَن لَّمْ تَكُنْ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُ مَوَدَّةٌ

"Husema - kama kwamba hapakuwa mapenzi baina yenu naye."

Maana yake: Kama kwamba hakuwa mfuasi wa Dini yako,

يَلِيَّتَنِي كُنْتُ مَعَهُمْ فَأَفُوزَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧٧﴾

"Laiti ningelikuwa pamoja nao nikafanikiwa mafanikio makubwa."

Kwa kugaiwa hisa katika ngawira na kumiliki hisa hiyo. Hili ndilo lengo lake kuu.

Uhamasishaji Kushiriki katika Jihad:

Kisha Allah تعالى Amesema,

﴿ فَلْيُقَاتِلْ ﴾

“Basi na wapigane.” Maana yake: Waumini.

﴿ فِي سَبِيلِ اللَّهِ الَّذِينَ يَشْرُونَ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا بِالْآخِرَةِ ۗ ﴾

“Katika njia ya Mwenyezi Mungu wale ambao wanao uza uhai wa dunia kwa Akhera.”

Maana yake: Wanauza Dini yao kwa thamani ndogo ya dunia, hii inatokana na ukafiri na kutokuwa na imani. Kisha Kauli ya Allah,

﴿ وَمَنْ يُقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَيُقْتَلْ أَوْ يَغْلِبْ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴾

“Na anayepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha akauliwa au akashinda basi Tutakuja mpa ujira mkubwa.”

Maana yake: Yeyote anayepigana kwa ajili ya Allah تعالى, ima alikuwa ameuawa au ameshinda, atapata malipo makubwa kutoka kwa Allah تعالى. Kama ilivyothibiti katika Sahihi Mbili,

﴿ وَتَكَفَّلَ اللَّهُ لِلْمُجَاهِدِ فِي سَبِيلِهِ، إِنْ تَوَفَّاهُ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ، أَوْ يُرْجِعَهُ إِلَى مَسْكَنِهِ الَّذِي خَرَجَ مِنْهُ، بِمَا نَالَ مِنْ أَجْرٍ أَوْ غَنِيمَةٍ ﴾

“Allah تعالى Amemdhaminia Mujahid katika njia yake, Akimfisha Atamuingiza Peponi; au Atamrudisha nyumbani kwake salama pamoja na zawadi au ngawira iliyopatikana.”¹

* * *

¹ Fat'hul Al-Bari 6:253, na Muslim 3:1496.

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ
 الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ
 هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أهلكها وَاجْعَل لَنَا مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا
 وَاجْعَل لَنَا مِنْ لَدُنْكَ نَصِيرًا ﴿٧٥﴾ الَّذِينَ ءَامَنُوا يُقَاتِلُونَ
 فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ الطَّاغُوتِ
 فَقَاتِلُوا أَوْلِيَاءَ الشَّيْطَانِ إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا ﴿٧٦﴾
 أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ قِيلَ لَهُمْ كُفُّوا أَيْدِيَكُمْ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ
 وَآتُوا الزَّكَاةَ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ إِذَا فَرِيقٌ مِنْهُمْ
 يَخْشَوْنَ النَّاسَ كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً وَقَالُوا رَبَّنَا لِمَ
 كَتَبْتَ عَلَيْنَا الْقِتَالَ لَوْلَا أَخَّرْتَنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ قُلْ مَتَّعَ
 الدُّنْيَا قَلِيلًا وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِمَنِ اتَّقَىٰ وَلَا تُظَلَمُونَ فَتِيلًا
 ﴿٧٧﴾ أَيْنَمَا تَكُونُوا يُدْرِككُمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ
 مُّشِيدَةٍ وَإِنْ تُصِبْهُمْ حَسَنَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ
 وَإِنْ تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِكَ قُلْ كُلٌّ مِنْ
 عِنْدِ اللَّهِ فَمَالِ هَتُّولَاءِ الْقَوْمِ لَا يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ حَدِيثًا
 ﴿٧٨﴾ مَا أَصَابَكَ مِنْ حَسَنَةٍ فَمِنَ اللَّهِ وَمَا أَصَابَكَ مِنْ
 سَيِّئَةٍ فَمِنَ نَفْسِكَ وَأَرْسَلْنَاكَ لِلنَّاسِ رَسُولًا وَكَفَىٰ بِاللَّهِ
 شَهِيدًا ﴿٧٩﴾

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ
 وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ
 وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا
 أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ
 أهلكها وَاجْعَل لَنَا مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا
 وَاجْعَل لَنَا مِنْ لَدُنْكَ نَصِيرًا ﴿٧٥﴾
 الَّذِينَ ءَامَنُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ
 وَالَّذِينَ كَفَرُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ
 الطَّاغُوتِ فَقَاتِلُوا أَوْلِيَاءَ الشَّيْطَانِ
 إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا ﴿٧٦﴾

75. Na mna nini msipigane katika njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanaoonewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anayetoka Kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anayetoka Kwako.

76. Walioamini wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, na waliokufuru wanapigana katika njia ya upotofu. Basi piganeni na marafiki wa Shet'ani. Hakika hila za Shetani ni dhaifu.

Kuhimiza Jihad Ili Kuwatetea Wanyonge

Allah تعالى Amewahimiza Waja wake Watiifu kupigana Jihad katika njia Yake na kujitahidi kuwaokoa Waislamu waliokandamizwa Makkah, wanaume, wanawake na watoto ambao hawakuwa na utulivu kwa sababu walikuwa wamebaki pale. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ

“Ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu.”

Ikiashiria Makkah, katika Aya kama hii, Allah تعالى Amesema,

وَكَايِنٍ مِّن قَرْيَةٍ هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِّن قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجْتكَ

“Ni miji mingapi ina nguvu kali kuliko mji wako ambao Tumekutoa.”

(47:13) Kisha Allah تعالى Anaelezea mji huu,

الظَّالِمِ أَهْلِهَا وَأَجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ وَلِيًّا وَأَجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ نَصِيرًا ﴿٧٥﴾

“Ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anayetoka Kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anayetoka Kwako.”

Maana yake: Tuletee walinzi na wasaidizi. Bukhari amemnukuu Ibn Abbas رضي الله عنهما akisema, “Mimi na mama yangu tulikuwa miongoni mwa waliokandamizwa (Makkah).”¹ Kisha Allah تعالى Akasema,

الَّذِينَ آمَنُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ كَفَرُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ الطَّاغُوتِ

“Walioamini wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, na waliokufuru wanapigana katika njia ya upotofu.”

Kwa hiyo, waumini wanapigana kwa kumtii Allah تعالى na kupata radhi Zake, ambapo makafiri wanapigana kumtii shetani. Kisha Allah تعالى Anawahimiza waumini kuwapiga maadui Zake.

فَقَاتِلُوا أَوْلِيَاءَ الشَّيْطَانِ إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا ﴿٧٦﴾

“Basi piganeni na marafiki wa Shetani. Hakika hila za Shetani ni dhaifu.”

¹ Fat’hul Al-Bari 8:103.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ قِيلَ لَهُمْ كُفُّوا أَيْدِيَكُمْ وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ فَلَمَّا كُتِبَ عَلَيْهِمُ
 الْقِتَالُ إِذَا فَرِيقٌ مِنْهُمْ مَخْشَوْنَ النَّاسَ كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً ۚ وَقَالُوا رَبَّنَا لِمَ كَتَبْتَ
 عَلَيْنَا الْقِتَالَ لَوْلَا أَخَّرْتَنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ ۗ قُلْ مَتَّعْتُ الدُّنْيَا قَلِيلًا وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِّمَنِ اتَّقَىٰ
 وَلَا تُظَلِّمُونَ فَتِيلًا ﴿٧٥﴾ أَيِنَّمَا تَكُونُوا يُدْرِكُكُمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشِيدَةٍ ۗ وَإِن
 تُصِبْهُمْ حَسَنَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ ۗ وَإِن تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِكَ
 ۗ قُلْ كُلٌّ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ ۗ فَمَالِ هَتُّؤُلَاءِ الْقَوْمِ لَا يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ حَدِيثًا ﴿٧٦﴾ مَا أَصَابَكَ
 مِنْ حَسَنَةٍ فَمِنَ اللَّهِ ۗ وَمَا أَصَابَكَ مِنْ سَيِّئَةٍ فَمِنَ نَفْسِكَ ۗ وَأَرْسَلْنَاكَ لِلنَّاسِ رَسُولًا ۗ
 وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٧٧﴾

77. Je, huwaoni wale walioambiwa: Izuieni mikono yenu, na simamisheni Sala na mtoe Zaka. Na walipoamrisha kupigana, mara kundi moja kati yao liliwaogopa watu kama kumwogopa Mwenyezi Mungu, au kwa khofu kubwa zaidi. Na wakasema: Mola Mlezi wetu! Kwa nini umetuamrisha kupigana? Laiti ungetuakhirishia kiasi ya muda kidogo hivi! Sema: Starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa mwenye kumchamungu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi wa kokwa ya tende.

78. Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu. Na likiwafikia jema wanasema: Hili limetoka kwa Mwenyezi Mungu. Na likiwafikia ovu wanasema: Hili limetoka kwako wewe. Sema: Yote yanatoka kwa Mwenyezi Mungu. Basi wana nini watu hawa hata hawakaribii kufahamu maneno?.

79. Jema liliokufikia limetokana na Mwenyezi Mungu. Na ovu lililo kusibu linatokana na nafsi yako. Nasi Tumekutuma kwa watu uwe ni Mtume. Na Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kutosha.

Kulaumiwa Waliopenda Kucheleweshwa Amri ya Jihad kwa Wale Waliokuwa Wanataka.

Mwanzoni mwa Uislamu, Waislamu waliokuwepo Makkah waliamrisha kuswali na kutoa Zakah/Sadaka sio ile iliyofikia *nisaab*, ili kuwafariji masikini katika wao. Aidha waliamrisha usamehevu na uvumilivu kwa mushirikina na kusubiri wakati ule. Hata hivyo, walitamani kuruhusiwa kupigana nao ili wawaadhibu adui zao. Hali ya wakati ule haikuruhusu vita kwa sababu nyingi. Mfano, Waislamu walikuwa wachache, wakilinganishwa na wingi wa maadui. Jiji la Waislamu lilikuwa mahali patakatifu na eneo tukufu juu ya ardhi, sababu hii ndio maana amri ya kupigana haikuteremshwa Makkah. Baadaye Waislamu walipodhibiti mji wao Madinah, wakawa na nguvu, uwezo na usaidizi, ndipo Jihad ilipofaradhiwa. Hata hivyo, amri ya Jihad ilipoteremshwa, kama waislamu walivyotaka, baadhi yao waliingiwa na wasiwasi na kujawa na woga wa kukabiliana na mushirikina katika medani ya vita.

وَقَالُوا رَبَّنَا لِمَ كَتَبْتَ عَلَيْنَا الْقِتَالَ لَوْلَا أَخَّرْتَنَا إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ

“Na wakasema: Mola Mlezi wetu! Kwa nini Umetuamrisha kupigana? Laiti Ungetuakhirishia kiasi ya muda kidogo hivi!”

Maana yake: Tunatamani lau Jihad ingeliakhirishwa mpaka baadaye kwa sababu ina maana ya kumwaga damu, kupatikana kwa mayatima na wajane. Katika Aya sawa na hiyo Allah تعالى Amesema,

وَيَقُولُ الَّذِينَ ءَامَنُوا لَوْلَا نُزِّلَتْ سُورَةٌ ۖ فَإِذَا نُزِّلَتْ سُورَةٌ مُحْكَمَةٌ وَذُكِرَ فِيهَا الْقِتَالُ

“Na waumini wanasema: Kwa nini haiteremshwi Sura? Na inapoteremshwa sura madhubuti na ikatajwa ndani yake khabari ya vita...” (47:20)

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى aliandika kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Abdur Rahman bin Awf رضي الله عنه na wafuasi wake kadha walikwenda kwa Mtume ﷺ alipokuwa Makkah na akasema, ‘Ewe Mtume wa Allah! Tulikuwa na nguvu tulipokuwa washirikina, lakini tuliposilimu, tukadhoofika.’ Mtume ﷺ akasema,

«إِنِّي أُمِرْتُ بِالْعَفْوِ فَلَا تُقَاتِلُوا الْقَوْمَ»

“Niliteremshwa kuwasamehe watu, hivyo msiwapige.”

Allah تعالى Alipomhamisha Mtume ﷺ Madinah, Alimuamuru kupigana, lakini baadhi ya Watu walirudi nyuma. Hivyo Allah تعالى Akateremsha ayah.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ قِيلَ لَهُمْ كُفُّوا أَيْدِيَكُمْ

“Je, huwaoni wale walioambiwa: Izuieni mikono yenu.”

Hadithi hii ilikusanywa na An-Nasai na Al-Hakim.¹ Kauli ya Allah تعالى,

قُلْ مَتَّعَ الدُّنْيَا قَلِيلٌ وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِمَنِ اتَّقَى

“Sema: Starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa mwenye kumchamungu.”

Maana yake: Makazi ya yule mwenye Taqwa ni bora kuliko maisha ya dunia.

وَلَا تُظَلِّمُونَ فَتِيلاً

“Wala hamtadhulumiwa hata uzi wa kokwa ya tende.”

Kwa amali zake njema. Bali, mtalipwa kikamilifu kwa amali zenu. Ahadi hii inawaelekeza mbali na maisha ya dunia na kuwafanya wawe na hamu na Akhera, wakati huo huo wakihimizwa kupigana Jihad.

Kifo Hakikwepeki.

Allah تعالى Amesema,

أَيُّنَمَا تَكُونُوا يُدْرِكَكُمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشِيدَةٍ

“Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu.”

¹ At – Tabari 8:549.

Maana yake: Kwa hakika mtakufa na hapana atakayeweza kuepa kifo. Allah تعالى Amesema,

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾

“Kila kilichopo juu yake kitatoweka.” (55:26)

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ ۗ

“Kila nafsi itaonja umauti..” (3:185)

وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّن قَبْلِكَ الْخُلْدَ ۗ

“...Na hatukumfanya mtu yeyote kabla yako kuishi milele.” (21:34)

Kwa hiyo kila nafsi itaonja kifo na hapana kitakachomuokoa mtu na kifo, ima alipigana Jihad au hakupigana kila mmoja ana wakati wake, na kipindi cha maisha chenye ukomo.

Katika maradhi yaliyofuatiwa na kifo chake, Khalid bin Al-Walid رضي الله عنه alisema akiwa Kitandani, “Nilishiriki katika vita kadha wa kadha, na kila sehemu ya mwili wangu ilipata majeraha kwa kupigwa au kuchomwa. Hata hivyo bado niko hai, nafia kitandani mwangu! Macho ya woga yasionje lepe la usingizi.” Kauli ya Allah تعالى,

وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشِيدَةٍ

“Na hatamkiwa katika ngome zilizo na nguvu.”

Maana yake: Zilizofanywa madhubuti, ngome zilizoimarishwa, zilizokwenda juu hapana hadhari au ngome itakayo zuia kifo.

¹ An-Nasai katika Al-Kubra 6:325 na Al-Hakim 2:307.

Wanafiki Walihisi Ndege Mbaya (Nuks) kwa Sababu ya Mtume ﷺ

Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ تُصِيبُهُمْ حَسَنَةٌ

“Na likiwafikilia jema.”

Maana yake: Miaka yenye neema; matunda mengi, mazao, watoto n.k. kama ilivyosemwa na Ibn Abban, Abu Al-Aliyah na As-Suddi.

يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ وَإِنْ تُصِيبُهُمْ سَيِّئَةٌ

“Wanasema: Hili limetoka kwa Mwenyezi Mungu. Na likiwafikilia ovu.”

Ukame, njaa, uhaba wa matunda na vyakula, vinavyowasibu watoto wao au wanyama, n.k. kama alivyosema Abu Al-Aliyah na As-Suddi,

يَقُولُوا هَذِهِ مِنْ عِنْدِكَ

“Wanasema: Hili limetoka kwako wewe.”

Maana yake: Kwa sababu yako na kuwa tulikufuata na tukaingia kwenye Dini yako. Allah تعالى Aliwazungumzia Watu wa Fir'awn,

فَإِذَا جَاءَتْهُمْ الْحَسَنَةُ قَالُوا لَنَا هَذِهِ وَإِنْ تُصِيبُهُمْ سَيِّئَةٌ يَطَّيَّرُوا بِمُوسَىٰ وَمَنْ مَعَهُ

“Likiwafika jema wakisema: Haya ni haki yetu. Na likiwafika ovu husema: Musa na walio pamoja naye ni wakorofi.” (7:131)

Allah تعالى Amesema,

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ

“Na katika watu wapo wanaomuabudu Mwenyezi Mungu kwa ukingoni.” (22:11)

Kauli sawa na hiyo ilitamkwa na wanafiki, ambao walisilimu kwa nje, lakini waliuchukia Uislamu katika nyoyo zao. Kwa sababu hii, walipofikwa na maafa waliyanasibisha na kumfuata Mtume ﷺ.

Kutokana na hayo Allah تعالی Aliteremsha,

قُلْ كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ

“Sema: Yote yanatokana na Mwenyezi Mungu.”

Kauli ya Allah تعالی kuwa vitu vyote vinatoka Kwake, maana yake, kila kitu kinatokea kwa Uamuzi na Amri ya Allah تعالی, na Uamuzi Wake ni kwa wote; wema na waovu, waumini na makafiri. Kisha Allah تعالی Alisema Akimkusudia Mtume wake ﷺ, na binadamu wote,

مَا أَصَابَكَ مِنْ حَسَنَةٍ فَمِنَ اللَّهِ

“Jema liliokufikia limetokana na Mwenyezi Mungu.”

Muradi wake, Neema za Allah تعالی, Rehema na Huruma Zake.

وَمَا أَصَابَكَ مِنْ سَيِّئَةٍ فَمِنَ نَفْسِكَ

“Na ovu liliokusibu linatokana na nafsi yako.”

Maana: Kwa sababu yako na kutokana na vitendo vyako. Vivyo hivyo Allah تعالی Amesema,

وَمَا أَصَابَكُمْ مِّنْ مُّصِيبَةٍ فَمِمَّا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ وَيَعْفُوا عَنْ كَثِيرٍ ﴿٤٢﴾

“Na misiba inayokusibuni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu. Naye Anasamehe mengi.” (42:30)

As-Suddi, Al-Hasan Al-Basri, Ibn Jurayj na Ibn Zayd walisema kuwa,

فَمِنَ نَفْسِكَ

“Limetoka kwako wewe.”

Maana, sababu ya makosa yako. Qatadah alisema,

فَمِنَ نَفْسِكَ

“Limetoka kwako wewe.”

Maana, kama adhabu kwako, Ewe mwana wa Adam, kwa sababu ya dhambi zako. Allah تعالی Amesema,

وَأَرْسَلْنَاكَ لِلنَّاسِ رَسُولًا

“Nasi Tumekutuma kwa watu uwe ni Mtume.”

Ili uwafikishie Amri za Allah تعالى, Anayotaka, Asiyoyataka, Anayoyakubali na Ayakataayo.

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٧٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kutosha.”

Kuwa Amekutuma. Aidha ni Shahidi juu yenu na wao, Anafhamu yale mnayoyafikisha kwao na ukanushaji na uasi dhidi ya ukweli.

* * *

مَّن يُطِيعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ ۗ وَمَنْ تَوَلَّىٰ فَمَا أَرْسَلْنَاكَ
 عَلَيْهِمْ حَفِيظًا ۗ وَيَقُولُونَ طَاعَةٌ فَإِذَا بَرَّوْا مِنْ
 عِنْدِكَ بَيَّتَ طَائِفَةٌ مِّنْهُمْ غَيْرَ الَّذِي تَقُولُ ۗ وَاللَّهُ يَكْتُبُ مَا
 يُبَيِّتُونَ ۗ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۗ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا
 ۗ أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْفُتْرَةَ ۗ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ
 لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا كَثِيرًا ۗ وَإِذَا جَاءَهُمْ أَمْرٌ مِنَ
 الْأَمْنِ أَوْ الْخَوْفِ أَذَاعُوا بِهِ ۗ وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَى الرَّسُولِ
 وَإِلَىٰ أُولِي الْأَمْرِ مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنْبِطُونَهُ مِنْهُمْ ۗ
 وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لَاتَّبَعْتُمُ الشَّيْطَانَ إِلَّا
 قَلِيلًا ۗ

مَّن يُطِيعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ ۗ
 وَمَنْ تَوَلَّىٰ فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ
 حَفِيظًا ۗ وَيَقُولُونَ طَاعَةٌ فَإِذَا
 بَرَّوْا مِنْ عِنْدِكَ بَيَّتَ طَائِفَةٌ مِّنْهُمْ
 غَيْرَ الَّذِي تَقُولُ ۗ وَاللَّهُ يَكْتُبُ مَا
 يُبَيِّتُونَ ۗ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ وَتَوَكَّلْ عَلَى
 اللَّهِ ۗ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ۗ

80. Mwenye kumtii Mtume basi ndio amemtii Mwenyezi Mungu. Na anayekengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao.

81. Na wanasema: Tunatii. Lakini wanapotoka kwako kundi moja miongoni mwao hupanga njama usiku kinyume na unayoyasema. Na Mwenyezi Mungu Anayaandika yote hayo wanayoyapangia njama za usiku. Basi waachilie mbali, na umtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mtegemewa wa kutosha.

Kumtii Mtume ﷺ ni Kumtii Allah تعالیٰ:

Allah تعالیٰ Ametaja kuwa yeyote anayemtii mja Wake na Mjumbe Wake, Muhammad ﷺ anamtii Allah تعالیٰ, na yeyote anayemuasi, anamuasi Allah تعالیٰ. Kwa hakika; lolote analotamka Mjumbe ﷺ sio utashi wake, lakini ni Wahyi. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالیٰ aliandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ أَطَاعَنِي فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ، وَمَنْ عَصَانِي فَقَدْ عَصَى اللَّهَ، وَمَنْ أَطَاعَ الْأَمِيرَ فَقَدْ أَطَاعَنِي، وَمَنْ عَصَى الْأَمِيرَ فَقَدْ عَصَانِي»

*"Yeyote anayenitii, anamtii Allah تعالى, na yeyote anayeniasi, anamuasi Allah. Yeyote anayemtii Amiri (kiongozi, mtawala) ananitii, na yeyote anayemuasi Amiri; ananiasi."*¹

Hadithi, hii imeandikwa katika Sahihi Mbili.² Kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ تَوَلَّىٰ فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا

"Na anayekengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao."

Maana yake: Msiwe na hofu naye. Kazi yako ni kufikisha, yeyote anayekutii, atapata furaha na mafanikio, nawe utapata malipo sawa na yake. Ama yule atakayekataa ulingano atakuwa amepotea, nawe hutobeba mzigo kwa yale ayafanyayo. Hadithi inasema,

«مَنْ يُطِيعِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ رَشَدَ، وَمَنْ يَعْصِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّهُ لَا يَضُرُّ إِلَّا نَفْسَهُ»

*"Mwenye kumtii Allah تعالى na Mtume wake, ameongoka, na mwenye kumuasi Allah na Mtume wake haidhuru isipokuwa nafsi yake."*²

Ujinga wa Wanafiki

Kauli ya Allah تعالى,

وَيَقُولُونَ طَاعَةٌ

"Na wanasema: Tunatii"

Allah تعالى Anaeleza kuwa wanafiki walijifanya waaminifu na watiifu. Maana: Wanapoondoka na kutokuwa pamoja nawe,

فَإِذَا بَرَّرُوا مِنَ عِنْدِكَ

"Lakini wanapotoka kwako."

Maana yake: Wanapoondoka na kutokuwa pamoja nawe,

¹ Ahmad 1:252.

² Fat'hul Al-Bari 6:135, na Muslim 3:1466.

بَيْتَ طَائِفَةٍ مِّنْهُمْ غَيْرِ الَّذِي تَقُولُ

“Hupanga njama usiku kinyume na unayoyasema.”

Wanakula njama wakati wa usiku kwa yaliyo kinyume na wanayojisingizia wanapokuwa pamoja nawe.

Kauli ya Allah تعالى،

وَاللَّهُ يَكْتُبُ مَا يُبَيِّنُونَ

“Na Mwenyezi Mungu Anayaandika yote hayo wanayoyapangia njama za usiku.”

Maana yake: Anazijua vyema njama zao na Anaziandika kwa amri Yake Aliyowaamuru waandishi Wake, malaika wenye kazi ya kuandika amali za waja. Hili ni tishio kutoka kwa Allah تعالى، linaloeleza kuwa Anajua yale ambayo wanafiki wanajaribu kuyaficha, njama zao za usiku, kumkana Mtume ﷺ na kumpinga, ingawa wanajisingizia kuwa waaminifu na watiifu kwake. Kwa hakika, Allah تعالى Atawaadhibu kwa tabia yao hii. Katika Aya kama hiyo, Allah تعالى Amesema،

وَيَقُولُونَ ءَأَمْنًا بِأَللَّهِ وَيَأْتِرَسُولٍ وَأَطَعْنَا

“Na wanasema, tumemuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na tumetii.” (24:47)

Mpaka mwisho wa Aya. Kauli ya Allah تعالى،

فَأَعْرَضَ عَنْهُمْ

“Basi waachilie mbali.”

Maana yake: Waache, wastahamilie, usiwaadhibu, usiwadhihirishe kwa watu na usiwaogope.

وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا

“...na umtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mtegemewa wa kutosha.”

Maana yake: Anatosha kuwa Mlinzi, Msaidizi kwa wanaomtegemea na kurejea Kwake.

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ ۚ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا كَثِيرًا ﴿٨٠﴾ وَإِذَا
 جَاءَهُمْ أَمْرٌ مِنَ الْأَمْنِ أَوْ الْخَوْفِ أَذَاعُوا بِهِ ۗ وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَى الرَّسُولِ وَإِلَىٰ أُولِي الْأَمْرِ
 مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنْبِطُونَهُ مِنْهُمْ ۗ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لَاتَّبَعْتُمُ الشَّيْطَانَ
 إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨١﴾

82. Hebu hawaizingatii hii Qur'ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangelikuta ndani yake khitilafu nyingi.

83. Na linapowafikia jambo lolote lililohusu amani au la kitisho wao hulitangaza. Na lau kuwa wangelilipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wale wanaochunguza wangelilijua. Na lau kuwa si Fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na Rehema Yake mngelimfuata Shetani ila wachache wenu tu.

Qur'an ni ya Kweli

Allah تعالیٰ Anawaamuru waitafakari Qur'an na Anawakataza kuipuuza, au kupuuza maana zake zenye hekima na maneno yenye ufasaha. Allah تعالیٰ Anaeleza kuwa hakuna kauli zisizowiana, zenye kukinzana, zenye kupingana au hitilafu katika Qur'an, kwa sababu ni ufunuo kutoka kwa Mwingi wa Hekima, Anayestahiki sifa zote njema. Kwa hiyo, Qur'an ni kweli inatoka kwa Mkweli Kabisa, Allah تعالیٰ. Ndio sababu Allah تعالیٰ Amesema katika Ayah nyingine,

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ ۚ أَمْ عَلَىٰ قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا ﴿٧٩﴾

“Je hawaizingatii Quraan au juu ya nyoyo kuna kufuli zake.” (47:24)

Kisha Allah تعالیٰ Akasema,

وَلَوْ كَانَ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ

“Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Ingekuwa uongo na kuundwa, kama washirikina wajinga na wanafiki wanavyofikiri,

لَوْجَدُوا فِيهِ اٰخْتِلَافًا

"Bila ya shaka wangelikuta ndani yake khitilafu." Hitilafu na kutokuwiana,

كَثِيْرًا

"Nyingi." Hata hivyo, Qur'an hii haina dosari, na kwa hiyo, inatoka kwa Allah تعالى. Kadhalika, Allah تعالى Anaeleza sifa za walio imara katika ujuzi,

كُلٌّ مِّنْ عِنْدِ رَبِّنَا

"Sisi tumeziamini, zote zimetoka kwa Mola wetu Mlezi." (3:7)

Maana: *Muhkam* (dhahiri kabisa) na *Mutashabih* (haziko wazi) za Qur'an zote ni kweli. Hivyo, wanazifahamu zisizo wazi kutokana na za wazi, hivyo wanaongoka. Ama wenye maradhi ya unafiki nyoyoni, wanazifahamu *Muhkam* kutokana na *Mutashabih*; na kwa kufanya hivyo wanapotea. Allah تعالى Amewasifu wenye elimu na kukosoa waovu. Imam Ahmad ameandika kuwa 'Amr bin Shu'ayb alisema, baba yake alisema, babu yake alisema, "Mimi na kaka tulikuwa mkutanoni, wenye thamani kubwa kwangu kuliko ngamia wekundu. Kaka yangu akaja na kukuta baadhi ya viongozi wa Maswahaba wa Mtume ﷺ wameketi karibu na mlango. Hatukutaka kuwaacha, basi, tulikaa karibu na vyumba. Wakaitaja Aya na kubishana mpaka wakapaza sauti zao. Mtume ﷺ alikasirika sana alipotoka uso wake ulikuwa mwekundu. Aliwarushia mchanga na kuwaambia,

«مَهْلًا يَا قَوْمِ، بِهَذَا أَهْلَيْتَ الْأَمَمَ مِنْ قَبْلِكُمْ، بِاِخْتِلَافِهِمْ عَلَى أَنْبِيَائِهِمْ، وَضَرْبِهِمِ
الْكُتْبَ بَعْضَهَا بِبَعْضٍ، إِنَّ الْقُرْآنَ لَمْ يَنْزَلْ يُكَذِّبُ بَعْضُهُ بَعْضًا، إِنَّمَا يُصَدِّقُ بَعْضُهُ
بَعْضًا، فَمَا عَرَفْتُمْ مِنْهُ فَاعْمَلُوا بِهِ، وَمَا جَهِلْتُمْ مِنْهُ فَارُدُّوهُ إِلَىٰ عَالِمِهِ»

*"Tazameni, enyi watu! Kwa hili, umma kabla yenu ziliangamizwa, kwa kubishana kwao na Mitume wao na baadhi ya Vitabu vyao kukinzana zenyewe. Qur'an haikinzani yenyewe. Bali, inajithibitisha ukweli wake. Hivyo, mliyoyajua humo basi yatumieni, na msichokijua katika hiyo, basi ipelekeni kwa mjuzi wake."*¹

¹ Ahmad 2:192.

Ahmad ameandika kuwa 'Abdullah bin 'Amr رضي الله عنه alisema, "Siku moja nilimuendea Mtume ﷺ Tulipokuwa tumeketi, watu wawili walibishana kuhusu Aya moja, na sauti zao zikapaa. Mtume ﷺ akasema,

«إِنَّمَا مَلَكَتِ الْأُمَّمُ قَبْلَكُمْ بِاخْتِلَافِهِمْ فِي الْكِتَابِ»

"Kwa hakika, zimeangamia umma kabla yenu kwa kutofautiana kwao juu ya Kitabu."¹

Muslim² na An-Nasa'i³ wameinukuu Hadithi hii.

Kukataza Kuarifu Habari Zisizo za Hakika na Zisizochunguzwa

Kauli ya Allah تعالى،

وَإِذَا جَاءَهُمْ أَمْرٌ مِّنَ الْأَمْنِ أَوْ الْخَوْفِ أَذَاعُوا بِهِ

"Na linapowafikia jambo lolote liliohusu amani au la kitisho wao hulitangaza."

Wanakaripiwa wenye kuingilia mambo kabla ya kuhakikisha ukweli wake, hali ya kuziarifu, na kueleza habari zao, ilhali habari hizo zinaweza zisiwe za kweli. Katika utangulizi wa Sahihi yake, Imam Muslim ameandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«كَفَى بِالْمَرْءِ كَذِبًا أَنْ يُحَدِّثَ بِكُلِّ مَا سَمِعَ»

"Inatosha mtu kuwa ni mwongo anaposimulia kila analosikia."⁴

Masimulizi haya pia yamekusanywa na Abu Dawud katika sura ya Adab (Adabu) katika *Sunan* yake.⁵ Katika Sahihi Mbili, imeandikwa kuwa Al-Mughirah bin Shu'bah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alikataza, "Kulisemwa" na, "Fulani amesema."⁶ Hadithi hii inawakusudia wale ambao mara kwa mara hufikisha kauli za watu bila ya kuchunguza uhakika wake na ukweli wa anachokisimulia. Sahih imeandika pia,

¹ Muslim 4:2053.

² Muslim 4:2053.

³ An-Nasai katika *Al-Kubra* 5:33

⁴ Muslim 1:10.

⁵ Abu Dawud 5:226.

«مَنْ حَدَّثَ بِحَدِيثٍ وَهُوَ يُرَى أَنَّهُ كَذِبٌ، فَهُوَ أَحَدُ الْكَاذِبِينَ»

“Mwenye kusimulia Hadithi moja huku akijua kuwa ni uongo, basi yeye ni katika waongo wawili (anayezusha na anayeeneza uongo).”¹

Hebu tutaje Hadithi ya ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه iliyopokewa katika Sahihi Mbili. ‘Umar رضي الله عنه alipoambiwa kuwa Mtume ﷺ aliwaacha wakeze, alikuja kutoka nyumbani kwake, akaingia Masjid na kuwakuta watu wakizungumzia habari hiyo. Hakusubiri na alikwenda kwa Mtume ﷺ kumuuliza nini hasa kilichojiri, akasema: “Umewaacha wakezo?” Mtume ﷺ alisema, “Hapana.” ‘Umar رضي الله عنه akasema, “Nilisema, *Allahu Akbar...*” na akaeleza Hadithi yote. Katika masimulizi ya Muslim, ‘Umar رضي الله عنه alisema, “Nikasema, ‘Je umewaacha?’ Akajibu, ‘Hapana. ‘Basi, nikasimama karibu na mlango wa Masjid nikapaza sauti, ‘Mtume ﷺ hakuacha wakeze.’ Kisha, ikashuka Aya hii,

وَإِذَا جَاءَهُمْ أَمْرٌ مِنَ الْأَمْنِ أَوْ الْخَوْفِ أَذَاعُوا بِهِ^ط وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَى الرَّسُولِ وَإِلَى أُولَى

الْأَمْرِ مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنْبِطُونَهُ

“Na linapowafikia jambo lolote lililohusu amani au la kitisho wao hilitangaza. Na lau kuwa wangelilipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kati yao, wale wanaochunguza wangelilijua.”²

Hivyo, nililichunguza vyema jambo hilo.” Aya hii inakusudia uchunguzi unaostahiki, au kuyatoa mambo kutoka katika vyanzo vyake vinavyostahiki. Kauli ya Allah تعالى،

لَا تَبْعَثُوا الشَّيْطَانَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٤٧﴾

“Mngelimfuata Shetani ila wachache wenu tu.”

Inakusudia waumini, kama ‘Ali bin Abi Talhah alivyosimulia kutoka kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما.³

* * *

¹ Muslim 5 na Abu Dawud 226.

² Muslim 1:9.

³ *Fat’hul Al-Bari* 9:187 na Muslim 2:1105.

فَقَتِلَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا تَكُفُّ إِلَّا نَفْسُكَ ۗ وَحَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ ۗ^ط
 عَسَى اللَّهُ أَنْ يَكُفَّ بَأْسَ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ وَاللَّهُ أَشَدُّ بَأْسًا وَأَشَدُّ
 تَنْكِيلًا ﴿٨٤﴾ مَنْ يَشْفَعْ شَفَعَةً حَسَنَةً يَكُنْ لَهُ نَصِيبٌ مِمَّا ۗ^ط
 وَمَنْ يَشْفَعْ شَفَعَةً سَيِّئَةً يَكُنْ لَهُ كِفْلٌ مِمَّا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ
 كُلِّ شَيْءٍ مُقِيمًا ﴿٨٥﴾ وَإِذَا حُيِّمُ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا بِأَحْسَنَ مِمَّا ۗ^ط
 أَوْزُدُوهَا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَسِيبًا ﴿٨٦﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ
 إِلَّا هُوَ ۗ لَيَجْمَعَنَّكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ ۗ وَمَنْ
 أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ حَدِيثًا ﴿٨٧﴾ * فَمَا لَكُمْ فِي الْأَنْفِيقِينَ فَفَتِنًا
 ۗ وَاللَّهُ أَرْكَسَهُم بِمَا كَسَبُوا ۗ أَتُرِيدُونَ أَنْ تَهْدُوا مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ ۗ^ط
 وَمَنْ يَضِلَّ اللَّهُ فَلَنْ يَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿٨٨﴾ وَدُّوا لَوْ تَكْفُرُونَ
 كَمَا كَفَرُوا فَتَكُونُونَ سَوَاءً ۗ فَلَا تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ أَوْلِيَاءَ حَتَّىٰ
 يُهَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۗ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَخُذُوهُمْ وَأَقْتُلُوهُمْ ۗ حَيْثُ
 وَجَدْتُمُوهُمْ ۗ وَلَا تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ وُليًا وَلَا نَصِيرًا ﴿٨٩﴾ إِلَّا
 الَّذِينَ يَصِلُونَ إِلَىٰ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ أَوْ جَاءُوكُمْ
 حَصْرَتِ صُدُورُهُمْ أَنْ يَقْتُلُوكُمْ أَوْ يَقْتُلُوا قَوْمَهُمْ ۗ وَلَوْ شَاءَ
 اللَّهُ لَسَلَطَهُمْ عَلَيْكُمْ ۗ فَلَقَاتِلُوكُمْ ۗ فَإِنْ آعَزَلُوكُمْ فَلَمْ يَقْتُلُوكُمْ
 وَأَلْفَوْا إِلَيْكُمْ أَلْسَلَمَ ۗ فَمَا جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ عَلَيْهِمْ سَبِيلًا ﴿٩٠﴾
 سَتَجِدُونَ ءآخِرِينَ يَرِيدُونَ أَنْ يُؤْمِنُوا بِمَا آمَنُوا قَوْمَهُمْ كُلٌّ مَا
 زُدُّوا إِلَىٰ الْآفْتِنَةِ ۗ أُرْكَسُوا فِيهَا ۗ فَإِنْ لَمْ يَحْتَرِكُوا ۗ وَيُلقُوا إِلَيْكُمْ
 أَلْسَلَمَ ۗ وَيَكْفُرُوا ۗ أَيْدِيَهُمْ فَخُذُوهُمْ وَأَقْتُلُوهُمْ ۗ حَيْثُ نَفِثْتُمُوهُمْ
 ۗ وَأُولَئِكَ جَعَلْنَا لَكُمْ عَلَيْهِمْ سُلْطَنًا مُبِينًا ﴿٩١﴾

فَقَتِلَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا تَكُفُّ إِلَّا نَفْسُكَ ۗ وَحَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ ۗ^ط
 عَسَى اللَّهُ أَنْ يَكُفَّ بَأْسَ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ وَاللَّهُ أَشَدُّ بَأْسًا وَأَشَدُّ
 تَنْكِيلًا ﴿٨٤﴾ مَنْ يَشْفَعْ شَفَعَةً حَسَنَةً يَكُنْ لَهُ نَصِيبٌ مِمَّا ۗ^ط
 وَمَنْ يَشْفَعْ شَفَعَةً سَيِّئَةً يَكُنْ لَهُ كِفْلٌ مِمَّا ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ
 كُلِّ شَيْءٍ مُقِيمًا ﴿٨٥﴾ وَإِذَا حُيِّمُ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا بِأَحْسَنَ مِمَّا ۗ^ط
 أَوْزُدُوهَا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَسِيبًا ﴿٨٦﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ
 إِلَّا هُوَ ۗ لَيَجْمَعَنَّكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ ۗ وَمَنْ
 أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ حَدِيثًا ﴿٨٧﴾ * فَمَا لَكُمْ فِي الْأَنْفِيقِينَ فَفَتِنًا
 ۗ وَاللَّهُ أَرْكَسَهُم بِمَا كَسَبُوا ۗ أَتُرِيدُونَ أَنْ تَهْدُوا مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ ۗ^ط
 وَمَنْ يَضِلَّ اللَّهُ فَلَنْ يَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿٨٨﴾ وَدُّوا لَوْ تَكْفُرُونَ
 كَمَا كَفَرُوا فَتَكُونُونَ سَوَاءً ۗ فَلَا تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ أَوْلِيَاءَ حَتَّىٰ
 يُهَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۗ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَخُذُوهُمْ وَأَقْتُلُوهُمْ ۗ حَيْثُ
 وَجَدْتُمُوهُمْ ۗ وَلَا تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ وُليًا وَلَا نَصِيرًا ﴿٨٩﴾ إِلَّا
 الَّذِينَ يَصِلُونَ إِلَىٰ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ أَوْ جَاءُوكُمْ
 حَصْرَتِ صُدُورُهُمْ أَنْ يَقْتُلُوكُمْ أَوْ يَقْتُلُوا قَوْمَهُمْ ۗ وَلَوْ شَاءَ
 اللَّهُ لَسَلَطَهُمْ عَلَيْكُمْ ۗ فَلَقَاتِلُوكُمْ ۗ فَإِنْ آعَزَلُوكُمْ فَلَمْ يَقْتُلُوكُمْ
 وَأَلْفَوْا إِلَيْكُمْ أَلْسَلَمَ ۗ فَمَا جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ عَلَيْهِمْ سَبِيلًا ﴿٩٠﴾
 سَتَجِدُونَ ءآخِرِينَ يَرِيدُونَ أَنْ يُؤْمِنُوا بِمَا آمَنُوا قَوْمَهُمْ كُلٌّ مَا
 زُدُّوا إِلَىٰ الْآفْتِنَةِ ۗ أُرْكَسُوا فِيهَا ۗ فَإِنْ لَمْ يَحْتَرِكُوا ۗ وَيُلقُوا إِلَيْكُمْ
 أَلْسَلَمَ ۗ وَيَكْفُرُوا ۗ أَيْدِيَهُمْ فَخُذُوهُمْ وَأَقْتُلُوهُمْ ۗ حَيْثُ نَفِثْتُمُوهُمْ
 ۗ وَأُولَئِكَ جَعَلْنَا لَكُمْ عَلَيْهِمْ سُلْطَنًا مُبِينًا ﴿٩١﴾

84. Basi pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hukalifishwi ila nafsi yako tu. Na wahimiza Waumini. Huenda Mwenyezi Mungu Akayazuia mashambulio ya waliokufuru. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mkali zaidi wa Kushambulia na Mkali zaidi wa Kuadhibu.

85. Mwenye kusaidia msaada mwema ana fungu lake katika hayo, na mwenye kusaidia msaada mwovu naye ana sehemu yake katika hayo. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza na ujuzi juu ya kila kitu.

86. Na mnapoamkiwa kwa maamkio yoyote, basi nanyi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuhisabu kila kitu.

87. Mwenyezi Mungu, hapana mola isipo kuwa Yeye. Kwa yakini Atakukusanyeni Siku ya Kiyama. Halina shaka hilo. Na ni nani msema kweli kuliko Mwenyezi Mungu?

Allah تعالیٰ Anamuamuru Mjumbe Wake Afanye Jihad

Allah تعالیٰ Anamuamuru mja Wake na Mjumbe Wake, Muhammad ﷺ, mwenyewe apigane Jihad na asijihusishe na wasiojiunga naye. Hivyo Allah تعالیٰ Anasema,

لَا تُكَلِّفُ إِلَّا نَفْسَكَ

“Hukalifishwi ila nafsi yako tu.”

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالیٰ ameandika kuwa Abu Ishaq alisema, “Nilimuuliza Al-Bara bin ‘Azib kuhusu mtu anayekutana na maadui mia moja na akapigana nao, je atakuwa katika waliokusudiwa katika Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَلَا تُلْقُوا بِأَيْدِيكُمْ إِلَى التَّهْلُكَةِ

“Wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo.” (2:195)

Akasema, ‘Allah تعالیٰ Alimuambia Mtume Wake ﷺ,

فَقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا تُكَلِّفُ إِلَّا نَفْسَكَ وَحَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ

“Basi pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hukalifishwi ila nafsi yako tu. Na wahimize Waumini.”

“Imam Ahmad amemnukuu Sulayman bin Dawud akisema kuwa Abu Bakr bin ‘Ayyash alisema kuwa Abu Ishaq alisema, “Nilimuuliza Al-Bara’, ‘Kama mtu atashambulia safu za washirikina, atakuwa anajitia katika maangamizi

mwenyewe?' Akasema, 'Hapana kwa sababu Allah تعالى Amemtuma Mjumbe Wake ﷺ na kumuamuru,

فَقَبِيلٌ فِي سَبِيلِ اللَّهِ لَا تُكَلِّفُ إِلَّا نَفْسَكَ

"Basi pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hukalifishwi ila nafsi yako tu."

Aya hiyo inahusu kutoa mali katika njia ya Allah تعالى.¹

Kuwashawishi Waumini Kupigana

Kauli ya Allah تعالى,

وَحَرَضَ الْمُؤْمِنِينَ

"Na wahimize Waumini."

Kupigana, kwa kuwahimiza na kuimarisha azma yao kuhusu hilo. Kwa mfano, Mtume ﷺ aliwaambia waumini katika vita vya Badr, alipokuwa akinyoosha safu zao,

«قَوْمُوا إِلَى جَنَّةِ عَرْضِهَا السَّمَاوَاتُ وَالْأَرْضُ»

"Simameni mwende katika pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi."²

Kuna Hadithi nyingi zinazohimiza Jihad. Al-Bukhari ameandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ، وَأَقَامَ الصَّلَاةَ، وَآتَى الزُّكَاةَ، وَصَامَ رَمَضَانَ، كَانَ حَقًّا عَلَى اللَّهِ أَنْ يُدْخِلَهُ الْجَنَّةَ، هَاجَرَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَوْ جَلَسَ فِي أَرْضِهِ الَّتِي وُلِدَ فِيهَا»

"Anayemuamini Allah na Mjumbe Wake, akasali, akatoa Zakah na kufunga mwezi wa Ramadhan, atakuwa na haki kwa Allah ya kuingizwa peponi, haijalishi kuwa alihama katika njia ya Allah au alibakia katika ardhi yake alikozaliwa."

¹ Ahmad 4:281.

² Muslim 3:1510.

Watu wakasema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Tuwajulishe watu habari hizi njema?'
Akasema,

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ مِائَةَ دَرَجَةٍ أَعَدَّهَا اللَّهُ لِلْمُجَاهِدِينَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، بَيْنَ كُلِّ دَرَجَتَيْنِ كَمَا
بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، فَإِذَا سَأَلْتُمْ اللَّهَ فَاسْأَلُوهُ الْفِرْدَوْسَ، فَإِنَّهُ وَسْطُ الْجَنَّةِ، وَأَعْلَى
الْجَنَّةِ، وَفَوْقَهُ عَرْشُ الرَّحْمَنِ، وَمِنْهُ تَفَجَّرُ أَنْهَارُ الْجَنَّةِ»

*"Peponi kuna daraja mia moja ambazo Allah تعالى Amewawekea Mujahidin wanaopigana katika njia Yake, masafa baina ya kila daraja mbili ni sawa na umbali baina ya mbingu na Ardhi. Hivyo, mnapomuomba Allah تعالى, muombeni Al-Firdaws, ambayo ni mahali bora zaidi na ya juu zaidi Peponi, juu yake kuna Arshi ya Mwingi wa Ukarimu (Allah) na kutoka humo hutiririka mito ya Peponi."*¹

Kuna masimulizi kadhaa ya Hadithi hii kutoka kwa 'Ubadah,² Mu`adh,³ na Abu-Darda'a رضي الله عنهم. Abu Sa`id Al-Khudri رضي الله عنه amesimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

«يَا أَبَا سَعِيدٍ! مَنْ رَضِيَ بِاللَّهِ رَبًّا، وَبِالْإِسْلَامِ دِينًا، وَبِمُحَمَّدٍ ﷺ نَبِيًّا، وَجَبَتْ لَهُ
الْجَنَّةُ»

"Ewe Abu Sa`id! Mwenye kumkubali Allah تعالى kuwa ni Mola wake Mlezi, kuwa Uislamu ni Dini yake na Muhammad ﷺ kuwa ni Mtume wake, basi Pepo itakuwa haki yake."

Abu Sa`id رضي الله عنه aliyapenda maneno hayo na akasema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Nikaririe maneno hayo." Mtume ﷺ akakariri maneno yake, kisha akasema,

«وَأُخْرَى يَرْفَعُ اللَّهُ الْعَبْدَ بِهَا مِائَةَ دَرَجَةٍ فِي الْجَنَّةِ، مَا بَيْنَ كُلِّ دَرَجَتَيْنِ كَمَا بَيْنَ
السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ»

"Na kuna amali nyingine ambayo kwayo, Allah Humpandisha mja wake daraja mia moja Peponi, baina ya kila daraja mbili ni umbali wa mbingu na Ardhi."

¹ Fat'hul Al-Bari 6:14.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 7:737.

³ Ibn Majah 2:1448.

Abu Sa'id رضي الله عنه alisema, "Ni ipi hiyo?, Ewe Mjumbe wa Allah." Akasema,

«الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

"Jihadi katika njia ya Allah."¹

Hadithi hii imekusanywa na Muslim. Kauli ya Allah تعالى،

عَسَى اللَّهُ أَنْ يَكُفَّ بَأْسَ الَّذِينَ كَفَرُوا

"Huenda Mwenyezi Mungu Akayazuia mashambulio ya waliokufuru."

Maana yake: Kwa kuwahimiza kupigana, azma yao itakuwa imetiliwa nguvu ya kukabiliana na adui vitani, kuutetea Uislamu na watu wake na kustahamili na kuwa na subira dhidi ya adui.

Kauli ya Allah تعالى،

وَاللَّهُ أَشَدُّ بَأْسًا وَأَشَدُّ تَنَكِيلًا

"Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mkali zaidi wa Kushambulia na Mkali zaidi wa Kuadhibu."

Maana yake: Muweza juu yao duniani na Akhera, kama Alivyosema katika Aya nyingine,

ذَلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَانتَصَرْنَا مِنْهُمْ وَلَكِنْ لِيَبْلُوَا بَعْضَكُمْ بِبَعْضٍ

"Ndio hivyo. Na lau Angelitaka Mwenyezi Mungu Angeliwashinda Mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu Akutieni mitihani nyinyi kwa nyinyi." (47:4).

Kuombea kwa Ajili ya Njia ya Heri au ya Shari

Kauli ya Allah تعالى،

مَنْ يَشْفَعْ شَفْعَةً حَسَنَةً يَكُنْ لَهُ نَصِيبٌ مِمَّا

"...na mwenye kusaidia msaada mwema naye ana sehemu yake katika hayo."

¹ Muslim 3:1501.

Maana yake: Mwenye kuombea jambo lenye kuleta heri, atapata fungu katika heri hiyo.

مَنْ يَشْفَعْ شَفَعَةً حَسَنَةً يَكُنْ لَهُ نَصِيبٌ مِّنْهَا

“Na mwenye kusaidia msaada mwovu naye ana sehemu yake katika hayo.”

Maana yake: Atabeba mzigo kutokana na uombezi wake na nia yake. Kwa mfano, imeandikwa katika Sahih kuwa Mtume ﷺ alisema,

«اشْفَعُوا تُؤَجَّرُوا، وَيَقْضِي اللهُ عَلَى لِسَانِ نَبِيِّهِ مَا شَاءَ»

“Ombeeni mtapata malipo yake. Na Allah تعالیٰ Ataamua chochote Anachotaka kwa maneno ya Mtume Wake.”¹

Mujahid bin Jabir alisema, “Aya hii ilishuka kuhusu uombezi wa watu kwa ajili ya kila mmoja.”²

Kisha Allah تعالیٰ Akasema,

وَكَانَ اللهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ مُّقِيتًا ﴿٢٥٦﴾

“Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Uweza na Ujuzi juu ya kila kitu.”

Ibn ‘Abbas, ‘Ata’, ‘Atiyah, Qatadah na Matar Al-Warraq رضي الله عنهم walisema kuwa,

﴿٢٥٦﴾ مُّقِيتًا

“Mwenye Uweza na Ujuzi”,

(*Muqit*) Maana yake: “Mwangelizi.”³ Mujahid alisema kuwa *Muqit* inamaanisha, ‘Shahidi’, na katika masimulizi mengine, ‘Mwenye Uweza wa Kutenda.’⁴

¹ Fat’hul Al-Bari 3:351.

² At-Tabari 8:581.

³ At-Tabari 8:583.

⁴ At-Tabari 8:583.

Kuitikia *Salam*, kwa Salam Bora Zaidi

Kauli ya Allah تعالى،

وَإِذَا حُيِّتُمْ بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا بِأَحْسَنَ مِنْهَا أَوْ رُدُّوهَا

“Na mnapoamkiwa kwa maamkio yoyote, basi nanyi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo.”

Maana yake: Kama Muislamu atakusalimieni kwa Salamu, basi itikieni kwa Salamu bora zaidi, au angalau sawa na Salamu iliyotolewa. Kwa hiyo, Salamu bora zaidi imependekewa, wakati wa kuitikia sawa na iliyotolewa ni wajibu. Imam Ahmad ameandika kuwa Abu Raja' Al-'Utaridi alisema kuwa 'Imran bin Husayn alisema kuwa mtu mmoja alikuja kwa Mtume ﷺ na kusema, “As-Salamu ‘Alaykum”. Mtume ﷺ akaitikia, na baada ya mtu huyo kuketi chini alisema, “Kumi.” Mtu mwingine akaja na kusema, “As-Salamu ‘Alaykum wa Rahmatullah, Ewe Mjumbe wa Allah.” Mtume ﷺ akaitikia, na baada ya mtu huyo kuketi chini alisema, “Ishirini.” Akaja mtu mwingine na kusema, “As-Salamu ‘Alaykum wa Rahmatullah wa Barakatuh.” Mtume ﷺ akaitikia na baada ya mtu huyo kuketi chini alisema, “Thelathini.”¹ Haya ni masimulizi yaliyoandikwa na Abu Dawud. At-Tirmidhi, An-Nasa'i na Al-Bazzar pia ameyaandika. At-Tirmidhi alisema, “*Hasan Gharib*”. Kuna Hadithi nyingi juu ya mada hii kutoka kwa Abu Sa'id, 'Ali, na Sahl bin Hanif رضي الله عنهم.² Muislamu anaposalimiwa kwa ukamilifu wa Salam, anawajibika kuitikia sawa na alivyosalimiwa.

Ama kuhusu *Ahl Adh-Dhimmah*,³ isianzishwe Salam wala kuongeza chochote wakati wa kuitikia maamkizi yao. Badala yake, kama ilivyoandikwa katika Sahihi Mbili kuwa maamkizi yao huitikiwa sawa na walivyosalimia. Ibn 'Umar رضي الله عنهما amesimulia kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِذَا سَلَّمَ عَلَيْكُمْ الْيَهُودُ، فَإِنَّمَا يَقُولُ أَحَدُهُمْ: السَّلَامُ عَلَيْكَ، فَقُلْ: وَعَلَيْكَ»

“Wayahudi wanapokusalimieni, mmoja wao husema, ‘As-Samu ‘Alayka (mauti juu yenu).’ Kwa hiyo, semeni, ‘Wa ‘Alayka (na juu yako).”⁴

¹ Ahmad 4:439.

² Abu Dawud 5:379. *Tuhfat Al-Ahwadhi* 7:463. *Kashf Al-Astar*. 2:418.

³ Wasio Waislamu katika udhibiti wa Waislamu.

⁴ *Fat'hul Al-Bari* 12:293 na Muslim 4:1706.

Katika Sahihi yake, Muslim ameandika kuwa Abu Hurayrah رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا تَبْدَأُوا الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى بِالسَّلَامِ، وَإِذَا لَقَيْتُمُوهُمْ فِي طَرِيقٍ فَاصْطَرِّوهُمْ إِلَىٰ أَضْيَاقِهِ»

*"Msiwaanzishie Salamu Wayahudi na Wakristo, na mnapowakuta njiani, wabaneni wapite katika sehemu nyembamba."*¹

Abu Dawud ameandika kuwa Abu Hurayrah رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَا تَدْخُلُوا الْجَنَّةَ حَتَّىٰ تُوْمِنُوا، وَلَا تُوْمِنُوا حَتَّىٰ تَحَابُّوا، أَفَلَا أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ أَمْرٍ إِذَا فَعَلْتُمُوهُ تَحَابَّبْتُمْ؟ أَفَسُوا السَّلَامَ بَيْنَكُمْ»

*"Naapa kwa Ambaye roho yangu iko Mkononi Mwake! Hamtaingia Peponi mpaka muamini, na hamtaamini mpaka mpendane. Nikujulisheni kitendo kitakachokufanyeni mpendane, Enezeni Salam miongoni mwenu."*¹

Kauli ya Allah تعالى،

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ

"Mwenyezi Mungu, hapana mola isipo kuwa Yeye."

Inaeleza kuwa Yeye Ndiye Pekee Mungu wa viumbe wote. Kisha Allah تعالى Akasema,

لَيَجْمَعَنَّكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ

"Kwa yakini Atakukusanyeni Siku ya Kiyama. Halina shaka hilo."

Kwa kuapa kuwa Atavikusanya vizazi vya mwanzo na vya baadaye katika sehemu moja, na Kumlipa au Kumuadhibu kila mmoja kulingana na matendo yake. Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ حَدِيثًا ﴿٢٧﴾

"Na ni nani msema kweli kuliko Mwenyezi Mungu?"

Maana yake: Hakuna anayetamka kauli ya ukweli zaidi kuliko Allah تعالى، katika Ahadi Yake, Maonyo, Masimulizi na Habari za yatakayokuja; hakuna mwenye haki ya kuabudiwa wala Mola Mlezi isipokuwa Yeye.

¹ Ahmad 4:1707. Hadithi hii inatakiwa kusomwa katika muktadha wake, kwa maana ya kujua mazingira ya maneno haya yalisemwa wakati gani. Katika Uislamu Mayahudi na wakristo wana haki nyingi sana ambazo hapana budi kutekelezwa (Mhariri).

² Abu Dawud 5:378.

* فَمَا لَكُمْ فِي النَّفِيقِينَ فَعْتَبِينَ وَاللَّهُ أَرْكَسَهُمْ بِمَا كَسَبُوا أَتُرِيدُونَ أَنْ تَهْدُوا مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ^ط
 وَمَنْ يُضِلِلِ اللَّهُ فَلَنْ تَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿٨٨﴾ وَدُوا لَوْ تَكْفُرُونَ كَمَا كَفَرُوا فَتَكُونُونَ سَوَاءً فَلَا
 تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ أَوْلِيَاءَ حَتَّىٰ يَهَاجِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ^ع فَإِنْ تَوَلَّوْا فَخُذُوهُمْ وَأَقْتُلُوهُمْ^ط حَيْثُ
 وَجَدْتُمُوهُمْ وَلَا تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ وُليًا وَلَا نَصِيرًا ﴿٨٩﴾ إِلَّا الَّذِينَ يَصِلُونَ إِلَىٰ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ
 وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ أَوْ جَاءُوكُمْ حَصِرَتْ صُدُورُهُمْ أَنْ يُقَاتِلُوكُمْ أَوْ يُقَاتِلُوا قَوْمَهُمْ^ع وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ
 لَسَلَّطَهُمْ عَلَيْكُمْ فَلَقَاتِلُوكُمْ^ع فَإِنْ أَعْتَزَلُوكُمْ فَلَمْ يُقَاتِلُوكُمْ وَأَلْقَوْا إِلَيْكُمُ السَّلَمَ فَمَا جَعَلَ اللَّهُ
 لَكُمْ عَلَيْهِمْ سَبِيلًا ﴿٩٠﴾ سَتَجِدُونَ ءَاخِرِينَ يُرِيدُونَ أَنْ يَأْمَنُوكُمْ وَيَأْمَنُوا قَوْمَهُمْ كُلٌّ مَا رَدُّوا
 إِلَىٰ الْفِتْنَةِ أُرْكَسُوا فِيهَا^ع فَإِنْ لَمْ يَعْتَزِلُوكُمْ وَيُلْقُوا إِلَيْكُمْ السَّلَمَ وَيَكْفُوا أَيْدِيَهُمْ فَخُذُوهُمْ
 وَأَقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ^ع وَأُولَئِكَ جَعَلْنَا لَكُمْ عَلَيْهِمْ سُلْطَانًا مُبِينًا ﴿٩١﴾

88. Mmekuwaje kuwa makundi mawili kwa khabari ya wanafiki, na hali Mwenyezi Mungu Amewageuza kwa sababu ya yale waliyo yachuma? Je! Mnataka kumwona mwongofu ambaye Mwenyezi Mungu amemhukumu kuwa kapotea? Na aliyemhukumu Mwenyezi Mungu kuwa amekwisha potea wewe hutampatia njia.

89. Wanapenda lau kuwa nanyi mngekufuru kama walivyokufuru wao, ili muwe sawa sawa. Basi msiwafanye marafiki miongoni mwao mpaka wahame kwa ajili ya Dini ya Mwenyezi Mungu. Na wakikengeuka basi wakamateni na wauweni popote mnapo wapata. Wala msifanye rafiki katika wao wala msaidizi.

90. Isipokuwa wale walio fungamana na watu ambao mna ahadi baina yenu na wao, au wanakujieni na vifua vyao vina dhiki kupigana nanyi, au kupigana na watu wao. Na lau angelipenda Mwenyezi Mungu Angeliwasaliti juu yenu wakapigana nanyi. Basi wakijitenga nanyi, wasipigane nanyi, na wakakuleteeni amani, basi Mwenyezi Mungu hakukupeni njia kupigana nao.

91. Mtawakuta wengine wanataka wapate salama kwenu na

salama kwa watu wao. Kila wakirudishwa kwenye fitna hudidimizwa humo. Ikiwa hawajitengi nanyi, na wakakuleteeni salama, na wakazuia mikono yao, basi wakamateni na wauweni popote mnapo wakuta. Na juu ya hao ndio Tumekupeni hoja zilizo wazi.

Kuwakaripia Maswahaba kwa Kutokuafikiana juu ya Wanafiki Wanaorejea Al-Madinah Kabla ya Uhud

Allah تعالى Amewakaripia waumini kwa kutokubaliana juu ya wanafiki. Kuna rai tofauti juu ya sababu za kushuka Ayah hii. Imam Ahmad ameandika kuwa Zayd bin Thabit alisema kuwa Mtume ﷺ alitembea kwa miguu kuelekea Uhud. Hata hivyo, baadhi ya watu waliofuatana naye walirejea Al-Madinah, na Maswahaba wa Mtume ﷺ waligawanyika katika makundi mawili kuhusu hao, moja lilisema kuwa wauliwe na jingine lilikataa. Allah تعالى Akashusha,

﴿ فَمَا لَكُمْ فِي الْمُنَافِقِينَ فَعْتَنَ ﴾

“Mmekuwaje kuwa makundi mawili kwa khabari ya wanaafiki.”

Mtume ﷺ amesema,

﴿ إِنَّهَا طَيِّبَةٌ، وَإِنَّهَا تُنْفِي الْخَبَثَ، كَمَا يَنْفِي الْكَبِيرُ خَبَثَ الْحَدِيدِ ﴾

“Hiyo (Al-Madinah) ni Taybah, na huondoa uchafu, kama kiriba kinavyoondoa kutu kutoka katika chuma.”¹ Sahihi Mbili pia zimeandika Hadithi hii.²

Al-'Awfi amesimulia kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Ayah hiyo ilishuka kuhusu baadhi ya watu katika Makkah waliosema kuwa wamesilimu, na wakati huo huo walikuwa wakiwasaidia washirikina. Wakati fulani, watu hao walitoka nje ya Makkah ili kutimiza baadhi ya haja na wakaambizana, “Tukikutana na Masahaba wa Muhammad ﷺ, hatutadhuriwa nao.” Waumini walipopata habari kuwa watu hao walitoka nje ya Makkah, baadhi yao walisema, “Hebu tuwaendee waoga hawa na kuwaua, kwa sababu wanamsaidia adui yenu dhidi yenu.” Hata hivyo, kikundi kingine cha Waumini kilisema, “Ametakasika Allah عزوجل! Mnawaua watu wanaosema kama

¹ Ahmad 5:184.

² Fat'hul Al-Bari 4:115 na Muslim 2:1007.

mnavyosema, kwa sababu tu hawakufanya Hijrah au kuacha ardhi yao, je inaruhusiwa kumwaga damu zao na kutaifisha mali zao katika hali hii," hivyo, waligawanyika katika makundi mawili, wakati huo wote Mtume ﷺ alikuwa pamoja nao, na hakukataza kundi lolote kurudiarudia kusema hoja yao. Baada ya hapo, Allah Alishusha,

﴿ فَمَا لَكُمْ فِي آلِنَفِيقِينَ فَعْتَبِينَ ﴾

"Mmekuwaje kuwa makundi mawili kwa habari ya wanafiki?"

Ibn Abi Hatim ameinukuu Hadithi hii. Kauli ya Allah تعالى،

﴿ وَاللَّهُ أَرْكَسَهُمْ بِمَا كَسَبُوا ﴾

"...na hali Mwenyezi Mungu Amewageuza kwa sababu ya yale waliyoyachuma?"

Maana yake: Aliwafanya warejee, na kuangukia katika makosa. Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa،

﴿ أَرْكَسَهُمْ ﴾

"Amewageuza." Maana yake: Aliwatupa.² Kauli ya Allah تعالى،

﴿ بِمَا كَسَبُوا ﴾

"Kwa sababu ya yale waliyoyachuma?" Maana yake: Kwa sababu ya ufidhuli na uasi wao kwa Mtume ﷺ na kufuata upotevu.

﴿ أُرِيدُونَ أَنْ تَهْتَدُوا مِنْ أَضَلِّ أَلْتُّهُ وَمَنْ يُضَلِّ أَلْتُّهُ فَلَنْ يَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴾

"Je! Mnataka kumwona mwongofu ambaye Mwenyezi Mungu Amemhukumu kuwa kapotea? Na aliyemhukumu Mwenyezi Mungu kuwa amekwishapotea wewe hutampatia njia."

Maana yake: Hatakuwa na njia, au uongofu. Kauli ya Allah تعالى،

﴿ وَدُّوا لَوْ تَكْفُرُونَ كَمَا كَفَرُوا فَتَكُونُونَ سَوَاءً ﴾

"Wanapenda lau kuwa nanyi mnggekufuru kama walivyokufuru wao, ili muwe sawa sawa."

Maana yake: Wanatamani uwe katika upotevu, ili, wewe na wao muwe sawa katika hilo. Hayo ni kwa sababu ya uadui wao mkubwa kwako na kukuchukia

¹ At-Tabari 9:10. Kama ilivyotangulia kutajwa, masimulizi ya Al 'Awfi si sahihi.

² At-Tabari 9:15.

mno. Kwa hiyo, Allah تعالى Amesema,

فَلَا تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ أَوْلِيَاءَ حَتَّىٰ يُهَاجِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَإِن تَوَلَّوْا

“Basi msiwafanye marafiki miongoni mwao mpaka wahame kwa ajili ya Dini ya Mwenyezi Mungu. Na wakikengeuka...”

Kama wanaacha Hijrah, kama alivyosimulia Al-'Awfi kutoka kwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما.¹ As-Suddi alisema kuwa sehemu hii ya Ayah inamaanisha, “kama watadhihirisha ukafiri wao.”

Wenye Kupigana na Wasiopigana

Allah تعالى Amewaepusha baadhi ya watu;

إِلَّا الَّذِينَ يَصِلُونَ إِلَىٰ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُم مِّيثَاقٌ

“Isipokuwa wale waliofungamana na watu ambao mna ahadi baina yenu na wao”

Maana yake: Isipokuwa wanaojiunga na kupata hifadhi kwa wale mliowekeana nao mkataba wa amani, au watu wa *Dhimmah*, basi watendeeni kama mnavyowatendea wale mliowekeana nao amani. Hii ni kauli ya As-Suddi, Ibn Zayd na Ibn Jarir رحمه الله تعالى.² Katika Sahihi yake, Al-Bukhari amenukuu kisa cha mkataba wa *Al-Hudaybiyyah*, ambapo kulitajwa kuwa aliyetaka kuwa na amani na Quraysh afanye nao mkataba, kisha wakaruhusiwa. Wale waliopenda kuwekeana amani na Muhammad ﷺ na Masahaba zake na kuwa na mkataba nao waliruhusiwa.³ Imesimuliwa kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema Aya hiyo ilifutwa kwa Kauli ya Allah تعالى,

فَإِذَا أَسْلَخَ الْأَشْهُرَ الْحُرْمَ فَاقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ

“Miezi mitukufu inapopita, basi wapigeni washirikina popote mnapowakuta.”(9:5)⁴

¹ At-Tabari 9:17.

² At-Tabari 9:19.

³ *Fat'hul Al-Bari* 5:388 na Ahmad 3:25.

⁴ At-Tabari 9:18.

Allah تعالی Amesema,

أَوْ جَاءَكُمْ حَصْرَتْ صُدُورُهُمْ

"Au wanakujieni na vifua vyao vikisitasita."

Inakusudia aina nyingine ya watu walio na udhuru wa kutokupigana. Hao wanaoowaendea Waislamu kwa kusitasita nyoyoni mwao kwa sababu wanachukia kupigana na Waislamu. Hawana moyo wa kupigana na Waislamu dhidi ya watu wao. Kwa hiyo, wao hawako pamoja na Waislamu wala dhidi yao.

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَسَلَّطْنَاهُمْ عَلَيْكُمْ

"Na lau angelipenda Mwenyezi Mungu Angeliwasaliti juu yenu wakapigana nanyi."

Maana yake: Ni kutokana na Rehema za Allah تعالی kuwa Amewazuia kupigana nanyi.

فَإِنْ أَعْرَضْتُمْ عَنْكُمْ فَلَمْ يَقْبَلُوا إِلَيْكُمْ أَلْسَلَمَ

"Basi wakijitenga nanyi, wasipigane nanyi, na wakakuleteeni amani"

Maana yake: Wanarejea katika amani,

فَمَا جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ عَلَيْهِمْ سَبِيلًا

"Basi Mwenyezi Mungu Hakukupeni njia kupigana nao."

Huna haki ya kuwaua, madamu wako katika nafasi hiyo. Hiyo ilikuwa nafasi ya Banu Hashim kabila la Mtume ﷺ, kama vile Al-'Abbas رضي الله عنه, aliyefuatana na washirikina katika vita vya Badr, kwa kuwa walijiunga na vita hivyo kwa kusita sana. Ndio sababu Mtume ﷺ aliamuru kuwa Al-'Abbas رضي الله عنه asiuliwe, bali alitekwa tu. Kauli ya Allah تعالی,

سَتَجِدُونََ آخَرِينَ يُرِيدُونَ أَنْ يَأْمَنُوا بِنُصْرَتِكَ وَيَأْمَنُوا قَوْمَهُمْ

"Mtawakuta wengine wanataka wapate salama kwenu na salama kwa watu wao."

Inakusudia aina ya watu kwa juu huonekana kama aina hiyo tuliyoeleza hivi punde. Hata hivyo, nia ya kila aina ni tofauti, kwani hao wa mwisho ni wanafiki. Wanajisingizia kuwa ni Waislamu na wako pamoja na Mtume ﷺ na Maswahaba zake, ili wapate usalama kwa Waislamu kwa ajili ya damu zao, mali zo na familia zao. Hata hivyo, wanawasaidia washirikina kisiri na wanaabudu wanayoyaabudu, ili nao pia kwao kuwe na amani. Watu hao wameungana na washirikina kisiri, kama Allah تعالی Alivyoeleza sifa zao,

كُلِّ مَا رُدُّوْا إِلَى الْفِتْنَةِ أُرِكْسُوا فِيهَا

“Kila wakirudishwa kwenye fitna hudidimizwa humo.”

Aya hii, Allah تعالی Amesema,

فَإِنْ لَّمْ يَعْزُبُوا عَنْكُمْ وَيُلْقُوا إِلَيْكُمْ السَّلَامَ

“Ikiwa hawajitengi nanyi, na wakakuleteeni salama”

Maana yake: Wanaishi katika Fitnah. As-Suddi amesema, Fitnah iliyotajwa hapa ni *Shirk*.¹ Ibn Jarir رحمه الله تعالی ameandika, Mujahid alisema, Ayah hiyo ilishuka kuhusu kikundi cha Makkah kilichozoea kumjia Mtume ﷺ Madinah kujifanya Waislamu. Hata hivyo, waliporejea kwa Maquraysh, walirudia kuabudu masanamu. Walitaka amani pande zote mbili. Allah تعالی Aliamuru kuwapiga, isipokuwa wakijitoa katika watu wanaopigana na kukimbilia amani.² Ndio sababu Allah تعالی Akasema,

وَيَكْفُرُوا بِأَيْدِيهِمْ

“...na wakazuia mikono yao.”

Maana yake: Kurudi katika tabia ya amani na ridhaa, na kujiepusha kukupigeni.

فَاخْذُوهُمْ

“Basi wakamateni”

¹ At-Tabari 9:28.

² At-Tabari 9:27.

وَأَقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ

“Na wauweni popote mnapowakuta.”

Popote mtakapowakuta,

وَأُولَئِكَ جَعَلْنَا لَكُمْ عَلَيْهِمْ سُلْطٰنًا مِّنَّا ﴿٨٦﴾

“Na juu ya hao ndio Tumekupeni hoja zilizo wazi.”

Maana yake: Kauli moja na ithibati ya wazi.

* * *

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ أَنْ يَقْتُلَ مُؤْمِنًا إِلَّا خَطَاً ۖ وَمَنْ قَتَلَ
 مُؤْمِنًا خَطَاً فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُؤْمِنَةٍ وَدِيَةٌ مُسْلَمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهِ
 إِلَّا أَنْ يَصَّدَّقُوا ۗ فَإِنْ كَانَ مِنْ قَوْمٍ عَدُوٍّ لَكُمْ وَهُوَ
 مُؤْمِنٌ فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُؤْمِنَةٍ ۗ وَإِنْ كَانَ مِنْ قَوْمٍ
 بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ فَدِيَةٌ مُسْلَمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهِ وَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ
 مُؤْمِنَةٍ ۗ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ تَوْبَةً مِّنَ اللَّهِ
 ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٩٢﴾ وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا
 مُتَعَمِدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ
 وَلَعَنَهُ وَأَعَدَّ لَهُ عَذَابًا عَظِيمًا ﴿٩٣﴾ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ
 ءَامَنُوا إِذَا ضَرَبْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَتَبَيَّنُوا وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ
 آتَىٰ إِلَيْكُمُ الْإِسْلَامَ لَسَتْ مُؤْمِنًا تَتَّبِعُونَ عَرَضَ
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فَعِنْدَ اللَّهِ مَغَانِمُ كَثِيرَةٌ كَذَلِكَ كُنْتُمْ
 مِن قَبْلُ فَمَنْ بَرَّ اللَّهُ عَلَيْكُمْ فَتَبَيَّنُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ
 بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿٩٤﴾

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ أَنْ يَقْتُلَ مُؤْمِنًا
 إِلَّا خَطَاً ۖ وَمَنْ قَتَلَ مُؤْمِنًا خَطَاً
 فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُؤْمِنَةٍ وَدِيَةٌ مُسْلَمَةٌ إِلَىٰ
 أَهْلِهِ إِلَّا أَنْ يَصَّدَّقُوا ۗ فَإِنْ كَانَ
 مِنْ قَوْمٍ عَدُوٍّ لَكُمْ وَهُوَ مُؤْمِنٌ
 فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُؤْمِنَةٍ ۗ وَإِنْ كَانَ
 مِنْ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ فَدِيَةٌ
 مُسْلَمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهِ وَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُؤْمِنَةٍ
 ۗ فَمَنْ لَمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ
 مُتَتَابِعَيْنِ تَوْبَةً مِّنَ اللَّهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ
 عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٩٢﴾ وَمَنْ يَقْتُلْ
 مُؤْمِنًا مُتَعَمِدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ
 خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَلَعَنَهُ
 وَأَعَدَّ لَهُ عَذَابًا عَظِيمًا ﴿٩٣﴾

92. Na haiwi Muumini kumuwa Muumini ila kwa kukosea. Na mwenye kumuwa Muumini kwa kukosea basi amkomboe mtumwa aliye Muumini, na atoe fidia kuwapa jamaa za maiti, isipokuwa waache wenyewe kuwa ni sadaka. Na akiwa ni jamaa wa maadui zenu, hali yeye ni Muumini, basi ni kumkomboa mtumwa aliye Muumini. Na akiwa ni miongoni wa watu ambao pana ahadi baina yenu na wao basi wapewe fidia watu wake na akombolewe mtumwa Muumini. Na asiyepata, basi afunge miezi miwili mfululizo, kuwa ni toba kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye Hekima.

93. Na mwenye kumuua Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu humo atadumu, na Mwenyezi Mungu Amemkasirikia, na Amemlaani, na Amemuandalia adhabu kubwa.

Hukumu Kuhusu Kumuuu Muumini Kimakosa

Allah تعالی Anaeleza kuwa muumini haruhusiwi kumuua nduguye muumini kwa hali yoyote ile. Katika Sahihi Mbili, kumeandikwa kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا يَجِلُّ دَمُ امْرِئٍ مُسْلِمٍ يَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَنَّي رَسُولُ اللَّهِ، إِلَّا بِإِخْتِي
ثَلَاثٍ: النَّفْسُ بِالنَّفْسِ، وَالنَّيْبُ الزَّانِي، وَالتَّارِكُ لِدِينِهِ الْمَفَارِقُ لِلْجَمَاعَةِ»

“Si halali damu ya Muislamu anayeshuhudia kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah na kwamba mimi ni Mjumbe wa Allah, isipokuwa katika moja ya matatu. (Nayo ni:) nafsi kwa nafsi, mzinifu aliyediriki ndoa, na mwenye kuritadi Dini na kuacha Jama`ah (jamii ya waumini waaminifu).”¹

Mtu anapotenda mojawapo kati ya makosa hayo matatu, wananchi wa kawaida hawapaswi kumuua kwa sababu hilo ni jukumu la kiongozi Muislamu au naibu wake. Kauli ya Allah تعالی,

إِلَّا خَطَاً

“Ila kwa kukosea.”

Kuna rai tofauti tofauti kuhusu sababu ya kushuka sehemu hii ya Ayah. Mujahid na wengine walisema kuwa ilishuka kuhusu ‘Ayyash bin Abi Rabi` ah, ndugu wa Abu Jahl kutoka kwa upande wa mama yake, Asma’ bint Makhrabah. ‘Ayyash alimuua mtu aliyetitwa Al-Harith bin Yazid Al-`Amiri, kutokana na kisasi cha kumtesa yeye na kaka yake kwa sababu ya kusilimu kwao. Mtu huyo baadaye alisilimu na kufanya Hijrah, lakini ‘Ayyash hakulijua hilo. Katika Siku ya ushindi wa Makkan, ‘Ayyash alimuona mtu huyo na akadhani kuwa bado alikuwa kafiri, basi akamshambulia na kumuua. Baadaye, Allah تعالی Alishusha Aya hii.²

¹ Fat’hul Al-Bari 12:209 na Muslim 3:1302.

² At-Tabari 9:82.

'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam alisema kuwa Ayah hii ilishuka kumhusu Abu Ad-Darda'a رضي الله عنه kwa sababu alimua mtu baada ya mtu huyo kusilimu, mara tu Abu Ad-Darda'a رضي الله عنه alipoinua panga juu yake. Jambo hili lilipofikishwa kwa Mtume ﷺ, Abu Ad-Darda'a رضي الله عنه alisema, "Aliyasema hayo ili kuepuka mauti tu." Mtume ﷺ akamuambia,

«هَلَّا شَقَقْتَ عَنْ قَلْبِهِ»

"Uliupasua moyo wake?"¹

Msingi wa kisa hiki ni katika Sahih, lakini hakimhusu Abu Ad-Darda'a رضي الله عنه. Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ قَتَلَ مُؤْمِنًا خَطَاً فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُؤْمِنَةٍ وَدِيَةٌ مُسَلَّمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهِ

"Na mwenye kumuua Muumini kwa kukosea basi amkomboe mtumwa aliye Muumini, na atoe diya kuwapa jamaa za maiti."

Hivyo, kuagiza masharti mawili kwa kuua kimakosa. Sharti la kwanza ni *Kaffarah* (faini) kwa ajili ya dhambi kubwa iliyofanyika, hata kama ilikua kimakosa. Kafara yake ni kumpa uhuru mtumwa Muislamu, sio mtumwa asiye Muislamu. Imam Ahmad ameandika kuwa mtu mmoja kutoka katika Ansar alisema kuwa alimleta kijakazi na kusema, "Ewe Mjumbe wa Allah! Nimempaa uhuru kijakazi, ili uone kama kijakazi huyu ni muumini, nimpe uhuru." Mtume ﷺ akamuuliza,

«أَتَشْهَدِينَ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ؟»

"Je, unashuhudia kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah?"

Akajibu, "Ndiyo." Akamuuliza,

«أَتَشْهَدِينَ أَنِّي رَسُولُ اللَّهِ؟»

"Unashuhudia kuwa mimi ni Mjumbe wa Allah."

Akajibu, "Ndiyo." Akamuuliza,

¹ At-Tabari 9:34.

«أَنْزَمِينَ بِالْبُعْثِ بَعْدَ الْمَوْتِ؟»

“Unaamini kufufuliwa baada ya mauti.”

Akajibu, “Ndiyo.” Mtume ﷺ akasema,

«أَغْنِيهَا»

“Mpe uhuru.”¹

Haya ni masimulizi ya hakika, na kutokujua jina la Sahaba huyo Ansari hakupunguzi uhakika wake. Kauli ya Allah تعالى,

وَدِيَّةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهَا

“Na atoe diya kuwapa jamaa za maiti.”

Ni jukumu la pili linalomhusu muuaji na familia ya aliyeuliwa, ambao watapokea dia kwa kuondokewa na ndugu yao. Diya hiyo inawajibika kutoa mafungu matano ya ngamia. Kama Imam Ahmad, na wakusanyaji wa *Sunan* walivyomnukuu Ibn Mas'ud رضي الله عنهما kuwa alisema; “Mtume ﷺ alihukumu katika mauaji yasiyokuwa ya makusudi, kutoa fidia ya ngamia (*binti makhadhi*) ishirini, na ngamia (*binti labuni*) ishirini, na ngamia (*Jadhaa*) ishirini na ngamia (*Hiqqa*) ishirini.”²

Haya ni kwa mujibu wa lafudhi ya An-Nasa'i. *Diyah* hii inatakiwa itoke kwa wakuu wa kabila la muuaji, si kutoka katika mali yake mwenyewe. Katika Sahihi Mbili, kumeandikwa kuwa Abu Hurayra رضي الله عنه alisema, “Wanawake wawili kutoka Hudhayl waligombana na mmoja wao akamtupia mwenzake jiwe na kumuua yeye na kijusi chake (kilicho tumboni mwake). Wakabishana mbele ya Mtume ﷺ na akaamua kuwa *Diyah* ya kijusi iwe kumpa uhuru mtumwa wa kiume au wa kike. Pia aliamua kuwa *Diyah* ya marehemu itoke kwa wakuu wa kabila la muuaji.”³ Hadithi hii inajulisha kuwa katika hali ya kilichoonekana kama mauaji ya makusudi, *Diyah* ni sawa na ile ya kua kimakosa (lakini si

¹ Ahmad 3:451.

² An-Nasai na. 4799, Ahmad 1:384, Abu Dawud na. 4545, At-Tirmidhi na. 1386 na Ibn Majah. 3641.

³ *Fat'hul Al-Bari* 12:209 na Muslim 3:1309.

bayana). Aina hiyo ya kwanza ina *Diyah* za aina tatu, kama yalivyo mauaji ya kukusudia, kwa sababu ni jambo lililo sawa na mauaji ya kukusudia. Al-Bukhari amenukuu katika Sahihi yake kuwa 'Abdullah bin 'Umar رضي الله عنهما alisema, "Mtume ﷺ alimtuma Khalid bin Al-Walid رضي الله عنه kwenda Banu Jadhimah na akawalingania Uislamu, lakini hawakujua kusema, 'Tumesilimu. 'Wakawa wanasema, 'Saba'na, Saba'na (tumekuwa Masabi). Khalid akaanza kuwaua, na habari hizo zilipofikishwa kwa Mtume ﷺ, aliinua mikono yake na kusema,

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَبْرَأُ إِلَيْكَ مِمَّا صَنَعَ خَالِدٌ»

*"Ewe Allah! Ninajitenga kwako kutokana na alichokifanya Khalid."*¹

Mtume ﷺ alimtuma 'Ali رضي الله عنه kwenda kulipa *Diyah* ya waliouliwa na kulipa fidia kwa mali iliyoharibiwa, mpaka kwa kiasi cha kurejesha hata bakuli la mbwa. Hadithi hii inajulisha kuwa kosa la kiongozi au naibu wake (kwa hapo ni Khalid) linalipwa kutoka katika Hazina ya Waislamu. Kauli ya Allah تعالى،

إِلَّا أَنْ يَصَّدَّقُوا

"Isipo kuwa waache wenyewe kuwa ni sadaka."

Maana yake: *Diyah* lazima wapewe familia ya aliyeuliwa, isipokuwa wakipoteza haki yao, katika hali hiyo *Diyah* haiwi na umuhimu. Kauli ya Allah تعالى،

فَإِنْ كَانَتْ مِنْ قَوْمٍ عَدُوٍّ لَكُمْ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُؤْمِنَةٍ

"Na akiwa ni jamaa wa maadui zenu, hali yeye ni Muumini, basi ni kumkomboa mtumwa aliye Muumini."

Maana yake: Kama aliyeuliwa alikuwa muumini, na familia ya muuaji ni ya makafiri, basi hawatapewa *Diyah*. Katika hali hii, muuaji atatakiwa tu kumpa uhuru mtumwa muumini. Kauli ya Allah تعالى،

وَإِنْ كَانَتْ مِنْ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ

"Na akiwa ni miongoni wa watu ambao pana ahadi baina yenu na wao."

¹ Fat'hul Al-Bari 7:653.

Maana yake: Kama familia ya aliyeuliwa ilitokana na *Ahl Adh-Dhimmah* au ambayo ina mkataba wa amani, basi wanastahiki *Diyah*; *Diyah* kamili kama aliyeuliwa alikuwa muumini, katika,

فَمَنْ لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ

“Na asiyepata, basi afunge miezi miwili mfululizo.”

Bila ya kukatisha saumu (katika siku za) miezi miwili. Kama atakatisha saumu bila ya uhalali, yaani ugonjwa, damu ya uzazi, basi atapaswa aanze upya. Kauli ya Allah تعالیٰ,

تَوْبَةٌ مِّنَ اللَّهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٣٧﴾

“Kuwa ni toba kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye Hekima.”

Maana yake: Hivi ndivyo anayeuua kimakosa anavyoweza kutubu, atafunga miezi miwili mfululizo kama hatampata mtumwa wa kumpa uhuru.

وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٣٧﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye Hekima.”

Tulishaeleza hapo mapema.

Onyo Juu ya Mauaji ya Makusudi

Baada ya Allah تعالیٰ kutaja hukumu ya mauaji yasiyo ya makusudi, Ametaja hukumu ya mauaji ya makusudi.

Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُّتَعَمِّدًا

“Na mwenye kumuua Muumini kwa kukusudia.”

Ayah hii ina onyo kali kwa wenye kutenda dhambi kubwa iliyotajwa pamoja na Shirk katika Ayat nyingi za Kitabu cha Allah تعالیٰ. Kwa mfano, katika *Surat Al-Furqan*. Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ

“Na ambao hawamuombi pamoja na Mwenyezi Mungu mola mwingine, wala hawau nafsi ambayo Allah Ameiharamisha ila kwa haki.” (25:68)

Kauli ya Allah تعالى،

﴿ قُلْ تَعَالَوْا أَتْلُ مَا حَرَّمَ رَبِّيَ عَلَيْكُمْ عَلَىٰ شَيْءٍ

“Sema: Njooi nikusomeeni Aliyokuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote.” (6:151)

Kuna Ayat na Hadithi nyingi zinazokataza mauaji. Katika Sahihi Mbili, kumeandikwa kuwa Ibn Mas‘ud رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

﴿أَوَّلُ مَا يُفْضَىٰ بَيْنَ النَّاسِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِي الدَّمَاءِ﴾

“Ya kwanza kuhukumiwa baina ya watu katika Siku ya Kiama ni katika damu.”¹

Katika Hadithi aliyoinukuu Abu Dawud, ‘Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه anaeleza kuwa Mtume ﷺ amesema,

﴿لَا يَزَالُ الْمُؤْمِنُ مُغْنِيًا صَالِحًا، مَا لَمْ يُصَبَّ دَمًا حَرَامًا، فَإِذَا أَصَابَ دَمًا حَرَامًا بَلَغَ﴾

“Muumini ataendelea kuwa mwema mtiifu, madamu hamwagi damu iliyoharamishwa. Anapomwaga damu, atakuwa na mizigo.”²

Hadithi nyingine inaeleza,

¹ Fat’hul Al-Bari 11:402 na Muslim 3:1304.

² Abu Dawud na. 4270, Jami’ Al-Masaniid 7:143.

«لَرَوَّالِ الدُّنْيَا أَهْوُونَ عِنْدَ اللَّهِ مِنْ قَتْلِ رَجُلٍ مُسْلِمٍ»

“Kuondoka dunia ni rahisi sana kwa Allah تعالى kuliko kumuua mtu Muislamu,”¹

Je, Toba ya Wanaoua kwa Makusudi, Inapokelewa?

Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alishikilia rai kuwa toba ya anayeuua muumini makusudi, haikubaliwi. Al-Bukhari ameandika kuwa Ibn Jubayr alisema, “Wasomi wa Al-Kufah walitofautiana kuhusu hilo, nilikwenda kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما kumuuliza hilo. Akasema, ‘Aya hii,

وَمَنْ يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُتَعَمِدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ

“Na mwenye kumuua Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu.”

Ilishuka kwa ajili hiyo na nyingine ikaifuta.² Muslim³ na An-Nasa’i⁴ pia wameinukuu. Hata hivyo, wanazuoni wengi wa *Salaf* na *Khalaf* walisema, toba ya muuaji inakubaliwa kama atatubu na kurejea kwa Allah تعالى kwa unyenyekevu, kwa kujisalimisha, na kufanya mema, basi Allah تعالى Atabadili maovu yake kuwa mema na kufidia hasara ya aliyeuliwa kwa kumpa malipo kwa sababu ya kuteseka kwake. Kauli ya Allah تعالى,

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ

“Na ambao hawamuombi pamoja na Mwenyezi Mungu mola mwingine...” (25:68) Mpaka,

إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا

“Isipokuwa mwenye kutubu na akafanya amali njema.” (19:60)

¹ *Tuhfat Al-Ahwadhi* 4:652.

² *Fat’hul Al-Bari* 8:106.

³ Muslim 4:2318.

⁴ An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:326.

Aya tuliyotaja hapo isitazamwe kama iliyofutwa au inatumika kwa makafiri waliosilimu tu, kwani hilo linakinzana na ufahamu wa ujumla wenye kuenea wa Aya hiyo na inahitaji ushahidi wa unaoiunga mkono. Allah تعالى Anajua zaidi. Kauli ya Allah تعالى,

﴿ قُلْ يٰعِبَادِيَ الَّذِينَ اَسْرَفُوْا عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوْا مِنْ رَّحْمَةِ اللّٰهِ ۗ

“Sema: enyi waja wangu ambao wamedhulumu nafsi zao msikate tamaa na Rehema ya Allah...”, (39:53)

Aya hii ni ya ujumla, inazingira kila aina ya madhambi, pamoja na kufuru, shirki, mashaka, unafiki, mauaji, dhambi, na kadhalika. Kwa hiyo, kila anayetubu kwa moyo safi dhidi ya makosa hayo, basi Allah تعالى Atamsamehe. Kauli ya Allah تعالى,

﴿ اِنَّ اللّٰهَ لَا يَغْفِرُ اَنْ يُشْرَكَ بِهٖ وَيَغْفِرُ مَا دُوْرَ ذٰلِكَ لِمَنْ يَّشَآءُ ۗ

“Hakika Allah Hasamehe kushirikishwa na Anasamehe yasiyokuwa hayo, kwa Amtakaye...”, (4:116)

Aya hii ni ya ujumla na inajumuisha kila dhambi isipokuwa Shirki, na imetajwa katika Surah hii, baada ya Ayah hii na kabla yake, ili kuhimiza kumtumaini Allah تعالى, na Allah تعالى Anajua zaidi. Imethibiti katika Sahihi Mbili, kuwa muisraeli aliuwa watu mia moja halafu akamuuliza msomi, “Je, inawezekana kwangu kufanya toba?” Akamjibu, “Nini kitakachokuzuia kutubu.” Basi, akamueleza aende katika ardhi nyingine ambapo Allah تعالى Alikuwa akiabudiwa. Akaanza kuhamia huko lakini akafariki njiani, na malaika wa rehema ndiye waliyemchukua.¹ Ingawa Hadithi hii inamhusu muisraeli, inaifaa zaidi jamii ya Kiislamu kuwa toba yao ikubaliwe. Kwa hakika, Allah تعالى Aliwaondolea mizigo na vikwazo walivyowekewa Mayahudi, na akamtuma Mtume wetu kwa kuleta njia nyepesi ya *Hanifiyyah*. Kama inavyoeleza Aya tukufu,

﴿ وَمَنْ يَّقْتُلْ مُؤْمِنًا مُّتَعَمِّدًا

“Na mwenye kumuwa Muumini kwa kukusudia.” Abu Hurayrah رضي الله عنه na wengi katika *Salaf* walisema kuwa hii ndiyo adhabu yake, kama Allah تعالى Ataamua kumuadhibu. Na hii ndio hali ya kila kitisho kinachotolewa kwa kila

¹ *Fat'hul Al-Bari* 6:591 na *Muslim* 4:2118.

dhambi. Kwa mfano, kunaweza kuwa na amali njema alizofanya zitakazomzuia asiadhibiwe kwa hilo, na Allah تعالى Anajua zaidi. Hata kama muuaji atalazimika kuingia Motoni - kama Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alivyoeleza kwa sababu toba yake haikukubaliwa, au hakuwa na amali njema za kumnusuru, hatabakia huko milele, bali kwa muda mrefu. Kuna hadithi *Mutawatir* zinazoeleza kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّهُ يُخْرِجُ مِنَ النَّارِ مَنْ كَانَ فِي قَلْبِهِ أُذُنِي ذَرَّةً مِنْ إِيْمَانِهِ»

*"Mwenye chembe ya imani moyoni mwake hatimaye atatoka motoni."*¹

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا ضَرَبْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَتَبَيَّنُوا وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ أَلْقَى إِلَيْكُمُ
الْسَّلَامَ لَسْتَ مُؤْمِنًا تَبْتَغُونَ عَرَضَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فَعِنْدَ اللَّهِ مَغَانِمٌ كَثِيرَةٌ
كَذَلِكَ كُنْتُمْ مِنْ قَبْلُ فَمَنْ ءَلَّهُ عَلَيْكُمْ فَتَبَيَّنُوا إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ

خَيْرًا ﴿٩٤﴾

94. Enyi mlio amini! Mnapo safiri katika njia ya Mwenyezi Mungu basi hakikisheni, wala msimuambie anayekutoleeni salamu: Wewe si Muumini; kwa kutaka manufaa ya maisha ya dunia hii, hali ya kuwa kwa Mwenyezi Mungu zipo ghanima nyingi. Hivyo ndivyo mlivyo kuwa nyinyi zamani, na Mwenyezi Mungu Akakunemesheni. Basi chunguzeni sawa sawa. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo Habari za mnayo yatenda.

Maamkizi ya Salam ni Dalili ya Uislamu

Imam Ahmad ameandika kuwa 'Ikrimah alisema kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Mtu mmoja kutoka kwa Bani Sulaym, aliyekuwa akihudumia kundi la kondoo, aliwakuta baadhi ya Masahaba wa Mtume ﷺ na akawatolea Salam. Wakaambizana, 'Ametoa Salam ili ajikinge dhidi yetu. 'Kisha wakamshambulia na kumuua. Wakawaleta kondoo wake kwa Mtume ﷺ, na Aya hii ilishuka,

¹ Al-Bukhari na. 44, 7509 na At-Tirmidhi na. 2598.

يٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا

"Enyi mlio amini!", mpaka mwisho wa Aya hiyo.¹ At-Tirmidhi aliinukuu katika (sura ya) *Tafsir* na akasema, "Hadithi hii ni *Hasan*, na pia imesimuliwa kutoka kwa Usamah bin Zayd رضي الله عنه."² Al-Hakim pia ameinukuu na kusema, "Isnadi yake ni *Sahih*, lakini hawakuikusanya."³ Al-Bukhari ameandika kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema;

يٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا ضَرَبْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ

"Enyi mlio amini! Mnapo safiri katika njia ya Mwenyezi Mungu."

"Mtu mmoja alikuwa anawahudumia kondoo wake na Waislamu wakamkuta. Akasema, 'As-Salamu 'Alaykum.' Hata hivyo, walimuua na kuchukua kondoo wake. Allah تعالى Akashusha Aya;

وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ ءَلْفَىٰ إِلَيْكُمْ ءالسَّلَامَ لَسْتَ مُؤْمِنًا تَبْتَغُونَ عَرَضَ الْحَيٰوةِ الدُّنْيَا

"...wala msimwambie anayekutoleeni salamu: Wewe si Muumini; kwa kutaka manufaa ya maisha ya dunia hii."

Ibn 'Abbas رضي الله عنهما amesema; "mali za duniani zilikuwa kondoo hao." na akasoma,

ءالسَّلَامَ

"Salamu"⁴ Imam Ahmad ameandika kuwa Al-Qa'qa' bin Abdullah bin Abi Hadrad amesimulia kuwa baba yake, 'Abdullah bin Abi Hadrad رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alitutuma kwenda Idam. Niliendesha mnyama nikiwa pamoja na kikundi cha Waislamu akiwemo Abu Qatadah, Al-Harith bin Rab' i na Muhallam bin Juthamah bin Qays. Tulienda mpaka tukafika Idam, ambapo 'Amr bin Al-Adbat Al-Ashja' i alitukuta akiwa juu ya ngamia wake. Alipotukuta alitutolea Salam, na sisi hatukumshambulia. Kwa sababu ya matatizo na ugomvi waliokuwa nao, Muhallam bin Juthamah alimuua na kuchukua ngamia wake. Waliporejea kwa Mtume ﷺ na kumueleza kilichotokea, sehemu ya Qur'an ilishuka kutuhusu,

¹ Ahmad 1:272.

² *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:386.

³ Al-Hakim 2:235.

⁴ *Fat'hul Al-Bari* 8:107.

يَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا صَرَّتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ

“Enyi mlio amini! Mnapo safiri katika njia ya Mwenyezi Mungu.” mpaka,

حَبِيرًا

“Khabiyraa.” Ahmad peke yake amenukuu Hadithi hii.¹ Al-Bukhari ameandika kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alimuambia Al-Miqdad رضي الله عنه,

«إِذَا كَانَ رَجُلٌ مُؤْمِنٌ يُخْفِي إِيمَانَهُ مَعَ قَوْمٍ كُفَّارٍ فَأُظْهِرَ إِيمَانَهُ فَتَتَلْتُهُ، فَكَذَلِكَ كُنْتُ أَنْتَ تُخْفِي إِيمَانَكَ بِمَكَّةَ مِنْ قَبْلِ»

“Iwapo mtu muumini anaficha imani yake pamoja na watu makafiri, akadhihirisha imani yake wakamuua. Basi vilevile wewe ulikuwa unaficha imani yako Makkah hapo kabla.”

Al-Bukhari amenukuu toleo hili fupi bila ya isnadi kamili ya wasimulizi.² Hata hivyo toleo refu zaidi lenye isnadi iliyoungana ya wasimulizi pia imenukuliwa. Al-Hafidh Abu Bakr Al-Bazzar رحمه الله تعالى ameandika kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mtume ﷺ alituma jeshi chini ya uongozi wa Al-Miqdad bin Al-Aswad na walipofika mahali palipokusudiwa, waliwakuta watu wameshatawanyika. Hata hivyo, mtu mmoja mwenye mali nyingi hakuondoka na akasema, ‘Nashuhudia kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى.” Lakini, Al-Miqdad رضي الله عنه alimuua, na mtu mmoja akamuambia, ‘Umemuua mtu baada ya kutamka: “Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى. Naapa kwa Allah nitamtajia Mtume ﷺ ulichofanya.” Waliporejea kwa Mtume ﷺ, walisema, ‘Ewe Mtume! Al-Miqdad amemuua mtu aliyeshuhudia kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى.” Akasema,

«ادْعُوا لِيِ الْمَقْدَادَ، يَا مَقْدَادُ! أَقْتَلْتَ رَجُلًا يَقُولُ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، فَكَيْفَ لَكَ بِإِلَهِ إِلَّا اللَّهُ غَدًا؟»

“Niitieni Al-Miqdad. (Alipofika alimuuliza) Ewe Miqdad! Umemuua mtu aliyetamka ‘hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah (Laa ila-ha illa Allah), Nani atakayekutetea wewe na kalima ya Tawhidi (iliyotamkwa na uliyemuua) siku ya kiyama?”

¹ Ahmad 6:11. Masimulizi haya si sahihi.

² Al-Bukhari 68:66.

Kisha Allah تعالى Akashusha;

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا إِذَا ضَرَبْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَتَبَيَّنُوا وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ آتَىٰ إِلَيْكُمُ
السَّلَامَ لَسْتَ مُؤْمِنًا تَبْتَغُونَ عَرَضَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فَعِنْدَ اللَّهِ مَغَانِمٌ كَثِيرَةٌ
كَذَٰلِكَ كُنْتُمْ مِّن قَبْلُ فَمَنْ ءَلَّهُ عَلَيْكُمْ فَتَبَيَّنُوا

“Enyi mlioamini! Mnaposafiri katika njia ya Mwenyezi Mungu basi hakikisheni, wala msimuwambie anaye kutoleeni salamu: Wewe si Muumini; kwa kutaka manufaa ya maisha ya dunia hii, hali ya kuwa kwa Mwenyezi Mungu zipo ghanima nyingi. Hivyo ndivyo mlivyo kuwa nyinyi zamani, na Mwenyezi Mungu Akakunemesheni. Basi chunguzeni sawa sawa.”

Mtume ﷺ alimuambia Al-Miqdad رضي الله عنه ،

«كَانَ رَجُلٌ مُّؤْمِنٌ يُخْفِي إِيمَانَهُ مَعَ قَوْمٍ كُفَّارٍ فَأَظْهَرَ إِيمَانَهُ فَفَتَنَتْهُ، فَكَذَلِكَ كُنْتَ أَنْتَ
تُخْفِي إِيمَانَكَ بِمَكَّةَ مِنْ قَبْلُ»

“Kulikuwa na mtu muumini anaificha imani yake baina ya makafiri, na amekutamkieni imani yake, lakini ukamuua, wakati huo huo ulikuwa ukificha imani yako hapo kabla, muda ukiwa Makkah.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

فَعِنْدَ اللَّهِ مَغَانِمٌ كَثِيرَةٌ

“Hali ya kuwa kwa Mwenyezi Mungu zipo ghanima nyingi.”

Maana yake: Bora zaidi kuliko mali za kidunia ulizotamani na kukufanya umuue aliyekutolea Salam na kukutamkia imani yake. Lakini, uliyapuuza yote hayo na kumtuhumu unafiki, ili kupata mali za kidunia. Hata hivyo, mali halisi iliyoko kwa Allah تعالى ni bora zaidi kuliko uliyoyapata. Kauli ya Allah تعالى،

كَذَٰلِكَ كُنْتُمْ مِّن قَبْلُ فَمَنْ ءَلَّهُ عَلَيْكُمْ

“Hivyo ndivyo mlivyo kuwa nyinyi zamani, na Mwenyezi Mungu Akakunemesheni.”

¹ Majma' Az-Zawaid 5:9.

Maana yake: Hapo kabla, ulikuwa katika hali hiyo hiyo kama mtu huyu aliyeficha imani yake dhidi ya watu wake. Tumeshazitaja Hadithi husika hapo juu.

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَذْكُرُوا إِذْ أَنْشَرْتُمْ قَلِيلًا مُسْتَضْعَفُونَ فِي الْأَرْضِ

“Na kumbukukeni mlipokuwa wachache mlipodhoofishwa katika ardhi.” (8:26)

'Abdur-Razzaq ameandika kuwa Sa' id bin Jubayr alisema kuhusu Kauli ya Allah تعالى،

كَذَلِكَ كُنْتُمْ مِّن قَبْلُ

“Hivyo ndivyo mlivyo kuwa nyinyi zamani.”

“Ulikuwa ukificha imani yako, kama mchungu kondoo alivyoificha imani yake.”¹

Kauli ya Allah تعالى،

فَتَبَيَّنُوا

“Basi chunguzeni sawa sawa.”

Kisha Akasema،

إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿٤٤﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Anazo Habari za mnayo yatenda.”

Na sehemu hii ya Aya ina kitisho na onyo, kama Sa' id bin Jubayr alivyoeleza.

* * *

¹ 'Abdur-Razzaq 1:170

لَا يَسْتَوِي الْقَاعِدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ غَيْرُ أُولِي الضَّرَرِ
 وَالْمُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ ۚ فَضَّلَ اللَّهُ
 الْمُجَاهِدِينَ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ عَلَى الْقَاعِدِينَ دَرَجَةً ۗ وَكُلًّا
 وَعَدَّ اللَّهُ الْحَسَنَى ۗ وَفَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَاهِدِينَ عَلَى الْقَاعِدِينَ
 أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٩٥﴾ دَرَجَاتٍ مِّنْهُ وَمَغْفِرَةً وَرَحْمَةً ۗ وَكَانَ اللَّهُ
 غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٩٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّيْتُمُ الْمَلَائِكَةَ ظَالِمِي
 أَنْفُسِهِمْ قَالُوا فِيهِمْ كُمْ ۗ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ ۗ
 قَالُوا أَلَمْ نَكُنْ أَرْضَ اللَّهِ وَسِعَةً فَنُهَاجِرُوا فِيهَا ۗ فَأُولَئِكَ
 مَاؤُنْهُمُ جَهَنَّمُ ۗ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٩٧﴾ إِلَّا الْمُسْتَضْعَفِينَ
 مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ لَا يَسْتَطِيعُونَ حِمْلَهُ وَلَا
 يَهْتَدُونَ سَبِيلًا ﴿٩٨﴾ فَأُولَئِكَ عَسَى اللَّهُ أَنْ يَعْفُوَ عَنْهُمْ ۗ
 وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٩٩﴾ * وَمَنْ يُهَاجِرْ فِي سَبِيلِ
 اللَّهِ يَجِدْ فِي الْأَرْضِ مُرَاعِمًا كَثِيرًا وَسِعَةً ۗ وَمَنْ يَخْرُجْ مِنْ
 بَيْتِهِ مُهَاجِرًا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ يُدْرِكْهُ الْمَوْتُ فَقَدْ وَقَعَ
 أَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿١٠٠﴾ وَإِذَا ضَرَبْتُمْ
 فِي الْأَرْضِ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ إِنْ
 خِفْتُمْ أَنْ يَفْتِنَكُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا ۗ إِنَّ الْكَافِرِينَ كَانُوا لَكُمْ
 عَدُوًّا مُّبِينًا ﴿١٠١﴾

لَا يَسْتَوِي الْقَاعِدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ
 غَيْرُ أُولِي الضَّرَرِ وَالْمُجَاهِدُونَ فِي
 سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ ۚ فَضَّلَ
 اللَّهُ الْمُجَاهِدِينَ بِأَمْوَالِهِمْ وَأَنْفُسِهِمْ
 عَلَى الْقَاعِدِينَ دَرَجَةً ۗ وَكُلًّا وَعَدَّ اللَّهُ
 الْحَسَنَى ۗ وَفَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَاهِدِينَ عَلَى
 الْقَاعِدِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٩٥﴾
 دَرَجَاتٍ مِّنْهُ وَمَغْفِرَةً وَرَحْمَةً ۗ وَكَانَ
 اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٩٦﴾

95. Hawawi sawa Waumini wanaokaa tu wala hawana dharura, na wale wanao-pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Mwenyezi Mungu Amewatukuza cheo wale wanaopigana kwa mali yao na nafsi zao kuliko wale wanaokaa tu. Ingawa Mwenyezi Mungu Amewahidi wote mashukio mema, lakini Mwenyezi Mungu Amewafadhili wanaopigana kwa ujira mkubwa kuliko wanaokaa tu.

96. Ni vyeo hivyo vinavyotoka Kwake, na Maghfira na Rehema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira na Mwenye Kurehemu.

Mujahid na Wasiojiunga na Jihadi Hawalingani, [na Jihad ni Fardh Kifayah]¹

Al-Bukhari ameandika kuwa Al-Bara' alisema, "Aya,

لَا يَسْتَوِي الْقَاعِدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

"Hawawi sawa Waumini wanaokaa tu."

Iliposhuka, Mtume ﷺ alimuita Zayd na kumuamuru kuiandika. Kisha, Ibn Umm Maktum رضي الله عنه alikuja na kusema kuwa alikuwa kipofu. Allah تعالى Akashusha,

غَيْرُ أُولَى الضَّرِّ

"Wala hawana dharura."²

Bukhari ameandika kuwa Sahl bin Sa' d As-Sa'di alisema, "Nilimuona Marwan bin Al-Hakam ameketi Masjid. Nilikuja na kuketi karibu yake. Alituambia kuwa Zayd bin Thabit رضي الله عنه alimuambia kuwa Mtume ﷺ alimsomea Aya hii,

لَا يَسْتَوِي الْقَاعِدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ غَيْرُ أُولَى الضَّرِّ وَالْمُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ

"Hawawi sawa Waumini wanaokaa tu wala hawana dharura, na wale wanaopigana katika njia ya Mwenyezi Mungu."

Ibn Umm Maktum رضي الله عنه alikuja kwa Mtume ﷺ alipokuwa akinisomea Aya hiyo. Ibn Umm Maktum رضي الله عنه alisema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Naapa kwa Allah تعالى, kama ningeweza, kwa hakika ningekiunga katika Jihad." Alikuwa kipofu.

Hivyo, Allah تعالى Akateremsha ufunuo kwa Mjumbe Wake na wakati huo paja lake lilikuwa juu ya la kwangu na likawa zito sana kwangu kiasi kwamba nilihofia kuwa paja langu lingevunjika. Hayo yaliisha baada ya Allah تعالى Kushusha,

¹ Kichwa hiki cha habari kimeongezwa hapa kwa manufaa ya wasomaji.

² Fat'hul Al-Bari 8:108.

غَيْرُ أُولَى الصَّرِيرِ

“Wala hawana dharura.”¹

Haya yamenukuliwa na Al-Bukhari. At-Tirmidhi ameandika kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema,

لَا يَسْتَوِي الْقَعِيدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ غَيْرُ أُولَى الصَّرِيرِ

“Hawawi sawa Waumini wanaokaa tu wala hawana dharura.”

Inakusudia wale ambao hawakwenda katika vita vya Badr na waliokwenda mpaka Badr.

Vita vya Badr vilipokaribia kuanza, Abu Ahmad bin Jahsh na Ibn Umm Maktum رضي الله عنهما walisema, ‘Sisi ni vipofu, Ewe Mjumbe wa Allah! Je, tuna udhuru?’ Aya,

لَا يَسْتَوِي الْقَعِيدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ غَيْرُ أُولَى الصَّرِيرِ

“Hawawi sawa Waumini wanaokaa tu wala hawana dharura.”

Ilishuka. Allah تعالى Aliwafanya wanaopigana kuwa juu ya wanaobakia majumbani ambao hawakuzuliwa kwa sababu ya ulemavu.

وَفَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَاهِدِينَ عَلَى الْقَعِيدِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٩٥﴾ دَرَجَاتٍ مِّنْهُ

“...na Mwenyezi Mungu Amewafadhili wanaopigana kwa ujira mkubwa kuliko wanao kaa tu. Ni vyeo hivyo vinavyo toka Kwake.”

“Juu ya Waumini wanaokaa nyumbani bila ya ulemavu unaowazuia.” Hayo ni maneno aliyonukuu At-Tirmidhi, ambaye alisema, “Hasan Gharib.”²

Kauli ya Allah تعالى,

لَا يَسْتَوِي الْقَعِيدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

“Hawawi sawa Waumini wanaokaa tu.”

Hii ni ya ujumla. Baadaye kidogo, ufunuo ulishuka pamoja na,

¹ Fat’hul Al-Bari 8:108.

² Tuhfat Al-Ahwadhi 8:388.

غَيْرُ أُولَى الضَّرَرِ

“...wala hawana dharura,”

Basi yeyote mwenye ulemavu, kama vile upofu, unyong’onyevu, au maradhi yanayowazuia kujiunga katika Jihad, hawakulinganishwa na Mujahidina wanaojitahidi katika njia ya Allah تعالى kwa nafsi zao na mali zao, kama walivyokuwa wale wasio na ulemavu na hawakujiunga katika jihadi. Katika Sahihi yake, Al-Bukhari ameandika kuwa Anas رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ بِالْمَدِينَةِ أَقْوَامًا مَا سِرْتُمْ مِنْ مَيْبِرٍ، وَلَا قَطَعْتُمْ مِنْ وَادٍ، إِلَّا وَهُمْ مَعَكُمْ فِيهِ»
قالوا: وهم بالمدينة يا رسول الله؟

“Kuna watu ambao walibakia Madina, ambao walikuwa pamoja nanyi katika kila kutembea mlilotembea na kila bonde mlilovuka.”

Walisema, “Walipokuwa wakingali Madina, Ewe Mjumbe wa Allah?” akasema,

«نَعَمْ حَبَسَهُمُ الْعُدْرَةُ»

“Ndiyo. Udhuru tu ndio uliowazuia wao (kujiunga nanyi).”¹

Kauli ya Allah تعالى,

وَكُلًّا وَعَدَ اللَّهُ الْحُسْنَىٰ

“Ingawa Mwenyezi Mungu Amewaahidi wote mashukio mema.”

Maana yake: Peponi na malipo makubwa. Ayah hii inajulisha kuwa Jihad si Fardhi kwa kila mmoja, bali ni *Fardh Kifayah* (jukumu la wote).

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَفَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَاهِدِينَ عَلَى الْقَاعِدِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٦٠﴾

“...lakini Mwenyezi Mungu Amewafadhili wanaopigana kwa ujira mkubwa kuliko wanaokaa tu.”

¹ Fat’hul Al-Bari 7:732.

Allah تعالى Anataja kuwapa vyumba Peponi, pamoja na msamaha Wake na rehema nyingi na baraka juu yao, kama upendeleo na utukufu kutoka Kwake. Hivyo, Alisema;

﴿٩٦﴾ دَرَجَاتٍ مِّنْهُ وَمَغْفِرَةً وَرَحْمَةً ۚ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٩٧﴾

“Ni vyeo hivyo vinavyotoka Kwake, na Maghfira na Rehema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira na Mwenye Kurehemu.”

Katika Sahihi Mbili, kumeandikwa kuwa Abu Sa'id Al-Khudri رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«إِنَّ فِي النِّجْوَةِ مِائَةَ دَرَجَةٍ، أَعَدَّهَا اللَّهُ لِلْمُجَاهِدِينَ فِي سَبِيلِهِ، مَا بَيْنَ كُلِّ دَرَجَتَيْنِ كَمَا بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ»

“Hakika katika Pepo kuna daraja mia moja, ambazo Allah تعالى Amewaandalia Mujahidin katika Njia Yake, baina ya daraja mbili ni masafa baina ya mbingu na Ardhi.”¹

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّيْتُمُ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ قَالُوا فِيهِمْ مِّمَّنْ كُنْتُمْ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّهِ وَسِعَةً فَتُهَاجِرُوا فِيهَا فَأُولَئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٩٦﴾ إِلَّا الْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ لَا يَسْتَطِيعُونَ حِيلَةً وَلَا يَهْتَدُونَ سَبِيلًا ﴿٩٧﴾ فَأُولَئِكَ عَسَى اللَّهُ أَنْ يَعْفُوَ عَنْهُمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٩٨﴾ *
وَمَنْ يُهَاجِرْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يَجِدْ فِي الْأَرْضِ مُرَاعِمًا كَثِيرًا وَسَعَةً ۗ وَمَنْ يَخْرُجْ مِنْ بَيْتِهِ مُهَاجِرًا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ يُدْرِكْهُ الْمَوْتُ فَقَدْ وَقَعَ أَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٩٩﴾

97. Hakika Malaika watawaambia wale ambao wamewafisha nao wamejidhulumu nafsi zao: Mlikuwa vipi? Watasema: Tulikuwa tunaonewa. Watawaambia: Kwani ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa na wasaa wa kuhamia humo? Basi hao makazi yao ni Jahannamu, nayo ni marejeo mabaya kabisa.

¹Muslim 5:1501.

98. Isipo kuwa wale waliokuwa wanyonge miongoni mwa wanaume na wanawake na watoto wasio na uweza wa hila ya kuongoza njia ya kuhama.

99. Basi hao huenda Mwenyezi Mungu Akawasamehe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Maghfira.

100. Na mwenye kuhama katika njia ya Mwenyezi Mungu atapata pengi duniani pa kukimbilia, na atapata wasaa. Na anayetoka nyumbani kwake kuhama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, kisha yakamfika mauti njiani basi umethibiti ujira wake kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Maghfira na Mwenye Kurehemu.

Kukatazwa Kuishi Pamoja na Makafiri Huku Uwezekano wa Kuhama Upo

Al-Bukhari ameandika kuwa Muhammad bin 'Abdur-Rahman, Abu Al-Aswad, alisema, "Watu wa Madinah walilazimishwa kuandaa jeshi (ili kupigana dhidi ya watu wa Ash-Sham katika kipindi cha Khilafah ya Abdullah bin Az-Zubayr huko Makkah, nami niliandikishwa jeshini. Kisha nikakutana na 'Ikrimah, mtumwa aliyepewa uhuru na Ibn 'Abbas رضي الله عنهما, na kumjulisha (hayo), na akanikataza sana kufanya hivyo, (Maana yake: kujiandikisha katika jeshi hilo), na akaniambia, 'Ibn 'Abbas رضي الله عنهما aliniambia kuwa baadhi ya Waislamu walikuwa wakitoka pamoja na washirikina kwa kuzidisha ukubwa wa jeshi lao dhidi ya Mtume ﷺ. Kisha mshale ulikuwa ukimchoma mmoja wao na kumuua, au alikatwa shingo (kwa panga) na kufa, na Allah تعالى Akashusha Aya,

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّيْنَاهُمْ لَمَلَكَاتُكَ ظَالِمِي أَنْفُسِهِمْ

"Hakika Malaika watawaambia wale ambao wamewafisha nao wamejidhulumu nafsi zao:"¹

Adh-Dhahhak alieleza kuwa Aya hii ilishuka kuhusu baadhi ya wanafiki waliojiunga na Mtume ﷺ lakini wakabakia Makkah na wakatoka pamoja na washirikina kwa ajili ya vita vya Badr. Waliuliwa pamoja na waliouliwa. Hivyo,

¹ Fat'hul Al-Bari 8:111.

Aya hii tukufu ikashuka¹ kuhusu walioishi pamoja na washirikina, huku wakiwa na uwezo wa kufanya Hijrah na kushindwa kutekeleza imani. Watu wa aina hiyo watakuwa wanajidhulumu wenyewe na kuangukia katika haramu kwa mujibu wa muafaka wa wanazuoni na pia kwa mujibu wa Aya hii,

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّيْتَهُمُ الْمَلَائِكَةُ ظَالِمِي أَنْفُسِهِمْ

“Hakika Malaika watawaambia wale ambao wamewafisha nao wamejidhulumu nafsi zao.”

Kwa kukusudia kutofanya Hijrah,

قَالُوا فِيهِمْ كُنْتُمْ

“‘Mlikuwa vipi?’ Watasema:”

Maana yake: Kwanini mmebakia hapa na hamkufanya Hijrah,

قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي الْأَرْضِ²

“Watasema: Tulikuwa tunaonewa katika ardhi.”

Maana yake: Hatuwezi kuachana na ardhi tunayoishi na kufanya Hijrah,

قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةً

“Watawaambia: Kwani ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa na wasaa...”

Abu Dawud ameandika kuwa Samurah bin Jundub رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَنْ جَامَعَ الْمُشْرِكَ وَسَكَنَ مَعَهُ فَإِنَّهُ مِثْلُهُ»

“Mwenye kuchanganyika na mshirikina na kuishi naye, naye ni kama yeye.”²

¹ At-Tabari 9:108.

² Abu Dawud 3:224.

Kauli ya Allah تعالى،

إِلَّا الْمُسْتَضْعِفِينَ

“Isipokuwa wale walio kuwa wanyonge...”

Mpaka mwisho wa Aya, ni dharura ambayo Allah تعالى Anawapa watu wa aina hii kutokuhama, kwa sababu hawawezi kujiondoa kutoka kwa washirikina. Na hata wakifanya hivyo, hawatajua njia ya kwenda.

Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

لَا يَسْتَطِيعُونَ حِيلَةً وَلَا يَهْتَدُونَ سَبِيلًا ﴿٩٥﴾

“Wasio na uweza wa hila ya kuongoza njia ya kuhama.”

Maana yake: Hawapati njia ya kuhama, Mujahid, 'Ikrimah na As-Suddi walisema.¹ Kauli ya Allah تعالى،

فَأَوْلَيْتِكَ عَسَى اللَّهُ أَنْ يَعْفُوَ عَنْهُمْ

“Basi hao huenda Mwenyezi Mungu Akawasamehe.”

Maana yake: Awasamehe kwa kutohama, na hapa, 'inawezekana' inamaanisha Atafanya hivyo،

وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٩٦﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe, Mwingi wa Maghfira.”

Al-Bukhari ameandika kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Huku Mtume ﷺ akiwa katika Sala ya 'Isha', alisema, 'Sami` Allahu Liman Hamidah. 'Halafu kabla ya kwenda kusujudu, alisema،

«اللَّهُمَّ أَنْجِ عِيَّاشَ بْنَ أَبِي رَبِيعَةَ، اللَّهُمَّ أَنْجِ سَلَمَةَ بْنَ هِشَامٍ، اللَّهُمَّ أَنْجِ الْوَلِيدَ بْنَ الْوَلِيدِ، اللَّهُمَّ أَنْجِ الْمُسْتَضْعِفِينَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ، اللَّهُمَّ اشْدُدْ وَطْأَتَكَ عَلَيَّ مُضْرًا، اللَّهُمَّ اجْعَلْهَا سِنِينَ كَسِنِي يُوسُفَ»

¹ At-Tabari 9:111.

*"Ewe Allah! Mnusuru 'Ayyash bin Abi Rabi`ah. Ewe Allah! Mnusuru Salamah bin Hisham. Ewe Allah! Mnusuru Al-Walid bin Al-Walid. Ewe Allah! Wanusuru Waislamu dhaifu. Ewe Allah! Kuwa mgumu kwa kabila la Mudhar. Ewe Allah! Wajaalie ukame kama ukame wa miaka (ya njaa) ya zama za Nabii Yusuf."*¹

Al-Bukhari ameandika kuwa Abu An-Nu'man alisema, Hammad bin Zayd alisema, Ayyub amesimulia kuwa Ibn Abi Mulaykah alisema, Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu aya,

إِلَّا الْمُسْتَضْعَفِينَ

"Isipokuwa wale walio kuwa wanyonge."

"Mimi na mama yangu tulikuwa pamoja na wale (wadhaifu) Aliowasamehe Allah تعالى."² Kauli ya Allah

* وَمَنْ يُهَاجِرْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يَمُوتْ فِي الْأَرْضِ مُرَاعِمًا كَثِيرًا وَسَعَةً

"Na mwenye kuhama katika njia ya Mwenyezi Mungu atapata pengi duniani pa kukimbilia, na atapata wasaa."

Hii inawahimiza Waumini kufanya *Hijrah* na kuwaacha washirikina, kwani popote anapohamia muumini, atapata mahali salama pa kukimbilia. Mujahid alisema kuwa,

مُرَاعِمًا كَثِيرًا

"Pengi pa kukimbilia."

Maana yake: Atapata njia ya kuyaacha asiyoyapenda. Kauli ya Allah تعالى,

وَسَعَةً

"Na atapata wasaa."

Inakusudia riziki. Qatadah pia alisema kuwa,

¹ Al-Bukhari na. 804.

² *Fat'hul Al-Bari* 8:113.

تَجِدُ فِي الْأَرْضِ مُرَاعِمًا كَثِيرًا وَسَعَةً

“Atapata pengi duniani pa kukimbilia, na atapata wasaa.”

Maana yake: Allah تعالى Atamtoa katika upotevu kwenda katika uongofu na kutoka katika umaskini kwenda katika utajiri.¹ Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ يَخْرُجْ مِنْ بَيْتِهِ مُهَاجِرًا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ يُدْرِكُهُ الْمَوْتُ فَقَدْ وَقَعَ أَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ

“Na anayetoka nyumbani kwake kuhama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, kisha yakamfika mauti njiani basi umethibiti ujira wake kwa Mwenyezi Mungu.”

Maana yake: Yeyote anayeanza kuhama na kufariki njiani, atapata malipo ya waliohama kwa ajili ya Allah تعالى.

Sahihi Mbili, pamoja na wakusanyaji wa *Musnad* na *Sunan*, wameandika kuwa ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema،

«إِنَّمَا الْأَعْمَالُ بِالنِّيَّاتِ، وَإِنَّمَا لِكُلِّ امْرِئٍ مَا نَوَى، فَمَنْ كَانَتْ هِجْرَتُهُ إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ، فَهِيَ هِجْرَتُهُ إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ، وَمَنْ كَانَتْ هِجْرَتُهُ إِلَى دُنْيَا يُصِيبُهَا، أَوْ امْرَأَةٍ يَتَرَوَّجُهَا، فَهِيَ هِجْرَتُهُ إِلَى مَا هَاجَرَ إِلَيْهِ»

“Malipo ya amali hutegemea nia, na kila mtu hulipwa kulingana na alichonua. Basi, anayehama kwa ajili ya Allah تعالى na Mjumbe Wake, basi kuhama kwake ni kwa ajili ya Allah تعالى na Mjumbe Wake. Na mwenye kuhama kwa njia ya dunia aipate au mwanamke amuo, basi kuhama kwake ni kwa ajili ya alichokihamia.”²

Hadithi hii ni ya ujumla, inatumika pia katika *Hijrah* na katika kila amali. Katika Sahihi Mbili, kumeandikwa kuwa mtu mmoja aliua watu tisini na tisa na akatimiza idadi ya mia moja - alipomuua mfanya ibada. Kisha akamuuliza mwanazuoni kama ana nafasi ya kutubu. Mwanazuoni huyo alisema, “Nini

¹ At-Tabari 9:121.

² *Fat’hul Al-Bari* 1:161, *Muslim* 3:1515, *Abu Dawud* 2:651, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 5:281, *An-Nasai* 7:713, *Ibn Majah* 2:1413, *Ahmad* 1:25.

kitakachokuzuia kutubu.” Mwanazuoni huyo alimuambia muuaji huyo ahame kutoka ardhi kwao na aende katika ardhi nyingine kunakoabudiwa Allah تعالى. Alipoondoka katika ardhi yake na kuanza kuhamia katika ardhi nyingine, alifikwa na mauti njiani. Malaika wa rehema na malaika wa adhabu walibishana kuhusu mtu huyo, ambapo wa rehema alisema kuwa huyo alitoka kwenda kutubu, mwingine akasema hajafika. Wakaamua kupima umbali baina ya sehemu hizo mbili na kuangalia wapi palikuwa karibu zaidi, na kutazamwa kuwa huyo ni wa ardhi ya huko. Allah تعالى Aliamuru ardhi ya watu wema isogee karibu na ardhi ya waovu isogee mbali. Malaika wakaona kuwa alifariki karibu na ardhi aliyokusudia kuhamia kwa umbali wa dhira moja, na kuwa malaika wa rehema wakaichukua roho yake. Katika masimulizi mengine, mauti yalipomfikia mtu huyo, alielekeza kifua chake upande wa mji wa watu wema aliokuwa akihamia.¹

وَإِذَا ضَرَبْتُمْ فِي الْأَرْضِ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ إِنَّ خِفَتُمْ أَنْ يُفْتِنَكُمْ
الَّذِينَ كَفَرُوا إِنَّ الْكَافِرِينَ كَانُوا لَكُمْ عَدُوًّا مُّبِينًا ﴿١٠١﴾

101. Na mnapo safiri katika nchi si vibaya kwenu kama mkifupisha Swala, iwapo mnachelea wasije wale waliokufuru wakakuleteeni maudhi. Hakika makafiri ni maadui zenu walio wazi wazi.

Sala ya Al-Qasr, Kufupisha Sala

Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذَا ضَرَبْتُمْ فِي الْأَرْضِ

“Na mnaposafiri katika nchi...”

Maana yake: Kama unasafiri katika Ardhi. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Alisema,

عَلِمَ أَنْ سَيَكُونُ مِنْكُمْ مَرْضَىٰ ۖ وَآخَرُونَ يَضْرِبُونَ فِي الْأَرْضِ يَبْتَغُونَ مِنْ فَضْلِ اللَّهِ

Anajua ya kuwa baadhi yenu watakuwa wagonjwa, na wengine wanasafiri katika ardhi wakitafuta Fadhila ya Mwenyezi Mungu (73:20)

¹ Fat'hul Al-Bari 6:591, Muslim 4:2118.

Kauli ya Allah تعالى،

فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ

“Si vibaya kwenu kama mkifupisha Sala.”

Kwa kupunguza rakaa za Sala, kutoka nne kuwa mbili. Kauli ya Allah تعالى،

إِنْ خِفْتُمْ أَنْ يَفْتِنَكُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Iwapo mnachelea wasije wale waliokufuru wakakuleteeni maudhi.”

Inakusudia uoga wa kawaida uliokuwepo wakati Ayah hii iliposhuka. Mwanzoni mwa Uislamu, na baada ya Hijrah, Waislamu walikuwa na hofu katika nyakati za safari zao nyingi. Badala yake, walizibana safari zao katika safari ndefu au fupi za kijeshi. Katika nyakati hizo, sehemu nyingi ni za wapiganaji maadui wa Uislamu na watu wao. Lakini hali hiyo ilipokoma, au hali mpya ilipoenea, hukumu za hali hizo huenda zisifahamike kinyume chake.

Kama Alivyosema Allah تعالى،

﴿وَلَا تُكْرِهُوا فَتِنَكُمْ عَلَىٰ إِلْغَاءِ الْإِيمَانِ ۚ إِنَّ أَرْدَنَ مَحْضًا﴾

“Wala msiwalazimishe banati zenu juu ya uasherati ikiwa wanataka kujihifadhi.”

Na Kauli Yake;

وَرَبِّبُكُمْ أَلَّتِي فِي حُجُورِكُمْ مِّنْ نِّسَائِكُمْ

“Na watoto wenu wa kambo walio katika ulinzi wenu waliozaliwa na wake zenu”.

Imam Ahmad ameandika kuwa Ya'la bin Umayyah alisema, “Nilimuuliza ‘Umar bin Al-Khattab رضي الله عنه kuhusu aya:

فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ ۚ إِنَّ خِفْتُمْ أَنْ يَفْتِنَكُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا

“Si vibaya kwenu kama mkifupisha Sala, iwapo mnachelea wasije wale waliokufuru wakakuleteeni maudhi.”

Allah تعالى sasa Amewapa Waislamu usalama,' 'Umar رضي الله عنه aliniambia, 'Nilishangazwa na jambo hilo na nikamuuliza Mtume ﷺ na akasema,

«صَدَقَةٌ تَصَدَّقَ اللهُ بِهَا عَلَيْكُمْ فَأَقْبَلُوا صَدَقَتَهُ»

*"Sadaka Aliyokupeni Allah, basi, ipokeeni sadaka Yake."*¹

Muslim na wakusanyaji wa *Sunan* wameinukuu Hadithi hii. At-Tirmidhi alisema, "*Hasan Sahih*".² 'Ali bin Al-Madini alisema, "Hadithi hii ni *Hasan Sahih* kutokana na masimulizi ya 'Umar رضي الله عنه, na hayakuhifadhiwa kwa njia nyingine isipokuwa hii, na wasimulizi wake wote wanajulikana." Abubakr Ibn Abi Shaybah ameandika kuwa Abu Hanzalah Hadha' alisema, "Nilimuuliza Ibn 'Umar رضي الله عنه kuhusu Sala ya *Qasr* na akasema, 'Ina *Rak`ah* mbili." Nikasema, vipi kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

إِنْ خِفْتُمْ أَنْ يَفْتِنَكُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا

"Iwapo mnachelea wasije wale waliokufuru wakakuleteeni maudhi."

'Sasa tuko salama.' Akasema, 'Hii ni Sunnah ya Mtume ﷺ.³

Al-Bukhari ameandika kuwa Anas رضي الله عنه alisema, "Tulitoka Madinah pamoja na Mtume ﷺ kuelekea Makkah; alikuwa akisali *Rak`ah* mbili mpaka tuliporejea Madinah." Alipoulizwa muda aliokuwepo Makkah, alisema, "Tulikaa Makkah siku kumi."⁴ Haya yameandikwa na jamaa.⁵

Imam Ahmad ameandika kuwa Harithah bin Wahb Al-Khuza'i alisema, "Nilisali nyuma ya Mtume ﷺ Sala za Dhuhr na 'Asr huko Mina, watu walipokuwa wengi kwa idadi na katika usalama, na alisali *Rak`ah* mbili."⁶

¹ Ahmad 1:25.

² Muslim 1:478, Abu Dawud 2:7, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 8:392, An-Nasai katika *Al-Kubra* 6:327 na Ibn Majah 1:339.

³ Ibn Abi Shaybah 2:447.

⁴ *Fat'hul Al-Bari* 2:653.

⁵ Muslim 1:481, Abu dawud 2:25, *Tuhfat Al-Ahwadhi* 3:110, An-Nasai 3:121 na Ibn Majah 1:342.

⁶ Ahmad 4:306.

Haya yamenukuliwa na jamaa isipokuwa Ibn Majah.¹ Masimulizi ya Al-Bukhari ya Hadithi hii yanasomeka hivi, "Mtume ﷺ alituongoza katika Sala huko Mina katika kipindi cha amani kwa kusali *Rak`ah* mbili."²



¹ *Fat'hul Al-Bari* 2:655, *Muslim* 1:484, *Abu Dawud* 2:493, *Tuhfat Al-Ahwadhi*3: 621na *An-nasai* 3;119.

² *Fat'hul Al-Bari* 2:655.

وَإِذَا كُنْتَ فِيهِمْ فَأَقَمْتَ لَهُمُ الصَّلَاةَ فَلْتَقُمْ طَائِفَةٌ مِنْهُمْ مَعَكَ وَلْيَأْخُذُوا مَعَكَ وَرَأْيَكُمْ وَرَأْيَكُمْ وَلَتَأْتِ طَائِفَةٌ أُخْرَى لَمْ يُصَلُّوا فَلْيُصَلُّوا مَعَكَ وَلْيَأْخُذُوا حِذْرَهُمْ وَأَسْلِحَتَهُمْ ۗ وَذَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ تَغْفُلُونَ عَنْ أَسْلِحَتِكُمْ وَأَمْتِعَتِكُمْ فَيَمِيلُونَ عَلَيْكُمْ مَيْلَةً وَاحِدَةً ۗ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ كَانَ بِكُمْ أذى مِّن مِّطَرٍ أَوْ كُنْتُمْ مَرَضَى أَنْ تَضَعُوا أَسْلِحَتَكُمْ ۗ وَخُذُوا حِذْرَكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِمًّا ﴿١٠٢﴾

فَإِذَا قَضَيْتُمُ الصَّلَاةَ فَادْكُرُوا اللَّهَ قِيَمًا وَتُؤَدُّوا عَلَيْهِمْ جُنُودًا ۗ وَإِذَا قَامَتِ الصَّلَاةُ فَاقِيمُوا الصَّلَاةَ ۗ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَّوْقُوفًا ﴿١٠٣﴾ وَلَا تَهِنُوا فِي ابْتِغَاءِ الْقَوْمِ ۗ إِنْ تَكُونُوا تَأْمِنُونَ فَإِنَّهُمْ يَأْتُمُونَكُمْ كَمَا تَأْتُمُونَ ۗ وَتَرْجُونَ مِنَ اللَّهِ مَا لَا يَرْجُونَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٠٤﴾

وَإِذَا كُنْتَ فِيهِمْ فَأَقَمْتَ لَهُمُ الصَّلَاةَ فَلْتَقُمْ طَائِفَةٌ مِنْهُمْ مَعَكَ وَلْيَأْخُذُوا مَعَكَ وَرَأْيَكُمْ وَرَأْيَكُمْ وَلَتَأْتِ طَائِفَةٌ أُخْرَى لَمْ يُصَلُّوا فَلْيُصَلُّوا مَعَكَ وَلْيَأْخُذُوا حِذْرَهُمْ وَأَسْلِحَتَهُمْ ۗ وَذَ الَّذِينَ كَفَرُوا لَوْ تَغْفُلُونَ عَنْ أَسْلِحَتِكُمْ وَأَمْتِعَتِكُمْ فَيَمِيلُونَ عَلَيْكُمْ مَيْلَةً وَاحِدَةً ۗ وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِنْ كَانَ بِكُمْ أذى مِّن مِّطَرٍ أَوْ كُنْتُمْ مَرَضَى أَنْ تَضَعُوا أَسْلِحَتَكُمْ ۗ وَخُذُوا حِذْرَكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِمًّا ﴿١٠٢﴾

102. Na unapokuwa pamoja nao, ukawasalisha, basi

kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe na wachukue silaha zao. Na watakapomaliza sijida zao, basi na wende nyuma yenu, na lije kundi jingine ambalo halijasali, lisali pamoja nawe. Nao wachukue hadhari yao na silaha zao. Waliokufuru wanapenda mghafilike na silaha zenu na vifaa vyenu ili wakuvamieni mvamio wa mara moja. Wala si vibaya kwenu ikiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mkawa wagonjwa, mkaziweka silaha zenu. Na chukueni hadhari yenu. Hakika Mwenyezi Mungu Amewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha.

Maelezo ya Sala ya Hofu

Sala ya Hofu ina mtindo tofauti, kwani adui wakati mwingine huwa upande wa Qiblah na wakati mwingine katika upande mwingine. Sala ya Hofu wakati mwingine huwa na *Rak'ah* nne, *Rak'ah* tatu, kwa Maghrib, na wakati mwingine *Rak'ah* kama Fajr na Sala ya safarini. Sala ya Hofu wakati mwingine husaliwa kwa jamaa, lakini vita vinapopiganwa, huenda Sala ya jamaa isiwezekane. Katika hali hii, kila mmoja anasali peke yake, kwa kuelekea Qiblah au vinginevyo, juu ya mnyama au kwa kutembea kwa miguu. Katika hali hii, wanaruhusiwa kutembea na kupigana, wakati huo huo kutekeleza vitendo vya Sala.

Baadhi ya wanazuoni walisema kuwa katika hali ya baadaye, waliswali *Rak'ah* moja tu, kwani Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisimulia, "Kwa maneno ya Mtume ﷺ, Allah تعالى Amefaradhisha sala ya *Rak'ah* nne akiwa mtu ni mkazi (hayupo safari), *Rak'ah* mbili safarini, na *Rak'ah* wakati wa hofu."

Muslim, Abu Dawud, An-Nasa'i na Ibn Majah wameinukuu.¹ Hii pia rai ya Ahmad bin Hanbal رحمه الله تعالى. Al-Mundhiri alisema, "Hii ni kauli ya 'Ata', Jabir, Al-Hasan, Mujahid, Al-Hakam, Qatadah na Hammad; na Tawus na Adh-Dhahhak pia ameipendelea." Abu 'Asim Al-'Abadi alitaja kuwa Muhammad bin Nasr Al-Marwazi رحمه الله تعالى alisema kuwa Sala ya *Fajr* inakuwa ya *Rak'ah* moja wakati wa hofu. Hii pia ni rai ya Ibn Hazm رحمه الله تعالى. Ishaq bin Rahwayh رحمه الله تعالى alisema, "Vita vinapopiganwa, *Rak'ah* moja katika wakati mnapoashiria kwa kichwa inakutosheni. Kama hamuwezi, basi sijida moja inatosha, kwa sababu sijida ni kumkumbuka Allah تعالى."

Sababu ya Kushuka Aya hii

Imam Ahmad ameandika kuwa Abu 'Ayyash Az-Zuraqi alisema kuwa, "Tulikuwa pamoja na Mtume ﷺ katika eneo la 'Usfan (sehemu maarufu karibu na Makkah), washirikina walipokutana nasi chini ya uongozi wa Khalid bin Al-Walid رضي الله عنه, na wakawa baina yetu na Qiblah. Mtume ﷺ alituongoza katika Sala ya Dhuhur, na washirikina wakasema, 'Walikuwa wameshughulishwa sana na jambo ambapo tulikuwa na fursa nzuri ya kuwashambulia.' Kisha wakasema,

¹ Muslim;687, Abu Dawud: 1247, An-nasai 3:169 na Ibn Majah: 1068.

'Baadaye, itafika Sala (ya `Asr) wanayoipenda mno kuliko watoto wao na nafsi zao.' Hata hivyo, Jibril عليه السلام alishuka na Aya hizi baina ya Sala za *Dhuhr* na 'Asr,

وَإِذَا كُنْتَ فِيهِمْ فَأَقَمْتَ لَهُمُ الصَّلَاةَ

“Na unapo kuwa pamoja nao, ukawasalisha.”

Ulipofika wakati wa Sala, Mtume ﷺ aliwaamuru Waislamu washike silaha zao na kutupanga safu mbili nyuma yake. Alipoinama, sote tuliinama nyuma yake. Alipoinua kichwa, tuliinua vichwa vyetu. Mtume ﷺ akasujudu pamoja na safu iliyokuwa nyuma yake, huku waliobaki wamesimama kulinda. Walipomaliza kusujudu na wakasimama, waliobakia waliketi na kusujudu, huku waliokuwa tayari wameshasujudu walisimama kulinda baada ya safu mbili kubadilishana mahali. Mtume ﷺ akainama na wote wakainama baada yake, kisha wakainua vichwa vyao baada ya Mtume ﷺ. Kisha Mtume ﷺ akasujudu pamoja na safu iliyokuwa nyuma yake, huku waliobakia wakasimama kwa ulinzi. Wale waliokwisha sujudu wakiwa katika hali ya kuketi, wengine walisujudu. Mtume ﷺ akatoa Taslim na kumaliza Sala. Mtume ﷺ aliswali Sala hii mara mbili, moja huko 'Usfan na nyingine katika ardhi ya Banu Sulaym.'"¹

Masimulizi haya yamenukuliwa na Abu Dawud na An-Nasa'i,² na yana isnadi ya hakika ya usimulizi na vitabu vingi vingine vinavyoiunga mkono.

Bukhari ameandika kuwa Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alisema, "Mtume ﷺ aliongoza Sala ya Hofu na watu wakasimama nyuma yake. Akasema *Allahu-Akbar* na watu wakasema vivyo hivyo. Akainama na baadhi yao wakainama. Kisha akasujudu na wao wakasujudu pia. Kisha akasimama kwa ajili ya *Rak`ah* ya pili na wale waliokwisha sali *Rak`ah* ya kwanza waliondoka ili kuwalinda ndugu zao. Kundi la pili liliungana nao na kuinama na kusujudu pamoja naye. Watu wote walikuwa katika Sala, lakini walikuwa wakilindana wakati wa Sala."³

Imam Ahmad ameandika kuwa Jabir bin 'Abdullah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ aliwaongoza katika Sala ya Hofu. Kundi moja lilisimama mbele yake na jingine nyuma yake. Mtume ﷺ aliongoza wale waliokuwa nyuma yake kwa

¹ Ahmad 4:59-60.

² Abu Dawud 2:28 na An-Nasai 3:176-177.

³ *Fat'hul Al-Bari* 2:502.

Rak`ah na sijida mbili. Kisha wakaenda mahali pa wale ambao hawakusali, huku wengine wakisimama katika mahali pao, na Mtume ﷺ alisali *Rak`ah* moja na sijida mbili halafu akatoa Salam. Kwa hiyo, Mtume ﷺ alisali *Rak`ah* mbili ilhali nao walisali moja. An-Nasa'i amenukuu Hadithi hii, huku Muslim ameinukuu kwa maneno mengine. Wakusanyaji wa Sahih, *Sunan* na *Musnad* wameinukuu katika Hadithi ya Jabir رضي الله عنه. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى ameandika kuwa Salim alisema kuwa baba yake alisema,

وَإِذَا كُنْتَ فِيهِمْ فَأَقَمْتَ لَهُمُ الصَّلَاةَ

“Na unapo kuwa pamoja nao, ukawasalisha...”

Inakusudia Sala ya hofu.

Mtume ﷺ aliliongoza kundi moja na kusali *Rak`ah* moja, huku kundi la pili likimkabili adui. Kisha kundi la pili lililomkabili adui lilikuja na Mtume ﷺ akawaongoza, kusali *Rak`ah* moja, na kisha akatoa Salam. Kila moja kati ya makundi hayo mawili likasimama na kuswali *Rak`ah* moja zadi (huku kundi jingine likisimama katika kulinda).” Jamaa wameikusanya Hadithi hii kukiwa na Ma'mar katika isnadi yake ya wasimulizi. Hadithi hii pia ina isnadi nyingi za masimulizi kutoka kwa Masahaba wengi, na Al-Hafidh Abubakr Ibn Marduwyah رحمه الله تعالى alikusanya masimulizi hayo mengi, kama alivyofanya Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Ama kuhusu amri ya kushika silaha katika kipindi cha Sala ya Hofu, kundi la wanazuoni lilisema kuwa ni wajibu kwa mujibu wa Ayah hiyo. Kinachothibitisha hayo ni Kauli ya Allah تعالى;

وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ إِن كَانَ بِكُمْ أَذًى مِّن مَّطَرٍ أَوْ كُنْتُمْ مَّرْضَىٰ أَن تَضَعُوا أَسْلِحَتَكُمْ
وَتُحَدِّثُوا جُنُودَكُمْ

“Wala si vibaya kwenu ikiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mkawa wagonjwa, mkaziweka silaha zenu. Na chukueni hadhari yenu.”

Maana yake: Ili inapolazimu, mtaweza kupata silaha zenu kwa urahisi,

إِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِمًّا

“Hakika Mwenyezi Mungu Amewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha.”

فَإِذَا قَضَيْتُمُ الصَّلَاةَ فَادْكُرُوا اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِكُمْ ۚ فَإِذَا اطْمَأْنَنْتُمْ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ ۚ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَىٰ الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَّوْقُوتًا ﴿١٠٣﴾ وَلَا تَهِنُوا فِي ابْتِغَاءِ الْقَوْمِ ۗ إِنْ تَكُونُوا تَأْلَمُونَ فَإِنَّهُمْ يَأْلَمُونَ كَمَا تَأْلَمُونَ ۗ وَتَرْجُونَ مِنَ اللَّهِ مَا لَا يَرْجُونَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٠٤﴾

103. Mkisha swali basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu mkisimama, na mkikaa, na mnapo jinyoosha kwa kulala. Na mtapotulia basi shikeni Sala kama dasturi. Kwani hakika Sala kwa Waumini ni faradhi iliyowekewa nyakati maalumu.

104. Wala msifanye ulegevu kuwafukuzia kaumu ya maadui. Ikiwa mnaumia, basi nao pia wanaumia kama mnavyoomia nyinyi. Nanyi mnataraji kwa Mwenyezi Mungu wasioyataraji wao. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye Hikima.

Amri ya Dhikri ya Kutosha Baada ya Sala ya Hofu

Allah تعالی Anaamuru Dhikr baada ya kumaliza Sala ya Hofu, hususani, ingawa Dhikr hiyo inahimizwa baada ya kumaliza Swala za aina nyingine kwa ujumla. Katika Sala ya Hofu, Dhikr imesisitizwa zaidi kwa sababu nguzo za Sala zimepungua kwa kuwa wanatembea wakati wa kuisali, n.k., si kama Sala zingine. Kauli ya Allah تعالی kuhusu miezi mitukufu,

فَلَا تَطْلُمُوا فِيهِنَّ أَنْفُسَكُمْ ۚ

“Basi msidhulumu humo nafsi zenu.” (9:36)

Ingawa dhuluma imekatazwa kwa mwaka mzima. Hata hivyo, dhuluma imeharamishwa wakati wa Miezi Mitukufu kwa sababu ya utukufu. Hivyo, Allah تعالی Amesema,

فَإِذَا قَضَيْتُمُ الصَّلَاةَ فَادْكُرُوا اللَّهَ قِيَمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِكُمْ ۚ

“Mkisha sali basi mkumbukeni Mwenyezi Mungu mkisimama, na mkikaa, na mnapo jinyoosha kwa kulala.”

Maana yake: Katika hali zote,

فَإِذَا أَطَمَأْنَنْتُمْ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ

“Na mtapotulia basi shikeni Sala kama dasturi.”

Mnapokuwa katika usalama na utulivu, basi hofu hupungua,

فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ

“Shikeni Sala.” Kwa kuifanya kama ilivyoamrishwa; kutimiza wajibu zake, kwa unyenyekevu, kutimiza rukuu na sijida n.k. Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ كِتَابًا مَوْقُوتًا

“Kwani hakika Sala kwa Waumini ni faradhi iliyowekewa nyakati maalumu.”

Maana yake: Imeamrishwa, kama Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alivyoeleza.¹ Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما pia alisema, “Sala ina wakati wake uliopangwa, kama ilivyo *Hajj*.”² Yamesimuliwa sawa na hayo kutoka kwa Mujahid, Salim bin ‘Abdullah, ‘Ali bin Al-Husayn, Muhammad bin ‘Ali, Al-Hasan, Muqatil. As-Suddi na ‘At iyah Al-‘Awfi.³

Kuhimizwa Kumkimbiza Adui Licha ya Majeraha

Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا تَهِنُوا فِي ابْتِغَاءِ الْقَوْمِ

“Wala msifanye ulegevu kuwafukuzia kaumu ya maadui.”

Maana yake: Msidhoofishe azma ya kumkimbiza adui yenu. Badala yake, wakimbizeni kwa nguvu, wapigeni na muwaogopeshe.

إِنْ تَكُونُوا تَأْلَمُونَ فَإِنَّهُمْ يَأْلَمُونَ كَمَا تَأْلَمُونَ

“Ikiwa mnaumia, basi nao pia wanaumia kama mnavyousia nyinyi.”

¹ Ahmad 3:298, A-nasai 3:174 na Muslim:840.

² Ad-Dur Al-Manthur 2:375.

³ At-Tabari 9:169.

Maana yake: Kama mnavyoteseka kwa majeraha na mauti, vivyo hivyo humtokea adui. Katika Aya nyingine, Allah تعالى Amesema,

إِنْ يَمَسُّكُمْ قَرْحٌ فَقَدْ مَسَّ الْقَوْمَ قَرْحٌ مِّثْلَهُ ۗ

“Mkipatwa na majeraha bila shaka wamepata watu majeraha mfano wenu.” (3:140)

Kisha Allah تعالى Akasema,

وَتَرْجُونَ مِنَ اللَّهِ مَا لَا يَرْجُونَ ۗ

“Nanyi mnataraji kwa Mwenyezi Mungu wasioyataraji wao.”

Maana yake: Nyinyi na wao mnalingana kuhusu majeraha na maumivu mnayoyapata. Hata hivyo, nyinyi mnatumaini malipo ya Allah تعالى, ushindi na msaada, kama Alivyoku ahidini katika Kitabu Chake na kwa maneno ya Mjumbe Wake. Kwa hakika, ahadi ya Allah تعالى ni kweli. Kwa upande mwingine, maadui zenu hawatumaini chochote katika hili. Basi, ni nyinyi, si wao, mtakaokuwa na shauku ya kupigana ili msimamishe Neno la Allah تعالى na kuliweka juu.

إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ

“Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na Mwenye Hekima.”

Maana yake: Yeye ni Mjuzi zaidi na Mwingi wa Hekima katika Maamuzi Yake yote Anayohukumu, Anayotaka na Kufanya katika Amri zote za kidunia na kidini, na Anastahiki sifa katika hali zote.

* * *

إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِتَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ بِمَا
 أَرْنَاكَ اللَّهُ وَلَا تَكُنَ لِلْخَائِبِينَ حَصِيمًا ﴿١٠٥﴾ وَأَسْتَغْفِرِ اللَّهَ
 إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١٠٦﴾ وَلَا تُجَادِلْ عَنِ
 الَّذِينَ يَخْتَانُونَ أَنْفُسَهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَنْ كَانَ خَوَانًا
 أَيْمًا ﴿١٠٧﴾ يَسْتَخْفُونَ مِنَ النَّاسِ وَلَا يَسْتَخْفُونَ مِنَ اللَّهِ
 وَهُوَ مَعَهُمْ إِذْ يُبَيِّتُونَ مَا لَا يَرْضَى مِنَ الْقَوْلِ وَكَانَ اللَّهُ
 بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطًا ﴿١٠٨﴾ هَتَأْتُمْ هَتُولًا جَدَلْتُمْ عَنْهُمْ فِي
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فَمَنْ يُجَادِلِ اللَّهَ عَنْهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَمْ مَنْ
 يَكُونُ عَلَيْهِمْ وَكِيلًا ﴿١٠٩﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ
 نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١١٠﴾ وَمَنْ
 يَكْسِبْ إِنَّمَا فَاِنَّمَا يَكْسِبُهُ عَلَى نَفْسِهِ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا
 حَكِيمًا ﴿١١١﴾ وَمَنْ يَكْسِبْ خَطِيئَةً أَوْ إِثْمًا ثُمَّ يَرْمِ بِهِ
 بَرِيئًا فَقَدْ احْتَمَلَ بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُبِينًا ﴿١١٢﴾ وَلَوْلَا فَضْلُ
 اللَّهِ عَلَيْكَ وَرَحْمَتُهُ هَمَّتْ طَائِفَةٌ مِنْهُمْ أَنْ يُضِلُّوكَ وَمَا
 يُضِلُّونَ إِلَّا أَنْفُسَهُمْ وَمَا يَضُرُّونَكَ مِنْ شَيْءٍ وَأَنْزَلَ
 اللَّهُ عَلَيْكَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَكَ مَا لَمْ تَكُنْ تَعْلَمُ
 وَكَانَ فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكَ عَظِيمًا ﴿١١٣﴾

إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ
 لِتَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ بِمَا أَرْنَاكَ اللَّهُ
 وَلَا تَكُنَ لِلْخَائِبِينَ حَصِيمًا ﴿١٠٥﴾
 وَأَسْتَغْفِرِ اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا
 رَحِيمًا ﴿١٠٦﴾ وَلَا تُجَادِلْ عَنِ
 الَّذِينَ يَخْتَانُونَ أَنْفُسَهُمْ إِنَّ اللَّهَ لَا
 يُحِبُّ مَنْ كَانَ خَوَانًا أَيْمًا ﴿١٠٧﴾
 يَسْتَخْفُونَ مِنَ النَّاسِ وَلَا يَسْتَخْفُونَ
 مِنَ اللَّهِ وَهُوَ مَعَهُمْ إِذْ يُبَيِّتُونَ مَا لَا
 يَرْضَى مِنَ الْقَوْلِ وَكَانَ اللَّهُ بِمَا
 يَعْمَلُونَ مُحِيطًا ﴿١٠٨﴾ هَتَأْتُمْ هَتُولًا
 جَدَلْتُمْ عَنْهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا
 فَمَنْ يُجَادِلِ اللَّهَ عَنْهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
 أَمْ مَنْ يَكُونُ عَلَيْهِمْ وَكِيلًا ﴿١٠٩﴾

105. Hakika Sisi Tumeku-
 teremshia Kitabu hiki kwa
 haki ili upate kuhukumu
 baina ya watu kwa alivyoku-
 oneshwa. Mwenyezi Mungu.

Wala usiwe mtetezi wa makhaini.

106. Na muombe maghira Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghira, Mwenye Kurehemu.

107. Wala usiwatetee wanaokhini nafsi zao. Hakika Mwenyezi Mungu Hampendi aliye khaini, mwenye dhambi.

108. Wanataka kujificha kwa watu, wala hawataki kujificha kwa Mwenyezi Mungu, Naye Yu pamoja nao pale wanapopanga njama usiku kwa maneno asiyoyapenda. Na Mwenyezi Mungu Anayajua vyema wanayoyatenda.

109. Hivyo nyinyi mmewatetea hawa katika uhai huu wa duniani. Basi nani atakayewatetea kwa Mwenyezi Mungu Siku ya Kiyama? Au ni nani atakuwa wakili wao wa kumtegemea?

Umuhimu wa Kuegemea katika Hukumu Alizoshusha Allah تعالى

Allah تعالى Anamuambia Mjumbe Wake, Muhammad ﷺ,

إِنَّا أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ

“Hakika Sisi Tumekuteremshia Kitabu hiki kwa haki.”

Maana yake: Kweli kimetoka kwa Allah تعالى na masimulizi yake na maamrishi ni ya kweli. Kisha Allah تعالى Akasema,

لِتَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ بِمَا أَرْنَاكَ اللَّهُ

“Ili upate kuhukumu baina ya watu kwa Alivyokuonesha Mwenyezi Mungu.”

Katika Sahihi Mbili, kumeandikwa kuwa Zaynab bint Umm Salamah رضي الله عنها alisema kuwa Umm Salamah رضي الله عنها alisema kuwa Mtume ﷺ alisikia kelele za watu waliokuwa wakibishana karibu na mlango wa chumbani kwake, na akatoka nje na kuwaambia,

«أَلَا إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ، وَإِنَّمَا أَنُفِصِي بِنَحْوِ مِمَّا أَسْمَعُ، وَلَعَلَّ أَحَدَكُمْ أَنْ يَكُونَ أَلْحَنَ بِحُجَّتِهِ مِنْ بَعْضِ فَأُقْضِي لَهُ، فَمَنْ قَضَيْتُ لَهُ بِحَقِّ مُسْلِمٍ، فَإِنَّمَا هِيَ قِطْعَةٌ مِنْ نَارٍ، فَلْيَحْمِلْهَا أَوْ لِيَذَرْهَا»

“Kwa hakika si vingine, mimi ni mtu, na ninahukumu kwa kuzingatia ninachosikia. Baadhi yenu mnaweza kuwa mahiri katika hoja zenu

kuliko wengine, basi nahukumu kwa kumpa haki. Kama nitahukumu kwa kumpa mtu haki ya Muislamu mwingine, basi hicho ni kipande cha moto. Basi, akichukue au akiache.”¹

Imam Ahmad ameandika kuwa Umm Salamah رضي الله عنها alisema, “Watu wawili katika Ansar walikuja kwa Mtume ﷺ kugombea mirathi ya zamani, lakini hawakuwa na ushahidi. Mtume ﷺ akasema,

«إِنَّكُمْ تَخْتَصِمُونَ إِلَيَّ، وَإِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ، وَلَعَلَّ بَعْضَكُمْ أَلْحَنُ بِحُجَّتِهِ مِنْ بَعْضٍ، وَإِنَّمَا أَقْضِي بَيْنَكُمْ عَلَى نَحْوِ مِمَّا أَسْمَعُ، فَمَنْ قَضَيْتُ لَهُ مِنْ حَقِّ أَخِيهِ شَيْئًا فَلَا يَأْخُذْهُ، فَإِنَّمَا أَقْطَعُ لَهُ قِطْعَةً مِنَ النَّارِ، يَأْتِي بِهَا إِسْطِطَامًا فِي يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

“Hakika nyinyi mnaniletea ugomvi wenu, mimi ni mwanadamu tu. Baadhi yenu ni fasaha wa hoja zake kuliko wengine. Mimi nahukumu baina yenu kwa mujibu wa ninachosikia. Hivyo, yeyote ninayemhukumia haki ya nduguye, asiichukue, kwani ninamkatia kipande cha moto, na ataviringishiwa shingoni mwake Siku ya Kiama.”

Watu wawili walilia na kila mmoja akasema, ‘ndugu yangu ameninyang’anya haki yangu.” Mtume ﷺ akasema,

«أَمَّا إِذْ قُلْتُمَا فَاذْهَبَا فَاقْتَسِمَا، ثُمَّ تَوَخَّيَا الْحَقَّ ثُمَّ اسْتَهَمَا، ثُمَّ لِيُحْلِلَ كُلُّ وَاحِدٍ مِنْكُمَا صَاحِبَهُ»

“Kwa kuwa mmesema hayo, basi nendeni mkagawe mirathi, na mjitahidi kuwa na uadilifu katika ugawaji. Kisha pigeni kura, na kila mmoja wenu amsamehe nduguye baada ya hapo (bila ya kujali aliyepata fungu bora zaidi).”²

Kauli ya Allah تعالى،

يَسْتَخْفُونَ مِنَ النَّاسِ وَلَا يَسْتَخْفُونَ مِنَ اللَّهِ

“Wanataka kujificha kwa watu, wala hawataki kujificha kwa Mwenyezi Mungu,”

¹At-Tabari 9:169.

²Ahmad 6:320.

Inawakaripia wanafiki kwa sababu wanaficha uovu wao dhidi ya watu ili wasiwakosoe. Lakini, wanafiki watadhihirisha uovu huo kwa Allah تعالى, Ambaye ni Mwangalizi Aliyetimia juu ya siri zao na Anajua yaliyo nyoyoni mwao. Ndio sababu Allah تعالى Akasema,

وَهُوَ مَعَهُمْ إِذْ يُبَيِّنُونَ مَا لَا يَرْضَىٰ مِنَ الْقَوْلِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطًا ﴿١٠٥﴾

“Naye Yu pamoja nao pale wanapopanga njama usiku kwa maneno asiyoypenda. Na Mwenyezi Mungu Anayajua vyema wanayoyatenda.”

Kuwahofisha na kuwaonya. Kisha Allah تعالى Akasema,

هَاتَأْتُمْ هَٰؤُلَاءِ جِدَلْتُمْ عَنْهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

“Hivyo nyinyi mmewatetea hawa katika uhai huu wa duniani.”

Maana yake: Chukulia kuwa watu hao wanapata hukumu kutoka kwa watawala kwa kuwanufaisha duniani, kwa kuwa watawala wanahukumu kulingana na yanayowadhihirikia. Hata hivyo, hali zao zitakuwaje katika Siku ya Kiama mbele ya Allah تعالى, Anayejua siri na yaliyofichikana zaidi. Atakayekuwa wakili wake katika Siku hiyo. Kwa hakika, hakuna atakayewasaidia katika Siku hiyo.

Hivyo, Kauli ya Allah تعالى,

أَمْ مَن يَكُونُ عَلَيْهِمْ وَكِيلًا ﴿١٠٦﴾

“Au ni nani atakuwa wakili wao wa kumtegemea?”

وَمَن يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿١٠٧﴾ وَمَن يَكْسِبْ إِثْمًا فَإِنَّمَا يَكْسِبُهُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٠٨﴾ وَمَن يَكْسِبْ خَطِيئَةً أَوْ إِثْمًا ثُمَّ يَرْمِ بِهِ بَرِيقًا فَقَدِ احْتَمَلَ بُهْتَانًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴿١٠٩﴾ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكَ وَرَحْمَتُهُ هَمَّتْ طَآئِفَةٌ مِّنْهُمْ أَن يُضِلُّوكَ وَمَا يُضِلُّونَ إِلَّا أَنفُسَهُمْ ۗ وَمَا يَضُرُّونَكَ مِن شَيْءٍ ۗ وَأَنزَلَ اللَّهُ عَلَيْكَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَّمَكَ مَا لَمْ تَكُن تَعْلَمُ ۗ

وَكَانَ فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكَ عَظِيمًا ﴿١١٠﴾

110. Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake, kisha akaomba maghfira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira, Mwenye Kurehemu.

111. Na anayechuma dhambi, basi ameichumia nafsi yake mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye Hekima.

112. Na atendaye kosa au dhambi kisha akamsingizia asiye na kosa, basi amejitwika dhulma na dhambi iliyo wazi.

113. Na lau kuwa si Fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako na Rehema Yake, kundi moja kati yao lingedhamiria kukupoteza. Wala hawapotezi ila nafsi zao, wala hawawezi kukudhuru kwa lolote. Na Mwenyezi Mungu Amekuteremshia Kitabu na Hikima na Amekufundisha uliyo kuwa huyajui. Na Fadhila za Mwenyezi Mungu zilizo juu yako ni kubwa.

Kuhimiza Kuomba Msamaha wa Allah تعالى, na Kuwaonya Wenye Kuwatumu Kimakosa Wasio na Makosa

Allah تعالى Anasisitiza Ukarimu Wake na Hisani, na miongoni mwake Anamsamehe mwenye kutubu Kwake dhidi ya uovu wowote anaotenda.

Kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظَلِّمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١١٠﴾

“Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake, kisha akaomba Maghfira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira, Mwenye Kurehemu.”

‘Ali bin Abi Talhah alisema kuwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu Aya hii, “Allah تعالى Anawajulisha Waja Wake kuhusu msamaha Wake, kupata ukarimu na rehema kunjufu. Hivyo, mwenye kutenda dhambi, ndogo au kubwa,

كَيْفَ يَسْتَغْفِرُ اللَّهُ غُفُورًا رَحِيمًا ﴿١١١﴾

“Kisha akaomba maghfira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira, Mwenye Kurehemu.”

Hata kama madhambi yake ni makubwa kuliko mbingu, ardhi na milima." Imam Ahmad رحمه الله تعالى ameandika kuwa 'Ali رضي الله عنه alisema, "Wakati wowote niliposikia jambo kutoka kwa Mtume ﷺ, Allah تعالى Alininufaisha Atakavyo kwa jambo hilo. Abu Bakr رضي الله عنه aliniambia, na Abu Bakr رضي الله عنه amesema kweli, kuwa Mtume ﷺ amesema,

«مَا مِنْ مُسْلِمٍ يُذْنِبُ ذَنْبًا، ثُمَّ يَتَوَضَّأُ فَيُصَلِّي رَكَعَتَيْنِ، ثُمَّ يَسْتَغْفِرُ اللَّهَ لِذَلِكَ الذَّنْبِ، إِلَّا غَفَرَ لَهُ»

"Hakuna Muislamu yoyote anayetenda dhambi kisha akachukua udhu, akasali Rak'ah mbili na kumuomba Allah تعالى msamaha kwa dhambi hiyo, isipokuwa Anamsamehe."

Halafu akasoma Aya hizi mbili,

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ

"Na anayetenda uovu au akajidhulumu nafsi yake,..."

Kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ يَكْسِبْ إِثْمًا فَإِنَّمَا يَكْسِبُهُ عَلَى نَفْسِهِ

"Na anayechuma dhambi, basi ameichumia nafsi yake mwenyewe."

Ni sawa na Kauli Yake nyingine,

وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ

"Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine." (6:164)

Hakuna wa kumuepusha yeyote mwingine. Badala yake, kila nafsi, si nyingine, atakayebeba mzigo wake. Ndio sababu Allah تعالى Amesema,

وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا

"Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye Hikima."

Maana yake: Hayo hufanyika kwa ujuzi Wake, Hekima, Uadilifu na Rehema.

وَعَلَّمَكَ مَا لَمْ تَكُن تَعْلَمُ

“Na Amekufundisha uliyu kuwa huyajui.”

Kabla hujashushiwa ufunuo huu. Kadhalika, Kauli ya Allah تعالى,

وَكَذَلِكَ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ رُوحًا مِّنْ أَمْرِنَا مَا كُنْتَ تَدْرِي مَا الْكِتَابُ

“Kadhalika Tumekufunulia wahyi kwa Amri Yetu, na hukuwa unajua nini Kitabu.” (42:52)

Mpaka mwisho wa Sura. Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا كُنْتَ تَرْجُو أَن يُلْقَىٰ إِلَيْكَ الْكِتَابُ إِلَّا رَحْمَةً مِّن رَّبِّكَ

“Na hukuwa unatarajia kupewa Kitabu isipokuwa Rehema ya Mola wako.” (28:86)

Hivyo Kauli ya Allah تعالى;

وَكَانَ فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكَ عَظِيمًا

“Na Fadhila za Mwenyezi Mungu zilizo juu yako ni kubwa.”

* * *

* لَا خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّن نَّجْوَاهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ ۗ وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١١٤﴾ وَمَن يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصَلِّهِ ۖ جَهَنَّمَ ۗ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿١١٥﴾ إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَن يَشَاءُ ۗ وَمَن يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿١١٦﴾ إِن يَدْعُونَ مِن دُونِهِ إِلَّا إِنثًا وَإِن يَدْعُونَ إِلَّا شَيْطَانًا مَّرِيدًا ﴿١١٧﴾ لَعَنَهُ اللَّهُ وَقَالَ لَأَتَّخِذَنَّ مِنْ عِبَادِكَ نَصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿١١٨﴾ وَلَا ضَلَّتْهُمْ وَلَا مَيَّنَتْهُمْ وَلَا مَرَّيْتَهُمْ فَلَيَبْتَئِكُنَّ آذَانَ الْأَنْعَامِ وَلَا مَرْيَمَ فَلَيَحْمِلُنَّ أَثْقَلَ حِمْلٍ ۗ وَمَن يَتَّخِذِ الشَّيْطَانَ وَلِيًّا مِّن دُونِ اللَّهِ فَقَدْ خَسِرَ خُسْرَانًا مُّبِينًا ﴿١١٩﴾ يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيهِمْ ۗ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿١٢٠﴾ أُولَٰئِكَ مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ وَلَا يَجِدُونَ عَنْهَا مَحِيصًا ﴿١٢١﴾ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَنُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرَىٰ مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ وَعَدَ اللَّهُ حَقًّا وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ قِيلًا ﴿١٢٢﴾

* لَا خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّن نَّجْوَاهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ ۗ وَمَن يَفْعَلْ ذَلِكَ ابْتِغَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١١٤﴾ وَمَن يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصَلِّهِ ۖ جَهَنَّمَ ۗ وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿١١٥﴾

114. Hakuna kheri katika mengi ya wanayoshauriana kwa siri, isipokuwa kwa yule anayeamrisha kutoa sadaka, au kutenda mema, au kupatanisha baina ya watu. Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi Tutakuja mpa ujira mkubwa.

115. Na anayempinga Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu, na akafuata njia isiyo kuwa ya Waumini, Tutamuelekeza

alikoелеkea, na Tutamuingiza katika Jahannamu. Na hayo ni marejeo maovu.

Najwa Adilifu, Mazungumzo ya Semi

Allah تعالى Amesema,

* لَا خَيْرَ فِي كَثِيرٍ مِّن نَّجْوَاهُمْ

“Hakuna kheri katika mengi ya wanayoshauriana kwa siri...”

Maana yake: Yale watu wanayoambizana.

إِلَّا مَن أَمَرَ بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلَاحٍ بَيْنَ النَّاسِ

“... isipokuwa kwa yule anayeamrisha kutoa sadaka, au kutenda mema, au kupatanisha baina ya watu.”

Maana yake: Isipokuwa kwa aina hii ya mazungumzo.

Imam Ahmad رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Umm Kulthum bint Uqbah رضي الله عنها alisema kuwa, alimsikia Mtume ﷺ akisema,

«لَيْسَ الْكَذَّابُ الَّذِي يُضِلُّ بَيْنَ النَّاسِ قَبِيحًا خَيْرًا، أَوْ يَقُولُ خَيْرًا»

“Sio muongo anayewapatanisha watu kwa kusema maneno yenye kheri.”Alisema pia, “Sijamsikia akiruhusu kusema uongo ila katika hali tatu. Katika vita, kusuluhisha watu, na maneno ya mume kwa mke na mke kwa mume.” Umm Kulthum bint Uqbah رضي الله عنها alikuwa katika wanawake matajiri, walioahidi utiifu kwa Mtume ﷺ,¹ Kikundi kilinukuu Hadithi hii, isipokuwa Ibn Majah.² Imam Ahmad amemnuuu Abu Ad-Dardaa رضي الله عنه akisema, Mtume ﷺ alisema,

«أَلَا أُخْبِرُكُمْ بِأَفْضَلِ مِنْ دَرَجَةِ الصَّيَامِ، وَالصَّلَاةِ، وَالصَّدَقَةِ؟»

“Nisikupeni habari bora zaidi kuliko daraja la fungu, Sala, Sadaka?”

Wakasema, ‘Kwanini (Usitujulishe), Ewe Mtume ﷺ.’ Akawaambia,

«إِضْلَاحُ ذَاتِ الْبَيْنِ»

“Kupatanisha watu waliogombana.”¹ Ahmad 6:403² Fat’h-Al-Bari 5:353, Muslim: 4:2011 na Abu Daud 5:218 na Tuhfat Al-Ahwadhi: 6:70 na An-Nasai katika Al-Kubraa 5:193.

Pia alisema:

«وَفَسَادُ ذَاتِ الْبَيْنِ هِيَ الْحَالِفَةُ»

“Na kugombanisha baina ya watu ni angamizo”.

Abu Dawud na At-Timidh¹ walinukuu Hadithi hii, na At-Tirmidhi alisema kuwa ni “Hasan Sahihi.” Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ أَتْبَعَاءَ مَرْضَاتِ اللَّهِ

“Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu.”

Kwa uaminifu na kungojea malipo kutoka kwa Allah تعالى, Aliye juu na Mtukufu zaidi,

فَسَوْفَ نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا

“...Basi Tutakuja mpa ujira mkubwa.” Maana yake: Malipo makubwa yasiyo kadirika.

Adhabu kwa Kumpinga Mtume ﷺ na Kufuata Njia Tofauti na Ile ya Waumini.

Kauli ya Allah تعالى,

وَمَنْ يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِنْ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَىٰ

“Na anayempinga Mtume baada ya kumdhahirikia uwongofu...”

Maana yake: Mwenye kushika njia kwa kukusudia nyingine dhidi ya sharia iliyoshushwa kwa Mtume ﷺ, baada ya ukweli kubainika. Kauli ya Allah تعالى,

وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ

“....na akafuata njia isiyo kuwa ya Waumini...”

Inakusudia aina ya tabia ambayo inafanana sana na sifa ya mwanzo na huenda khitilafu hizi ni za maandishi katika sheria (Qur'an au Sunnah) au khitilafu za Ummah wa Muhammad ﷺ waliyokubaliana. Ummah wa Muhammad ﷺ umekingwa na makosa wanapokubaliana wote katika jambo, nalo linatokana na kutukuzwa kwao na kuadhimishwa Mtume wao. Zipo Hadithi sahihi nyingi juu ya somo hili. Allah تعالى Alionya kuhusu hili aliposema,

¹ Ahmad 6:444, Abu Dawud 9:49 na At-Tirmidhi 2509.

نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصَلِّهِ ۖ جَهَنَّمَ ط وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿١١٤﴾

“...Tutamuelekeza alikoelekea, na Tutamuingiza katika Jahannamu. Na hayo ni marejeo maovu.”

Maana yake: Mmoja anapofuata njia hii chafu, Tutamuadhibu kwa kuifanya njia kuonekana nzuri katika nafsi yake, na Tutamrembeshea ili aweze kuvutika zaidi. Kwa mfano, Allah تعالى Aliposema,

فَدَرَنِي وَمَنْ يُكَذِّبْ بِهَذَا الْحَدِيثِ ط سَنَسْتَدْرِجُهُمْ مِّنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٨﴾

“Basi niache na wanaokadhibisha maneno haya! Tutawavutia kidogo kidogo kwa mahali wasipo pajua.” (68:44)

فَلَمَّا زَاغُوا أَزَاعَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ

“Walipopotoka, Mwenyezi Mungu Aliziachia nyoyo zao zipotoke.” (61:5)

وَتَذَرُهُمْ فِي طُعَيْنِهِمْ يَعْصَمُونَ ﴿١١٥﴾

“...Tunawaacha katika maasi yao wakitangatanga...” (6:110)

Allah تعالى Aliufanya moto kuwa kipambanuzi cha watu wa aina hiyo siku ya kiyama. Kwa hakika njia ya wale wanaokwepa muongozo sahihi wataingizwa Motoni siku ya Kiyama. Kama ilivyotolewa ushahidi na Kauli ya Allah تعالى,

﴿١١٦﴾ أَحْشُرُوا الَّذِينَ ظَلَمُوا وَأَزْوَاجَهُمْ

“Wakusanyeni waliodhulumu, na wake zao,...” (37:22)

Na Kauli ya Allah تعالى,

وَرَزَا الْمَجْرُمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُمْ مُوَاقِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُوا عَنْهَا مَصْرِفًا ﴿١١٧﴾

“Na wakhalifu watauona Moto na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuuepuka.” (18:53)

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ ۚ وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ

ضَلَّ ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿١١٨﴾ ۚ إِنَّ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ إِلَّا إِنثًا وَإِنْ يَدْعُونَ إِلَّا شَيْطَانًا

مَّرِيدًا ﴿١١٩﴾ ۚ لَعَنَهُ اللَّهُ وَقَالَ لَأَتَّخِذَنَّ مِنْ عِبَادِكَ نَصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿١٢٠﴾ وَلَا ضَلِيلَهُمْ

وَلَا مَنِيْنَهُمْ وَلَا مَرْتَبَهُمْ فَلْيَبْتِكُنْ ءَاذَانَ الْاَنْعَامِ وَلَا مَرْتَبَهُمْ فَلْيَغْيِرْ خَلْقَ اللّٰهِ وَمَنْ
يَتَّخِذِ الشَّيْطٰنَ وَلِيًّا مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ فَقَدْ خَسِرَ خُسْرٰنًا مُّبِيْنًا ﴿١١٦﴾ يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيْهِمْ وَمَا
يَعِدُهُمُ الشَّيْطٰنُ اِلَّا غُرُوْرًا ﴿١١٧﴾ اُوْلٰئِكَ مَاوٰهُمْ جَهَنَّمُ وَلَا يَخْرُجُوْنَ عَنْهَا حٰيْصًا ﴿١١٨﴾
وَالَّذِيْنَ ءَامَنُوْا وَعَمِلُوْا الصّٰلِحٰتِ سَنُدْخِلُهُمْ جَنَّٰتٍ تَجْرِيْ مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِيْنَ
فِيْهَا اَبَدًا وَعَدَّ اللّٰهُ حَقًّا وَمَنْ اَصْدَقُ مِنَ اللّٰهِ قِيْلًا ﴿١١٩﴾

116. Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehi kushirikishwa na kitu. Lakini Yeye Husamehe yasiyo kuwa hayo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu basi huyo amepotea upotovu wa mbali.

117. Wao hawawaombi badala ya Mwenyezi Mungu ila masanamu yenye majina ya kike, hawamuombi ila Shetani aliyeani.

118. Mwenyezi Mungu Amemlaani. Naye Shetani alisema: Kwa yakini nitawachukua sehemu maalumu katika waja wako.

119. Na hakika nitawapoteza na nitawatia matamano, na nitawaamrisha, basi watakata masikio ya wanyama, na nitawaamrisha, basi watabadili Aliyumba Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumfanya Shetani kuwa ni mlinzi wake badala ya Mwenyezi Mungu, basi huyo amekhasiri khasara ya dhahiri.

120. Anawaahidi na anawatia tamaa. Na Shetani hawaahidi ila udanganyifu.

121. Hao makao yao ni Jahannamu, na wala hawapati makimbilio kutoka humo.

122. Na wale walioamini na wakatenda mema, Tutawaingiza katika Bustani zipitayo mito kati yake. Watadumu humo milele. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo kweli. Na nani mkweli zaidi kwa usemi kuliko Mwenyezi Mungu.

Shirki Haitosamehewa, kwa Hakika Mushirikina Wanaabudu Shetani

Tulizungumza Kauli ya Allah تعالی،

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ

“Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehi kushirikishwa na kitu. Lakini Yeye Husamehe yasiyo kuwa hayo kwa Amtakaye.”

Mwanzo wa sura hii tumeeleza mengi kuhusu aya hii. Na Kauli Yake Allah تعالی،

وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿١١٤﴾

“Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu basi huyo amepotea upotovu wa mbali.”

Maana yake: Atakuwa amechukua njia nyingine isiyo sahihi, akachepuka muongozo na uadilifu, akajiagamiza duniani na Akhera, na akapoteza faraja duniani na Akhera. Juwaybir alisema kuwa Adh-Dhahhak aliizungumzia Kauli ya Allah تعالی،

إِنْ يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ إِلَّا إِنْتَنَا

“Wao hawawaombi badala yake Yeye ila masanamu yenye majina ya kike.”

Mushirikina walidai malaika ni binti za Allah تعالی،¹ wakisema, “Tunawaabudu ili watukurubishe kwa Allah تعالی.” Waliwachukulia malaika kama miungu, kwa kusema visanamu vya kike na kuamua kuwa, “Hivi visanamu vinashabihiana na mabinti wa Allah (maana yake: Malaika) ambao tunawaabudu.” Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالی،

أَفَرَأَيْتُمُ اللَّاتَ وَالْعُزَّىٰ ﴿١١٥﴾

“Je! Mmemuona Lata na Uzza?” (53:19)

Na Kauli Yake Allah،

وَجَعَلُوا الْمَلَائِكَةَ الَّذِينَ هُمْ عِبَادُ الرَّحْمَنِ إِنْتَنَا

“Na wakawafanya Malaika, ambao ni waja wa Mwingi wa Rehema, ni wanawake!” (43:19)

¹ At-Tabari 9:209.

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَجَعَلُوا بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْجَنَّةِ نَسَبًا

“Na wameweka mahusiano ya nasaba baina yake na majini.”
(37:158)

وَإِنْ يَدْعُونَ إِلَّا شَيْطَانًا مَّرِيدًا ﴿٣٧﴾

“...wala hawamuombi ila Shetani aliyeasi.”

Maana yake: Shetani amewaamrisha wafanye hivyo na akafanya ionekane kuwa sawa nzuri katika macho yao. Hivyo, wanaabudu shetani kwa dhati, kama Allah تعالى Alivyosema:

* أَلَمْ أَعْهَدْ إِلَيْكُمْ يٰٓبَنِي آدَمَ أَنْ لَا تَعْبُدُوا الشَّيْطَانَ

“Je! Sikuagana nanyi, enyi wanaadamu, kuwa msimuabudu Shetani?” (36:60)

Allah تعالى Amesema kuwa siku ya Hukumu, Malaika watabainisha kuhusu mushrikina waliokuwa wakiwaabudu hapa duniani:

بَلْ كَانُوا يَعْبُدُونَ الْجِنَّ أَكْثَرُهُمْ بِهِمْ مُّؤْمِنُونَ ﴿٣٨﴾

“Bali wao walikuwa wakiwaabudu majini; wengi wao wakiwaamini hao.” (34:41)

Na Kauli Yake،

لَعَنَهُ اللَّهُ

“Mwenyezi Mungu Amemlaani.”

Maana yake: Alimfukuza na akamuondolea Huruma Yake.

لَأَتَّخِذَنَّ مِنْ عِبَادِكَ نَصِيبًا مَّفْرُوضًا ﴿٣٩﴾

“...Kwa yakini nitawachukua sehemu maalumu katika waja wako.”

¹ At-Tabari 9:209.

Maana yake: Fungu maalumu lijulikanalo. Muqatil bin Hayyan alitoa maelezo, "Katika kila elfu moja, mia tisa tisini na tisa wataingizwa Motoni na mmoja Peponi."

وَلَا ضِلَّيْنَهُمْ

"Na hakika nitawapoteza."

Maana yake: Wasijue njia sahihi

وَلَا مَنِينَهُمْ

"...na nitawatia matamano..."

Kuwaghilibu wasifanye toba, kufahamisha matarajio yasiyokuwepo, kuwashajiisha wacheleweshe na kuahirisha amali njema, na kuwachanganya. Na Kauli Yake,

وَلَا مَرْنَهُمْ فَلْيَبْتِكُنْ إِذَابَ الْأَتْعَمِ

"...na nitawaamrisha, basi watakata masikio ya wanyama."

Maana yake: Kukata masikio yao ili wapate daraja la 'Bashirah'¹, Saibah² na Wasilah.³ Kama walivyoelezea Qatadah na As-Suddi.⁴

وَلَا مَرْنَهُمْ فَلْيَغْيِرْ خَلْقَ اللَّهِ

"...na nitawaamrisha, basi watabadili Aliyoumba Mwenyezi Mungu..."

Maana yake: Kuchinja na kutia alama, kwa mujibu wa Al-Hasan bin Abi Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى. Katika Sahihi yake, Muslim alinukuu kuharamishwa kutia alama uso, ambayo katika maneno yake amesema: "Allah تعالى Amlaani yeyote anayefanya hivyo."⁵ Pia imenukuliwa katika Sahihi kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنهما, "Allah تعالى Awalaani wenye Tatoo na wenye kuchora, na

¹Ngamia ambaye maziwa yake yaliwekwa kwa ajili ya masanamu na hapana aliyeruhusiwa kumkemea.

²Ngamia aliyeachiwa na kulishwa kwa ajili ya masanamu na hakubebeshwa chochote.

³Ngamia aliyeachwa huru kwa ajili ya masanamu kwa sababu alizaa ngamia jike katika mzao wa kwanza, na akazaa tena jike katika mzao wa pili.

⁴At - Tabari 9:214.

⁵Muslim 3:1618 na Fat'hul Bari 10:392.

wanaonyoa nyusi na yule anayewanyoa, na wale wanaochonga meno kwa ajili ya urembo, wanabadilisha kilichoumbwa na Allah تعالیٰ. Kisha akasema, 'Kwa nini nisimlaani mtu aliyelaaniwa na Mtume ﷺ ambapo kitabu cha Allah تعالیٰ kinaamrisha.' Akirejea Aya,

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا وَاتَّقُوا اللَّهَ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥٩﴾

"Na anachokupeni Mtume chukueni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu." (59:7)¹

Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَمَنْ يَتَّخِذِ الشَّيْطَانَ وَلِيًّا مِّن دُونِ اللَّهِ فَقَدْ خَسِرَ خُسْرَانًا مُّبِينًا ﴿٦٠﴾

"Na mwenye kumfanya Shetani kuwa ni mlinzi wake badala ya Mwenyezi Mungu, basi huyo amekhasiri khasara ya dhahiri."

Ina maana, atakuwa amepoteza maisha ya dunia na ya Akhera. Kwa hakika hii ni aina ya upotovu ambayo haiwezi kulipizwa au kuhifadhiwa.

Kauli ya Allah تعالیٰ,

يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيهِمْ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٦١﴾

"Anawaahidi na anawatia tamaa. Na Shetani hawaahidi ila udanganyifu."

Inawaelezea ukweli halisi: Bila shaka, huwapa ahadi za ghibiba wafuasi wake na huwahadaa mpaka waamini kuwa wao ni washindi hapa duniani na Akhera. Kwa sababu hii Allah تعالیٰ Amesema,

وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٦١﴾

"Na Shetani hawaahidi ila udanganyifu."

¹ Fat'hul Bari 8:498.

Allah تعالى Anaeleza kuwa siku ya kurejea,

وَقَالَ الشَّيْطَانُ لَمَّا قُضِيَ الْأَمْرُ إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعَدَ الْحَقُّ وَوَعَدْتُكُمْ فَأَخْلَفْتُكُمْ
وَمَا كَانَ لِي عَلَيْكُمْ مِّنْ سُلْطَانٍ

“Na Shetani atasema itapokatwa hukumu: Hakika Mwenyezi Mungu Alikuahidini ahadi ya kweli. Nami nilikuahidini; lakini sikukutimizieni. Na sikuwa na mamlaka juu yenu...” (14:22)

Mpaka,

إِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Hakika madhalimu watakuwa na adhabu chungu.” (14:22)

Kauli ya Allah تعالى, “Ulaaika.” Yaani: Wale wamfatao shetani na waliotiwa tamaa nae. Kauli ya Allah تعالى,

أُولَئِكَ

“Hao.” Inahusu wale wanaopenda na kupendelea yale walioachiwa na kuhakikishiwa na shetani.

مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ

“...makao yao ni Jahannamu...”

وَلَا يَجِدُونَ عَنْهَا مَحِيصًا

“...na wala hawapati makimbilio kutoka humo...”

Kuwa ni mwisho na makazi siku ya kufufuliwa. Maana yake: Hawatoweza kukwepa, kuinga au kuepuka Jahanamu,

Malipo kwa Waja Wema

Kisha Allah تعالى Akataja hali za waja wema na heshima maridhawa watakayoichuma mwishoni. Allah تعالى Amesema,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

“Na wale walioamini na wakatenda mema.”

Maana yake: Nyoyo zao zilisadiki ukweli na viungo vyao vilinyenyekea amali njema walizoamriwa, wakati huo huo wakiacha mambo maovu waliyokatazwa kufanya.

سُنْدُخُلُومٍ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

“...Tutawaingiza katika Bustani zipitayo mito kati yake...”

Muradi wake, watafikiri wapi wangependa mito hiyo itiririke na wataelekea huko,

خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا

“Wataidumu humo milele.”

Maana yake: Bila kikomo wala kutolewa humo,

وَعَدَ اللَّهُ حَقًّا وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ قِيلًا

“...Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo kweli.”

Hii ni ahadi ya kweli kutoka kwa Allah تعالی, hapana shaka, Ahadi ya Allah تعالی ni kweli. Kisha Allah تعالی Amesema,

وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ قِيلًا

“Na nani mkweli zaidi kwa usemi kuliko Mwenyezi Mungu.”

Kadhalika hapana Mola mwingine asiyekuwa yeye, Mtume ﷺ alikuwa akisema katika hutuba zake,

«إِنَّ أَصْدَقَ الْحَدِيثِ كَلَامُ اللَّهِ، وَخَيْرَ الْهَدْيِ هَدْيُ مُحَمَّدٍ ﷺ، وَشَرُّ الْأُمُورِ مُخَدَّنَاتُهَا، وَكُلُّ مُخَدَّنَةٍ بَدْعَةٌ، وَكُلُّ بَدْعَةٍ ضَلَالَةٌ، وَكُلُّ ضَلَالَةٍ فِي النَّارِ»

“Hakika masimulizi ya kweli zaidi ni Maneno ya Allah تعالی, na bora ya muongozo ni muongozo wa Muhammad ﷺ. Na shari ya mambo ni uzushi wake, na kila uzushi ni bidaa, na kila bidaa ni upotevu, na kila upotevu ni Motoni.”

* * *

لَيْسَ بِأَمَانِيكُمْ وَلَا أَمَانِي أَهْلِ الْكِتَابِ مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا
 يُجْزَى بِهِ وَلَا يَجِدْ لَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿١٢٣﴾
 وَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ
 مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظَلَّمُونَ نَقِيرًا ﴿١٢٤﴾
 وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ وَاتَّبَعَ
 مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۗ وَاتَّخَذَ اللَّهُ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٢٥﴾ وَلِلَّهِ
 مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ
 شَيْءٍ مُّحِيطًا ﴿١٢٦﴾ وَاسْتَفْتُونَكَ فِي النِّسَاءِ ۗ قُلِ اللَّهُ
 يُفْتِيكُمْ فِيهِنَّ وَمَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتَابِ فِي يَتِمَى
 النِّسَاءِ الَّتِي لَا تُوْتُوْنَهُنَّ مَا كُتِبَ لَهُنَّ وَتَرْغَبُونَ أَنْ
 تَنْكِحُوهُنَّ ۗ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الْوَالِدِ وَأَنْ تَقُومُوا
 لِلْيَتَامَىٰ بِالْقِسْطِ ۗ وَمَا تَفَعَّلُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِهِ
 عَلِيمًا ﴿١٢٧﴾

لَيْسَ بِأَمَانِيكُمْ وَلَا أَمَانِي أَهْلِ
 الْكِتَابِ مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَى
 بِهِ وَلَا يَجِدْ لَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا
 وَلَا نَصِيرًا ﴿١٢٣﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ
 مِنَ الصَّالِحَاتِ مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ
 وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ يَدْخُلُونَ
 الْجَنَّةَ وَلَا يُظَلَّمُونَ نَقِيرًا ﴿١٢٤﴾
 وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِمَّنْ أَسْلَمَ
 وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ وَاتَّبَعَ
 مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا ۗ وَاتَّخَذَ اللَّهُ
 إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٢٥﴾ وَلِلَّهِ
 مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ
 وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيطًا ﴿١٢٦﴾

123. Si kwa matamano yenu, wala matamano ya Watu wa Kitabu! Anayefanya ubaya atalipwa kwalo, wala hatajipatia mlinzi wala wa kumnusuru, isipo kuwa Mwenyezi Mungu.

124. Na anayefanya mema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini - basi hao wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa hata kadiri ya tundu ya kokwa ya tende.

125. Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule aliyeusilimisha uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa mwema, na anafuata mila ya Ibrahim mwongofu? Na Mwenyezi Mungu Alimfanya Ibrahim kuwa ni rafiki mwendani.

126. Ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo duniani. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuvizunguka vitu vyote.

Ufanisi Unafikiwa kwa Kufanya Amali Njema na Sio Ndoto za Mchana

Qatadah alisema, Tulielezwa kuwa Waislamu na Watu wa Kitabu walishindana kwa kila mmoja kujifakharisha alipo, Watu wa kitabu walisema, 'Mtume wetu alitangulia kabla ya Mtume wenu, na kitabu chetu kilikuja kabla ya chenu, kwa hiyo sisi tuna haki zaidi kwa Allah تعالی kuliko nyinyi.' Waislamu walijibu, 'Bali tuna haki zaidi kwa Allah تعالی kuliko nyie. Mtume wetu ni wa mwisho na kitabu chetu kinakusanya vitabu vyote vilivyopita.' Allah تعالی ndipo Alipotremsha,

لَيْسَ بِأَمَانِيكُمْ وَلَا أَمَانِي أَهْلِ الْكِتَابِ مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَى بِهِ

***“Si kwa matamano yenu, wala matamano ya Watu wa Kitabu!
Anayefanya ubaya atalipwa kwalo”***

وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ

***“Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule aliye usilimisha uso wake
kwa Mwenyezi Mungu, naye akawa mwema.”***

Kisha Allah تعالی Aliunga mkono hoja ya waislamu dhidi ya wapinzani wa dini nyingine.¹ Kauli sawa na hizo zilinasibishwa na As-Suddi, Masruq, Adh-Dhahhak na Abu Salih, na wengineo.² Al-Awfi alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما aliitolea maelezo Aya (4:125):

“Wafuasi wa dini mbalimbali walibishana, watu wa Taurati walisema, ‘kitabu chetu ni bora kuliko kitabu kingine chochote na Mtume wetu ni bora kuliko Mtume yeyote. Watu wa Injili nao wakasema vivyo hivyo.’ Ama Waislamu wao walisema, ‘Hakuna dini nyingine isipokuwa Uislamu tu na kitabu chetu kimefuta kila kitabu, Mtume wetu ni Mtume wa mwisho, na tuliamrisha kuamini vitabu vyenu na kushikamana kwa kukifanyia kazi kitabu chetu”. Allah تعالی Akawahukumu baina yao, kwa kusema,

¹ At-Twabary 9:229.

² At-Twabary 9:229-231.

لَيْسَ بِأَمَانِيكُمْ وَلَا أَمَانِي أَهْلِ الْكِتَابِ مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَى بِهِ

***“Si kwa matamania yenu, wala matamania ya Watu wa Kitabu!
Anayefanya ubaya atalipwa kwalo.”***

Aya hii inaashiria kuwa suala la dini sio tu kwa ajili ya matamania na njozi za mchana au kwa matarajio yasiyo na mashiko. Bali, dini iliyokubaliwa inategemea kilichomo ndani ya nafsi na ambacho kimethibitishwa na matendo, si kweli kuwa mmoja anapotamka jambo hulifikia kwa madai yake. Si kweli kila anayedai kuwa yuko kwenye ukweli, ndivyo alivyo, kwa sababu ya kauli yake tu, mpaka madai yake yapate uthibitisho kutoka kwa Allah تعالى.

Kama Kauli ya Allah تعالى inavyosema,

لَيْسَ بِأَمَانِيكُمْ وَلَا أَمَانِي أَهْلِ الْكِتَابِ

“Si kwa matamania yenu, wala matamania ya Watu wa Kitabu!”

Maana yake: Uislamu hautofikiwa na wewe au nyie kwa utashi tu. Bali msingi ni kumtii Allah تعالى na kufuata yale aliyoyaamrisha kupitia ulimi wa Mtume ﷺ. Baadaye Allah تعالى Amesema,

مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَى بِهِ

“Anayefanya ubaya atalipwa kwalo.”

Hii ni kama Kauli nyingine ya Allah تعالى,

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٢٠٦﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٢٠٧﴾

“Basi anayetenda chembe ya wema, atauona! Na anayetenda chembe ya uovu atauona!”

Na ilinukuliwa kuwa Aya hizi zilipoteremshwa, zilikuwa nzito na ngumu kwa maswahaba wengi. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Aisha رضي الله عنها alisema, ‘Nilisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Najua aya iliyo ngumu ndani ya Qur’an.” Akasema, “Ni ipi Ewe Aishah!’ Nilisema,

¹ At - Twabary 9:229-231.

مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَ بِهِ

“Anayefanya ubaya atalipwa kwalo.”

«هُوَ مَا يُصِيبُ الْعَبْدَ الْمُؤْمِنَ، حَتَّى التَّكْبِيَةِ يُنْكَبُهَا»

“Hayo ndiyo yanayomfika mja muumini, hata matatizo yanayomkera.”¹

Ibn Jarir رحمه الله تعالى na Abu Dawud رحمه الله تعالى waliinukuu Hadithi hii.² Said bin Mansur alinukuu kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema, “Wakati aya,

مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَ بِهِ

“Anayefanya ubaya atalipwa kwalo.”

Ilipoteremshwa, ilikuwa ni nzito na ngumu kwa Waislamu. Mtume ﷺ akasema,

«سَدُّوْا وَقَارِبُوْا، فَإِنَّ فِي كُلِّ مَا يُصَابُ بِهِ الْمُسْلِمُ كَفَّارَةٌ، حَتَّى الشُّوْكَةِ يُشَاكُّهَا،
وَالنَّكْبَةِ يُنْكَبُهَا»

“Shikamaneni na karibianeni, kwani katika kila kinachomsibu Muislamu, kuna kafara hata ikiwa mwiba unaomchoma katika ngozi yake na madhila ayapatayo, itakuwa ni Kafara kwake (ni faida itakayomuondolea madhambi yake).”³

Na vivyo hivyo alipokea Ahmad kupitia kwa Sufyani bin Uyaynah. Pia ilinukuliwa na Muslim na At-Tirmidhi na An-Nasai.⁴ Kauli ya Allah تعالى,

وَلَا يَجِدْ لَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿٦٦﴾

“...wala hatajipatia mlinzi wala wa kumnusuru, isipokuwa Mwenyezi Mungu...”

Ali bin Abi Talha alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, “Mpaka atakapotubia na Allah تعالى Atamsamehe”⁵ Ilinukuliwa na Ibn Abi Hatim

رحمته الله تعالى

¹ At - Tabari 9:244.

² At - Tabari 9:246 na Abu Dawud 3:471

³ Said bin Mansour 4:1378.

⁴ Ahmad 2:248.

⁵ Muslim 4:1993, Tuhfatul Ahwadhi 8:400 na An-Nasai katika Al-Kubraa 6:328.

وَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ مِنْ ذَكَرٍ أَوْ أُنْثَىٰ وَهُوَ مُؤْمِنٌ

“Na anayefanya mema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini.”

Allah تعالی Anataja fidia kwa amali mbovu na kuwa kwa hakika Atawaadhibu waja, ama hapa duniani, ambayo ni bora kwake, au kesho kiyama, tunaomba hifadhi kwa Allah تعالی kutokana na mwisho huo. Aidha tunamuomba Allah تعالی maisha bora hapa duniani na akhera na Tunamuomba msamaha Wake na huruma Yake. Kisha Allah تعالی Anataja Wema Wake, Ukarimu na Huruma katika kuzikubali amali njema za waja Wake, ima ni wanaume au wanawake, kwa masharti kwamba wanakuwa waumini. Aidha Anaeleza kuwa Atawaingiza waumini peponi na Hatopunguza chochote katika amali zao njema, hata ikiwa uzito wa punje ya *Naqir*, kitone katika kokwa ya tende. Hapo nyuma tulijadili *Fatil* – unyuzi mrefu katika kokwa ya tende, na vyote hivyo, pamoja na *Naqir*. Kadhalika *Qitmir* utando mwembamba juu ya kokwa ya tende vilitajwa ndani ya Qur'an. Kisha Allah تعالی Amesema,

وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُ لِلَّهِ

“Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule aliyeusilimisha uso wake kwa Mwenyezi Mungu”

Maana yake: Anatekeleza vitendo vizuri kwa uaminifu kwa ajili ya Mola na huku akisubiri malipo kutoka kwa Allah تعالی,

وَهُوَ مُحْسِنٌ

“... **akawa mwema...**” Akifuata muongozo sahihi aliouamuru Allah تعالی katika Dini ya kweli ambayo alimtuma nayo Mtume ﷺ. Haya ni masharti mawili bila kutekelezwa hapana amali itakayopokewa kwa mtu yeyote, uaminifu na usahihi. Amali huwa adilifu inapofanywa kwa ajili Yake Allah تعالی Pekee na inakuwa sahihi inapofuata sharia. Hivyo amali inakuwa sahihi kwa nje kwa kufuata sunnah na inakuwa sahihi kwa ndani kwa uaminifu. Endapo amali itakosa moja kati ya sifa hizo, amali huwa batili. Kwa mfano, endapo mtu atakosa msingi wa uaminifu (ikhlas) katika kazi yake, basi mtu huyu atakuwa ni mnafiki ambaye anajionesha kwa watu. Ama yeyote asiyefuata shariah, anakuwa

mjinga na mtu aliyepotea. Wakati mmoja wenu anapozijumuisha nguzo hizo, matendo yake yatakuwa matendo ya muumini muaminifu ambaye amali zake njema zitakubaliwa na madhambi yake kufutwa. Hivyo Allah تعالى Amesema,

وَاتَّبَعَ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا

“Na anafuata mila ya Ibrahim mwongofu?”

Naye ni Muhammad ﷺ pamoja na wafuasi wake hadi siku ya kiyama. Kisha Allah تعالى Alisema katika aya nyingine.

إِنَّ أَوْلَى النَّاسِ بِإِبْرَاهِيمَ لَلَّذِينَ اتَّبَعُوهُ وَهَذَا النَّبِيُّ

“Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahim ni wale waliomfuata yeye na Nabii huyu.” (3:68)

Na Kauli Yake Allah تعالى,

ثُمَّ أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ أَنْ اتَّبِعْ مِلَّةَ إِبْرَاهِيمَ حَنِيفًا وَمَا كَانَ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٣﴾

“Kisha Tukakufunulia ya kwamba ufuate mila ya Ibrahim, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.” (16:123)

Hanifa - kwa kudhamiria na kufahamu maana yake ni kuepuka shirki, anakwenda kwenye ukweli kwa umakinifu, hamruhusu yeyote kumkwaza au kumzuia.

Ibrahim Khalil wa Allah تعالى

Kauli ya Allah تعالى,

وَاتَّخَذَ اللَّهُ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٢٤﴾

“Na Mwenyezi Mungu Alimfanya Ibrahim kuwa ni rafiki mwendani.”

Inashajiisha kumfuata Ibrahim *Khalil* عليه السلام, kwa sababu alikuwa ni Imam mila yake ilifuatwa na kuigwa. Kwani alifikia upeo wa ukaribu wa Allah تعالى, kila mja anatafuta jambo hilo. Alipata daraja la *Khalil*, daraja la juu sana la mapenzi. Alilipata hilo kutokana na utiifu wake kwa Mola wake, kama Allah تعالى Alivyosema:

وإِبْرَاهِيمَ الَّذِي وَفَّى ﴿١٢٧﴾

“Na Ibrahim aliyetimiza ahadi?” (53:37)

﴿ وَإِذْ آتَيْنَا إِبْرَاهِيمَ رُبُّهُ بِكَلِمَاتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ﴾

“Na Mola wake Mlezi Alipomjaribu Ibrahim kwa Kumpa amri fulani, naye akazitimiza...” (2:124)

Na Kauli Yake nyingine kuhusu Ibrahim عليه السلام,

﴿ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ الْمُشْرِكِينَ ﴾

“Hakika Ibrahim alikuwa mfano mwema, mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu, mwongofu, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.” (16:120)

Aya zinazofuata baada ya hapo. Bukhari alimnukuu Amri bin Maymun akisema kuwa Muadh رضي الله عنه aliporejea kutoka Yemen, aliwasalisha Sala ya Fajr na alisoma:

﴿ وَأَتَّخَذَ اللَّهُ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا ﴾

“...Na Mwenyezi Mungu Alimfanya Ibrahim kuwa ni rafiki mwendani...”

Mmoja kati ya watu waliokuwepo alisema, “Bila shaka jicho la mama wa Ibrahim عليه السلام limeliwazika.” Ibrahim عليه السلام aliitwa Khalil wa Allah تعالى kutokana na mapenzi makubwa na Mola wake kutokana na vitendo vyake vya utiifu vilivyopelekea Allah تعالى Kumpenda na Kumridhia. Tunalazimika kutaja kuwa katika Sahihi mbili imeandikwa kuwa Abu Said Al-Khudri رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alipotoa hutuba yake ya mwisho, alisema,

«أَمَا بَعْدُ، أَيُّهَا النَّاسُ فَلَوْ كُنْتُ مُتَّخِذًا مِنْ أَهْلِ الْأَرْضِ خَلِيلًا، لَأَتَّخَذْتُ أَبَا بَكْرٍ
ابْنَ أَبِي قُحَافَةَ خَلِيلًا، وَلَكِنْ صَاحِبُكُمْ خَلِيلُ اللَّهِ»

“Enyi Watu! Iwapo nilitakiwa kumchagua Khalil miongoni mwa watu, ningemchukua, Abubakar bin Abi Quhafah kuwa Khalil wangu. Hata hivyo, Sahibu wenu (yaani yeye) ni Khalil wa Allah.”¹

¹ At - Tabari 9:239.

Jundub bin Abdullah Al-Bajali, Abdullah bin Amr bin Al-A's na Abdullah bin Mas'ud رضي الله عنهم walisimulia kuwa Mtume ﷺ alisema,

«إِنَّ اللَّهَ اتَّخَذَنِي خَلِيلًا، كَمَا اتَّخَذَ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلًا»

*"Hakika Allah Alinichagua kuwa Khalil Wake, kama Alivyomchagua Ibrahim kuwa Khalil wake."*¹

Kauli ya Allah تعالى، وَيَلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

"Ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo duniani."

Maana yake: Kila kitu na kila mmoja ni mali yake, waja na viumbe, na Ana Mamlaka kamili juu ya vyote hivyo. Hapana mmoja anayeweza kutengua Uamuzi wa Allah تعالى au kusaili Hukumu Yake. Haulizwi juu ya yale Ayafanyayo kutokana na Uhuru Wake, Uwezo, Uadilifu, Hekima, Upole na Rehema. Kauli ya Allah تعالى،

وَكَانَ اللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيطًا ﴿١٢٦﴾

"Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kuvizunguka vitu vyote"

Maana yake: Anajua kila kitu na hapana kipitacho cha waja Wake au kujificha kwake. Hapana hata chenye uzito wa atomi, kinachoweza kukwepa Uoni Wake, mbinguni na ardhini, wala chochote kidogo au kikubwa kuliko hicho,

وَسْتَفْتُونَكَ فِي النِّسَاءِ ۗ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِيهِنَّ وَمَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتَابِ فِي يَتِمَّى

النِّسَاءِ الَّتِي لَا تُؤْتُونَهُنَّ مَا كُتِبَ لَهُنَّ وَتَرْغَبُونَ أَن تَنْكِحُوهُنَّ ۚ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ

الْوَالِدَانِ وَأَن تَقُومُوا لِلْيَتَامَىٰ بِالْقِسْطِ ۗ وَمَا تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِهِ عَلِيمًا ﴿١٢٧﴾

"Wanakuuliza nini sharia ya wanawake. Sema: Mwenyezi Mungu Anakutoleeni fatwa juu yao, na mnayosomewa humu Kitabuni kuhusu mayatima wanawake ambao hamuapi walichoandikiwa, na mnapenda kuwaoa, na kuhusu wanyonge katika watoto, na

¹ Fat'hul Bari 7:662.

kwamba muwasimamie mayatima kwa uadilifu. Na kheri yoyote mnayofanya Mwenyezi Mungu Anaijua."

Hukumu Kuhusu Mayatima wa Kike

Bukhari alinukuu kuwa Aisha رضي الله عنها aliizungumzia aya hii,

وَسْتَفْتُونَكَ فِي النِّسَاءِ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِيهِنَّ

"Wanakuuliza nini sharia ya wanawake. Sema: Mwenyezi Mungu Anakutoleeni fatwa juu yao."

Mpaka,

وَنَزَّاعُونَ أَنْ تَنْكِحُوهُنَّ

"...na mnapenda kuwaoa...", "Hiki ni kisa cha mtu anayemlea binti yatima, akiwa muangalizi na mrithi wake. Fedha zake zinachanganyika na za binti kiasi anashirikiana nae hata tawi la mtende alilonalo. Hivyo anataka kumuoa mwenyewe (kwa maslahi ya mali) na anachukia kumuoza mtu mwingine, ambaye watashirikiana fedha zake, katika hisa ya fedha zilizochanganyika na za binti. Hivyo, anakataa kumuoza kwa mtu mwingine. Aya hii iliteremshwa."¹ Pia Muslim ameinukuu,² Ibn Abi Hatim amemnukuu Aisha رضي الله عنها akisema, "Watu walimuuliza Mtume ﷺ (kuhusu binti yatima) hivyo Allah تعالى Akateremsha,

وَسْتَفْتُونَكَ فِي النِّسَاءِ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِيهِنَّ وَمَا يُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتَابِ

"...Wanakuuliza nini sharia ya wanawake. Sema: Mwenyezi Mungu Anakutoleeni fatwa juu yao, na mnayosomewa humu Kitabuni..."

Kinachokusudiwa na kauli ya Allah تعالى, "Kuhusu unachosomewa ndani ya kitabu katika Aya iliyopita ambayo alisema:

وَإِنْ خِفْتُمْ أَلَّا تُقْسِطُوا فِي الْيَتَامَىٰ فَانكِحُوا مَا طَابَ لَكُمْ مِنَ النِّسَاءِ

"Na ikiwa mnaogopa kuwa hatowafanyia mayatima uadilifu, basi oeni mnaowapenda.."³

¹ Fat'hul Bari 7:15 na Muslim 4:1854.

² Muslim 1:377, Ibn Majah 1:50 na Muslim 4:1855.

³ Fat'hul Bari 8:114.

Kisha alisema, Kauli ya Allah تعالى،

وَتَرَعْبُونَ أَنْ تَنْكِحُوهُنَّ

“...na mnapenda kuwaoa...”

Aidha inahusu utashi wa mlezi kutomuoa binti yatima aliye chini ya uangalizi wake, kama hana mali au uzuri. Walezi walizuiwa kuo a mabinti mayatima wenye mali na wazuri bila kuwatendea haki, kama walivyozuiwa kuwaoa wakati si wazuri au si matajiri. Msingi wa Hadithi hii umeandikwa ndani ya sahihi mbili.

Vivyo hivyo mwanaume anapokuwa mlezi wa binti yatima angelipendelea kumuoa yeye mwenyewe. Katika kufanya hivyo, basi amuo e mwanamke mwingine, kwani Allah تعالى Amelifanya jambo hili jepesi kwa Waislamu.¹

Na hii ndio maana ya aya ya kwanza mwanzoni mwa sura. Kuna wakati mwingine mlezi hapendi kumuoa yatima aliye chini ya ulezi wake, kwa sababu hamvutii machoni. Katika hali hii, Allah تعالى Amemzuia mlezi kumzuia binti kuolewa na mume mwingine kwa kuchelea mume wake atatumia fedha ambazo ni shirika ya binti na mlezi.

Ali bin Abi Talha alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuhusu aya ambayo ni Kauli Yake, **“kuhusu mayatima wanawake”** kuwa wakati wa Jahiliyyah, mlezi wa yatima wa kike angelimfunika na kilemba chake, na afanyapo hivyo, hapana mtu atakayemuoa. Kama alikuwa mzuri na alitaka kuo a mtu atakayemuoa, alimuoa na alimiliki mali yake. Endapo hakuwa mzuri, hakumruhusu aolewe mpaka kufariki dunia, na baada ya kufariki dunia alirithi mali yake. Allah تعالى Aliharamisha tabia hii.² Pia alizungumzia Kauli ya Allah تعالى،

وَأَلْمَسْتَضْعَفِينَ مِنْ آلِوَالِدِنَ

“Na kuhusu wanyonge katika watoto.”

Kuwa katika zama za Jahiliyyah, walikuwa wakiwanyima watoto wadogo na wanawake fungu la mirathi. Hivyo Kauli ya Allah تعالى،

¹ Fat'hul Bari 9:6 na Muslim 4:2313.

² At - Tabari 9:264.

لَا تُؤْتُونَهُنَّ مَا كُتِبَ لَهُنَّ

“Hamuwapi walicho andikiwa.”

Allah تعالى Alilikataza hilo na kila mmoja mwenye sehemu yake aichukue. Kisha Akasema,

لِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثِيَيْنِ

“Fungu la mwanamume ni kama fungu la wanawake wawili.”

(4:11)

Bila kujali kuwa ni watoto au watu wazima, kama alivyosema Said bin Jubayr na wenzake .¹

Said bin Jubayr alizungumzia Kauli ya Allah تعالى,

وَأَنْ تَقُومُوا لِلَّيْتِمَىٰ بِالْقِسْطِ

“Na kwamba muwasimamie mayatima kwa uadilifu.”

Kama ilivyo atakapokuwa mzuri na tajiri ungelipenda kumuoa na kuwa naye, hivyo anapokuwa sio mzuri na Maskini, muoe na uwe naye.

Kauli ya Allah تعالى,

وَمَا تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِهِ عَلِيمًا

“Na kheri yoyote mnyafanya Mwenyezi Mungu Anaijua.”

Inahimiza kufanya amali njema na kutekeleza amri, na anaeleza kuwa Allah تعالى Anayafahamu yote hayo na Atawalipa kwayo kwa vilivyo bora na kwa hali iliyo nzuri.

* * *

¹ Attwayalisi 449 Sanadi Dhaifu.

وَإِنِ امْرَأَةٌ خَافَتْ مِنْ بَعْلِهَا نُشُورًا أَوْ إِعْرَاضًا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يُصْلِحَا بَيْنَهُمَا صُلْحًا وَالصُّلْحُ خَيْرٌ وَأُحْضِرَتِ الْأَنْفُسُ الشُّحَّ وَإِنْ تُحْسِنُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١٢٨﴾ وَلَنْ تَسْتَطِيعُوا أَنْ تَعْدِلُوا بَيْنَ النِّسَاءِ وَلَوْ حَرَصْتُمْ فَلَا تَمِيلُوا كُلَّ الْمِيلِ فَتَدْرُوهَا كَالْمُعَلَّقَةِ وَإِنْ تُصْلِحُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١٢٩﴾ وَإِنْ يَتَفَرَّقَا يُغْنِ اللَّهُ كُلًّا مِنْ سَعَتِهِ وَكَانَ اللَّهُ وَاسِعًا حَكِيمًا ﴿١٣٠﴾ وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَلَقَدْ وَصَّيْنَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَإِيَّاكُمْ أَنْ اتَّقُوا اللَّهَ وَإِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَكَانَ اللَّهُ غَنِيًّا حَمِيدًا ﴿١٣١﴾ وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَكَفَى بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿١٣٢﴾ إِنَّ يَسَاءَ يُذْهِبِكُمْ أَيُّهَا النَّاسُ وَيَأْتِ بِفَاحِشَاتٍ ؕ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ قَدِيرًا ﴿١٣٣﴾ مَنْ كَانَ يُرِيدُ ثَوَابَ الدُّنْيَا فَعِنْدَ اللَّهِ ثَوَابُ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَكَانَ اللَّهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿١٣٤﴾

وَإِنِ امْرَأَةٌ خَافَتْ مِنْ بَعْلِهَا نُشُورًا أَوْ إِعْرَاضًا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يُصْلِحَا بَيْنَهُمَا صُلْحًا وَالصُّلْحُ خَيْرٌ وَأُحْضِرَتِ الْأَنْفُسُ الشُّحَّ وَإِنْ تُحْسِنُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١٢٨﴾ وَلَنْ تَسْتَطِيعُوا أَنْ تَعْدِلُوا بَيْنَ النِّسَاءِ وَلَوْ حَرَصْتُمْ فَلَا تَمِيلُوا كُلَّ الْمِيلِ فَتَدْرُوهَا كَالْمُعَلَّقَةِ وَإِنْ تُصْلِحُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١٢٩﴾ وَإِنْ يَتَفَرَّقَا يُغْنِ اللَّهُ كُلًّا مِنْ سَعَتِهِ وَكَانَ اللَّهُ وَاسِعًا حَكِيمًا ﴿١٣٠﴾

128. Na mwanamke akihisi majivuno na magomvi kutoka kwa mumewe (upande mmoja), basi si vibaya kwao wakisikizana

kwa suluhu. Na suluhu ni bora. Na nafsi zimeumbiwa tabia ya ubakhili mkubwa tamaa na choyo. Na mkifanya wema na mkamchamungu basi hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyatenda.

129. Wala hamtaweza kufanya uadilifu baina ya wake, hata mkipupia. Kwa hivyo msimili (upande mmoja) moja kwa moja mkamuwacha (mmojo) kama aliyetundikwa. Na mkisikizana na mkamchamungu basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghira na Mwenye Kurehemu.

130. Na wakitengana Mwenyezi Mungu Atamtosheleza kila mmoja katika wao kwa ukunjufu wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu Mwenye Hekima.

Hukumu Inayohusu Kujitenga kwa Mume

Allah تعالى Ameeleza, na hivyo Kuhukumu, kuwa baadhi ya wakati mume hujiweka mbali na mke, wakati mwingine huwa upande wake na wakati mwingine huachana naye katika hali ya mwanzo, mke anapochelea kuwa mume anajitenga naye au anamkimbia, anaruhusiwa kusamehe haki zote au baadhi, kama vile chakula, mavazi, malazi na kadhalika na mume anatakiwa kukubali tahfifu kutoka kwa mke. Hivyo, hapana madhara kama atatoa tahfifu hiyo, na kama mume ataikubali.

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يُصَلِّحَا بَيْنَهُمَا صُلْحًا

“Basi si vibaya kwao wakisikizana kwa suluhu.”

Kisha Akasema,

وَالصُّلْحُ خَيْرٌ

“Na suluhu ni bora.” Kuliko kumuacha na kumtaliki. Kauli ya Allah تعالى,

وَأَحْضَرْتُ الْأَنْفُسُ الشُّحَّ

“Na nafsi zimewekewa machoni mwake tamaa na choyo.”

Maana yake: kupatikana muafaka, hata kama itabidi kusamehe baadhi ya haki ni bora kuliko kuachana.

Abu Dawud At-Tayalisi amenukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Sawdah, aliogopa kuwa Mtume ﷺ angelimtaliki na alisema, “Ewe Mjumbe wa Allah! Usinitaliki, mpe Aishah siku yangu.” Na alifanya hivyo. Na Baadaye Allah تعالى Alishusha,

وَإِنْ أَمْرًا خَافَتْ مِنْ بَعْلِهَا نُشُوزًا أَوْ إِعْرَاضًا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا

“Na mwanamke akichelea kutupwa au kutojaliwa na mumewe, basi si vibaya kwao...”

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema "Makubaliano yeyote wanayokubaliana kati ya mume na mke yanaridhiwa."¹ At - Tirmidhi alinukuu na akasema ni "Hasan Gharib."²

Katika Sahihi Mbili, ilinukuliwa kuwa Aishah رضي الله عنها alisema kuwa Sawdah bint Zam'ah رضي الله عنها alipokuwa mtu mzima sana, alimuachia yeye siku yake, na Mtume ﷺ alikuwa akiutumia usiku wa Sawdah kwa Aishah رضي الله عنها.³ Kuna masimulizi sawa na haya yaliyokusanywa na Bukhari.⁴ Bukhari pia alinukuu kuwa Aishah رضي الله عنها alitolea maelezo, (4:128) kuwa inahusu, "Mtu aliyemuoa ajuza na hana haja naye na anataka kumtaliki." Hivyo Anasema,

وَإِنْ أَرْأَتْ خَافَتْ مِنْ بَعْلِهَا نُشُورًا أَوْ إِعْرَاضًا

"Na mwanamke akichelea kutupwa au kutojaliwa."

Hivyo aya hii ndipo ilipoteremshwa."⁵

Maana ya "Suluhu ni Bora."

Allah تعالى Amesema,

وَالصُّلْحُ خَيْرٌ

"Na suluhu ni bora."

Ali bin Abi Talhan alisimulia kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa aya hii inahusu, "Pale Mume anapomhiarisha mke kuchagua kukaa naye au kuondoka kwa kuwa hii ni bora kuliko mume kupendelea wake wengine."¹

Hata hivyo, maana iliyo wazi inahusu suluhu ambapo mke anasamehe baadhi ya haki zake alizokuwa nazo kwa mumewe, na mume akikubali tahafifu hiyo, na muafaka huu ni bora kuliko talaka. Kwa mfano, Mtume ﷺ alimbakisha Sawdah bint Zam'ah رضي الله عنها kuwa mkewe. Baada ya kumuachia Aishah رضي الله عنها siku yake. Kwa kumbakiza miongoni mwa wakeze, Ummah wake

¹ At - Tabari 9:255.

² Musnad At-Tayalisi: 349

³ Tuhfatul Ahwadhi 8:403

⁴ Fat'hul Bari 9:233 na Muslim 2:1085.

⁵ Fat'hul Bari 5:257.

⁶ At - Tabari 9:272.

ungelimuiga. Kwa kuwa muafaka na amani ni bora kwa Allah تعالى kuliko talaka. Allah تعالى Amesema,

وَالصُّلْحُ خَيْرٌ

“Na suluhu ni bora.”

Allah تعالى Hapendi Talaka.

وَإِنْ تَحْسَبُوا أَنَّكُمْ مُؤْمِنُونَ وَاللَّهُ يَعْلَمُ حَيْثُ لَا تَحْتَسِبُونَ

“Na mkifanya wema na mkamchamungu basi hakika Mwenyezi Mungu Anazo khabari za yote mnayoyatenda.”

Endapo unamvumilia mke unayemchukia na ukamtendea wema basi Allah تعالى Anajua alifanyalo na Atakulipa malipo maridhawa. Kauli ya Allah تعالى,

وَلَنْ تَسْتَطِيعُوا أَنْ تَعْدِلُوا بَيْنَ النِّسَاءِ وَلَوْ حَرَصْتُمْ

“Wala hamtaweza kufanya uadilifu baina ya wake, hata mkikakamia.”

Maana yake: Enyi watu! Hamtoweza kuwafanyia uadilifu wake zenu kwa kila kitu. Hata mmoja wenu anapogawa siku sawa baina ya wake, bado kutakuwa na tofauti ya mapenzi, utashi, na mahaba, kama Ibn Abbas, Ubaydah As-Salmani, Mujahid, Al-Hasan Al-Basri na Adh-Dhahhak bin Muzahim رضي الله عنهم walivyosema.¹ Imam Ahmad na wakusanyaji wa *Sunan* walinukuu kuwa Aisha رضي الله عنها alisema, “Mtume ﷺ alikuwa akiwatendea wakeze sawa sawa na akatangaza. “Ewe Allah! Huu ni mgawanyo kwa kile ninachomiliki, hivyo Usinilaumu kwa kila Unachomiliki ambacho similiki.” Akikusudia moyo wake. Hayo ni maneno aliyokusanya Abu Dawud,² na Isnad yake ni Sahihi.

Kauli ya Allah تعالى,

فَلَا تَمِيلُوا كُلَّ الْمَيْلِ

“Kwa hivyo msimili moja kwa moja...”

Maana yake: Ukimpenda mkeo mmoja zaidi ya wengine, usizidishe kumtendea hivyo moja kwa moja.

¹ At - Twabari 9:285-287.

² Abu Dawud 21:34, Tuhfatul Ahwadhi 1140, Ibn Majah 1:971, na Nasai 7:63.

فَتَدْرُوها كَالْمُعَلِّقَةِ

“Mkamuwacha (mmojo) kama aliyetundikwa.”

Inahusu mke au wake wengine, maana akabaki kama aliyetundikwa. Ibn Abbas, Mujahid Said bin Jubayr, Al-Hasan, Adh-Dhahhak, Ar-Rabi bin Anas, As-Suddi na Muqatil bin Hayyan رضي الله عنهم walisema kuwa *Mu'allaqah* - kutungikwa maana yake, “Hajatalikiwa wala kubaki kama mke.”¹

Abu Dawud At-Tayalisi رحمه الله تعالى amemnuuu Abu Hurayrah عنه رضي الله akisema, Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ كَانَتْ لَهُ امْرَأَتَانِ فَمَالَ إِلَى إِحْدَاهُمَا، جَاءَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَأَحَدُ شِقَيْهِ سَاقِطٌ»

“Yeyote mwenye wake wawili na akaegemea zaidi kwa mmoja wao, atakuja siku ya Kiyama akiburuza upande wake mmoja.”³

Na Kauli ya Allah تعالى،

وَإِنْ تَصْلِحُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٣٢﴾

“Na mkisikizana na mkamchamungu basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira na Mwenye Kurehemu.”

Aya inasema, ukitenda haki na ukagawa sawa katika uliyo na uwezo nayo, na huku ukimuogopa Allah تعالى katika hali zote, hivyo Allah تعالى Atakusamehe kwa upendeleo uliowafanyia baadhi ya wakezo. Kisha Allah تعالى Amesema,

وَإِنْ يَتَفَرَّقَا يُغْنِ اللَّهُ كُلًّا مِّن سَعَتِهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ وَاسِعًا حَكِيمًا ﴿٣٣﴾

“Na wakitengana Mwenyezi Mungu Atamtosheleza kila mmoja katika wao kwa ukunjufu wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu Mwenye Hekima.”

Hii ni hali ya tatu kati ya mume na mke, ambapo talaka inatuka. Allah تعالى Anaeleza kuwa endapo mume na mke watatengana kwa talaka, basi, Allah تعالى Atamtosha kwa Kumpa mume mke bora zaidi na mwanamke mume bora zaidi, maana ya,

¹ At - Tabari 9:290-292.

² Musnad At-Tayalisi 322.

وَكَانَ اللَّهُ وَاسِعًا حَكِيمًا ﴿١٢٨﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mkunjufu Mwenye Hekima.”

Neema Zake hazina kifani, Utajiri Wake hauna kikomo, Yeye Mjuzi wa yote katika Matendo Yake, Maamuzi na Sheria.

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَلَقَدْ وَصَّيْنَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَإِيَّاكُمْ أَنْ اتَّقُوا اللَّهَ ۚ وَإِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَنِيًّا حَمِيدًا ﴿١٢٩﴾ وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَكَفَى بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿١٣٠﴾ إِنَّ يَسْرًا يُذْهِبُكُمْ أَيُّهَا النَّاسُ وَيَأْتِ بِآخِرِينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ قَدِيرًا ﴿١٣١﴾ مَنْ كَانَ يُرِيدُ ثَوَابَ الدُّنْيَا فَعِنْدَ اللَّهِ ثَوَابُ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿١٣٢﴾

131. Na ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote viliomo katika mbingu na viliomo katika dunia. Na kwa hakika Tuliwausia waliopewa Kitabu kabla yenu, na nyinyi pia, kwamba mumche Mwenyezi Mungu. Na mkikataa, basi ni vya Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo duniani. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitosha, na Msifiwa.

132. Na ni vya Mwenyezi Mungu viliomo katika mbingu na viliomo katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mlinzi.

133. Akitaka Atakuondoeni, enyi watu! Na Awalete wengineo. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa hayo.

134. Anayetaka malipo ya dunia, basi kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo ya dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kuona.

Usia na Umuhimu wa Kumcha Allah تعالیٰ;

Allah تعالیٰ Anaeleza kuwa Yeye Ndie Mmiliki wa mbingu na ardhi na kuwa Yeye Ndiye Mwenye Mamlaka ya Juu. Kwa sababu hiyo Allah تعالیٰ Amesema,

وَلَقَدْ وَصَّيْنَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَإِيَّاكُمْ

“Na kwa hakika Tuliwausia waliopewa Kitabu kabla yenu, na nyinyi pia, kwamba mumche Mwenyezi Mungu.”

Muradi wake, Tumekupendekezeeni Tulilowapendekezea Watu wa Kitabu, Kumcha Allah تعالیٰ, kwa kumuabudu Yeye Pekee bila ya mshirika. Kisha Allah تعالیٰ Amesema,

وَإِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

“Na mkikataa, basi ni vya Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo duniani.”

Katika aya nyingine, Allah تعالیٰ Amesema kuwa Musa عليه السلام aliwaambia watu wake,

إِنْ تَكْفُرُوا أَنْتُمْ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَأِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ

“Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitosha, Msifiwa.” (14:8)

Allah تعالیٰ Amesema,

فَكَفَرُوا وَتَوَلَّوْا وَاسْتَغْنَى اللَّهُ وَاللَّهُ غَنِيٌّ حَمِيدٌ

“Basi wakakufuru, na wakageuka upande. Mwenyezi Mungu Akawa hana haja nao. Na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, si Mhitaji, naye ni Msifiwa.” (64:6)

Maana yake: Yeye ni Mkwasi Asiyetaka kutoka kwa waja wake, na Anastahili shukrani zote katika Maamuzi Yake na Maamrishi Yake. Maana ya Kauli ya Allah تعالیٰ,

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَكَفَى بِاللَّهِ وَكِيلًا

“Na ni vya Mwenyezi Mungu viliomo katika mbingu na viliomo katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Mlinzi.”

Anaiona kila nafsi, na Anajua inachostahiki, Yeye ni Muangaliaji Anashuhudia kila kitu. Kauli ya Allah تعالیٰ,

إِنَّ يَشَأْ يُذْهِبْكُمْ أَيُّهَا النَّاسُ وَيَأْتِ بِآخَرِينَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ ذَٰلِكَ قَدِيرًا ﴿١٢٨﴾

“Akitaka Atakuondoeni, enyi watu! Na Awalete wengineo. Na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa hayo.”

Maana yake: Ana uwezo kukuondosha na kuleta watu wengine iwapo utamkanusha Yeye. Katika aya sawa na hiyo, Allah تعالى Amesema,

وَإِن تَوَلَّوْا يَسْتَبَدِلْ قَوْمًا غَيْرَكُمْ ثُمَّ لَا يَكُونُوا أَمْثَلَكُمْ ﴿١٢٩﴾

“Na mkigeuka Atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi.” (47:38)

Kauli ya Allah تعالى,

مَنْ كَانَ يُرِيدُ ثَوَابَ الدُّنْيَا فَعِنْدَ اللَّهِ ثَوَابُ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

“Anayetaka malipo ya dunia, basi kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo ya dunia na Akhera.”

Maana yake: Enyi mnaopenda maisha ya dunia, jueni kwamba Allah تعالى ana malipo kwa maisha ya dunia na Akhera kwa hiyo ukimuomba Allah تعالى kwa yote, Atakutajirisha, Atakupa na Atakutosheleza kama Allah تعالى Alivyosema,

فَمَنْ النَّاسِ مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا وَمَا لَهُ فِي الْآخِرَةِ مِنْ خَلْقٍ ﴿١٣٠﴾ وَمِنْهُمْ

مَنْ يَقُولُ رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ ﴿١٣١﴾ أُولَٰئِكَ

لَهُمْ نَصِيبٌ مِّمَّا كَسَبُوا ۗ

“Na mkishatimiza ibada zenu basi mtajeni Mwenyezi Mungu kama mlivyokuwa mkiwataja baba zenu au mtajeni zaidi. Na wapo baadhi ya watu wanao sema: Mola wetu Mlezi, tupe duniani! Naye katika Akhera hana sehemu yoyote. Na katika wao wapo wanao sema: Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na Utulinde na adhabu ya Moto! Hao ndio watakaopata sehemu yao kwa sababu ya yale waliyoyachuma...” (2:200-202)

Kauli Yake Allah تعالى،

مَنْ كَانَ يُرِيدُ حَرْثَ الْآخِرَةِ نَزِدْ لَهُ فِي حَرْثِهِ

“Mwenye kutaka mavuno ya Akhera Tutamzidishia katika mavuno yake.” (42:20)

Na Kauli Yake nyingine,

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَّلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَنْ نُرِيدُ

“Anayetaka yapitayo upesi upesi, Tutafanya haraka kumletea hapa hapa Tunayoyataka kwa Tumtakaye...” (17:18)

Mpaka,

أَنْظُرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ

“Angalia vipi Tulivyo wafadhili baadhi yao kuliko wenginewe.” (17:21)

Hivyo Allah تعالى Amesema hapa,

وَكَانَ اللَّهُ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿١٧٤﴾

“Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kuona.”

* * *

شُهِدَآءَ لِلَّهِ

“... mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu...”,

Ni sawa na Kauli Yake:

وَأَقِيمُوا الشَّهَادَةَ لِلَّهِ

“Na simamisheni ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.” (65:2)

Ushahidi unatakiwa kutolewa kwa ukamilifu, kwa ajili ya Allah تعالى, hivyo kufanya ushahidi sawa, wa haki, na usio na mabadiliko au kufutwa.

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

وَلَوْ عَلَىٰ أَنْفُسِكُمْ

“..ijapo kuwa ni juu ya nafsi zenu..”

Maana yake: Toa ushahidi ulio sawa, na useme kweli utakapoulizwa, hata kama matokeo yake ni madhara kwako. Kwa hakika Allah تعالى Atafanya njia ya kutokea na unafuu kwa wote wanaomtii Yeye kwa kila jambo.

Kauli ya Allah تعالى,

أَوْ آلَوَالِدَيْنِ وَالْأَقْرَبِينَ

“...au wazazi wawili na jamaa zenu...”

Maana yake: Hata kama unatakiwa utoe ushahidi dhidi ya wazazi na ndugu zako, usiwapendeleee. Bali, toa ushahidi ulio sawa na ushahidi wa haki hata kama watadhurika wakati wa mchakato huo, kwani ukweli uko juu ya kila mtu na unatakiwa kwa kila mtu. Kauli ya Allah تعالى,

إِنْ يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا فَاللَّهُ أَوْلَىٰ بِهِمَا

“...Akiwa tajiri au masikini Mwenyezi Mungu Anawastahikia zaidi...”

Maana yake: Hao wote Allah تعالى Ndie Anayestahiki zaidi. Na ujue hayo ndiyo yaliyo katika maslaha yao. Kauli Yake تعالى,

فَلَا تَتَّبِعُوا أَهْوَىٰ أَنْ تَعْدِلُوا

“...Basi msifuate matamano, mkaacha kufanya uadilifu...”

Maana yake: Yasikuchukueni matamaniao na mapenzi yenu au kuchukia na bughdha zenu kwa watu ikawapelekeeni kutofanya uadilifu katika mambo yenu, bali shikamaneni na uadilifu katika hali zote.

Kama Alivyosema Allah تعالى،

وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَاٰنُ قَوْمٍ عَلٰٓى اَلَّا تَعْدِلُوْا اَوْ اَعْدِلُوْا هُوَ اَقْرَبُ لِلتَّقْوٰى

“Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu. Fanyeni uadilifu. Hivyo ndio kuwa karibu mno na uchamungu...”
(5:8)

Mtume ﷺ alimpeleka Abdullah bin Rawaha رضي الله عنه kukusanya kodi ya matunda na mazao ya Mayahudi wa Khaybar, walitaka kumpa hongo ili awasahilishie mambo, akawaambia, ‘Wallah! Nimetoka kwa kiumbe adhimu kwangu (Muhammad ﷺ) nanyi nawachukia zaidi kuliko idadi sawa ya Nyani na Nguruwe. Hata hivyo mapenzi yangu kwake Mtume ﷺ na chuki dhidi yenu hainizuii kuwatendea haki.” Kwa hilo, walisema, “Hii (haki) ndio misingi ambayo mbingu na ardhi viliumbwa.” Tutaitaja Hadithi hii baadaye katika *Surat Al-Maida* (sura ya 5) Allah تعالى Akipenda.

Kauli ya Allah تعالى baadaye،

وَإِنْ تَلَوْتُمْ أَوْ تَعْرَضُونَ

“Na mkiupotoa au mkajitenga nao...”

Maana yake: “Mkiuharibu ushahidi na mkaubadilisha.”¹ Kwa mujibu wa Mujahid na wengineo katika *Salaf. Talwu* ni pamoja na upotoshaji na kuongeza kwa kukusudia. Kwa mfano, Allah تعالى Amesema،

وَإِنْ مِنْهُمْ لَفَرِيقًا يَلُودْنَ اَلْسِنَتَهُم بِاَلْكِتٰبِ

“Na wapo baadhi yao wanaopindua ndimi zao katika kusoma Kitabu.” (3:78)

¹ At - Tabari 9:308.

Kujitenga ni Njia ya Kuzuia na Kuficha Ushahidi

Kauli ya Allah تعالى،

وَمَنْ يَكْتُمْهَا فَإِنَّهُ آثِمٌ قَلْبُهُ

“Na atakayeficha basi hakika moyo wake ni wenye kutenda dhambi.” (2:283)

Mtume ﷺ alisema,

«خَيْرُ الشُّهَدَاءِ الَّذِي يَأْتِي بِشَهَادَتِهِ قَبْلَ أَنْ يُسْأَلَهَا»

“Shahidi mzuri ni yule anayetoa ushahidi kabla hajaulizwa kufanya hivyo.”¹

Kisha Allah تعالى Ameonya,

فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿٣٥﴾

“...basi Mwenyezi Mungu Anajua vyema mnayo yatenda.”

Na Atakulipa au Kukuadhibu kufuatana na amali.

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا ءَامِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ءَالِكِتَابِ الَّذِي نَزَّلَ عَلَىٰ رَسُولِهِ ءَالِكِتَابِ

الَّذِي أَنْزَلَ مِنْ قَبْلُ ءَوَمَنْ يَكْفُرْ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ ءَالْيَوْمِ ءَالْآخِرِ فَقَدْ ضَلَّ

ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿٣٦﴾

“Enyi mlio amini! Muaminini Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Kitabu Alichokiteremsha juu ya Mtume wake, na Kitabu Alichokiteremsha kabla yake. Na anayemkataa Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya Akhera, basi huyo amekwisha potelea mbali.” (4:136)

Utaratibu wa Kuwa na Imani Baada ya Kuwa Muumini

Allah تعالى Anaamuru waja wake waumini kushika misingi yote ya Imani, matawi, nguzo na jiwe la msingi. Hii haitajwi kama ziada bali mtazamo wa kukamilisha imani na kuendelea kuidumisha. Mfano, muumini anasoma kila siku katika Sala tano.

¹Muslim 3:1344.

أَهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ ﴿١٣٥﴾

"Tuongoe njia iliyonyooka." Ambayo ina maana tuongoze njia iliyonyooka na tuongozee uongozi na utunyooshee juu yake. Allah تعالى Anawaamuru waumini kumuamini Yeye na Mjumbe Wake, kama Alivyosema,

يَتَّيِبُهَا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا ءَامِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ

"Enyi mliaoamini! Muaminini Mwenyezi Mungu, na Mtume wake."

Kauli ya Allah تعالى،

وَأَلْكَتَبِ الَّذِي نَزَّلَ عَلَى رَسُولِهِ

"...na Kitabu Alichokiteremsha juu ya Mtume Wake..."

Inarejea katika Qur'an ambapo،

وَأَلْكَتَبِ الَّذِي أَنْزَلَ مِنْ قَبْلُ

"...na Kitabu Alichokiteremsha kabla yake..."

Inarejea kwenye vitabu vitakatifu vilivyoteremshwa. Kisha Allah تعالى Amesema،

وَمَنْ يَكْفُرْ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿١٣٦﴾

"Na anayemkataa Mwenyezi Mungu, na Malaika wake, na Vitabu vyake, na Mitume wake, na Siku ya Akhera, basi huyo amekwisha potelea mbali."

Maana yake: Watakuwa wamekengeuka kutoka katika uongozi ulio sahihi na wamejiweka mbali na njia Yake.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا ثُمَّ ءَامَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا ثُمَّ ءَزْدَادُوا كُفْرًا لَمْ يَكُنِ اللَّهُ لِيُغْفِرْ لَهُمْ

وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ سَبِيلًا ﴿١٣٧﴾ بِئْسَ الْمُنْتَفِقِينَ بَأَنَّ هُمْ عَدَابًا أَلِيمًا ﴿١٣٨﴾ الَّذِينَ يَتَّخِذُونَ

الْكُفْرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ؕ أَيَتَغُورُونَ عِنْدَهُمُ الْعِزَّةُ فَإِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا ﴿١٣٩﴾

وَقَدْ نَزَّلَ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتَابِ أَنْ إِذَا سَمِعْتُمْ ءَايَاتِ اللَّهِ يُكْفَرُ بِهَا وَيُسْتَهْزَأُ بِهَا فَلَا تَقْعُدُوا

مَعَهُمْ حَتَّى تَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ ؕ إِنَّكُمْ إِذَا مِتُّمُوهُمْ ؕ إِنَّ اللَّهَ جَامِعُ الْمُنْتَفِقِينَ

وَالْكُفْرِينَ فِي جَهَنَّمَ جَمِيعًا ﴿١٤٠﴾

137. Hakika walioamini, kisha wakakufuru, kisha wakaamini, kisha wakazidi ukafiri, Mwenyezi Mungu hakuwa Mwenye Kuwasamehe wala Kuwaongoza njia.

138. Wabashirie wanafiki kwamba watapata adhabu chungu,

139. Wale ambao huwafanya makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je! Wanataka wapate kwao utukufu? Basi hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu.

140. Naye Amekwisha kuteremshieni katika Kitabu hiki ya kwamba mnaposikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakanushwa na zinafanyiwa kejeli, basi msikae pamoja nao, mpaka waingie katika mazungumzo mengine. Hivyo mtakuwa nanyi mfano wao hao. Hakika Mwenyezi Mungu Atawakusanya wanafiki na makafiri wote pamoja katika Jahannamu”.

Sifa Bainifu za Wanafiki na Hatima yao:

Allah تعالی Ameeleza kuwa yeyote atakayesilimu, akaritadi, akarejea tena, akaritadi tena na akabaki katika ukafiri na akazidisha ukafiri mpaka akafariki dunia, basi hatokuwa na fursa ya kukubaliwa toba baada ya kufa. Wala Allah تعالی Hatomsamehe au Kumuondoa kutoka upotovu kwenda kwenye uongofu sahihi. Kwa sababu hii, Allah تعالی Amesema,

لَمْ يَكُنِ اللَّهُ لِيَغْفِرْ لَهُمْ وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ سَبِيلًا ﴿١٣٧﴾

“...Mwenyezi Mungu Hakuwa Mwenye Kuwasamehe wala Kuwaongoza njia”

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی alinukuu kuwa, baba yake alisema kuwa Ahmad bin Abdallah alisimulia kuwa Hafs bin Jami alisema kuwa Ikrimah alimnukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alitoa maelezo kuhusu,

ثُمَّ أَزْدَادُوا كُفْرًا

“Kisha wakazidi ukafiri.”

“Watabaki kwenye ukafiri mpaka watakapofariki dunia.” Mujahid alisema vivyo hivyo.¹ Kisha Allah تعالی Amesema,

¹At - Tabari 9:315.

بَشِيرِ الْمُتَنَفِقِينَ بِأَنَّ هُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٣٥﴾

“Wabashirie wanafiki kwamba watapata adhabu chungu.”

Hivyo, wanafiki wana sifa hii, kwani wameamini kisha wanakufuru, kwa sababu hii nyoyo zao zimepigwa muhuri. Allah تعالى Anawaelezea wanafiki kuwafanya makafiri kuwa marafiki badala ya waumini, maana wao ni waunga mkono makafiri wa dhahiri, kwani wanawatii na wakiwa pembeni pamoja nao husema, **“Sisi tu pamoja nanyi, hakika sisi tunawacheza shere.”** Maana yake: Wanawacheza shere waumini, katika kuwadhihirishia kuwa wanaafikiana nao. Mwenyezi Mungu kwa kuchukizwa na tabia yao ya kuwa pamoja na makafiri Anasema,

أَيَّتُغُونَ عَنْهُمْ الْعِزَّةَ

“Je! Wanataka wapate kwao utukufu?”

Kisha Allah تعالى Anaelezea kuwa Heshima, Nguvu na Sifa zinamstahiki Yeye Pekee bila washirika na kwa wale ambao Allah تعالى Anawapa sifa hizo.

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعِزَّةَ فَلِلَّهِ الْعِزَّةُ جَمِيعًا

“Mwenye kutaka utukufu basi Utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu.” (35:10) Na,

وَاللَّهُ الْعِزَّةُ وَلِرَسُولِهِ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَلَكِنَّ الْمُتَنَفِقِينَ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٦٣﴾

“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Utukufu - Yeye, na Mtume Wake, na Waumini. Lakini wanafiki hawajui.” (63:8)

Makusudio ya kutafuta utukufu kwa Allah تعالى ni ile hali ya kujikurubisha na ibada Yake, na kuwepo utaratibu mzima katika maisha ya Muumini. Kauli ya Allah تعالى,

وَقَدْ نَزَّلَ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتَابِ أَنْ إِذَا سَمِعْتُمْ آيَاتَ اللَّهِ يُكْفَرُ بِهَا وَيُسْتَهْزَأُ بِهَا فَلَا تَقْعُدُوا

مَعَهُمْ حَتَّى تَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ ۗ إِنَّكُمْ إِذَا مِتْلَهُمْ

“Naye Amekwisha kuteremshieni katika Kitabu hiki ya kwamba mnaposikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakanushwa na zinafanyiwa kejeli, basi msikae pamoja nao, mpaka waingie katika mazungumzo mengine. Hivyo mtakuwa nanyi mfano wao hao.”

Aya hii ina maana, iwapo bado mnafanya yaliyokatazwa, baada ya kujua kukatazwa kwake, mkakaa nao ambapo aya za Allah تعالى zimezuia, mkafanya Istihizai na mkakanusha, na mkapitisha mwendo huo, hivyo mmeshiriki nao katika yale wayafanyao. Hivyo Allah تعالى Amesema,

إِنكُرُوا إِذَا مِثْلَهُمْ

“...Hivyo mtakuwa nanyi mfano wao hao.”

Kuhusu mizigo watakayo chukua, kila ambacho kimeshateremshwa ndani ya kitabu – kama aya inavyo sema, ni aya katika *Al-An'am* (6) ambayo iliteremshwa Makkah.

وَإِذَا رَأَيْتَ الَّذِينَ يَخُوضُونَ فِي آيَاتِنَا فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ

“Na unapowaona wanaoziingilia Aya Zetu, basi jitenge nao.” (6:68)

Muqatil bin Hayyan alisema kuwa, aya hii imeondosha hukumu iliyopo katika *Surat Al-An'aam*. Maana yake: Imeondoshwa Kauli ya Allah تعالى,

إِنكُرُوا إِذَا مِثْلَهُمْ

“...Hivyo mtakuwa nanyi mfano wao hao...” Kwa Kauli Yake,

وَمَا عَلَى الَّذِينَ يَتَّقُونَ مِنْ حِسَابِهِمْ مِنْ شَيْءٍ وَلَكِنْ ذُكِّرُوا لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ﴿٦٩﴾

“Wala wamchao Mungu hawana jukumu lolote kwao, lakini ni kukumbusha, asaa wapate kujiepusha.” (6:69)

Kauli ya Allah تعالى,

إِنَّ اللَّهَ جَامِعُ الْمُنَافِقِينَ وَالْكَافِرِينَ فِي جَهَنَّمَ جَمِيعًا ﴿٦٩﴾

“Hakika Mwenyezi Mungu Atawakusanya wanafiki na makafiri wote pamoja katika Jahannamu.”

Maana yake: Kama vile wanafiki walivyoshiriki katika kufuru ya wasioamini, Allah تعالى Atawaunganisha pamoja kuishi Motoni milele, wakiishi katika mateso, adhabu, wamefungwa minyororo, wamedhikishwa na wakinywa maji yanayochemka.

الَّذِينَ يَتَرْتُصُونَ بِكُمْ فَإِنْ كَانَ لَكُمْ مِنَ اللَّهِ قَالُوا أَلَمْ
 نَكُنْ مَعَكُمْ وَإِنْ كَانَ لِلْكَافِرِينَ نَصِيبٌ قَالُوا أَلَمْ نَسْتَحْوِذْ
 عَلَيْكُمْ وَنَمْنَعَكُمْ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ۚ فَاللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ
 الْقِيَامَةِ ۗ وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا ﴿١٤١﴾
 إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيعُهُمْ وَإِذَا قَامُوا إِلَى
 الصَّلَاةِ قَامُوا كُسَالَى يُرَاءُونَ النَّاسَ وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّهَ إِلَّا
 قَلِيلًا ﴿١٤٢﴾ مُذَبَّذِينَ بَيْنَ ذَلِكَ لَا إِلَى هَتُولَاءٍ وَلَا إِلَى
 هَتُولَاءٍ ۚ وَمَنْ يَضِلْ اللَّهُ فَمَا لَهُ سَبِيلًا ﴿١٤٣﴾ يَا أَيُّهَا
 الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ
 الْمُؤْمِنِينَ ۚ أَتُرِيدُونَ أَنْ تَجْعَلُوا لِلَّهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا مُبِينًا
 ﴿١٤٤﴾ إِنَّ الْمُنَافِقِينَ فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ وَلَنْ تَجِدَ
 لَهُمْ نَصِيرًا ﴿١٤٥﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا وَأَصْلَحُوا وَاعْتَصَمُوا
 بِاللَّهِ وَأَخْلَصُوا دِينَهُمْ لِلَّهِ فَأُولَٰئِكَ مَعَ الْمُؤْمِنِينَ ۗ
 وَسَوْفَ يُؤْتِي اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٤٦﴾ مَا يَفْعَلُ
 اللَّهُ بِعَدَابِكُمْ إِنْ شَكَرْتُمْ وَءَامَنْتُمْ ۚ وَكَانَ اللَّهُ شَاكِرًا
 عَلِيمًا ﴿١٤٧﴾

الَّذِينَ يَتَرْتُصُونَ بِكُمْ فَإِنْ كَانَ لَكُمْ مِنَ اللَّهِ قَالُوا أَلَمْ
 نَكُنْ مَعَكُمْ وَإِنْ كَانَ لِلْكَافِرِينَ نَصِيبٌ قَالُوا أَلَمْ
 نَسْتَحْوِذْ عَلَيْكُمْ وَنَمْنَعَكُمْ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ۚ فَاللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ
 الْقِيَامَةِ ۗ وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ
 عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا ﴿١٤١﴾

141. "Wale ambao wanaku-
 ngojeeni, mkipata ushindi
 unaotoka kwa Mwenyezi
 Mungu wao husema: Si
 tulikuwa pamoja nanyi vile?
 Na ikiwa ni sehemu ya
 makafiri kushinda wao
 huwaambia: Hatukuwa ni
 waweza wa kukushindeni,
 nasi tukakuingeni na hawa
 Waumini? Basi Mwenyezi
 Mungu Atahukumu baina
 yenu Siku ya Kiyama, wala
 Mwenyezi Mungu Hata-
 wapa makafiri njia ya
 kuwashinda Waumini."

Wanafiki Wanasubiri Kuona Yatayowapata Waislamu

Allah تعالى Ameeleza kuwa wanafiki wanaangalia na kusubiri madhara yatakayo wafika waumini, na wakiona kuanguka kwa dola yao na kudhihiri kwa ukafiri,

فَإِنْ كَانَ لَكُمْ فَتْحٌ مِّنَ اللَّهِ

“...mkipata ushindi unaotoka kwa Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Ushindi na Ngawira,

قَالُوا أَلَمْ نَكُنْ مَعَكُمْ

“...husema: Si tulikuwa pamoja nanyi vile?...”

Walijaribu kujikurubisha kwa waumini na kauli hii, hata hivyo,

وَإِنْ كَانَ لِلْكَافِرِينَ نَصِيبٌ

“Na ikiwa ni sehemu ya makafiri kushinda.”

Kwa wakati mwingine kupata ushindi juu ya waumini baadhi ya wakati, kama ilivyojiri katika Uhud. Kwa hakika Mitume wanapewa mitihani, lakini ushindi wa mwisho ni wao,

قَالُوا أَلَمْ نَسْتَحِذْ عَلَيْكُمْ وَنَمْنَعَكُمْ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ

“...huwaambia: Hatukuwa ni waweza wa kukushindeni, nasi tukakuingeni na hawa Waumini...”

Maana yake: Hatukuwasaidia kwa siri na tukajitahidi kuwachanganya waumini na tukadhoofisha azma zao, mpaka mkawashinda? Kauli hii ya wanafiki ni juhudi za kuimarisha mahusiano na makafiri, kwa sababu wanajifanya marafiki wa pande zote ili wawe salama na madhara yao, kutokana na imani yao dhaifu na kutokuwa na uhakika.

Allah تعالى Amesema,

فَاللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

“Basi Mwenyezi Mungu Atahukumu baina yenu Siku ya Kiyama..”

Maana yake: Kwa jinsi Anavyowafahamu, Enyi wanafiki, kwa hiyo msidanganyike kwa kuwa chini ya kivuli cha Ulinzi wa Sharia ya Kiislamu hapa

duniani, ambayo inatokana na Hikima ya Allah تعالى. Kwa hakika Siku ya Kiyama, kujifanya kwenu hakutawanufaisha, kwa sababu katika siku hiyo, siri za nyoyo zitawekwa wazi na yaliyomo ndani ya mioyo yatakusanywa.

Allah تعالى Amesema,

وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا ﴿١٤١﴾

“...wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini.”

Abdur-Razaq kutoka kwa Yas'igh Al-Kindi amesema kuwa, 'Alikuja mtu kwa Ali bin Abi Talib رضي الله عنه kisha akauliza, "Vipi kuhusu aya hii,

وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا ﴿١٤١﴾

“...wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini.”

Ali bin Abi Talib رضي الله عنه akasema, 'Sogea kwangu, kisha akasema,

فَاللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا ﴿١٤١﴾

“Basi Mwenyezi Mungu Atahukumu baina yenu Siku ya Kiyama, wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini.”¹

Vivyo hivyo amepokea Ibn Jarir رحمه الله تعالى kutoka kwa 'Atwa Al-Kharasani kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.

وَلَنْ يَجْعَلَ اللَّهُ لِلْكَافِرِينَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا ﴿١٤١﴾

“...wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini.”

Akasema, “hayo yatatokea Siku ya Kiyama.”² As- Suddi alimnukuu kuwa Abu Malik Al-Ashjai alisema kuwa itatokea siku ya Kiyama.³ As-Suddi alisema kuwa “**njia**” maana yake, ushahidi.⁴ Inawezekana kuwa maana ya, ‘...**wala Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia ya kuwashinda Waumini.**’ Kwa maana ya

¹AbduRazaq 1:175.

²At - Tabari 9:328.

³At - Tabari 9:328.

duniani kwa kuwatawala moja kwa moja, japokuwa baadhi ya wakati wanawashinda baadhi ya Waislamu. Hata hivyo, Ushindi wa mwisho utakuwa kwa waumini hapa duniani na kesho Akhera.

Allah تعالى Amesema,

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

“Hakika bila ya shaka Sisi tunawanusuru Mitume wetu na walio amini katika uhai wa duniani.” (40:51)

Hili ni jibu kwa wanafiki kwa kile wanachokitamani na kukisubiri ili waone dola ya Kiislamu inaanguka na hii inakanusha utashi wa wanafiki kwa maangamivu ya makafiri, wakizihofia nafsi zao wenyewe endapo ni washindi.

Allah تعالى Amesema,

فَتَرَى الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ يُسْرِعُونَ فِيهِمْ

“...Utawaona wale wenye maradhi nyoyoni mwao wanakimbilia kwao...” (5:52) Mpaka,

﴿تَدْبِيرٌ﴾

“...wenye kujuta...”

إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِيعُهُمْ وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كُسَالًا يُرَاءُونَ

النَّاسَ وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّهَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٢﴾ مُدْبِدِينَ بَيْنَ ذَلِكَ لَا إِلَى هَتُّولَاءٍ وَلَا إِلَى

هَتُّولَاءٍ ۗ وَمَنْ يَضِلَّ اللَّهُ فَلَنْ نَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿٥٣﴾

142. Hakika wanafiki wanamkhadaa Mwenyezi Mungu, na hali ni Yeye Ndiye Mwenye Kuwakhadaa wao. Na wanapoinuka kusali huinuka kwa uvivu, wanajionesha kwa watu tu, wala hawamdhukuru Mwenyezi Mungu ila kidogo tu.

143. Wanakwenda na kurudi kati ya ukafiri na imani. Huku hawako na huko hawako. Na ambaye Mwenyezi Mungu Amemuwacha kupotea, kabisa hutompatia njia.

Wanafiki Wanajaribu Kumdanganya Allah تعالى na Wakijiunga Baina ya Waumini na Makafiri.

Mwanzoni mwa *Suratu Al-Baqarah* (2), tulitaja Kauli ya Allah تعالى،

تُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا

“Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu na wale walio amini.” (2:9)

Hapa, Allah تعالى Ameeleza,

إِنَّ الْمُنَافِقِينَ يُخَدِّعُونَ اللَّهَ وَهُوَ خَدِّعُهُمْ

“Hakika wanafiki wanamkhadaa Mwenyezi Mungu, na hali ni Yeye Ndiye Mwenye Kuwakhadaa wao.”

Hapana shaka yeyote kuwa Allah تعالى Hawezi kudanganywa, kwani Anajua kwa yakini siri na yaliyojificha katika nyoyo.

Hata hivyo, wanafiki kutokana na ujinga wao, uchache wa elimu na udhaifu wa akili zao, wanadhani kuwa kwa vile walifanikiwa kuwadanganya watu, wakitumia sharia ya Kiislamu kama kinga kwao, watapata daraja stahiki kwa Allah تعالى siku ya Kiyama na kumdanganya pia.

Allah تعالى Anaeleza kuwa Siku hiyo, wanafiki wataapa Kwake kuwa walikuwa katika njia sahihi; wakidhani kuwa kauli kama hiyo itawanufaisha kwa Allah تعالى. Mathalan, Allah تعالى Amesema,

يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ اللَّهُ جَمِيعًا فَيَحْلِفُونَ لَهُ كَمَا يَحْلِفُونَ لَكَرُ

“Siku Atakayowafufua Mwenyezi Mungu wote, wamuwapie kama wanavyokuwapieni nyinyi.” (58:18)

Kauli ya Allah تعالى،

وَهُوَ خَدِّعُهُمْ

“Na hali ni Yeye Ndiye Mwenye Kuwakhadaa wao.”

Maana yake: Atawapoteza zaidi katika udhalimu na upotofu. Aidha Atawazuia kufikia ukweli hapa duniani na siku ya ufufuo. Kama Alivyosema Allah تعالى،

يَوْمَ يَقُولُ الْمُنْفِقُونَ وَالْمُنْفِقَتُ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا انظُرُونَا نَقْتَسِبْ مِن نُّورِكُمْ

“Siku wanafiki wanaume na wanaafiki wanawake watapo waambia walio amini: Tungojeni ili tupate mwangaza katika nuru yenu.” (57:13). Mpaka,

وَبَيْسَ الْمَصِيرُ

“Na ni marejeo maovu yalioje!” (57:15)

Hadithi imeeleza,

«مَنْ سَمِعَ سَمِعَ اللهُ بِهِ، وَمَنْ رَأَى رَأَى اللهُ بِهِ»

“Mwenye kutaka kusikilizwa, Allah تعالى Atamsikilizisha, na anayetaka kuonekana, Allah تعالى Atamfanya aonekane.”¹

Kauli ya Allah تعالى,

وَإِذَا قَامُوا إِلَى الصَّلَاةِ قَامُوا كُسَالٍ

“Na wanapoinuka kusali huinuka kwa unyong’onyo.”

Hii ni sifa bainifu ya wanafiki wanapokuwa katika ibada ya Sala ambayo imetukuka. Wanaposimama katika Sala, wanasimama kivivu kwa sababu hawakusudii kuisimamisha wala hawaiamini; wanaidhalilisha, wala hawajui maana yake, hii ndio sifa kuu yao na ni wasifu wao wa nje. Ama juu ya nyoyo zao, Allah تعالى Amesema,

يُرَاءُونَ النَّاسَ

“Wanajionesha kwa watu tu.”

Maana yake: Hawana ikhlas wala hawana muamala mzuri na Mwenyezi Mungu, ila wanawaonesha watu kificho chao na kujifanya kwao. Hawana unyenyekevu wanapomuabudu Allah تعالى.

Bali, wanajionesha kwa watu ili wawe karibu nao. Mara nyingi huwa hawahudhuria Swala ambazo wanaweza kujificha, kama vile Sala ya Isha na Sala ya Subhi. Hizi ni Sala hujiri wakati wa kiza. Katika Sahihi Mbili, imenukuliwa kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ At - Tabari 9:328.

«أَنْقُلَ الصَّلَاةَ عَلَى الْمُنَافِقِينَ صَلَاةَ الْعِشَاءِ وَصَلَاةَ الْفَجْرِ، وَلَوْ يَعْلَمُونَ مَا فِيهِمَا
لَأَتَوْهُمَا وَلَوْ حَبْوًا، وَلَقَدْ هَمَمْتُ أَنْ أَمَرَ بِالصَّلَاةِ فَتَقَامَ، ثُمَّ أَمَرَ رَجُلًا فَيُصَلِّيَ
بِالنَّاسِ، ثُمَّ أَنْطَلِقَ مَعِيَ بِرِجَالٍ مَعَهُمْ حُزْمٌ مِنْ حَطَبٍ، إِلَى قَوْمٍ لَا يَشْهَدُونَ
الصَّلَاةَ، فَأَحْرَقَ عَلَيْهِمْ بُيُوتَهُمْ بِالنَّارِ».

“Sala nzito zaidi kwa wanafiki ni Sala ya Isha na al-Fajri. Iwapo wangelijua thawabu zake wangekwenda kuzisali hata kwa kutambaa. Nilikaribia kumuamuru mtu atoe Adhana ya Sala, kisha nimuamuru mmoja awe Imam, kisha niwaamuru baadhi ya watu wakusanye kuni na niende nao kuzichoma nyumba za watu ambao hawakuhudhuria Sala ya jamaa.”¹

Katika Riwaya Nyingine,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَوْ عَلِمَ أَحَدُهُمْ أَنَّهُ يَجِدُ عَرَفًا سَيِّئًا أَوْ مِرْمَانِينَ حَسَنَيْنِ،
لَشَهِدَ الصَّلَاةَ، وَلَوْ لَا مَا فِي الْبُيُوتِ مِنَ النَّسَاءِ وَالذَّرِّيَّةِ لَحَرَّقْتُ عَلَيْهِمْ بُيُوتَهُمْ
بِالنَّارِ»

“Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake, iwapo mmoja wenu angelijua kuwa angepata mfupa wenye nyama nzuri au vipande vidogo vya nyama katikati ya mbavu mbili, angelikwenda kusali, na kama nyumba zisingelikuwa na wanawake na watoto, ningelizichoma nyumba zao juu yao.”²

Ama Kauli Yake Allah تعالى،

وَلَا يَذْكُرُونَ اللَّهَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٣١﴾

“...Wala hawamdhukuru Mwenyezi Mungu ila kidogo tu.”

Maana yake: Katika Sala zao hawanyenyeki wala hawajui wanayoyasema, bali wao katika Sala zao husahau na wanazifanyia mchezo, na wanakwepa mambo ya kheri. Imam Malik رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa 'Alaa bin Abdur-Rahman kutoka kwa Anas bin Malik رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema,

¹ Fat'hul Bari 2:53 na Muslim 1:451.

² Fat'hul Bari 2:248 na Muslim 1:325.

«تِلْكَ صَلَاةُ الْمُتَافِي، تِلْكَ صَلَاةُ الْمُتَافِي، تِلْكَ صَلَاةُ الْمُتَافِي، يَجْلِسُ يَرْقُبُ
النُّمُسَ، حَتَّى إِذَا كَانَتْ بَيْنَ قَرْنَيْ الشَّيْطَانِ، قَامَ فَتَقَرَّ أَرْبَعًا، لَا يَذْكُرُ اللَّهَ فِيهَا إِلَّا
قَلِيلًا»

“Hiyo ndio Swala ya Mnafiki, hiyo ndio Swala ya Mnafiki, hiyo ndio Swala ya Mnafiki, husubiri jua hadi linapofika katika pembe mbili za shetani, ndipo anaposimama na kudonoa mara nne (Asri), hawamdhukuru Mwenyezi Mungu isipokuwa kidogo tu.”¹

Na vivyo hivyo amepokea Muslim, At-Tirmidhi, An-Nisai. At - Tirmidhi amesema kuwa Hadithi hii ni Hassan Sahihi.² Kauli ya Allah تعالى،

مُذْتَبِّينَ بَيْنَ ذَلِكَ لَا إِلَى هَتُولَاءِ وَلَا إِلَى هَتُولَاءِ^ع

“Wanayumbayumba baina ya huku na huko. Huku hawako na huko hawako.”

Maana yake: Ni kuwa wanafiki wanayumba kati ya Imani na ukafiri. Hivyo hawapo na waumini kwa ndani au kwa nje, wala na makafiri kwa ndani au kwa nje; bali dhahiri huonekana wapo pamoja na Waislamu, lakini kwa ndani ya nyoyo zao wapo pamoja na makafiri. Baadhi yao huwa na mashaka, mara wapo upande wa waislamu na wakati mwingine upande wa makafiri.

كُلَّمَا أَضَاءَ لَهُمْ مَشَوْا فِيهِ وَإِذَا أَظْلَمَ عَلَيْهِمْ قَامُوا

“Kila ukiwatolea mwangaza huenda, na unapowafanyia giza husimama.” (2:20) Mujahid anasema kuhusu aya,

مُذْتَبِّينَ بَيْنَ ذَلِكَ لَا إِلَى هَتُولَاءِ

“Wanayumbayumba baina ya huku na huko. Huku hawako.”

Maana yake: Hawapo pamoja na maswahaba wa Mtume ﷺ

لَا إِلَى هَتُولَاءِ

“Na huko hawako.” Kwa Mayahudi.

¹ At - Tabari 9:272.

² At - Tabari 9:285-287.

Ibn Jarir alinukuu kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَثَلُ الْمُنَافِقِ كَمَثَلِ الشَّاةِ الْعَاثِرَةِ بَيْنَ الْغَنَمَيْنِ، تَعْبُرُ إِلَى هَذِهِ مَرَّةً، وَإِلَى هَذِهِ مَرَّةً،
وَلَا تَذَرِي أُتَيْتَهُمَا تَتَّبِعُ»

*"Mfano wa Wanafiki ni mfano wa kondoo anayejitenga baina ya makundi mawili, kuna wakati anakwenda kwenye kundi moja, na baadaye jingine, amechanganyikiwa hajui afuate lipi."*¹

Muslim pekee ndiye aliyenukuu.² Kwa sababu hii baadaye Allah تعالى Amesema,

وَمَنْ يُضَلِلِ اللَّهَ فَلَنْ يَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿٨٨﴾

"Na Aliyemhukumu Mwenyezi Mungu kuwa amekwishapotea wewe hutampatia njia..." (4:88)

Maana yake: Atakayemuondoa katika njia ya uongofu,

فَلَنْ يَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿١٧﴾

"...basi hutampatia mlinzi wala mwongozi..." (18:17) Kwani,

مَنْ يُضَلِلِ اللَّهَ فَلَا هَادِيَ لَهُ

"Aliyemuwacha Mwenyezi Mungu kupotea hana wa kumuongoa." (7:186)

Hivyo wanafiki Allah تعالى Anawapotosha, kwenye njia ya usalama hawatopata muongozaji wa kuwaongoza, wala wa kuwaokoa. Hapana anayeweza kuzuia Uamuzi wa Allah تعالى, na Haulizwi kuhusu Ayafanyayo, ambapo wote wataulizwa.

يَتَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَتَّخِذُوا الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ ؕ أُرِيدُونَ أَنْ تَجْعَلُوا لِلَّهِ
عَلَيْكُمْ سُلْطَنًا مُبِينًا ﴿١٧﴾ إِنَّ الْتَنَفِقِينَ فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ وَلَنْ يَجِدَ لَهُمْ
نَصِيرًا ﴿١٨﴾ إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا وَأَصْلَحُوا وَاعْتَصَمُوا بِاللَّهِ وَأَخْلَصُوا دِينَهُمْ لِلَّهِ فَأُولَٰئِكَ
مَعَ الْمُؤْمِنِينَ ؕ وَسَوْفَ يُؤْتِي اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٩﴾ مَا يَفْعَلُ اللَّهُ بِعَدَابِكُمْ
إِنْ شَكَرْتُمْ وَءَامَنْتُمْ ؕ وَكَانَ اللَّهُ شَاكِرًا عَلِيمًا ﴿٢٠﴾

¹Al-Muwatwa 1:220.

²Muslim 1:4324, Tuhfatul Ahwadhi 1:497 na An-Nasai 1:254.

144. Enyi mlioamini! Msiwafanye makafiri kuwa ndio marafiki badala ya Waumini. Je, mnataka Mwenyezi Mungu Awe na hoja iliyo wazi juu yenu?

145. Hakika wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa Motoni, wala hutompata yeyote wa kuwanusuru.

146. Isipokuwa wale waliotubu, na wakatengeneza na wakashikamana na Mwenyezi Mungu, na wakamtakasia Dini yao Mwenyezi Mungu. Basi hao ni pamoja na Waumini. Na Mwenyezi Mungu Atakuja wapa Waumini ujira mkubwa.

147. Mwenyezi Mungu Hakuadhibuni mkimshukuru na mkamuamini. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kupokea shukrani na Ndiye Mwenye Kujua.

Kuharamishwa kwa Wilayah na Makafiri

Allah تعالى Amewaharamisha waja wake kuwafanya makafiri marafiki badala ya waumini. Hii ni pamoja na kuwa marafiki na washirika ambao ni makafiri, akiwashauri, na kuwa wandani wao na kutoa siri za waumini. Katika aya nyingine, Allah تعالى Amesema;

لَا يَتَّخِذِ الْمُؤْمِنُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِ الْمُؤْمِنِينَ وَمَنْ يَفْعَلْ ذَلِكَ فَلَيْسَ مِنَ اللَّهِ فِي شَيْءٍ إِلَّا أَنْ تَتَّقُوا مِنْهُمْ تُقَنَّةً وَيُحَذِّرْكُمْ اللَّهُ نَفْسَهُ ۗ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ ﴿٢٨﴾

“Waumini wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi wao badala ya Waumini. Na anayefanya hivyo, basi hatakuwa chochote mbele ya Mwenyezi Mungu. Ila ikiwa kwa ajili ya kujilinda na shari zao. Na Mwenyezi Mungu Anakuhadharisheni naye. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.” (3:28)

Maana yake: Alikuonyeni kuhusu Adhabu Yake ikiwa mtaangukia katika yale Aliyoyakataza. Ndio sababu Allah تعالى Akasema hapa,

أُتْرِدُونَ أَنْ نَجْعَلُوا لِلَّهِ عَلَيْكُمْ سُلْطَانًا مُبِينًا ﴿٢٨﴾

“Je, mnataka Mwenyezi Mungu Awe na hoja iliyo wazi juu yenu?”

Maana yake: Ushahidi dhidi yenu unaowahakikishia kupata Adhabu Yake. Ibn Hatim رضي الله عنهما رحمة الله تعالى alisimulia kuwa Ibn Abbas

سُلْطَنَا مُبِينًا ﴿١٤٦﴾

“Hoja iliyo wazi.”

“Neno *Sultani* ndani ya Qur’an maana yake ushahidi.” Kuna Isnadi sahihi kwa kauli hii, ambayo pia kauli ya Mujahid, Ikrimah, Said bin Jubayr, Muhammad bin Ka’ab Al-Qurazi, Adh-Dhahhak, As-Suddi na An-Nadhira bin Arabi.

Wanafiki na Marafiki wa Makafiri Wako katika Moto wa Chini, Isipokuwa Wakitubia.

Kisha Allah تعالى Amesema kuwa,

إِنَّ الْمُنْفِقِينَ فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ وَلَنْ يَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا ﴿١٤٧﴾

“Hakika wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa Motoni, wala hutompata yeyote wa kuwanusuru.”

Siku ya Kufufuliwa kwa kubobea kwao katika *Kufr*. Al-Wahbi (Ali bin Abi Talha) alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ

“...katika tabaka ya chini kabisa Motoni..”

Maana yake: Chini ya Moto.¹ Baadhi ya wanazuoni walisema kuwa moto una kina cha chini kama ilivyo pepo ina madaraja ya juu.

Ibn Abi Hatim رضي الله عنه رحمة الله تعالى alinukuu kuwa Abdullah bin Mas’ud رضي الله عنه alisema kuwa,

إِنَّ الْمُنْفِقِينَ فِي الدَّرَكِ الْأَسْفَلِ مِنَ النَّارِ

“Hakika wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa Motoni..”

¹ Muslim 4:2146.

Ndani ya majeneza ya moto yaliyowazingira, kwani yamefungwa na kutiwa lakiri.¹ Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa, Ibn Mas'ud رضي الله عنه alipoulizwa kuhusu wanafiki, alisema, "Watatiwa ndani ya majeneza yaliyotengezwa kwa moto, na yatafungwa na kutiwa katika kina cha chini cha Motoni."

وَلَنْ نَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا ﴿١٤٦﴾

"...wala hutompata yeyote wa kuwanusuru."

Maana yake: Wa kuwaokoa kutoka katika mahangaiko na adhabu iumizayo. Kisha Allah تعالى Ameeleza kuwa yeyote miongoni mwa wanafiki watakaotubia hapa duniani, Allah تعالى Atakubali toba yake na masikitiko yake. Endapo toba yake ilikuwa ya kweli na kisha ikafuatia kwa kutenda amali njema, wakati akimtegemea Mola wake katika mambo yake yote. Allah تعالى Amesema,

إِلَّا الَّذِينَ تَابُوا وَأَصْلَحُوا وَاعْتَصَمُوا بِاللَّهِ وَأَخْلَصُوا دِينَهُمْ لِلَّهِ

"...Isipokuwa wale waliotubu, na wakatengeneza na wakashikamana na Mwenyezi Mungu, na wakamtakasia Dini yao Mwenyezi Mungu..."

Wakibadilisha kujionesha kwa uaminifu, ili amali zao njema ziwanufaishe, hata kama ni chembe ndogo.

فَأُولَٰئِكَ مَعَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٤٧﴾

"Basi hao ni pamoja na Waumini." Katika siku ya Ufufuo.

وَسَوْفَ يُؤْتِي اللَّهُ الْمُؤْمِنِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٤٨﴾

"Na Mwenyezi Mungu Atakuja wapa Waumini ujira mkubwa."

Kisha Allah تعالى Anaeleza kuwa Yeye ni Tajiri mno katika kumuhitajia yeyote na kuwa Huwaadhibu waja kwa sababu ya dhambi zao. Kauli ya Allah تعالى,

¹ At - Tabari 9:339.

مَا يَفْعَلُ اللَّهُ بِعَذَابِكُمْ إِنْ شَكَرْتُمْ وَءَامَنْتُمْ

“Mwenyezi Mungu Hakuadhibuni mkimshukuru na mkamuamini...”

Kwa kusahihisha matendo yenu na kumuamini Allah تعالى na Mjumbe wake ﷻ.

وَكَانَ اللَّهُ شَاكِرًا عَلِيمًا

“Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kupokea shukrani na Ndiye Mwenye Kujua.”

Allah تعالى Anawaridhia wale wanaomridhia Yeye, na Anajua wale ambao nyoyo zao zinamuamini Yeye, na Atawalipa malipo maridhawa.

* * *

* لَا تُحِبُّ اللَّهُ الْجَهْرَ بِالسُّوءِ مِنَ الْقَوْلِ إِلَّا مَنْ ظَلَمَ ۗ
 وَكَانَ اللَّهُ سَمِيعًا عَلِيمًا ﴿١٤٨﴾ إِنْ تُبَدُّوا خَيْرًا أَوْ تُخَفُّوهُ أَوْ
 تَعْفُوا عَنْ سُوءِ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفْوًا قَدِيرًا ﴿١٤٩﴾ إِنْ
 الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ
 اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُوا نُؤْمِنُ بِبَعْضِ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ
 وَيُرِيدُونَ أَنْ يَتَّخِذُوا بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١٥٠﴾ أُولَئِكَ هُمُ
 الْكَافِرُونَ حَقًّا ۗ وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُهِينًا ﴿١٥١﴾
 وَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَلَمْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ أَحَدٍ مِنْهُمْ
 أُولَئِكَ سَوْفَ يُؤْتِيهِمْ أَجْرُهُمْ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا
 ﴿١٥٢﴾ يَسْأَلُكَ أَهْلُ الْكِتَابِ أَنْ تُنزِلَ عَلَيْهِمْ كِتَابًا مِنَ
 السَّمَاءِ ۗ فَقَدْ سَأَلُوا مُوسَىٰ أَكْبَرَ مِنْ ذَلِكَ فَقَالُوا أَرِنَا اللَّهَ
 جَهْرَةً فَأَخَذَتْهُمُ الصَّاعِقَةُ بِظُلْمِهِمْ ۗ ثُمَّ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ
 مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَاتُ فَعَفَوْنَا عَنْ ذَلِكَ ۗ وَءَاتَيْنَا
 مُوسَىٰ سُلْطَانًا مُبِينًا ﴿١٥٣﴾ وَرَفَعْنَا فَوْقَهُمُ الطُّورَ بِمِثْقِهِمْ
 وَقُلْنَا لَهُمْ ادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا وَقُلْنَا لَهُمْ لَا تَعْدُوا فِي
 السَّبْتِ وَأَخَذْنَا مِنْهُمْ مِيثَاقًا غَلِيظًا ﴿١٥٤﴾

* لَا تُحِبُّ اللَّهُ الْجَهْرَ بِالسُّوءِ مِنَ الْقَوْلِ إِلَّا مَنْ ظَلَمَ ۗ
 وَكَانَ اللَّهُ سَمِيعًا عَلِيمًا ﴿١٤٨﴾ إِنْ تُبَدُّوا خَيْرًا أَوْ
 تُخَفُّوهُ أَوْ تَعْفُوا عَنْ سُوءِ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفْوًا قَدِيرًا ﴿١٤٩﴾

148. Mwenyezi Mungu Hapendi uovu kudhihirishwa kwa maneno ila kwa mwenye kudhulumiwa. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwenye Kusikia na Mwenye Kujua.

149. Mkiidhihirisha wema au mkiuficha, au mkiyasamehe maovu, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira na Muweza.

Rukhsa ya Kutangaza Uovu kwa Aliyedhulumiwa

Ali Bin Abi Talha alisema kuwa رضي الله عنهما Hivyo Allah Amesema, aliitolea maelezo aya hii,

* لَا تُحِبُّ اللَّهُ الْجَهْرَ بِالسُّوءِ مِنَ الْقَوْلِ

“Mwenyezi Mungu Hapendi uovu uenezwe kwa maneno.”

Allah تعالى Hapendi mtu yeyote kumuomba Yeye dhidi ya mtu mwingine, isipokuwa mtu huyo alikosewa. Katika hali hii, Allah تعالى Anamruhusu mtu kumuomba Yeye dhidi ya yeyote aliyemkosea. Hivyo Allah تعالى Amesema,

إِلَّا مَنْ ظَلِمَ

“...ila kwa mwenye kudhulumiwa...”

Hata hivyo ni bora kusubiri.¹ Al-Hasan Al-Basri رحمه الله تعالى alisema, “Mmoja wenu akimuomba Allah تعالى (kwa laana) dhidi ya yeyote aliyemfanyia ubaya. Basi, aombe dua, ‘Ewe Allah! Nisaidie dhidi yake na mpoke haki zangu.”² Katika riwaya nyingine, Al-Hassan alisema, “Allah تعالى Ameruhusu mtu kumuomba Yeye dhidi ya yeyote aliyemkosea bila kuchupa mipaka.” Abdul-Karim bin Malik Al-Jazari alizungumza kuhusu aya hii, Mtu anapotukana, unaweza kumtukana kwa kulipizia. Lakini anapokuzulia uongo, huwezi nawe kumzulia uongo.

Kwa dalili ya Kauli Yake Allah تعالى,

وَلَمَنْ أَنْتَصَرَ بَعْدَ ظُلْمِهِ فَأُولَئِكَ مَا عَلَيْهِمْ مِنْ سَبِيلٍ ﴿٤١﴾

“Na wanaojitetea baada ya kudhulumiwa, hao hapana njia ya kuwalaumu.” (42:41)

Kauli ya Allah تعالى,

«الْمُسْتَبَانَ مَا قَالَا، فَعَلَى الْبَادِي مِنْهُمَا مَا لَمْ يَغْتَدِ الْمُظْلَمُونَ»

“Maneno yoyote yatamkwayo na wale wenye kulaaniana, basi Yule aliyeanza anaubeba mzigo huo, isipokuwa yule aliyedhulumiwa akivuka mipaka.”

Allah تعالى Amesema,

إِنْ تَبَدُّوا خَيْرًا أَوْ خَفَوْهُ أَوْ تَعَفُّوا عَنْ سُوءِ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُوًّا قَدِيرًا ﴿٤٢﴾

“Mkidhihirisha wema au mkiuficha, au mkiyasamehe maovu, hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira na Muweza.”

Ina maana: Nyie binadamu, mkikiri kufanyiwa wema, au kuuficha na kuwasamehe waliokukoseeni, basi hili litawapeleka karibu na Allah تعالى na kuwaongezea malipo kutoka Kwake. Miongoni mwa sifa za Allah تعالى ni kuwa

¹ At - Tabari 9:344.

² At - Tabari 9:344.

Husamehe waja Wake, japo kuwa Ana Uwezo wa Kuwaadhibu. Hivyo Allah تعالى Amesema,

فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا قَدِيرًا ﴿١٥٠﴾

“...hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira na Muweza.”

Ilezwe kuwa baadhi ya malaika wanaobeba Kiti cha enzi, wanamtukuza kwa kusema, “Shukrani zote ni Stahiki Yako kwa Ustahamilivu Wako japokuwa Unafahamu (maovu yote yaliyofanywa).” Baadhi yao wanaomba, “Shukrani zote Unastahiki Wewe kwa Msamaha Wako japokuwa Una Uweza (wa Kuadhibu).” Hadithi sahihi inasema,

«مَا نَقَصَ مَالٌ مِنْ صَدَقَةٍ، وَلَا زَادَ اللَّهُ عَبْدًا بِغَفْرِ إِلَّا عِزًّا، وَمَنْ تَوَاصَعَ لِلَّهِ رَزَعَهُ اللَّهُ»

“Mali haipungui kwa kutoa Sadaka, na Allah تعالى Atamuongezea mja heshima na utukufu kwa ajili ya kusamehe. Na yule anayenyenyekea kwa ajili Yake (kwa kutojikuzi), Allah تعالى Atapandisha daraja lake.”¹

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُوا رَبُّنَا لَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ إِن كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا إِلاَّ فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿١٥١﴾
 إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُوا رَبُّنَا لَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ إِن كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا إِلاَّ فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿١٥٢﴾
 إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُوا رَبُّنَا لَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ إِن كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا إِلاَّ فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿١٥٣﴾
 إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيُرِيدُونَ أَنْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ اللَّهِ وَرُسُلِهِ وَيَقُولُوا رَبُّنَا لَأَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ إِن كُنَّا نَسْمَعُ أَوْ نَعْقِلُ مَا كُنَّا إِلاَّ فِتْنَةً لِلَّذِينَ كَفَرُوا لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿١٥٤﴾

150. Hakika wale wanaomkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake, na wanataka kufarikisha baina ya Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, kwa kusema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa. Na wanataka kushika njia iliyo kati kati ya haya,

151. Hao ndio makafiri kweli. Na Tumewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha.

152. Na waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, wala wasimfarikishe yeyote kati yao, hao Atawapa ujira wao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira, na Mwenye Kurehemu.

¹Muslim 4:2001.

Kuamini Baadhi ya Mitume na Kuwakana Wengine ni Ukafiri Halisi

Allah تعالی Anawatishia wale wanaomuamini Yeye na Mitume Yake, kama vile Mayahudi na Wakristo, ambao wanamtofautisha Allah تعالی na Mitume Yake katika Imani. Wanawaamini baadhi ya Mitume na kuwakataa wengine, wakifuata utashi na matamaniao yao na mila za mababu zao. Hawana ushahidi wowote kuhusu kuwatofautisha kwao. Kwa sababu hapana ushahidi huo. Bali wanafuata matamaniao yao na dhana zao.

Mayahudi, Allah تعالی Awalaani, wanaamini Mitume isipokuwa Isa عليه السلام na Muhammad ﷺ. Wakristo wanaamini Mitume lakini wanamkana Mtume wa mwisho, lakiri (muhuri), na aliyetukuka zaidi kuliko Mitume yote, Muhammad ﷺ. Zaidi ya hayo, Samirah (Samaritano) hawamuamini Mtume yeyote baada ya Yuwsha (Joshua), mrithi wa Musa bin Imran عليه السلام. Majuusi (Zoroastrians) inasemekana wanamuamini Mtume mmoja tu anayelitwa Zoroaster, japokuwa hawaamini sheria aliyokuja nayo, waliitupilia mbali na Allah تعالی ni Mjuzi zaidi. Kwa hiyo yeyote anayemkana Mtume mmoja wa Allah تعالی, atakuwa amewakana wote, kwa sababu binadamu wanatakiwa kuamini kila Mtume aliyetumwa na Allah تعالی kwa binadamu duniani. Na yeyote anayemkana Mtume mmoja kwa sababu ya inda, upendeleo na utashi binafsi, anadhihirisha kuwa imani yake kwa Mitume mingine ni batili, bali ni kitendo cha kufuata matakwa yake.

Ndiyo sababu Allah تعالی Amesema,

إِنَّ الَّذِينَ يَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ

“Hakika wale wanao mkataa Mwenyezi Mungu na Mitume wake..” (4:150)

Maana yake: Katika Imani. Kisha Allah تعالی Anawaelezea,

وَيَقُولُونَ نُوْمِنُ بِبَعْضٍ وَنَكْفُرُ بِبَعْضٍ وَيُرِيدُونَ أَنْ يَتَّخِذُوا بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١٥٠﴾

“...kwa kusema: Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa. Na wanataka kushika njia iliyo kati kati ya haya.”

Maana yake: Kutoamini kwao Mitume ambayo wanadai kuwa kuko wazi; kwa kuwa madai yao ya kuamini Mtume fulani si kweli, kwani kama kweli

walimuamini, basi wangeliswaamini na Mitume wengine, hususani iwapo Mtume mwingine alikuwa na ushahidi wenye nguvu na ukweli. Allah تعالى Amesema,

وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿١٤٨﴾

“Na Tumewaandalia makafiri adhabu ya kudhalilisha.”

Hii ni adhabu kwa kuwadharau Mitume ambao waliwakanusha, kwa kupuuza yale Mitume waliyowaletea kutoka kwa Allah تعالى, na kwa sababu wanajishughulisha na umiliki wa mali za dunia. Au mwenendo wao unaweza kuwa ni matokeo ya kufahamishwa yaliyoletwa na Mtume ﷺ baada ya kupambanuliwa na ukweli, kama vile wanazuoni wa Kiyahudi walivyofanya enzi za Muhammad ﷺ. Mayahudi walimuonea gere kwa sababu alipewa Utume Mkuu na Allah تعالى hivyo wakaamua kumkhalifu na kumkadhibisha na wakamfanyia kila aina ya uadui ikiwemo kutaka kumuua. Kwa ajili ya hayo Mwenyezi Mungu Aliwatumia maangamizi katika maisha ya dunia, ambayo itafuatwa na fadhaa kubwa siku ya Kiyama.

Kauli ya Allah تعالى

وَضَرَبْتَ عَلَيْهِمُ الدِّيلَةَ وَالْمَسْكَنَةَ وَبَاءَ وَبِغَضَبٍ مِّنَ اللَّهِ

“Na wakapigwa na unyonge, na umasikini, na wakastahili ghadhabu ya Mwenyezi Mungu.” (2:61)

Hapa duniani na kesho Akhera. Kauli ya Allah تعالى,

وَالَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ وَلَمْ يُفَرِّقُوا بَيْنَ أَحَدٍ مِّنْهُمْ

“Na wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake, wala wasimfarikishe yeyote kati yao.” (4:152)

Hii inahusu Umma wa Muhammad ﷺ wanaoamini kila kitabu alichoteremsha Allah تعالى na kwa kila Mtume aliyetumwa na Allah تعالى. Kama Alivyosema,

ءَامَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِن رَّبِّهِ ۖ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ ءَامَنَ بِاللَّهِ

“Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola Mlezi Wake, na Waumini vile vile. Wote wamemuamini Mwenyezi Mungu.” (2:152)

Kisha Allah تعالى Ameeru kuwa Amewaandalia zawadi nzuri isiyo na kifani na vitu vizuri,

أُولَئِكَ سَوْفَ يُؤْتِيهِمْ أَجْرُهُمْ

“...hao Atawapa ujira wao...” (4:152)

Kwa sababu ya kumuamini Allah تعالى na Mitume Yake,

وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا

“...Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Maghfira, na Mwenye Kurehemu.”

يَسْأَلُكَ أَهْلُ الْكِتَابِ أَنْ تُنزِلَ عَلَيْهِمْ كِتَابًا مِّنَ السَّمَاءِ فَقَدْ سَأَلُوا مُوسَىٰ أَكْبَرَ مِنْ ذَلِكَ فَقَالُوا أَرِنَا اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْهُمُ الصَّعِقَةُ بِظُلْمِهِمْ ثُمَّ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ مِن بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ الْبَيِّنَاتُ فَعَفَوْنَا عَنِ ذَلِكَ ۗ وَآتَيْنَا مُوسَىٰ سُلْطٰنًا مُّبِينًا ﴿١٥٣﴾ وَرَفَعْنَا فَوْقَهُمُ الطُّورَ بِمِيثَاقِهِمْ وَقُلْنَا لَهُمُ ادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا وَقُلْنَا لَهُمْ لَا تَعْدُوا فِي السَّبْتِ وَأَخَذْنَا مِنْهُمْ مِّيثَاقًا غَلِيظًا ﴿١٥٤﴾

153. Watu wa Kitabu wanakutaka uwateremshie kitabu kutoka mbinguni. Na kwa hakika walikwisha mtaka Musa makubwa kuliko hayo. Walisema: Tuoneshe Mwenyezi Mungu wazi wazi. Wakapigwa na radi kwa hiyo dhulma yao. Kisha wakamchukua ndama kumuabudu, baada ya kwisha wajia hoja zilizo wazi. Nasi Tukasamehe hayo, na Tukampa Musa nguvu zilizo dhahiri.

154. Na Tukanyanyua mlima juu yao kwa kufanya agano nao. Na Tukawaambia: Ingilieni mlangoni kwa unyenyekevu. Na Tukawaambia: Msiivunje Siku ya Sabato (Jumaa mosi). Na Tukachukua kwao ahadi iliyo madhubuti.

Ukorofi wa Mayahudi

Muhammad bin Ka'b Al-Suddi na Qadatah walisema kuwa Mayahudi walimtaka Mtume ﷺ kusababisha kitabu kushuka chini kutoka mbinguni, kama Taurat ilivyoshuka kwa Musa عليه السلام.¹ Ibn Jurayj alisema kuwa Mayahudi walimtaka Mtume ﷺ kusababisha vitabu kushuka chini vikiwa na majina ya miongoni mwao, vikithibitisha ukweli aliotumwa nao.¹

Mayahudi waliyataka haya kwa sababu ya ujui wao, kukataa ukweli na ukafiri wao. Makafiri wa kikuraishi pia waliuliza mambo yaliyo sawa na haya kutoka kwa Mtume ﷺ, kama ilivyotajwa katika Surat Al-Isra.

وَقَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَأْتِيَنَا

“Na walisema: Hatutakuamini mpaka ututimbulie chemchem katika ardhi hii.” (17:90)

Allah تعالى Amesema kwa ajili hiyo,

فَقَدْ سَأَلُوا مُوسَىٰ أَكْبَرَ مِنْ ذَلِكَ فَقَالُوا أَرِنَا اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْهُمُ الصَّيْغَةُ بِظُلْمِهِمْ

“...Na kwa hakika walikwisha mtaka Musa makubwa kuliko hayo. Walisema: Tuoneshe Mwenyezi Mungu wazi wazi. Wakapigwa na radi kwa hiyo dhulma yao...”

Upotofu, kuchupa mipaka, kuhama na kuasi: sehemu hii ilielezwa ndani ya Surat Al-Baqarah.

وَإِذْ قُلْتُمْ يَا مُوسَىٰ لَنْ نُؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ نَرَى اللَّهَ جَهْرَةً فَأَخَذَتْكُمُ الصَّيْغَةُ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ

ثُمَّ بَعَثْنَاكُم مِّنْ بَعْدِ مَوْتِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٥٦﴾

“Na mliposema: Ewe Musa! Hatutakuamini mpaka tumuwone Mwenyezi Mungu waziwazi. Ikakunyakueni radi nanyi mnaangalia. Kisha Tukakufufueni baada ya kufa kwenu, ili mpate kushukuru.” (2:55-56)

¹ At - Tabari 9:356 – 357.

Kauli ya Allah تعالى,

ثُمَّ أَخَذُوا الْعِجْلَ مِنْ بَعْدِ مَا جَاءَتْهُمْ آيَاتُنَا

“Kisha wakamchukua ndama kumuabudu, baada ya kwishawajia hoja zilizo wazi.”

Maana yake: Baada ya kushuhudia miujiza ya kushangaza na ushahidi usiopingika katika mikono ya Musa عليه السلام alipokuwa Misri. Pia walishuhudia khatima ya adui yao Firauni na askari wake, wote walipozama baharini. Hata hivyo baadaye kidogo, walipowapata watu wakiabudu masanamu, walimuambia Musa عليه السلام,

أَجْعَلْ لَنَا إِلَهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ

“...Hebu tufanyie na sisi miungu kama hawa walivyokuwa na miungu...” (7:138)

Allah تعالى Anaelezea kisa cha Mayahudi walioabudu Ng'ombe katika Surat Al-Araf (7) na Surat Twaha (20) baada ya Musa عليه السلام kwenda kukutana na Mola Wake. Musa عليه السلام aliporejea, Allah تعالى Alitoa Amri kwa Mayahudi ili wakubaliwe toba ilikuwa baadhi yao kuwaua wenza wao. Walikubali Amri hiyo na Allah تعالى Aliwafufua baadaye.

Allah تعالى Amesema hapa,

فَعَفَوْنَا عَنْ ذَلِكَ وَإِنَّا لَمُوسَىٰ سُلْطٰنًا مُّبِينًا ﴿١٣٨﴾

“...Nasi Tukasamehe hayo, na Tukampa Musa nguvu zilizo dhahiri.”

Kisha Kauli ya Allah تعالى,

وَرَفَعْنَا فَوْقَهُمُ الطُّورَ بِمِثْقَلِ ذَرَّةٍ

“Na Tukanyanyua mlima juu yao...”

Nayo ni pindi walipoacha kulazimiana na hukumu na sheria zilizo katika Taurati. Na likadhihiri alichokuja nacho Musa عليه السلام na Mwenyezi Mungu Kunyanyua jabali juu yao, kisha wakalazimiana na alichokuja nacho Musa عليه السلام na wakasujudu na wakawa wanaangalia juu ya vichwa vyao kwa khofu isije kuwaangukia kama Alivyosema Allah تعالى,

﴿ وَإِذْ نَتَقْنَا الْجَبَلَ فَوْقَهُمْ كَأَنَّهُمْ ظُلَّةٌ وَظَنُّوا أَنَّهُمْ وَقَعَ بِيْنَهُمْ خُذُوا مَا آتَيْنَاكُمْ ﴾

“Na pale Tulipounyanyua mlima juu yao ukawa kama kwamba ni kiwingu kilichowafunika, na wakadhani kuwa utawaangukia, (Tukawaambia): Kamateni kwa nguvu Tuli yokupeni...” (7:171)

Kisha Allah تعالى Akasema,

﴿ وَقُلْنَا لَهُمْ ادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا ﴾

“...Na Tukawaambia: Ingilieni mlangoni kwa unyenyekevu...”

Maana yake: Pia walivunja Amri hii kwa maneno na vitendo. Waliamriwa kuingia Bayt Al-Maqdis (Jerusalem) hali ya kuwa wameinama hali ya kuwa wakisema, “Hittah” maana yake, ‘Ewe Allah! Tufutie madhambi yetu ya kutekeleza Jihadi.’ Hii ilikuwa sababu ya kuhangaika kwao katika jangwa la Tich kwa miaka arubaini, bado waliingia Nyumba kwa kutambaa kwa nyuma nyuma hali ya kuwa huku wakisoma ‘Hiintah (punje ya shairi) mahali pa sharah (nywele).

﴿ وَقُلْنَا لَهُمْ لَا تَعْدُوا فِي السَّبْتِ ﴾

“Na Tukawaambia: Msiivunje Siku ya Sabato (Jumaa mosi).”

Muradi, Tuliwaamuru waiheshimu sabato na waheshimu kile Alichowaharamisha Allah تعالى siku ile.

﴿ وَأَخَذْنَا مِنْهُم مِّيثَاقًا عَلِيمًا ﴾

“Na Tukachukua kwao ahadi iliyo madhubuti.”

Aya hii inamaanisha, ahadi yenye nguvu. Waliasi wakachupa mipaka na walifanya yale ambayo Allah تعالى Aliyoyaharamisha kwa kufanya udanganyifu na ila (dosari), kama ilivyodhukuriwa katika Surat Al-Araf (7) katika Kauli Yake Allah تعالى,

﴿ وَسَأَلَهُمْ عَنِ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ حَاضِرَةَ الْبَحْرِ ﴾

“Na waulize habari za mji uliokuwa kando ya bahari...” (7:163)

* * *

فِيمَا نَقَضِهِمْ مِيثَقَهُمْ وَكُفِّرِهِمْ بِعَايَتِ اللَّهِ وَقَتْلِهِمُ الْأَنْبِيَاءَ
 بِغَيْرِ حَقٍّ وَقَوْلِهِمْ قُلُوبُنَا غُلْفٌ ۚ بَلْ طَبَعَ اللَّهُ عَلَيْهَا بِكُفْرِهِمْ
 فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٥٥﴾ وَكُفِّرِهِمْ وَقَوْلِهِمْ عَلَىٰ مَرْيَمَ
 بِهَتْنًا عَظِيمًا ﴿١٥٦﴾ وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَىٰ ابْنَ
 مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَٰكِن شُبِّهَ لَهُمْ ۚ وَإِنَّ
 الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ مِّنْهُ ۚ مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا
 اتِّبَاعَ الظَّنِّ ۚ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا ﴿١٥٧﴾ بَلْ رَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ ۚ وَكَانَ
 اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٥٨﴾ وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ إِلَّا لَيُؤْمِنَنَّ
 بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِمْ ۗ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِدًا ﴿١٥٩﴾
 فَيُظَلَّمُونَ مِنَ الَّذِينَ هَادُوا حَرَمًا عَلَيْهِمْ طَبِئَتْ أُحْلَتْ لَهُمْ
 وَبِصَدْرِهِمْ عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ كَثِيرًا ﴿١٦٠﴾ وَأَخَذَهُمُ الزَّلْزَلَةُ وَقَدْ
 جُئُوا عَنْهُ وَأَكْلِهِمْ أَمْوَالِ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ ۗ وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ
 مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٦١﴾ لَٰكِنِ الرَّاسِخُونَ فِي الْعِلْمِ مِنْهُمْ
 وَالْمُؤْمِنُونَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ ۗ
 وَالْقِيمِينَ الصَّلَاةَ وَالْمُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَالْمُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ
 وَالْيَوْمِ الْآخِرِ أُولَٰئِكَ سَنُؤْتِيهِمْ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٦٢﴾

فِيمَا نَقَضِهِمْ مِيثَقَهُمْ وَكُفِّرِهِمْ
 بِعَايَتِ اللَّهِ وَقَتْلِهِمُ الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقٍّ
 وَقَوْلِهِمْ قُلُوبُنَا غُلْفٌ ۚ بَلْ طَبَعَ اللَّهُ
 عَلَيْهَا بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا
 ﴿١٥٥﴾ وَكُفِّرِهِمْ وَقَوْلِهِمْ عَلَىٰ مَرْيَمَ
 بِهَتْنًا عَظِيمًا ﴿١٥٦﴾ وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا
 الْمَسِيحَ عِيسَىٰ ابْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ
 وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَٰكِن شُبِّهَ لَهُمْ
 ۚ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ
 مِّنْهُ ۚ مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتِّبَاعَ
 الظَّنِّ ۚ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا ﴿١٥٧﴾ بَلْ
 رَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا
 حَكِيمًا ﴿١٥٨﴾ وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ
 إِلَّا لَيُؤْمِنَنَّ بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِمْ ۗ وَيَوْمَ
 الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِدًا ﴿١٥٩﴾

155. Basi kwa sababu ya kuvunja kwao ahadi zao, na

kuzikataa kwao ishara za Mwenyezi Mungu, na kuwauwa kwao Manabii bila ya haki, na kusema kwao: Nyoyo zetu zimefumbwa; bali Mwenyezi Mungu Amezipiga muhuri kwa kufuru zao, basi hawaamini ila kidogo tu.

156. Na pia kwa kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa,

157. Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuuwa wala

hawakumsulubu, bali walifananishiwa tu. Na hakika walio khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Wala hawakumuwa kwa yakini.

158. Bali Mwenyezi Mungu Alimuinua kwake (mbinguni), na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.

159. Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

Makosa Makubwa ya Mayahudi

Madhambi yaliyotajwa hapo ni miongoni mwa madhambi yaliyofanywa na mayahudi, ambayo yalifanya walaaniwe na wakawekwa mbali na muongozo sahihi. Mayahudi, walivunja ahadi na viapo Allah تعالى Alivyochukua kutoka kwao. Walikanusha Ayah za Allah تعالى, yaani dalili zake na ushahidi na miujiza waliyoshuhudia katika mikono ya Mitume yao. Allah تعالى Amesema,

وَقَتَلِهِمُ الْأَنْبِيَاءَ بِغَيْرِ حَقِّ

“...na kuwauwa kwao Manabii bila ya haki...”

Kwa sababu ya makosa mengi na maovu dhidi ya Mitume wa Allah تعالى, kwani waliwaua Mitume wengi, Allah تعالى Awawie radhi wote. Kauli yao,

قُلُوبُنَا غُلْفٌ

“...Nyoyo zetu zimefumbwa...”

Muradi wake kuwa walizungushiwa kifuniko. Kwa mujibu wa Abbas, Mujahid, Said bin Jabayr, Ikrimah, As-Suddi na Qatadah رضي الله عنهم¹, maneno haya ni sawa na yale waliyosema mushirikina,

وَقَالُوا قُلُوبُنَا فِي أَكِنَّةٍ مِّمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ

“Na wakasema: Nyoyo zetu zimo katika vifuniko kwa hayo unayo tuitia...” (41:5)

¹At - Tabari 9:364.

Allah تعالیٰ Amesema,

بَلْ طَبَعَ اللَّهُ عَلَيْهَا بِكُفْرِهِمْ

“...bali Mwenyezi Mungu Amezipiga muhuri kwa kufuru zao...”

Ni kama vile kutoa udhuru kuwa mioyo yao haiielewi yaliyosemwa na Mtume ﷺ kwa kuwa mioyo yao imefunikwa. Hivyo wanadai, Allah تعالیٰ Alisema kuwa mioyo yao imepigwa mihuri kutokana na ukafiri wao, kama tulivyotaja kabla tulipokuwa tunaelezea *Surat Al-Baqarah*. Kisha Allah تعالیٰ Amesema,

فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا

“...basi hawaamini ila kidogo tu...” Kwani nyoyo zao zimezama kwenye kufuru, kuchupa mipaka na imani dhaifu.

Maneno Machafu Waliyoyatamka Mayahudi Dhidi ya Maryamu na Madai Yao Kuwa Walimuua Issa عليه السلام.

Allah تعالیٰ Amesema,

وَبِكُفْرِهِمْ وَقَوْلِهِمْ عَلَىٰ مَرْيَمَ هَتَنًا عَظِيمًا

“...Na pia kwa kufuru zao na kumsingizia kwao Maryamu uwongo mkubwa...”

Ali bin Talha alisema kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alieleza kuwa Mayahudi walimshutumu Maryam kwa uzinzi.¹ Hii pia ni kauli ya As-Suddi, Juwaybir, Muhammad bin Ishaq na wengineo.² Maana hii pia ni wazi katika aya, kama Mayahudi walivyo mshutumu Maryam na mwanawe kwa shutuma zisizo kifani. Walimlaumu kwa kuzini na kudai kuwa alikuwa akizini huku yumo katika hedhi. Laana ya Allah تعالیٰ inaendelea kuwashukia mpaka siku ya Hukumu. Aidha Mayahudi walisema,

وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَىٰ ابْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ

“Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu...”

Maana yake: Tulimuua mtu aliyedai kuwa Mtume ﷺ, Mayahudi waliropoka maneno hayo kwa kejeli na mzaha, kama mushirikina walivyosema,

¹ At - Tabari 9:367.

² At - Tabari 9:367.

وَقَالُوا يَا أَيُّهَا الَّذِي نُزِّلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ إِنَّكَ لَمَجْنُونٌ ﴿١٥٦﴾

“Na walisema: Ewe uliyeteremshiwa Ukumbusho! Hakika wewe ni mwendawazimu.” (15:6)

Katika jumla ya kuelezea habari za Mayahudi, Allah تعالی Awalaani, Awakasirikie na Awaadhibu, ni kuwa Allah تعالی Alipomtuma Issa عليه السلام, Mtume Wake aliyekuja na dalili za wazi kabisa, walimuonea wivu kwa sababu ya utume wake na miujiza iliyokuwa dhahiri, ya kuwaponya vipofu, wenye mbalanga, ukoma na kuwafufua wafu, yote haya kwa uwezo aliopewa na Allah تعالی. Pia alifinyanga umbile la ndege kwa udongo na akilipuliza na kuwa ndege mwenye kuruka, kwa Idhini ya Allah تعالی.

Issa عليه السلام alifanya miujiza mingine mingi aliyobarikiwa na Allah تعالی, bali Mayahudi walimkanusha, kumbeza na walijitahidi kumdhuru. Mtume wa Allah Issa عليه السلام hakuweza kuishi katika sehemu moja kwa muda mrefu, hivyo kila mara alikuwa safarini pamoja na mama yake, amani iwe juu yao. Hata hivyo Mayahudi hawakuwa radhi, na walimuendea mfalme wa Damascus wa wakati ule, kafiri aliyekuwa akiabudu nyota. Walimueleza kuwa alikuwepo mtu *Bayt Al-Maqdis* akiwapotosha watu na kuwafarakanisha huko Jerusalem na akiwasumbua watu wa mfalme. Mfalme alikasirika na akamuandikia msaidizi wake Jerusalem amtie nguvuni na asitische vurumai zake, wamsulubu na amvishe taji la miiba. Makamu wa Mfalme, alipopeleka amri ile, walitoka na baadhi ya mayahudi na kwenda kwa Issa عليه السلام, na alikuwa na wasaidizi wake kiasi cha kumi na wawili au kumi na watatu na inasemekana kuwa walikuwa kumi na saba. Siku hiyo ilikuwa ni siku ya Ijumaa jioni. Walimzingira Issa عليه السلام nyumbani kwake, na alipohisi kuwa walikaribia kuingia na wangaliondoka aliwaambia wafuasi wake, “Nani anajitolea kufanana nami, na kuwa atakuwa pamoja nami peponi?” Kijana mmoja alijitolea, lakini Issa عليه السلام alimuona mdogo sana. Aliuliza swali tena mara ya pili na ya tatu, kila mara yule kijana alijitolea, ile hali ikamfanya Issa عليه السلام aseme, “Vyema basi atakuwa yule mtu.” Allah تعالی Alifanya yule kijana kuonekana sawa na Issa عليه السلام, na wakati huo paa likawa wazi na Issa عليه السلام akapitiwa na usingizi na akarufaishwa mbinguni akiwa usingizini. Allah تعالی Amesema,

إِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَىٰ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ

“(Kumbukeni) Pale Mwenyezi Mungu Aliposema: Ewe Isa! Mimi Nitakutimizia muda wako wa kuishi (hawatakuua hao maadui). Na Nitakunyanyua Kwangu.” (3:55)

Issa عليه السلام aliporufaishwa, wale waliokuwemo ndani ya nyumba walitoka nje, wale watu waliozingira nyumba walipomuona yule mtu aliyefanana na Issa عليه السلام, walidhani ndiye Issa عليه السلام. Hivyo walimchukua usiku, wakamsulubu na wakamuweka taji la miiba juu ya kichwa chake, kisha Mayahudi walijisifia kuwa walimuua Issa عليه السلام na baadhi ya wakristo waliyakubali madai yao kutokana na ujinga wao na kushindwa kutafakari. Ama wale waliokuwa ndani na Issa عليه السلام, walishuhudia kurufaishwa kwake kwenda mbinguni, ambapo waliosalia walidhani kuwa Mayahudi walimuua Issa عليه السلام kwa kumsulubu, Aidha walisema kuwa Maryam alikaa chini ya maiti ya mtu aliyesulubiwa huku akilia, na wakasema maiti alizungumza naye yote haya ulikuwa mtihani kutoka kwa Allah تعالى kwa waja wake kuonesha Hekima Yake, Allah تعالى Amelieleza suala hili ndani ya Qur'an Takatifu ambayo Alimpelekea kwa kumpa usaidizi kwa kumpa miujiza kwa miujiza na ushahidi usiopingika. Allah تعالى, ni Bwana wa ulimwengu Ajuaye siri, ya yanayofichwa na nafsi na yatakayotokea baada ya Kuyaamuru na yasiyokuwa yakiwa na jinsi yatakavyokuwa, Amesema,

وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَٰكِن شُبِّهَ هُمْ

“...nao hawakumuua wala hawakumsulubu, bali walifananishiwa tu...”

Inahusu mtu ambaye Mayahudi walidhani kuwa ni Issa عليه السلام. Ndipo Allah تعالى Akasema baada ya hapo:

وَإِنَّ الَّذِينَ اٰخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ مِّنْهُ مَا لَهُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتِّبَاعَ الظَّنِّ

“...Na hakika waliokhitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu...”

Inahusu Mayahudi waliodai kumuua Issa عليه السلام na wakristo wajinga waliowaamini, kwa hakika wote wamechanganyika na wamepotoshwa ndio sababu Allah تعالى Alisema,

وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا

“...Wala hawakumuua kwa yakini.”

Maana yake: Hawana uhakika kuwa waliyemuua ndiye Issa عليه السلام. Bali wana mashaka na wamechanganyikiwa kuhusu suala hili.

بَلْ رَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيْهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٥٥﴾

“Bali Mwenyezi Mungu Alimuinua kwake (mbinguni), na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Maana yake: Ni Yeye Allah تعالى, na hana udhaifu wala wale waliokimbilia Kwake kwa msaada hatowakataa na Akawaacha wafadhaike,

حَكِيمًا ﴿١٥٦﴾

“Mwenye hikima.” Katika yote Anayoamua na Anayofundisha kwa viumbe wake hakika Allah تعالى ni Mwenye Hikima iliyo wazi na dalili zilizo wazi na Utawala Uliotukuka. Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alipokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, “Kabla ya kumrufaisha Issa عليه السلام mbinguni. Issa عليه السلام alikwenda kwa wafuasi wake ambao walikuwa kumi na wawili ndani ya nyumba. Alipowasili nywele zake zilitiririka maji na alisema, “walio miongoni mwenu ambao waliniamini mara kumi na mbili watakuja kunikufuru baada ya kuniamini,” kisha alisema, “Nani anayejitolea taswira yake iwe sawa na yangu, na auwawe badala yangu. Atakuwa pamoja nami peponi?”

Mmoja wao aliyekuwa mdogo kabisa alijitolea na Issa عليه السلام akamuambia akae kitako: Issa عليه السلام akataka tena mtu wa kujitolea, na yule kijana Mdogo akajitolea tena na Issa عليه السلام akamuambia akae tena. Kisha yule kijana alijitolea tena na Issa عليه السلام akasema, “Atakuwa yule mtu.” Na sura ya Issa عليه السلام ilivishwa kwa yule mtu wakati Issa عليه السلام alirufaishwa peponi kupitia tundu katika paa la nyumba. Mayahudi walipokuja kumtafuta Issa عليه السلام, walimkuta yule kijana na wakamsulubu. Baadhi ya wafuasi wa Issa عليه السلام hawakumuamini mara kumi. Kisha wakagawika katika makundi matatu. Kundi moja, *Al-Ya'qubiyyah* walisema, “Mwenyezi Mungu alibaki nasi kama alivyotaka na kisha akapaa kwenda mbinguni.” Kundi jingine *An-Nasturiyyah* walisema, “Mtoto wa Mungu alikuwa nasi kama alivyotaka, Allah تعالى Akamchukua mbinguni.” Na kundi la tatu likasema kuwa, “alikuwepo Mtume pamoja nasi kisha Allah تعالى Akamrufaisha.” Makundi mawili ya makafiri walishirikiana dhidi ya kundi la Waislamu na wakawauwa. Toka tukio hilo, Uislamu ulihifadhiwa mpaka Allah تعالى Alipomtuma Muhammad ﷺ.¹ Nasai alipokea kutoka kwa Abu Kurayb ambaye alinukuu kutoka kwa Abu Muawiyah mfano wake.² Wengi miongoni mwa *Salaf* walieleza kuwa Issa عليه السلام aliuliza kuwa

¹ Ibn Abi Hatim 4:1110.

² An-Nasai katika *Al-Kubraa* 6:489.

endapo mmoja wao angelijitolea kuonekana kama yeye, na kuwa angeliuawa badala ya Issa عليه السلام, na kuwa angelikuwa wako peponi.

Wakristo Watamuamini Issa عليه السلام Kabla Hajafariki Dunia

Allah تعالى Amesema,

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ إِلَّا لِيُؤْمِنُوا بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِ^ط وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا ﴿١٥٩﴾

159. "Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao."

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema,

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ إِلَّا لِيُؤْمِنُوا بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِ

"Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake."

Kabla ya kutawafu Issa عليه السلام, mwana wa Maryam. Al-Awf alinukuu kauli sawa na hiyo kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.¹ Abu Maliki aliitolea maelezo,

إِلَّا لِيُؤْمِنُوا بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِ

"...ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake." Hili litajiri baada ya Issa عليه السلام kurejea na baada ya kufariki dunia, na wakati huo, watu wote wa kitabu watamuamini.²

Hadithi Kuhusu Kushuka kwa Issa عليه السلام Kabla ya Kiyama, na Ujumbe Wake.

Katika mlango juu ya Mitume katika sahihi yake, chini ya anuani, "kushuka kwa Issa عليه السلام, Mwana wa Maryam," Bukhari alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَيُوشِكَنَّ أَنْ يَنْزَلَ فِيكُمْ ابْنُ مَرْيَمَ حَكَمًا عَدْلًا، فَيَكْبِرَ الصَّلِيبَ، وَيَقْتُلَ الْخَنَازِيرَ، وَيَضَعِ الْجِزْيَةَ، وَيَبْيِضَ الْمَالَ حَتَّى لَا يَقْبَلَهُ أَحَدٌ، حَتَّى تَكُونَ السَّجْدَةُ خَيْرًا لَهُمْ مِنَ الدُّنْيَا وَمَا فِيهَا»

¹ At - Tabari 9:380.

² At - Tabari 9:380.

"Naapa kwa ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake, mwana wa Maryam (Issa) karibu atashuka kwenu, kuwa kiongozi muadilifu na atavunja msalaba, ataua nguruwe na kufuta Jizya (kodi), mali itajaa hadi hakuna yoyote atakayeipokea (sadaka). Zama hizo, sijda moja itakuwa bora kuliko dunia na vilivyomo ndani yake."

وَإِنَّ مِنْ أَهْلِ الْكِتَابِ إِلَّا لِيُؤْمِنُوا بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِمْ وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا ﴿١٥٥﴾

"Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao."¹

Muslim aliinukuu Hadithi hii.² Hivyo Kauli ya Allah تعالى،

قَبْلَ مَوْتِهِمْ

"Kabla ya kufa kwake." Inahusu kutawafu Issa عليه السلام، mwana wa Maryam.

Hadithi Nyingine ya Abu Hurayrah رضي الله عنه

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema،

«لِيَهْلُنَّ عَيْسَى بِفَجِّ الرُّوحَاءِ بِالْحَجِّ أَوْ الْعُمْرَةِ، أَوْ لِيَتَّيَهُمَا جَمِيعًا»

*"Issa atasoma Ihlal kutoka katika njia ya mlima ya Ar-Rawha kwa ajili ya Hija na Umrah au vyote."*³

Muslim pia aliirekodi.⁴ Ahmad alirekodi kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema،

«يُنزِلُ عَيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ فَيَقْتُلُ الْخَنزِيرَ، وَيَمْحُو الصَّلِيبَ، وَتُجْمَعُ لَهُ الصَّلَاةُ، وَتُعْطَى الْمَالُ حَتَّى لَا يُقْبَلَ، وَيَضَعُ الْخَرَاجَ، وَيُنزِلُ الرُّوحَاءَ فَيَحُجُّ مِنْهَا أَوْ يَغْتَمِرُ أَوْ يَجْمَعُهُمَا»

"Issa mwana wa Maryam atashuka na ataua nguruwe, atavunja msalaba, ataongoza Swala ya jamaa na atagawa mali mpaka

¹ Fat'hul Bari 6:566.

² Muslim 1:135 na Fat'hul Bari 5:44, 4:483.

³ Ahmad 2:513.

⁴ Muslim 1:135.

haitopokelewa na yeyote. Pia atapiga marufuku Jizyah na atakwenda Ar-Rawha kisha kuelekea Kuhiji au kufanya Umra au vyote pamoja."

Kisha Abu Hurayrah رضي الله عنه alisoma,

وَإِن مِّنْ أَهْلِ الْكِتَابِ إِلَّا لِيُؤْمِنَنَّ بِهِ قَبْلَ مَوْتِهِ

"Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake."

Hanzalah رضي الله عنه alisema, "Abu Hurayrah رضي الله عنه aliongeza, Watamuamini Issa عليه السلام kabla ya kufariki dunia, lakini sijui kuwa hii ilikuwa sehemu ya Hadithi ya Mtume au lilikuwa ni jambo alilosema Abu Hurayrah رضي الله عنه mwenyewe."¹ Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى naye alirekodi Hadithi hii.

Hadithi Nyingine

Bukhari alinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«كَيْفَ بِكُمْ إِذَا نَزَلَ فِيكُمْ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ وَإِمَامُكُمْ مِنْكُمْ»

"Mtakuwaje pindi Masih, mwana wa Maryam (Issa) atakapowashukia wakati Imam wenu ni mtu miongoni mwenu?"²

Imam Ahmad na Muslim walinukuu Hadithi hii.³

Hadithi Nyingine

Imam Ahmad alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْأَنْبِيَاءُ إِخْوَةٌ لِعَلَّاتِ، أُمَّهَاتُهُمْ شَتَّى، وَدِينُهُمْ وَاحِدٌ، وَإِنِّي أَوْلَى النَّاسِ بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ، لِأَنَّهُ لَمْ يَكُنْ نَبِيًّا بَيْنِي وَبَيْنَهُ، وَإِنَّهُ نَازِلٌ فَإِذَا رَأَيْتُمُوهُ فَأَعْرِفُوهُ: رَجُلٌ مَرْبُوعٌ إِلَى الْحُمْرَةِ وَالْبِيَاضِ، عَلَيْهِ ثَوْبَانِ مُمَصَّرَانِ، تَأَنَّ رَأْسَهُ يَقَطُرُ، وَإِن لَّمْ يُصْبَهُ بَلَلٌ، فَيَدُقُّ الصَّلِيبَ، وَيَقْتُلُ الْخَنْزِيرَ، وَيَضَعُ الْجِزْيَةَ، وَيَدْعُو النَّاسَ إِلَى الْإِسْلَامِ، وَيُهْلِكُ اللَّهُ فِي زَمَانِهِ الْجَمَلَ كُلَّهَا إِلَّا الْإِسْلَامَ، وَيُهْلِكُ اللَّهُ فِي زَمَانِهِ الْمَسِيحَ

¹ Ahmad 2:290.

² Fat'hul Bari 6:566.

³ Ahmad 2:272 na Muslim 1:136 – 137.

الدَّجَالِ، ثُمَّ تَقَعُ الْأَمْنَةُ عَلَى الْأَرْضِ حَتَّى تَزْتَعَ الْأَسْوَدُ مَعَ الْإِبِلِ، وَالنَّمَارُ مَعَ
الْبَقَرِ، وَالذَّنَابُ مَعَ الْعَمَمِ، وَيَلْعَبُ الصَّبِيَانُ بِالْحَيَاتِ لَا تَضُرُّهُمْ، فَيَمُكُّتُ أَرْبَعِينَ
سَنَةً ثُمَّ يَتَوَفَّى، وَيُصَلِّي عَلَيْهِ الْمُسْلِمُونَ»

“Mitume ni ndugu kwa baba; mama zao ni tofauti, lakini Dini yao ni moja. Mimi zaidi ya binadamu yeyote, nina haki zaidi kwa Issa, mwana wa Maryam, kwani hapakuwa na Mtume kati yake na yangu: atashuka na kama utamuona, mfahamuni, kuwa, ni mtu wa miraba mine, rangi ya mwili wake ni kati ya nyekundu na nyeupe, atashuka huku amevalia nguo mbili ndefu za rangi ya njano. Kichwa chake kitaonekana kama kinavuja maji, pamoja na kuwa hakuna maji yoyote. Atavunja msalaba, ataua nguruwe na kufuta Jizyah na atawalingania watu kwenye Uislamu. Wakati wa zama zake Allah Ataziangamiza dini zote isipokuwa Uislamu na Allah Atamuangamiza Al-Masih Ad-Dajjal (Massiah wa uongo). Amani itaenea duniani, kiasi ambacho simba watachanganyika na Ngamia, wanyama wakali wa mbugani na ng’ombe na mbweha na kondoo. Watoto watacheza na nyoka, na hawatawadhuru. Issa ataishi kwa miaka arubaini. Na kisha atafariki dunia, na Waislamu watamzika.”

Abu Dawud pia ameinukuu.¹

Hadithi Nyingine.

Katika Sahih yake, Muslim alinukuu kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه alitamka kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى يَنْزِلَ الرُّومُ بِالْأَعْمَاقِ أَوْ بِدَابِقٍ، فَيَخْرُجُ إِلَيْهِمْ جَيْشٌ مِنَ
الْمَدِينَةِ مِنْ خِيَارِ أَهْلِ الْأَرْضِ يَوْمَئِذٍ، فَإِذَا تَصَافَوْا، قَالَتِ الرُّومُ: خَلُّوا بَيْنَنَا وَبَيْنَ
الَّذِينَ سَبَّوْنَا مِنَّا نَقَاتِلَهُمْ، فَيَقُولُ الْمُسْلِمُونَ: لَا وَاللَّهِ، لَا نُحَلِّي بَيْنَكُمْ وَبَيْنَ إِخْوَانِنَا،
فَيَقَاتِلُونَهُمْ، [فَيَنْهَزُهُمْ] نُلْتُ لَا يَتُوبُ اللَّهُ عَلَيْهِمْ أَبَدًا، وَيَقْتُلُ نُلْتُ أَفْضَلَ الشَّهَدَاءِ عِنْدَ
اللَّهِ، وَيَنْسَحُ الثَّلْثَ لَا يُقْتَلُونَ أَبَدًا، فَيَفْتَحُونَ فُسْطَاطِيْنِيَّةً، فَيَبْنِيْنَ هُمْ يَقْسِمُونَ الْغَنَائِمَ
قَدْ عَلَفُوا سُبُوقَهُمْ بِالرَّيْثُونَ، إِذْ صَاحَ فِيهِمُ الشَّيْطَانُ: إِنَّ الْمَسِيحَ قَدْ خَلَفَكُمْ فِي
أَهْلِيكُمْ، فَيَخْرُجُونَ، وَذَلِكَ بَاطِلٌ، فَإِذَا جَاءُوا الشَّامَ خَرَجَ، فَيَبْنِيْنَ هُمْ يُعَدُّونَ

¹ Ahmad 2:406, Abu Dawud; 4334, At - Tabari 9:388.

لِلْقِتَالِ يُسَوِّرُونَ الصُّفُوفَ، إِذْ أُتِمَّتِ الصَّلَاةُ فَيَنْزِلُ عَيْسَى ابْنُ مَرْيَمَ، فَأَمَّهُمْ، فَإِذَا رَأَى
عَدُوَّ اللَّهِ، ذَابَ كَمَا يَذُوبُ الْجِلْحُ فِي الْمَاءِ، فَلَوْ نَرَكُهُ لَأَنْدَابَ حَتَّى يَهْلِكَ، وَلَكِنْ
يَقْتُلُهُ اللَّهُ بِيَدِهِ، فَيَرِيهِمْ دَمَهُ فِي حَرْبِيهِ»

"Hakitosimama Kiyama mpaka Warumi waitawale Al-A'maq au Dabiq¹ kisha litawatokea Jeshi bora katika ardhi watakuja kutoka Madina na kupambana nao. Watakapokabiliana uso kwa uso, warumi watasema, 'Tuwapige waliowateka baadhi yetu!' Waislamu watasema, 'Hapana, Wallahi, hatutowaruhusu muwafikie ndugu zetu.' Watapigana nao. Theluthi nyingine watauawa, na hao ni mashahidi bora mbele ya Allah. Theluthi ya mwisho watashinda, na theluthi hii haitadhuriwa na Fitnah, na wataiteka Istanbul. Wakati watakapokuwa wanagawana ngawira baada ya kuzitundika panga juu ya mitende, shetani atawapigia kelele, huku akisema, 'Masih (Ad-Dajjal) amewazuia watu wema.' Watakwenda kukutana na Ad-Dajjal huko Ash-Sham. Hii itakuwa indhari ya uongo, na watakapofika As-Sham, ndipo Ad-Dajjal atajitokeza. Waislamu watakapokuwa wakipanga safu kwa ajili ya vita na adhana kutolewa, Issa mwana wa Maryam, atashuka na kuwaswalisha. Adui wa Allah (Massiah) wa uongo atakapomuona, atayeyuka kama chumvi inavyoyayuka ndani ya maji, na kama sehemu itasalia nayo itayeyuka mpaka afe. Kwa Idhini ya Allah Dajali atauliwa kwa mkono wa Issa na atawaonesha Waislamu damu yake kwenye mkuki wake."²

Muslim alinukuu kuwa Abdullah bin Amri رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«لَقَاتِلَنَّ الْيَهُودَ فَلَقَاتِلْتُهُمْ، حَتَّى يَقُولَ الْحَجَرُ: يَا مُسْلِمُ هَذَا يَهُودِيٌّ فَتَعَالَ فَاتْتَلُهُ»

"Mtawapiga Mayahudi na kuwaua, mpaka jiwe litakaposema, 'Ewe Muislamu! Kuna Myahudi hapa, njoo umuue."³

«لَا تَقُومُ السَّاعَةُ حَتَّى يُقَاتِلَ الْمُسْلِمُونَ الْيَهُودَ، فَيَقْتُلُهُمُ الْمُسْلِمُونَ حَتَّى يَخْتَبِئَ
الْيَهُودِيُّ مِنْ وَرَاءِ الْحَجَرِ وَالشَّجَرِ، فَيَقُولُ الْحَجَرُ وَالشَّجَرُ: يَا مُسْلِمُ يَا عَبْدَ اللَّهِ هَذَا
يَهُودِيٌّ خَلْفِي فَتَعَالَ فَاتْتَلُهُ - إِلَّا الْغَرْقَدَ فَإِنَّهُ مِنْ شَجَرِ الْيَهُودِ»

¹Miji miwili jirani na Aleppo nchini Syria.

²Muslim 4:2221.

³Muslim 4:2238.

"Kiyama hakitoanza mpaka baada ya Waislamu kuwapiga Mayahudi na kuwaua. Yahudi atajificha nyuma ya jiwe au mti, na mti utasema, Ewe'Muislamu! Ewe mtumishi wa Allah! Huyu ni Yahudi nyuma yangu, njoo umuuwe! Isipokuwa Al-Gharqad, kwa kuwa ni mti wa Mayahudi."

Muslim bin Al-Hajjaj alinukuu ndani ya Sahih yake kuwa An-Nawwas bin Saman رضي الله عنه alisema, "Mtume ﷺ alimtaja Ad-Dajjal siku moja na akawa anamdhalilisha (kwa sababu ni kipofu na huku akidai kuwa ni mungu) na akisema maneno mabaya juu yake mpaka tukadhani alikuwa amejificha ndani ya bustani ya mitende (Madinah). Tulipopita kwa Mtume ﷺ, alihisi hamu yetu ya kutaka kujua jambo. Akauliza:

«مَا شَأْنُكُمْ؟»

"Mna nini?" Tukasema, 'Ewe Mjumbe wa Allah! Mwanzo, ulimtaja Ad-Dajjal na ambapo ukamdhalilisha na ukazungumza ubaya wake mpaka tukadhani alikuwa amejificha ndani ya bustani ya mitende (ya Madinah). Alisema

«غَيْرُ الدَّجَالِ أَخَوْفِي عَلَيْكُمْ، إِنْ بَخْرُجَ وَأَنَا فِيكُمْ فَأَنَا حَاجِبُهُ دُونَكُمْ، وَإِنْ يَخْرُجَ
وَلَسْتُ فِيكُمْ فَأَمْرُؤُ حَاجِبٌ نَفْسِهِ، وَاللَّهُ خَلِيفَتِي عَلَى كُلِّ مُسْلِمٍ. إِنَّهُ شَابٌ قَطَطٌ،
عَيْنُهُ طَافِيَةٌ كَأَنِّي أَنَسِبُهُ بِعَبْدِ الْعُرَى بْنِ قَطَنِ، مَنْ أَدْرَكَهُ مِنْكُمْ فَلْيَقْرَأْ عَلَيْهِ نَوَاحِ
سُورَةِ الْكَهْفِ، إِنَّهُ خَارِجٌ مِنْ خَلَّةٍ بَيْنَ الشَّامِ وَالْعِرَاقِ، فَعَاثٌ بَيْبِنَا وَعَاثٌ شِمَالًا،
بِأَعْبَادِ اللَّهِ فَانْبُتُوا»

"Nakuhofieni zaidi ya Ad-Dajjal! Akitokea nami nipo miongoni mwenu, nitakuwa hasimu wake kwa niaba yenu. Na akitokea wakati sipo miongoni mwenu, kila mtu atajitegemea na Allah Atakuwa msaidizi wa kila Muislamu baada yangu. Ni kijana, ana nywele zilizosokotwa na jicho lake limetobolewa. Nilidhani kuwa anafanana na Abdul – Uzza bin Qatan. Yeyote atakayeishi kwa muda mrefu na akakutana na Ad-Dajjal, basi na asome mwanzo mwa Surat Al-Kahf, atatokezea katika njia kati ya As-Sham (Syria) na Iraq. Atazusha balaa, kulia na kushoto enyi Waja wa Allah! Shikamaneni".

Tukauliza, "Ewe Mjumbe wa Allah! Atakaa duniani kwa muda gani?" Akajibu,

¹ Muslim 4:2250.

«أَزْبَعُونَ يَوْمًا، يَوْمَ كَسَنِيَّ، وَيَوْمَ كَسَنَهِيَ، وَيَوْمَ كَجَمْعِي، وَسَائِرُ أَيَّامِهِ كَأَيَّامِكُمْ»

"Siku arubaini. Siku moja sawa na mwaka, siku moja sawa na mwezi na siku moja sawa na wiki, siku zake zilizosalia zitakuwa sawa na siku yenu moja."

Tukamuambia, "Ewe Mjumbe wa Allah! Kuhusu siku inayolingana na mwaka, Je Swala za siku moja zitatosha?" Akajibu,

«لَا، أَقْدُرُوا لَهُ قَدْرَهُ»

"Hapana zihesabuni kwa kipimo chake".

Tukauliza, 'Ewe Mtume ٤٤, mwendo wake utakuwaje juu ya ardhi?' Akasema,

«كَالْعَيْثِ اسْتَدْبَرْتَهُ الرِّيحُ فَيَأْتِي عَلَى قَوْمٍ يَدْعُوهُمْ فَيُؤْمِنُونَ بِهِ، وَيَسْتَجِيبُونَ لَهُ، فَيَأْمُرُ السَّمَاءَ فَتُمْطِرُ، وَالْأَرْضَ فَتَنْثَبُ، فَتَرْوِحُ عَلَيْهِمْ سَارِحَتَهُمْ أَطْوَلَ مَا كَانَتْ ذُرَى، وَأَسْبَغَهُ ضُرُوعًا، وَأَمَدَهُ خَوَاصِرَ، ثُمَّ يَأْتِي الْقَوْمَ فَيَدْعُوهُمْ فَيَرُدُّونَ عَلَيْهِ قَوْلَهُ، فَيَنْصَرِفُ عَنْهُمْ فَيُضْبِحُونَ مُنْجِلِينَ لَيْسَ بِأَيْدِيهِمْ شَيْءٌ مِنْ أَمْوَالِهِمْ وَيَمُرُّ بِالْخَرِيبَةِ يَقُولُ لَهَا: أَخْرَجِي كُنُوزَكَ، فَتَبْعُهُ كُنُوزُهَا كَيْعَابِيبِ التَّحْلِ، ثُمَّ يَدْعُو رَجُلًا مُمْتَلِكًا شَبَابًا فَيَضْرِبُهُ بِالسِّنْبِ، فَيَقْطَعُهُ جِزْلَتَيْنِ رَمِيَةَ الْغَرَضِ، ثُمَّ يَدْعُوهُ، فَيَقْبَلُ وَيَتَهَلَّلُ وَجْهَهُ وَيَضْحَكُ، فَيَيْنَمَا هُوَ كَذَلِكَ إِذْ بَعَثَ اللَّهُ الْمَسِيحَ ابْنَ مَرْيَمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ، فَيَنْزِلُ عِنْدَ الْمَنَارَةِ الْبَيْضَاءِ شَرْقِيٍّ دِمَشْقَ بَيْنَ مَهْرُودَتَيْنِ، وَاصْبَعًا كَفَيْهِ عَلَى أُجْنِحَةِ مَلَكَتَيْنِ، إِذَا طَاطَأَ رَأْسُهُ قَطَرَ، وَإِذَا رَفَعَهُ تَحَدَّرَ مِنْهُ جُمَانٌ كَاللُّؤْلُؤِ، وَلَا يَجِلُّ لِكَاْفِرٍ يَجِدُ رِيحَ نَفْسِهِ إِلَّا مَاتَ، وَنَفْسُهُ يَنْتَهِي حَيْثُ يَنْتَهِي طَرْفُهُ، فَيَطْلُبُهُ حَتَّى يَدْرِكَهُ بِيَابِ لُدٍّ، فَيَقْتُلُهُ، ثُمَّ يَأْتِي عِيسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ فَرَمَا قَدْ عَصَمَهُمُ اللَّهُ مِنْهُ، فَيَنْسَحُ عَنْ جُورِهِمْ، وَيُحَدِّثُهُمْ بَدْرَجَاتِهِمْ فِي الْجَنَّةِ، فَيَيْنَمَا هُوَ كَذَلِكَ إِذْ أَوْحَى اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ إِلَى عِيسَى: إِنِّي قَدْ أَخْرَجْتُ عِبَادًا لِي لَا يَدَانِ لِأَحَدٍ بِقَاتِلِهِمْ، فَحَرَّزْ عِبَادِي إِلَى الطُّورِ، وَيَبْعَثُ اللَّهُ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ وَهُمْ مِنْ كُلِّ حَدْبٍ يَنْسِلُونَ، فَيَمُرُّ أَوْلَاهُمْ عَلَى بُحَيْرَةِ طَبْرِتَةَ فَيَسْرُبُونَ مَا فِيهَا، وَيَمُرُّ آخِرُهُمْ فَيَقُولُونَ: لَقَدْ كَانَ بِهِذِهِ مَرَّةً مَاءٌ، وَيُحْصِرُ نَبِيَّ اللَّهِ عِيسَى وَأَصْحَابَهُ، حَتَّى يَكُونَ رَأْسُ الثُّورِ لِأَحَدِهِمْ خَيْرٌ مِنْ مِقَاةِ دِينَارٍ لِأَحَدِكُمْ الْيَوْمَ، فَيَرْغَبُ نَبِيَّ اللَّهِ عِيسَى وَأَصْحَابُهُ، فَيُرْسِلُ اللَّهُ عَلَيْهِمُ النَّعْفَ فِي رِقَابِهِمْ، فَيُضْبِحُونَ فَرَسَى كَمَوْتِ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ، ثُمَّ يَهْبِطُ نَبِيَّ اللَّهِ عِيسَى

وَأَصْحَابُهُ إِلَى الْأَرْضِ، فَلَا يَجِدُونَ فِي الْأَرْضِ مَوْضِعَ شِبْرٍ إِلَّا مَلَأَهُ زَهْمُهُمْ
وَبَتْنُهُمْ، فَيَرْغَبُ نَبِيُّ اللَّهِ عِيسَى وَأَصْحَابُهُ إِلَى اللَّهِ، فَيُرْسِلُ اللَّهُ، طَيْرًا كَأَغْنَانِي
الْبُهْتِ، فَتَحْمِلُهُمْ فَتَطْرَحُهُمْ حَيْثُ شَاءَ اللَّهُ، ثُمَّ يُرْسِلُ اللَّهُ مَطَرًا لَا يَكُنُ مِنْهُ بَيْتٌ
مَدْرِي، وَلَا وَبْرِي، فَيَغْسِلُ الْأَرْضَ حَتَّى يَتْرُكَهَا كَالرُّلْفَةِ، ثُمَّ يَقَالُ لِلْأَرْضِ: أَخْرِجِي
كَمْرِكَ وَرُدِّي بَرَكَتِكَ، فَيَوْمِئِذٍ تَأْكُلُ الْعِصَابَةُ مِنَ الرُّمَاتِ، وَيَسْتَظِلُّونَ بِقِحْفِهَا، وَيُبَارِكُ
اللَّهُ فِي الرُّسْلِ حَتَّى إِنَّ اللَّسْعَةَ مِنَ الْإِبِلِ لَتَكْفِي الْفِتَامَ، [مِنَ النَّاسِ وَاللُّقْمَةَ مِنَ النَّمِ
لَتَكْفِي الْقِحْذَ مِنَ النَّاسِ]، فَيَتِمُّ هُمْ كَذَلِكَ إِذْ بَعَثَ اللَّهُ رِيحًا طَيِّبَةً، فَتَأْخُذُهُمْ تَحْتَ
أَبْطَاطِهِمْ، فَتَقْبِضُ رُوحَ كُلِّ مُؤْمِنٍ وَكُلِّ مُسْلِمٍ، وَيَبْقَى شِرَارُ النَّاسِ يَتَهَارَجُونَ فِيهَا
تَهَارَجَ الْحُمْرِ، فَعَلَيْهِمْ نَقُومُ السَّاعَةِ،

"Kama wimbi linaposukumwa na upepo. Atawaendea watu na atawalingania katika dini yake, watamuamini na kumkubali. Ataiamuru mbingu na mvua itanyesha, ardhi nayo itaotesha mimea. Ng'ombe nao watarejea wakiwa na manyoya marefu, na chuchu zao zimejaa maziwa na matumbo yamejaa. Atawaendea watu wengine na atawalingania katika dini yake, na watakataa wito wake. Kisha atawaacha wataamka asubuhi wakiwa masikini, wakiwa wamepoteza mali yao yote. Atapita katika ardhi isiyo na watu, na ataiambia, "Toa hazina yako" na hazina yake itamfuata kama kundi la nyuki. Atamuita kijana na atampiga panga moja na kumkata vipande viwili na vitagawanyika vipande hivyo umbali kati ya mwindaji na mnyama. Atamuita maiti naye atakuja, uso wake utameremeta kwa furaha na kicheko.

Baadaye wakati yote hayo yanatokea kwa hila za Dajjal, Allah Atampeleka Masih (Issa), mwana wa Maryam. Atashuka, jirani na mnara. Kaskazini mwa Damascus atakuwa amevaa nguo zenye rangi ya zafarani na mikono yake itakuwa juu ya mbawa za malaika wawili. Kila akiinamisha kichwa matone humwagika. Kila anapoinua kichwa chake, mawe ya thamani mithili ya lulu yanaanguka. Hapana kafiri atakayepona kutokana na pumzi za Issa, ambayo inafika masafa ya upeo wake wa macho. Atamsaka Ad-Dajjal na atamfuata katika milango ya (mji wa Palestina) Ludda ambapo inafika masafa ya upeo wake wa macho. Atamsaka Ad-Dajjal na atamfuata katika

milango ya (mji wa Palestina) Ludda ambapo atamuua. Kundi la watu, kwa msaada wa Allah, watamgomea na watasalimika na hila za Ad-Dajjal, watapita kwa Issa na atawapaka mafuta nyuso zao na atawapa habari juu ya madaraja yao peponi.

Muda mfupi baadaye, wakati haya yakitokea na Issa, Allah Atamuwekea wazi, 'Niliwainua watu Niliowaumba ambao hawawezi kupigwa. Kwa hiyo, wakusanye waja wangu na uende nao At-Tur (milima ya Musa katika Sinai).’ Kisha Allah Atawafufua Ya-Juj na Maajuj na wataogelea, vikosi vyao vya mbele vitafika ziwa Tabariah, Bahari ya Galilaya na watakunywa maji yake yote. Majeshi yao ya mwisho watasema wakati wakipita pembezoni mwa ziwa, 'Ziwa hili wakati mmoja lilikuwa moja!' Wakati huo, Issa, Mtume wa Allah, atakuwa amedhikika pamoja na wafuasi wake mpaka dume la ng'ombe lina thamani zaidi ya Dinar mia za leo. Isa, Mtume wa Allah, na wafuasi wake watamuomba Allah Awasaidie na Allah Atampeleka An-Naghaf (kiwavi) katika shingo ya Ya-Juj na Majuj! Kutapambazuka, na wote watakufa kama kifo cha nafsi moja. Baadaye, Isa, Mtume wa Allah, atavuka na wafuasi wake bondeni (kutoka Mlima At-Turi). Watakuta kuwa kipande cha ardhi sawa na kiganja kilicho wazi kwa maiti zilizooza, Isa, Mtume wa Allah, na wafuasi wake wataomba Dua kwa Allah. Allah Atawapeleka ndege wakubwa kama shingo ya Ngamia watachukua (maiti za Ya-Juj na Maajuj) na Atawatupa popote Allah Atakaporidhia. Baadaye Allah Atapeleka nuta ambayo haitasalimisha nyumba za tope na manyoya na itasafisha ardhi mpaka iwe safi kama kioo. Ardhi itaamrisha na Allah, 'Toa matunda na pata Baraka.' Kisha kundi litakula Matufaa na watahifadhi katika kivuli cha ngozi yake. Maziwa yatabarikiwa kiasi na Ngamia watatoa maziwa mengi ya kutosha watu wengi. Wakati huo, Allah Atapeleka upepo ambao utawashinda nguvu Waislamu chini ya mikono yao na utachukua kila roho ya muumini Muislamu. Waovu miongoni mwao watabaki, watafanya jimai hadharani kama punda. Kwao wao, Kiyama kitaanza.”¹

¹Muslim 4:2250.

Imam Ahmad na wakusanyaji wa suna, pia waliinukuu hadithi hii.¹ Tutaidhukuru Hadithi hii tena tukitumia Isnadi iliyokusanywa na Ahmad ikielezea Kauli ya Allah تعالى katika *Surat Al-Anbiya* (Sura ya 21).

حَتَّىٰ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ

“Mpaka watapofunguliwa Juju na Maajuju..” (21:96)

Katika zama zetu, katika mwaka 741 mnara mweupe ulijengwa katika Masjid Umayyad (Damaskas) kwa mawe, pahala pa mnara ulioteketewa na moto uliodhaniwa kuwashwa na Manasara. Laana ya Allah تعالى iendelee kuwafikia mpaka siku ya Kiyama. Kuna uwezekano mkubwa kuwa mnara huu ndio atakaoshukia Issa عليه السلام, Kwa mujibu wa Hadithi hii.

Hadithi Nyingine:

Muslim alinukuu ndani ya Sahihi yake kuwa Yaquub bin 'Asim bin Urwahdin Masudi Al-Thaqafi alisema, “Nilimsikia Abdullah bin Amri akimuambia mtu aliyemuuliza, ‘Ni hadithi gani hii unayoisimulia?, Unadai kuwa saa itanza kadha wa kadha.” Akasema, “*Subhanallah* (Ametakasika Allah تعالى). Ama alisema, “Hapana apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى.” Nilikuwa karibu nisimsimulie kitu mtu yeyote. Nilisema tu, “Karibu, mtashuhudia tukio kubwa, Nyumba (Al-Kaabah) itateketewa kwa moto, na mambo kadha wa kadha yatatokea.” Kisha akasema, “Mtume ﷺ alisema,

«يَخْرُجُ الدَّجَالُ فِي أُمَّتِي فَيَمُوتُكَتُ أَرْبَعِينَ، لَا أَذْرِي أَرْبَعِينَ يَوْمًا أَوْ أَرْبَعِينَ شَهْرًا أَوْ أَرْبَعِينَ عَامًا، فَيَبْعَثُ اللَّهُ تَعَالَى عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ كَأَنَّهُ عُرْوَةٌ بَيْنَ مَسْعُودٍ، فَيَطْلُبُهُ فَيُهْلِكُهُ، ثُمَّ يَمُوتُكَتُ النَّاسُ سَبْعَ سِنِينَ لَيْسَ بَيْنَ اثْنَيْنِ عِدَاوَةٌ، ثُمَّ يُرْسِلُ اللَّهُ رِيحًا بَارِدَةً مِنْ قِبَلِ الشَّامِ، فَلَا يَبْقَى عَلَى وَجْهِ الْأَرْضِ أَحَدٌ فِي قَلْبِهِ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ مِنْ خَيْرٍ - أَوْ إِيْمَانٍ - إِلَّا قَبَضَتْهُ، حَتَّىٰ لَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ دَخَلَ فِي كَبِدِ جَبَلٍ لَدَخَلْتَهُ عَلَيْهِ حَتَّىٰ تَقْبِضَهُ» قَالَ: سَمِعْتَهَا مِنْ رَسُولِ اللَّهِ ﷺ «فَيَقْفَى شِرَارُ النَّاسِ فِي حِفْوِ الطَّيْرِ وَأَخْلَامِ السَّبَاعِ، لَا يَعْرِفُونَ مَعْرُوفًا، وَلَا يُنْكِرُونَ مُنْكَرًا، فَيَمْتَلِ لَهُمُ الشَّيْطَانُ قَبُولًا: أَلَا تَسْتَجِيبُونَ؟ فَيَقُولُونَ: فَمَا تَأْمُرْنَا؟ فَيَأْمُرُهُمْ بِعِبَادَةِ الْأَوْثَانِ، وَهُمْ فِي ذَلِكَ دَارٌ

¹ Ahmad 4:181, Abu Dawud 4:497, Tuhfatul Ahwadhi: 6:499, An-Nasai katika Al-Kubraa 5:15 na Ibn Majah 2:1356.

رَزَقْنَاهُمْ، حَسَنَ عَيْشِهِمْ، ثُمَّ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ فَلَا يَسْمَعُهُ أَحَدٌ إِلَّا أَصْعَى لَيْتًا وَرَزَعَ لَيْتًا، قَالَ: وَأَوَّلُ مَنْ يَسْمَعُهُ رَجُلٌ يَلُوطُ حَوْضَ إِبِلِهِ، قَالَ: تَبْصَعُونَ وَيَبْصَعُونَ النَّاسُ، ثُمَّ يُرْسِلُ اللَّهُ - أَوْ قَالَ: يُنَزِّلُ اللَّهُ - مَطَرًا كَأَنَّهُ الظَّلُّ - أَوْ قَالَ الظَّلُّ - نَعْمَانُ الشَّاكُّ - فَتَنْبِتُ مِنْهُ أَجْسَادَ النَّاسِ، ثُمَّ يُنْفَخُ فِيهِ أُخْرَى فَإِذَا هُمْ قِيَامٌ يَنْظُرُونَ. ثُمَّ يُقَالُ: أَيُّهَا النَّاسُ: هَلُمُّوا إِلَى رَبِّكُمْ،

“Ad-Dajjal atatokea katika Taifa langu na atabakia kwa arobaini” (Msimuliaji hana uhakika kuwa ni siku arubaini, miezi au miaka?) Kisha, Allah Atamteremsha Issa, mwana wa Maryam anafanana na Urwah bin Mas'ud atamtafuta Ad-Dajjal na kumuua. Watu watasalia kwa miaka saba bila kuhasimiana baina yao. Allah Atapeleka upepo baridi kutoka Ash-Sham ambao hautamuacha mtu juu ya uso wa dunia hata mwenye wito wa imani sawa na atomi, bali utachukua afya yake. Hata kama mmoja wenu atakimbia katikati ya majabali, utampata na kushika (nafsi yake). Baadaye watu waovu zaidi watabaki. Watakuwa wepesi mithili ya Ndege na maumbile ya wanyama. Hawatajua au kufurahia wema au kukataza au kujua uovu. Shetani atatokea na atawaambia, “Mtanifuata!” Watasema, “Utatuamrisha nini?” Atawaamrisha kuabudu masanamu. Wakati huo, chakula chao kitakuwa kingi na maisha yao yatakuwa bora. Kisha parapanda litapulizwa na kila mtu atakayelisikia atainamisha upande mmoja wa kichwa chake na atainua wa pili (Akijaribu kusikiliza sauti ya mbali). Mtu wa kwanza atakayesikia parapanda ni mtu anayeandaa bwawa la maji kwa ajili ya Ngamia wake, naye na watu watachukuliwa. Allah Atateremsha mvua kubwa na miili ya watu itamea. Parapanda litapulizwa tena watu watafufuliwa huku wakiangalia yanayojiri. Wataambiwa, “Enyi watu! Njooi kwa Mola wenu.”

وَقَفُّوهُمْ^ط إِنَّهُمْ مَسْئُولُونَ ﴿٣٧﴾

“Na wasimamisheni. Hakika hao watasailiwa:...” (37:24)

«ثم يقال: أخرجوا بعث النار، فيقال: من كم؟ فيقال: من كل ألف تسعمائة وتسعة وتسعين، قال: فذلك يوم»

Kisha patasemwa, 'Watenganishe watu watakoingizwa motoni!' Pataulizwa, 'Kiasi gani?' Itasemwa, 'kwa kila alfu moja mia tisa na tisini na tisa.' Hiyo ndiyo siku yenyewe?'

﴿٧﴾ **يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا**

"...itawafanya watoto wadogo waote mvi?" Na,

يَوْمَ يُكْشَفُ عَنْ سَاقٍ

"Siku utakapo wekwa wazi mudi..." (68:42)¹

Wasifu wa Issa عليه السلام.

Kama tulivyotaja mwanzo, Abdur-Rahman bin Adam alisimulia kuwa Abu Huraira رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«فَإِذَا رَأَيْتُمُوهُ فَاعْرِفُوهُ: رَجُلٌ مَرْبُوعٌ إِلَى الْحُمْرَةِ وَالْبِيَاضِ، عَلَيْهِ نَوْبَانِ مُمَصَّرَانِ، كَأَنَّ رَأْسَهُ يَقَطَّرُ وَإِنْ لَمْ يُصِبْهُ بَلَلٌ»

"Mkimuona Isa, mtambueni. Ni mtu wa miraba minne, ni mwenye ngozi kati ya nyekundu na nyeupe. Atashuka huku amevalia nguo ya rangi ya njano. Kichwa chake kitaonekana kama kimeroa na maji, ljpakuwa hakuwa ameguswa na umajimaji."²

Katika Hadithi iliyosimuliwa na An-Nawwas bin Sam'aan رضى الله عنه alisema,

«فَيَنْزِلُ عِنْدَ الْمَنَارَةِ الْبَيْضَاءِ شَرْقِيٍّ دِمَشْقَ بَيْنَ مَهْرُودَتَيْنِ وَاحِصًا كَفَيْهِ عَلَى أَجْنِحَةٍ مَلَكَيْنِ، إِذَا طَاطَأَ رَأْسَهُ قَطَّرَ، وَإِذَا رَفَعَهُ تَحَدَّرَ مِنْهُ مِثْلُ جُمَانِ اللَّزْلُوكِ، لَا يَجِلُّ لِكَافِرٍ يَجِدُ رِيحَ نَفْسِهِ إِلَّا مَاتَ، وَنَفْسُهُ يَتَّبِعِي حَيْثُ يَتَّبِعِي طَرَفُهُ»

"Atashuka kwenye mnara mweupe mashariki ya Damascus. Akiwa amevaa nguo mbili za rangi zafarani isiyokoa, mikono yake ikiwa juu ya mbawa za malaika wawili, anaposhusha kichwa chake, matone yatadondoka. Hapana kafiri atakayevumilia pumzi za Issa na pumzi zake zitakwenda umbali wa upeo wa macho."³

Bukhari na Muslim walinukuu kutoka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

¹ Muslim 4:2258.

² Abu Dawud 4:498.

³ Muslim 4:3253.

«لَيْلَةَ أُسْرِي بِي لَقِيتُ مُوسَى»

“Nilikutana na Musa usiku niliophelekwa.”

Mtume ﷺ kisha alimuelezea na kusema,

«مُضْطَرَبٌ، رَجُلٌ الرَّأْسُ كَأَنَّهُ مِنْ رِجَالِ شَنْوَاءَ»

“Kama ninavyofikiri, “Alikuwa mtu mrefu, mwenye nywele kama mtu wa kabila la shanuah.”

Mtume ﷺ aliendelea kusema,

«وَلَقِيتُ عِيسَى فَنَعْتَهُ النَّبِيَّ ﷺ فَقَالَ: «رَبْعَةٌ أَحْمَرُ كَأَنَّهُ خَرَجَ مِنْ دِيمَاسٍ» يَعْنِي الْحَمَامَ، «وَرَأَيْتُ إِبْرَاهِيمَ وَأَنَا أَشْبَهُ وَلَدِهِ بِهِ»

“Nilikutana na Mtume Issa akaanza kumuelezea kwa kusema, Alikuwa mrefu wa wastani na alikuwa na uso mwekundu kama vile alikuwa ametoka kuoga. Nilimuona Ibrahim ambaye nilifanana naye kuliko watoto wake.”

Bukhari alinukuu kuwa Mujahid alisema kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«رَأَيْتُ مُوسَى وَعِيسَى وَإِبْرَاهِيمَ، فَأَمَّا عِيسَى فَأَحْمَرٌ جَعْدٌ عَرِيضُ الصَّدْرِ، وَأَمَّا مُوسَى فَأَدَمٌ جَسِيمٌ سَبَطٌ، كَأَنَّهُ مِنْ رِجَالِ الرُّطِّ»

“Nilimuona Musa, Issa na Ibrahim, ama Issa ni mwekundu, umbo lake sio pana sana. Ama Mussa ni Hudhurungi, alikuwa na nywele zilizonyooka na refu kama watu wa Az-Zuti (wenye miili mikubwa).”²

Imamu Bukhari na Imamu Muslim walinukuu kuwa Naafi alisema, kuwa Abdullah bin Umar رضي الله عنهما alisema, “Mtume ﷺ mara moja alimtaja Masihi Ad-Dajjal kwa watu na akasema,

«إِنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِأَعْوَرَ، أَلَا إِنَّ الْمَسِيحَ الدَّجَالَ أَعْوَرُ الْعَيْنِ الْيُمْنَى، كَانَ عَيْنُهُ عَيْبَةً طَائِفَةً»

¹ Fat'hul Bari 6:493 na Muslim 1:154.

² Fat'hul Bari 6:549.

*"Allah Hana sifa ya upofu lakini Masihi Ad-Dajjal amepofuka jicho la kulia. Jicho lake ni kama tufaa lililojitokeza."*¹

Muslim alinukuu kuwa Mtume ﷺ alisema,

«وَأَرَانِي اللَّهَ عِنْدَ الْكَعْبَةِ فِي الْمَنَامِ، فَإِذَا رَجُلٌ آدَمُ كَأَحْسَنِ مَا تَرَى مِنْ آدَمِ الرَّجَالِ، تَضْرِبُ لِمَتُهُ بَيْنَ مَتَكَيْبِهِ، رَجُلٌ الشَّعْرِ، يَقَطُرُ رَأْسُهُ مَاءً، وَاضِعًا يَدَيْهِ عَلَى مَتَكَيْبِي رَجُلَيْنِ، وَهُوَ يَطُوفُ بِالْبَيْتِ، فَقُلْتُ: مَنْ هَذَا؟ فَقَالُوا: هُوَ الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ، ثُمَّ رَأَيْتُ وَرَاءَهُ رَجُلًا جَعْدًا قَطِطًا، أُغْوَرَ الْعَيْنِ الْيُمْنَى، كَأَشْبَهَ مَنْ رَأَيْتُ بِابْنِ قَطَنِ، وَاضِعًا يَدَيْهِ عَلَى مَتَكَيْبِي رَجُلٍ، يَطُوفُ بِالْبَيْتِ، فَقُلْتُ: مَنْ هَذَا؟ قَالُوا: الْمَسِيحُ الدَّجَالُ،

*"Allah Aliniwezesha kumuona mtu anayeng'aa mwenye rangi nzuri mithili ya mwanga, mtu huyo mwenye rangi, alikuwa na nywele zilizochanwa zimeangukia mabega yake. Nywele zake zilivuja maji na alikuwa amewaegemea watu wawili mabegani wakati akizunguka Kaaba. Nikauliza ni nani mtu huyo? Nikaelezwa, huyo ni Masihi mwana wa Maryam. Nyuma yake nilimuona mwenye nywele zilizokunjana aliyekuwa amepofuka jicho la kulia. Alikuwa anamshabihi bin Qatan, na alikuwa ameegemea bega la mtu huku akiizunguka Nyumba. Nikauliza ni nani mtu huyo? Nikaelezwa, huyo ni Masihi Ad-Dajjal."*²

Al-Bukhari alinukuu kuwa Salim alisema, baba yake alisema, hapana Wallah! Mtume ﷺ hakusema kuwa Issa عليه السلام alikuwa na wajihhi mwekundu bali alisema,

«بَيْنَمَا أَنَا نَائِمٌ أَطُوفُ بِالْكَعْبَةِ، فَإِذَا رَجُلٌ آدَمُ سَبَطَ الشَّعْرَ، يَتَهَادَى بَيْنَ رَجُلَيْنِ، يَنْظِفُ رَأْسَهُ مَاءً - أَوْ يَهْرَأَى رَأْسَهُ مَاءً - فَقُلْتُ: مَنْ هَذَا؟ فَقَالُوا: ابْنُ مَرْيَمَ، فَذَهَبَتْ أَلْتَصْتُ، فَإِذَا رَجُلٌ أَحْمَرُ جَسِيمٌ، جَعْدُ الرَّأْسِ، أُغْوَرَ عَيْنَيْهِ الْيُمْنَى، كَأَنَّ عَيْنَهُ عَيْبَةٌ طَافِيَةٌ، قُلْتُ: مَنْ هَذَا؟ قَالُوا: الدَّجَالُ، وَأَقْرَبُ النَّاسِ بِهَ سَبَبًا ابْنُ قَطَنِ»

"Wakati nikiwa usingizini nikitufu Kaabah (ndotoni) ghafla nilimuona mtu mwenye rangi ya hudhurungi na mwenye nywele nyingi akitembea kati ya wanaume wawili na maji yakichuruzika. Yakidondoka kutoka kichwani mwake. Nikauliza, 'huyu ni nani?' Watu

¹ Muslim 4:2248.

² Muslim 1:154.

wakajibu, "huyu ni mwana wa Maryam" kisha niliangalia nyuma na kumuona mtu mwekundu, mnene mwenye nywele zilizojisokota, amepofuka jicho la kulia, ambalo kama tufaa lililojitokeza, "Nikauliza, huyu ni nani?" Wakajibu, "huyu ni Ad-Dajjali anamshabihi sana Ibn Qatan."

Az-Zuhri alielezea kuwa Ibn Qatan alikuwa mtu wa kabila la Khuzah ambaye alifariki dunia enzi za Jahiliyyah.¹ Haya ni maneno ya Bukhari. Kauli ya Allah

تعالى،

وَيَوْمَ الْقِيَامَةِ يَكُونُ عَلَيْهِمْ شَهِدًا ﴿١٥٦﴾

"...Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao."

Qatadah alisema, "Atashuhudia mbele yao kuwa alifikisha Ujumbe kutoka kwa Allah تعالى na kuwa si vinginevyo bali yeye ni mja wake." Katika kauli nyingine sawa na hiyo mwishoni mwa Surat Al-Maidah,

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يٰعِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ ءَأَنْتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ

"Na pale Mwenyezi Mungu Atakapo sema: Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu..." (5:116)

Mpaka،

الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ ﴿١٥٧﴾

"Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima."

فَيُظَلِّمِ مِنَ الَّذِينَ هَادُوا حَرَمَنَا عَلَيْهِمْ طَبَّيْتِ أَجَلْتِ هُمْ وَبَصَدِهِمْ عَنِ سَبِيلِ اللَّهِ كَثِيرًا ﴿١٥٨﴾ وَأَخَذِهِمُ الرِّبَا وَقَدْ هُمُوا عَنْهُ وَأَكَلِهِمْ أَمْوَالَ النَّاسِ بِالْبَاطِلِ ؕ وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٥٩﴾ لَيْكِنَ الرِّسْخُونَ فِي الْعِلْمِ مِنْهُمْ وَالْمُؤْمِنُونَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ ؕ وَالْمُقِيمِينَ الصَّلَاةَ ؕ وَالْمُؤْتُونَ الزَّكَاةَ وَالْمُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ
الْآخِرِ أُولَئِكَ سَنُؤْتِيهِمْ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٦٠﴾

160. Basi kwa dhulma yao Mayahudi Tuliwaharimishia vitu vizuri walivyohalalishiwa. Na kwa sababu ya kuwazuilia kwao watu wengi na njia ya Mwenyezi Mungu،

161. Na kuchukua kwao riba، nao wamekatazwa، na kula kwao

mali ya watu kwa dhulma. Basi Tumewaandalia makafiri katika wao adhabu yenye uchungu.

162. Lakini waliobobea katika ilimu miongoni mwao, na Waumini, wanayaamini uliyoteremshiwa wewe, na yaliyoteremshwa kabla yako. Na wanaoshika Sala, na wakatoa Zaka, na wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho - hao Tutawapa malipo makubwa.

Mayahudi Waliharamishiwa Baadhi ya Vyakula Kutokana na Kutokuwa Waadilifu na Kutenda Maovu.

Allah تعالی Anaeleza kuwa sababu ya kuchupa mipaka, na kufanya makosa makubwa, Allah تعالی Aliwaharamishia Mayahudi baadhi ya mambo ya halali na mazuri ambayo kabla ya hapo yalikuwa halali kwao. Kuharamishwa huku inawezekana kwa sharia, ikiwa na maana kuwa mayahudi walipotosha tafsiri ya kitabu chao na kugeuza taarifa juu ya yale waliyohalalishwa, hivyo kutokana na kuzidisha mambo na kufanya zaidi katika dini. Walijiharamishia baadhi ya vitu. Pia inaweza kuwa na maana kuwa ndani ya Taurati, Allah تعالی Aliwaharamishia baadhi ya vitu ambavyo vilikuwa halali kabla.

﴿ كُلُّ الطَّعَامِ كَانَ حَلَالًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ إِلَّا مَا حَرَّمَ إِسْرَائِيلُ عَلَىٰ نَفْسِهِ مِن قَبْلِ أَنْ تُنزَلَ التَّوْرَةُ ﴾

“Kila chakula kilikuwa halali kwa Wana wa Israili isipokuwa alichu jizuilia Israili mwenyewe kabla haijateremshwa Taurati.” (3:93)

Tuliitaja aya hii kabla, ambayo ina maana kuwa wana wa Israil walihalalishiwa vyakula vyote kabla ya kuteremshwa kwa Taurati, isipokuwa nyama ya ngamia na maziwa ambayo Waisrail walijiharamishia wenyewe. Baadaye Allah تعالی Aliharamisha vitu vingi ndani ya Taurat. Allah تعالی Amesema ndani ya Surat Al-An'am (Surat ya 6),

وَعَلَى الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا كُلَّ ذِي ظُفْرٍ مِّنَ الْبَقَرِ وَالْغَنَمِ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ شُحُومَهُمَا إِلَّا مَا حَمَلَتْ ظُهُورُهُمَا أَوْ الْحَوَايَا أَوْ مَا اخْتَلَطَ بِعَظْمٍ ذَٰلِكَ جَزَيْنَاهُم بِبَغْيِهِمْ وَإِنَّا لَصَدِيقُونَ ﴿٦١﴾

“Na wale walio fuata dini ya Kiyahudi Tumewaharimishia kila mwenye kucha. Na katika ng’ombe na kondoo na mbuzi Tumewaharimishia shahamu yao, isipo kuwa ile iliyobeba migongo yao au matumbo yao, au iliyogandamana na mifupa. Tuliwalipa hivyo kwa sababu ya uasi wao. Na bila ya shaka Sisi ndio wasema kweli.” (6:146)

Ina maana: Tuliwaharamishia vitu hivyo kwa sababu walistahili kutokana na kuchupa mipaka, udhalimu na kumkiuka Mtume wao na kubishana naye. Hivyo Allah تعالى Amesema,

فَيُظْلَمُ مِنْ الَّذِينَ هَادُوا حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ طَيِّبَاتٍ أُحِلَّتْ لَهُمْ وَبِصَدِّهِمْ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ كَثِيرًا ﴿١٤٦﴾

“Basi kwa dhulma yao Mayahudi Tuliwaharimishia vitu vizuri walivyohalalishiwa. Na kwa sababu ya kuwazuilia kwao watu wengi na njia ya Mwenyezi Mungu.”

Aya hii inaeleza kuwa walijizuia wenyewe na wengine kutofuata ukweli, na hiyo ndio tabia waliyodumu nayo toka zamani hadi sasa. Kwa sababu hii walikuwa bado ni maadui wa Mitume huku wakiwauwa Mitume wengi. Pia waliwakana Muhammad ﷺ na Issa عليه السلام, Allah تعالى Amesema,

وَأَخَذِهِمُ الرِّبَا وَقَدْ نُهُوا عَنْهُ

“Na kuchukua kwao riba, nao wamekatazwa.”

Allah تعالى Aliwaharamishia kula Riba hata hivyo walifanya wakitumia hila na mizunguko, hivyo kuwapoka watu mali zao kwa dhuluma. Allah تعالى Amesema,

وَأَعْتَدْنَا لِلْكَافِرِينَ مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٤٧﴾

“Basi Tumewaandalia makafiri katika wao adhabu yenye uchungu.”

Kisha Allah تعالى Amesema,

لَيْكِنِ الرَّاسِخُونَ فِي الْعِلْمِ مِنْهُمْ

“Lakini walioboba katika ilimu miongoni mwao.”

Wameshikana na dini na wenye ilimu inayonufaisha. Tulitaja mada hii tulipokuwa tukifasiri Surah Al-Imran (3).

وَالْمُؤْمِنُونَ

“...na Waumini...”

Inahusu waliobobea katika ilimu,

وَالَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِنْ قَبْلِكَ وَبِالْآخِرَةِ هُمْ يُوقِنُونَ ﴿٤٥﴾

“Na ambao wanayaamini yaliyoteremshwa kwako, na yaliyo teremshwa kabla yako; na Akhera wana yakini nayo.” (2:4)

Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema, Aya hii ilishushwa kwa mintaarafu ya Abdullah bin Salam, Tha'labah bin Sa'yah, Zayd bin Sa'yah na Asad bin Ubayd ambao walisilimu na waliaamini aliyokuja nayo Muhammad ﷺ kutoka kwa Allah تعالى.

Allah تعالى Amesema,

وَالْمُؤْتُونَ الزَّكَاةَ

“Na wakatoa Zaka.”

Hii itakuwa inahusu sadaka iliyofaradhishwa juu ya mali ya mtu, au wale wanaojitakasa wenyewe au maana zote. Allah تعالى Ndiye Mjuzi wa yote.

وَالْمُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ

“Na wanaomuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho.”

Wanaamini kuwa hapana mola apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah تعالى, kuamini kufufuliwa baada ya kifo na malipo au adhabu kwa mema au maovu.

Kauli ya Allah تعالى,

أُولَئِكَ

“...hao..” Watu ambao wameelezewa na Aya hapo juu,

سَنُؤْتِيهِمْ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٦﴾

“... Tutawapa malipo makubwa...” Maana yake: Pepo.

* * *

* إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَأَوْحَيْنَا إِلَى إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَعِيسَىٰ وَأَيُّوبَ وَيُونُسَ وَهَارُونَ وَسُلَيْمَانَ ۗ وَآتَيْنَا دَاوُدَ زَبُورًا ﴿١٦٣﴾ وَرُسُلًا قَدْ قَصَصْنَاهُمْ عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ وَرُسُلًا لَمْ نَقْصُصْهُمْ عَلَيْكَ ۗ وَكَلَّمَ اللَّهُ مُوسَىٰ تَكْلِيمًا ﴿١٦٤﴾ رُسُلًا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيمًا حَكِيمًا ﴿١٦٥﴾ لَيْسَ لَكَ مِنَ الْأَمْرِ شَيْءٌ سَأَلْنَاهُ عَنِ السَّيْلِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا غَدِيرًا ﴿١٦٦﴾ وَإِنِ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ قَدْ ضَلُّوا ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿١٦٧﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَظَلَمُوا لَمْ يَكُنِ اللَّهُ لِيَغْفِرَ لَهُمْ وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ طَرِيقًا ﴿١٦٨﴾ إِلَّا طَرِيقَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ وَكَانَ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿١٦٩﴾ يَتَأْتِيهِمُ النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمُ الرُّسُولُ بِالْحَقِّ مِنْ رَبِّكُمْ فَآمَنُوا خَيْرًا لَكُمْ ۗ وَإِن تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٧٠﴾

* إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ ۗ وَأَوْحَيْنَا إِلَى إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَالْأَسْبَاطِ وَعِيسَىٰ وَأَيُّوبَ وَيُونُسَ وَهَارُونَ وَسُلَيْمَانَ ۗ وَآتَيْنَا دَاوُدَ زَبُورًا ﴿١٦٣﴾ وَرُسُلًا قَدْ قَصَصْنَاهُمْ عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ وَرُسُلًا لَمْ نَقْصُصْهُمْ عَلَيْكَ ۗ وَكَلَّمَ اللَّهُ مُوسَىٰ تَكْلِيمًا ﴿١٦٤﴾ رُسُلًا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيمًا حَكِيمًا ﴿١٦٥﴾

163. Hakika Sisi Tumekuletea wahyi wewe kama Tulivyowapelekea wahyi Nuhu na Manabii walio-kuwa baada yake. Na

Tulimpelekea wahyi Ibrahim na Ismail na Is-haka na Yaakub na wajukuu zake, na Isa na Ayub na Yunus na Harun na Suleiman, na Daud Tukampa Zaburi.

164. Na Mitume Tuliokwisha kukuhadithia kabla yake, na Mitume wengine hatukukuhadithia. Na Mwenyezi Mungu Alinena na Musa kwa maneno.

165. Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.

Wahyi Ulikuwa kwa Mtume Muhammad ﷺ, Kama Ulivyokuja kwa Mitume Kabla Yake.

Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Muhammad bin Abi Muhammad, alisema kuwa Ikrimah, au Said bin Jubayr, kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما kuwa alisema, "Sukayn na 'Adi bin Zayd walisema, "Ewe Muhammad! Hatufahamu kuwa Allah تعالى Aliteremsha chochote kwa mtu yeyote baada ya Musa عليه السلام." Allah تعالى Aliteremsha majibu dhidi ya kauli yao.

﴿ إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ ﴾

"Hakika Sisi Tumekuletea wahyi wewe kama Tulivyowapelekea wahyi Nuhu na Manabii waliokuwa baada yake."

Allah تعالى Anaeleza kuwa Aliteremsha wahyi kwa waja Wake na Mjumbe Muhammad ﷺ kama alivyoteremsha wahyi kwa Mitume waliotangulia. Allah تعالى Amesema,

﴿ إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ كَمَا أَوْحَيْنَا إِلَى نُوحٍ وَالنَّبِيِّينَ مِنْ بَعْدِهِ ﴾

"Hakika Sisi Tumekuletea wahyi wewe kama Tulivyowapelekea wahyi Nuhu na Manabii walio kuwa baada yake."

Mpaka,

﴿ وَآتَيْنَا دَاوُدَ زَبُورًا ﴾

"...na Daud Tukampa Zaburi."

Zaburi ni jina la Kitabu kilichoteremshwa kwa Mtume Dawud عليه السلام.

Mitume Ishirini na Watano Wametajwa Ndani ya Qur'an

﴿ وَرُسُلًا قَدْ قَصَصْنَاهُمْ عَلَيْكَ مِنْ قَبْلُ وَرُسُلًا لَمْ نَقْصُصْهُمْ عَلَيْكَ ﴾

"Na Mitume Tuliokwisha Kukuhadithia kabla yake, na Mitume wengine hatukukuhadithia."

Kabla ya kushushwa kwa aya hii. Yafuatayo ni majina ya Mitume ambao Allah تعالى Amewataja ndani ya Qur'an. Wao ni:- Adam, Idris, Nuh, Hud, Salih, Ibrahim, Lut, Ismail, Is'haq, Yaqub, Yusuf, Ayyub, Shu'ayb, Musa, Harun, Yunus, Dawud,

¹ At - Tabari 9:400.

Sulayman, Ilyasa, Al-Yasa, Zakariya, Yahya, na Isa - Amani ya Mwenyezi Mungu ziwe juu yao na kiongozi wao Muhammad ﷺ. Wanazuoni mbalimbali wa Tafsiri pia walimuorodhesha Dhul-Kifl عليه السلام miongoni mwa Mitume.

Kauli ya Allah تعالى،

وَرُسُلًا لَّمْ نَقْضُصُهُمْ عَلَيْكَ

“Mitume wengine hatukukuhadithia.”

Maana yake: Kuna Mitume wengine ambao hawakutajwa ndani ya Qur'an.

Utukufu wa Musa عليه السلام

Allah تعالى Amesema،

وَكَلَّمَ اللَّهُ مُوسَى تَكْلِيمًا

“Na Musa alinena na Mwenyezi Mungu kwa maneno.”

Hii ni heshima kwa Musa عليه السلام na kwa sababu hii aliitwa *Kalim*, ambaye Allah تعالى Alizungumza naye moja kwa moja. Al-Hafiz Abubakar bin Marduwayh رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Abdul-Jabbar bin Abdillah alisema, “Mtu mmoja alikuja kwa Abubakar bin Ayyash na alisema, “Nilimsikia Mtu akisoma (aya hii kwa njia hii), kwamba Musa عليه السلام ndiye aliyemsemesha Mwenyezi Mungu kwa kuweka irabu ya *Fat'ha* katika neno Allah تعالى.

“Wakallama LLaha Musa Taktima.”

“Na Musa alimsemesha Mwenyezi Mungu kwa Maneno.”

Abubakar bin Abi Ayyash alimkasirikia sana mtu yule aliyesoma aya tofauti, na akasema, “Hasomi mtu usomaji wa namna hii isipokuwa mtu huyo ni kafiri.” Mimi nilisoma kwa Al-A'mash, naye alisoma kwa Yahya bin Wathaab na Yahya akasoma kwa Abi Abdur-Rahman, naye alisoma kwa Ali bin Abi Talib رضي الله عنه، naye Ali رضي الله عنه alisoma kwa Mtume ﷺ،

وَكَلَّمَ اللَّهُ مُوسَى تَكْلِيمًا

“Na Mwenyezi Mungu Alinena na Musa kwa maneno.”¹

Abubakar bin Abi Ayyash alizidisha hasira kwa mtu yule kwa sababu alibadilisha maneno na maana،

¹ At - Tabari katika kitabu chake Al-Awsat 3325.

وَكَلَّمَ اللَّهُ مُوسَى تَكْوِيمًا ﴿١٦٣﴾

“Na Mwenyezi Mungu Alinena na Musa kwa maneno.”¹

(katika aya hiyo ndani ya Qur'an - Jina la Allah تعالى linaishia na *dhwamma* mwisho na huyo msomaji alisoma kwa *fat-ha* mwisho).

Mtu huyo alikuwa *Mu'tazilah* ambao walikanusha kuwa Allah تعالى Alizungumza na Musa عليه السلام na wanakanusha kuwa Alizungumza na kiumbe wake yeyote. Tulielezwa kuwa baadhi ya *Mu'tazilah* wakati mmoja walisoma aya kwa mtindo ule, hivyo mwalimu mmoja aliyekuwepo alimuambia, “Ewe mtoto wa mwanamke unayenuka! utafanya nini kuhusiana na Kauli ya Allah تعالى,

وَلَمَّا جَاءَ مُوسَى لِمِيقَاتِنَا وَكَلَّمَهُ رَبُّهُ

“Na alipokuja Musa kwenye miadi Yetu, na Mola wake Mlezi akamsemeza.”

Sheikh alikuwa na maana, aya iliyotangulia haiwezi kubadilishwa.

Sababu za Kupelekwa Mtume ﷺ ni Kusimamisha Hoja.

Allah تعالى Amesema,

رُسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ

“Mitume hao ni wabashiri na waonyaji.”

Maana yake: Mtume ﷺ huleta habari njema kwa wale wanaomtii Allah تعالى. Na wanafanya amali njema zinazomridhisha Yeye. Pia wanaonya juu ya adhabu Yake na Mateso kwa wale wanaovunja Maamrisho Yake. Baadae Allah تعالى Amesema,

لَعَلَّ يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٦٤﴾

“...ili watu wasiwe na hoja juu ya Mwenyezi Mungu baada ya kuletewa Mitume. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hikima.”

Allah تعالى Aliteremsha Vitabu Vyake na Akawatuma Mitume Wake na bishara njema na maonyo. Akaelezea Asiyoyataka na Ayaridhiayo na Ayachukiayo na Asiyoyapenda na kutoyaridhia. Kwa njia hii hapa hamna atakayekuwa na udhuru kwa Allah تعالى. Allah تعالى Amesema katika aya nyingine,

وَلَوْ أَنَّا أَهْلَكْنَاهُمْ بِعَذَابٍ مِّن قَبْلِهِ لَقَالُوا رَبَّنَا لَوْلَا أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا فَنَتَّبِعَ آيَاتِكَ
مِن قَبْلِ أَنْ نَذِلَّ وَنَخْزَىٰ ﴿١٦٣﴾

“Na lau kuwa Tuliwaangamiza kwa adhabu kabla yake, wangeli sema: Ewe Mola wetu Mlezi! Kwa nini Usituletee Mtume tukazi-fuata ishara zako kabla hatujadhalilika na kuhizika.” (20:134)

Kadhalika Kauli Yake,

وَلَوْلَا أَنْ تُصِيبَهُمْ مُّصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ أَيْدِيهِمْ

“Na usije kuwasibu msiba kwa iliyoyatanguliza mikono yao.” (28:47)

Amenukuu katika sahihi mbili kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنهما alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا أَحَدٌ أَغْيَرُ مِنَ اللَّهِ، مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ حَرَّمَ الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَّنَ، وَلَا أَحَدٌ أَحَبُّ إِلَيْهِ الْمَذْحُجُ مِنَ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ، مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ مَدَحَ نَفْسَهُ، وَلَا أَحَدٌ أَحَبُّ إِلَيْهِ الْعُدْرُ مِنَ اللَّهِ، مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ بَعَثَ النَّبِيِّنَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ»

“Hapana mtu yeyote aliye na wivu zaidi ya Allah kwa sababu hiyo Aliharamisha maovu yote kufanywa dhahiri au kwa siri: Hapana apendaye kutukuzwa zaidi ya Allah, na kwa sababu hii Amejitukuza Mwenyewe. Hapana apendaye kutoa udhuru zaidi ya Allah, na kwa sababu hiyo Alituma Mitume kuwa wabashiri wa wema na waonyaji.”

Katika mapokezi mengine, Mtume ﷺ alisema,

«مِنْ أَجْلِ ذَلِكَ أَرْسَلَ رَسُولَهُ وَأَنْزَلَ كُتُبَهُ»

“Kwa sababu hiyo Alipeleka Mitume Wake na Akateremsha vitabu Vyake.”¹

¹ Fat-hul Bari 8:146 na Muslim 4:2114.

لَكِنَّ اللَّهَ يَشْهَدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ أَنْزَلَهُ بِعِلْمِهِ ۗ وَالْمَلٰٓئِكَةُ يَشْهَدُونَ ۗ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا
 ﴿١٦٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ قَدْ ضَلُّوا ضَلٰٓلًا بَعِيدًا ﴿١٦٧﴾ إِنَّ الَّذِينَ
 كَفَرُوا وَظَلَمُوا لَمْ يَكُنِ اللَّهُ لِيَغْفِرَ لَهُمْ وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ طَرِيقًا ﴿١٦٨﴾ إِلَّا طَرِيقَ جَهَنَّمَ
 خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۗ وَكَانَ ذٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿١٦٩﴾ يَتَأَيُّبُ النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمُ الرَّسُولُ
 بِالْحَقِّ مِن رَّبِّكُمْ فَآمِنُوا خَيْرًا لَّكُمْ ۗ وَإِن تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَكَانَ
 اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٧٠﴾

166. Lakini Mwenyezi Mungu Anayashuhudia Aliyokuteremshia wewe. Ameyateremsha kwa Kujua Kwake na Malaika pia wanashuhudia. Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Shahidi.

167. Hakika waliokufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, wamekwisha potelea mbali.

168. Hakika wale waliokufuru na wakadhulumu hawi Mwenyezi Mungu wa Kuwasamehe wala Kuwaongoa njia.

169. Isipo kuwa njia ya Jahannamu. Humo watadumu milele. Na hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.

170. Enyi Watu! Amekwishakujieni Mtume huyu na haki itokayo kwa Mola wenu Mlezi. Basi aminini, ndiyo kheri yenu. Na mkikakanusha basi hakika viliomo mbinguni na duniani ni vya Mwenyezi Mungu tu. Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye Hikima.

Kauli ya Allah تعالى،

﴿ إِنَّا أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ ﴾

“Hakika Sisi Tumekuletea wahyi wewe.”

Inathibitisha utume wake na majibu kwa wanaokana utume wake miongoni mwa washirikina na watu wa kitabu.

Allah تعالى Amesema,

لَكِنَّ اللَّهَ يَشْهَدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ

“Lakini Mwenyezi Mungu Anayashuhudia Aliyokuteremshia wewe.”

Maana yake: Hata kama watakanusha, kukengeuka na kutokuamini, Ewe Muhammad ﷺ, Allah تعالى Amethibitisha ya kuwa wewe ni Mjumbe Wake ambaye Alikuteremshia Kitabu Chake, Qur'an Takatifu.

وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِّنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ

“...wala wao hawajui chochote katika vilio katika Ujuzi Wake, ila kwa Atakalo Mwenyewe.” (2:255)

Kwa hiyo Allah تعالى Akasema,

أَنْزَلَهُ بِعِلْمِهِ

“Ameyateremsha kwa Kujua Kwake.”

Kwa Kujua Kwake Aliwawezesha waja Wake kuipata elimu, kujua dalili zilizo wazi na ukweli, kila Anachokipenda Allah تعالى na Kukiridhia Anachokichukia na Kutokiridhia, na Kujua visivyoonekana kama yaliyopita na yajayo. Hii ni pamoja na kujua Sifa Zake adhimu ambazo hapana Mtume au Malaika awezaye kuzijua bila Idhini ya Allah تعالى. Vivyo hivyo Allah تعالى Amesema,

وَلَا يُحِيطُونَ بِهِ عِلْمًا

“Wala wao hawawezi kumjua Yeye vilivyo.” (20:110)

Kauli ya Allah تعالى,

وَأَلْمَلْتِكُمْ يَشْهَدُونَ

“.. na Malaika pia wanashuhudia.”

Kwa ukweli wa uliokuja nayo na yale uliyoteremshiwa, pamoja na ushahidi wa Allah تعالى juu ya hayo.

Kauli ya Allah تعالى,

وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا

“...Na Mwenyezi Mungu Anatosha kuwa Shahidi.”

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ قَدْ ضَلُّوا ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿١٦٧﴾

“Hakika waliokufuru na wakazuilia njia ya Mwenyezi Mungu, wamekwisha potelea mbali.”

Kwa kuwa wao wenyewe ni makafiri hawafuati ukweli wanajitahidi kuwazuia watu kufuata na kuingia katika Dini ya Allah تعالى kwa hiyo wamekanusha ukweli, wamekengeuka na wamekuwa mbali na haki.

Aidha Allah تعالى Ametaja Hukumu Yake dhidi ya wale wanaokanusha aya Zake, Kitabu na Mtume Wake wale wanaojikosea wenyewe kwa kutosadiki na kuwazuia wengine katika njia ya Mwenyezi Mungu, walifanya dhambi na wakakiuka Makatazo Yake, Allah تعالى Ameeleza kuwa Hatowasamehe kabisa,

وَلَا يَهْدِيهِمْ طَرِيقًا ﴿١٦٨﴾

“...wala kuwaongoa njia.” Maana yake: Njia ya kheri,

إِلَّا طَرِيقَ جَهَنَّمَ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا

“...Isipokuwa njia ya Jahannamu. Humo watadumu milele.”

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ قَدْ جَاءُكُمْ الرَّسُولُ بِالْحَقِّ مِنْ رَبِّكُمْ فَآمَنُوا خَيْرًا لَكُمْ

“Enyi Watu! Amekwishakujieni Mtume huyu na haki itokayo kwa Mola wenu Mlezi. Basi aminini, ndiyo kheri yenu.”

Aya hii ina maana, Muhammad ﷺ amewajia na muongozo, Dini ya ukweli na dalili iliyo wazi kutoka kwa Allah تعالى; kwa hiyo, muamini aliyowaleteeni na mumfuate, kwani hii ni bora kwenu.

Kisha Allah تعالى Amesema katika aya nyingine,

وَإِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

“....Na mkikakanusha basi hakika viliomo mbinguni na duniani ni vya Mwenyezi Mungu tu...”

Maana yake: Yeye ni mkwasi, kama Alivyosema,

وَقَالَ مُوسَىٰ إِنَّ تَكْفُرُوا أَنْتُمْ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا فَأِنَّ اللَّهَ لَغَنِيٌّ حَمِيدٌ ﴿١٦٣﴾

“Na Musa alisema: Mkikufuru nyinyi na wote waliomo duniani, hakika Mwenyezi Mungu ni Mkwasi, Anajitoshwa, Msifiwa.” (14:8)

Katika aya ya kabla yake Kauli ya Allah تعالى،

وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٦٤﴾

“Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye Hekima.”

Maana yake: Kwa anayestahiki hidaya kwenu nyinyi basi Atampa. Ama Yule anayestahiki kupotoshwa basi Atamuacha vivyo hivyo.

حَكِيمًا ﴿١٦٥﴾

“Mwenye Hikima.”

Katika Kauli Zake, Ayafanyayo na katika Hukumu Zake zote,

* * *

يَتَأَهَّلَ الْكِتَابَ لَا تَعْلَمُوا فِي دِينِكُمْ وَلَا تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ
 إِلَّا الْحَقَّ ۚ إِنَّمَا الْمَسِيحُ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ رَسُولُ اللَّهِ
 وَكَلِمَتُهُ أَلْقِنَاهَا إِلَى مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِنْهُ ۖ فَآمَنُوا بِاللَّهِ
 وَرُسُلِهِ ۗ وَلَا تَقُولُوا ثَلَاثَةٌ ۚ انْتَهُوا خَيْرًا لَكُمْ ۚ إِنَّمَا اللَّهُ
 إِلَهٌُ وَاحِدٌ ۗ سُبْحَانَهُ أَنْ يَكُونَ لَهُ وَلَدٌ ۗ لَهُ مَا فِي
 السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَكَفَى بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿١٧١﴾ لَنْ
 يَسْتَنْكِفَ الْمَسِيحُ أَنْ يَكُونَ عَبْدًا لِلَّهِ وَلَا الْمَلَائِكَةُ
 الْمُقَرَّبُونَ ۗ وَمَنْ يَسْتَنْكِفْ عَنْ عِبَادَتِهِ وَيَسْتَكْبِرْ
 فَسَيَحْشُرُهُمْ إِلَيْهِ جَمِيعًا ﴿١٧٢﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا
 وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُوَفِّيهِمْ أُجُورَهُمْ وَيَزِيدُهُمْ مِنْ
 فَضْلِهِ ۗ وَأَمَّا الَّذِينَ اسْتَنكَفُوا وَاسْتَكْبَرُوا فَيُعَذِّبُهُمْ
 عَذَابًا أَلِيمًا وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا
 ﴿١٧٣﴾ يَتَأَيُّبُ النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ بُرْهَانٌ مِنْ رَبِّكُمْ وَأَنْزَلْنَا
 إِلَيْكُمْ نُورًا مُبِينًا ﴿١٧٤﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ
 وَأَعْتَصَمُوا بِهِ فَيَسْجُدْ لِحُجَّتِهِمْ فِي رَحْمَةِ رَبِّهِمْ وَفَضْلِ تَحِيَّتِهِمْ
 إِلَيْهِ صِرَاطًا مُسْتَقِيمًا ﴿١٧٥﴾ يَسْتَفْتُونَكَ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ
 فِي الْكَلْبَلَةِ ۚ إِنْ أَمَرُوا هَلْكَ لَيْسَ لَهُ وَلَدٌ ۗ وَلَمْ أُخْتٌ فَلَهَا
 يَصِفُ مَا تَرَكَ ۗ وَهُوَ بِرِثَتِهَا إِنْ لَمْ يَكُنْ هَا وَوَلَدٌ ۚ فَإِنْ كَانَتْ
 أَنْثَىٰ فَلَهُمَا الْوَالِدَانِ مِمَّا تَرَكَ ۚ وَإِنْ كَانُوا إِخْوَةً رِجَالًا
 وَنِسَاءً فَلِلَّذَكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثَىٰ ۗ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ أَنْ
 تَضِلُّوا ۗ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٧٦﴾

يَتَأَهَّلَ الْكِتَابَ لَا تَعْلَمُوا فِي
 دِينِكُمْ وَلَا تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا
 الْحَقَّ ۚ إِنَّمَا الْمَسِيحُ عِيسَى ابْنُ
 مَرْيَمَ رَسُولُ اللَّهِ وَكَلِمَتُهُ
 أَلْقِنَاهَا إِلَى مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِنْهُ
 فَآمَنُوا بِاللَّهِ وَرُسُلِهِ ۗ وَلَا
 تَقُولُوا ثَلَاثَةٌ ۚ انْتَهُوا خَيْرًا
 لَكُمْ ۚ إِنَّمَا اللَّهُ إِلَهٌُ
 وَاحِدٌ ۗ سُبْحَانَهُ أَنْ يَكُونَ لَهُ
 وَلَدٌ ۗ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا
 فِي الْأَرْضِ ۗ وَكَفَى بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿١٧١﴾

171. "Enyi Watu wa Kitabu!
 msivuke mipaka katika dini
 yenu, wala msimseme
 Mwenyezi Mungu ila kwa
 lilio kweli. Hakika Masihi
 Isa mwana wa Maryamu ni
 Mtume wa Mwenyezi
 Mungu, na neno lake tu
 Alilompelekea Maryamu,
 na ni roho iliyotoka Kwake.
 Basi Muaminini Mwenyezi
 Mungu na Mitume Wake.
 Wala msiseme: Utatu.
 Komeni! Itakuwa kheri
 kwenu. Hakika Mwenyezi
 Mungu ni Mungu Mmoja tu.
 Ametukuka Yeye na kuwa
 na mwana. Ni Vyake Yeye
 vyote viliomo katika
 mbingu na katika ardhi. Na
 Mwenyezi Mungu ni
 Mtegemewa wa kutosha."

Kukatazwa kwa Watu wa Kitabu Kufanya Ghulu'u Katika Dini na Kumpa Sifa Asizokuwa Nazo Isa Mwana wa Maryam عليه السلام.

Watu wa kitabu (*Ahlul-Kitaab*) waliharamishiwa kufanya *ghuluu* katika Dini (kuzidisha ziada isiyotakiwa). Allah تعالى Aliwakataza watu wa kitabu kuchupa mipaka katika Dini ambayo ni kawaida yao hususani miongoni mwa wakristo ambao walitia chumvi kuhusu Isa عليه السلام na sifa zake mpaka walimpandisha juu ya daraja alilopewa na Allah تعالى. Walimbadilishia daraja lake kutoka darala la utume kuwa Mungu ambaye walimuabudu kama walivyomuabudu Allah تعالى. Walizidisha zaidi kwa wale waliodai kuwa ni wafuasi wake, wakidai kuwa walikuwa na hali fulani ya utukufu na hivyo kuwafanya watu wafuate kila neno walilotamka ima ni kweli au uongo, iwe na uongozi au upotoshaji. Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema,

أَتَّخَذُوا أَحْبَابَهُمْ وَرَهْبَنَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ اللَّهِ

“Wamewafanya makuhani wao na watawa wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu.” (9:31)

Imam Ahmad alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنه kutoka kwa Umar رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا تُطْرُقُنِي كَمَا أَطْرَبَ النَّصَارِيُّ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ. فَإِنَّمَا أَنَا عَبْدٌ فَقُولُوا: عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ»

“Msikithirisha kunisifu kama wakristo walivyomsifu Isa Mwana wa Maryam kwa hakika, Mimi ni mja, hivyo semeni, mja wa Allah na Mjumbe Wake.”¹

Kwa mujibu wa Bukhari na tamko lake ni, *“Kwa hakika mimi ni mja, basi semeni, Mja wa Allah na Mtume Wake.”²*

Imam Ahmad alinukuu kuwa Anas bin Malik رضي الله عنه alisema kuwa mtu mmoja alisema, *“Ewe Muhammad! Wewe ni bwana wetu na mtoto wa bwana wetu, mtu muadilifu zaidi na mtoto wa mtu muadilifu zaidi.”* Mtume ﷺ alisema,

¹ Ahmad 1:33.

² *Fat'hul Bari* 6:551.

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ! عَلَيْكُمْ بِقَوْلِكُمْ، وَلَا يَسْتَهْوِيَنَّكُمُ الشَّيْطَانُ، أَنَا مُحَمَّدٌ بْنُ عَبْدِ اللَّهِ، عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ، وَاللَّهِ مَا أَحِبُّ أَنْ تَرْفَعُونِي فَوْقَ مَنَزَلَتِي الَّتِي أَنْزَلَنِي اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ»

*"Enyi watu, semeni mnachotaka kusema, lakini msimruhusu shetani kuwaghilibu, Mimi ni Muhammad bin Abdillahi, mja wa Allah na Mjumbe wake. WaAllah! Sipendi kupandishwa daraja zaidi ya vile Allah Alivyonipa."*¹

Kauli ya Allah تعالی،

وَلَا تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ

"..wala msimseme Mwenyezi Mungu ila kwa lilio kweli."

Maana yake: Msiseme uongo na kudai kuwa Allah تعالی Ana mke au mtoto, Allah تعالی ni Mtukufu sana kuliko sifa wanazompa. Allah تعالی Anatukuzwa, Anasifiwa na Kuhishimiwa kwa Uwezo Wake na Ukubwa Wake, na hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Yeye. Allah تعالی Amesema,

إِنَّمَا الْمَسِيحُ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ رَسُولُ اللَّهِ وَكَلِمَتُهُ أَلْقَاهَا إِلَى مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِنْهُ

"...Hakika Masihi Isa mwana wa Maryamu ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na neno Lake tu Alilompelekea Maryamu, na ni roho iliyotoka Kwake. Basi Muaminini Mwenyezi Mungu na Mitume Wake."

Isa عليه السلام ni mja tu wa Allah تعالی na mmoja wapo katika viumbe Wake. Allah تعالی Alimuambia, "Kuwa" na akawa, na Alimtuma kuwa Mtume, Isa عليه السلام alikuwa neno toka kwa Allah تعالی ambalo Aliliweka kwa Maryam. Maana: Alimuumba kwa neno 'kuwa' alilolipeleka Jibril عليه السلام kwa Maryam. Jibril عليه السلام alipulizia maisha ya Isa عليه السلام kwa Maryam kwa uwezo aliopewa na Allah تعالی, na matokeo yake akatokea Isa عليه السلام. Tukio hilo lilikuwa badala ya mahusiano ya mume na mke yenye kuleta zao la mtoto. Kwa sababu hii Isa عليه السلام alikuwa ni neno, na Ruh aliyewmbwa na Allah تعالی, kwa kuwa hakuwepo baba wa kumzaa. Bali, alitokea kwa kupitia neno Alilotamka Allah تعالی, 'Kuwa na akawa' kupitia roho ambayo Allah تعالی Alimtuma Jibril عليه السلام. Allah تعالی Amesema,

¹ Ahmad 3:153.

مَا الْمَسِيحُ ابْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِ الرُّسُلُ وَأُمُّهُ صِدِّيقَةٌ ۗ كَانَا يَأْكُلَانِ الطَّعَامَ ۗ

“Masihi mwana wa Maryam si chochote ila ni Mtume. Wamekwisha pita Mitume kabla yake. Na mama yake ni mwanamke mkweli. Wote wawili walikuwa wakila chakula.”
(5:75)

Kauli ya Allah تعالى،

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ ۗ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾

“Hakika mfano wa Isa kwa Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa Adam; Alimuumba kwa udongo kisha Akamwambia: Kuwa! Basi akawa.” (3:59)

وَالَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهَا مِنْ رُوحِنَا وَجَعَلْنَاهَا وَابْنَهَا آيَةً لِلْعَالَمِينَ ﴿٩١﴾

“Na mwanamke aliyelinda uke wake, na Tukampulizia katika roho Yetu, na Tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni Ishara kwa walimwengu.” (21:91)

وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرَانَ الَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا

“Na Maryam bint wa Imrani, aliyelinda ubikira wake.” (66:12)

Na Allah تعالى Alimzungumzia Masihi,

إِنَّ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ

“Hakuwa yeye (Isa) ila ni Mtumwa Tuliye mneemesha.” (43:59)

Maana ya Kauli ya Allah تعالى، “Neno Lake na Roho Itokayo Kwake.”

“Abdur-Razzaq alisimulia kutoka kwa Mamar nae kuwa Qatadah alisema kuhusu aya,

وَكَلِمَتُهُ أَلْفَنَاهَا إِلَىٰ مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِنْهُ

“... neno Lake tu Alilompelekea Maryamu, na ni roho iliyotoka Kwake.”

Ni sawa na Kauli Yake,



“*Kuwa*” Ikawa.¹

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Ahmad bin Sinan Al-Wastwiyyu alisema kuwa alimsikia Shadha bin Yahya akieleza Kauli ya Allah تعالى,

وَكَلِمَتُهُ أَلْقَاهَا إِلَى مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِنْهُ

“...na neno Lake tu Alilompelekea Maryamu, na ni roho iliyotoka Kwake.”

Isa عليه السلام hakuwa neno, bali Isa عليه السلام alikuwa kwa sababu ya neno.² Bukhari alinukuu kuwa Ubadah bin As-Samit رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«مَنْ شَهِدَ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَخَذَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، وَأَنَّ عِيسَى عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ وَكَلِمَتُهُ أَلْقَاهَا إِلَى مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِنْهُ، وَأَنَّ الْجَنَّةَ حَقٌّ، وَالنَّارَ حَقٌّ، أَدْخَلَهُ اللَّهُ الْجَنَّةَ عَلَى مَا كَانَ مِنَ الْعَمَلِ»

“Mwenye kushuhudia kuwa hapana mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah Pekee hana washirika, na kuwa Muhammad ni mja na Mtume Wake, na kuwa Isa ni mja na Mjumbe wa Allah na neno Lake Alilompulizia Maryam na roho iliyotoka kwake, na kuwa pepo ni kweli na Moto ni kweli; Allah Atamuingiza peponi kutokana na amali alizofanya.”³

Katika masimulizi mengine, Mtume ﷺ alisema,

«مِنْ أَبْوَابِ الْجَنَّةِ الثَّمَانِيَةِ يَدْخُلُ مِنْ أَيِّهَا شَاءَ»

“Kupitia katika moja ya milango minane ya Peponi autakao”⁴

Muslim pia alinukuu kama hivyo.⁵ *Ruh* kutoka kwa Allah تعالى, katika aya na hadithi ni sawa na Kauli ya Allah تعالى,

¹ AbdurRazzaq 1:177.

² Ibn Abi Haatim 6310.

³ *Fat'hul al-Bari* 6:546.

⁴ *Fat'hul al-Bari* 6:547.

⁵ Muslim 1:57.

وَسَخَّرَ لَكُم مَّا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ جَمِيعًا مِّنْهُ

“Na Amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka Kwake.” (45:13)

Maana, ‘Vyote ni viumbe vyake’ “kutoka Kwake haina maana kuwa ni sehemu Yake kama wanavyodai Manasara - Laana ya Allah iendelee kuwashukia. Kusema kuwa kitu kinatoka kwa Allah تعالى, ni kama vile kusema ‘roho ya Allah تعالى’, ‘Ngamia wa kike wa Allah تعالى’, au ‘Nyumba ya Allah تعالى’ ina maana kuvitukuza hivyo vitu na kuonesha kuwa Anavimiliki na ni Vyake.

Allah تعالى Amesema,

هٰذِهِ نَاقَةٌ اَللّٰهُ

“Huyu ngamia wa Mwenyezi Mungu.” (11:64)

Kauli ya Allah تعالى,

وَطَهَّرَ بَيْتِي لِلطَّٰبِثِيْنَ

“...na isafishe Nyumba Yangu kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu.” (22:26)

Au kama ilivyokuja katika Hadithi sahihi imesema,

«فَاَدْخُلْ عَلٰى رَبِّيْ فِي دَارِهِ»

“Nitaingia kwa Mola Wangu ndani ya Nyumba Yake.”¹

Mifano yote hii inakusudiwa kutukuza vitu hivyo vinapohusishwa na Allah تعالى katika utaratibu huu. Allah تعالى Amesema,

فَقٰمِنُوْا بِاللّٰهِ وَرَسُوْلِهِ

“...Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake..” (64:8)

Kuamini kuwa Allah تعالى ni Mmoja na Pekee na kuwa hana mtoto au mke, Jueni kuwa kwa hakika Isa عليه السلام ni mja na Mjumbe wa Allah تعالى. Allah تعالى Alisema baada ya hapo.

¹ Al-Bukhari 7440.

وَلَا تَقُولُوا ثَلَاثَةً

“Wala msiseme: Utatu....”

Msiwatukuze Isa عليه السلام na mama yake kuwa waungu sawa na Allah تعالى. Allah تعالى ni Mtukufu zaidi kuliko wanavyomsifu yeye. Aya hii ni kama aya iliyokuwepo katika Surat Al-Maida (sura ya 5). Allah تعالى Amesema mwisho wa Sura hiyo hiyo,

لَقَدْ كَفَرَ الَّذِينَ قَالُوا إِنَّ اللَّهَ ثَالِثُ ثَلَاثَةٍ وَمَا مِنْ إِلَهٍ إِلَّا إِلَهٌ وَاحِدٌ

“Kwa hakika wamekufuru walio sema: Mwenyezi Mungu ni wa tatu wa Utatu. Hali hakuna wa kuabudiwa ila Mungu Mmoja.” (5:73)

Na mwishoni mwake,

وَإِذْ قَالَ اللَّهُ يَعْيسَى ابْنُ مَرْيَمَ مَا أَنْتَ لِلنَّاسِ لِحُجَّتِي

“Na pale Mwenyezi Mungu Atakaposema: Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi ..”

Manasara, Laana ya Allah تعالى iwafikie, hawana mipaka ya kukufuru kwa sababu ya ujinga wao, hivyo kauli zao za kukengeuka na kupotoka kwao kunazidi. Baadhi wanaamini kuwa Isa عليه السلام ni Allah تعالى, wengine wanaamini ni mmoja katika nafsi tatu na wengine wanaamini ni mtoto wa Allah تعالى. Imani zao ni nyingi na zinapingana zenyewe, baadhi ya watu wanasema, iwapo Wakristo kumi watakutana, basi watakuwa katika madhehebu kumi na moja!!

Madhehebu ya Kikristo

Said bin Batriq, Askofu wa Alexandria na mwanachuoni maarufu wa Kikristo, aliyetajwa katika mwaka 400 baada ya Hijra, kuwa Baraza la Kikristo, lilikutana wakati wa utawala wa Constantine, ambaye alijenga mji wenye jina lake. Katika Baraza hilo wakristo waliunda kitu walichokiita dhamana kuu ambayo kwa dhati ni kuvunja dhamana kuu. Walikuwemo maaskofu mia mbili katika Baraza hilo, na walikuwa wamekwenda kombo kiasi cha kuunda madhehebu mengine, ambapo baadhi ya madhehebu ilikuwa na wafuasi ishirini, hamsini au mia moja. Mke wa Mfalme alipoona kuwa walikuwepo zaidi ya maaskofu mia tatu waliokuwa na fikra moja, alikubaliana nao na akajiunga na imani

yao. Constantine ambaye alikuwa mwanafalsafa aliyejitenga – aliunga mkono madhehebu haya ambayo kwa heshima yake makanisa yalijengwa na watoto waliopewa mafundisho, ambayo walibatizwa kwa imani hiyo, na vitabu juu ya imani hiyo viliandikwa wakati huo mfalme alizikandamiza madhehebu mengine. Baraza jingine liliunda madhehebu iliyoitwa Jacobites: ambapo Nestorius walianzisha baraza la tatu. Madhehebu hizi tatu zilikubaliana kuwa Isa alikuwa mtakatifu, lakini walitofautiana kuhusu jinsi utakatifu wa Isa عليه السلام ulivyohusiana na ubinadamu, walikuwa katika umoja au mungu amejiingiza kwa Isa عليه السلام! Madhehebu zote tatu hizo kila moja inalikufurisha kundi jingine. Ama Waislamu wanaona makundi yote matatu yamepotea kama vile Allah تعالى Anavyosema,

أَنْتَهُوا خَيْرًا لَّكُمْ

“Komeni! Itakuwa kheri kwenu...” Maana yake: Itakuwa bora kwenu,

إِنَّمَا اللَّهُ إِلَهُهُ وَوَاحِدٌ ط سُبْحَانَهُ أَنْ يَكُونَ لَهُ وَلَدٌ لَهُ

“Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu Mmoja tu. Ametukuka Yeye na kuwa na mwana.”

Maana yake: ni Mtakatifu kuliko dai la aina hiyo.

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿١٣٢﴾

“Ni Vyake Yeye vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mtegemewa wa kutosha.” (4:132)

Kwani wote ni viumbe Wake, waja na mali ziko chini ya Udhhibiti Wake, na Yeye Ndiye Mtoaji wa mambo kwa hiyo Atawezaje kuwa na mke au mtoto miongoni mwao,

بَدِيعُ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ط اَنْ يَكُونَ لَهُ وَلَدٌ

“Yeye Ndiye Muumbaji wa mbingu na ardhi bila ya ruwaza. Itakuwaje Awe na mwana....” (6:101)

Kauli Yake,

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمٰنُ وَلَدًا ﴿٨٨﴾ لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا ﴿٨٩﴾

“Na wao ati husema kuwa Arrahmani Mwingi wa Rehema ana mwana! Hakika mmeleta jambo la kuchusha mno!” (19:88-89)

Mpaka,

﴿١٧٢﴾ فَرَدَا

“...Peke yake.” (19:95)

لَنْ يَسْتَنْكِفَ الْمَسِيحُ أَنْ يَكُونَ عَبْدًا لِلَّهِ وَلَا الْمَلَائِكَةُ الْمُقَرَّبُونَ^٤ وَمَنْ يَسْتَنْكِفْ عَنْ عِبَادَتِهِ وَيَسْتَكْبِرْ فَسَيَحْشُرُهُمْ إِلَيْهِ جَمِيعًا ﴿١٧٢﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُوَفِّيهِمْ أُجُورَهُمْ وَيَزِيدُهُمْ مِنْ فَضْلِهِ^٥ وَأَمَّا الَّذِينَ اسْتَنكَفُوا وَاسْتَكْبَرُوا فَيَعَذِّبُهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿١٧٣﴾

172. “Masihi hatafanya kiburi cha kutokuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu, wala Malaika waliokurubishwa/sogezwa. Na watakaokataa kwa kiburi kuwa watumwa wa Mwenyezi Mungu na kufanya kiburi, basi Atawakusanya wote Kwake.”

173. “Na ama walioamini na wakatenda mema Atawalipa ujira wao sawa sawa, na Atawazidishia kwa Fadhila Yake. Na ama wale walioona uvunjifu na wakafanya kiburi, basi Atawaadhibu adhabu iliyo chungu. Wala hawatopata mlinzi wala wa kuwanusuru asiye kuwa Mwenyezi Mungu.”

Mitume na Malaika Hawajifaharishi katika Kumuabudu Allah تعالی

Ibn Abi Hatim رحمه الله تعالی alinukuu kuwa Ibn Abbas رضي الله عنهما alisema kuwa fahari ina maana ya kibri, Qatadah alisema kuwa,

لَنْ يَسْتَنْكِفَ الْمَسِيحُ أَنْ يَكُونَ عَبْدًا لِلَّهِ وَلَا الْمَلَائِكَةُ الْمُقَرَّبُونَ

“Masihi hatafanya kiburi dhidi ya kuwa mtumwa wa Mwenyezi Mungu, wala Malaika waliokurubishwa/sogezwa.”

Maana yake: Hawajifakharishi au hawawezi kuwa na kiburi.¹

﴿١٧٣﴾ وَمَنْ يَسْتَنْكِفْ عَنْ عِبَادَتِهِ وَيَسْتَكْبِرْ فَسَيَحْشُرُهُمْ إِلَيْهِ جَمِيعًا

“Na watakaokataa kwa kiburi kuwa watumwa wa Mwenyezi Mungu na kufanya kiburi, basi Atawakusanya wote Kwake.”

¹ At - Tabari 9:424.

Maana yake: Atawakusanya siku ya ufufuo. Kisha Allah تعالى Atawahukumu baina yao na kwa Hukumu Yake adilifu ambayo haina dhuluma wala haikosi.

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُوَفِّيهِمْ أُجُورَهُمْ وَيَزِيدُهُم مِّن فَضْلِهِ

“Na ama walioamini na wakatenda mema Atawalipa ujira wao sawa sawa, na Atawazidishia kwa Fadhila Yake.”

Allah تعالى Atawalipa malipo kamili kwa amali zao njema na Atawapa fadhila Zake, Upendo, na Huruma nyingi.

وَأَمَّا الَّذِينَ ءَسْتَنكفُؤا وَءَسْتَكْبِرُوا

“...Na ama wale walioona uvunjifu na wakafanya kiburi.”

Maana yake: Walioacha kumtii Allah تعالى na kumuabudu na kufanya kiburi,

فَيُعَذِّبُهُم عَذَابًا أَلِيمًا وَلَا يَجِدُونَ لَهُم مِّن دُونِ اللَّهِ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿١٧٦﴾

“..basi Atawaadhibu adhabu iliyo chungu. Wala hawatopata mlinzi wala wa kuwanusuru asiye kuwa Mwenyezi Mungu.”

Ni kama Kauli Yake Allah تعالى,

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَن عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَءِخِرِينَ ﴿١٧٧﴾

“Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike.” (40:60)

Maana yake: Hali ya kuwa wanyonge, waliodhalilika na kutothaminiwa kama vile walivyokuwa wanatakabari na kujiona, kwa kuwa walikuwa wakorofi na waasi.

يَأْتِيهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَهُم بُرْهَانٌ مِّن رَّبِّكُمْ وَأُنزِلْنَا إِلَيْكُمْ نُورًا مُّبِينًا ﴿١٧٨﴾ فَأَمَّا الَّذِينَ

ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَأَعْتَصَمُوا بِهِ فَيَسْجُدْ لَهُمْ فِي رَحْمَةِ مِنِّهِ وَفَضْلِ وَهَيْبَتِهِم إِلَيْهِ صِرَاطًا

مُسْتَقِيمًا ﴿١٧٩﴾

174. Enyi watu! Umekufikieni ushahidi kutoka kwa Mola wenu Mlezi. Na Tumekuteremshieni Nuru iliyo wazi.

175. Ama wale waliomuamini Mwenyezi Mungu, na wakashikamana Naye, basi Atawatia katika Rehema Yake na Fadhila, na Atawaongoa kwenye Njia Iliyonyooka.

Maelezo ya Wahyi Uliotoka kwa Allah تعالى

Allah تعالى Amewaeleza binadamu wote kuwa ushahidi ulio wazi uliwafikia kutoka Kwake, ambao unaondosha uwezekano wa udhuru au kuwa chanzo cha dhana potofu. Allah تعالى Amesema,

وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ نُورًا مُبِينًا ﴿١٧٤﴾

“Na Tumekuteremshieni Nuru iliyo wazi.”

Maana yake: Mwangaza ulio wazi kuhusu haki ambayo inapelekea katika ukweli. Ibn Jurayj na wengine walisema, ‘Ni Qur’an.’¹

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا بِاللَّهِ وَأَعْتَصَمُوا بِهِ

“Ama wale waliomuamini Mwenyezi Mungu, na wakashikamana Naye...”

Kwa kumuabudu Yeye na kumtegemea Yeye kwa kila kitu. Ibn Jurayj alisema kuwa sehemu hii ya aya ina maana, ‘Wanamuamini Allah تعالى na wanaizingatia na kushikamana na Qur’an,’²

فَسَيَدْخُلُهُمْ فِي رَحْمَةٍ مِّنْهُ وَفَضْلٍ

“...basi Atawatia katika Rehema Yake na Fadhila,...”

Maana yake: Atawapa Fadhila Zake na Atawaingiza peponi: Na Ataongeza na Kuzidisha malipo yao na vyeo vyao kama Fadhila kutoka Kwake.

وَيَهْدِيهِمْ إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمًا ﴿١٧٥﴾

“...na Atawaongoa kwenye njia iliyonyooka.”

¹ At - Tabari 9:428.

² At - Tabari 9:429.

Maana yake: Njia iliyo wazi isiyo na uufisadi na kukengeuka. Hii ndio sifa ya waumini hapa duniani na kesho kiyama, kuwa kwao katika njia iliyonyooka na iliyo salama katika masuala ya vitendo na imani. Akhera watakuwa katika njia iliyonyooka ya Allah تعالى inayoelekea kwenye mabustani ya peponi.

يَسْتَفْتُونَكَ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِي الْكَلْبَةِ ۚ إِنَّ آمْرُؤَا هَلَكَ لَيْسَ لَهُ وَلَدٌ ۚ وَآلَةُ أُخْتٍ فَلَهَا
 يَصِفُ مَا تَرَكَ ۚ وَهُوَ يَرِثُهَا ۚ إِنَّ لَمْ يَكُنْ لَهَا وَلَدٌ ۚ فَإِنْ كَانَتَا أَثْتَتَيْنِ فَلَهُمَا الثَّلَاثَانِ مِمَّا تَرَكَ ۚ
 وَإِنْ كَانُوا إِخْوَةً رِجَالًا وَنِسَاءً فَلِلذَّكَرِ مِثْلُ حَظِّ الْأُنثَيَيْنِ ۚ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ أَنْ تَضِلُّوا ۚ
 وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿١٧٦﴾

176. "Wanakuomba uhukumu, sema: Mwenyezi Mungu Anakupeni hukumu juu ya mkiwa. Ikiwa mtu amekufa, naye hana mtoto, lakini anaye ndugu wa kike, basi huyo atapata nusu ya alichocha maiti. Na mwanamume atamrithi ndugu wa kike ikiwa hana mwana. Na ikiwa wao ni ndugu wa kike wawili, basi watapata thuluthi mbili za alichocha maiti. Na wakiwa ndugu wanaume na wanawake, basi mwanamume atapata sehemu iliyo sawa na ya wanawake wawili. Mwenyezi Mungu Anakubainishieni ili msipotee; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."

Hii ni aya ya Mwisho Kuteremshwa, Hukumu ya Al-Kalala

Bukhari alinukuu kuwa Al-Bara alisema kuwa Surah ya mwisho kuteremshwa ilikuwa Surah Al-Bara'ah (sura ya 9) na aya ya mwisho kuteremshwa ilikuwa ni hii.¹

يَسْتَفْتُونَكَ

"Wanakuomba uhukumu."

Imam Ahmad alinukuu kuwa Jabir bin Abdullah رضي الله عنه alisema, Mtume ﷺ alikuja kunitazama nilipokuwa mgonjwa sina fahamu. Alitawadha na akanimwagia maji yaliyobakia, au aliagiza nimwagiwe. Nilipopata fahamu, nilisema, kuwa Hanirithi mimi ila *Kalalah*, sasa itakuwaje kwa mirathi

¹ Fat'hul Bari 8:117.

nitakayoiacha? Baadaye Allah تعالى Aliteremsha aya kuhusu *Faraidhi* (Mirathi 4:11).¹ Sahihi mbili na pia kundi la wapokezi walinukuu.² Katika moja ya maelezo, Jabir رضي الله عنه alisema kuwa aya juu ya mirathi iliteremshwa,

يَسْتَفْتُونَكَ قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ فِي الْكَلَالَةِ

“Wanakuomba uhukumu, sema: Mwenyezi Mungu Anakupeni hukumu juu ya mkiwa.”³

Kana kwamba maana ya maneno (Mwenyezi Mungu Hujua zaidi) ya aya yanaonesha kuwa swali lilihusu *Kalalah*,

قُلِ اللَّهُ يُفْتِيكُمْ

“Sema: Mwenyezi Mungu Anakupeni hukumu.”

Tulitaja maana ya *Kalalah* kabla, kuwa ina maana ya taji lililozunguka sehemu zote za kichwa. Ndio maana wanazuoni wakaeleza kuwa *Kalalah* inahusu mtu aliyefariki dunia na hakuacha wazazi wala watoto. Baadhi wanasema kuwa *Kalalah* inahusu mtu asiye na watoto, kama aya inavyoeleza,

إِنْ أَمْرًا هَلَكَ لَيْسَ لَهُ وَلَدٌ

“...ikiwa mtu amekufa, naye hana mtoto...”

Maana ya hukumu ya *Kalalah* ilimchanganya kiongozi wa waumini Umar bin Al-Khataab رضي الله عنه. Ilinukuliwa katika sahihi mbili kuwa Umar رضي الله عنه alisema, kuna mambo matatu ambayo nilitamani kuwa Mtume ﷺ angelitu-fafanulia ili tukashikamane na maelezo yake. (Nayo ni mafungu ya mirathi ya) babu, *Kalalah* na aina fulani ya Riba.⁴

Imam Ahmad alimnukuu Maa'dan Abi Talhah akisema kuwa Umar bin Al-Khataab رضي الله عنه alisema, “Hapana kitu nilichomuuliza Mtume ﷺ kuhusu maana yake zaidi ya *Kalalah*, mpaka siku moja akanichoma kifua kwa kidole chake na akasema,

¹ Ahmad 3:298.

² Fat'hul Bari 12:26 na Muslim 3:1235.

³ Fat'hul Bari 12:5, Muslim 3:1235, Abu Dawud 3:308, Tuhfatul Ahwadh 6:273, An-Nasai katika Al-Kubraa 4:59 na Ibn Majah 1:462.

⁴ Fat'hul Bari 1:48 na Muslim 4:2322.

«يَكْفِيكَ آيَةُ الصَّبِّبِ الَّتِي فِي آخِرِ سُورَةِ النِّسَاءِ»

“Ayatu Sswayf iliyo mwishoni mwa Surat An-Nisaa inakutosheleza.”¹

Ahmad alitaja masimulizi mafupi ya Hadithi hii, Muslim alinukuu aina ndefu ya Hadithi hii.²

Maana ya aya hii

Allah تعالی Amesema,

إِنْ أَمْرُؤُا هَلَكَ

“...Ikiwa mtu amekufa.”

Maana yake: Amekufa. Allah تعالی Amesema hapa,

كُلُّ شَيْءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجْهَهُ^ع

“Kila kitu kitatoweka, ila Dhati Yake...” (28:88)

Kila kitu kitaondoka na kila mtu atakufa isipokuwa Allah تعالی Peke Yake. Kama Alivyosema Allah تعالی,

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهَ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾

“Kila kilioko juu yake kitatoweka. Na Atabakia Mwenyewe Mola wako Mlezi Mwenye Utukufu na Ukarimu.” (55:26-27)

Ama Kauli Yake Allah تعالی,

لَيْسَ لَهُ وَلَدٌ

“...naye hana mtoto...”

Inaashiria mtu ambaye hana mtoto wala wazazi. Linalothibitsha hilo, ni lile Alilosema Allah تعالی baadaye,

وَلَهُ أَخْتٌ فَلَهَا نِصْفُ مَا تَرَكَ

“...lakini anaye ndugu wa kike, basi huyo atapata nusu ya alichocha maiti.”

¹ Ahmad 1:36.

² Muslim 3:1236.

Angelikuwepo mzazi, dada asingalirithi chochote, kwani anamziba kisheria na kuna makubaliano ya wanazuoni katika hili kwa hiyo aya hii inahusu mtu anayekufa bila kuacha wazazi au watoto. Kama ilivyo wazi kwa wanaotafakari maana yake. Hii ni kwa sababu anapokuwepo mzazi aliye hai, dada harithi chochote, achilia nusu ya mirathi. Ibn Jarir رحمه الله تعالى na wengineo wametaja kuwa Ibn Abbas, Ibn Az-Zubayr رضي الله عنهما walikuwa wakihukumu kuwa iwapo mtu amekufa na akawaacha binti na dada, dada harithi chochote. Walisoma,

إِنْ أَمْرُؤُا هَلَكَ لَيْسَ لَهُ وَلَدٌ وَلَهُ أُخْتُ فَلَهَا نِصْفُ مَا تَرَكَ

“Ikiwa mtu amekufa, naye hana mtoto, lakini anaye ndugu wa kike, basi huyo atapata nusu ya alichocha maiti.”

Walisema kuwa endapo mtu anamuacha binti, hivyo amemuacha mtoto kwa hiyo dada hapati kitu. Wanazuoni walio wengi hawakukubaliana, wakisema kuwa binti anapata nusu na dada nusu nyingine, wakitegemea ushahidi mwingine. Aya hii (4:176) hapo juu inampa dada nusu ya urithi ikiwa hilo limewekwa wazi. Ama kumpa dada nusu katika hali nyingine, Bukhari alinukuu kuwa Sulayman alisema kuwa Ibrahi aliripoti kuwa Al-Aswad alisema, ‘Wakati wa Mtume ﷺ Muadh bin Jabal رضي الله عنه alitoa hukumu kuwa dada anapata nusu, na binti nusu nyingine.’ Kisha Sulayman akasema, ‘Alihukumu hivi na wala haikutajwa wakati wa Mtume ﷺ.’¹

Bukhari alimnukuu Huzayl bin Shurahbil akisema, “Abu Musa al-Ash`ari رضي الله عنه aliulizwa kuhusu hili, alikuwepo binti, mjukuu na dada kurithi: akasema, “Binti ana nusu na dada ana nusu.” Nenda kamuulize Ibn Mas`ud رضي الله عنه, japokuwa nadhani atakubaliana nami. Hivyo Ibn Mas`ud رضي الله عنه aliulizwa na akaambiwa jibu la Abu Musa رضي الله عنه, Ibn Mas`ud رضي الله عنه akasema, ‘Ningekengeuka na nisingekuwa katika walioongozwa, Nitatoa hukumu kama hukumu ya Mtume ﷺ. Binti anapata nusu, na mjukuu anapata sudusi (1/6), na mafungu ya hawa wawili ni sawa na thuluthi mbili, kinacho baki ni cha dada.” Tukarudi kwa Abu Musa رضي الله عنه na tukampa jibu la Ibn Mas`udi رضي الله عنه, na alisema, “Msiniulize (hukumu za kisheria) madam mwanazuoni huyu bado tunaye.”²

¹ Al-Bukhari 6741.

² Al-Bukhari 6736.

وَهُوَ يَرْتُهَا إِنْ لَمْ يَكُنْ لَهَا وَلَدٌ

“...Na mwanamume atamrithi ndugu wa kike ikiwa hana mwana...”

Ayah hii ina maana, kaka anarithi mali yote iliyoachwa (na marehemu *Kalalah*) na dada iwapo hakuacha nyuma mtoto au wazazi. Iwapo alikuwa na mzazi, kaka yake hatorithi chochote, iwapo yupo mtu anayepata fungu maalum katika mrithi kama vile mume, au kaka wa kambo upande wa mama, wanachukua mafungu yao na yaliyosalia anapewa kaka. Imenukuliwa katika sahihi mbili kuwa Ibn Abbas رضى الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ alisema,

«الْحَقُّوا الْفَرَائِضَ بِأَهْلِهَا، فَمَا أَبْتِ الْفَرَائِضُ فَلِأَوْلَى رَجُلٍ ذَكَرٍ»

“Wapeni Mirathi watu wake, na chochote kinachobaki ni hisa ya ndugu wa kiume wa karibu.”¹

فَإِنْ كَانَتَا أَنْتَتَيْنِ فَلَهُمَا الثُّلُثَانِ مِمَّا تَرَكَ

“Na ikiwa wao ni ndugu wa kike wawili, basi watapata thuluthi mbili za alichocha maiti.”

Maana yake: Endapo mtu anakufa kwenye *Kalalah* ana dada wawili, wanapata theluthi mbili ya mirathi. Zaidi ya dada wawili wanagawana theluthi mbili kutokana na ayah hii. Wanazuoni walichukua hukumu inayohusu mabinti wawili au zaidi kuwa wanagawana theluthi mbili, kama ilivyo hisa ya dada wawili au zaidi ilichukuliwa kutoka aya kuhusu mabinti. Katika Kauli Yake Allah تعالى،

فَإِنْ كَانَتَا أَنْتَتَيْنِ فَلَهُمَا الثُّلُثَانِ مِمَّا تَرَكَ

“Na ikiwa wanawake zaidi ya wawili, basi watapata thuluthi mbili za alichokiacha maiti.” (4:11)

Allah تعالى Amesema,

فَإِنْ كُنَّ نِسَاءً فَوْقَ أَنْتَتَيْنِ فَلَهُنَّ ثُلُثَا مَا تَرَكَ

“...Na wakiwa ndugu wanaume na wanawake, basi mwanamume atapata sehemu iliyo sawa na ya wanawake wawili.”

¹ Fat'hul Bari 12:17 na Muslim 3:1233.

Hili ni fungu ambalo ndugu wa kiume (watoto, wajukuu, kaka) kwa kawaida hupata. Yaani mara mbili ya kile wakipatacho wanawake.

Allah تعالى Amesema.

يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمُ

“...Mwenyezi Mungu Anakubainishieni...”

Inafaradhisha na Sharia Yake inaweka mipaka, ikifafanua Hukumu Yake,

أَنْ تَضِلُّوا

“...ili msipotee...”

Maana yake: Ili msije kupotea katika haki baada ya bayana.

وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“...na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.”

Allah تعالى Anajua kwa dhati matokeo ya kila kitu na faida inayopatikana kwa waja Wake. Pia Anajua anachostahili kila ndugu kutokana na mirathi, kwa mujibu wa daraja la uhusiano alilionalo na maiti.

Ibn Jarir رحمه الله تعالى alinukuu kuwa Tariq bin Shahab alisema kuwa Umar رضي الله عنه aliwakusanya Maswahaba wa Mtume ﷺ na kusema ‘Nitahukumu *Kalalah* ambayo hata wanawake wataizungumzia vyumbani mwao.’ Kisha nyoka akatokezea ndani ya nyumba na watu wakatawanyika. Umar رضي الله عنه alisema, “Lau Allah تعالى Aliridhia hili (hukumu ya Umar رضي الله عنه) kutokea ingetokea.”¹ Isnadi ya Hadithi hii ni sahihi. Al-Hakim, Abu Abdullah An-Naysaburi alinukuu kuwa Umar bin Khattab رضي الله عنه alisema, “Kama nilimuuliza Mtume ﷺ kuhusu vitu vitatu ingelikuwa bora kwangu kuliko Ngamia wekundu. (Nayo ni) nani atakuwa Khalifa baada yake, kuhusu watu waliosema, yafaa kupigana nao watu waliokiri utoaji wa Zaka lakini hawatoi? Na kuhusu *kalalah*.” Al-Hakim alisema, “Isnad yake ni sahihi kwa mujibu wa Shaykhan na hawakuiandika.”²

¹ At - Tabari 9:439.

² At - Tabari 2:304.

Pia Ibn Jarir رحمه الله تعالى alisema kuwa ilinukuliwa kuwa Umar رضي الله عنه alisema, "Naona haya kujadili hukumu iliyotolewa na Abubakar رضي الله عنه." Abubakar رضي الله عنه alikuwa akisema kuwa *kalalah* ni mtu asiyekuwa na wazazi au watoto.¹ Kauli ya Abubakar رضي الله عنه ilikubaliwa na wanazuoni wengi miongoni mwa Maswahaba, wafuasi wao na maimamu wa mwanzo na wa sasa. Hii pia ni hukumu iliyo ndani ya Qur'an. Allah تعالى Ameeleza kwa Kuweka wazi hukumu ya *Kalalah*, Aliposema,

يَبِينُ اللَّهُ لَكُمْ أَنْ تَضِلُّوا وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٦٧﴾

"Mungu Anakubainishieni ili msipotee; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu."

Na Allah تعالى ni Mjuzi zaidi.

* * *

¹ At-Tabari 9:437.